4000 1

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

SHULE YA SHAHADA ZA UZAMILI

UAINISHAJI WA USHAIRI WA KISWAHILI: DHIMA YA METHALI

NA

JOSEPH NYEHITA MAITARIA
SHULE YA FANI NA SAYANSI ZA KIJAMII

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA MINTARAFU YA KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA YA Ph.D (KISWAHILI).
CHUO KIKUU CHA KENYATTA

2012

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Maitaria, J.
Uainishaji wa ushauri wa kiswahili: dhima

2012/407663

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote kile.

JOSEPH NYEHITA MAITARIA

20.01.2012

TAREHE

C82/12005/09

NAMBARI YA KUSAJILIWA

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika chuo hiki.

PROF. CLARA MOMANYI

KITIVO CHA FANI NA SAYANSI ZA KIJAMII

CHUO KIKUU CHA KIKATOLIKI CHA AFRIKA MASHARIKI

20th January, 2012

TAREHE

DKT. RICHARD M. WAFULA

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

20th January, 2012

TAREHE

HAKI ZA KUHIFADHI UCHAPISHAJI

"Haki za kunakili kwa njia yoyote ile ni za mwandishi na Chuo Kikuu cha Kenyatta".

IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia dhima ya methali katika kuainishia ushairi wa Kiswahili. Ili kufanikisha lengo hilo, uchanganuzi umefanywa kwa kuzingatia tungo mahususi za Said Ahmed Mohamed (2001), Kithaka wa Mberia (2001), Alamin Mazrui (1994), Akilimali Snow-White (1974), Euphrase Kezilahabi (1974) na Abdilatif Abdalla (1974). Hao ni miongoni mwa watunzi mashuhuri wa ushairi wa Kiswahili hapa Afrika Mashariki kuanzia mwaka wa 1970 hadi wakati wa sasa. Mihimili iliyoongoza utafiti huu ilitokana na nadharia mbili: Fomula ya Kisimulizi na ile ya Semiotiki. Aidha, utafiti ulifanywa maktabani na nyanjani.

Tasnifu hii imegawanyjka katika sura saba. Sura ya kwanza, imeshughulikia mada na madhumuni ya utafiti. Udurusu wa maandishi yaliyohusu mada ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia iliyoongoza utafiti huu pia iliigusiwa. Sura ya pili, imeshughulikia namna methali zilivyotumiwa kama fomula katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Maelezo hayo yameimarisha utathmini wa uwiano uliopo baina ya fani na maudhui katika mashairi hayo teule. Nayo sura ya tatu, imechanganua baadhi ya mashairi ya Akilimali Snow-White na ya Abdilatif Abdalla ili kufafanulia dhima ya methali katika ushairi uliozingatia arudhi za kimapokeo. Sura ya nne, imechanganua baadhi ya mashairi ya Said Ahmed Mohamed na ya Alamin Mazrui. Uchanganuzi huo umebainisha jinsi ushairi wa kati ulivyotumia methali chache na ulivyoshirikisha kauli zilizoibuliwa kwa makusudi. Kadhalika, sura ya tano imechanganua baadhi ya mashairi ya Kithaka wa Mberia na ya Euphrase Kezilahabi ili kubainisha mwelekeo kuhusu matumizi ya methali chache mno au kutotumiwa kwazo katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Aidha,

sura hiyo imedhihirisha dhima ya methali kupitia kwa maudhui yaliyowasilishwa. Sura ya sita, imebainisha uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia matumizi ya methali. Uainishaji huo umependekeza kuwa ushairi wa Kiswahili huweza kugawanywa zaidi kimakundi. Sura ya saba, ni hitimisho la tasnifu. Mambo muhimu ambayo yamezingatiwa ni pamoja na muhtasari, matokeo, matatizo na mapendekezo kuhusu jinsi ushairi wa Kiswahili unavyoweza kufanyiwa utafiti zaidi. Aidha, sura hiyo imejaribu kujibu maswali ya utafiti kulingana na uchanganuzi wa mashairi yaliyozingatiwa.

SHUKRANI

Baada ya kujitosa na kupiga mbizi katika bahari hiyo hadi nikafika ufuoni salama salimini, namshukuru Mwenyezi Mungu. Ningependa kutoa shukurani zangu za dhati kwa wasimamizi wa kazi hii: Prof. Clara Momanyi na Dkt. Richard M. Wafula. Kwa hakika mliweza kuniongoza na kunielekeza ili nisizame baharini. Kila wakati mlikuwa tayari kunishika mkono na kunionyesha mbinu za kuepukana na vizingiti kwa hadhari. Ingawa safari ilikuwa ngumu, mliifanya rahisi: kwa mawazo mliyonipa bila kunihini, hasa kupitia kwa kalamu zenu nyekundu zilizoona nilipopotoka. Ingekuwa si kwa kujitolea kwenu, ukingoni ningefika japo kwa shaka. Kwa hakika mlikuwepo kila wakati nilipohitaji uelekezi.

Kadhalika, nawashukuru wanaidara wote walionihimiza ili kuweza kujitosa na kuikabili bahari. Kuna wale walionichochea kuianza safari hiyo, hasa nilipokuwa nikiliandaa pendekezo la utafiti na wakati nilipokuwa nikiliwasilisha. Maswali niliyoulizwa, ya kwa nini na maoni niliyopewa na Prof. Kitula King'ei na Prof. Catherine Ndungo yalijenga msingi katika kuichonga na kuipa kazi hii mwelekeo uliostahili. Naye, Dkt. Edwin W. Masinde hakusita kuniuliza kila mara hatua niliyofikia katika utafiti wangu. Dkt. Leonard M. Chacha, nakushukuru siyo tu kwa urafiki bali pia kwa kukubali kupitia baadhi ya sura nilizoziandika na kunipa ushauri. Dkt. Jackton Onyango, ulinifaa katika uwasilishaji wa marejeleo. Prof. Ireri Mbaabu, Dkt. Miriam Kenyani Osore, Dkt. Alice Mwihaki, Dkt. Pamela Y. Ngugi, Dkt. Sheila Ryanga, Dkt. Peter Karanja, Mwl. Peter M. Mugambi, Mwl. Evaline S. Mudhune, Mwl. Hannah Gathenji, Mwl. Eliphas K. Kamunde, Mwl. Mutegi Mukobwa na Mwl. Gerald M. Matti (kwa sasa ni marehemu); sitawasahau kwa

kuwa karibu nami nilipokuwa mahututi katika hospitali M.P.Shah. Wanaidara wengine ambao pia walinitia moyo ni Bw. David Ondigo, Bw. Samson Ndulu, Bi. Leah Kimani, Bi. Margaret Mwihia, Bi. Grace Kinyua, Bi. Julia Ng'ang'a na John Waweru.

Ningependa pia kuwashukuru akina Prof. Kimani wa Njogu, Prof. Chacha Nyaigotti-Chacha, Prof. Rocha Chimerah, Prof. Francis Imbuga, Prof. Mikhail Gromov, Dkt. James Onyango Ogolla, Dkt. Kisa Amateshe, Dkt. Charles Kesero, Dkt. Eric Wainaina, Dkt. Peter M. Nzunga, Dkt. Vincent Were na Dkt. Ezekiel Alembi (kwa sasa ni marehemu). Asanteni kwa mawaidha mliyonipa wakati nilipokuwa napiga mbizi na kuelea baharini. Nilipokuwa Dar es Salaam, nilisaidiwa sana na Prof. F. E. M. K. Senkoro, Prof. Abdu M. Khamisi, Prof.Yared M. Kihore, Prof. M. M. Mulokozi, Prof. Y. I. Rubanza. Sitasahau kauli ya Prof. J. S. Madumulla kuwa, 'wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka'. Pia, nawakushukuru sana wahudumu wa makavazi na maktaba ya TATAKI. Kwa mfano, mkurugenzi wa TATAKI, Dkt. Aldin K. Mutembei, aliniruhusu kusoma vitabu, majarida na tasnifu zilizopatikana katika taasisi hiyo. Miongoni mwa wale walionisaidia kupata vitabu na majarida ni, Bi. Everlyne Mshighwa na Bw. Vincent Geoffrey Nkondokaya.

Nilipokuwa mwambao wa Kenya nilijifunza mengi kuhusu ushairi wa Kiswahili kupitia kwa: Prof. Sheikh Nabhany, Bi. Amira M. Saidi, Bw. Mohamed Kirua Mchambi, Bw. Hamza Abubakar, Bi. E. Mchozi, Bi. Zainabu N. Ali na Bw. Karisa J. Ngao.

Pia, namshukuru kwa dhati mke wangu Bi. Selina Rhobi ambaye alinivumilia na kunitia moyo wakati wote nilipokuwa nikipambana na bahari hadi nilipokivuka kivuko. Huo ni ushuhuda wa jitihada zetu.

Wanangu, Ghati, Chacha, Bhoke na Mwita mlinitia moyo bila kuelewa, kwa vicheko na furaha mlivyokuwa nayo kila tulipojumuika pamoja. Ndugu zangu wote, asanteni kwa imani na upendo wenu usiotetereka. Dkt. Kazungu, umekuwa ukinifadhili na kunihimiza kufika ufuoni. Kila wakati umekuwa ukinikumbusha kuhusu 'karne hii'. Ndugu Safari, mchango wako ulinifaa sana. Maneno, sitakusahau kwa kuwa karibu nami kila wakati. Pia, sitamsahau Mh. Shadrack Rogers Manga, siyo tu kama baba bali pia kwa kunihimiza kuimaliza safari hiyo.

Kadhalika, nakishukuru kikundi chetu cha maombi cha Kiu River-Kahawa Sukari (Kanisa la *Deliverance*) kunikumbuka kwa maombi ya mara kwa mara. Bw. na Bi. E.K. Koimett, sitawasahau kamwe kwa nasaha, upendo na ukarimu wenu usiotetereka. Mungu awabariki kwa udugu na ujirani mwema.

Ningependa pia kukishukuru Chuo Kikuu cha Kenyatta kupitia kwa mradi wa Naibu wa Chuo, ambapo baadhi ya malipo ya karo yaliweza kugharimiwa. Vile vile, ufadhili wa utafiti ulinisaidia sana kupata data nilizohitaji. Shule ya uzamili ilisaidia kwa mchango wawarsha za kitaaluma walizoziandaa na pia kupitia kwa mikakati ya kufuatilia maendeleo ya utafiti wangu. Zaidi ya hayo, nakishukuru chuo kwa kunipa likizo ya

muhula mmoja ili kuweza kushughulikia kwa makini utafiti na uandishi wa tasnifu. Ufadhili huo umechangia pakubwa katika kuikamilisha safari hiyo.

Mwisho, Bi. Anne Kiigi na Bi. Sheila M. Ozengo, pokeeni shukrani zangu za dhati kwa kuihifadhi kazi hii kimaandishi. Kupitia kwa juhudi zenu, kazi hiyo iliwasilishwa kwa wakati: Mungu abariki kazi ya mikono yenu.

Kwa hakika niliupata msaada kutoka kwa watu mbalimabli ingawa sikuweza kuwataja kwa majina lakini sijawasahau, nawashukuruni mno.

TABARAKA

Kwa wazazi wangu, Maitaria Mohenda (Tata, Nyamasani Gakomora) na Ghati Nyambebe (Oma, Chongore Omotengi): mlitaka nikijue Kiingereza na sasa nakifahamu Kiswahili.

Kwa mke wangu Selina Rhobi: Kazi hii ni matokeo ya upendo na uvumilivu wako.

Kwa wanangu Ghati, Chacha, Bhoke na Mwita: Pigeni mbizi zaidi.

YALIYOMO

Ikirari ii

Haki za Kuhifadhi Uchapishaji iii

Ikisiri iv

Shukrani vi

Tabaraka x

Yaliyomo xi

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA TASNIFU

1.0 Utangulizi 1

1.1 Ufafanuzi wa Dhana Muhimu 1

1.2 Usuli wa Utafiti 4

1.3 Mada ya Utafiti 8

1.4 Maswali ya Utafiti 9

1.5 Madhumuni ya Utafiti 10

1.6 Sababu za Kuchagua Mada 10

1.7 Udurusu wa Maandishi 14

1.8 Misingi ya Nadharia 23

1.9 Upeo na Mipaka ya Tasnifu 34

1.10 Mbinu za Utafiti 36

SURA YA PILI

METHALI KAMA FOMULA YA UTUNZI KATIKA USHAIRI WA KISWAHILI

2.0 Utangulizi 44

2.1 Fani katika utunzi na Uwasilishaji wa Ushairi 45

2.1.1 Methali kama Kichepuo cha Kufafanulia Maelezo ya Msingi 49

2.1.2 Methali kama Kiunzi cha Usimulizi na Udhibiti wa Muundo 51

2.1.3 Methali kama Msingi wa Kuteua Matini Nyinginezo Zilizoshirikishwa... 53

2.1.4 Methali kama Kauli za Makusudi Kutegemea Athari Itakayoibushwa katika Hadhira 56

2.1.5 Methali kama Chombo cha Kuwasilishia Dhamira na Muhtasari wa Maudhui 59

2.1.6 Methali kama Chombo cha Kubainishia Uhalisi wa Maisha na Kuifadhi Utamaduni wa Jamii 62

2.1.7 Methali kama Kauli za Kujengea Mapigo ya Ridhimu na Udhibiti wa Mwendo 64

2.1.8 Methali kama Kauli Zinazokumbukika kwa Urahisi 68

2.1.9 Methali kama Chombo cha Kufumbia Fumbo 70

2.1.10 Methali kama Chombo cha Kudhibiti Kaida za Kisarufi 73

2.1.11 Methali kama Nguzo ya Kubainisha Miktadha ya Kijamii..... 75

2.1.12 Methali kama Kiashiria cha Ufasiri wa Ujumbe 77

2.1.13 Methali kama Mbinu ya Kujengea Taharuki 79

2.1.14 Methali kama Chombo cha Kuwasilishia Mabadiliko ya Kijamii 83

2.1.15 Methali kama Chemichemi ya Kujengea Mtazamo Mpya wa Kiuwasilishaji 85

2.1.16 Methali kama Chombo cha Kuwasilishia Hisi na Kubainishia Itikadi ya Mtunzi 88

2.1.17 Methali kama Kauli Teule za Kuielekeza na Kuiadilisha Jamii 91

2.1.18 Methali kama Kipengele cha Kudhihirisha Weledi wa Lugha 94

2.1.19 Methali kama Chombo cha Kujengea Taswira na Isitiari 96

2.1.20 Methali kama Chombo cha Kuibulia na Kujengea Usambamba..... 99

2.3 Kiishilio 102

SURA YA TATU

UCHANGANUZI WA USHAIRI WA KIMAPOKEO KWA LENGO LA KUTATHMINI MATUMIZI YA METHALI

3.0 Utangulizi 106

3.1 Uchanganuzi wa Ushairi wa Abdilatif Abdalla: *Sauti ya Dhiki*..... 107

3.1.1 Shairi: Mnazi Vuta N'kuvute 107

3.1.1.1 Mpiga ngumi ukuta, huumiza mkonowe 108

3.1.1.1.1 Methali kama kauli ya kusawiri na kubainisha mahusiano ya wahusika 108

3.1.1.1.2 Tahadhari inayotolewa kupitia kwa methali 110

3.1.1.1.3 Uwasilishaji wa muhtasari wa ujumbe kutokana na methali 112

3.1.1.1.4 Methali kama mbinu ya kumtafakarisha msomaji 113

3.1.1.1.5 Ujenzi wa taharuki kutokana na matumizi ya methali 115

3.1.1.1.6 Ubainishaji wa mapisi kupitia kwa matumizi ya methali 117

3.1.1.1.7 Uibushaji wa mikinzano ya kitabaka kutokana na methali 118

3.1.1.2 Heri nusu ya shari, kuliko shari kamili 120

3.1.1.2.1 Matumizi ya methali kama dhihirisho la ubinafsi na dhuluma 121

3.1.1.2.2 Methali kama msingi wa kuendeleza zaidi ujumbe unaowasilishwa 122

3.1.1.2.3 Ujenzi wa taharuki kutokana na methali 124

3.1.1.2.4 Methali kama mbinu ya kuwasilishia isitiari 125

3.1.2 Shairi: Mwerevu Hajinyowi 127

3.1.2.1 Methali kama kichocheo cha kujengea kisa 127

3.1.2.2 Methali kama chombo cha kuundia isitiari 129

3.1.2.3 Methali kama mbinu ya kusaili na kutafakarisha 132

3.1.2.4 Ujenzi wa taharuki kutokana na matumizi ya methali 134

3.1.2.5 Methali kama chombo cha uzindushi na uwasilishaji wa maadili 136

3.1.3 Shairi: Zindukani 137

3.1.3.1 Ukipanda siku ya mvuwa, utakula siku ya juwa 138

3.1.3.1.1. Methali kama Mbinu ya Kujengea Usuli au Dibaji..... 138

3.1.3.1.2 Uibushaji wa taswira kutokana na matumizi ya methali 140

3.1.3.1.3 Methali kama chombo cha uzindushi 143

3.1.3.2 Kingoja kusaidiwa, tutakufa masikini 145

3.1.3.2.1 Methali kama mbinu ya kuimarishia zaidi taharuki 145

3.1.3.2.2 Methali kama msingi wa ujenzi wa taswira 147

3.1.3.2.3 Methali kama msingi wa kuibulia isitiari 149

3.1.3.2.4 Methali kama mhimili wa kuendeleza mawazo 150

3.1.4 Shairi: Kutendana 151

3.1.4.1 Mtu huwa Hakutupa, Amfaapo Mwenzake 153

3.1.4.1.1 Methali kama Mbinu ya kujengea Dibaji..... 153

3.1.4.1.2 Uibushaji wa Kinaya Kupitia kwa Methali 154

3.1.4.1.3 Methali kama Mbinu ya Kuibushia Viona Nyuma na Mbele 155

3.1.4.1.4 Methali kama Mbinu ya Kujengea Upeo wa Juu..... 157

3.1.4.1.5 Uibushaji wa Isitiari Kutokana na Methali 159

3.1.4.2 Nyege ni Kunyegezana 160

3.1.4.2.1 Methali kama Msingi wa Kuzua na Kuendeleza Usemezano 161

3.1.4.2.2 Methali kama Mbinu ya Kubainishia Mwelekeo wa Mshairi 163

3.1.4.2.3 Uwasilishaji wa Maadili Kutokana na Methali 165

3.1.4.2.4 Methali kama Msingi wa Kuwasiri Mahusiano ya Wahusika 167

3.1.4.3 Mjinga 'Meerevuka, Mwerevu u Mashakani 169

3.1.4.3.1 Uwasilishaji wa Uibuaji wa Isitiari kutokana na Methali 169

3.1.4.3.2 Uundaji wa Taharuki kutokana na Matumizi ya Methali..... 171

3.1.4.3.3 Methali kama Mbinu ya kujengea Viona Nyuma na Mbele 174

3.1.4.3.4 Methali kama msingi wa Ujenzi wa Muundo 176

3.1.4.3.5 Methali kama Chombo cha Kubainishia Uzindushi wa Mwanamke 177

3.2 Uchanganuzi wa ushairi wa K. H. A Akilimali Snow-White:

Usanifu wa Ushairi 179

3.2.1 Shairi: Subira 180

3.2.1.1 Methali kama Kichocheo cha Utunzi na Uwasilishaji wa Mawanzo..... 180

3.2.1.2 Methali kama Msingi wa Kubainishia Falsafa na Itikadi ya Mshairi 183

3.2.1.3 Uwasilishaji wa Maadili kutokana na Methali 185

3.2.1.4 Methali kama Chombo cha Utafakari na Usaili 186

3.2.2 Shairi: Alie Kwenda Kaenda 187

3.2.2.1 Methali kama Kiunzi cha Utunzi na Uwasilishaji 187

3.2.2.2 Uibushwaji wa Isitiari kutokana na Methali 190

3.2.2.3 Methali kama Msingi wa Kujengea Itikadi na Mwelekeo wa Mtunzi 192

3.2.2.4 Methali kama Kielekezo cha Kuudhibti Muundo 193

3.2.3 Shairi: Mganga Hatajiganga 194

3.2.3.1 Methali kama Kichocheo cha Kutungia Kisa..... 194

3.2.3.2 Uwasilishaji wa Mawazo Kiisitiari kutokana na Matumizi ya Methali 197

3.2.3.3 Methali kama Nguzo ya kuwasilishia Mawazo ya Uzindushi na Utangamano 199

3.2.3.4 Methali kama Chombo cha Kuwasilishia Muhtasari wa Ujumbe 201

3.2.4 Shairi: Umoja ni Ngome Kuu 202

3.2.4.1 Methali kama Kielekezo cha Kuibulia na Kuwasilishia Mawazo 202

3.2.4.2 Methali kama Msingi wa Kuundia Taswira 205

3.2.4.3 Methali kama Mhimili wa Kuundia Isitiari 207

3.2.4.4 Methali kama Mbinu ya Kuwasilishia Muhtasari wa Ujumbe..... 209

3.2.4.5 Methali kama Nguzo ya Muundo 211

3.3 Kiishilio 212

SURA YA NNE

UCHANGANUZI WA USHAIRI WA KATI KWA LENGO LA KUTATHMINI MATUMIZI YA METHALI

4.0 Utangulizi 214

4.1 Uchanganuzi wa Ushairi wa Alamin Mazrui: *Chembe cha Moyo* 215

4.1.1 Shairi: Usijiangamize 216

4.1.1.1 Methali kama Chombo cha Uwasilishaji wa Muhtasari wa Ujumbe ... 216

4.1.1.2 Methali kama Kichocheo cha Kutafakarisha na Kuwasilisha Ujumbe 219

4.1.1.3 Methali kama Mbinu ya Kuibulia Maudhui ya Uzindushi 222

4.1.1.4 Methali kama Chombo cha Kubainishia Itikadi na Mwelekeo wa Mtunzi 224

4.1.1.5 Methali kama Mbinu ya Ujenzi wa Upeo wa Juu 227

4.1.1.6 Ujenzi wa Usambamba Kutokana na Matumizi ya Methali 229

4.1.1.7 Methali kama Mhimili wa Muundo na Wizani 232

4.1.2 Shairi: Hasira Hasara? 233

4.1.2.1 Methali kama Msingi wa Kuibulia na Kuwasilishia Mawazo 234

4.1.2.2 Methali kama Mbinu ya Kuibulia Usaili na Utafakari 238

4.1.3 Shairi: Mgongano 241

4.1.3.1 Methali kama kchocheo cha Kuibulia na Uwasilishaji wa Mawazo 241

4.1.3.2 Uibushaji na Uwasilishaji wa Ujumbe Kiisitiari kutokana na Methali .. 244

4.1.3.3 Methali kama Mbinu ya Kuibulia Usambamba 248

4.1.3.4 Methali kama Mhimili wa Muundo 250

4.1.4 Shairi: Kula Njama 251

4.1.4.1 Uundaji wa Kinaya kutokana na Methali 252

4.1.4.2 Methali kama Chombo cha Kubainishia Mwelekeo na Itikadi ya Mshairi 255

4.1.4.3 Methali kama Kauli ya Kubainishia Maudhui ya Ukoloni-Mamboleo na Uzindushi 258

4.1.4.4 Methali kama Mhimili wa Kuibulia na Kuwasilishia Muhtasari wa Mawazo 262

4.1.4.5 Uibushaji wa Isitiari kutokana na Methali 265

4.1.4.6 Methali kama Mbinu ya Kuibulia Usemezano 268

4.2 Uchanganuzi wa Ushairi wa Said A. Mohamed: *Jicho la Ndani* 270

4.2.1 Shairi: Mara Mia La! 271

4.2.1.1 Methali kama Msingi wa Kuibulia na Kusawiria Mawazo 272

4.2.1.2 Methali kama Mbinu ya Kuibulia Usemezano 274

4.2.1.3 Methali kama Kauli ya Kuwasilisha Uzindushi na Maadili 276

4.2.1.4 Methali kama Mbinu ya Kuundia Taswira 278

4.2.1.5 Methali kama Mhimili wa Muundo na Mahadhi 280

4.2.2 Shairi: Jicho Geni 282

4.2.2.1 Methali kama Msingi wa Kuibulia na Kuwasilishia Ujumbe 283

4.2.2.2 Methali kama Chombo cha Kubainishia Mwelekeo wa Mshairi na Uzindushi 284

4.2.2.3 Uundaji wa Kejeli kutokana na Methali 286

4.2.2.4 Methali kama Mbinu ya Kuibulia na kuwasilishia Ujumbe Kitaharuki 288

4.2.2.5 Methali kama Mbinu ya Ujenzi wa Usambamba katika Uwasilishaji wa Mawazo 290

4.2.3 Shairi: Kesho 292

4.2.3.1 Methali kama Msingi wa Kuwasilishia Maudhui ya Uzindushi 292

4.2.3.2 Methali kama Msingi wa Kujengea Usambamba 295

4.2.3.3 Methali kama Mbinu ya Kujengea Taharuki 297

4.2.4 Shairi: Nguvu Hazilei 300

4.2.4.1 Methali kama Msingi wa Kuibulia na Kuwasilishia Ujumbe 300

4.2.4.2 Methali kama Mbinu ya Kubainishia Mwelekeo wa Mshairi 302

4.2.4.3 Ujenzi wa Taharuki kutokana na Methali 304

4.2.4.4 Methali kama Msingi wa Kuudhibiti Muundo 306

4.3 Kiishilio 307

SURA YA TANO

UCHANGANUZI WA USHAIRI HURU KWA LENGO LA KUTATHMINI MATUMIZI YA METHALI

5.0 Utangulizi 309

5.1 Uchanganuzi wa Ushairi wa Euphrase Kezilahabi: *Kichomi* 311

5.1.1 Shairi: Mafahali Wapigana 311

5.1.1.1 Kauli teule za Msanii kama Msingi wa Kuundia Taswira na Uwasilishaji wa Ujumbe 312

5.1.1.2 Matumizi ya Viakifishi kama Mbinu ya Kujengea Usimulizi na Udhibiti wa Muundo 314

5.1.1.3 Matumizi ya Kauli Zinazofahamika kama Msingi wa Uwasilishaji 319

5.1.1.4 Ujenzi wa Sitiari kama Msingi wa Kuitafakarisha Hadhira 321

5.1.1.5 Uibushaji wa Usaili kutokana na Uelekezi wa kauli teule za mshairi 324

5.1.1.6 Kauli za Kibinafsi katika Ujenzi wa Mwangwi wa Methali 327

5.1.1.7 Uibushaji wa Maudhui ya Kisiasa kutokana na Matumizi ya Kauli Zilizokinzana 329

5.1.2 Shairi: Nimechoka 333

5.1.2.1 Usawiri na Uwasilishaji wa Ujumbe kutokana na Kauli Zinazojenga Taswira 333

5.1.2.2 Matumizi ya Mbinu ya Usimulizi na Uakifishi katika Kuibulia Msuko wa Vitushi 337

5.1.2.3 Uendelezaji wa Mawazo na Ujenzi wa Taharuki kutokana na Kauli Elekezi..... 340

5.1.2.4 Ujenzi wa Usaili na Utafakari kutokana na Matumizi ya Kauli za Makusudi..... 344

5.1.2.5 Matumizi ya Viakifishi na Uradidi wa Maneno kama Mbinu ya Kujengea Muundo, Ridhimu na Mahadhi 350

5.1.3 Shairi: Kuchambua Mchele 353

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

5.1.3.1 Matumizi ya Taswira na Isitiari kama Mbinu ya Kusawiri
na Kuibulia Mawazo 354
5.1.3.2Matumizi ya Usimulizi kama Msingi wa Kuibulia Hisi 360
5.1.4 Shairi: Hadithi ya Mzee 363
5.1.4.1 Utambaji kama Mbinu ya Utunzi na Uwasilishaji katika Shairi 364
5.1.4.2 Ujenzi wa Taswira kama Mbinu ya Usawiri na Uwasilishaji wa Ujumbe.. 367
5.1.4.3 Kauli za Makusudi kama Msingi wa Kuibulia Taharuki na
Kuendeleza Mawazo 372
5.1.4.4 Matumizi ya Kauli Teule za Makusudi katika Usawiri
na Ubainishaji wa Maudhui ya Ukoloni-Mamboleo 378
5.1.4.5 Matumizi ya Isitiari kama Chombo cha Kuibulia Utafakari mawazo..... 381
5.2 Uchanganuzi wa Ushairi wa Kithaka wa Mberia: *Bara Jingine* 384
5.2.1 Shairi: Hatujaaga Ndoto 384
5.2.1.1 Matumizi ya Kauli au Matini za Makusudi kama Kichocheo
cha Utunzi na Uwasilishaji 385
5.2.1.2 Matumizi ya Kauli za Kibinafsi kama Mbinu ya Kuundia Taswira na
Isitiari 389
5.2.1.3 Ujenzi wa Muundo, Mahadhi na Ridhimu kutokana na Matumizi ya
Kauli za Makusudi 394
5.2.2 Shairi: Bara Jingine 398
5.2.2.1 Matumizi ya Kauli za Kibinafsi kama Msingi wa Kuibulia, Kusawiri na
Kuwasilisha Ujumbe Kuhusu Ujenzi wa Jamii Mpya 399

5.2.2.2 Ujenzi wa Taswira na Isitiari kutokana na Kauli za Makusudi Zilizotumika..... 404

5.2.2.3 Kauli za Kibinafsi kama Msingi wa Kuibulia na Kubainishia Itikadi ya Mshairi 410

5.2.2.4 Mbinu ya Usambamba kama Msingi wa Kuukoleza Uwasilishaji wa Ujumbe 413

5.2.2.5 Ujenzi wa Muundo, Mahadhi na Ridhimu kutokana na Uelekezo wa Viakifishi 417

5.2.3 Shairi: Mruko wa Nyuki 419

5.2.3.1 Ufumbaji na Ufumbuaji wa Fumbo kwa Kuzingatia Mwangwi wa Methali 420

5.2.3.2 Matumizi ya Kauli Teule kama Msingi wa Kusawiri na Kuwasilishia Maadili 422

5.2.3.3 Ujenzi wa Muundo na Mahadhi kutokana na Matini Mahususi Zinazotumika kwa Uelekezo wa Viakifishi..... 425

5.2.4 Shairi: Nakumbuka Ulivyokuwa 428

5.2.4.1 Utunzi kutokana na Uelekezo wa Anwani na Kauli Teule Zinazoibuliwa Kibinafsi 429

5.2.4.2 Ujenzi wa Taswira kama Mbinu ya Kuwasilishia Ujumbe 431

5.2.4.3 Muundo na Mahadhi kutokana na Kauli za Kibinafsi 434

5.3 Kiishilio 438

SURA YA SITA

AINISHO LA USHAIRI WA KISWAHILI KWA KUZINGATIA MATUMIZI YA METHALI

6.0 Utangulizi 441

6.1 Uainishaji wa Awali wa Ushairi wa Kiswahili 442

6.2 Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili Unaopendekezwa 450

6.2.1 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali kama Anwani 452

6.2.2 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali Moja 458

6.2.3 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali Nusu 465

6.2.4 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali Mbili au Zaidi 471

6.2.5 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali kama Kauli 479

6.2.6 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali kama Kibwagizo au Kiishilio 483

6.2.7 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali kama Mwangwi..... 490

6.3 Jedwali Linalowasilisha Ruwaza ya Matumizi ya Methali Katika Ushairi wa Kiswahili..... 500

6.4 Kiishilio 502

SURA YA SABA

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

7.0 Utangulizi 505

7.1 Hitimisho na Matokeo ya Utafiti 505

7.2 Matatizo 522

7.3 Mapendekezo 523

MAREJELEO 525

Makala 525

Tasnifu 532

Vitabu 536

VIAMBATISHO 554

Orodha ya Viambatisho 554

Kiambatisho I: Mashairi ya Kimapokeo 554

Kiambatisho II: Mashairi ya Kati 554

Kiambatisho III: Mashairi Huru 554

Kiambatisho IV: Maswali ya Hojaji 555

Kiambatisho V: Orodha ya Wahojiwa 564

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA TASNIFU

1.0 UTANGULIZI

Utafiti huu umetathmini dhima ya methali katika uainishaji wa ushairi wa Kiswahili. Ushairi kama utanzu muhimu wa fasihi hutumia kauli na matini mahususi za lugha kama chombo cha kuudhibiti muundo, kubainishia mtindo na kuwasilishia maudhui. Katika muktadha huo, washairi wa Kiswahili wamekuwa wakitumia methali kwa namna tofauti tofauti kulingana na uelekezo wa maudhui ambayo huibuliwa, mbali na ubainishaji wa mitindo na miundo katika tungo hizo.

Ni kutokana na hali hiyo, ndipo mtafiti amehakiki kazi maalumu za washairi ili kuelewa dhima ya methali katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Washairi mahususi waliozingatiwa ni Saidi Ahmed Mohamed (2002), Kithaka wa Mberia (2001), Alamin Mazrui (1994), Akilimali K.H.A. Snow-White (1974), Euphrase Kezilahabi (1974) na Abdilatif Abdalla (1973).

1.1 UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU

Methali

Ni aina ya semi au matini za kisanii ambazo zimeibuliwa ili kuwasilishia maadili yanayotokana na tajiriba au uhalisi wa jamii. Aidha, ni kauli za kimapokeo zilizosheheni busara na elimu kuhusu maisha na falsafa ya jamii mahususi. Vile vile, methali ni miongoni mwa semi fupi fupi zenye kuufumba ujumbe ambao huwasilishwa kupitia kwa

tamathali za usemi. Matumizi na maana yazo huweza kufafanuliwa kwa kuzingatia miktadha mahususi ya utamaduni na uhalisi wa maisha katika jamii.

Kauli nyinginezo za Lugha zilizobuniwa kwa makusudi

Ni mafungu ya maneno au sentensi ambazo huwekwa pamoja ili kuleta maana maalumu, pana au isiyo ya kawaida. Hiyo ni mifumo ya maneno au matini mahususi ambazo hubuniwa kibinafsi na wasanii au na kundi finyu katika jamii. Kimatumizi, huwa ni sawa na methali lakini tofauti ni kuwa; zina mwelekeo wa kibinafsi. Aidha, matumizi yazo huashiria maana nyingine ambayo hujikita katika utamaduni na uhalisi wa maisha ya watu. Miundo hiyo inapotumiwa katika mawasiliano ya jamii, hupanua au hubadilisha maana dhahiri ili kuleta maana maalumu iliyokusudiwa. Kimsingi, matumizi hayo huwa ni ya kimafumbo, kitaashira au kiisitiari ambapo huukoleza zaidi ujumbe ambao huwasilishwa.

Ushairi wa Sasa wa Kiswahili

Katika muktadha wa utafiti, hizo ni tungo za kishairi ambazo zimesawiriwa na zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, ni tungo ambazo zimekuwa zikitungwa na wasanii wa Kiswahili kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1960. Katika miaka ya 1970 hadi wakati wa sasa, tungo hizo zimekuwa maarufu miongoni mwa watunzi wa sanaa hii. Ushairi huu hushirikisha mashairi ambayo huzingatia zaidi arudhi, yale ambayo hayazingatii mno arudhi na yale ambayo hayakuzingatia arudhi hizo katika usawiri na uwasilishaji wake.

Ushairi wa Kati

Ni tungo za ushairi wa Kiswahili ambazo hushirikisha kwa kiasi fulani baadhi ya arudhi za kimapokeo katika utunzi wake. Katika tungo hizo, kuna baadhi ya mashairi ambayo hayazingatii mno arudhi hizo bali huzua mitindo na miundo mahususi ya lugha kuwa mbinu ya usawiri na uwasilishaji wake. Tungo hizo zilianza kujitokeza zaidi mwanzoni mwa miaka ya 1960 na kuendelea kutumiwa hadi wakati wa sasa.

Mabadiliko

Ni hali iliyopo kwa wakati wa sasa ambapo ushairi wa Kiswahili hutungwa na kuwasilishwa ama kwa kushirikisha zaidi arudhi za kimapokeo, kiasi fulani cha arudhi hizo au kutozingatia kabisa kanuni hizo. Kwa hivyo, ushairi wa Kiswahili kwa wakati wa sasa hutungwa kwa kuzingatia mitindo tofauti tofauti ambapo yote hukubalika kuwa nyenzo muhimu katika uwasilishaji wa utanzu huu.

Ushairi wa Kiswahili

Ni utungo wa ushairi ambao hutungwa na huwasilishwa kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, ni tungo ambazo huzingatia muktadha pana wa utamaduni na uhalisi wa maisha katika jamii za Afrika Mashariki. Hali hiyo imetokana na sababu kwamba, lugha ya Kiswahili hivi sasa, ni chombo muhimu cha mawasiliano ya jamii katika Afrika ya Mashariki na kwingineko.

1.2 USULI WA UTAFITI

Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu na huendelea kustawishwa kifani, kiumbuji na kimaudhui (Wamitila 2002, Momanyi 1998 na Mulokozi na Sengo 1995). Hali hiyo imetokana na dhima ya utanzu huo katika jamii za Afrika Mashariki ambazo hutumia lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, hapo awali utanzu huo ulikuwa ukitungwa kimasimulizi na baadaye kimaandishi miongoni mwa jamii za waswahili zilizoishi katika upwa wa Afrika Mashariki. Kiswahili kilipoenea na kuwa maarufu katika mataifa ya Afrika Mashariki, ushairi uliweza kutungwa kwa kuzingatia tamaduni za jamii pana zaidi (Mbaga 1978 na Mbughuni 1978). Kwa njia ya ubunifu, ushairi umekuwa ni nguzo ya kusawiria na kuwasilishia uhalisi wa maisha ya watu katika miktadha mahususi ya kitamaduni. Fauka ya hayo, fani au matumizi ya lugha na maudhui ambayo huibuliwa katika ushairi wa Kiswahili huweza kustawishwa, kubadilika au baadhi yazo kupitwa na wakati (Babusa 2005 na Njogu na Chimerah 1999).

Isitoshe, ushairi wa Kiswahili ulikuwa katika masimulizi na kuwasilishwa kama nyimbo au kughaniwa kisha baadaye ulianza kutungwa na kuhifadhiwa kimaandishi (King'ei na Kemoli 2001 na Njogu 1993). Aidha, ukikaririwa au ukisomwa kwa sauti hubainisha matumizi ya lugha ambayo ni ya kiwango cha juu cha usanii, hasa ulinganishwapo na tanzu zingine za fasihi andishi ya Kiswahili kama vile riwaya, hadithi fupi na tamthilia. Aghalabu, mshairi wa Kiswahili ana uhuru mkubwa katika matumizi na ubunifu wa msamiati, uumbaji wa miundo mbalimbali ya kisintaksia pamoja na tamathali za usemi (Zubkova-Bertonani, 2008). Kadhalika Senkoro (1988) amekariri kwamba, kinachofanya maudhui kuwa muhimu katika ushairi ni uwasilishaji wake kupitia kwa ishara mahususi

za lugha ambazo hujengeka katika tamathali za usemi. Kwa ujumla, sanaa hiyo iko katika uteuzi na mpangilio maalumu wa maneno (Mwai, 1988). Kutokana na matumizi mahususi ya lugha na mbinu za uwasilishaji, ushairi huweza kujenga mazingira ya kuiathiri na kuigusa mioyo ya hadhira (Kisia na Mwarandani 2007, King'ei na Kisovi 2005 na Mulokozi na Sengo 1995). Kwa hivyo, katika utunzi na uwasilishaji wake hutegemea mno uwiano uliopo kati ya fani iliyotumiwa na dhamira au maudhui yaliyoibuliwa.

Isitoshe, msanii anapotunga shairi huwa amethiriwa kwa kiwango kikubwa tajiriba yake ambayo imefungamana na utamaduni wa jamii uliomzunguka. Kwa sababu hiyo, ushairi wa Kiswahili hubainisha uhusiano mkubwa na jamii husika (Imbosa 1990 na Chacha 1987). Katika mantiki hiyo, ushairi hupata umuhimu wake kutokana na utamaduni wa jamii. Kimsingi, kunga za uwasilishaji na miundo ya lugha ambayo hutumika ni ile iliyoibuliwa katika misingi ya utamaduni wa jamii husika. Methali kama kipengele cha lugha ya kimapokeo katika jamii, aghalabu hutumika mno katika uwasilishaji tungo za fasihi simulizi. (Wamitila 2008 na Ligami na Barasa 2006). Kwa maoni ya mtafiti, hali hiyo imetokana na kuwepo kwa matumizi ya methali ambayo ni miongoni mwa misemo ya hekima na busara iliyotumika kimapokezi katika mawasiliano ya jamii. Kutokana na dhima yazo katika jamii, zimeweza kutumiwa na kurithishwa kimapokeo kutoka kizazi kimoja hadi kingine (Ndungo 1998). Hivyo, methali ni kiungo muhimu cha lugha ambacho kimeweza kutumiwa katika kuyatafakari na kuyaratili maisha huku zikifichua falsafa na hekima ya jamii katika muktadha wa utamaduni wa watu (Gesero 2009:iv).

Kadhalika, baadhi ya wasanii wa ushairi wa Kiswahili huchelea kutotumia methali kama kipengele mahususi katika tungo zao (Kunemah 2008:ix). Mwelekeo huo ndio uliowaelekeza baadhi ya wahakiki wa fasihi wa hapo awali kuchukulia kuwa, methali ni ushairi mdogo wa Kiswahili (Knappert 1979 na Harries 1962). Mawazo hayo pia yaliendelezwa kwa kiwango fulani na Syambo na Mazrui (1992) kwamba, matumizi ya vina na mizani katika ushairi wa Kiswahili yalitokana na kuwepo kwa methali katika mawasiliano ya jamii.

Isitoshe, ushairi wa Kiswahili una ithibati sufufu ya matumizi ya methali. Hata hivyo, kuna baadhi tungo ambazo hazikutumia kwa uwazi methali. Kwa hivyo zaidi ya methali, baadhi hutumia miundo maalumu ya lugha ya kitamathali ambayo huibuliwa kibinafsi na hutumiwa kwa makusudi katika usawiri na uwasilishaji wa maudhui kwenye utungo. Ingawa ushairi hutumia au haujatumia methali kwa uwazi, tungo hizo huweza kuzingatia mitindo na miundo teule ya lugha ili kuwasilishia ujumbe ambao huakisi uhalisi wa jamii.

Fauka ya hayo, mabadiliko mbalimbali yameweza kutokea katika Afrika Mashariki ambayo yameathiri mno mitazamo ya jamii kuhusu maisha na utamaduni wao. Methali nazo zimeendelea kutumiwa katika ushairi wa Kiswahili kama nyenzo ya kuwasilishia maadili muhimu na kuhifadhi utamaduni wa jamii. Baadhi ya washairi ambao wametumia wingi wa methali katika uwasilishaji wa tungo zao, ni kama vile: Wallah (1988), Karama (1985), Mbega (1984), Uvetie (1983), Khan (1981), Amana (1982), Massamba (1976), Snow-White (1974), Abdalla (1973) na Nassir (1971). Tofauti na hali hiyo, kuna wasanii wengine ambao hawakutumia kabisa methali katika tungo zao.

Aidha, methali chache zilizotumiwa huwa ni kama kauli miongoni mwa matini zingine katika uwasilishaji wake. Miongoni mwa wasanii hao ni kama vile Wamitila (2004), wa Mberia (2001), Kahigi na Mulokozi (1979) na Kezilahabi (1974). Kadhalika, kuna baadhi ya wasanii ambao wametumia idadi ndogo ya methali katika diwani zao kwa kushirikisha arudhi za kimapokeo na mitindo ya mashairi huru. Baadhi ya watunzi wenye mwelekeo huo ni kama vile Khatib (2003), Mohamed (2002), King'ei (1999) na Mazrui (1994).

Kwa hivyo, uteuzi wa kauli za lugha zilizotumiwa katika utunzi na usawiri wa ushairi huashiria ya kuwa, methali ni miongoni mwa tamathali za usemi ambazo huweza kutumiwa au kutotumiwa kwa uwazi kwenye uwasilishaji wake. Hali hiyo huenda imetokana na athari za mabadiliko ya kitamaduni ambayo imeshuhudiwa katika maisha ya watu. Ikiwa ni hivyo, kuna kauli zingine ambazo hutumika na hujibainisha katika tamathali za usemi. Kauli hizo pia huweza kuchangia au kushirikishwa katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi. Katika muktadha huo, utafiti huu umechunguza jinsi watunzi hutumia au wasivyotumia methali kwa uwazi katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Kwa kuzingatia hali hiyo, mashairi hayo yamechambuliwa ili kubainisha mambo ya msingi ambayo huchangia matumizi hayo ya methali. Kwa hivyo, utafiti huu umechunguza uwezekano wa ushairi wa Kiswahili kuainishwa kutokana na dhima ya methali katika tungo hizo.

1.3 MADA YA UTAFITI

Utafiti huu umechanganua dhima ya methali katika kuainishia mabadiliko ya kimtindo katika ushairi wa Kiswahili. Ingawa mashairi mengi ya Kiswahili yana ithibati ya matumizi ya methali, jambo kwamba methali huweza kutumiwa kama kipengele cha kubainisha mabadiliko ya kimtindo katika mashairi halijatafitiwa kwa kina. Kadhalika, methali zimekuwa zikitumiwa kama mbinu muhimu katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili, japo dhima yazo hazijashughulikiwa kikamilifu.

Uhakiki wa ushairi wa Kiswahili umebainisha matumizi mbalimbali ya miundo teule ya lugha ambayo imebuniwa kibinafsi au kwa makusudi na ile iliyozowewa katika mawasiliano ya jamii. Baadhi ya vipengele teule vya lugha ambavyo vimekuwa vikitumiwa vikitumitumiwa mno katika uwasilishaji wa ushairi ni kama vile methali, nahau na misimu (Mohamed 2002, Njogu na Chimerah 1999, Njogu 1996, Imbosa 1990, Kahigi na Mulokozi 1979). Vile vile, tafiti zilizowahi kufanywa hapo awali zimejikita zaidi kwenye maudhui na miundo ya ushairi. Kadhalika, methali huendelea kutumiwa mahususi katika na uwasilishaji wa ujumbe katika ushairi wa Kiswahili. Hivyo, utafiti huu umechunguza na umetathmini matumizi ya methali katika ushairi wa Kiswahili ili kuchangia tafiti za awali zilizowahi kufanywa kuhusu lugha katika ushairi.

Kutokana na udurusu wa maandishi na uhakiki wa ushairi wa Kiswahili ambao mtafiti ameufanya hapo awali umedhihirika kuwa, matumizi ya methali yamepitia mabadiliko mbalimbali ambayo yameathiri sura, mitindo na muundo wa utungo huu. Kwa mfano, kwa wakati huu wa sasa kuna mashairi ambayo hutumia methali nyingi, chache ama ule

usiobainisha kwa uwazi matumizi ya methali katika uwasilishaji wake. Mashairi yaliyopatikana katika diwani teule yaliweza kuchanganuliwa ili kubainisha mwelekeo wa watunzi kuhusu matumizi ya methali katika tungo hizo. Diwani mahususi ambazo zimechanganuliwa katika utafiti huu ni: *Jicho la Ndani* (2002), *Bara Jingine* (2001), *Chembe cha Moyo* (1974), *Usanifu wa Ushairi* (1974), *Kichomi* (1974) na *Sauti ya Dhiki* (1973). Aidha, mitindo mbalimbali ya matumizi ya methali katika uwasilishaji wa ushairi imeathiri mielekeo iliyozowewa ambayo imezua mitazamo mbalimbali kuhusu utanzu huu.

1.4 MASWALI YA UTAFITI

Utafiti huu ulitarajia kujibu maswali yafuatayo:

i. Methali humsaidia vipi mtunzi wa ushairi wa Kiswahili katika utunzi na uwasilishaji wa maudhui ambayo huakisi uhalisi wa kijamii?

ii. Ni sababu zipi za kijamii au za kisanaa ambazo humwelekeza msanii wa ushairi kutumia au kutotumia kwa uwazi methali?

iii. Kauli au matini zingine ambazo hujikita katika tamathali za usemi na zile ambazo hubuniwa kwa makusudi au kibinafsi, hupewa nafasi gani katika uwasilishaji wa ushairi huu?

iv. Matumizi ya methali huweza kutumiwa vipi kama mbinu ya kuainishia mitindo mbali mbali katika ushairi wa Kiswahili?

v. Mabadiliko ya kitamaduni katika jamii huathiri vipi ufasiri wa matumizi ya methali katika ushairi huu?

1.5 MADHUMUNI YA UTAFITI

Malengo ya utafiti yalikuwa ni:

i. Kueleza kuwa, utunzi wa ushairi wa Kiswahili huzingatia matini mahususi za lugha ambazo hupatikana katika mapokeo ya watunzi.

ii. Kufafanua matumizi ya methali kama mbinu ambayo hutumika zaidi katika uwasilishaji wa ujumbe katika ushairi wa Kiswahili.

iii. Kutathmini jinsi methali huweza kutumiwa kama mbinu ya kuainishia mabadiliko ya kiuwasilishaji katika ushairi wa Kiswahili.

iv. Kudhihirisha kwamba, mabadiliko ya kiwakati na ya kitamaduni katika jamii ndiyo huathiri uteuzi wa matini au kauli teule za lugha ya kitamathali kwenye ushairi wa Kiswahili.

v. Kuthibitisha kuwa matini au kauli mahususi ambazo hutumika katika utunzi wa ushairi wa Kiswahili huweza kufasiriwa vyema kwa kuzingatia ishara au vipengele vya utamaduni na uhalisi wa jamii.

vi. Kueleza namna mitazamo ya nadharia ya Fomula ya Kisimulizi na nadharia ya Semiotiki huweza kujenga kielelezo cha kufafanulia matini na mbinu mahususi zilizotumiwa katika uwasikishaji wa ushairi wa Kiswahili.

1.6 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Mtafiti ameufanya utafiti huu huku akizingatia kwamba, ushairi wa Kiswahili huweza kuyakinishwa vyema zaidi kwa kuzingatia matini au kauli za kimapokeo na zile zinazoibuliwa kibinafsi na wasanii. Aidha, lugha ndiyo malighafi ya msingi katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Lugha ambayo hutumiwa katika utungo huo

huwa yenye kuzingatia mpangilio maalumu wa maneno ambao huteuliwa kwa makini na kwa ufasaha zaidi ili kuweza kuwasilisha ujumbe uliotarajiwa (Indede 2008 na Msokile 1992).

Kimsingi, umuhimu wa ushairi wa Kiswahili hutokana na uwiano uliopo kati ya umbuji wa fani zilizotumiwa na maudhui ambayo huwasilishwa katika muktadha wa utamaduni wa jamii (Nchebere 2009 na Nzuki 2002). Kutokana na matumizi ya methali kama kipengele cha kimapokeo na kauli zingine ambazo huibuliwa kibinafsi, zinapohakikiwa huweza kubainisha maendeleo, mielekeo na mabadiliko ya msingi katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti huu umetathmini kutumiwa au kutotumiwa kwa methali kama mbinu ya kubainishia maendeleo, mielekeo na mabadiliko ambayo hudhihirika katika uwasilishaji wa ushairi huo.

Aidha, uteuzi wa matini au kauli na ubunifu au usarifu wa maneno hufanywa kwa makini na kwa ufanifu mkubwa ukilinganishwa na tanzu zingine za fasihi andishi ya Kiswahili kama vile riwaya, hadithi fupi na tamthilia. Aidha, uteuzi wa kunga au mbinu za uwasilishaji na ufasaha wa lugha huweza kujenga uzami wa maana na udhibiti wa dhamira na maudhui katika tungo za ushairi wa Kiswahili (Kisia na Mwarandani 2007:1). Kutokana na ubunifu na matumizi hayo ya lugha, ushairi huweza kufafanuliwa na kubianishwa kimaudhui, kimtindo na kifani (Wamitila 2008:226). Kwa hivyo, utafiti huu umetathmini kutumiwa au kutotumia kwa methali kama mbinu ya kubainihsia maendeleo, mielekeo na mabadiliko katika utungo huu.

Miongoni mwa waandishi na wahakiki wa hapo awali kama vile Knappert (1979), Allen (1971) na Harries (1962) walipobaini kuwa, matumizi ya methali yamekithiri mno katika ushairi wa Kiswahili, walichukulia kuwa chanzo au asili ya utunzi na uwasilishaji wa utungo huu ni methali. Chambilecho Knappert (1979:45):

> Asili iliyowapa washairi wa Kiswahili ilhamu ya kutunga mashairi ilikuwa wingi wa methali; hazina ya fasihi simulizi iliyokuwa imefichika katika mioyo ya wazee wa Kiswahili.

Mwelekeo huo umemaanisha kwamba, baadhi ya mashairi ya Kiswahili huweza kunufaika zaidi kutokana na kuwepo kwa tunu za methali zilizorithishwa kimapokeo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hata hivyo, kuna ithibati ambayo hudhihirisha kuwa, baadhi ya washairi wa Kiswahili, hasa wale ambao hawakuzingatia zaidi arudhi za kimapokeo wamekuwa wakitumia kauli zilizoibua mwangwi wa methali katika ujumbe uliowasilishwa. Miongoni mwa wasanii hao ni kama vile Mberia 2001, Kahigi na Mulokozi (1979) na Kezilahabi (1974). Vile vile, hali hiyo huweza kubainisha kuwa, kuna kundi la washairi wa Kiswahili ambalo hustahabu kutumia methali chache ni kama vile Khatib (2003), Mohamed (2002) na Mazrui (1994). Mwelekeo huo umeashiria kuwa, ushairi huweza ama kutumia au kutotumia methali katika uwasilishaji wa tungo hizo. Kwa hivyo, utafiti huu umetathmini kwa uketo dhima ya methali katika ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia athari za mabadiliko ya kitamaduni na uhalisi wa maisha ya watu katika jamii.

Ushairi kama utungo muhimu wa fasihi katika jamii ya Afrika Mashariki, una historia ndefu (Mulokozi na Sengo 1995). Kupitia kwa ushairi huo, jamii pana ya Afrika Mashariki huweza kusawiri matukio ya kihistoria, kijamii na kitamaduni (Momanyi

1998). Kimsingi, ushairi wa Kiswahili kwa wakati wa sasa, umepanuka na umeweza kustawisha zaidi baadhi ya vipengele vya miundo ya teule ya lugha iliyozowewa miongoni mwa jamii au kuibua mitindo mipya ambayo hujengwa katika tamathali za usemi (Gromov 2006:124). Mitindo hiyo pia hutumika zaidi katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Hiyo imetokana na sababu kwamba, ushairi wa Kiswahili kama utanzu wa fasihi yoyote ile huweza kuathirika kifani na kimaudhui kutokana na mabadiliko ya kiwakati, kitamaduni na uhalisi wa maisha ya watu katika jamii (Mulokozi 2008). Katika muktadha huo, mabadiliko hayo ndiyo hujenga mazingira ambayo huweza kusababisha kuzuka kwa mtindo mpya katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi huo.

Isitoshe, kwa wakati wa sasa, Kiswahili si lugha ya wanajamii wa mwambao wa Afrika Mashariki tu, bali matumizi hayo yameshamiri hata katika kanda ya Afrika Mashariki na ya kati (Mbaabu 1996 na Whiteley 1969). Kadhalika, maenezi hayo yamechangia pakubwa katika ustawishaji na umaarufu wa tanzu mbalimbali za fasihi, ushairi ukiwemo. Kwa hivyo, ushairi wa Kiswahili kwa wakati wa sasa hutungwa kwa kuzingatia zaidi arudhi za kimapokeo na ule usiozingatia kabisa arudhi hizo (Sanka 1988 na Njogu 1979). Ingawa hivyo, utungo huo una mwelekeo wa kutumia methali kama nyenzo ya kuhifadhi utamaduni na pia kuwasilishia maadili katika jamii (Mulokozi na Sengo 1995 na Noor 1988). Kwa sababu hiyo, utafiti huu umechunguza na umefafanua baadhi ya athari za maenezi ya Kiswahili na mabadiliko ya kitamaduni ambayo imesababisha matumizi mbalimbali ya methali katika muktadha wa utunzi na uwasilishaji wa ushairi huo.

Kutokana na udurusu wa maandishi na mapitio ya tafiti mbalimbali za awali, hakuna utafiti uliojulikana ambao umeweza kuchunguza matumizi ya methali kama chombo cha utunzi na kama mbinu ya kuainishia ushairi wa Kiswahili. Aidha, hakuna utafiti uliojulikana ambao umeweza kuchunguza kwa kina namna mabadiliko ya kimtindo yalivyoathiri, kustawisha, kudhoofisha au kudumaza baadhi ya vipengele vya lugha katika muktadha wa ushairi huo.

1.7 UDURUSU WA MAANDISHI

Kuna tafiti zilizofanywa na maandishi mbalimbali yaliyoandikwa kuhusu matumizi ya methali na kauli au miundo mingine mahususi ya lugha ya kitamathali katika ushairi kwa jumla. Kwa hivyo, mtafiti amefafanua na ameonyesha mchango uliotokana na kazi hizo huku akibainisha tofauti iliyopo na utafiti huu.

Kwa mfano, utafiti wa Babusa (2005) umeshughulikia uainishaji wa mashairi ya Kiswahili kwa kuzingatia vigezo badalia uliotokana na maudhui na miundo ya lugha ambayo hutumiwa katika utunzi na uwasilishaji wa utungo huo. Pia, amechanganua historia ya mashairi ya Kiswahili kiwakati na vile yalivyoainishwa kabla ya kuzuka kwa kiumbiumbi cha mgogoro uliosababishwa na mitindo iliyozingatiwa katika uwasilishaji wa 'Ushairi Huru' wa Kiswahili. Alivyoeleza ni kwamba, kutokana na namna maudhui yaliyoibushwa na wasanii wa mashairi ya Kiswahili yaliweza kuainishwa zaidi kimakundi. Zaidi ya hayo, amedhihirisha jinsi baadhi ya vipengele vya miundo ya lugha vilivyoweza kutumika katika uainishaji wa ushairi wa Kiswahili. Maelezo hayo yalichangia utafiti huu kwa ambavyo aliyaainisha baadhi ya mashairi ya Kiswahili kwa

kuzingatia kipengele cha muundo katika ushairi na maudhui yaliyowasilishwa. Utafiti huu umezingatia matumizi ya matini teule kama vile methali zilivyotumika kama mbinu ya utunzi na ya kusawiri maudhui ambayo huwasilishwa katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu pia umeshughulikia namna watunzi huteua matini mahususi kuwa nyenzo ya kuibulia umbuji na upataji wa vipengele vya arudhi kama vile mizani, vina, mishororo na vibwagizo au vimalizio katika ushairi huo. Fauka na hayo, kutumiwa au kutotumiwa kwa methali kumehusishwa katika utafiti huu kama mbinu iwezayo kutumiwa katika kuainishia ushairi huo kwa makundi.

Kadhalika, Masinde (2003) ameshughulikia swala la maendeleo na mabadiliko ya maudhui katika ushairi andishi wa Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, amedhihirisha kuwa maudhui ambayo husawiriwa katika ushairi wa Kiswahili huathiriwa kwa kiwango kikubwa na mabadiliko mbalimbali ya kihistoria na ya kitamaduni katika jamii. Utafiti huu umenufaishwa kwa mwelekeo kwamba, ujumbe katika ushairi huathirika kwa mabadiliko ya kitamaduni ambayo hutokea katika maisha ya jamii. Zaidi ya hayo, utafiti huu umezingatia matumizi ya methali kama fani mahususi ya lugha na kuonyesha jinsi huweza kutumika katika kuibulia na kusawiri mabadiliko ya maudhui katika ushairi wa Kiswahili. Vile vile, utafiti huu umetathmini jinsi mabadiliko ya kitamaduni yalivyoweza kuathiri uteuzi na matumizi ya baadhi ya vipengele vya tamathali za usemi ambavyo hutumika katika uwasilishaji wa ushairi huo

Naye Ndungo (1998), amefafanua baadhi ya methali hupatikana katika jamii za Gikuyu na Waswahili kama chombo cha kubainishia taswira mbali mbali za mwanamke. Katika

kazi hiyo, amefafanua dhana ya methali kama usemi wa kitamathali ambao husheheni utamaduni na matukio mbalimbali yanayohusu mielekeo, falsafa na maono ya jamii. Kadhalika amefafanua kuwa, methali ni kipengele cha utamaduni ambacho huufumba na huuwasilisha muhtasari wa ujumbe. Kutokana na maelezo yaliyotolewa, methali ni kauli au ishara ambazo hujenga au huibua isitiari na itaswira katika uwasilishaji wa mashairi. Pia, amebainisha kuwa methali zinapotumiwa katika mawasiliano ya watu, huwa ni kioo cha kudhihirishia uhalisi wa maisha na utamaduni wa jamii. Kwa hivyo, taswira ya jamii huweza kudhihirika kupitia kwa matumizi ya methali. Ingawa hivyo, methali pia huweza kuzingatiwa kama kauli au matini ambazo huweza kutumiwa mahususi katika kutungia na kuwasilishia tungo mbalimbali za kifashi hususa, ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, muktadha ambamo methali hutumiwa katika ushairi uliweza kuzingatiwa na kufafanuliwa.

Baadhi ya watafiti kama vile Maitaria (1998), King'ei (1982), Parker (1974) na Seitel (1972) wamehakiki methali kama kipengele mahususi cha lugha ambacho huweza kufasiriwa kwa namna mbalimbali kutegemea miktadha ya kitamaduni na uhalisi wa jamii. Kwa sababu, methali huibuliwa katika jamii kwa kuzingatia vipengele vya utamaduni mahususi wa watu. Aidha, waandishi mbalimbali kama vile Babusa (2009), Gesero (2009), Waihiga na Kagwa (2007), Andambi na Murono (2005), Wamitila (2002), Ndalu na King'ei (1997), Karama na Saidi (1983) na Abudu na Baruwa (1980) wamezikusanya methali, kuzipanga kiabujadi na kuzitolea ufafanuzi wa kijumla. Hivyo, mchango uliounufaisha utafiti huu ni kwamba, methali ni mojawapo ya kauli ambazo zimejengwa katika tamathali za usemi na pia huibushwa katika mazingira halisi ya jamii

na utamaduni wake. Kwa kuzingatia maelezo hayo, tayari matumizi ya kijumla kuhusu methali yamebainishwa. Kwa hivyo, utafiti huu umetathmini zaidi kipengele cha methali kama kauli maalumu ambazo hujibainisha katika tamathali za usemi ambapo huweza kutumiwa kama chombo cha utunzi na pia kama mbinu ya kuwasilishia mawazo au maudhui na maadili katika muktadha wa utamaduni wa jamii.

Karama (1996) na Momanyi (1991) wameuhakiki *Utendi wa Inkishafi* kwa kuzingatia mitazamo tofauti. Kwa mfano, Karama amefafanua kuwa katika utendi wa Kiswahili kuna usemezano wa sauti nyingi yaani: za wasemeza na wasemezwa. Katikati ya sauti hizo kuna usemi ambao ni kiungo au kiunzi muhimu cha pande hizo mbili. Utafiti huu umepiga hatua mbele kwamba, usemi hupatikana katikati ya wasemeza na wasemezwa ni matini mahususi ya lugha ambayo huteuliwa na kutumika ili wasanii waweze kuwasiliana vyema na wasemezwa. Maelezo hayo yamekariri kwamba, mtunzi sharti kutilia maanani hadhira. Baadhi ya mambo hayo ni kama vile kauli teule zilizozowewa katika jamii au zile ambazo zimeibuliwa kwa makusudi na kutumiwa katika usawiri na uwasilishaji wa tungo hizo. Naye Momanyi, amezingatia kipengele cha taswira katika *Utendi wa Inkishafi* kama kielelezo cha uhalisi wa maisha ya jamii. Aidha, Momanyi ameshughulikia swala la historia kwa azma ya kueleza zaidi namna uhalisi wa jamii ulivyo bainishwa katika utendi huo. Alichokieleza Momanyi ni kwamba, utunzi wa ushairi wa Kiswahili huathiriwa kwa kiasi fulani kutokana na uhalisi uliopo katika jamii. Jambo hilo huzingatiwa ili kumfanya msanii kuibua taswira ambazo hutumika katika uwasilishaji wa ushairi huo. Tofauti na tafiti hizo za Karama na Momanyi, utafiti huu umehusisha kipengele cha methali kama mbinu mojawapo ya kuwasiliana na hadhira na

pia kama chombo cha kuibulia na kuwasilishia taswira ambazo zimejengwa katika ushairi wa Kiswahili.

Katika kueleza umuhimu wa mtindo katika ushairi, Darvin na Wamuhu (1994) wamesisistiza kwamba, matumizi ya miundo maalumu iliyotumiwa katika ushairi itazamwe kama mtindo wa kusawiri na kuubulia maudhui ambayo yamewasilishwa. Mitindo ambayo iliyopendekezwa ni ile iwezayo kusaidia katika kuibulia hisi na ujenzi wa usambamba katika uwasilishaji wa ushairi. Hisi hizo hudhibitiwa kwa matumizi ya takriri, onomatopea, mizani, urari wa vina na wizani wa ridhimu zilizojengwa katika uwasilishaji wa utungo. Kadhalika imefafanuliwa kwamba, ushairi hupaswa kuimbwa, kughaniwa au kusomwa kwa sauti ili ujumi ambao huibuliwa kupitia kwa matumizi ya maneno teule kuweza kuhisika. Maelezo hayo yameunufaisha utafiti huu, kwa ambavyo ushairi wa Kiswahili hutungwa kwa kuzingatia mno kauli teule za lugha ili kuweza kuwasilishwa kimasimulizi au kwa hati za kimaandishi. Zaidi ya hayo, utafiti huu umetathmini namna methali huweza kutumiwa kama chombo cha kuudhibiti muundo, kuwasilishia hisi na maudhui ambayo huwasilishwa katika ushairi huo.

Kwa upande mwingine, Imbosa (1990), amehakiki jazanda zilizoibuliwa na zilizotumika katika baadhi ya mashairi ya Muyaka wa Hajji. Aidha, amefafanua jazanda kama mbinu ya uwasilishaji katika ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, matumizi hayo hustahili kuhakikiwa, kuchambuliwa na kufafanuliwa. Kwa sababu zinapochambuliwa, hadhira hupata ufahamu ambao huakisi siyo tu umbuji wa msanii bali pia uhalisi wa maisha na utamaduni wa watu. Kutokana na maelezo hayo, msanii huweza huibua jazanda

kutokana na tajiriba yake katika jamii. Kadhalika, imebainishwa kwamba maudhui katika ushairi husawiriwa na huwasilishwa vyema kutokana na jinsi jazanda zilivyojengwa na zilivyotumika. Katika muktadha huo, amezingatia baadhi maneno teule yaliyotumika kujengea jazanda, kuibulia hisi na uwasilishaji wa maudhui katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu umechukulia methali siyo tu kama dhihirisho mojawapo la tamathali za usemi bali pia kama mbinu mahususi ambayo huweza kutumiwa katika kuudhibiti muundo, mtindo na uwasilishaji wa maudhui katika ushairi wa Kiswahili.

Naye Chacha (1987), amedhihirisha ya kwamba ushairi wa Kiswahili umebadilika na umeendelea kuathiriwa kwa kiasi kikubwa kwa upande wa fani inayotumika na maudhui yanayowasilishwa. Aidha, tathmini hiyo imezingatia jazanda zilizoibuliwa katika muktadha wa ushairi wa Kiswahili. Isitoshe, imedahiliwa kwamba, jazanda ambazo hupatikana katika tungo hizo huweza kufafanuliwa vyema kwa kuzingatia muktadha wa utamaduni na uhalisi wa maisha ya watu. Kutokana na maelezo hayo, ujumbe ambao husilishwa katika shairi, hupata ufasiri mwafaka kwa kuzingatia vipengele vya utamaduni mahususi. Utafiti huu umenufaishwa kwa ufafanuzi wa Chacha kwamba, maudhui katika ushairi wa Kiswahili huweza kubadilika sana kutokana na mabadiliko ya utamaduni yanayotokea katika jamii. Kwa hivyo, utafiti huu umetathmini matumizi ya methali kama mbinu ambayo hutumika katika usawiri, uwasilishaji na ubainishaji mtindo katika ushairi wa Kiswahili.

Uhakiki wa Mulokozi (1986) umebainisha kuwa, kuna uwiano kati ya maudhui yaliyoibuliwa na kauli au miundo teule ya lugha ya kimapokeo ambayo hutumika katika

utunzi na uwasilishaji wa tenzi za jamii ya Kihaya. Kilichozingatiwa katika uwasilishaji huo ni unyambuaji wa neno teule ambalo hupatikana katika mapokeo ya jamii ya Kihaya. Katika mantiki hiyo, dhana hizo huweza kutumiwa kuwa dira au msingi wa kuibulia au kusawiri mawazo yaliwasilishwa katika tungo za tenzi. Baadhi ya maneno hayo huweza ama kutumiwa moja kwa moja au kunyambuliwa ili yaweze kujisimamia au kuwasilishia dhana mahususi ya kijamii. Kwa hivyo, neno au kauli hiyo huweza kuvyazwa na kupewa upya wa kimtazamo na kimatumizi katika ushairi. Kadhalika ameeleza kwamba, watunzi wa tenzi za Kihaya huzingatia utaratibu maalumu katika utunzi na uwasilishaji wa utanzu huo. Kwa mfano, mtunzi huutanguliza ujumbe aliotauka kuuwasilisha, kisha hutumia kauli za makusudi au za kibinafsi katika harakati za kuufaragua zaidi ujumbe na baadaye kuuhitimisha utungo. Ingawa utafiti huu haukuzingatia muktadha wa tenzi hizo, utaratibu huo pia hudhihirika katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Aidha, utafiti wa Mulokozi umechangia utafiti huu kwa ambavyo baadhi ya kauli au maneno teule ambayo hupatikana katika mapokeo ya jamii huweza pia kuwa msingi wa kujengewa kisa kirefu katika ushairi na tenzi za Kiswahili. Tofauti na utafiti huo, utafiti huu umezingatia ruwaza ya maneno kama vile methali ambazo pia hupatikana katika mapokeo ya jamii. Mifumo au kauli hizo, hutumika mno katika ushairi wa Kiswahili huwa ni dira ya usawiri, ufaraguzi wa matukio na uwasilishaji wa maudhui. Hata hivyo haimaanishi kuwa, kauli maalumu zisizokuwa methali si mali ya jamii bali watunzi wa mashairi huzitumia kwa ustadi ili kuwasilishia ujumbe kwa utafakari zaidi. Kwa hivyo, kauli ambazo ni za kimapokeo na zile zisizokuwa za kimapokeo zimeweza kuchanganuliwa ili kufafanulia umuhimu wake katika ushairi wa Kiswahili. Kadhalika, matumizi ya methali hazijadumazwa kwa mabadiliko ya kiwakati na kitamaduni bali huweza kuvyazwa upya

au kufanyiwa marekebisho madogo ili kuweza kukabiliana na mabadiliko hayo ya kijamii nay a kimtindo.

Wanyoike (1976) ameeleza kwa ujumla baadhi ya vipengele mahususi vya lugha ambavyo hutumiwa mno katika uwasilishaji wa ushairi. Kilichobainishwa ni kwamba, mtunzi huuchukulia ujumbe ambao huwasilishwa kuwa wa muhimu zaidi katika ushairi. Kwa hivyo, humbidi kuzingatia uteuzi wa kauli au miundo ya lugha, mbinu na kunga mbalimbali ili kuweza kuibua au kuiteka hisi na kuiathiri hadhira. Kadhalika vifungu hivyo vya maneno, huweza kutumiwa wa ustadi ili kuweza kuuibulia au kuuwasilisha ujumbe ulionuiwa kwa kuitafakarisha zaidi hadhira. Ili kutekeleza lengo hilo, mtunzi hupanga maneno au kwa kuvyaza miundo maalumu ambayo huweza kuwasilisha ujumbe kitaswira, kimafumbo au kiisitiari. Kwa hivyo, kauli au miundo hiyo ya lugha huichochea hadhira kuzingatia siyo tu fani mahususi iliyotumiwa, bali pia huzingatia ujumbe ambao husawiriwa na huwasilishwa. Ufafanuzi huo umeujengea utafiti huu mwelekeo wa kutathmini dhima na utendakazi wa baadhi ya miundo mahususi ya lugha iliyotumiwa hususa, methali katika ushairi wa Kiswahili. Aidha, utafiti huu umetathmini jinsi mabadiliko ya kijamii huweza kuwaathiri watunzi wa ushairi kwa upande wa uteuzi wa kauli au miundo mahususi ya lugha iliyozowewa na ile ambayo haijazowewa ili kufafanua jinsi zilivyotumiwa kama mbinu ya uwasilishaji katika ushairi wa Kiswahili.

Kadhalika, Abedi (1954) amefafanua baadhi ya kanuni au arudhi za kiutunzi ambazo hupaswa kuzingatiwa katika utunzi wa ushairi wa Kiswahili. Baadhi ya arudhi zillizopendekezwa ni zile ambazo zimekuwa zikitumiwa mno katika uwasilishaji wa

ushairi wa Waswahili. Miongoni mwa vipengele hivyo vya kiarudhi ni kama vile idadi maalumu ya mizani, urari wa vina, kibwagizo, ridhimu, mikarara na wizani. Ufafanuzi huo umejikita zaidi katika vipengele ambavyo huzingatiwa kwenye utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili wa kimapokeo. Utafiti huu umenufaishwa kwa mawazo hayo kwamba, baadhi ya mashairi hayo kwa wakati wa sasa pia hutungwa na kuwasilishwa kwa kushirikisha baadhi ya vipengele hivyo vya kiarudhi. Zaidi ya hayo imezingatiwa kuwa, uti wa mgongo katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili ni kauli au miundo teule ya lugha ambayo pia huibua au haiibui matumizi hayo ya arudhi. Miundo hiyo ya lugha huweza huegemea katika lugha teule ya kimapokeo au iliyovyazwa kwa makusudi katika ushairi wa Kiswahili. Vile vile imechukulia kuwa, tungo za ushairi wa Kiswahili kwa hivi sasa umepanuka na umevuka mipaka ya Waswahili kama jamii na hutumiwa katika jamii mbalimbali za Afrika Mashariki, ya kati na kwingineko.

Kutokana na udurusu wa tafiti na tahakiki mbalimbali zilizopitiwa, imebainika kuwa, methali na tamathali nyinginezo zilizobuniwa kibinafsi na kwa makusudi huwa ni tunu za fani zitumikazo katika usawiri na uwasilishaji wa maudhui katika muktadha wa ushairi wa Kiswahili na fasihi kwa ujumla. Kwa mfano, methali zimefafanuliwa kwa kuzingatia miktadha ya utamaduni na mawasiliano ya jamii. Kadhalika, ushairi wa Kiswahili umeshughulikiwa kwa kuzingatia maudhui, historia, miundo na baadhi ya fani zilizohusishwa katika uwasilishaji wa utanzu huo. Hata hivyo, tafiti na tahakiki zilizopitiwa zimebaisha kuwa, hazikuzingatia kwa uketo dhima ya methali katika utunzi,

utathmini au uelekezaji wa jinsi mabadiliko ya kitamaduni na uhalisi wa jamii yalivyoweza kuathiri matumizi hayo katika ushairi wa Kiswahili.

1.8 MISINGI YA NADHARIA

Nadharia ambazo ziliupa mwelekeo utafiti huu ni Fomula ya Kisimulizi na ile ya Kisemiotiki. Kwa maoni ya mtafiti, mihimili ya nadharia hizo ziliweza kujenga msingi wa kufafanua, kuhakiki na kutathmini dhima ya methali katika kuainishiamashairi ya Kiswahili.

Nadharia ya Fomula ya kisimulizi ilipendekezwa hapo mwanzoni na Milman Parry mwaka wa 1939. Kimsingi, nadharia hiyo huziakisi tungo za ushairi simulizi na nyimbo kama zenye miundo na vifungu vya matini teule za kimapokeo ambazo hupatikana katika utamaduni wa jamii. Aghalabu, matini hizo zimekuwa zikitumiwa mno katika utunzi, usawiri na uwasilishaji wa baadhi ya tanzu za fasihi simulizi. Fauka ya hayo, Fomula ya Kisimulizi huweza pia kufafanuliwa kama kielelezo au ruwaza ambazo huzingatiwa katika utunzi na uwasilishaji wa tanzu mahususi za fasihi simulizi. Kwa mfano, katika baadhi ya tanzu za fasihi simulizi kuna utaratibu au mtindo maalumu ambao huzingatiwa katika utangulizi, msuko wa vitushi au ujumbe unaowasilishwa na mitindo ya uhitimishaji wa tungo. Kwa kuzingatia mtazamo huo, Parry aliweza kubainisha na kufafanua zaidi mihimili ya Fomula ya Kisimulizi kama mbinu ya uhakiki na ya utunzi katika baadhi ya tanzu za fasihi simulizi.

Aidha, Milman Parry alianza uchunguzi wake mwaka wa 1923 hadi alipofariki mwaka wa 1939. Alihakiki baadhi ya vipengele na miundo mahususi ya lugha vilivyokaririwa katika baadhi ya tungo za fasihi simulizi hususa, ushairi simulizi na nyimbo. Baada ya mauko yake, mawazo hayo yaliendelezwa na Albert Lord, ambaye alikuwa mwanafunzi au mfuasi wake. Kabla ya Parry, baadhi ya wahakiki wa fasihi kama vile Wood (1767) na Wolf (1775) waliuona urudiaji na ukariri wa vifungu vya matini katika tanzu hizo kama udhaifu kwa upande wa mtunzi. Katika ufafanuzi zaidi wa madai hayo, Wood na Worf waliurejelea ushairi simulizi wa Homer. Mtunzi huyo alikuwa ni malenga na manju msifika wa Kigiriki katika enzi zake. Parry aliupinga mtazamo huo hasi. Kwa kuzingatia ushairi uo huo wa Homer, Milman Parry alikuwa katika mstari wa mbele kubainisha ya kuwa, msanii huyo hakuwa msomi na tungo zake ziliegemea kwenye matini mahususi ambazo zilithaminiwa mno katika mapokeo ya jamii. Kwa hivyo, mifumo au ruwaza hiyo ya maneno ilikuwa ni nyenzo muhimu katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi simulizi na nyimbo. Kadhalika, uwasilishaji wa maudhui katika ushairi wa Homer ulijengeka katika misingi ya utamaduni na uhalisi wa jamii.

Zaidi ya hayo, ilibainishwa kwamba, mtunzi wa ushairi simulizi na nyimbo huwa ana muda mfupi katika maandalizi ya uwasilishaji. Kwa sababu, huhitajika kuutunga na kuuwasilisha utungo papo hapo kutokana na muktadha wa tukio na mahitaji ya ha
Kwa hivyo, mtunzi huteua matini ambazo tayari zimekubaliwa, z
kuthaminiwa na kutumiwa kimapokezi katika mawasiliano ya jam
zilizosheheni busara; zilitumiwa kama nyenzo ya kuwasilishia he
muktadha wa utamaduni na uhalisi wa jamii. Aidha, vifu

ya

ruwaza maalumu ya kimofolojia vilivyoakisi mfumo wa kisintaksia. Kwa hivyo, katika muktadha wa ushairi simulizi na nyimbo, vipengele hivyo maalumu vilitumika bila ya kufanyiwa marekebisho yoyote ya msingi. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, matini hizo zilitumiwa ili kuuwasilishia utamaduni, falsafa na uhalisi wa jamii. Kutokana na umaarufu wake katika jamii na miundo isiyobadilika, huufanya ushairi simulizi na nyimbo siyo tu kupata ukariri wa vina, mizani na umuwala katika utungo, bali pia kuwa chanzo cha utunzi huku matumizi hayo yakiacha athari kubwa kwenye dhamiri na sikio la hadhira.

Kwa kuifafanua zaidi mihimili ya nadharia hiyo, Lord (1960) amekiriri kwamba, ushairi simulizi na nyimbo hushirikisha vipengele vya matini teule za kimapokeo ambavyo huunufaisha zaidi utungo huo. Kadhalika mchango wa Lord ni kwamba, matini hizo huhitaji utafakari na usaili katika ufafanuzi ambao huzingatia maana dhahiri na batini. Kwa hivyo, matini hizo huwa ni zile zilizokubaliwa na zilizosherehekewa zaidi katika utamaduni wa jamii. Kwa sababu hizo, mtunzi huweza kuzitumia kuwa dira au kipago cha kusawiri visa virefu kulingana na yaliyonuiwa kuwasilishwa kwa hadhira. Kimsingi, ujumbe huwasilishwa kwa kuzingatia ishara au matini hizo hutegemea zaidi athari ambayo msanii hukusudia kuibua katika hadhira. Aidha, matini hizo huweza kukaririwa kwa malengo ya kuukoleza zaidi ujumbe au kujenga usambamba katika ushairi si na nyimbo.

Nadharia hiyo imeweza pia kurutubishwa kwa mawazo ya wahaki' ya Propp (1968), Fowler (1966) na Levi-Strauss (1963). Waha'

matini teule ambazo hutokana na mapokeo ya jamii zinapotumiwa katika utanzu wa fasihi, hazipaswi kuwa sugu au zenye miundo ya aina moja. Kwa sababu, msanii huwa na uhuru au hiari ya kutumia miundo ya matini zilizopo au kuivyaza upya kulingana na hisi au ujumbe ulionuiwa kuuwasilishwa. Aidha, wametoa tahadhari kuwa, mabadiliko hayo huweza kujiri taratibu kwa kuzingatia athari za kitamaduni na uhalisi wa jamii. Baadaye, miundo hiyo iliyovyazwa; huzowewa, hukubaliwa na huingizwa katika kanzi ya matini teule za jamii. Vile vile Nagler (1974), ameichangia zaidi nadharia hiyo kwamba, mifumo hiyo ya maneno inapotumika ipasavyo husaidia kuumua na kuurutubisha ujumi siyo tu kwenye ushairi simulizi na nyimbo bali pia katika na uwasilishaji wa tanzu mbalimbali za fasihi kwa ujumla.

Kwa ujumla mihimili ya nadharia hiyo ni kama ifuatayo:

i. Mtunzi wa ushairi simulizi na nyimbo ana muda mfupi wa maandalizi. Kwa hivyo, huteua matini teule zilizopo katika mapokeo ya jamii ili iwe dira au chanzo cha utunzi na wa kujieleza.

ii. Matini teule ambazo hutumika katika ushairi huwa ni zile zilizosheheni busara na hekima ya jamii.

iii. Matini teule ambazo hutumiwa kwenye ushairi huwa zimejengwa katika muktadha wa utamaduni wa jamii na hurithishwa kimapokeo kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

iv. Matini hizo huweza kutumiwa katika kuundia mifumo ya mishororo mahususi au huchopekwa katika muktadha ya matini zingine zipatikanazo katika ushairi au nyimbo ili kuwezesha upataji wa mizani, urari wa vina na hata vibwagizo.

v. Matini hizo teule hutumiwa kama mbinu ya kuukariri ujumbe na kuumua ujumi katika ushairi simulizi na nyimbo.

vi. Ingawa matini hizo teule hazibadiliki, huweza kuvyazwa upya. Kwa sababu, mtunzi ana uhuru wa kuisanii kazi hiyo kulingana na ujumbe ambao huwasilishwa.

Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi imetumiwa katika utafiti huu kwa lengo la kuzihakiki baadhi ya matini teule za lugha ambazo huhusishwa kwenye utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Aidha, utafiti huu umetathmini matumizi ya matini teule za kimapokeo kama vile methali na kauli nyinginezo ambazo hubuniwa kwa makusudi au kibinafsi na kutumiwa katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Kadhalika maelezo hayo yametumika kama kigezo cha kujibu swali: Je, methali ni ubunifu wa kibinafsi au ni elementi ambazo huelea katika anga ya jamii husika? Fauka ya hayo, nadharia hiyo imetumiwa kwa azma ya kufafanua mchango wa matini hizo katika uibuaji, usawiri na uwasilishaji wa maudhui katika ushairi wa Kiswahili.

Kadhalika, nadharia ya Semiotiki imechangia ile ya Fomula ya Kisimulizi kwa ambavyo imesaidia katika kuhakiki na kufafanulia kauli au miundo ya lugha iliyotumika katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Kimsingi, nadharia ya Semiotiki huzingatia miundo ya lugha zijengwazo kwa ishara ambazo huweza kufasiriwa na kufafanuliwa na hadhira kwa kurejelea miktadha mahususi ya kitamaduni katika maisha ya jamii.
Semiotiki kama nadharia ya uhakiki ilipata umaarufu baada ya udhaifu wa wanamiundo kudhihirishwa kuanzia mwaka wa 1970. Kwa mfano, baadhi ya wanamiundo walijikita

zaidi katika kuhakiki na kufafanua miundo ya lugha iliyotumika katika mawasiliano ya kijamii badala ya kubainisha wazi uwiano uliopo baina ya matumizi ya miundo hiyo kama ishara na kile ambacho huwakilishwa katika utamaduni wa jamii (Peck na Coyle 1984, Hawkes 1977 na Pierce 1977). Kwa mujibu wa Scholes (1982) na Urban (1992) ni kwamba, nadharia ya Semiotiki si ngeni bali ilidokezewa hapo mwanzoni na mwanaisimu, Ferdinand de Saussure (1857-1913). Kadhalika, misingi na mihimili hiyo iliweza kufafanuliwa kwa uwazi zaidi na Charles Pierce (1977). Kwa mujibu wa Ferdinand de Saussure, lugha ni mfumo wa ishara. Katika muktadha huo, ushairi na fasihi kwa ujumla huwa ni zao la utamaduni wa jamii na ni sanaa ambayo hutumia ishara teule za lugha.

Kwa kuifafanua zaidi miundo hiyo ya lugha, Ferdinand de Saussure (keshatajwa) aliweza kutofautisha dhana ya ishara kwa pembe mbili zilizowiana: kiashiria na kiashiriwa. Hii humaanisha kwamba, kiashiria (matini, kauli teule au mifumo ya maneno maalumu) haiwezi kufasirika au kueleweka kwa kuzingatia matumizi yake katika muktadha wa mahusiano yake na viashiria vingine. Katika mantiki hiyo, kila kiashiria kina upatanisho wake katika kiashiria (vipengele vya utamaduni). Kama alivyoeleza Scholes (1982), miundo ya lugha hujenga utaratibu au kielelezo cha kudhihirishia utamaduni na taratibu za kijamii. Kulingana na wanamiundo, chombo cha kuwasilishia ujumbe katika jamii ni miundo mahususi ya lugha; lakini ujumbe ambao huibua matumizi ya miundo ya lugha haubainishwa wala haukufafanuliwa.

Kutokana na upungufu huo wa wanamiundo, kulizuka nadharia ya Semiotiki. Ni Charles Pierce (1977) aliyeibainisha zaidi dhana ya kiashiria kama yenye yambwa na kifasiri.

Katika ufafanuzi huo, ilidhihirishwa kwamba; kila ishara, yaani matumizi ya matini au kitendo cha kijamii huweza kuchochea tafakuri ya kurejelea au kupatanisha na muktadha wa utamaduni na uhalisi wa jamii. Kilichokisisitizwa ni kwamba, viashiria ambavyo hutumiwa katika jamii huwa vimejengwa katika misingi ambayo huweza kufafanuliwa na kufasiriwa. Kwa hivyo, matumizi hayo hayawezi katu kutenganishwa na miktadha ya utamaduni na uhalisi wa jamii.

Kwa kurejelea ufafanuzi wa Pierce umebainisha kwamba, viashiria mahususi vya lugha kama vile methali vilivyojengwa katika tamathali za usemi hutumika mno katika mawasiliano ya jamii. Kwa hivyo, kauli hizo teule huakisi maana dhihiri na maana batini. Kifasihi, methali au kauli teule huweza kufasirika kwa namna mbalimbali kutegemea maana iliyokusudiwa kuwasilishwa katika utanzu mahususi. Vile vile, kisemiotiki, matumizi ya methali huweza pia kuhamishiwa au kutekelezwa kupitia kwa viashiria vingine ambavyo hubainika katika tamathali za usemi au miundo mingine ya lugha ambayo pia ni muhimu. Mabadiliko ya aina hiyo inapotokea hudhihirisha kwamba, kuna uwezekano wa kutumia au kutotumia methali katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Aidha, dhima ya methali inapotekelezwa kupitia kwa miundo mingine ya lugha katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi huweza kuchukuliwa kuwa ni chanzo cha mabadiliko ambayo huweza kuathiri matumizi, mitindo na miundo ya lugha katika kazi ya fasihi hususa, ushairi wa Kiswahili.

Kitengo cha nadharia ya Semiotiki iliyohusu fasihi iliweza kutumiwa hapo mwanzoni katika miaka ya 1960, ambapo Jacobson aliibua kanuni au vipengele sita vya msingi

vilivyohusishwa katika mawasiliano ya kifasihi. Vipengele hivyo, ni kama vile: mtunzi, mpokezi, muktadha, matini, utanzu na lugha. Kulingana na mhakiki huyo, mtunzi wa fasihi hususa, ushairi huwasilishwa kwa hadhira kupitia kwa matini teule ambazo hujibainisha katika tamathali za usemi. Kwa kuzingatia utungo wa ushairi, ilibainishwa kuwa, miundo ya lugha ambayo hutumika zaidi katika uwasilishaji wa utungo huwa ni ya kitamathali. Kadhalika, tamathali hizo huweza kuwa za aina mbili: kauli za kitaashira (metonomia) na kauli za kiisitiari (kimafumbo). Kulingana na ufafanuzi huo, lugha ya kitamathali na hasa hasa ile ya kiisitiari inapotumiwa katika utunzi wa ushairi, huukoleza zaidi ujumbe ambao huwasilishwa kwa kujenga mazingira ya usaili na utafakari katika akili ya hadhira. Kwa mfano, mshairi huweza kutumia ubadilishaji wa maneno ya lugha yaliyozowewa katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi. Kwa njia hii, ujumbe unaowasilishwa katika ushairi huwa bayana na usiokuwa na utata wowote. Aina nyingine ya ubadilishaji wa maneno, ni ule wa kiisitiari ambapo, kimatumizi kauli au maneno hupewa sura mpya. Kulingana na Jakobson, ubadilishaji huo utokeapo katika uwasilishaji wa shairi, lugha hiyo huwa ni ya mshindo, kuvutia, kutafakarisha na kuliathiri sikio la hadhira. Kwa njia hiyo, ujumbe ambao huwasilishwa huwa si wa moja kwa moja bali ni wa kiisitiari au kimafumbo.

Kilichosisitizwa hapa ni kuwa, lugha ya kiisitiari ni muhimu zaidi na hutumiwa kwa makusudi katika uwasilishaji wa tanzu mbalimbali za fasihi kama vile, ushairi. Kwa sababu, matumizi hayo humtosa msomaji au msikilizaji katika utafakari ili kuweza kuupata ujumbe ambao umewasilishwa kwa njia ya utata na kimafumbo. Kulingana na Wafula (1994), kuwepo kwa sanaa, yaani fasihi, ni thibitisho kuwa matumizi ya kauli za

lugha huweza kufinyangwa upya au kiumbuji kwa kuzingatia mitindo ya kitamathali ili kuuwasilishia ujumbe ambao umekusudiwa. Kadhalika, methali huwa zimeundwa kiustadi kwa maneno machache lakini ufafanuzi wake ni mpana kulingana na miktadha ya kimatumizi katika jamii. Kwa hivyo, watunzi wana hiari ya kutumia idadi chache ya maneno ili kubainishia au kuwasilishia maana pana. Zaidi ya hayo imekaririwa kwamba, matumizi ya methali au lugha ya kitamathali inapotumika katika utanzu wowote wa fasihi hudhihirika na hufasirika vyema kwa kuzingatia miktadha mahususi ya mawasiliano na utamaduni wa jamii.

Kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki, mihimili yake ni kama ifuatayo:

i. Ishara hutumiwa katika kujenga ruwaza au miundo maalumu. Kwamba, kauli za lugha huweza kuwa ni tamko au neno moja ambapo kwa kushirikiana na ishara zingine ili kuunda mfumo wa ruwaza ya kauli katika mawasiliano ya watu.

ii. Ishara au matini zitumikazo katika ushairi huweza kuwa za moja kwa moja au za kiisitiari. Iwapo ni ishara za kiisitiari, ufafanuzi wake hujikita katika miktadha ya kitamaduni na uhalisi wa jamii.

iii. Ishara hutumiwa katika miktadha ya ishara zingine. Kwamba, matumizi ya ishara moja haina nguvu au maana iwapo haikutumiwa sambamba na ishara zingine.

iv. Ishara zitumiwazo katika ushairi huwa ni vipengele vya lugha ambavyo hujirejelea, ni rahisi kutambulika na kukumbukika katika kazi yoyote ya fasihi.

v. Ishara hutumiwa mahususi kuwasilishia ujumbe katika kazi maalumu ya fasihi kwa kuzingatia muktadha wa utamaduni wa jamii.

Mihimili ya nadharia ya Semiotiki imeunufaisha utafiti huu kwa ambavyo ilinuiwa kutathmini matumizi ya methali kama miundo au kauli mahususi za lugha katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Kwa vile methali ni ishara zilizojengwa katika tamathali za usemi, huweza kufasiriwa vyema kwa kuzingatia vipengele vya utamaduni na tajiriba ya jamii. Kwa hivyo, methali ni aina ya tamathali ambazo zina maana dhahiri na batini. Kwa hivyo, umuhimu huo hutokana na upatanisho wa matumizi yake ambayo hupatikana ndani na nje ya miktadha ya ushairi. Kadhalika, nadharia ya Semiotiki imetumiwa katika utafiti huu kwa kujenga muktadha wa kufasiri miundo mahususi ya lugha iliyoibuniwa na jamii na ile iliyobuniwa kibinafsi katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Isitoshe, nadharia hiyo imetumiwa kufafanulia dhana kwamba kutumiwa au kutotumiwa kwa methali katika ushairi hutokana na hisi za mtunzi kwa kuzingatia mabadiliko ya kitamaduni na uhalisi wa jamii. Vile vile, nadharia hiyo huakisi matini au miundo teule ambayo hupatikana katika mawasiliano ya jamii. Kwa mtazamo wa utafiti huu imemaanisha ya kwamba, dhima na utendakazi wa mojawapo ya kauli au miundo ya lugha huweza pia kushughulikiwa kupitia kwa aina nyinginezo za lugha. Kwa hivyo, mtafiti amezingatia mtazamo huo ili kuhakiki jinsi kutumia au kutotumia kwa methali kunavyoweza kuwa ni mbinu ya kutathmini mabadiliko ya kimtindo katika ushairi wa Kiswahili.

Vipengele vya nadharia ya Fomula ya Kisimulizi na Semiotiki vimetumiwa na mtafiti kutathmini nafasi ya methali katika utunzi na pia kufafanulia mabadiliko katika ushairi wa Kiswahili. Kimsingi, nadharia hizo huwiana na hukamilisha, kwa ambavyo huzieleza, huzichanganua na huzifasiri kazi za fasihi kwa kuzingatia muktadha wa utamaduni na uhalisi wa maisha ya watu katika jamii. Kwa sababu, vipengele vya nadharia hizo ni vingi mno, mtafiti ameshirikisha baadhi yazo ili kujengea mihimili mahususi ambayo iliweza kutumiwa katika kuuelekeza utafiti huu. Mihimili hiyo mahususi iliyozingatiwa katika utafiti huu ni kama ifuatayo:

i. Matini teule za kimapokeo kama vile methali, hutumika kama chanzo au msingi wa utunzi katika ushairi.

ii. Mtunzi wa ushairi ana muda mfupi wa maandalizi na wa kujieleza. Kwa hivyo, matini au miundo teule za lugha inayobuniwa kwa makusudi au na jamii hutumika ili kujengea mishororo au mistari katika utungo.

iii. Matini teule zilizotumika katika ushairi hujengeka katika tamathali za usemi. Kwa hivyo, ufafanuzi na ufasiri wake huzingatia miktadha mahususi ya utamaduni na uhalisi wa jamii.

iv. Mtunzi wa ushairi hutumia matini maalumu ambazo hujirejelea, kwa lengo la kuusawiri na kuuwasilishia ujumbe kimuhtasari kwa njia ambayo hugusa hisi na huiathiri hadhira.

v. Dhima ya kauli teule ya kimapokeo huweza kuhamishiwa na kutekelezwa kupitia kwa matini nyinginezo zilizobuniwa kwa makusudi au kibinafsi kutegemea mabadiliko ya kitamaduni katika jamii.

1.9 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Utafiti huu umeshughulikia maendeleo na mabadiliko ya kimtindo ambayo huhusishwa katika ushairi wa Kiswahili nchini Kenya na Tanzania. Tungo hizo zimekuwa zikitungwa na zikihifadhiwa kimaandishi kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1960 na kuimarishwa zaidi katika miaka ya kati ya mwaka 1970 hadi wakati wa sasa. Katika kipindi hicho, mabadiliko mbalimbali ya kitamaduni na ya kijamii ambayo yameza kutokea na kuathiri mitazamo ya jamii kuhusu utamaduni na maisha kwa ujumla. Katika muktadha wa fasihi, hicho kiliokuwa ni kipindi muhimu katika historia ya mataifa hayo. Kwa sababu, mataifa hayo yalikuwa yamepata uhuru na mwongo mmoja ulikuwa umepita. Pia, ni katika kipindi hicho ambapo watunzi mbalimbali wa ushairi wa Kiswahili waliweza kutunga mashairi kwa mitazamo mitatu: yaliyozingatia zaidi arudhi za kimapokeo; yaliyozingatia kiasi fulani cha arudhi na yasiyozingatia kabisa arudhi hizo. Ingawa mashairi hayo yametungwa kwa kuzingatia mitindo tofauti ya uwasilishaji. mashairi yote hayo yamechangia katika usawiri na uwasilishaji kuhusu uhalisi wa jamii.

Nchi za Kenya na Tanzania ziliteuliwa kwa ambavyo ushairi wa Kiswahili umestawishwa kwa kiwango kikubwa na umeendelea kutumiwa kama nyenzo ya kuhifadhia utamaduni na kupitishia maadili ya jamii. Kadhalika, kuna washairi wengi wa Kiswahili katika nchi hizo ambao wamechangia si haba katika uwanja huo. Hata hivyo, ni washairi sita tu ambao walizingatiwa katika utafiti huu kuwa kiwakilishi cha washairi wengine maarufu waliopatikana katika kipindi hichona hadi wakati wa sasa. Washairi hao ni: Abdilatif Abdalla, Akilimali K.H.A. Snow-White, Alamin Mazrui, Said Ahmed Mohamed, Kithaka wa Mberia na Euphrase Kezilahabi.

Watunzi hao waliteuliwa kwa makusudi. Kwa sababu, wamezingatia au hawakuzingatia kwa uwazi matumizi ya methali katika uwasilishaji wa mashairi yao. Kwa mfano, Abdilatif Abdalla na Akilimali K.H.A. Snow-White wametumia methali kwa wingi katika tungo zao. Kwa upande mwingine, Alamin Mazrui na Said Ahmed Mohamed wametumia methali chache katika tungo zao. Zaidi ya hayo, wasanii kama vile Kithaka wa Mberia na Euphrase Kezilahabi wametumia methali chache zaidi na hata pale zilipotumiwa, huwa ni kama kauli mojawapo katika uwasilishaji wa mashairi yaliyopatikana katika hifadhi za diwani zao.

Ingawa washairi hao teule wametunga mashairi mengi ambayo hupatikana katika zaidi ya diwani moja, utafiti huu ulizingatia mashairi ambayo yalipatikana katika diwani moja moja kwa kila mtunzi. Kwa hivyo, mashairi yaliyochanganuliwa katika utafiti huu ni yale yaliyotokana na diwani mahususi zifuatazo:

i. Mohamed, S.A. (2002): *Jicho la Ndani*

ii. Wa Mberia, K. (2001): *Bara Jingine*

iii. Mazrui, A. (1994): *Chembe cha Moyo*

iv. Snow-White, K.H.A. (1974): *Usanifu wa Ushairi*

v. Kezilahabi, E. (1974): *Kichomi*

vi. Abdalla, A. (1973): *Sauti ya Dhiki*

Kwa hivyo, kupitia kwa diwani hizo za ushairi wa Kiswahili, mtafiti aliweza kupata data zilizohusishwa katika uchanganuzi wa dhima ya methali katika ushairi wa Kiswahili.

1.10 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulihusisha utafiti wa maktabani na nyanjani ili kupata data ya msingi na ya upili kuhusu dhima ya methali katika uainishaji wa ushairi wa Kiswahili.

A. Ukusanyaji wa Data

1. Utafiti katika Maktaba

Utafiti huu kwa kiasi kikubwa umefanywa katika maktaba za kitaifa na za vyuo vikuu zilizopatikana Afrika Mashariki hususa, Kenya na Tanzania. Maktaba hizo ni kama vile: Chuo Kikuu cha Egerton, Kenyatta, Nairobi, Moi na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Maktaba hizo zimehifadhi makala, tasnifu, majarida, vitabu na machapisho muhimu yaliyohusu tafiti mbalimbali zilizowahi kufanywa kuhusu methali na ushairi wa Kiswahili.

Kwa hivyo, kupitia kwa usomaji, mtafiti aliweza kuteua diwani zilizohifadhi mashairi yaliyochanganuliwa. Pia, mtafiti alipata kuelewa mazingira na miktadha iliyoibua matumizi ya methali katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Pale ambapo ilibainika kwamba baadhi ya washairi hawakutumia methali, mtafiti alipata maelezo ya msingi kuhusu miundo mingine ya lugha iliyoibuliwa kibinafsi na kutumiwa katika uwasilishaji wa mashairi.

Kadhalika, data ya upili ilijenga msingi wa kufafanua na kutathmini dhima ya methali katika ushairi wa Kiswahili. Aidha, data hizo zilitumiwa kama kielelezo cha kutambua sababu ya kutumiwa kwa methali katika mashairi hayo. Endapo baadhi ya washairi

hawatumia methali katika tungo hizo, utafiti huu ulifafanua siyo tu sababu za kutotumia methali bali pia kuionyesha na kuieleza miundo hiyo iliyotumiwa kuwa mbadala. Kadhalika, maelezo yaliyopatikana maktabani yaliweza kukadiria nadharia ambazo zilikuwa mwafaka katika utafiti huu.

2. *Utafiti* wa Nyanjani

Utafiti wa nyanjani ulizingatiwa ili kupata data ya upili ambayo ilichangia maelezo yaliyopatikana kupitia kwa udurusu wa maktabani kuhusu matumizi ya methali na kauli nyinginezo zilizohusishwa kwa makusudi katika ushairi wa Kiswahili. Kimsingi mpaka wakati huu wa sasa, ushairi wa Kiswahili ni utanzu ambao ni hai na huendelea kutungwa kimasimulizi na kimaandishi kwa kuzingatia miktadha halisi ya maisha na utamaduni wa jamii. Kwa hivyo, mtafiti alipata habari kamili na maelezo yaliyohusiana na miktadha ambamo washairi hutumia au hawatumia methali kwa uwazi kama mbinu ya utunzi na ya uwasilishaji wa maudhui.

Kadhalika, ushairi ambao huwasilishwa kimaandishi, aghalabu hukusudiwa kughaniwa, kusomwa kwa sauti au kutongolewa kimasimulizi ili ujumi ulioibushwa kutokana na matumizi ya lugha kuweza kudhihirika kwa hadhira. Vile vile, methali kama kipengele mahususi cha lugha, hutumiwa mno katika utunzi wa ushairi simulizi na andishi.

Ili kutekeleza shughuli hiyo, mtafiti alizuru vitongoji viwili vinavyopatikana katika mwambao wa Kenya na Tanzania. Nchini Kenya mtafiti aliweza kuzuru kitongoji cha Kibokoni na nchini Tanzania mtafiti alizuru kitongoji cha Kinondoni. Kutokana matokeo

ya utafiti wa kimajaribio uliofanywa hapo awali, vitongoji hivyo vina ithibati ya wasanii ambao hutunga na huwasilisha tungo zao kimasimulizi. Kimsingi, ushairi simulizi hutumika mno miongoni mwa jamii ya vijijini hasa katika sherehe muhimu za kijamii kama vile jando, unyago na arusi (Okpewho 1992). Kadhalika, kauli za kimapokeo ndizo hutumika zaidi katika tungo za kimasimulizi (Nagler, 1974). Aidha, mmoja kati ya washairi waliozingatiwa, yaani Abdilatif Abdalla alitunga mashairi hayo kwa kuzingatia mazingira na utamaduni wa Waswahili wa pwani ya Kenya. Kwa ambavyo mshairi huyo kwa sasa huishi Ujerumani, mtafiti aliwasiliana naye kupitia kwa barua pepe na pia kumtumia maswali ya hojaji. Vile vile, mtafiti aliwahoji baadhi ya watunzi mashuhuri wa ushairi wa Kiswahili. Washairi hao ni wale ambao hutunga mashairi na kuyawasilisha kimasimulizi kwa wakati wa sasa. Pia, baadhi ya watunzi hao huwa wana wanafunzi ambao hufundishwa taratibu ambazo hupaswa kuzingatiwa katika kutunga mashairi hayo.

Katika mji wa Dar es Salaam nchini Tanzania, mtafiti aliwahoji baadhi ya watunzi ambao huzingatia methali chache na wale wasiotumia kabisa kipengele cha methali katika tungo. Hao ni wale ambao kazi zao zilihusishwa au hazikuhusishwa moja kwa moja katika utafiti huu. Maoni hayo yalijenga msingi wa kufafanulia sababu zilizowapa kariha au ilihamu ya utunzi. Aidha, mtafiti aliwahoji baadhi ya wahakiki walioshughulikia diwani mahususi zilizohusishwa katika utafiti huu. Lengo la kuwahoji wahakiki lilikuwa ni kuelezwa kuhusu sababu zilizowaelekeza wasanii kutumia kauli teule na maudhui ya kijumla yalioibuliwa katika kazi hizo asilia. Vile vile, mtafiti aliuzuru mji wa Nairobi kwa azma ya kuwahoji baadhi ya watunzi wa ushairi wa Kiswahili waliozingatia au kutozingatia arudhi za kimapokezo. Aidha, miji hiyo miwili yaani Nairobi na Dar es

Salaam ilizuriwa kwa ambavyo ilikuwa rahisi kuwafikia baadhi ya wataalamu wa lugha na wahakiki wa fasihi.

3. Data za Kimsingi

Data iliyohusishwa katika utafiti huu iliteuliwa kwa kuzingatia mbinu kusudio. Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu na umeendelea kutungwa kimasimulizi au kwa kutumia hati za maandishi katika uwasilishaji wa tungo hizo.

Hata hivyo, utafiti huu ulizingatia ushairi wa Kiswahili uliotungwa na kuhifadhiwa kimaandishi katika Afrika Mashariki kati ya mwaka 1970 hadi sasa. Katika kipindi hicho, wasanii wengi maarufu wamekuwa wakitunga tungo zao kwa kuzingatia utamaduni na uhalisi wa jamii mbalimbali za Afrika Mashariki.

Ingawa kuna wasanii wengi mashuhuri waliotunga mashairi ya Kiswahili na kuchapisha zaidi ya diwani moja, si diwani zao zote zilizoshughulikiwa katika utafiti huu. Utafiti huu umezingatia mashairi teule ambayo hupatikana katika diwani za wasanii sita tu. Kutokana na diwani hizo, ni mashairi manne tu ndiyo yaliyohakikiwa kwa kila mtunzi. Kwa hivyo, utafiti huu ulihusisha jumla ya mashairi ishirini na manne. Aidha, data iliyochanganuliwa ilitokana na makundi matatu mahususi ya ushairi wa Kiswahili kama ifuatavyo:

i) Ushairi wa Kiswahili waliotumia methali kwa wingi. Kundi hili limewakilishwa na ushairi wa Akilimali K.H.A. Snow-White (1974) *Usanifu wa Ushairi* na Abdilatif Abdalla (1973) *Sauti ya Dhiki*.

ii) Ushairi wa Kiswahili uliotumia methali chache katika utunzi na uwasilishaji wake. Kundi hili limewakilishwa na Said Ahmed Mohamed (2002) *Jicho la Ndani* na Alamin Mazrui (1988) *Chembe cha Moyo*.

iii) Ushairi wa Kiswahili uliotumia methali chache zaidi au usiotumia kabisa methali katika utunzi na uwasilishaji wake. Kundi hili limewakilishwa na Kithaka wa Mberia (2001) *Bara Jingine* na Euphrase Kezilahabi (1974) *Kichomi*.

Kama ilivyobainishwa, watunzi hao teule katika makundi hayo matatu wametoka Kenya na Tanzania. Sababu mahususi ya kuwateua watunzi hao ni kwamba, utanzu wa ushairi wa Kiswahili umekuzwa na umestawishwa kwa kiwango kikubwa katika nchi hizo kuliko nchini Uganda. Vile vile, lugha ya Kiswahili hutumika zaidi miongoni mwa wananchi katika nchi hizo kama lugha ya taifa pia kama na rasmi.

B. Mbinu za Ukusanyaji Data

Udurusu wa diwani mbalimbali zilizochapishwa nchini Kenya na Tanzania kulimsaidia mtafiti kuteua diwani zilizohusishwa katika utafiti huu. Pia, katika ukusanyaji wa data, mtafiti alitumia mbinu mahususi: maswali ya hojaji, utazamaji na usaili wa ana kwa ana. Maswali ya hojaji yalitayarishwa na kutumwa moja kwa moja kwa waliokusudiwa kwa njia ya posta, kipepesi, barua pepe au kupelekwa moja kwa moja kwa walengwa. Mbinu ya maswali ya ana kwa ana ilitumiwa kwa kuzingatia walengwa wa makundi matatu maalumu kama ifuatavyo:

i. Washairi waliotumia methali nyingi katika mashairi yao.

ii. Washairi waliotumia methali chache katika mashairi yao.

iii. Washairi waliotumia methali chache zaidi au kutotumia kabisa methali katika mashairi yao.

Kwa ujumla utafiti huu ulizingatia walengwa thelathini tu kama ifuatavyo:

i. Washairi wanne kutoka kila kikundi (kama ilivyobainishwa katika uteuzi wa sampuli). Waliozingatiwa ni wale ambao wametunga wamechapisha diwani moja ya ushairi au zaidi. Hata hivyo, waliohusishwa walikuwa ni watunzi wa kazi asilia ambazo zilihusishwa na wale ambao kazi zao hazikuhusishwa moja kwa moja katika utafiti huu.

ii. Washairi sita ambao hutunga na huwasilisha kimasimulizi tungo zao za ushairi.

iii. Washairi sita ambao wametunga tungo zao na kuchapishwa katika kusanyiko la mashairi, majarida au magazetini.

iv. Wataalamu au wahakiki sita wa fasihi. Aidha, waliohusishwa ni wahadhiri wa vyuo vikuu na wahakiki wa fasihi kwa ujumla.

Data ambazo zilipatikana kupitia kwa usaili wa ana kwa ana zilihifadhiwa katika kinasa sauti, video au kunukuliwa moja kwa moja. Kundi la wahojiwa ambalo hutunga na kuwasilisha mashairi yao kimasimulizi, kwa kuwa wengi wao hawajui kusoma wala kuandika; mbinu ya usaili wa ana kwa ana ilisaidifu. Mbinu ya hojaji ilitumiwa kwa walengwa wanaojua kusoma na kuandika. Kadhalika, mbinu hii ya hojaji ilitumika kwa makusudi kwa ambavyo walengwa wengi walifikiwa kwa muda mfupi na kwa gharama ndogo.

Kwa hivyo, maelezo yaliyopatikana maktabani na nyanjani yalijenga msingi wa kuhakiki na kutathmini matumizi ya methali kama chombo cha utunzi na pia kama mbinu ya kuainishia ushairi wa Kiswahili.

C. Uchanganuzi wa Data

Data ya msingi ilitokana na diwani teule za mashairi zilizotungwa na wasanii teule wa ushairi wa Kiswahili. Data hiyo iliweza kujenga msingi wa kufafanulia namna watunzi walivyotumia methali katika uwasilishaji wa tungo hizo. Kadhalika, maelezo ya maktabani na nyanjani yalitumiwa kama data ya msingi na ya upili kwa lengo la kutathmini kutumika au kutotumika kwa methali katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi huu. Vile vile, data hizo zilitumiwa katika kuainishia ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia dhima ya methali. Maelezo hayo yalihusu matumizi ya kijumla ya methali kama chombo cha utunzi na pia kama mbinu ya kuwasilishia ushairi wa Kiswahili.

D. Uwasilishaji wa Data

Data iliyopatikana katika utafiti, ilichanganuliwa kwa kuzingatia maswali na madhumuni ya utafiti kwa uelekezo wa nadharia zilizotumiwa. Mwishowe, mtafiti aliwasilisha matokeo ya utafiti kwa lugha ya nathari huku akitoa mifano ya kushadidia hoja zilizotolewa kuhusu dhima ya methali katika kuainishia ushairi wa Kiswahili.

Aidha, uwasilishaji katika tasnifu umezingatia sura saba kama ifuatavyo:

Sura ya Kwanza

Sehemu hii imejumuisha: swala la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu za kuchagua swala la utafiti, upeo, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti.

Sura ya Pili

Matumizi ya methali kama fomula ya utunzi katika ushairi wa Kiswahili.

Sura ya Tatu

Uchanganuzi wa ushairi ya kimapokeo kwa lengo la kutathmini matumizi ya methali.

Sura ya Nne

Uchanganuzi wa ushairi wa kati kwa lengo la kutathmini matumizi ya methali.

Sura ya Tano

Uchanganuzi wa ushairi huru kwa lengo la kutathmini matumizi ya methali.

Sura ya Sita

Ainisho la ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia matumizi ya methali.

Sura ya Saba

Hitimisho na mapendekezo kutokana na uchanganuzi wa matokeo kuhusu dhima na utendakazi wa methali katika ushairi wa Kiswahili.

SURA YA PILI

METHALI KAMA FOMULA YA UTUNZI KATIKA USHAIRI WA KISWAHILI

2.0 UTANGULIZI

Sura hii imefafanua namna washairi wa Kiswahili walivyotumia kipengele cha methali kama fomula ya utunzi na uwasilishaji katika tungo zao. Mawazo katika tungo za ushairi huibuliwa na huwasilishwa kwa kuzingatia utaratibu maalumu. Kwa mfano, mshairi huteua kauli ambazo hutumika katika usawiri na uwasilishaji wa mawazo huisika. Zaidi ya hayo, mtunzi hufahamu ni kauli gani ambazo hupaswa kutumika mwanzoni au baadaye katika uwasilishaji wa utungo. Katika muktadha huo, mtunzi stadi huhakikisha kuwa mawazo hudhibitiwa kwa miundo teule ya kauli zilizotumiwa. Katika mazingira ya Afrika Mashariki, ushairi wa Kiswahili una historia ndefu (Mulokozi na Sengo 1995). Kwa mfano, hapo awali tungo zilikuwa zikitungwa, kuwasilishwa kimasimulizi na kuhifadhiwa katika bongo za watu. Hati za uandishi zilipoanza kutumika, baadhi ya tungo zilianza kutungwa na kuwasilishwa kimaandishi kwa kuzingatia arudhi za kimapokeo. Kwa wakati wa sasa, mashairi ya Kiswahili hutungwa ama kwa kuzingatia au kutozingatia arudhi za kimapokeo. Hata hivyo, makundi hayo mawili huwakilisha ushairi wa Kiswahili kwa ambavyo huibua na huakisi utamaduni na uhalisi wa maisha ya jamii ya Afrika Mashariki.

Kadhalika, utunzi wa ushairi huanza kwa hisi au mchomo ambao husababishwa na athari za kimazingira, utamaduni na uhalisi wa maisha katika jamii (Mulokozi na Kahigi 1982). Chombo cha kuwasilishia hisi hizo huwa ni miundo teule ya lugha hupatikana kwa

urahisi katika mawasiliano ya jamii. Miundo hiyo, huweza kuwa ni ile ambayo imeibuliwa kwa makusudi au kibinafsi na kutumiwa katika mashairi ya Kiswahili.

Isitoshe, hisi ambazo huibuliwa sharti ziambatane na mitazamo ya fikra za watunzi ambapo huwa ni dira mahususi ya kuwaongoza katika kuteua kauli mwafaka zinazosaidia katika kusawiri na kueleza mawazo yaliyonuiwa kuwasilishwa. Kwa sababu hiyo, mshairi huweza kujenga uhusiano wa karibu na hadhira kusudiwa. Kimsingi, hadhira ndiyo huwasilishwa na huufasiri ujumbe uliosawiriwa. Utungo huo huhitaji kufungamanishwa na umbuji wa fani na maudhui ambayo huwasilishwa (Zubkova-Bertoncini 2008). Kwa hivyo, mshairi hupaswa kuwa makini na mahiri katika kuteua methali, msamiati au miundo ya lugha ambayo huweza humsaidia katika utunzi na uwasilishaji wa ujumbe. Kwa kutumia kauli teule ziliundwa katika tamathali za usemi, ushairi huweza kuwasilishwa kimafumbo, kiisitiari na kitaswira. Kimsingi, lugha ya Kiswahili au nyingine yoyote ile, huwa ni kanzi ya miundo maalumu na vipengele mbalimbali vya lugha. Hata hivyo, sura hii imezingatia matumizi ya methali kama fomula ya kuundia na kuibulia kauli nyinginezo, miundo na mitindo iliyotumiwa katika uwasilishaji wa ujumbe katika ushairi.

2.1 FANI KATIKA UTUNZI NA UWASILISHAJI WA USHAIRI

Ushairi ni utanzu wa fasihi ambao hutofautiana na riwaya na tamthilia hasa katika umbo na matumizi maalumu ya lugha. Wakati ambapo fasihi ya kinathari kama vile tamthilia na riwaya hutumia lugha ya mjazo au ya mtiririko, ushairi hutumia zaidi lugha ya mkato kama nyenzo ya kuwasilishia maudhui kitaswira, kimafumbo na kimuhtasari (Gibbe 1990

na Senkoro 1988). Hali hiyo imetokana na hoja kwamba, mshairi huwa hana wakati mwingi wa kujieleza au kufafanua zaidi maelezo na mifano iliyotolewa. Kadhalika, ushairi wa Kiswahili una matumizi ya upeo wa juu wa lugha hasa ukilinganishwa na aina zingine za fasihi andishi. Kwa hivyo, kila kipengele cha lugha kilichoteuliwa na kutumiwa katika utungo huo, hushikilia nafasi muhimu katika uwasilishaji wake. Kwa sababu, utamu wa lugha haupo tu katika maudhui au kilichoelezwa bali kwa ujumi wa lugha huzidi kutokana na umbuji au ustadi uliotumiwa katika uwasilishaji wa maudhui (Kunemah 2008 na Khatib 1999:76). Isitoshe mgodi wa fasihi ya Kiswahili; hasa katika tanzu hai za tamathali za usemi, ni dafina isiyoweza kuchimbwa na kumalizika. Hivyo, utajiri huo hubainika katika tanzu zote za fasihi hususa, ushairi wa Kiswahili. Huo ni ushuhuda wa ukuu wa fasihi ya Kiswahili na uhai wake. Katika mantiki hiyo, mtunzi hutarajiwa awe mwenye umilisi mkubwa wa lugha katika kuuwasilisha ujumbe kwa hadhira bayana au fiche. Katika utunzi wa kazi ya fasihi hususa ushairi wa Kiswahili, lugha ndiyo chombo na malighafi muhimu ambayo hutumiwa katika usawiri na uwasilishaji wa ujumbe.

Kadhalika, mtunzi wa ushairi huwa ana hiari ya kuteua kauli au miundo mahususi ya lugha iliyopo katika mawasiliano ya jamii na kuipuuza ile ambayo huihisi kwamba haitaweza kusaidia katika ubainishaji na uelekezaji wa mawazo, maono na fikra katika utungo. Uteuzi huo huzingatia zaidi athari ambayo imekusudiwa kuibuliwa katika akili, kwa azma ya kuielekeza mielekeo ya hadhira. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mtunzi wa ushairi hana wakati mwingi wa kueleza au kufaragua kwa kina mawazo na hisi zake (Pierce 1977 na Propp 1968). Kwa hivyo, mtunzi hutumia kauli za

mkato au miundo mahususi za lugha kama vile methali na semi nyinginezo ambazo hujengwa katika tamathali za usemi ili kuweza kuyadhibiti na kuyasawiri mawazo ambayo huwasilishwa kimuhtasari.

Kimsingi, mtunzi wa ushairi wa Kiswahili hupata msukumo au ilhamu ya kuutunga kutokana na tajiriba ambayo hufungamana kabisa na uhalisi wa utamaduni na maisha ya jamii (Imbosa 1990, Noor 1988 na Chacha 1987). Fauka ya hayo, miundo na vipengele mahususi vya lugha ambavyo hutumiwa katika ushairi sharti kuweza kusaidia katika uwasilishaji wa ujumbe uliokusudiwa. Ujumbe unapomfikia msomaji ndipo hueleweka kwa yakini kwamba, mtunzi ameweza kufanikiwa katika kuwasiliana na hadhira yake. Aidha, mshairi wa Kiswahili ambaye hupuuza uteuzi mwafaka wa miundo ya lugha huenda shairi lake likawa chapwa, chakavu na la kuchosha. Matokeo ni kwamba, shairi linalowasilishwa huenda lisiwe lenye kugusa hisi. Hadhira isipopata kishawishi cha kuupenda ushairi kwa kunga zilizotumiwa, ujumbe kusudiwa hautakuwa umewasilishwa ipasavyo (Darvin na Wamuhu 1994 na Mulokozi na Kahigi 1982). Kulingana na nadharia ya Semiotiki ni kuwa, miundo mwafaka ya lugha ni ile ambayo husheheni sitiari, ishara na tamathali za usemi zinazochochea usaili na tafakuri ya hadhira. Kwa hivyo, ni muhimu hadhira kuweza kupata kichocheo cha kujiuliza maswali ya kiutafakari kila wakati inapousoma utungo huu. Katika utunzi, miundo mahususi ya kauli zilizotumiwa huwa ni ile ambayo husaidia katika ufasiri wa ujumbe kwa kuzingatia miktadha mbalimbali ipatikanayo ndani ya ushairi na ile iliyopo katika uhalisi wa maisha ya jamii.

Kwa kutumia kauli mahususi hususa methali; hadhira huweza kufunuliwa kwa ubunifu ukweli wa maisha ambao huafiki miktadha ya uhalisi wa maisha na utamaduni wa jamii (Wamitila 2008 na Lo Liyong 1992). Lugha ya Kiswahili kama vile ilivyo katika lugha mbalimbali za kilimwengu, ina ukwasi mkubwa wa semi fupifupi kama vile methali, nahau na misimu. Semi ambazo hutumiwa katika uwasilishaji, huufanya utungo kutajirika zaidi kiuchambuzi (Mosha 2002 na Senkoro 1988). Kwa hivyo msomaji anapoichambua miundo hiyo, huweza kuubainisha na kuupata ujumbe uliokusudiwa.

Mshairi anapotumia methali kama fomula au chombo cha utunzi na uwasilishaji isichukuliwe kuwa ni hali ya kubainisha tu umahiri au ukwasi wa lugha, bali pia ni msingi wa kufaulisha upokezi wa ujumbe (Hawkes 1979, Olsen 1973 na Nowottny 1968). Kutokana na matumizi ya methali, ushairi wa Kiswahili huweza kuwa ni utanzu wenye dhima maalumu ya kuelimisha, kutafakarisha na kuhifadhi amali adimu za utamaduni wa jamii. Kimaudhui, matumizi ya methali katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili hushabihiana na vitendawili, lakini huwa ni tofauti na semi nyinginezo ambazo ni fupi fupi kama vile nahau na misimu ambazo huzaliwa, hukuzwa, hudhofishwa au hufishwa (Wamitila 2006 na Mulokozi 1975). Kwa hivyo, zinapotumika katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi hutegemea zaidi kipindi au wakati maalumu na dhima wazo katika jamii. Iwapo uhalisi wa maisha na utamaduni wa jamii umeathirika au umebadilika kwa namna fulani, semi hizo huenda zisitumike sana katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi. Kwa hivyo, ushairi wa Kiswahili ni utanzu ulio hai.katika mantiki hiyo, kunga au fani zitumikazo huweza kubadilika kutegemea mabadiliko yanavyojiri katika jamii. Kwa hivyo, semi hizo hutumiwa mno katika miktadha

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

mahususi ya kitamaduni, kijamii na ya kihistoria. Endapo pana mabadiliko ya kitamaduni na kijamii, watunzi hao hutumia zile ambazo huchukuana vyema na miktadha ya mabadiliko hayo (Jalala 2008 na Kitogo 2002).

Kutokana na kutumiwa au kutotumiwa kwa methali, ushairi wa Kiswahili huweza kuwa wenye michepuo mbalimbali ya vijitanzu kama vile: ushairi wa kimapokeo, ushairi wa kati na ushairi huru. Kwa ujumla, ushairi wa Kiswahili ni matokeo ya matumizi ya miundo na vipengele mahususi vya lugha katika uwasilishaji wake. Mambo hayo, huufanya utungo kuwasilishwa kwa mitindo tofauti tofauti.

2.1.1. Methali kama Kichepuo cha Kufafanulia Maelezo ya Msingi

Kimsingi, methali ni sanaa ya lugha yenye mpangilio maalumu wa maneno teule yenye umuwala. Hiyo ndiyo sababu, baadhi ya wahakiki wa fasihi wa hapo awali kuchukulia kuwa methali ni ushairi mdogo (Knappert 1979, Allen 1971 na Harries 1962). Kadhalika, methali ni miongoni mwa semi fupifupi ambazo zimebuniwa kutokana na mazingira mahususi ya utamaduni na uhalisi wa jamii. Ingawa methali ni semi fupi fupi zilizojengwa katika tamathali za usemi, maana na matumizi yazo huwa ni pana mno. Kwa hivyo, ujumbe huweza kufasiriwa na kufafanuliwa kwa kuzingatia miktadha mahususi ya utamaduni wa jamii.

Kimaudhui, lengo la matumizi ya methali ni kuusawiri uhalisi wa maisha, kutafakarisha na kuiadilisha jamii (Gesero 2009, Mieder na Sobieski 2003, Osiemo 1997 na Kuhenga 1977). Kutokana na dhima na utendakazi wazo katika jamii, methali zimeweza

kurithishwa kimapokeo kutoka kizazi kimoja hadi kingine (Waihiga na Kagwa 2007, Parker 1974 na Seitel 1972). Kwa hivyo, methali hupaswa kuchukuliwa kama chombo muhimu cha mawasiliano katika jamii. Aidha ufasiri wazo kama ishara au kauli zilizotumika katika ushairi, hujikita katika miktadha ya utamaduni na uhalisi wa jamii.

Kimsingi, methali zimekuwa zikitumiwa katika miktadha ya mawasiliano ya jamii kama mizani ya kuratili ukweli wa maisha, kuhifadhi utamaduni na kufunulia falsafa za jamii kwa njia inayogusa hisi. Lugha ya Kiswahili ina ukwasi mkubwa wa methali ambazo huweza kutumiwa katika kupatanisha na takribani kila muktadha wa jamii (Ndungo 1998 na King'ei 1982). Kwa hivyo, kila tukio katika jamii hupata mshabaha wake katika methali ambazo hushrikishwa katika mawasiliano ya jamii (Kunemah 2008 na Wamitila 2008). Licha ya kwamba methali ni fani mahususi katika mawasiliano ya jamii; hutumiwa pia kama chombo cha utunzi na cha kuibulia ujumbe katika tanzu mbalimbali za fasihi andishi hususa, ushairi wa Kiswahili.

Kwa kuzingatia dhima ya methali, mshairi huweza kupata kwa urahisi sentensi au kauli msingi kuwa dira na kichocheo mwafaka cha kutungia kisa na vile vile kuwa chombo cha kufaragulia mawazo yaliyoakisi utamaduni na uhalisi wa maisha. Kwa kawaida, mtunzi huwa ana mchomo ambao hutokana na tajriba yake katika maisha ya jamii. Mchomo huo wa ndani kwa ndani huhitaji kuwasilishwa kwa kauli au mizungu ya lugha. Kwa kutumia methali, mtunzi wa ushairi huweza kupatanisha matukio na miktadha mbalimbali ambayo hupatikana kwa urahisi katika uhalisi wa utamaduni wa jamii. Kwa ambavyo methali huhitaji kufafanuliwa na kutolewa mifano halisi, mtunzi hupata upenu wa kusawiri na

kufaragua kisa na ujumbe unaowasilishwa. Kadhalika, hadhira huweza kujengewa mazingira dhahiri ya kuuelewa ujumbe hasa kwa kurejelea maelezo yaliyotolewa katika utungo.

2.1.2 Methali kama Kiunzi Cha Usimulizi na Udhibiti wa Muundo

Utunzi wa ushairi wa Kiswahili huzingatia utaratibu maalumu katika usawiri na uwasilishaji wa ujumbe kwa hadhira. Utaratibu huo ni pamoja na jinsi mtunzi alivyotanguliza, alivyofaragua mawazo au hisi zake na hatimaye alivyohitimisha utungo. Katika muktadha wa nadharia ya Fomula ya kisimulizi, mtunzi anapoushughulikia utungo huteua kwa makini baadhi ya maneno au kauli za lugha ili kuweza kujenga msingi wa kujieleza au kujifaragua (Wood 1971 na Whallon 1969). Mtunzi wa ushairi wa Kiswahili, kwa kawaida huwa ana mawazo ambayo humchoma au humkereketa na hupenda kuyawasilisha kwa hadhira. Kwa hivyo, matumizi ya miundo hiyo hulifanya shairi kuweza kuwasilisha maana ya msingi na ujumbe uliokusudiwa na wakati uo huo kudumisha ujumi katika utungo (Nagler 1974). Mifumo msingi ya kauli teule ambayo hutumiwa ni pamoja na methali, ambazo pia huweza kuibulia fomula ya utunzi na uwasilishaji wa ujumbe katika shairi lililokusudiwa.

Kulingana na Lord (1970), mtunzi hodari wa ushairi hatumii kauli teule kiholela bali huwa ni nyenzo muhimu ya kuusanifu na kuuwasilisha ujumbe muhimu katika utungo. Kwa hivyo, mawazo ambayo huibuliwa, huweza kuwasilishwa kupitia kwa kauli hizo ambapo ni pamoja na methali. Kwa hivyo, mawazo yaliyowasilishwa huwa hayamtatanishi msomaji au msikilizaji wa ushairi. Kwa mfano, katika ushairi ambao

huzingatia arudhi za kimapokeo ni sharti kuweza kuwasilishwa kwa vipengele vya kiarudhi kama vile idadi maalumu ya mizani na urari wa vina (Babusa 2005 na Kandoro 1983). Kwa ambavyo methali ni kauli ambazo hujidhihirisha katika miundo isyobadilika, huweza kutumiwa kuwa chombo cha kuudhibiti muundo wa ushairi wa Kiswahili. Methali iliyotumiwa au zilitumiwa katika utungo, husaidia katika kujenga mazingira ya kuibulia baadhi ya arudhi kama vile mizani, mishororo na vina. Hata hivyo, jambo hilo hutegemea ni wapi imetumiwa au imejitokeza katika muktadha wa uwasilishaji wa ushairi. Endapo methali imetumiwa mwanzoni mwa ushairi huwa ni ya msingi zaidi katika uelekezaji wa muundo wa utungo.

Kadhalika, methali inapotumiwa kama kibwagizo au kiishilio hubidi kuhakikisha kuwa mishororo au mistari ya awali katika uwasilishaji wa utungo huibua uwiano wa aina fulani (Scholes 1982 na Pierce 1982). Katika muktadha wa uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili, mtunzi anapotumia methali hupata uelekezi na msingi wa kushirikisha kauli nyinginezo za kibinafsi ambapo kwa pamoja husaidia katika ujenzi wa muundo na pia kushadidia zaidi ujumbe ulioibuliwa kupitia kwa matumizi ya kauli hizo. Kwa hivyo, kauli au matini nyinginezo zilizotumika katika uwasilishaji, huibuliwa kutokana na uelekezo wa methali husika. Kwa sababu, ujumbe mahususi ambao huwasiliswa kutokana na matumizi ya methali huweza kufasirika na kueleweka vyema zaidi kwa kuzingatia kauli zingine zipatikanazo katika mazingira ya kabla au baada ya methali kutumiwa. Kimsingi, methali kama ishara huweza kufafanuliwa kwa usahihi kwa kuzingatia ishara au kauli zingine zilizotumiwa katika shairi (Osiemo 1997). Kimaudhui, methali zina utata kutokana na maana ya kijumla iliyoibuliwa. Hata hivyo, utata huo

hupata suluhisho kupitia kwa matumizi ya methali ambayo hugota ndipo katika muktadha ulioibuliwa na uliojengwa katika utungo. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, utata katika shairi ni mbinu ambayo hutumiwa ili kuweza kujenga mazingira ya kuufanya utungo kuwasilishwa kimafumbo, kitaswira na kiisitiari.

2.1.3 Methali kama Msingi wa Kuteua Matini Nyinginezo Zilizoshirikishwa

Methali ni kifungu kifupi cha maneno teule ya kimapokeo ambayo hutumika zaidi kama kichocheo cha utunzi na cha uwasilishaji katika shairi la Kiswahili. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, tungo za fasihi simulizi kama vile nyimbo na ushairi hutungwa kwa kushirikisha matini teule za kimapokeo (Lord 1970 na Nagler 1967). Kadhalika, mtunzi wa ushairi andishi wa Kiswahili hunufaishwa kwa matini hizo za kimapokeo hususa, matumizi ya methali. Mshairi wa Kiswahili anapotumia methali katika tungo, hupata mwau wa kuibulia na kusarifu visa virefu kulingana na yale ambayo ametarajia kuwasilisha katika utungo.

Kwa kuzingatia methali, mshairi hupata ilhamu ya kufinyanga na kueleza fikra zake kwa hadhira. Wazo hilo limeelekezwa zaidi kupitia kwa nadharia ya Semiotiki kwamba, kauli msingi za lugha ambazo hutumika katika tungo haziwezi kujisimamia zenyewe bali hupata maana katika muktadha wa mifumo ya ishara au kauli zingine zilizoafiki muundo wa methali iliyopo au zilizopo (Innis 1985). Hata hivyo, katika uwasilishaji wa ushairi huru ambao huweza kushirikisha au kukiuka uelekezo huo. Kimsingi, utunzi na uwasilishaji wa ushairi huru wa Kiswahili haujikiti katika arudhi za kimapokeo bali

huibua kwa makusudi kauli ambazo huaafiki na huakisi hisi zilizoibuliwa katika maudhui yaliyosawiriwa kwa mwendo uliodhibitiwa na msanii.

Mtunzi wa ushairi wa Kiswahili hutumia methali kama mfumo wa maneno teule wenye uwezo wa kusarifia na kuwasilishia ujumbe kusudiwa. Kwa kawaida, matumizi ya methali hupatikana kwa wingi katika tamaduni na mawasiliano ya jamii. Kutokana na sababu hiyo, mshairi huwa mwenye nafasi ya kuchopoa mojawapo ili kuweza kutumiwa kama msingi mwafaka wa kudokezea ujumbe au hisi zinazotakiwa kuwasilishwa. Kimsingi, mshairi wa huwa ana chemichemi ya mawazo au ujumbe ambao angependa kuubainisha na kuueleza kwa hadhira. Anapokuwa na mawazo au mchomo wa hisi fulani, mshairi hupitia kwa tuo baadhi ya methali ambazo huzielewa au zile zipatikanazo katika jamii ili kuweza kuteua ile au zile zilizo mwafaka zaidi katika kuwasilishia ujumbe wake. Kwa hivyo, methali iliyotumiwa au zilizotumiwa huwa ni dira ya kubulia na kushirikisha matini au kauli zingine ambazo pia ni za msingi. Kutokana na methali mahususi zilizoteuliwa, mtunzi wa ushairi wa Kiswahili hupata msukumo wa kupanga, kuratibu na kufafanulia mfululizo wa mawazo, fikra na falsafa katika utungo

Kadhalika, mshairi wa Kiswahili anapoamua kutumia methali kama anwani, au mwanzoni mwa shairi, tayari huwa amejenga mazingira ya kuwaandaa kimbele wasomaji kuhusu mwelekeo alionao na aina ya ujumbe ambao hutarajiwa kuwasilishwa. Kwa ambavyo mtunzi wa mashairi hana muda mrefu wa kujieleza, methali iliyoiteuliwa na iliyoitumika katika muktadha wa matini nyinginezo humpa fursa ya kuyawasilisha mawazo kwa njia ya muhtasari (Hedley 1998). Hadhira nayo huweza kupata fursa ya kutunga utafakari katika akili ili kuweza kufafanua maelezo za ziada. Maelezo hayo

huwa hayafafanuliwi kwa kina, bali huachwa kwa makusudi ili kujenga mazingira ya kuishirikisha hadhira katika kuutafakari na kuupata ujumbe wa ndani uliokusudiwa (Frolova 2008 na Kahigi na Mulokozi 1979). Uziada au maelezo mengineyo yaliyoachwa na msanii hujenga mwau wa kijalizo cha maelezo ambayo huachwa kwa makusudi katika shairi. Hilo huweza kuwa sababu mojawapo ambayo huwafanya baadhi ya watunzi kutotumia kwa uwazi methali iliyokusudiwa au zilizokusudiwa katika utungo (Taz. Sura ya sita kwa maelezo zaidi).

Isitoshe, kuna baadhi ya maswali ambayo msomaji au msikilizaji wa ushairi huweza kujiuliza anapokumbana na matumizi ya methali. Miongoni mwa maswali hayo ni kama:

- Kwa nini mshairi ametumia methali hiyo?
- Kutatokea nini baada ya methali hiyo kutumika?
- Msanii hutaka kuuelezea nini kupitia kwa methali hiyo?

Kwa hivyo, methali huweza kutumiwa katika uwasilishaji wa mashairi kama fupa linalohitaji mnofu. Maswali ambayo huibuliwa kutokana na matumizi ya methali katika shairi, huweza kujibiwa moja kwa moja na msomaji iwapo atakuwa mwenye subira katika kulisoma kwa tuo shairi.

Kadhalika, maswali hayo huweza kujibiwa na mshairi kwa ufasaha zaidi, lakini hana nafasi wala nia ya kufanya hivyo (Gibbe 1990 na Abdalla 1973). Kwa namna hiyo, mshairi hutumia ufundi na ujuzi wa lugha alionao ili kuishirikisha hadhira ya dhati katika usomaji na ufasiri wa ujumbe katika shairi. Hadhira hulisoma shairi kwa lengo la

kujiburudisha huenda isiupate uhondo wa ujumbe uliowasilishwa lakini ikaupata ujumi kutokana na methali iliyotumiwa. Kwa mantinki hiyo, dhima ya fasihi hubainishwa kupitia kwa lugha iliyotumika katika shairi. Kwamba, utungo wa fasihi hupaswa kuburudisha na vile vile kueilimisha jamii (Njogu 2004). Kimsingi, baadhi ya washairi huuficha ujumbe uliowasilishwa kupitia kwa miundo mahususi ya lugha ambayo hujibainisha kitamathali.

2.1.4 Matumizi ya Methali kama Kauli za Makusudi Kutegemea Athari Itayoibuliwa katika Hadhira

Mtunzi wa mashairi hufahamu kwamba, hajitungii yeye mwenyewe ila hutunga kwa lengo la kuuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Aidha, mshairi anapotunga utungo huwa na madhumuni ya kuuwasilisha ujumbe kwa namna ambavyo huweza kumvutia msomaji wake (Mulokozi na Kahigi 1982). Kwa hivyo, huwa mwenye hadhari kubwa katika uteuzi wa kauli au msamiati iliyoyatumika ili shairi lisije likamkinaisha au likamkifu msomaji. Anapokabiliwa na hatari hiyo, mshairi huanza kulipamba shairi kwa kauli na miundo teule ya lugha (Darvin na Wamuhu 1994 na Kezilahabi 1977). Kwa mfano, mshairi huweza kutumia methali ambayo humfanya msomaji kujiingiza katika utafakari zaidi kuhusu ujumbe huo na kuuhusisha utungo na uhalisi wa maisha ya jamii.

Katika msingi huo, mshairi hulisoma shairi lake mara kwa mara kuhakikisha kuwa ujumbe umefumbimbwa kwa kujengewa kauli au miundo teule iliyotumika. Aidha, lengo ni kuhakikisha kuwa, ujumbe umesawiriwa na umewasilishwa kwa hadhira kusudiwa. Kwa hivyo mtunzi hutarajia kuwa, ujumbe unaowasilishwa na umewafikia

wasomaji bila utata wowote. Utata huo ndiyo huondolewa na mshairi anaporudia kuusoma utungo wake mara kwa mara. Aidha, kiungo muhimu cha mawasiliano baina yake na mpokezi wa ujumbe ni kauli na miundo mahususi ya lugha iliyoteuliw na kutumiwa kwa makusudi.

Kimsingi, ushairi wa Kiswahili huzingatia kwa dhati matokeo ya mawasiliano baina ya mshairi na hadhira. Kando na pande hizo mbili, miundo mahususi ya lugha inayotumika huwa ni muhimu katika uwasilishaji wa ujumbe katika shairi (Karama 1996). Kadhalika, dhana ya utata ni mbinu maalumu katika uwasilishaji wa ushairi. Utata, kama mbinu ya uwasilishaji humfaidi katika pembe tatu. Kwanza, humsaidia mshairi kujijengea mizungu ya kunga katika uwasilishaji wa ujumbe. Pili, humfanya mshairi kuichuja hadhira: ya dhati na ya chati. Tatu, humfanya mtunzi kutobainisha waziwazi ujumbe unaowasilishwa.

Ushairi wa Kiswahili hushirikisha kauli au miundo mbalimbali ya lugha; mojawapo ni methali. Methali hizo huwa ni viunzi muhimu vya mawasiliano baina ya mshairi na hadhira. Mshairi anapoteua na anapotumia methali katika ushairi, hutilia maanani wapokezi wa ujumbe. Hiyo hutokana na ukweli kwamba, lugha yeyote ile huwa ina methali chungu nzima na mtunzi ana hiari ya kutumia methali yoyote aitakayo ilimradi ameweza kuusawiri ujumbe na kuuwasilisha kwa wasomaji wake (Gesero 2009, na Wamitila 2006). Mshairi wa Kiswahili hajafungika katika matumizi ya methali, kwa sababu huweza kuzitumia jinsi zilivyo, kutumia kipande au kuzitumia kwa kuidokezea tu.

Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi ni kwamba, ingawa matini teule zinazotumika katika utunzi na uwasilishaji wa kazi mahususi ya fasihi kama vile ushairi na nyimbo huwa hazibadiliki; mtunzi huweza kutumia uhuru wa kiusanii ili kuivyaza upya kulingana na ujumbe au athari anayotarajiwa kuiacha kwa hadhira (Propp 1968). Aidha, mtunzi anapobaini kwamba methali moja haikidhi mahitaji ya kiuwasilishaji, huweza kutumia mbili au zaidi katika shairi moja. Kwa mfano, Abdilatif Abdalla katika diwani yake ya *Sauti ya Dhiki*, ametumia methali tatu katika uwasilishaji wa shairi la 'Mnazi Vuta N'kute' (Abdalla 1973:17-22).

Uteuzi na matumizi ya methali katika utunzi na uwasilishaji wa shairi hufanywa kiustadi na ufanifu mkubwa ili ikidhi siyo tu mahitaji ya kiumbuji, bali pia kwa kuizingatia hadhira kusudiwa. Kwa hivyo, ni muhimu kutilia maanani kiwango cha ufahamu, mielekeo na hisi za wasomaji au wapokezi. Jambo hilo hudhihirika zaidi katika uwasilishaji wa ushairi simulizi. Kwa kuielewa hadhira, mshairi huzingatia zaidi tajiriba, itikadi, miktadha na mazingira ya kijamii ambayo imeibua matumizi ya methali hiyo. Matumizi hayo huweza kusaidia pia katika kukabiliana, kwa kiasi fulani na utata ambao huzuka kutokana na upokezi wa ujumbe katika shairi ambalo limewasilishwa.

Katika muktadha wa uwasilishaji, mshairi mahiri hufanya uteuzi na kuzingatia matumizi ya methali ambazo hulenga zaidi tajiriba yake na uzoefu wa hadhira. Aidha, mtunzi hutarajiwa kuwa mweledi katika uteuzi wa matini na kunga mwafaka ambazo husaidia katika kuwasiliana na wasomaji wake. Kwa sababu, asipowasiliana vizuri na hadhira yake, ujumbe huweza kupwaya na hautakuwa wenye manufaa katika jamii. Kadhalika,

ni muhimu kuelewa kuwa, matumizi ya methali huweza kujenga mahusiano mema ya kimawasiliano baina yake na hadhira au kubomoa kabisa mahusiano hayo (Ndungo 1998, Maitaria 1991 na King'ei 1987). Kimsingi, udhibiti wa mawasiliano katika ushairi wa Kiswahili hutokana na kauli mahususi za lugha ambazo hushirikishwa katika ubainishaji wa ujumbe. Kwa hivyo, matini teule za tamathali za usemi ambazo hutumika zaidi katika uwasilishaji wa ushairi ni zile ambazo husheheni hekima na busara ya jamii (Ligami na Barasa 2006 na Senkoro 1988). Katika muktadha huo, mshairi wa Kiswahili anapotumia methali ambazo hufahamika kwa urahisi katika jamii humwondolea msomaji vikwazo au matatizo ya kiusomaji ambayo huweza kukumbana nayo kuanzia mwanzo hadi mwisho wa utungo. Matumizi mwafaka ya methali katika utungo humhamasisha na humsisimua msomaji ili kuweza kutafakari mawazo yaliyowasilishwa.

2.1.5 Methali kama Chombo cha Kuwasilishia Dhamira na Muhtasari wa Maudhui

Mtunzi wa ushairi ana wajibu wa kuteua na kuchuja miundo na maneno ya lugha ili yabaki yale ya lazima tu katika utungo. Miundo hiyo ya lugha hukusudiwa kubeba mawazo, mafunzo na hisi ambazo zimekusudiwa kuwasilishwa kimuhtasari kwa hadhira. Muhtasari wa mawazo huwasilishwa kutokana na ushikamano wa matumizi ya kauli na miundo mbalimbali ya lugha katika shairi. Kimsingi, shairi ni ufupisho wa maelezo au habari ndefu (Wallah 1998 na Senkoro 1982). Aidha, mawaidha ambayo hupatikana katika shairi moja huweza kuwa ni maudhui kamili yanayowasilishwa kwenye riwaya au tamthilia. Kwa hivyo, mshairi huuwasilisha ujumbe wake kimuhtasari tu huku akimwachia kwa makusudi msomaji kuufafanua zaidi ujumbe uliokusudiwa.

huwasilishwa kwa mshindo, uwazi na msisitizo zaidi. Katika mantiki hiyo, hadhira huweza kupanua mawazo au ujumbe kwa kuzingatia miktadha mingine ambayo hupatikana kwa urahisi katika uhalisi wa maisha na utamaduni wa jamii.

Kadhalika, methali ambazo hutumiwa katika shairi husaidia katika a kuibulia na kubainishia dhamira, imani, mwelekeo na falsafa ya mtunzi. Dhamira pamoja na maudhui ambayo ni kiini cha ushairi, huhitaji kuwasilishwa kwa maelezo ya kina lakini mshairi hustahabu kuyawasilisha kwa muhtasari kwa hadhira. Hiyo ndiyo sababu hadhira huweza, hata baada ya kipindi kirefu kupita; kukumbuka kiini cha maudhui yaliyowasilishwa. Kwa ambavyo mshairi habainishi kwa kina ujumbe, mawazo yaliyowasilishwa huweza kufasiriwa kwa kuzingatia miundo teule ya lugha ambayo ni pamoja na matumizi ya methali.

Vile vile, mshairi la Kiswahili hufahamu kuwa nguzo muhimu katika utungo hutokana na kauli au miundo teule ya lugha. Kutokana na matumizi hiyo, maudhui ambayo yameibuliwa huweza kubainishwa na kuwasilishwa. Mshairi anapotumia methali kama ishara ya uwasilishaji katika utungo, huweza kujenga muktadha wa kuelekeza na kuwasilisha mawazo kwa muhtasari. Kwa hivyo, methali iliyotumika au zilizotumika huwa ni vito angavu katika uwasilishaji wa tungo. Kwa sababu, matumizi hayo hufahamika kimazoea katika mapokeo na mawasiliano ya watu (Gesero 2009). Kwa kawaida, hadhira haiwezi kukumbuka au kuhifadhi maelezo marefu yaliyotolewa katika utungo. Hata hivyo, hadhira huweza kuukumbuka kwa urahisi ujumbe na mawazo

yaliyowasilishwa kwa muhtasari. Ufupi wa ujumbe huweza kuhifadhiwa katika akili na kumbukumbu ya msomaji kwa kuzingatia methali zilizotumiwa katika utungo.

2.1.6 Methali kama Chombo cha Kubainishia Uhalisi wa Maisha na Kuhifadhi Utamaduni wa Jamii

Kimsingi, ushairi wa Kiswahili hutungwa na husawiriwa kwa kuzingatia uhalisi wa kihistoria, maisha ya watu na utamaduni wa jamii. Katika mantiki hiyo, ushairi kama kazi yoyote ya fasihi huibuka katika mazingira halisi ya jamii (Wamitila 2006). Kwa hivyo, shairi zuri la Kiswahili ni lile lenye uzito wa kimaudhui yaliyojengwa katika utamaduni wa jamii na kwa kutumia kauli mahususi ya lugha. Kauli hizo ni zile ambazo huchipuka na hutumiwa katika misingi ya utamaduni na uhalisi wa jamii. Vile vile, miundo hiyo aghalabu hutumiwa na watu katika maingiliano na mawasiliano ya kila siku. Jamii huienzi na huitukuza zaidi miundo hiyo teule ambayo ni pamoja na methali. Kwa sababu hudhihirishia tajiriba, mielekeo, itikadi na uhalisi wa maisha ya jamii. Kwa bahati, jamii mbalimbali ambazo hupatikana katika kanda ya Afrika Mashariki na kwingineko, zina methali ambazo hutumika katika kuakisi na kuhifadhi tamaduni zao (Finnegan 1977). Aghalabu, methali zitumiwazo katika mawasiliano ya jamii hujenga uhalisi wa mandhari ya kitamaduni katika jamii mahususi (Waihiga na Kagwa 2007 na Ndungo 1998).

Kwa hivyo, methali huweza kutumiwa katika kuibulia na kuwasilishia maudhui katika utungo wa ushairi. Kwa sababu, methali hufungamana na uhalisi wa maisha utamaduni wa watu. Aidha, kuibuka kwa methali huhusishwa na chimbuko la lugha miongoni mwa

jamii (Kunemah 2008). Katika mantiki hiyo, watunzi wa mashairi ya Kiswahili hutumia methali katika tungo ili kufungamanisha mawazo dhahiri yaliyoibuliwa na mazingira ya utamaduni maalumu yaliyowazaa, kuwalea na kuwakuza. Kwa hivyo, zaidi ya kuwa msarifu wa lugha, mshairi huwa ni mlinzi na mlezi au mhifadhi wa utamaduni wa watu. Isitoshe, ushirikishwaji wa kauli teule katika ushairi huufanya utungo kutajirika katika fani na uwasilishaji wa maudhui. Kwa mintarafu hiyo, matumizi ya methali katika ushairi wa Kiswahili huwa ni mlezi bora wa tamaduni zinazopatikana katika kanda ya Afrika Mashariki na kwingineko. Kwa sababu, Kiswahili na fasihi yake kwa wakati wa sasa si mali ya jamii ya pwani kama ilivyokuwa katika karne za hapo awali, bali ni kiwakilishi cha uhalisi wa utamaduni wa jamii za Afrika ya Mashariki na popote ambako hutumika kama chombo cha mawasiliano.

Watunzi wa ushairi wa Kiswahili aghalabu hutumia methali kama nyenzo muhimu ya kusawiri kwa ubunifu matukio halisi ya kihistoria yaliyowahi kutokea katika jamii (Mulokozi 2008 na Chacha 1987). Kwa kufanya hivyo, ushairi wa Kiswahili huwa ni kioo ambamo wanajamii hurejelea historia na matukio mbalimbali yaliyopitika katika tamaduni zao. Mawazo hayo yameweza kudhihirishwa kupitia kwa mashairi yafuatayo: 'Mnazi vuta N'kuvute' (Abdallah 1973:17-22); 'Hadithi ya Mzee' (Kezilahabi 1974: 69-72) na 'Mruko wa Nyuki' (wa Mberia 2001:20-25). Kwa ambavyo methali ni zao la jamii, matumizi yazo hulifanya shairi kukubaliwa kuwa mali ya jamii na wala si ya mtu binafsi. Kwa sababu hiyo, wasomaji wa ushairi wa Kiswahili huustahi na huuenzi utanzu huu kuwa kiwakilishi mwafaka cha amali na utamaduni wao.

Mashairi ya Kiswahili ambayo hutumia methali kama kipengele cha mawasiliano, huweza kuwasilishwa kwa kuzingatia tamaduni mbalimbali za Afrika Mashariki na kwingineko (Gesero 2009 na Kunemah 2008). Katika muktadha huo, mashairi ya Kiswahili huwa kama bohari la kuhifadhi utamaduni wa mwafrika hasa pale ambapo lugha ya Kiswahili hutumiwa zaidi katika mawasiliano ya kijamii. Aidha, mashairi yanayoshirikisha matumizi ya methali ni nyenzo muhimu ambayo huufanya utanzu huu kuwa hifadhi na urithi halisi wa utamaduni wa Afrika. Hali hiyo hutokana na sababu kwamba, ushairi wa Kiswahili pamoja na matumizi ya methali ndani yake, huweza kufasiriwa kwa kuzingatia uhalisi wa maisha na utamaduni wa jamii za Afrika Mashariki. Hadhira inapoamua kuufasiri ujumbe unaopatikana katika ushairi wa Kiswahili nje ya muktadha wa uhalisi huo, huweza kuupotosha ujumbe uliowasilishwa.

2.1.7 Methali kama Kauli za Kujengea Mapigo ya Ridhimu na Udhibiti wa Mwendo

Methali hutumiwa katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili kutokana na sifa zake kiumbo na kimuundo. Baadhi ya wahakiki wa hapo awali walichukulia methali kuwa ni ushairi mdogo (Knappert 1979, Allen 1971 na Harries 1962). Sifa hizo za kiumbo na kimuundo huzifanya methali za Kiswahili kuwa zenye ridhimu na mapigo ya kishairi (Syambo na Mazrui 1992). Kadhalika, methali si waadhi tu bali ni pambo zuri sana la lugha (Karama na Saidi 2002). Kwa hivyo, methali huweza kutumiwa mahususi kama chombo cha kuujengea na kuufanya ushairi kuwa wenye ujumi na mvuto teule wa lugha.

Methali zilizotumiwa katika mawasiliano ya jamii, zinaposomwa kwa sauti au kimoyomoyo hudhihirisha mawimbi ya kupanda na kushuka. Sifa zizo hizo za kiujumi na kimuundo aghalabu hupatikana pia katika mashairi ya Kiswahili (Gibbe 1998, Senkoro 1988 na Abdalla 1973). Kwa hivyo, methali huweza kutumika jinsi zilivyo bila ya kufanyiwa marekebisho yoyote. Kwa sababu, muundo na umbo la methali halijabadilika tangu jadi. Neno moja linapoondolewa, methali hiyo haiwezi kujisimamia. Isitoshe, methali huwa na pande mbili ambazo hujengana na hukamilishana. Sehemu ya pili ya methali huwa ni matokeo ya matarajio ya sehemu ya kwanza (Gesero 2009, Wamitila 2006 na Wafula 1999). Hapa inaeleweka kuwa, sehemu ya mwanzo huweza pia kutumika kama kienzo cha methali nzima. Kimsingi, sehemu ya pili huweza isitumike katika mawasiliano ya watu na pia katika uwasilishaji wa mishororo ya shairi. Kwa sababu, kidokezo cha methali huwa kimedhihirishwa kupitia sehemu ya awali.

Ushairi wa Kiswahili unapozingatiwa, hubainisha kuwa tukio ambalo huwasilishwa au husimuliwa huweza kuwa wenye mwendo wa kasi au wa taratibu. Mwendo huo, huibuliwa hasa kupitia kwa mpangilio wa irabu mahususi katika muundo wa maneno unaotumika katika uwasilishaji wa shairi (Mwihaki 1998 na Senkoro 1998). Iwapo mwendo wa kadhia ambayo huwasilishwa katika shairi huwa wa kasi; mshairi huteua na hutumia methali ambazo hulandana na mwendo huo. Kwa hivyo, methali iliyoteuliwa na kutumiwa sharti ilandane na mapigo ya shairi husika. Uzingatifu wa matumizi ya methali, hulifanya shairi liwe lenye kuibua mwendo au ridhimu inayolingana na mawazo yaliyowasilishwa. Kimsingi, mawazo hayo hukusudiwa kuiathiri na kuibua hisi maalumu katika akili ya msomaji. Kwa hivyo, uteuzi na matumizi ya methali haufanywi kiholela

bali utendakazi wazo hufungamanishwa kiustadi na athari ambayo imetokana na ujumbe uliowasilishwa. Ingawa ushairi andishi la Kiswahili hutungwa na huwasilishwa kwa kuzingatia hati za maandishi, utanzu huo huweza kusomwa kwa sauti ili ujumi wa matumizi teule ya lugha kuweza kudhihirishwa.

Isitoshe, mpangilio wa mistari au mishororo unaoshirikisha matumizi ya methali katika beti za shairi la Kiswahili, humfanya msomaji kuusoma kwa kasi au taratibu kulingana na mpangilio mahususi wa sauti, silabi au maneno. Vile vile, maneno ambayo hupatikana katika miundo ya mistari au mishororo ya shairi hayawezi katu kupanguliwa. Kwa sababu, mtunzi huziba kabisa kila upenu ambao huweza kupatikana ili pasiwe na mwanya mwingine wa kulisoma shairi ila kwa mwendo uliokusudiwa (Mazungumzo na Nabhany tarehe 26, Mei 2011). Hiyo ni mbinu mwafaka ambayo hutumiwa mahususi ili kutenganisha na kuuwasilisha ujumbe mzito na ule mwepesi. Kwa mfano, mtunzi anapouwasilisha ujumbe mwepesi au ule usiohitaji utafakari zaidi, usomaji wake huwa ni wa mwendo wa haraka haraka. Muktadha huo hubadilika na kuwa wa aste aste hasa pale ambapo, mtunzi huitarajia hadhira kutafakari zaidi kauli zilizotumika katika uwasilishaji wa ujumbe (Mazungumzo na Senkoro ya tarehe 23, Septemba 2010). Kwa hivyo, mshairi wa Kiswahili huhitaji kuwa mahiri katika uteuzi wa methali zinazohusishwa kwenye shairi. Katika hali hiyo, mshairi asipofanya uteuzi wa methali iliyosadifu huenda shairi lisiweze kuibua na kuwasilisha athari na mahadhi yanayokusudiwa.

Matumizi ya methali katika utunzi wa ushairi wa Kiswahili huruhusu kwa kiwango fulani, udondoshaji au uchopekaji wa uziada wa sauti kama vile irabu na silabi. Mbinu

hiyo ya mazida au inkisari humsaidia mtunzi kuwa na uhuru wa kudondosha baadhi ya viunganishi, sauti au hata kipande cha sentensi (Noor 1988). Udondoshwaji huo wa sauti, silabi au maneno hujenga mazingira ya kuzingatia zaidi sehemu ya mwanzo au ya mwisho ya methali zinazotumika katika uwasilishaji wa ushairi. Katika mantiki hiyo, mtunzi huweza kudondosha baadhi ya sauti, silabi au maneno katika methali. Anapofanya hivyo, huwa mwangalifu zaidi ili kuhakikisha kwamba mantiki na maana ya methali iliyorejelewa hujisimamia na hueleweka. Kadhalika, udondoshaji huo hufanyika pale ambapo mtunzi hujenga upatanisho wa vina, miundo au idadi maalumu ya mizani katika shairi (Njogu 2004, King'ei 1999, Mohamed 1990). Kutokana na udondoshaji huo, methali huweza kutumiwa kama ukwapi, utao, kibwagizo au kimalizio katika shairi la Kiswahili. Tungo nyingi zenye mwelekeo huo ni zile ambazo hutungwa kwa kuzingatia zaidi arudhi za kimapokeo.

Hata hivyo, uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili unaotumia methali pia huimarisha ujumi wa lugha katika utanzu huo. Hiyo hutokana kwa uelekezo wa umbo na muundo wa methali. Jambo hilo, huwezekana kwa kuzingatia miundo mingine ya lugha ambayo huibuliwa kwa makusudi na hujengwa katika tamathali za usemi mahususi. Kwa hivyo, msomaji wa ushairi huburudika na wakati uo huo huupata ujumbe amao huwasilishwa kwa njia iliyo mwafaka zaidi. Kadhalika, msomaji hujengewa mazingira ya kulikabili shairi kwa hadhari na kwa mwendo uliokusudiwa.

2.1.8 Methali kama Kauli Zinazokumbukika kwa Urahisi

Kwa kawaida, umbo fupi la methali halibadiliki na aghalabu hutumika kama lilivyo katika muktadha wa utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Kadhalika, maneno ambayo hutumika katika muundo wa methali huwa ni ndogo mno lakini yenye uhitaji wa ufasiri wa kina au kutolewa maelezo marefu yaliyofungamana na uhalisi wa utamaduni wa jamii. Ufupi huo wa kauli na maneno msingi hurahisisha kumbukumbu yazo. Kadhalika, matumizi ya methali ni muhimu katika kuibulia muundo wa shairi. Kwa sababu, huweza kutumika kama nyenzo ya ujenzi wa mishororo na pia kuakisi ujumbe ambao huwasilishwa. Aidha methali kama kauli, hutumika katika muktadha wa sentensi zilizopo kwenye utungo. Kwa hivyo, methali hutumika kama matini ndani ya matini katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili (Wamitila 2001). Vile vile, methali hutumiwa ili kupata mantiki ambayo huibuliwa katika muktadha wa kauli zingine katika shairi. Kwa ambavyo umbo la methali huwa halibadiliki, hadhira huweza kulitambua kwa urahisi uwepo wazo katika shairi.

Kwa hivyo, mashairi ya Kiswahili hutumia methali kwa lengo la kurahisisha kumbukumbu ya wasomaji kuhusu ujumbe uliowasilishwa. Katika muktadha wa upokezi, msomaji hawezi kukumbuka mkururo wa maneno au miundo mbalimbali ya lugha iliyotumiwa katika uwasilishaji wa ujumbe kwenye ushairi. Kauli hizo, ni pamoja na methali ambazo hutumiwa kwa misingi ya kuubeba na kuuwasilisha ujumbe wa ndani. Kimsingi, mshairi ya Kiswahili huwa hategemei matumizi ya muundo wa sentensi au kauli moja bali kongamano la miundo mbalimbali ya lugha ambayo hupatikana katika mawasiliano ya jamii. Kwa sababu hiyo, mawazo au ujumbe huweza kufafanuliwa kwa

kuzingatia miundo hiyo mbalimbali ya lugha (Jilala 2008, Kisia na Mwarandani 2007 na Karama 1985). Katika uwasilishaji wa utungo huo, methali na miundo teule ya lugha hutumiwa ni ile ambayo huzowewa na hukumbukwa kwa urahisi.

Kwa ambavyo methali ni semi fupi fupi, zinapotumiwa katika ushairi wa Kiswahili humnufaisha siyo tu mtunzi bali pia huwa ni dira ya kuifanya hadhira kuuelewa na kuuzingatia ujumbe unaowasilishwa. Mtunzi wa ushairi huzichukulia methali kama matini za lugha ambazo huweza kutumiwa katika shairi kwa kusudi maalumu la kiuwasilishaji. Kwa mfano, matumizi ya methali humsaidia mtunzi wa tungo za kifasihi kuwasilishia ujumbe kimuhtasari (Osiemo 1997 na Mbega 1984). Hadhira nayo hurahisishiwa kumbukumbu ya baadhi ya miundo hiyo teule ya lugha iliyotumiwa katika shairi.

Katika muktadha wa uwasilishaji wa ushairi, methali hutumiwa katika kuibulia anwani, ujenzi wa mishororo au mistari na pia katika upataji wa kibwagizo au kiishilio (Gibbe 1990 na Kandoro 1983). Kwa hivyo, mtunzi anapotumia njia mojawapo ya hizo, hueleweka kuwa, imeshikilia nafasi muhimu katika uwasilishaji wa utungo. Aidha, huirejesha akili na tafakuri ya hadhira katika methali kama kauli teule ambazo zimetumiwa katika shairi kutokana na kutambulika kwazo kwa urahisi. Kwa kuzingatia methali ambazo zimetumiwa, hadhira huweza kuupata ujumbe ambao umekusudiwa kwa haraka na kwa muhtasari. Kwamba, kuna baadhi ya methali ambazo si rahisi kueleweka kwa wepesi ila huhitaji kiwango cha juu cha utafakari katika muktadha wa utamaduni uliorejelewa. Kwa sababu, baadhi ya methali huwasilisha ujumbe kiisitiari, kitaswira na

kiishara ambapo huibidi hadhira kuwa na weledi katika utafakari (Mutembei 2001 na Steen 1994). Hata baada ya kipindi kirefu kupita, hadhira huweza kukumbuka kwa urahisi methali zilizotumiwa katika ushairi lililosomwa. Hadhira ya ushairi huweza kukosa kukumbuka kauli zingine za kijumla zilizotumiwa ambapo matumizi ya methali huwa ni vito angavu zaidi katika utungo uliowasilishwa. Kwa njia hiyo, mawazo ya mtunzi husaki kwa mwafaka zaidi katika akili ya msomaji.

Kadhalika, ni muhimu kufahamu kuwa maneno ambayo yametumiwa katika methali ni yale yale ambayo hupatikana katika mawasiliano ya kila siku. Methali zilizotumiwa katika uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili, ni zile ambazo zimekuwepo katika mawasiliano na mapokezi ya jamii tangu jadi. Hata hivyo, kimsingi methali hukumbukwa kwa urahisi na zinapotumiwa kwa uwazi huirahisishia hadhira kuukumbuka na kuuelewa ujumbe ambao umewasilishwa.

2.1.9 Methali kama Chombo cha Kufumbia Fumbo

Ufumbaji ni mbinu mojawapo muhimu katika utunzi na mawasiliano ya kifasihi hususa, ushairi wa Kiswahili. Kimsingi, ujumbe au mawazo katika mashairi huwasilishwa kwa hadhira kimafumbo au kwa kutumia lugha fiche ya kitamathali. Ujumbe uliosetiriwa katika miundo mahususi ya lugha inayopatikana katika ushairi wa Kiswahili huhitaji jicho pevu la upekuzi ili kuupata kwa njia rahisi. Kadhalika, methali ni usemi hujibainisha zaidi kimafumbo. Kwa hivyo, huhitaji kufasiriwa na kufumbuliwa (Noor 1988 na Abdalla 1973). Kwa sababu hiyo, mshairi hutumia methali kama mbinu ya kuusetiri zaidi ujumbe ambao umewasilishwa kwa makusudi. Kadhalika, mshairi huweza

kuuwasilisha ujumbe kwa hadhira kusudiwa ambayo ni ya dhati huku akiitenga hadhira bandia (Noor 1988 na Abdalla 1973).

Kimsingi, matumizi ya mafumbo katika ushairi hufumbwa katika miundo ya maneno au ishara ambazo huweza kufumbuliwa na hadhira lengwa bila utata. Matumizi ya methali katika ushairi, huufanya utanzu kujengewa kichocheo cha kuwatafakarisha wasomaji ili kuupata ujumbe uliokusudiwa (Frolova 2008 na Ombuge na Kisia 1999).

Aghalabu, methali zitumiwazo katika mashairi ya Kiswahili husaidia katika kuuficha ujumbe kuhusu maswala nyeti ya kijamii. Kimsingi, mtunzi ndiye anayefumba ujumbe unaowasilishwa katika utungo (Mazungumzo yangu na Sheikh Nabhany ya tarehe 20, Oktoba 2010). Kwa mfano, mtunzi anapouwasilisha ujumbe muhimu unaozungumzia maswala tatizi ya kijamii na ya kisiasa yaliyopigwa marufuku na serikali ya nchi, huhitaji mweledi katika kuufumba ujumbe uliowasilishwa. Mshairi huufumba ujumbe katika miundo teule ya lugha na pia huweza kufanya hivyo kwa kuhusisha matumizi ya methali. Hapa ikumbukwe kuwa, ufumbaji huo haunuiwi kumtenga msomaji, bali matumizi yazo huufanya ushairi kutokuubaisha wazi ujumbe uliokusudiwa. Kwa msomaji asiyekuwa mwenye subira huuona utungo uliotumia methali kama usiofaa kutokana na mtazamo finyu au wa kijuujuu. Katika muktadha huo, mshairi hutumia mbinu ya kimafumbo ili kufumba mawazo hayo ili yasijulikane ila tu kwa wale wanaokusudiwa (Noor 1988 na Msami 1982). Kwa njia hiyo, methali hutumiwa kujenga msingi wa kuitenga hadhira ambayo haijakusudiwa. Hata hivyo, msomaji wa kijuujuu hupata tija kutokana na kauli za kimafumbo zilizotumika katika uwasilishaji wa utungo. Kwamba, msomaji anapolidurusu shairi huvutiwa kwa mizungu ya lugha iliyotumika na ujumi unaoibushwa.

Kadhalika, ufumbuzi wa fumbo la methali katika ushairi wa Kiswahili huhitaji umahiri wa kufikiri na kuihusisha maana iliyoibuliwa na miktadha yenye uhalisi wa maisha na utamaduni wa jamii. Hali hiyo hutokana na sababu kwamba, maneno yaliyotumiwa katika ufumbaji katika mashairi ya Kiswahili ni yale yale yanayopatikana katika mawasiliano ya kila siku ya watu (Ramadhan 1973). Hapa isieleweke kuwa, si maneno magumu tu ambayo hutumiwa katika ufumbaji wa ujumbe wa mshairi. Kwa hivyo, matumizi ya methali kama fumbo, ni mbinu ambao hutumiwa kwa hiari au kwa makusudi kutokana na mazingira ambayo humkabili mtunzi wa fasihi.

Aidha mtunzi wa fasihi hususa, mshairi ana hiari ya kutoboa yote ambayo humkera na kwa uwazi au huyasema kwa mafumbo (Gibbe 1990 na Mulokozi na Kahigi 1982). Kwa kutumia methali, mshairi huweza kuusetiri ujumbe katika shairi, lakini ujumbe huo huweza kueleweka kwa msomaji aliye makini na wa dhati. Isitoshe, lugha ya mafumbo ina mvuto wake (Mazrui na Noor 1976). Kwa mfano, mshairi anapokaripia kwa matumizi ya mafumbo, hadhira haiwezi kupata misingi ya kughafilika kwa ghafla, pia hawezi kutoneshwa hisia kwa mara moja. Kwa hivyo, hiyo ni sababu mojawapo ambayo huwafanya washairi wa Kiswahili kutumia methali kama mbinu ya kuwasilishia ujumbe kimafumbo. Hata hivyo, uwasilishaji wa kimafumbo ambayo hutumia methali hurutubishwa zaidi kwa uzingativu wa kauli nyinginezo za usemi zilizotumiwa katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili.

2.1.10 Methali kama Chombo cha Kudhibiti Kaida za Kisarufi

Mtunzi anapouwasilisha utungo huhakikisha kuwa masharti ya kisarufi yamezingatiwa. Ili kuifanya miundo ya lugha inayotumika katika kuuwasilisha ujumbe uliokamilika katika utungo, ni muhimu kwa mshairi kuzingatia kauli ambazo hujengeka katika utaratibu wa kisarufi. Hilo hutokana na sababu kwamba, sarufi ya lugha ni muhimu kuzingatiwa katika mawasiliano ya kijamii ambapo hupatanisha kwa mantiki na kile hurejelewa katika utungo (Winfred 1965). Kwa kuzingatia taratibu za kisarufi, ushairi wa Kiswahili hujenga umuwala wa mawasiliano yanayohitajika baina ya mtunzi na hadhira hiyo. Kwa sadfa, miundo ya methali ambayo hutumika katika mashairi ya Kiswahili huwa zimejikita katika taratibu kamilifu za kisarufi. Kwa hivyo, kauli za kimapokeo zinapotumiwa katika utunzi wa mashairi hazihitaji marekebisho ya kimsingi (Propp 1968, Fowler 1966 na Levi-strauss 1963). Kwa hivyo, mshairi wa Kiswahili hutumia methali kama kigezo au mizani ya kuhakikisha kuwa kauli zilizoshirikishwa katika utunzi na uwasilishaji wa utungo hufuata muundo ulioibuliwa kwa vipashio vya kauli mahususi zilizotumiwa. Hiyo haimaanishi ya kwamba, mshairi wa Kiswahili hana uhuru wa kishairi katika kuusarifu utungo. Umuhimu wa matumizi ya methali ni kuhakikisha kwamba, ujumbe unaowasilishwa umedhibitiwa kwa uelekezo wa kauli hizo. Kimsingi, mtunzi wa mashairi anapoamua kutozingatia sheria za sarufi, pia hadhira huelewa kwamba mtunzi amefanya hivyo kwa makusudi (Njogu na Chimerah 1999). Kwa sababu, mshairi wa Kiswahili na mpokezi huelewana kwa upande wa ukiushi huo wa kisarufi. Kwa hivyo, mawasiliano hayatingwi wala hayaathiriwi kwa utata. Kadhalika, mshairi kuhakikisha kuwa miundo ya lugha inayotumika kama mishororo au mistari huwa imekamilika kimaana. Katika muktadha huo, mtunzi wa ushairi wa

Kiswahili ana hiari ya kuacha au kudondosha silabi, maneno au hata kipande cha methali katika miundo mbalimbali ya mishororo au sentensi zinazotumika katika utungo. Kimtindo, baadhi ya maneno hayo katika ushairi wa Kiswahili hudondoshwa kwa makusudi. Kama vile ilivyoelezwa hapo awali, kimuundo methali za Kiswahili huwa zina sehemu mbili za msingi. Kimantiki, sehemu ya awali katika methali ndiyo ya msingi.

Mshairi anapoamua kudondosha sehemu yoyote ya kipashio katika methali aghalabu huwa ni ile ya pili ambayo haiathiri maana ya msingi iliyorejelewa (Wamitila 2006). Zaidi ya hayo, mbinu hiyo ya udondoshaji hutumika mahususi ili msomaji apate nafasi ya kujaliza sauti au maneno baki. Isitoshe, msomaji hupata fursa ya kujenga usaili, utafakari na kujaliza maelezo baki ambayo si ya msingi zaidi katika kauli iliyotumika. Kwa ambavyo methali hujibainisha katika miundo ya lugha iliyokamilika kisarufi, hutumiwa katika utunzi wa mashairi ili kuwasilisha ujumbe uliotarajiwa kama utanzu ndani ya utanzu. Hiyo hutokana na sababu kwamba, methali ni utanzu maalumu katika fasihi simulizi ambao huweza kushirikishwa katika uwasilishaji wa tanzu zingine za fasihi hususa, ushairi wa Kiswahili. Matumizi hayo pia huwa ni matini iliyokamilika ndani ya shairi. Kwa hivyo, uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili hayana dosari yoyote ya kisarufi na huweza kutumika jinsi zilivyo au huweza kufanyiwa marekebisho machache kutokana na uhuru wa kishairi.

Matumizi ya methali kama miundo teule ya lugha iliyojikita katika misingi ya kisarufi ya jamii, huhitaji kutumiwa kwa ustadi mkubwa katika utunzi na uwasilishaji wa ujumbe

katika mashairi ya Kiswahili. Msanii anapozingatia misingi ya kisarufi katika muktadha wa utunzi huhakikisha kwamba, wasomaji na wahakiki wa lugha hawapati misingi ya kuwasuta. Iwapo mtunzi hutumia zaidi uhuru wa kishairi, huenda mishororo au kauli zilizopo katika ushairi zikakosa mantiki au zikazua utata usioeleweka miongoni mwa hadhira. Aidha, miundo hiyo ya lugha ambayo haieleweki; matokeo ni kuzua utata katika uwasilishaji wa ujumbe kwenye ushairi wa Kiswahili. Utata na usousarufi huo ndio huondolewa kwa kutumia methali katika uwasilishaji wa utungo.

2.1.11 Methali kama Nguzo ya Kubainishia Miktadha ya Kijamii

Miundo maalumu ya lugha inayotumika katika utunzi na uwasilishaji wa mashairi, hupata maana na fasiri zilizokusudiwa kwa kuzingatia miktadha mahususi ya kijamii. Kwa hivyo, baadhi ya kauli hizo kama vile methali zilizotumiwa katika uwasilishaji wa ushairi huubainisha utungo kuwa wenye upekee wa sajili ya lugha. Sajili hiyo hutofautiana kwa kiwango fulani na miundo ya lugha ambayo hutumika katika tanzu za kinathari (Kisia na Mwarandani 2007). Methali zinapozingatiwa zenyewe huwa hazisadifu maana yoyote ya hadi pale zinapotumiwa na kufasiriwa katika miktadha halisi ya utamaduni katika jamii. Kimsingi, methali zina fasiri mbalimbali ambazo huweza kuzua utata lakini matumizi hayo mahususi hueleweka kwa kuzingatia lengo na muktadha wa jamii unaosawiriwa na kuhusishwa katika ushairi wa Kiswahili. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, kauli zinazotumika mno katika uwasilishaji wa ushairi ni za kiisitiari ambapo huweza kufasirika kwa namna mbalimbali kutegemea jinsi mtunzi alivyozitumia (Mitchell na Naggy 2000 na Hawkes 1977). Hiyo humaanisha kuwa, upatanisho na matumizi ya methali katika uwasilishaji wa ushairi huhitaji tajiriba pana la usarifu wa lugha kwa

ujumla. Kwa hivyo, mtunzi anapoamua kuitumia au kuzitumia methali huelewa fika kwamba, kuna zingine ambazo hupingana kimaana. Aidha, kuna methali mbalimbali ambazo huweza kutumika katika uwasilishaji wa fikra au ujumbe sawia katika mawasiliano ya watu katika jamii (Wafula 1994 na Msokile 1992). Kwa sababu hiyo, mshairi huteua methali ambazo hukidhi uwasilishaji wa ujumbe uliokusudiwa.

Mwafaka wa matumizi ya methali katika ushairi wa Kiswahili hutegemea muktadha unaoibuliwa na kuzingatiwa. Methali iliyoteuliwa au zilizoteuliwa sharti iwe au ziwe zimefungamana na tukio au miktadha maalumu ya kiwakati, pahali na mazingira ya jamii. Kadhalika mtunzi huelewa kwamba, methali isipozingatia au zisipozingatia muktadha maalumu wa jamii huenda ujumbe ukawa legelege na usiwasilishwe ipasavyo kwa hadhira. Lengo la mshairi si kuzua utata katika utungo bali ni kuuwasilisha kikamilifu ujumbe kwa hadhira kusudiwa. Kwa hivyo, matumizi mwafaka ya methali, humfanya msomaji kuupata ujumbe na kuelewa muktadha wa kijamii unaorejelewa katika shairi linalosawiriwa. Kwa njia hiyo muktadha wa matukio katika jamii hupata mshabaha wake katika methali ambazo zimetumiwa kwenye ushairi. Ingawa muktadha ambao huibuliwa na hupatanishwa na matumizi ya methali mahususi ni muhimu, hadhira huweza kutafakari matumizi yazo katika miktadha mingine ambayo sawia au tofauti na ile ambayo hupatikana katika uhalisi wa utamaduni wa jamii. Kwa hivyo, matumizi hayo huwa ni mbinu ambayo hupanua utafakari wa ujumbe uliowasilishwa katika ushairi kwa kurejelea miktadha au matukio mengine ambayo hupatikana katika jamii.

2.1.12 Methali kama Kiashiria Msingi cha Ufasiri wa Ujumbe

Miundo mahususi ya lugha ambayo hutumika zaidi katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili ni ile iliyojengwa katika tamathali za usemi. Kwa kuzingatia miundo hiyo, huufanya ushairi kuwasilisha maana fiche au batini. Kadhalika, methali hudhihirisha ukuu wake kifani katika tamathali za usemi, picha za kisanaa, ishara na vipengele vingine vya fasihi (Osiemo 1997 na Khatib 1981). Kwa hivyo, methali hutumiwa katika utunzi wa ushairi ili kuufanya ujumbe uliowasilishwa kuweza kukolezwa zaidi na kufasiriwa kwa kuzingatia tamathali hizo za usemi. Mshairi anapotunga utungo, humtaka msomaji kuzingatia siyo tu maana ya wazi inayobainika katika mfumo wa maneno uliotumika bali kama mbinu iliyojengwa kwa makusudi kwa azma ya kutafakarisha na kuhamisha maana iliyowasilishwa (Imbosa 1990 na Wanyoike 1976). Methali, sawia na kipengele chochote cha lugha kilichojidhihirisha katika tamathali za usemi, ni ishara ambayo huashiria au hurejelea dhana halisi katika jamii.

Kimsingi, methali zina maana ya juujuu au iliyowazi na ile batini. Maana iliyo dhahiri hupatikana kwenye maneno ambayo yametumika katika methali ambapo huweza kuwa ni kichocheo cha kutafakari na kufasiri maana ya ndani inayokusudiwa katika uwasilishaji ujumbe (Madumulla 1995). Kadhalika, methali huwa ni mbinu ambayo hutumiwa ili kuipambanua hadhira yenye nia ya kuupata ujumbe wa ndani na ile inayopitia usomaji wa mashairi kijuujuu. Hadhira lengwa huwa ni ile iliyo na hamu ya kuupata ujumbe wa ndani uliosetiriwa katika shairi (Noor 1988 na Mayaka 1986). Kwa hivyo, mshairi anapotumia methali katika utungo, huwa si lengo lake kuishurutisha hadhira kumeza au kuupokea ujumbe uliowasilishwa. Jambo ambalo hutatarajiwa na mshairi ni kuchochea

utafakari na ufasiri ujumbe wa ndani uliopewa kipaumbele kwa mtazamo mpana wa jamii.

Kimatumizi, ushairi usiobainisha wazi ujumbe; huchochea utafakari wa mawazo yaliyowasilishwa ili yasaki kikamilifu katika akili ya msomaji. Katika ushairi, hakuna fasiri au ufumbuzi wa jibu la moja kwa moja. Kwa sababu, miundo ya lugha iliyotumiwa katika utunzi na uwasilishaji wake hujikita zaidi katika lugha ya kitamathali. Aidha, ujumbe mahususi ambao huwawasilishwa hutegemea zaidi jinsi msomaji amelikabili shairi hilo kwa kuzingatia miundo teule ya lugha ilivyotumiwa. Kwa ambavyo methali ni ishara ambayo huchochea tafakuri ya hadhira, ni sharti hadhira lengwa iurejelee na kuupatanisha ujumbe uliowasilishwa kwa kuzingatia miktadha ya jamii (Pierce 1977 na Jakobson 1960). Hivyo, methali zilizotumiwa katika tungo za ushairi au nyimbo huwa zenye uwiano wa pembe tatu ambazo huchangiana na hushirikiana (Hawkes 1977 na Scholes 1974). Sehemu hizo ni: kizungumzwa, kifananishi na kiungo. Kizungumzwa, ni dhana au tukio ambalo limelorejelewa na mtunzi kama vile mawazo au ujumbe uliowasilishwa. Kifananishi nacho ni, jambo ambalo humithilishwa kwa kuzingatia muktadha wa tukio na mawazo ya mshairi. Kadhalika, kiungo ni sifa bainifu ya kile kilichomithilishwa. Hayo ni baadhi ya mambo muhimu ambayo hadhira hupaswa kuyaelewa wakati wa kuusoma ushairi. Katika uwasilishaji wa shairi, mambo hayo hudokezewa katika utungo.

Kwa kutumia methali katika uwasilishajia, mshairi huwa amejengea muktadha mwafaka ya kusema alilolitaka kulisema ingawa kwa muhtasari tu. Kama vile mafumbo, mshairi

anapotumia methali katika utungo, hawasilishi mawazo kwa wazi bali ufafanuzi na ufasiri wake hutegemea tajiriba na uwezo wa msomaji. Mawazo hayo huaafiki mtazamo wa nadharia ya Semiotiki kwamba, kauli ambazo hutumiwa katika baadhi ya tungo za fasihi huweza kufasiriwa vizuri kwa kuzingatia uhalisi wa maisha na utamaduni wa jamii (Njogu 1996 na Olsen 1973). Ushairi wa Kiswahili ambao hutumia methali huufanya utungo huo kuwa hai, wenye mvuto wa kiujumi na wenye kutamba kwingi katika nyanja mbalimbali za maisha ya jamii. Kutokana na jinsi methali ilivyotumiwa katika uwasilishaji wa mawazo, ushairi wa Kiswahili huweza kuwa ni nyenzo mwafaka ya kumulika na kutafakarisha maswala mbalimbali ambayo humithilishwa kwa ubunifu katika utungo.

2.1.13 Methali kama Mbinu ya Kujengea Taharuki

Mbinu ya taharuki hutumiwa zaidi katika tanzu za fasihi andishi kama vile riwaya na tamthilia. Vile vile, hutumiwa kwa kiwango fulani katika ushairi wa Kiswahili. Mshairi huweza kuitumia mbinu hiyo kwa kushirikisha kipengele cha methali. Hiyo hutokana na sababu kwamba, methali iliyotumiwa katika utanzu wa fasihi huwa kito angavu chenye upekee wake. Mshairi huweza kutumia methali kama mbinu ya taharuki ili kuibua na kujenga muktadha wenye mguso ambao huisisimua hadhira. Taharuki kama mbinu ya kifasihi imekuwa ikitumiwa mno katika uwasilishaji wa fasihi ya kinathari na tamthilia (Wafula na Njogu 2007 na Njogu na Chimerah 1999). Kwa kiwango fulani, mbinu hiyo hujitokeza kama kichochezi cha kuibulia ilihamu ya hadhira katika baadhi ya tanzu za fasihi simulizi kama vile ngano za masimulizi, nyimbo na ushairi wa Kiswahili.

Katika ushairi andishi wa Kiswahili, mbinu ya taharuki hurutubishwa zaidi kupitia kwa kauli ambazo hujibainisha katika tamathali za usemi. Kauli hizo ni kama vile methali, vitendawili, nahau au misimu ambazo hutumika ili kumfanya msomaji kuwa mwenye ustahimilivu na subira ya kutaka kuelewa zaidi kuhusu ujumbe unaowasilishwa. Kwa hivyo, msomaji hawezi katu kuelewa ujumbe ambao huwasilishwa iwapo hatausoma utungo wote. Hivyo ieleweke kuwa, mtunzi huweza kutumia methali moja, mbili au zaidi. Idadi ya methali ambazo hutumiwa katika uwasilishaji wa ushairi, hutegemea ufundi na maudhui mbalimbali ambayo huibushwa kwa mwelekeo uliouchukuliwa. Iwapo methali zilizotumiwa ni zaidi ya moja basi, kila moja huwa imeshikilia nafasi muhimu katika uwasilishaji wa hoja au maudhui yamewiana au yametofautiana. Aidha, matumizi hayo hukuza taharuki katika shairi lililowasiishwa.

Kwa hivyo, methali zilizotumiwa husaidia katika kumdhibiti msomaji kwa kuichochea hamu ya kutaka kuanza na kuendelea kulisoma shairi kwa utafakari kuanzia mwanzo hadi mwisho wake. Kimsingi, mshairi anapotunga shairi huwa ana ujumbe maalumu ambao huwasilishwa kwa hadhira (Masinde 2007 na Babusa 2003). Ujumbe huo huweza kufumbwa kiufundi katika methali zilizotumiwa katika harakati za usawiri na uwasilishaji wa utungo. Kadhalika, ujumbe huo huwasilishwa kiawamu na kwa utaratibu maalumu. Methali zilizotumiwa kwa mwafaka, humpa msomaji nafasi ya kuufafanua na kuufasiri ujumbe uliowasilishwa katika ushairi wa Kiswahili. Methali huweza kuchopekwa kwa makusudi na kiufundi kama sentensi kamili, kishazi au mshororo katika ushairi la Kiswahili. Kwa hivyo, matumizi hayo huweza kutokea popote katika ushairi.

Ikiwa hivyo, mtunzi humweka msomaji ili kuwa tayari kupata mawazo au mifano mingine ambayo hubainisha zaidi maudhui au dhamira zilizo wasilishwa katika utungo.

Hadhira inapokumbana na methali iliyochopekwa katika safu ya utungo, humsisimua msomaji kwa ambavyo hujengewa msukumo wa kutaka kujua zaidi kuhusu ujumbe wa ndani unawasilishwa. Kwa mfano, hadhira huweza kujiuliza mkururo wa maswali ya kwa nini, hasa inapokumbana na methali iliyotumiwa kwa makusudi katika shairi la Kiswahili. Hapa ieleweke kuwa methali inapotumiwa mwanzoni mwa shairi, mwanzoni mwa beti au kama kibwagizo; huwa ni ya msingi zaidi katika kujengea taharuki. Mtunzi huwa ana jukumu kubwa la kuikuza na kuishikilia hamu ya msomaji kuanzia mwanzo hadi mwisho wa shairi. Kwa kiwango fulani ushikamano wa mawazo ambayo huwasilishwa hudhibitiwa kwa viona mbele na nyuma. Kadhalika, mawazo hayo hutiliwa nguvu kutokana na kauli msingi zilizotumiwa, miongoni mwa kauli hizo ni methali. Katika muktadha huo, msomaji huweza kulidurusu shairi kwa kuzingatia mawazo mapya yaliyobuliwa na kuyapatanisha na yale ya awali.

Zaidi ya hayo, iwapo hadhira haitadhibitiwa kikamilifu, huenda hamu hiyo ya kutaka kuendelea kulisoma shairi ikadidimia au kuathirika. Endapo msomaji atakosa kuendelea kulisoma shairi zima, kuna uwezekano kwamba hatafaidika kutokana na uhondo wa mawazo ambayo huwasilishwa. Kwa sababu, hoja ambazo huwasilishwa katika shairi huchangiana, huendezana na hukamilishana. Baadhi ya wahakiki wa ushairi wa Kiswahili huchukulia kuwa kibwagizo ndicho kiini cha shairi (Kisia na Mwarandani 2007, Kuvuna, Mvati na Maliachi 1992 na Abedi 1954). Mawazo kama hayo huweza

kumpotosha msomaji wa shairi. Kwa vile anapozingatia zaidi kimalizio au kibwagizo kinachotumika huweza kuupata kikamifu muhtasari au msimamo ambao umejengwa katika shairi. Ili kuyakinisha ujumbe, ni muhimu kwa hadhira kulisoma shairi lote ingawa matumizi ya methali katika kibwagizo au kimalizio huweza kumpa msomaji fununu ya dhamira au maudhui yaliyowasilishwa.

Kadhalika, mtunzi anapotumia methali zaidi ya moja huweza kupata upenu wa kufaragua au kuibusha kimantiki matukio mengine muhimu katika shairi. Kwa mfano, muktadha wa tukio moja lililorejelewa katika methali huweza kuwa ni ufunuo wa matukio mengine muhimu ambayo huhitaji kutolewa maelezo ya kina kwa hadhira. Ujenzi huo wa mshikamano wa matukio katika ushairi huweza kukidhiwa pia kupitia kwa methali mahususi ilivyotumiwa au zilivyotumiwa katika shairi. Kwa hivyo, mtunzi anapotumia methali hashurutishwi kutoa ufafanuzi wa kina bali hutumia maneno teule kuwa kauli za msingi. Maelezo mengine huweza kutolewa na hadhira kwa wakati wake.

Mbinu ya taharuki katika uwasilishaji wa ujumbe katika ushairi wa Kiswahili huhitaji umahiri wa hali ya juu kuhusu uteuzi wa miundo mahususi ya lugha (Mbugua 2005, Musungu 2005 na Alembi 2002). Kwa sababu, mtunzi anapotumia methali na kuzua matukio ambayo hayaoani na mawazo yaliyoibuliwa, basi utungo hautaeleweka na hautakuwa wenye ushikamano wa kimantiki. Taharuki mwafaka katika shairi humpa msomaji mshawasha wa kiudadisi na kiusaili kwa kile kilichoelezwa au kilichodokezwa. Kwa hivyo, taharuki katika utunzi na uwasilishaji ni mbinu ambayo humfanya msomaji asichoke katikati au kusitisha usomaji wake kabla hajamaliza kulisoma shairi lote.

Katika hali hiyo, mtunzi huhitaji kuwa mahiri katika uteuzi wa lugha ambayo hutumiwa ili ujumbe kuweza kumfikia msomaji kwa uwazi na kwa njia mwafaka zaidi. Kutokana na matumizi hayo teule ambayo hujenga taharuki, hadhira huwa yenye jicho dadisi huku akili ikiduru kupata ufunuo zaidi wa ujumbe uliowasilishwa.

2.1.14 Methali kama Chombo cha Kuwasilishia Mabadiliko ya Kijamii

Mabadiliko mbalimbali ya kitamaduni, kiwakati na kijamii yameweza kutokea katika kanda ya Afrika Mashariki. Kwa mfano, kwa wakati wa sasa lugha ya Kiswahili hutumika kama chombo mahususi katika mawasiliano mapana miongoni mwa jamii za Afrika Mashariki (Mbaabu 1996 na Njogu na Chimerah 1999). Kwa hivyo, kimatumizi lugha ya Kiswahili na fasihi yake hususa, ushairi umekuwa ni wakilisho la maisha na utamaduni wa jamii pana (Mtesigwa 2001, Momanyi 1998 na Chacha 1987). Kiumbiumbi hicho cha mabadiliko yameweza kuathiri takribani kila kipengele cha utamaduni na kuathiri mkondo wa maisha ya jamii. Matumizi ya methali katika ushairi wa Kiswahili huweza kumfanya mshairi kukabiliana na kuyawasilisha mabadiliko hayo yaliyojiri katika jamii. Kimsingi, mabadiliko hayo huweza kuathiri fikra na mtazamo ya uhalisi wa maisha kuhusu mielekeo, utamaduni, itikadi na falsafa katika jamii.

Mabadiliko katika jamii ni ya lazima na mshairi wa Kiswahili hana budi kujenga mwelekeo mpya ambao huweza kukabiliana na mabadiliko hayo pindi yatokeapo katika jamii. Kwa hivyo, msanii huweza kuzingatia mbinu, mitindo na miundo mahususi ya lugha inayotumika katika usawiri na uwasilishaji wa utungo huu. Miundo hiyo inapotumika, husaidia zaidi katika kuwasilisha mabadiliko hayo katika utunzi na

uwasilishaji wa ushairi. Huenda hiyo ndiyo sababu ya kuwepo kwa baadhi ya mashairi kuzingatia zaidi methali na yale ambayo hayana matumizi mengi ya methali au chache zaidi au hayana kabisa matumizi hayo.

Methali zinazotumika wakati wa sasa katika mawasiliano ya jamii zimekuwepo na zimekuwa zikitumiwa kimapokeo kwa muda mrefu katika jamii. Kutokana na hekima na busara iliyomo ndani ya methali, zimeweza kuwasilishwa kimapokeo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kimatumizi, methali si semi gutu zenye hekima za kimgando. Kwa sababu, mtunzi wa ushairi huibua uhuru wa kishairi ambao humfanya kuzitumia methali hizo kulingana na hisi au mwelekeo alionao. Japo methali ni kauli ambazo hudhihirisha kwa ujumla utamaduni na uhalisi wa kale, mshairi wa Kiswahili huweza kuzitumia ili kuelezea mengi katika muktadha wa maisha ya sasa (Meena 1975). Kwa ambavyo methali hujengeka katika tamathali za usemi, hazina fasiri moja mahususi. Kwa hivyo, huweza kuwa zenye umuhimu ambao haujapitwa na wakati. Kulingana na nadharia ya Semiotiki, tamko au kauli ambazo hutumika katika mawasiliano ya jamii huwa ni ishara zinazohitaji kufasiriwa katika muktadha wa utamaduni wa jamii (Akporobaro 2004). Ili maana mahususi kuweza kuwasilishwa, matumizi ya methali hupatanishwa na miktadha mingine mipya au maalumu katika jamii ya wakati wa sasa.

Kimsingi, tangu jadi methali zimekuwa zikitumiwa kama kito au nakshi za kukoleza mawasiliano ya ana kwa ana na pia kushirikishwa kama matini teule katika utunzi na uwasilishaji wa tanzu za fasihi simulizi. Katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili huweza kutumia methali ili kuibulia maudhui au ujumbe ambao huakisi athari za

mawasiliano ya jamii. Hiyo hutokana na mizungu iliyotumika katika kuifinyanga miundo iliyozowewa ili iwe yenye upya ndani yake. Kwa hivyo, matumizi ya methali katika ushairi wa Kiswahili huweza kuutoa utanzu huo kwenye ukuu kuu wa miundo ya lugha iliyozowewa katika mawasiliano ya jamii na kuufanya uwe wenye upya wa mtazamo.

Kimsingi, mawazo au ujumbe ambao husawiriwa na huwasilishwa kwa hadhira huwa wenye mshindo mkubwa kutokana na miundo teule ya lugha inayotumika katika shairi (Barthes 1981 na Lukacs 1962). Miundo hiyo teule ni pamoja na methali zinapotumika katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, inapotumika kiustadi na kiusanii huifanya hadhira kupokea maudhui kwa mtazamo mpya, hata kama maudhui au ujumbe huo umekwisha kuelezwa hapo awali na baadhi ya watunzi (Wamitila 2008 na Omari 2006). Kadhalika, hadhira huweza kutanua uwezekano wa kubadili mitazamo yao kuhusu mielekeo na upokezaji wa ujumbe kutokana na miundo hiyo iliyotumiwa katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Mitindo katika uwasilishaji na miundo ya lugha ambayo imezowewa katika jamii na kutumiwa katika utunzi wa ushairi wa Kiswahili huudumaza na kuuviza utanzu huu (Gromov 2006).

Kinyume na mawazo hayo, methali zimeendelea kushikilia nafasi muhimu katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi. Matumizi ya methali katika ushairi wa Kiswahili hurutubisha umbuji wa fani inayotumika na kuwa yenye maono zaidi kwenye utanzu huu. Kulingana na nadharia ya Semiotiki, utanzu wa fasihi si lazima kuweza kuwasilishwa kwa miundo ya lugha iliyozowewa katika mawasiliano ya jamii (Indede 2008). Aidha, matumizi ya

lugha ya kawaida huweza kuvyazwa zaidi ili ichukue sura mpya. Upya wa matumizi ya lugha katika uwasilishaji wa ushairi huufanya utungo huu kuwa wenye utajiri wa kiumbuji na wa kufasirika (Eco 1984, Culler 1981 na Jacobson 1960). Kwa hivyo, methali zinapotumika kwa ufasaha na kwa kuzingatia uhuru wa kisanii, mshairi huweza kutilia nguvu miundo ya lugha iliyozowewa na iliyoshirikishwa katika utungo.

Kutokana na matumizi ya methali katika ushairi, vionjo mbalimbali vya ufahamu hufunguliwa na huathiriwa huku fikra ya hadhira ikichochewa kwa ustadi. Kwa sababu hiyo, ushairi hupata utajiri wa kiuchambuzi, chemichemi ya ujumi wa kiumbuji na utamu wake hutokana na miundo hiyo ya lugha teule iliyotumika katika shairi (Njogu 1993). Kadhalika, uchochezi wa ufasiri wa ujumbe uliowasilishwa katika ushairi huweza kutanuliwa zaidi kutokana na matumizi mwafaka ya methali. Kwa hivyo, matumizi ya methali huufanya ushairi kuwasilishwa na kupokewa kwa ufunguzi mpya wa kimtazamo kulingana na uwezo wa kiufasiri wa hadhira. Katika muktadha huo, ushairi huweza kuwasilishwa kwa kuzingatia methali zilizofahamika katika jamii lakini huhitaji uzami wa tafakuri ili kuelewa ujumbe ambao umepitishwa na mtunzi. Kimsingi, ujumbe au maudhui ambayo huwasilishwa huweza kuwa ni yale yale hutokana na mazingira ya jamii ambapo matumizi ya methali katika ushairi wa Kiswahili huufanya utungo kuwa wenye mtazamo mpya wa kiufasiri na kimawasiliano.

2.1.16 Methali Kama Chombo cha Kuwasilishia Hisi na Kubainisha Itikadi ya Mtunzi

Miundo au kauli mahususi ya lugha hutumika katika ushairi ili kubainishia na kuwasilishia mawazo ambayo hutokana na hisi. Katika muktadha huo, matini zilizotumiwa ndizo kuubeba ujumbe ambao umewasilishwa katika ushairi. Kadhalika, matumizi ya miundo mahususi ya lugha huchochea hisi za wasomaji kuhusu maswala ya kijamii ambayo husawiriwa na huwakilishwa. Kwa hivyo, mshairi hawezi kulitungia na kuliwasilishia jambo lolote lile linalohusu mazingira ambayo hupatikana katika jamii bila ya kuwa na mshawasha uliomsukuma hadi kuweza kushika kalamu na kuanza kutunga shairi lake. Jambo hilo pengine huwa limemgusa moyo na kumkera mno mawazoni (Frolova 2008 na Kuvuna, Mvati na Maliachi 1992). Katika muktadha huo, mshairi hapati liwazo la moyo hadi pale amebainisha hisi hizo na kuziwasilisha kwa hadhira (Senkoro 1988 na Chacha 1987). Isitoshe, mpekecho wa mawazo hayo huwa yamefumbikwa katika mwelekeo mahususi ambao huumba na hujenga hisi ambazo huwasilishwa. Aidha, uteuzi na matumizi ya methali humfanya mtunzi kusawiri, kubainisha na kuwasilisha mpekecho wa hisi hizo kwa ufasaha zaidi. Kwa sababu, lugha ambayo imetumiwa si ya wazi bali ni ya kimafumbo. Kwa hivyo, hisi na itikadi ya mtunzi huweza kubainishwa zaidi kwa kuzingatia kauli teule zilizotumiwa kama vile methali.

Baadhi ya wahakiki wa ushairi wa Kiswahili wana mawazo kwamba, huu ni utanzu ambao huwasilishwa kwa kuzingatia mantiki na mpangilio maalumu wa maneno ambao kwa kawaida, ni lugha iliyojengwa katika tamathali za usemi (Mulokozi na Kahigi 1982,

Leech 1969 na Nowottny 1968). Kauli hizo huwa ni zile teule, ambazo hutumika katika ushairi ili kueleza mawazo au hisi fulani kuhusu maswala mbalimbali ya maisha ya mwanadamu kwa njia inayoburudisha na kugusa moyo (Frolova 2008 na Mwamzandi 2002). Kwa hivyo, miundo ya lugha teule iliyotumiwa humfaidi mtunzi wa mashairi katika kuwasilisha hisi hizo kwa uelekezo wa makusudi ambao huiathiri hadhira. Kwa sababu, kila kauli ilizotumiwa katika uwasilishaji wa ushairi huwa ni ile ambayo imeteuliwa kwa makusudi na kutumiwa kwa mwelekeo wa mtunzi.

Hata hivyo, si lazima shairi kuweza kutungwa ili uburudishe moyo iwapo lengo la mshairi si hilo. Kwa sababu, badhi ya watunzi wa ushairi wa Kiswahili husawiri na huwasilisha mawazo kwa njia ambayo hukera na huhuzunisha moyo (Senkoro 1988 na Kezilahabi 1977). Aidha, kauli teule zituzotumikazo utunzi na uwasilishaji wa ushairi ni zile ambazo huibuliwa kwa uelekezi wa hisi na mchomo wa mtunzi (Osiemo 1997, Steen 1994, Wanyoike 1976 na Mohamed 1977). Jambo lililozingatiwa hapa ni kwamba, hisi hubainishwa kwa hadhira lengwa kupitia kwa kauli teule zinazotumika katika uwasilishaji wa utungo. Hisi hizo huweza kuwa za kuburudisha au kukirihisha kutegemea mwelekeo wa ujumbe unaozingatiwa. Kutokana na matumizi ya methali, mtunzi huweza kubainisha kiubunifu hisi (ingawa si lazima) na wakati uo huo kuchochea hisi za hadhira.

Ushairi mzuri wa Kiswahili ni ule unaowasilisha hisi zinazolandana na ujumbe wa mshairi. Kwa hivyo, ni muhimu iwapo mtunzi kufanya uteuzi mzuri wa miundo maalumu ya lugha ambayo huwa ni dira ya kuelekeza ufumbaji wa ujumbe

uliowasilishwa na pia inayoathiri usomaji wa shairi. Miundo hiyo mahususi inayotumika mno katika utunzi wa mashairi ni ile ambayo imejengwa katika tamathali za usemi. Kwa ambavyo katika mawasiliano ya jamii kuna methali zenye miundo maalumu, huweza kutumika katika utunzi wa mashairi ili utungo huo uchochee hisi fulani kwa hadhira. Hiyo haimaanishi kuwa ni methali tu ambazo huchochea hisi za wasomaji bali hata kauli zingine zilizobuniwa kibinafsi huweza kutekeleza dhima hiyo.

Mshairi anapotunga shairi huwa ana mwelekeo wenye mchecheto wa aina fulani hutokana na tajiriba au uhalisi wa mazingira hayo (Njogu 1993 na Massamba 1983). Kadhalika, methali ni zao mahususi la jamii ambapo huweza kupatanishwa na miktadha yoyote mbalimbali inayopatikana ndani na nje ya ushairi husika. Kwa kutumia methali, mshairi huweza kubainisha na kuwasilisha ujumbe kutokana na hisi zinazoibushwa na tajiriba la uhalisi huo wa maisha ya jamii. Aidha, matumizi hayo huweza kubainisha zaidi hisi na mwelekeo wa fikra za mshairi katika utungo. Uteuzi mwafaka wa methali katika ushairi, huwa ni dira ya kujengea mihimili ya kufafanulia ujumbe kwa kuzingatia mtazamo, mwelekeo na hisi za mtunzi. Mtunzi hufahamu kwamba, hisi katika utungo sharti kujengwa na kuwasilishwa kwa njia ambayo huweza kufasiriwa kwa mwafaka kutokana na kauli mahususi zilizotumiwa hususa, methali.

Ingawa lugha ya Kiswahili ina methali anuwai, uteuzi mwafaka ni muhimu kuzingati
ili ujumbe unaowasilishwa usiwe ni mlundiko wa mawazo tu bali iwe ni mbinu
hadhira kutunga hisi maalumu mawazoni. Kwa hivyo, methali ambazo h
mwafaka katika utunzi na uwasilishaji wa hisi, ushairi huacha athari k

katika ufasiri na upokezi wa ujumbe ambao umekusudiwa. Kutokana na matumizi ya methali, hadhira huweza kujenga picha ya kimawazo na sitiari ambazo huufanya ushairi uwe ni kivutio au kielekezo cha kuelewa mwelekeo na maono ya mtunzi.

2.1.17 Methali kama Kauli Teule za Kuielekeza na Kuiadilisha Jamii

Methali katika ushairi wa Kiswahili huweza kutumika kama nyenzo au mizani ya kupimia uhalisi wa maisha na kuwasilishia maadili katika jamii. Aghalabu, watunzi wa ushairi wa Kiswahili huutumia utanzu huu kwa lengo la kuwasilisha uhalisi wa maisha katika muktadha wa utamaduni wa jamii. Kwa mfano, ushairi wa Kiswahili hutumia kauli za lugha ambazo ni mfumo wa maneno ambayo husheheni hekima na busara tangu kale. Katika muktadha huo, hubainishia, hupimia maisha na kufunzia maadili katika jamii. Vile vile, ushairi wa Kiswahili ni utanzu maarufu ambao hutegemewa zaidi katika uelekezaji na kutoa maongozi mema katika jamii (Abdalla 1973 na Mnyampala 1970). Jambo hilo limwezekana kutokana na uteuzi na matumizi ya methali ambazo hupatikana kwa urahisi katika mawasiliano ya watu (Gesero 2009 na Maitaria 2008).

Kimsingi, uamilifu wa ushairi wa Kiswahili pia hupata uhai wake wa kimaadili kutokana na matumizi ya methali zilizotumiwa katika utanzu huu. Kadhalika, methali huweza kutumiwa katika kusawiri, kupimia uhalisi, kuelekeza na kukashifu baadhi ya matendo ya watu katika jamii. Kwa hivyo, matumizi hayo huufanya ushairi kupitishia maadili ambayo tayari yameyakinishwa na yamekubaliwa katika jamii. Mawazo au ujumbe ambao umewasilishwa, hurutubishwa zaidi kutokana na matumizi ya methali ambazo

huchota au huteka maudhui hayo katika mazingira maalumu yapatikanayo katika jamii (Kunemah 2008 na Msokile 1992).

Kadhalika, ushairi ni utungo wenye ujumbe au mawazo ambao huwasilishwa kwa hadhira kutokana na upangaji mzuri wa maneno fasaha ya mizani na kwa kifupi ili kuonyesha ukweli fulani wa maisha (Mulokozi na Kahigi 1982 na Kezilahabi 1977). Hata hivyo, maneno fasaha si lazima kutokana na methali bali pia huweza kupitia kwa kauli zilizobuniwa kwa makusudi na kutumiwa katika uwasilishaji wa shairi. Katika muktadha huo, upangaji na uteuzi mzuri wa maneno fasaha katika utunzi wa ushairi wa Kiswahili huweza pia kutokana na matumizi ya methali ambayo huashiria ukweli fulani wa maisha katika jamii. Kwa kuzingatia matumizi ya methali katika mashairi ya Kiswahili, huufanya utungo kuusawiri uhalisi wa maisha ya jamii katika muktadha wa utamaduni. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mojawapo ya taratibu ambao huzizingatiwa katika uwasilishaji wa tungo za ushairi na nyimbo ni matumizi ya kauli teule za kimapokeo. Aidha, kauli hizo huwa ni maarufu kutokana na maudhui ya kimaadili ambayo huibuliwa (Nagler 1974 na Lord 1960).

Kutokana na matumizi ya methali katika ushairi wa Kiswahili, msomaji au msikilizaji huwa kama mwanafunzi anayejifunza mengi kuhusu ukweli ambao huubainisha uhalisi wa maisha ya jamii. Kwa kutumia methali katika tungo, watunzi huwasilisha mafunzo adhimu ambayo hutarajiwa kumjenga msomaji kuwa mwanajamii na pia kumwelekeza katika kukabiliana na uhalisi wa maisha. Kimsingi, washairi wa Kiswahili huwa ni watu wenye upeo wa juu kuhusu maisha, wenye kuona mbali, walioelimika katika mambo

mengi yanayohusu dunia na wenye lengo la kutoa uelekezi mwema katika jamii (Mazungumzo na Sheikh Nabhany (tarehe 26 Machi, 2011). Kwa hivyo, mshairi wa Kiswahili huwa ni kama mwalimu ambaye hutegemewa kwa dhati katika jamii. Iwapo mtunzi wa ushairi hutumia nafasi hiyo vibaya kuwalaghai watu, hukiuka wadhifa na wajibu huo katika jamii.

Mtunzi wa mashairi anapotumia vizuri methali katika utungo, husaidia siyo tu kuwasilisha maudhui ya kijumla bali pia kuidhinisha maongozi na mielekeo bora katika jamii. Hadhira inapousoma ushairi, hujengewa misingi ya manufaa ya uadilifu ili iweze kujiepusha na mambo thakili katika jamii. Hilo ni jukumu muhimu ambalo mtunzi wa ushairi wa Kiswahili hutwishwa. Kwa sababu, yeye ni mtu ambaye huwajibika na hutegemewa katika jamii. Kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, utungo wa fasihi kama vile ushairi na nyimbo hupata umaarufu wake kupitia kwa kushirikishwa kwa kauli za kimapokeo ambazo hutoa maongozi ya kimaadili katika jamii (Lord 1960 na Levi-Strauss 1955). Kwa hivyo, kauli teule zinazotumika, ushairi wa Kiswahili huwa kama kioo cha jamii cha kujitazama, kujikosoa na kujirekebisha (Abdalla 1973). Hapa ieleweke kwamba, jamii nyingi za Kiafrika hupenda watu wawe wenye maelewano mema na utangamano miongoni mwao (Maitaria 2008). Ingawa mshairi huwa habainishi wazi kuhusu ukweli huo wa maisha, huweza kutumia methali ili utungo usiwe wenye utusani ndani yake na wakati uo huo kupitisha mafunzo ya kimaadili (Noor 1988). Hata kama shairi ambalo hurejelewa lina ujumbe wa kukemea au kushutumu baadhi ya matendo maovu katika jamii, mshairi hapaswi kukwepa ukweli huo. Kwa hivyo, mshairi huweza kuuwasilisha ujumbe kutokana na uteuzi mzuri wa

methali ambazo ni zao la jamii. Kwa njia hiyo, mtunzi wa ushairi wa Kiswahili hawezi katu kulaumiwa na jamii bali hadhira hutarajiwa kurejelea misingi ya kauli zilizobuniwa na zilizokubalika katika uhalisi wa utamaduni wa jamii ya mtunzi.

2.1.18 Methali kama Kipengele cha Kudhihirishia Weledi wa Lugha

Msanii wa ushairi wa Kiswahili huzingatia uteuzi mwafaka wa msamiati na miundo teule ya lugha inayotumika katika utunzi na uwasilishaji wa utungo. Ushairi huo unapozingatiwa, hubainisha miundo mbalimbali ya lugha iliyotumika kwa makusudi na kwa ustadi mkubwa (Njogu na Chimerah 1999, Njogu 1996 na Senkoro 1988). Isitoshe, uwanja wa ushairi wa Kiswahili husaidia katika kudhihirishia ujuzi au umahiri wa msamiati na miundo teule ya lugha katika kuwasilishia ujumbe kwa wasomaji (Zubkova-Bertoncini 2008). Kwa hivyo katika uwasilishaji wa ushairi, kuna matumizi ya miundo maalumu ya lugha iliyozoweleka katika mawasiliano ya jamii.

Kadhalika, katika usawiri wa ushairi wa Kiswahili kuna miundo sufufu ya lugha ambayo haijajulikana au haijazowewa katika mawasiliano ya jamii (Abdulaziz 1979 na Nassir 1971). Kwa hivyo, mshairi huweza kuifinyanga kiufundi miundo ya lugha iliyozoweleka katika jamii na kuifanya iwe yenye mielekeo tofauti na sura mpya. Katika muktadha huo, utunzi na uwasilishaji huo huzingatia siyo tu miundo ya lugha iliyozoweleka katika jamii bali pia kauli zilizobuniwa kwa maksuudi ili kuchangia zaidi miundo hiyo. Kwa kuzingatia nadharia ya Semiotiki, mawazo au ujumbe huweza kuwasilishwa kupitia kwa visawe vya ishara au kupitia kwa kauli ambazo ni tofauti na ujumbe huwa uo huo (Scholes na Parry 1971). Kwa mfano, kauli ambazo hutumika kujengea taswira na isitiari

ni ile ya kawaida katika mawasiliano ya jamii, huifanya hadhira kupata nafasi ya kuchochea tafakuri zao ili kuufasiri upya ujumbe unliowasilishwa katika shairi.

Weledi wa mtunzi humfanya kuteua miundo fulani ya methali na kuiacha ile isiyoweza kumnufaisha. Hapa ieleweke kwamba, ushairi na fasihi kwa ujumla, hutumia lugha inayoubainisha ukweli wa maisha kwa njia ya ubunifu. Kwa hivyo, kuna uwiano wa karibu baina ya kauli mahususi zilizotumiwa na tajiriba la msanii (Fowler 1996). Hata hivyo, mshairi hodari wa Kiswahili huwa ana mizungu na njia mbalimbali za kuumulia na kuuwasilishia ujumbe. Aidha, methali ambazo hutumiwa hutokana na uzoefu na tajiriba ya utunzi. Vile vile, methali zilizotumiwa huwa zimechopekwa ili kuweza kuwiana na kauli zingine zilizopo katika shairi. Kwa hivyo, matumizi ya methali husaidia katika kuusawiri ujumbe kwa kuzingatia athari maalumu ambayo hukusudiwa kuibuliwa katika shairi.

Methali ambayo hutumiwa katika ushairi wa Kiswahili kama chombo cha mawasiliano, huhitaji umahiri wa kiupembuzi katika kupatanisha muundo wa utungo na uibushaji wa mawazo ambayo huwasilishwa. Kwa sababu ya ujuzi wa lugha alionao, mshairi hana wasiwasi katika kuisarifu upya miundo hiyo ya lugha ili iweze kumtumikia kama chombo cha kuuwasilisha ujumbe katika utungo. Kifani, methali zinapotumiwa vizuri katika ushairi wa Kiswahili, humsaidia mtunzi kubainishwa na wahakiki wa fasihi kuwa bora anapolinganishwa na washairi wengine ambao hawana ujuzi mkubwa wa kuisarifu lugha. Ingawa mtunzi hodari wa ushairi ana mizungu mbalimbali za kuwasilishia ujumbe wake, kila wakati huwa tayari kuzinoa na kuzipiga msasa mbinu alizonazo za lugha ili ziwe

bora zaidi. Kwa mfano, mashairi ya 'Mnazi: Vuta N'kuvute' na 'Kutendana' ambayo hupatikana katika *Sauti ya Dhiki* (Abdalla 1973:17-22, 89-110) yametumia methali zaidi ya moja katika uwasilishaji. Katika muktadha huo, imedhihirishwa kuwa utungo huweza kutumia methali zaidi ambapo kila moja hushikilia nafasi muhimu.

2.1.19 Methali kama Chombo cha Kujengea Taswira na Isitiari

Mtunzi hodari wa mashairi ya Kiswahili huhakikisha kuwa utungo ambao unawasilishwa umezingatia kauli au miundo mwafaka ya lugha. Miundo hiyo teule husaidia katika kuuwasilisha ujumbe kwa hadhira kwa njia iliyo mwafaka (Syambo na Mazrui 1992). Aidha mtunzi anapofanya hivyo, huweza kudhibiti na kuchochea hamu ya usomaji. Kwa sababu, ushairi ambao huzingatia mbinu za aina moja katika uwasilishaji huichosha na huikifu hadhira. Kadhalika, ushairi unaowasilishwa kwa kuzingatia kunga mwafaka za uwasilishaji, hufungua na huathiri vionjo vya milango yote ya ufahamu (King'ei na Amata 2001, Mutembei 1993 na Senkoro 1988). Kwa hivyo, ushairi mzuri wa Kiswahili ni ule ambao huchochea hisi za hadhira kwa namna mbalimbali kutokana na mizungu katika uteuzi matini na miundo ya lugha.

Kimsingi, miundo mahususi ya lugha huteuliwa kimakusudi na mshairi ili kujenga taswira ambayo hukusudiwa kujengwa katika akili ya wasomaji (Wamitila 2006 na Nyanchama 2004). Baadhi ya taswira ambazo hutumika zaidi katika utunzi wa ushairi ni kama: taswira zionekanazo, za mawazo na zile za hisi. Methali ambazo hutumika kwa mwafaka huweza kujenga taswira au picha za kimawazo ambapo huusukuma mbele ujumbe unaowasilishwa katika shairi la Kiswahili. Picha hizo hurutubishwa zaidi kwa

matini za kiisitiari ambazo zimefundikwa ndani yake. Taswira na isitiari ni mbinu ambazo huchangiana na hukamilishana katika uwasilishaji wa shairi (Musungu 2005). Kadhalika, methali ni kauli ambazo hujibainisha zaidi katika tamathali za usemi kama vile tashibihi, takriri, tashihisi, kinaya na kejeli. Kwa hivyo, methali ambazo zimetumiwa katika ushairi huifanya hadhira kuusoma utungo kwa tuo, hadhari na kwa utafakari zaidi. Mbinu ya taswira na isitiari kwa pamoja, huufanya ushairi wa Kiswahili uwe hai na mpevu zaidi. Kwa sababu, hadhira hudhibitiwa na hushirikishwa kakamilifu katika jitihada za kuupokea ujumbe uliokusudiwa.

Mshairi wa Kiswahili anapouwasilisha utungo kwa kuzingatia mbinu ya taswira na isitiari zilizojengwa kutokana na methali husaidia kuibua na kuathiri vionjo mbalimbali vya ufahamu wa hadhira. Katika mawazo ya hadhira, vionjo hivyo ambavyo huibuliwa ni kama vile ya kusikia, kuona, kunusa, kuonja na kugusa (Mulokozi na Kahigi 1982). Kwa hivyo, matumizi ya methali teule katika ushairi wa Kiswahili, humfaidi msomaji au msikilizaji kutunga hisi za aina fulani kulingana na lengo au mawazo yaliyowasilishwa. Kwa mtunzi, uwasilishaji wa ushairi hudhibitiwa zaidi kwa tamathali za usemi zilizoibuliwa. Kwa hivyo, dhima ya matumizi hayo huwa zenye pembe mbili ambapo humfaidi mtunzi na msomaji wa utungo.

Shairi la Kiswahili lililojengwa katika taswira na isitiari mwafaka huvuta hamu ya msomaji kutaka kuendelea kusoma mara kwa mara. Kwa sababu hiyo, ushairi hutarajiwa kuibua hisi na mguso wa aina fulani ulioakisi uhalisi wa maisha ya jamii. Mbinu ya taswira ambayo ni mwafaka kwenye shairi, ni matokeo ya uwiano uliopo baina ya

miundo teule ya lugha ambayo hutumiwa kufananisha au kumithilisha tukio na uhalisi wa maisha katika jamii. Kimsingi, mtunzi wa ushairi wa Kiswahili hutumia miundo teule ya lugha ya kawaida ambayo pia husaidia katika kuunda picha za kimawazo katika akili ya msomaji au msikilizaji kuhusu ujumbe ambao umewasilishwa. Matumizi hayo ya uwasilishaji, huwa ni mbinu ya kumfanya msomaji katika kuhifadhi na kurejelea fani mahususi zilizotumiwa na maudhui ambayo yamebuliwa katika utngo (Peck na Coyle 1984 na Olsen 1973). Kwa ambavyo methali zina ufunuo wa kimawazo, aghalabu hutumiwa kuwa nyenzo ya kuibulia kauli nyinginezo za makusudi katika uwasilishaji wa ujumbe. Katika muktadha huo, msomaji au msikilizaji wa ushairi huweza kuupokea ujumbe kwa uwazi zaidi huku akiupatanisha na tajiriba ambayo huhusu uhalisi wa maisha katika jamii.

Washairi hodari wa Kiswahili hutumia mbinu ya taswira na isitiari kwa azma ya kuzinasa hisi za hadhira kwa kuziundia picha kamili ambazo huhitaji utafakari na ufasiri wa ujumbe ambao umechochewa au kuwasilishwa. Kadhalika, matumizi ya methali ambayo huwasilishwa kama taswira na isitiari kamili katika ushairi wa Kiswahili husaidia katika kubainisha zaidi ujumbe kwa njia ya picha ya kimaono na ya kimawazo.

Picha za kimawazo zinazoundwa kupitia kwa matumizi ya methali katika ushairi wa Kiswahili humfanya msomaji kusaili na kutafakari mawazo ya mshairi yanayowasilishwa. Hadhira inapofanya hivyo, huweza kuupata ujumbe kwa usahihi na uwazi zaidi. Kwa ambavyo ushairi wa Kiswahili ni utungo mfupi, mawazo ya mtunzi huwasilishwa kimuhtasari na kwa njia ya picha. Kulingana na nadharia ya Fomula ya

Kisimulizi, mtunzi wa nyimbo au ushairi hana muda mwingi wa kujieleza kwa hivyo huteua kauli ambazo husaidia katika uwasilishaji wa ujumbe (Wood 1971 na Whallon 1969). Kama ilivyokwisha kuelezwa hapo awali ni kwamba, ujumbe ambao huwasilishwa katika shairi huwa haufafanuliwi kwa kina. Kwa hivyo, kauli ambazo hutumiaa ni zile ambazo huuwasilisha ujumbe kimaono na kiisitiari. Kutokana na matumizi hayo, msanii huweza kuwa na mbinu ambazo huchangia zaidi katika uwasilishaji wa utungo.

2.1.20 Methali kama Chombo cha Kuibulia na Kujengea Usambamba

Mshairi wa Kiswahili hutumia kauli au miundo maalumu ya maneno ambayo hufanana kimaana na kimuundo (Wamitila 2002 na Mulokozi na Kahigi 1979). Kimsingi, mshairi anapotunga ushairi huwa na dhamira maalumu. Dhamira yiyo hiyo ya mtunzi huweza kufafanuliwa zaidi kupitia kwa urejelezi wa miundo ya lugha iliyotumika. Miundo hii huweza kufanana au kutofautiana na ile teule iliyozingatiwa.

Matumizi ya methali huufanya ushairi kuukariri na kuufafanua ujumbe kwa kuzingatia kauli tofauti tofauti katika uwasilishaji wa ushairi. Zaidi ya kuukoleza ujumbe, huwa ni kunga au mbinu mahususi ya uwasilishaji. Katika muktadha huo, ushairi huweza kutumia methali kama mbinu ya kujengea dibaji au usuli wa ujumbe ambao umewasilishwa. Vile vile kwa kutumia methali, ushairi huweza kuwasilishwa kwa miundo tofauti tofauti ambayo hujengana na hukamilishana. Katika kuushadidia na kufafanua zaidi ujumbe, utungo huo huweza kutumia miundo mingine ya lugha kwa uelekezo wa ujumbe ulioibuliwa na uliofumbwa kiusanii katika methali iliyotumiwa. Kwa hivyo, mshairi

huweza kudhihirisha ustadi wa kiumbuji katika kuuwasilisha utungo huo. Isitoshe, shairi ambalo limewasilishwa kwa kuzingatia mbinu ya usambamba huwa una uzito wa kiuchambuzi na kifani.

Matumizi mwafaka ya methali katika utunzi wa ushairi humfanya msomaji kuuelewa ujumbe uo huo kwa kuzingatia maelezo ambayo hupatikana katika miundo mingine iliyoteuliwa na kutumiwa kwa makusudi. Kwa sababu hiyo, usomaji wa ushairi wa Kiswhaili huvutia na wala haukifu kutokana na mizungu iliyotumika. Aidha, matumizi ya methali humsaidia zaidi mshairi kuvyaza miundo mbalimbali ya lugha katika harakati ya kuwasilisha ujumbe. Kimsingi, miundo ya aina moja au ile iliyozowewa humchosha msomaji wa ushairi. Kwa kawaida msomaji huwa havutiwi kwa miundo ya aina moja iliyotumiwa katika kujieleza. Isitoshe, mtunzi huweza kusutwa kuwa amepwelewa katika mizungu ya uwasilishaji. Matumizi ya mbinu ya usambamba katika ushairi yasichukuliwe kuwa ni dhihirisho la kuishiwa au ufilisi wa kujieleza (Leech 1969). Iwapo imewasilishwa dhamira au maudhui mahususi, hubidi mawazo hayo kukaririwa kwa kutumia kauli na miundo mingine ya lugha ili ujumbe kuweza usaki kwa mwafaka zaidi katika akili na mawazo ya mpokezi.

Kutokana na matumizi hayo ya methali katika ushairi, wasomaji huupata kwa urahisi ujumbe wa ndani uliowasilishwa. Kwa sababu ujumbe huo, hukaririwa kwa kauli zingine ambazo pia ni muhimu katika uwasilishaji wa utungo (Nagler 1967). Kwa sababu, mshairi huenda akatumia methali ambayo ina utata au isiyoeleweka kwa urahisi katika mawasiliano ya jamii. Katika muktadha huo, mbinu ya usambamba huweza kutumika

kwa makusudi kama dira ya kufafanulia zaidi maudhui yanayowasilishwa na pia kama mbinu ya kuongoza katika kuupata ujumbe uliokusudiwa. Kwa hivyo, usambamba ambao huibuliwa kupitia kwa methali katika uwasilishaji wa ushairi, huwa ni mbinu mwafaka zaidi humsaidia mshairi kutumia na kuangazia mifano mbalimbali inayopatikana katika mawasiliano ya kawaida katika jamii. Katika muktadha huo, mtunzi hutumia kauli ambazo huwa ni tofauti lakini zenye kushadidia kwa ustadi wazo moja ambalo huwasilishwa katika utungo.

Kutokana na sababu hiyo, mtunzi hupaswa kuwa mweledi katika uteuzi wa methali ambayo husaidia katika kuuwasilisha ujumbe kwa mizungu au njia angavu zaidi. Methali zinazotumika humfanya mtunzi kuufafanua zaidi ujumbe ambao umekusudiwa kwa njia tofauti ambayo ni bayana na katu haiitatanisha hadhira. Ingawa utata huo ni mbinu muhimu katika uwasilishaji, wakati mwingine mshairi huweza kuhisi kuwa ujumbe uliowasilishwa haujapitishwa ilivyostahili. Kwa hivyo, huweza kuondolewa katika ushairi kwa kuzingatia mbinu ya usambamba. Kwa ambavyo methali huweza kuwa ni kauli zilizozowewa katika mawasiliano ya jamii, huweza pia kutumika kiusanii kama mbinu ya kuibua na kujengea usambamba katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Iwapo hadhira inapata matatizo ya kufasiri maana iliyokusudiwa katika methali, maelezo hutolewa husadifu katika kuufafanua zaidi ujumbe uo huo. Kwa hivyo, mbinu ya usambamba ambayo hushirikisha matumizi ya methali katika utunzi na uwasilishaji, huufanya ujumbe kuweza kubainishwa kwa uwazi zaidi.

2.3 KIISHILIO

Sura hii imechanganua namna methali huweza kutumiwa kama fomula katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, imebainishwa kuwa methali ni kauli au msingi katika utunzi na uwasilishaji wa mashairi. Matumizi ya methali huwa siyo tu mbinu ya kuudhibiti muundo wa ushairi na ubainishaji wa mtindo bali pia huutajirisha na kuutilia nguvu ujumbe ambao umewasilishwa.

Kwa ambavyo methali ni miongoni mwa kauli maarufu zilitumiwa katika mawasiliano ya jamii. Kwa hivyo, zimekuwa zikishikilia nafasi muhimu katika utunzi na uwasilishaji wa mawazo katika ushairi. Kadhalika, methali ni kipengele ambacho kinahitaji kujengewa kisa, hutolewa ufafanuzi wa maelezo ya kina kwa kuzingatia tajiriba na hisi za mshairi. Ujumbe huo huweza kudokezewa na kuwasilishwa kimuhtasari kwa kuzingatia methali moja au zaidi ambazo hupatikana katika mawasiliano ya jamii. Katika muktadha huo, methali huweza kutumika katika tungo za kimapokeo, tungo za kati na tungo za ushairi huru. Isitoshe, matumizi ya methali kwenye utunzi wa ushairi huurejesha na huuweka ushairi andishi wa Kiswahili ambao hudai ukale wake katika miktadha na misingi ya utunzi na ya uwasilishaji. Kwa sababu, hapo awali na hata wakati wa sasa, baadhi ya tungo ambazo huzingatia arudhi za kimapokeo hutungwa na huwasilishwa kwa mbinu za kimasimulizi.

Kadhalika, wakati wa sasa bado kuna wasanii wengi ambao hutunga tungo na kwa kuzitongoa bila kuziandika. Kwa hivyo katika jamii ya sasa, ushairi wa Kiswahili umetamalaki katika fasihi andishi na simulizi. Kwa mfano, kabla ya hati za uandishi

kuvumbuliwa, ushairi wa Kiswahili ulikuwa ukitungwa na kuwasilishwa kimasimulizi. Kadhalika imebainishwa kuwa, tungo hizo hushirikisha zaidi kauli teule kama vile methali katika uwasilishaji.

Vile vile, imethibitishwa kuwa methali ni chombo cha kuichochea na kuitafakarisha hadhira katika usomaji wa ushairi. Kwa kuzingatia methali zilizotumika, wapokezi huupokea ujumbe uliowasilishwa kwa upevu na kwa kina zaidi. Kwa ambavyo methali ni zao la utamaduni wa jamii, ujumbe ambao hukusudiwa katika ushairi wa Kiswahili hujengwa katika misingi na muktadha wa utamaduni na uhalisi wa maisha ya watu. Isitoshe, methali ni miongoni mwa vito muhimu ambavyo hutumika katika kutilia nakshi na kukikweza kiwango cha lugha ambacho hutumika katika uwasilishaji wa tanzu za fasihi kama vile ushairi.

Katika sura hii imefafanua kuwa, matumizi ya methali huufanya utanzu wa ushair kuweza kuchukuliwa kuwa ni zao la utamduni wa jamii. Kwa kufanya hivyo, wanajamii huukumbatia na huuenzi ushairi wa Kiswahili kama chombo mwafaka cha kuhifadhi uhalisi wa maisha ya jamii katika muktadha wa utamaduni wao. Hiyo hutokana na sababu kwamba, ushairi wa Kiswahili hushirikisha matumizi ya methali zilizofinyangwa kwa kuzingatia mazingira mahususi ya watu. Kwa hivyo, methali zilizotumika katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi huweza kufasiriwa kwa kuzingatia utamaduni pana wa jamii ya Afrika.

Kadhalika, mshairi wa Kiswahili ana uhuru wa kuteua kauli yoyote ya lugha ili iweze kutumika katika usawiri na uwasilishaji utungo. Kauli hizo ni zile ambazo ni maarufu

katika mawasiliano ya jamii au zile ambazo hubuniwa kwa makusudi. Kimsingi, miundo hiyo ya lugha teule aghalabu hujibainisha katika tamathali za usemi. Kwa sadfa, miundo ya methali huwa imeleweka kwa kuzingatia misingi ya tamathali za usemi. Katika muktadha wa uwasilishaji, ushairi umenufaika zaidi kutokana na uwepo wa methali katika jamii. Vile vile, katika ushairi wa Kiswahili kuna matumizi ya kauli ambazo hubuniwa kwa makusudi. Ingawa kauli hizo huweza pia kukidhi mawasiliano, matumizi yazo hufafanua zaidi methali zilizotumika katika shairi. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, mshairi anapouwasilisha utungo huwa ana hiari ya kutumia kwa uwazi au kutotumia kwa uwazi kauli hizo za kimapokeo kama vile methali.

Kwa hivyo, hakuna ulazima wowote wa kutumia methali kwa uwazi katika uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili. Utungo ulitumia au usiotumia methali kwa uwazi, huwa ni mitindo ya kujenga fani ambayo huudhibiti muundo na umbo katika shairi. Isitoshe, ujumbe na mawazo ambayo huwasilishwa hufumbwa katika kauli hizo teule zilizotumika katika utungo. Washairi wa Kiswahili ambao hawakutumia methali kwa uwazi katika utungo, haimaanishi ya kwamba huuuuzia dhima na utendakazi wa methali katika uwasilishaji wao. Jambo la msingi ni kwamba, mashairi hayo yasiyotumia methali bayana, ujumbe ambao huwasilishwa huwa umejengewa mwangwi wa methali. Kwa hivyo, huweza kufasirika vyema kwa kuzingatia methali mahususi ambazo hupatikana kwa urahisi katika mawasiliano ya jamii. Kwa sababu, kila tukio muhimu katika jamii huweza kuwasilishwa kwa mshabaha wa methali zilizopo.

Isitoshe, sura hii imebainishwa kuwa matumizi ya methali huwa ni bayana zaidi katika utunzi wa mashairi ya kimapokeo kutokana na umbo na muundo ambao huruhusu kutumika kwa methali. Mashairi huru nayo hayana ulazima wowote wa kutumia methali moja kwa moja. Kwa sababu, ujumbe ambao uliowasilishwa huweza kuhusishwa moja kwa moja kupitia kwa methali mahususi. Katika muktadha huo, matumizi ya methali huweza kuwa kigezo cha kuuainishia ushairi huu.

SURA YA TATU

UCHANGANUZI WA USHAIRI WA KIMAPOKEO KWA LENGO LA KUTATHMINI MATUMIZI YA METHALI

3.0 UTANGULIZI

Sura hii imehakiki baadhi ya mashairi ya Kiswahili ambayo huzingatia arudhi za kimapokeo kwa malengo ya kutathmini dhima ya methali katika utunzi na uwasilishaji. Katika kitengo hiki, kuna washairi wengi ambao wameweza kutunga na kuchapisha tungo zao katika diwani mbalimbali. Miongoni mwa watunzi hao ni kama vile Nyamaume 1999, Mzenga na Hijazy 1995, Karama 1985, Amana 1982, Khan 1981, Kandoro 1978, Mayoka 1977, Snow-White 1974 na Abdalla 1973. Hata hivyo, mashairi mahususi yaliyochanganuliwa ni yale yaliyohifadhiwa katika diwani mbili: *Sauti ya Dhiki* (Abdilatif Abdalla) na *Usanifu wa Ushairi* (K.H.A Akilimali Snow-White). Diwani hizo mbili zina mashairi ambayo yana ithibati kubwa ya matumizi ya methali katika uwasilishaji.

Kadhalika, ni mashairi manne kutoka kila diwani ndiyo yaliyochanganuliwa. Kwa hivyo, sura hii imetathmini uwiano uliopo kati ya methali zilizotumika na mawazo yaliyowasilishwa. Aidha, mifano mbalimbali kutokana na mashairi hayo teule ilizingatiwa ili kubainisha namna taswira na isitiari zilivyoundwa kupitia kwa methali zilizotumika. Isitoshe, sura hii pia imedhihirisha namna ujumbe au mawazo husawiriwa na huwasilishwa kimuhtasari kwa kuzingatia muktadha ambamo methali hutumiwa. Vile vile, sura hii imebainisha namna matumizi ya makusudi ya methali yamesaidia katika kujenga taharuki katika udurusu au usomaji wa mashairi.

Kwa ambavyo methali hutumika mno katika mawasiliano ya jamii, sura hii imetathmini matumizi na ufasiri wazo katika mkabala mpana wa utamaduni na uhalisi wa maisha ya jamii. Aidha, methali zilizotumiwa katika mashairi teule zimechanganuliwa ili kubainisha ufaafu wake kama chombo cha kuibulia na uwasilishaji wa maadili na pia kama chombo cha kuashiria hisi na mwelekeo wa washairi.

3.1 UCHANGANUZI WA USHAIRI WA ABDILATIF ABDALLA: *SAUTI YA DHIKI*

Diwani ya *Sauti ya Dhiki* ilitungwa na kuchapishwa mwaka wa 1973 na Shirika la Oxford University Pess (K) Ltd. Diwani hiyo ina jumla ya mashairi arobaini. Hata hivyo, ni mashairi manne tu ndiyo yaliyochanganiuliwa. Mashairi hayo teule ni:

i. Mnazi Vuta N'kuvute
ii. Mwerevu Hajinyowi
iii. Zindukani
iv. Kutendana

3.1.1 Shairi: Mnazi Vuta N'kuvute

Shairi hili ni la muundo wa tarbia na lina beti arobaini na nne. Mshairi ameliwasilisha shairi hili kimalumbano kwa kuwashirikisha wahusika wawili: *Alii* na *Badi*. Kadhalika, mshairi ametumia methali mbili zinazochangiana katika uwasilishaji wake. Methali mahususi zilizotumika ni: *mpiga ngumi ukuta, huumiza mkonowe* na *Heri nusu ya shari, kuliko shari kamili.*

3.1.1.1 Mpiga Ngumi Ukuta, Huumiza Mkonowe

Methali hiyo imetumiwa katika ubeti wa kumi na nane. Kwa ambavyo shairi ni refu, methali hiyo imetumiwa katika beti za awali. Kadhalika, imetumiwa kama mshororo wa tatu katika ubeti huo. Maana ya methali hiyo ni kuwa, mtu anapopigana na ukuta, ni yeye ambaye hujidhuru. Kwa sababu *ukuta* hauhisi uchungu wala maumivu yoyote. Vile vile, methali hiyo ina maana batini kwamba, mtu dhalili hawezi kukabiliana na yule mwenye nguvu. Kiuwasilishaji, methali hiyo imetumiwa kama mbinu ya kutekelezea mambo muhimu yafuatayo.

3.1.1.1 .1 Methali kama Kauli ya Kusawiri na Kubainishia Mahusiano ya Wahusika

Katika shairi hili kuna wahusika wawili: Alii na Badi. Kulingana na maelezo yaliyowasilishwa ni kwamba, wahusika hao wawili waliurithi mnazi kutoka kwa wavyele wao ili uweze kuwanufaisha kutokana na matunda au nazi zake. Wazazi wa vijana hao waliuenzi mti huo na walikuwa wenye matarajio kuwa, wana wao pia watafuata nyayo zao. Haukupita muda mrefu, yaani baada ya mauko ya wazazi wao, vijana hawa wakawa wenye mielekeo au itikadi zilizohitilafiana. Kwa mfano, Alii na Badi walikuwa tayari wamefanya mkataba kwamba, kila mmoja angekuwa na zamu ya kuuparaga mti huo ili kujichumia au kujiangulia nazi. Badi alikuwa wa awali kupanda juu ya mnazi. Alii naye alikuwa chini ya mnazi huku akisubiri kwa shauku kubwa kuwa wakati wake utawadia. Jambo hilo halikutimilia, kwa sababu Badi alikataa katakata kushuka chini. Kwa ambavyo Badi alikuwa mwenye uwezo, aliweza kujijengea ngome yenye nguvu kutokana na nazi alizohodhi. Machoni pa Badi, Alii alionekana mtu dhalili na mchochole kwa vile hakuwa na uwezo wa kupata nazi.

Kutokana na matumizi ya methali ya *Mpiga ngumi ukuta, huumiza mkonowe*, mshairi ameweza kubainisha vitimbi vya ubahili na udhalimu wa Badi dhidi ya Alii. Kadhalika, kwa kutumia methali hiyo, ameweza kumfunulia msomaji kiburi, ubinafsi na ukosefu wa utu uliochipuza katika dhamiri ya Badi. Kabla ya kauli hiyo kutumiwa, Alii alikuwa mwenye subira na hekima ya kumnasihi mwenziwe kuurejelea wosia na maagizo walioachiwa na wazazi wao. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli mahususi za kimapokeo hutumiwa katika mawasiliano ya jamii na pia katika tungo za kifasihi ili kupitishia ujumbe wa kimaadili na kukosoa matendo yasiyofaa (Propp 1968). Katika muktadha wa shairi, methali imetumiwa kuupitisha ujumbe huo muhimu. Hata hivyo, nasaha zote za Alii hazikufua dafu. Kwa ambavyo ni Badi aliyeitumia kauli ya methali, mshairi humtarajia msomaji kuunda mwelekeo au mazingira mahususi kuhusu mhusika huyo. Kwamba, Badi ni mwenye majivuno, ubinafsi na mkosefu wa utu. Mtu kama huyo hawezi katu kuthaminiwa katika jamii. Kulingana na maelezo yaliyotolewa ni kuwa, rasilimali ya jamii huweza kuporwa au kunyakuliwa kimabavu ili kuweza kukidhi au kunufaisha maslahi ya kibinafsi.

Kwa upande wa Alii hutarajiwa kuchukuliwa kama mtu mwema, aliyejaa utu, utulivu na mwenye akili iliyotuama. Kadhalika, kupitia kwa methali, mshairi amemdhihirisha Alii kama mwanajamii aliyebaini kuwa amenyanyaswa, haki hiyo imenyakuliwa na imedhulumiwa. Vile vile, msomaji hujengewa muktadha wa kumaizi uhusiano wa kizandiki baina ya Badi na Alii. Kwa hivyo, ushairi huwa na dhima ya kubainisha hali halisi ya maisha katika jamii. Katika kuzingatia utafakari zaidi wa methali iliyotumiwa, msomaji huweza kung'amua kuwa mahusiano baina ya Badi na Alii si murwa na wala

haukujengeka katika misingi ya utu. Katika muktadha huo, mtunzi ameutilia shaka utajiri na uwezo alionao Badi. Kimsingi, Badi amejineemesha siyo kwa juhudi zake bali kwa kumnyanyasa Alii. Kwa hivyo, matumizi ya methali huweza kusaidia katika kubaini ukakamavu wa Badi ambao umempofusha hadi kiwango cha kuutokomeza utu kwa binadamu wenziwe.

3.1.1.1.2 Tahadhari inayotolewa Kupitia kwa Methali

Mshairi ametumia methali ya *Mpiga ngumi ukuta, huumiza mkonowe* siyo tu kudhihirishia uwezo wa kimabavu alionao mhusika Badi bali pia kama msingi wa kumwonya na kumtahadharisha Alii kutarajia makabiliano makali ambayo huweza kutokea. Kupitia kwa methali, imemfunuliwa kuwa, Alii anapoidai haki hiyo juu ya mnazi, sharti afahamu kuwa hataipata wala kuridhiwa ila kwa kutumia nguvu na kumwaga damu. Kadhalika, imebainishwa kuwa Badi hataridhi matakwa ya Alii kwa urahisi bali alihitaji kulazimishwa au kushurutishwa kuuona ukweli ingawa mchungu. Katika beti za mwanzo katika shairi, mhusika Badi alitumia kauli mbalimbali za kumkejeli na kumdhalilisha Alii. Kwa mfano, Badi tayari amekata shauri kuwa hatashuka kutoka juu ya mnazi. Kwa kuzingatia nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kukatalia kwa Badi juu ya mnazi kumejenga usuli wa ufaraguzi wa matukio katika utungo. Hapa ieleweke kwamba, Badi amekwisha onja tamu ya asali, kwa hivyo hutarajia kuuchonga mzinga; yaani kuuhodhi kikamilifu mnazi. Alii alipojaribu kumnasihi Badi, alichukuliwa kama mtu aliyenyemelea tamu na uhondo wa mwenziwe.

Zaidi ya hayo, Alii alighasiwa na kushangazwaa kumwona Badi alivyoendelea kuusaliti wosia wa wavyele wao. Kwa ambavyo Alii ana uwezo kichele wa kiuchumi, lielewa kuwa alihitaji kuzua mbinu au kupanga mikakati mwafaka za kuidai haki hiyo huku akielewa kwamba huenda akaparuzwa kwa kucha kali za Badi. Kutokana na matumizi ya methali hiyo, mshairi ameweza kumbainisha Badi kama mtu hatari ambaye huweza kutumia mamlaka au uwezo alionao ili kumwangamiza na kumwondoa yeyote (Alii akiwemo) ambaye humhisi kuwa kizingiti au kikwazo cha mafanikio hayo. Aidha, matumizi ya methali yamesaidia katika kudhihirisha kwamba, hata ingawa Badi hujichukulia kuwa amefikia kilele cha ufanisi, hali hiyo haiwezi kuwa shwari daima. Kwa mfano, viongozi ambao hung'ang'ania madaraka hujidai kuwa ni masultani au vigogo waliochaguliwa na Mungu. Ujumbe huo pia umebainishwa katika ubeti wa shairi 'Joho la Maisha' (Mvungi 1982:31-32) kama ifuatavyo:

Asema yeye ajua, ni yeye alijulia
Wengine hawajajua, ni Mola kamchagua
Wengine watachafua, joho hili la maua,
Joho la uzi mwekundu, sijui lavaliwaje

Katika muktadha wa kauli zilizopigiwa mstari, wazo ambalo limewasilishwa ni kwamba, jamii hutambua vitimbi na majivuno ya viongozi kama hao wasiokuwa na utu. Hata katika shairi la 'Mnazi vuta N'kuvute', Alii tayari amezinduka na ameanza kuidai halali hiyo. Katika beti za hapo mwanzo, yaani kabla ya matumizi ya methali hiyo, Badi alikuwa akimwona Alii kama mtu aliyeweza kurairaiwa au kurubuniwa kwa urahisi; kumbe sivyo alivyodhaniwa. Kwa hivyo, mshairi amepotumia methali hiyo ili kutoa tahadhari kwa watu kama akina Badi kwamba, wasiporidhi matakwa ya kina Alii mambo hutarajiwa kuwaendea mrama.

3.1.1.1.3 Uwasilishaji wa Muhtasari wa Ujumbe Kutokana na Methali

Mshairi amewasilisha mawazo kwa kina kupitia kwa ufafanuzi na maelezo aliyotolewa katika shairi hili. Kwa uelekezo wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mtunzi huteua kauli msingi kuwa dira ya kujengea kisa na pia katika ufaraguzi wa hoja (Barthes 1973). Kadhalika, hoja hizo huweza kufafanuliwa kwa kauli zilizotumiwa kwa makusudi (Mulokozi 1986). Aidha, mawazo yayo hayo huweza pia kufumbwa na kuwasilishwa kimuhtasari kwa kuzingatia methali iliyotumiwa katika utungo. Kwa mfano, kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa kumi na saba, yaani kabla ya matumizi ya methali, ameelezwa kwa kina umuhimu wa mnazi na pia amebainisha mahusiano baina ya Badi na Alii. Kutokana na usawiri wa matukio mbalimbali yaliyowasilishwa, msomaji huweza kubaini kuwa, Badi ni mwenye uchu mkubwa wa kuuhodhi mnazi na matunda yake. Aidha, kutokana na ubinafsi na tamaa, Badi ametajirika mno kwa ambavyo ameumiliki mnazi ilihali Alii ambaye ni mwenza katika ushirika huo ameathirika si haba katika mahusiano yao. Maelezo hayo yamedhihirisha kuwa, Alii ametendewa mengi maovu kwa kuhiniwa haki hiyo ingawa amekuwa akivumilia kwa uelekezi wa utu alionao. Aidha kilichobainishwa ni kwamba, mwenye mamlaka na uwezo wa kiuchumi ni Badi. Maelezo hayo yamewasilishwa katika beti za mwanzo kabla ya methali kutumiwa kama kauli ya mhusika Badi. Kwa hivyo, methali hiyo imetumiwa kwa makusudi katika uwasilishaji wa ujumbe katika shairi. Kuna uwezekano kwamba, mshairi amehisi kuwa, msomaji amepwelewa au hataweza kukumbuka mkururo wa maelezo yaliyowasilishwa. Katika mazingira hayo, mshairi ameamua kutumia methali hiyo ili msomaji aweze kuubaini ujumbe au mawazo kwa muhtasari. Kwa mfano, Badi amefananishwa na *ukuta* imara usioweza kuyumbishwa. Iwapo Alii ameamua kukabiliana na Badi, hana budi

kuathirika vibaya. Kadhalika, methali hiyo imetumiwa ili kuweza kuibua mkururo wa maswali ambayo kwa pamoja, husaidia katika kupanua mantiki iliyofumbwa katika methali. Baadhi ya maswali hayo ni kama:

- kwa nini Badi amejifananisha na ukuta?
- kwa nini Alii amechukuliwa kama mtu aliyetaka kukabiliana na ukuta ilihali hufahamu kuwa atauumiza mkono wake?

Hayo ni baadhi ya maswali ya kibalagha ambayo hayahitaji kutolewa majibu bali hubwagiwa msomaji ili kuweza kuyatafakari kwa kuyatolea majibu. Kulingana na nadharia ya Semiotiki, kauli ambazo hujengwa katika tamathali za usemi huhitaji kutolewa mifano na ufafanuzi zaidi kwa kuzingatia uhalisi wa maisha na utamaduni wa watu (Hawkes 1977 na Olsen 1973). Kwa njia hiyo, mshairi ametumia methali kwa makusudi kama nyenzo ya kuibulia ujumbe kwa muhtasari huku akimchochea msomaji kujaliza maelezo mengineyo ya msingi ambayo huhusiana moja kwa moja na ujumbe uliowasilishwa.

3.1.1.1.4 Methali kama Mbinu ya Kumtafakarisha Msomaji

Mshairi ametumia methali ya '*Mpiga ngumi, ukuta huumiza mkonowe*' kama mbinu mwafaka ya kumshirikisha na kumtafakarisha msomaji. Hapa ieleweke kuwa, mshairi hana muda mwingi wa kujieleza bali huusawiri na kuuwasilisha ujumbe kwa kuzingatia kichocheo cha lugha teule (Wood 1970). Katika muktadha huo, mshari ametumia methali kwa malengo ya kuibulia tafakuri ya msomaji ili kujenga usaili na ufasiri wa ujumbe uliofumbwa katika methali. Kadhalika, mtunzi hataki kubwaga au kuwasilisha

mawazo tu bali hujenga muktadha wa kumshirikisha kiufundi msomaji katika kufasiri na kupatanisha matumizi ya methali na ujumbe uliowasilishwa. Kwa hivyo, kazi za fasihi hujumuisha vipengele mbalimbali vya fani ambavyo yamesaidia kufafanulia mambo muhimu katika jamii (Chacha, 1992:1). Kwa mfano, msomaji anapokumbana na methali ya '*Mpiga ngumi ukuta, huumiza mkonowe*' husita na kujiuliza sababu ya kutumika kwa methali hiyo. Anapofika katika sehemu ambapo methali imetumiwa, kasi na mwendo wa usomi wa shairi hudhibitiwa au hupungua huku akitafakari kuhusu matumizi hayo katika muktadha wa shairi. Kwa mfano, matumizi hayo ya methali huweza kusaidia katika kumrejesha msomaji kusaili zaidi kuhusu mwelekeo wa Badi kama mhusika na pia sababu zilizofanya kutumiwa kwa methali hiyo. Kwa hivyo, methali imesaidia katika kujenga mazingira ya kuibulia athari ya msanii katika shairi.

Kadhalika, msomaji amejengewa sitiari ambayo huweza kufafanuliwa ndani na nje ya muktadha wa shairi. Kwa sababu hiyo, uwasilishaji huo umeoanisha matumizi ya methali iliyopo na uhalisi wa maisha na utamaduni wa jamii. Aidha, ni kutokana na kutafakari huo ndipo msomaji hubaini kuwa kinachomaanishwa ni mivutano ya kiuchumi ambayo imesakini katika jamii ya mshairi. Kwa mfano, uhuru wa Kenya ulipiganiwa na wanajamii wote kutokana na msukumo wa kizalendo. Nchi ilipopata uhuru, viongozi wawili wa Chama cha K.A.N.U, yaani Jomo Kenyatta na Jaramogi Oginga Odinga walikuwa na maafikiano ya kimkataba ya kushika hatamu za uongozi kwa kupokezana.

Makubaliano hayo hayakudumu kwa sababu viongozi hawa Badi (Kenyatta) na Alii (Jaramogi) walikuwa na itikadi zilizohitilafiana (Chacha 1987). Kadhalika, Kenyatta

alipata nafasi ya awali ya kuongoza nchi lakini kutokana na uelekezi wa itikadi hiyo hakutaka kubanduka uongozini licha ya nasaha alizopewa na Jaramogi. Jaramogi alijiondoa katika chama hicho kutokana na mwelekeo wa itikadi zilizohitilafiana. Kwa sababu hiyo, Jaramogi aliunda chama chake cha K.P.U. Mahusiano baina ya viongozi hawa hayakuwa murwa huku Jaramogi akikabiliwa vikali kwa vitisho (Odinga 1967:300). Ni kutokana na utafakari wa methali na mawazo yaliyoibuliwa, ndipo msomaji huweza kupatanisha yale yaliyowasilishwa na uhalisi wa kihistoria katika jamii. Hapa ieleweke kuwa shairi huwa gumu lakini ikiwa mtu hutaka kulifahamu, ni lazima kutambua muktadha na hali na wakati lilipotungwa. Hivyo ndivyo mashairi yoyote yalivyo (Chiraghdin 1977:2). Aidha, kwa kuizingatia hali hiyo, msomaji huweza kubaini undani wa ujumbe unaowasilishwa. Kwa hivyo, methali imetumika kama isitiari ambayo huhitaji kufasiriwa kwa jicho pekuzi ili ujumbe uliofumbwa huweza kufumbuliwa.

3.1.1.1.5 Ujenzi wa Taharuki Kutokana na Matumizi ya Methali

Maelezo ambayo hupatikana katika shairi, hasa kati ya ubeti wa kwanza hadi wa kumi na saba yaani, kabla ya methali hiyo kutumiwa, tayari msomaji hupata ufunuo kuhusu namna mambo yalivyokuwa hapo awali kabla na baada ya vifo vya wazazi wa Badi na Alii. Kadhalika, mahusiano ambayo si mwafaka baina ya Badi na Alii pia yamezingatiwa na yamebainishwa kupitia kwa maelezo yaliyotolewa. Kwa mfano, *mnazi* ulikuwa umerithishwa kwa Badi na Alii ili kuweza kutumiwa kwa manufaa yao na ya aila zao. Muda haukupita, Badi aliamua kutumia hila na udanganyifu ili kumtoa Alii katika ushirika huo.

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Maelezo ya kina yaliyotolewa, yaani kabla ya methali kutumika ni kana kwamba, yote yaliyopaswa kuwasilishwa yametimilika. Kwa ambavyo methali hujengwa katika tamathali za usemi imeweza kupanua, kupunguza au kubadilisha maana dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu ya kishairi iliyokusudiwa na mtunzi (Mulokozi na Kahigi 1979:32). Kwa hivyo, mizungu iliyoibuliwa kupitia kwa methali iliyotumika huweza kuwa kienzo cha kuimarisha na kuukuza ujumbe uliokwisha kuwasilishwa na yale yanayotarajiwa. Kwa mfano, Alii amejaribu kwa uwezo wake wote kumfahamisha mwenzake kuhusu umuhimu wa kuzingatia utu na kubadilisha nyendo zake. Badi kwa upande wake, amechachamaa kuwa katu hataweza kughairi imani hiyo kuhusu mnazi. Katika muktadha huo, hamu ya kuendelea kulidurusu shairi ingeweza kuishilia hapo, lakini kiufundi mshairi ameweza kumdhibiti msomaji ili kuendelea kulisoma shairi zima. Ni wakati huo ndipo mshairi ameamua kwa makusudi kutumia methali ya *'Mpiga ngumi ukuta, huumiza mkonowe'*. Kwa hivyo, msomaji ameweza kuundiwa muktadha wa kujiuliza swali lifuatalo:

- Ni kwa nini kuna mageuko ya mambo ilihali Alii amekwisha kumweleza Badi kuhusu umuhimu wa kubadili mwelekeo wake?

Katika hatua hiyo, msomaji wa shairi huwa amechochewa hamu ya kutaka kuelewa ni mambo yapiambayo huweza kujiri baadaye katika mahusiano baina ya Badi na Alii.

Kadhalika, mkururo wa maswali zaidi ambayo huweza kuzuka na kumjia msomaji baada ya kukumbana na matumizi ya methali hiyo ni kama:

- Ni hatua gani ambayo Badi au Alii huweza kuichukua?
- Matokeo au athari ya hatua hiyo huweza kuwa ipi?

Hapo awali, mshairi amemsawiri Alii kama mtulivu, mwenye utu na subira, lakini haijeleweka bayana iwapo atastahabu kuwa mwenye mwelekeo wa matao ya chini kutokana na kauli ya Badi. Hayo ni baadhi ya maswali ambayo huchochewa kwa makusudi ili kumpa msomaji msukumo na mchecheto wa kutaka kuendelea kulisoma shairi hili hadi mwisho. Hali hiyo huweza kufahamisha zaidi kuhusu mawazo yanayowasilishwa katika shairi.

3.1.1.1.6 Ubainishaji wa Mapisi Kupitia kwa Matumizi ya Methali

Kwa kuzingatia methali iliyotumiwa, mshairi ameweza kudokezea na kufahamisha kuhusu uhalisi wa maisha na athari ya mkondo wa kadhia zilizopitiwa na wahusika Badi na Alii. Kimsingi, baadhi ya kauli za kimapokeo kama vile vitendawili vya Kiswahili huweza kuwa ni hifadhi ya matukio yaliyopitika katika jamii (Momanyi 2006). Katika muktadha wa ushairi, hali hiyo pia imebainishwa kwa kuzingatia methali ambazo zimetumiwa. Kwa mfano, mshairi alipotumia methali ya '*Mpiga ngumi ukuta, huumiza mkonowe*', imesaidia siyo tu kuzingatia kadhia zilizosambaratisha mahusiano ya sasa ya akina Badi na Alii bali pia, kuwa kujenga ufahamu wa kadhia au hali hiyo. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, Badi ni mwenye mamlaka na uwezo mkubwa wa kiuchumi ilihali Alii ameathirika mno kutokana na mfumo dhalimu wa uhodhi wa kimabavu wa rasilimali iliyopo katika jamii.

Kwa ambavyo, methali iliyotumika imejitokeza kabla ya ile nyingine ya: *Heri nusu ya shari, kuliko shari kamili*, huashiria kuwa mtunzi angependa msomaji azingatie zaidi kuhusu maisha ya awali baina ya Badi na Alii. Hata hivyo, Badi alizua hila na kutumia

ujanja wa kumbandua mwenzake katika umiliki huo. Kwa kuzingatia maelezo hayo, mshairi humtaka msomaji kuweza kuangazia zaidi mahusiano hayo ya awali baina ya Badi na Alii na hasa kabla ya methali inayotumiwa kujitokeza. Ni kutokana na msingi huo, hadhira huweza kuelewa au kumaizi mahusiano hayo yenye mikinzano baina ya Badi na Alii. Isitoshe, kupitia kwayo, mshairi humtarajia msomaji kusaili na kutafakari zaidi vipengele vya kihistoria vilivyoathiri mahusiano murwa yaliyopitika baina ya Badi na Alii. Kwa mfano, wavyele wao waliishi kwa amani, upendo na umoja hadi kuwa washirika katika mnazi. Kadhalika, wazazi hao walitaka wana wao kuweza kufuata nyayo zao za utu na ushirika lakini mwafaka huo haukutimilika kutokana na mwelekeo hasi na ubinafsi wa Badi. Kwa sababu ya ubinafsi, Badi aliamua kujilimbikizia mali bila ya kujali hali ya ukata ambao umemkuta Alii. Kwa hivyo matumizi ya methali, ymesaidia katika kujenga muktadha wa kuelewa kwa undani sababu za kihistoria, kijamii na kitamaduni zilizoathiri mahusiano hayo baina ya Badi na Alii.

3.1.1.1.7 Ubainishaji wa Mikinzano ya Kitabaka Kutokana na Methali

Zaidi ya maelezo yaliyotolewa, matumizi ya methali yamesaidia kusawiri na kuwasilisha mikinzano ya kitabaka iliyoota mizizi na kushamiri katika jamii. Tabaka lenye uwezo wa kiuchumi limewasilishwa kupitia kwa mhusika Badi ilihali tabaka la ukata limewasilishwa kupitia kwa Alii. Katika muktadha wa matumizi ya methali ya '*Mpiga ngumi ukuta, huumiza mkonowe*', mazingira ya kitabaka katika jamii hajawezi kutokea kwa kisadfa bali huibuka kutokana na mielekeo hasi na itikadi zilizoundwa katika jamii (Fenon 1967 na Odinga 1967). Mamlaka na uwezo alionao Badi ilitokana kwa hila zilizotumiwa katika kumdhulumu na kumfilisi Alii. Kadhalika, Badi hapigwi mshipa

wala hajali dhiki zilizomsibu na zilizomwandama mwenziwe. Hali hiyo pia imebainishwa katika shairi 'upepo wa wakati' (Kezilahabi 1974:4) ambapo imetongowa:

Tazama walivyojinyakulia madaraka
Wanavyoshika pesa kama watoto
Ni picha ya bandia
Askari mwehu na bunduki yake
Na kutunyamazisha!

Dondoo hilo limedhihirisha namna utawala wa nyonyaji unavyoshamiri kwa mtutu wa bunduki. Hali hiyo ndiyo huzua utabaka na uhasama katika jamii. Katika muktadha huo, masilahi ya Badi ndiyo yaliyopewa kipaumbele na kustawishwa kutokana na mfumo dhalimu wa uhodhi wa nguzo za rasilimali katika jamii.

Aidha katika shairi la 'Mnazi: Vuta N'kuvute', imebainishwa kwamba, mwanajamii aliyedhulumiwa anapozinduka hukaza kani ya kuidai haki hiyo; kwanza kwa kutumia nasaha kama alivyofanya Alii. Kwa ambavyo Badi aliona kuwa kauli na madai ya Alii huenda yakahatarisha maslahi yake. Kwa hivyo, alikataa katakata kusikiliza wito au busara ya Alii. Hali ya kitabaka iliyosawiriwa na kuwasilishwa ndiyo kiini cha mvutano na migaragazo katika jamii. Kwa upande wa Badi, alikuwa mwenye mawazo kuwa mali aliyonayo ni 'halali' yake ilihali Alii haawamini kutokana na ulaghai uliotumika. Kwa hivyo, ushairi na fasihi kwa ujumla huweza kutumia kauli hai zilizohusu maisha na mapambano ya kujihami dhidi ya unyanyaswaji ambao hupatikana katika jamii (Coser 1963:2). Uhalisi huo ndiyo umebainishwa kupitia kwa methali iliyotumika katika utungo. Kadhalika, Badi hujiona mwerevu na wala haoni soni ya kutumia vitisho ili kuweza daima kuwa katika hatamu za utawala. Swali ambalo mshairi angependa msomaji kuzingatia kutokana na methali iliyotumika ni:

- Je, Alii ataridhi kuwa katika tabaka la chini ilihali ametambua kilichmsababishia hali hiyo ni Badi?

Pindi msomaji anapokumbana na methali hiyo, huchochewa hamu ya kutaka kuendelea kulisoma shairi kwa tuo ili kuweza kutambua jawabu la fumbo hilo. Aidha, msingi wa mikinzano ya kitabaka katika jamii hutokana na ubinafsi miongoni mwa wanajamii wachache. Kwa hivyo, hali kama hiyo haipaswi kuwepo endapo utangamano katika jamii umejengwa na umejikita katika misingi ya utu na upendo.

3.1.1.2 Heri Nusu ya Shari, Kuliko Shari Kamili

Methali hiyo imetumika baada ya ile ya kwanza ya '*Mpiga ngumi ukuta, huumiza mkonowe*'. Aidha, methali hiyo imejitokeza katika ubeti wa ishirini na sita hususa, mshororo wa tatu. Kwa hivyo, mshairi ameitumia methali kwa makusudi ili kuendeleza mawazo yaliwasilishwa hapo awali. Katika muktadha huo, methali pamoja na ile ya mwanzo huchangiana na hukamilishana katika uwasilishaji wa mawazo au ujumbe. Katika ubeti huo mahususi, methali hiyo imetumika katika kuundia na kukamilishia mshororo wa tatu. Kadhalika, ikumbukwe kuwa mhusika yuyo huyo ndiye aliyetumia methali ya mwanzo pia kuitumia methali ya *Heri nusu ya shari, kuliko shari kamili.* Isitoshe, mshairi ameitumia methali hiyo kama mbinu ya usawiri na uwasilishaji kama ilivyobainishwa.

3.1.1.2.1 Matumizi ya Methali kama Dhihirisho la Ubinafsi na Dhuluma

Katika shairi hili, mshairi ametumia methali kuibulia mawazo mazito yaliyobainisha ubinafsi na dhuluma ambao umesakini katika jamii. Kupitia kwa methali, mshairi humtaka msomaji abaini ubinafsi na dhuluma alizonazo Badi dhidi ya Alii. Hapo awali kabla ya kutumiwa kwa methali hiyo, mshairi alikuwa tayari ametoa maelezo ambayo yamemsawiri Alii kama mhusika mwenye utuvu na busara. Hata hivyo, nasaha alizotoa Alii kwa Badi hazikutiliwa maanani.

Kadhalika, kiburi alichonacho Badi kimesawiriwa kuwasilishwa vyema kupitia kwa methali hiyo kwamba, hakutaki wala hakuwa mwenye nia ya kumshirikisha Alii katika kuumiliki *mnazi* na mazao yake. Kwa mfano, mhusika Badi amekuwa akimrairai Alii ili kaweza kuridhi fungu dogo la nazi alilopewa. Alii kwa upande wake aliuona huo kama ujanja uliotumika na mwanzake ili kumpoka haki yake. Kwa hivyo, Alii alikataa kata kata kutwaa alichopewa huku akimtaka Badi ampe haki ya iliyo kamili. Mali haramu aliyonayo Badi ilimvimbisha kichwa na kuwa mwenye kiburi sugu. Katika maongezi na malumbano yao, Alii alimwona Badi kama katili na aliyeuzika utu. Kilichobainishwa katika shairi, na hasa kupitia kwa methali iliyotumika ni kwamba, wahusika hawa wawili wana itikadi na mielekeo ambayo imehitilafiana. Kutokana na ukosefu wa nazi, Alii na aila hiyo imedhikishwa na imefukarishwa. Alii ana mawazo kuwa endapo atakapokubali fungu dogo alilopewa litamshushia hadhi na uaminifu wake, siyo tu kwa aila yake bali pia machoni mwa jamii pana. Vile vile, ubinafsi wa Badi umempofusha kiasi cha kumfanya kutozingatia utu na haki. Kutokana na mikinzano hiyo, Alii ameweza kuteseka na kuathirika mno kimaisha lakini alistahabu kuwa katika hali hiyo hadi atakapoizumbua

halali hiyo iliyo kamili. Kadhalika, mshairi humtaka msomaji abaini kuwa: *nusu shari* ni kifumba macho au dawa ambayo itamfanya Alii na aila yake iendelee kuwa hai bila matamanio yoyote maishani. Kwa sababu, kuna tuhuma na mvutano katika pande hizo mbili. Zaidi ya hayo, methali imetumiwa kuibulia utu na busara ya Alii na kubainisha uzandiki uliofichika ndani ya Badi. Kwa hivyo, hao ni wahusika ambao wametengana kimwelekeo kama mbingu na ardhi. Katika muktadha huo, methali iliyotumiwa humfanya msomaji kuelewa vizuri wasifu na hulka ya Badi, kwamba ni mja asiyejali dhiki ambazo zimemsibu mwanajamii mwenzake. Jambo ambalo Badi amelipa kipaumbele na lililotawala, ni namna anavyoweza kulijaza tumbo lake. Kwa upande wa Alii ametumia muda mwingi kumtahadharisha mwenziwe kuhusu ubaya wa mkondo aliouchukuwa.

3.1.1.2.2 Methali kama Msingi wa Kuendeleza Zaidi Ujumbe Unaowasilishwa

Mifumo dhalimu na mivutano ya kiuchumi, ni baadhi ya maswala ya msingi yaliyoishughulisha kalamu ya mshairi. Kwa kutumia methali ya *Heri nusu ya shari, kuliko shari kamili,* mtunzi ameweza kufafanua na kubainisha zaidi chanzo cha mivutano dhalimu ya kiuchumi ambayo imesakini katika jamii. Kwa mfano, Badi amewasilishwa kama mtu ambaye ametumia ujanja au 'uwerevu' katika kuubinafsisha mnazi. Ukosefu wa utu, uchoyo na ubinafsi alionao ndio uliomkweza kiuchumi ilihali Alii ametokomezwa katika lindi la uhitaji na ulitima. Hata hivyo, itikadi na mwelekeo uliowasilishwa ni kwamba, hali ya kitabaka katika jamii hujengeka katika misingi potoshi ya kidhahania. Kwa sababu ya kutotaka usawa katika jamii, Badi ameuvunja mwafaka wa mkataba wa ushirika uliokuwepo awali kabla ya mauko ya wazazi wao. Kwa

ambavyo Badi ndiye anayemrai na kumtaka Alii kuweza kuridhika kwa *nusu shari*. Hali hiyo imebainisha kuwa, aliyerejelewa hana hisi za huruma wala utu kwa mwenzake.

Kadhalika katika uwasilishaji wa shairi, methali imetumiwa ili kuifumba itikadi na mwelekeo wa mshairi. Isitoshe imebainshwa kuwa, hali ya mvutano ya kiuchumi katika jamii imejengwa katika misingi ya ubinafsi na uzandiki. Kwa kuzingatia nadharia ya Semiotiki, hoja moja huweza kuibuliwa na kuendelezwa kupitia kwa kauli mbalimbali zilizotumika na zilizoshirikishwa katika uwasilishaji wa ujumbe (Steen 1974). Isitoshe shairi hilo limetumia methali mbili ambazo zimechangiana katika uwasilishaji na uendelezaji wa ujumbe. Kwa hivyo, shairi limeshirikisha na limewasilisha hoja zaidi ya moja. Kwa hivyo, limejenga mazingira ya uhitaji methali zaidi ya moja. Kadhalika, matumizi hayo hupunguza machofu katika usomaji wa shairi. Katika muktadha huo, methali moja haitoshi. Kwa sababu, shairi limesawiri maudhui pana yaliyohitaji ufafanuzi wa kina. Mwelekeo ambao umewasilishwa ni kwamba, mtu ambaye hutumia hila katika kujikweza kiuchumi katu hawezi kuuthamini utu wala kumthamini yule aliye chini. Kutokana na maelezo hayo na hasa kupitia kwa methali ni kwamba, mtu aliye chini kiuchumi hustahili kuzua mbinu za kujikomboa yeye mwenyewe au kuungana na wenzake walionyanyaswa ili kuweza kujinasua na kuboresha hali zao za kimaisha katika jamii. Naye Alii amesawiriwa kama mtu ambaye tayari amezinduka na amemaizi hila zilizotumiwa na Badi kumdhulumu. Katika muktadha huo, mshairi humwona Badi kama mwewe ambaye huotea kifaranga. Kwa hivyo, tahadhari imetolewa kuwa mapambano dhidi ya tabaka dhalimu katika jamii huhitaji mbinu mwafaka yenyeambazo huzingatia hadhari ili kujihami na mipwaruzo ya 'mwewe'.

3.1.1.2.3 Ujenzi wa Taharuki Kutokana na Methali

Methali hiyo ya, *Heri nusu ya shari, kuliko shari kamili*, imetumika kama msingi wa kuibulia zaidi matukio na kujengea taharuki katika uwasilishaji wa shairi. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, kauli msingi za kimapokeo kama vile methali hujibainisha zaidi kiisitiari na huendeleza usaili. Kijuujuu, dhana hizo huwa na maana dhahiri ambayo humwelekeza msomaji kupata ujumbe batini (Jacobson 1960). Aidha, matumizi hayo husaidia katika kuibulia na kujenga mazingira ambayo huchochea zaidi ilihamu na humdhibiti msomaji wa shairi. Kwa mfano, msomaji anapokumbana na methali iliyotumika, hutarajiwa kujenga na kujiuliza mkururo wa maswali ambayo hayawezi kukidhiwa ila kwa kuendelea kulidurusu kwa makini shairi ambalo limezingatiwa kuanzia mwanzo hadi tamati. Kadhalika kwa kutumia methali, mshairi amepunguza kwa ustadi mwendo wa usomaji wa shairi na kumtaka anayelisoma azidi kutafakari kwa udadisi matumizi hayo ya methali huku akizingatia mawazo au ujumbe uliowasilishwa. Mathalani, msomaji huweza kijiuliza:

- Kwa nini, Badi amepewa au ametumia kauli hiyo ya methali?
- Mshairi ametarajia nini kwa kutumia metahli hiyo?

Kadhalika, mshairi humtarajia msomaji kuzingatia mazingira alimojikuta Badi na jinsi alivyoitumia kauli hiyo. Maswali hayo, hujenga mazingira ya kumfanya msomaji kutaka kufumbua fumbo hilo lililofumbwa kwenye methali. Naye, mshairi hujipa nafasi ya kupiga kasi katika kuufafanua zaidi ujumbe ambao huwasilishwa. Kutokana na uchochezi wa methali, msanii hatarajii msomaji kusitisha usomaji wake bali kuwa na ari ya kutaka kuendelea hadi mwisho wa shairi. Kwa hivyo, matumizi ya methali hiyo si

kwa manufaa ya msomaji tu bali pia huwa ni nyenzo muhimu ya kujenga ufaraguzi na uwasilishaji wa mawazo katika shairi. Isitoshe, mshairi ameweza kufaragua vitushi ambavyo vimechangia uwasilishaji wa ujumbe hadi kufikia upeo wa juu katika utungo. Kwa mfano, kwa kutumia methali, mshairi ameweza kupanua na kufafanua zaidi mahusiano na mikinzano fiche baina ya Badi na Alii. Katika muktadha huo, mshairi pia hupata nafasi ya kuelezea zaidi mikakati ya mapambano aliyonayo Alii dhidi ya mtesi wake. Kutokana na maelezo yaliyotolewa, Alii ni mvumilivu na mwenye subira lakini hali hiyo pia hutarajiwa iwe na kikomo. Kwa hivyo, alivyoitumia methali kwa makusudi ni kama ambaye humshawishi msomaji ili kuweza kuendelea kupiga mbizi katika usomaji wa shairi ili aupate ufunuo wa ujumbe. Msomaji anapoamua kukomea hapo penye methali hataweza kuuupata kwa ukamilifu uhondo au ujumbe uliowasilishwa.

3.1.1.2.4 Methali kama Mbinu ya Kuwasilishia Isitiari

Lengo la mshairi katika usawiri wa utungo si kumfanya msomaji kuzingatia tu ujumbe ambao umewasilishwa kupitia kwa methali yenyewe, bali pia kuhusisha kikamilifu matumizi hayo kwa kuumua tajiriba yake kuhusu utamaduni na uhalisi wa jamii. Kwa hivyo, ujumbe uliowasilishwa kupitia kwa methali huhitaji kufasiriwa na kufafanuliwa zaidi si kwa kuzingatia tu maelezo yaliyotolewa, bali pia kupanua ufasiri wake katika muktadha wa mazingira na uhalisi wa jamii husika ya mshairi.

Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, kauli msingi zilitumiwa katika uwasilishaji wa utungo, hutekeleza mambo mawili ya muhimu: kuibulia ujumbe bayana na ujumbe ambao huhitaji utafakari na usaili wa kauli zilizotumiwa (Mosha 2002). Kwa mfano,

ingawa Badi na Alii ni wahusika waliobuniwa; vitendo na mahusiano yao huweza kumithilishwa kwa vitendo na mahusiano sawia ya jamii katika uhalisi wake. Kwa kufanya hivyo, ujumbe husaki zaidi katika akili na tafakuri ya msomaji.

Kadhalika, adili linalowasilishwa na linalopatikana katika methali hiyo huweza kumfanya msomaji kujinasibisha au kujitenga na nyendo ambazo zimewasilishwa kupitia kwa usawiri wa wahusika hao. Hiyo ni dhima mojawapo ambayo hutekelezwa kupitia kwa methali, kwa kuwa hizo ni semi ambazo hufundika hekima na busara ya jamii (Parker 1994). Kwa mfano, Badi ni maskini wa utu kinyume na Alii. Katika muktadha huo, matarajio ya mshairi ni kwamba, msomaji ataushikilia utu wa mhusika Alii na kuutokomeza ubinafsi wa Badi. Kwa hivyo, methali imetumika kitaashira ili ujumbe uliowasilishwa kuweza kutafakarisha zaidi kwa kuzingatia uhalisi na utamaduni wa watu.

Kadhalika, msomaji hutarajiwa kujenga usaili wa matumizi ya methali iliyotumika katika muktadha wa mahusiano baina ya Badi na Alii ambayo huweza kubainishwa na kufasirika ndani na nje ya shairi. Kwa mfano, mahusiano baina ya Badi na Alii si murwa kutokana na itikadi potoshi iliyozuliwa na Badi kuhusu uhodhi na mbinu batili za uzalishaji mali katika jamii. Katika uwasilishaji, mshairi ametumia *mnazi* na *nazi* kama ishara ambayo huweza kutambulika na kufasirika katika akili ya msomaji. Kwa kuzingatia vidokezi vya taashira hizo ndipo msomaji huweza kubaini na kufahamu mvutano wa kimahusiano baina ya Badi na Alii. Kwa hivyo, mshairi ameitumia kwa makusudi methali hiyo ili kujenga mazingira ya kufumba maelezo pana ambayo huhitaji

kutolewa ufasiri na ufafanuzi wa kina. Isitoshe kauli zingine ambazo zimeibuliwa kwa makusudi, zimechangia ujumbe uliowasilishwa kupitia kwa methali.

3.1.2 Shairi: Muwerevu Hajinyowi

Shairi hili limewasilishwa kwa kuzingatia muundo wa tarbia na lina beti tano. Katika uwasilishaji, methali moja ya *Muwerevu Hajinyoi* ndiyo iliyotumiwa. Aidha, shairi hilo limewasilisha mivutano ya kitabaka kama vile ilivyobainishwa katika shairi la 'Mnazi: Vuta N'kuvute' (Uk. 17-22) ambapo kumesawiriwa mazingira ya watawala (Badi) na watawaliwa (Alii).

3.1.2.1 Methali kama Kichocheo cha Kujengea Kisa

Mshairi ametumia methali hiyo kuwa mbinu ambayo imesaidia katika kujengea kisa au kuwasilishia mawazo katika shairi. Kimsingi, mshairi huwa na ujumbe, mawazo au jambo ambalo angependa kuliwasilisha kwa msomaji (Kezilahabi 1976 na Mulokozi 1975). Kwa hivyo, hisi au mchomo alionao huweza kufafanuliwa kwa mwelekeo tarajiwa kwa kuzingatia methali iliyotumiwa. Kwa mfano, katika utungo huu msanii amekirihishwa na mwelekeo wa baadhi ya viongozi wa Afrika ambao walibahatika kupata nyadhifa hizo muhimu katika jamii. Viongozi hao huchaguliwa ili kushika hatamu hizo muhimu lakini badala ya kujenga mahusiano na maelewano mema, huwa wenye ubinafsi, kiburi na kuwapuuza wale waliowakweza. Kwa ambavyo wamenafasika, hujifananisha na miungu iliyopaswa kuabudiwa katika jamii. Hali hiyo pia imebainishwa katika shairi la 'Jinamizi' (Kezilahabi 1974:1). Katika kusawiri maguvu hayo ya viongozi, imetongolewa kuwa mtawaliwa:

Aliinua kichwa chake juu ya maji
Utawala wa chuma ulimtoboa fuvu
La kichwa na kutupwa mtumbwini
Halafu alifikiria Afrika
Na siasa kwa ujumla
Mafuvu

Dondoo hilo limewasilisha taswira ya vipigo ambavyo watawaliwa huvipata pindi wanapojiingiza katika harakati za kuidai haki au wanaposaili uongozi uliopo.

Kutokana na matumizi ya methali katika shairi la 'Muwerevu Hajinyowi' mshairi amewasawiri viongozi hao kama vikwazo au visiki katika harakati za maendeleo katika jamii. Kulingana na maelezo yaliyotolewa ni kwamba, ingawa watawaliwa hawana nyadhifa za hadhi katika jamiii, hupaswa kuheshimiwa na kutoa mchango wao kuhusu namna uongozi ulivyotekelezwa kwa manufaa ya umma kwa ujumla (Maitaria na Maina 2011). Viongozi ambao hawashirikishi mawazo ya jamii, huenda watu wakahisi kudharauliwa. Hali kama hiyo inapodhihirika, huathiri mno misingi ya ushikamano na utangamano katika jamii. Kwa hivyo, mshairi ametumia methali ili kuweza kupanga mawazo kimantiki.

Zaidi ya hayo, matumizi ya methali yameweza kusaidia katika kuibulia baadhi ya mifano ambayo hushadidia mawazo yanayowasilishwa. Katika muktadha huo ieleweke kwamba, busara ya methali iliyotumika hujikita katika utamaduni na uhalisi wa jamii. Vile vile, ameitumia methali kauli ya kukemea na kukashifu baadhi ya vitendo hasi katika jamii. Kwa hivyo, mtunzi amejijengea mazingira ya kutokuwa na wasiwasi wowote; kwa ambavyo ni hekima au ujumbe ambao tayari hukukubalika katika utamaduni wa jamii.

Kwa sababu hiyo, mshairi hasiti kuwasuta viongozi ambao huenda wakaangamia. Aidha, mshairi ameweza kutambua na kubainisha kuwa kiburi walichonacho viongozi ni kujitakia nakama ambayo hayapasi kuwepo endapo mja hujiepusha nayo. Iwapo viongozi hao hujichukulia kuwa mababe au miungu katika jamii huenda siku za usoni wakajutia mielekeo na matendo yao.

Matumizi ya methali hiyo yamefaidi katika kufaragua mchomo na mwelekeo wa mawazo na pia kuufanya ujumbe ambao umewasilishwa, kufasiriwa katika muktadha wa utamaduni na uhalisi wa maisha katika jamii. Kwa namna hiyo, mshairi humfanya msomaji kufahamu na kutafakari mwelekeo wa itikadi iliyowasilishwa kuhusu viongozi bandia katika jamii. Kwa ambavyo mshairi ameitumia methali hiyo kama anwani, tayari msomaji huwa amedokezewa kimbele kuhusu matarajio ya ujumbe unaowasilishwa. Kutokana na mawazo yaliyoibuliwa, mshairi ameiteua na kuifanya methali kuwa anwani na kauli msingi katika kuibulia kisa katika uwasilishaji wa utungo.

3.1.2.3 Methali kama Chombo cha Kuundia Isitiari

Kutokana na mazingira mabaya ya kisiasa na kiuchumi, mshairi haridhishwi na jinsi viongozi katika jamii hutekeleza wajibu wao. Ingawa methali iliyotumiwa katika utungo huibua taswira, imeweza pia kuwasilisha ujumbe kiisitiari. Kipengele cha isitiari kama mbinu ya uwasilishaji imeirutubisha ile ya taswira. Kwa mfano, mshairi ameijengea hadhira mazingira ya kuibulia usaili. Kwa hivyo, hadhira huweza kujengewa mazingira ya kujiuliza kuwa:

- *Muwerevu Hajinyoi* na endapo ameamua kujinyoa matokeo yatakuwa nini?

Katika muktadha huo, ujumbe umewasilishwa kwa usaili kwa kuzingatia taswira inayoibushwa. Ni katika kupiga bongo, ndipo msomaji humaizi kuwa kilichorejewa kupitia kwa maneno yaliyotumika si kinyozi bali ni maswala ya kisiasa katika jamii. Kimsingi, kiongozi huteuliwa na jamii kushikilia nyadhifa hizo muhimu, yaani kuwaongoza watu katika harakati za maendeleo katika jamii. Baadhi ya viongozi, kama vile kinyozi, huchukulia nyadhifa hizo kama upenu wa kujichumia na kuwasahau wale waliomkweza. Aidha, mali waliyojilimbikizia kwa ulaghai huwafanya kuwa na kiburi kiasi cha kutotaka kutilia maanani mawazo ambayo hutolewa katika jamii.

Isitoshe, viongozi ambao hujichukulia kuwa miungu wadogo miongoni mwa wanajamii; hujutia matendo yao hapo baadaye. Kwa hivyo, viongozi hao huwa wenye mikiki ya kiburi na majitwazo huku wakisahau kule walikotoka. Kutokana na vitimbi hivyo, hujifanya kuwa miungu iliyopaswa kuabudiwa na kusujudiwa. Mwanajamii yeyote ambaye huukashifu au huukosoa utawala huo, hukabiliwa kwa vitisho na adhabu kali. Kadhalika, viongozi hao hujifanya kama wakamilifu na wasiokuwa na dosari yoyote katika yale wanayoyatenda na kuyasema. Kupitia kwa methali, mshairi ameweza kubainisha utovu kiburi miongoni mwa viongozi katika jamii.

Kulingana na maelezo yaliyotolewa na kupitia kwa methali iliyotumika ni kwamba, viongozi hustahili kuwa wenye hekima na wenye kuwastahi wanajamii wenzao. Vile vile, mawazo yaliyowasilishwa ni kwamba, kiongozi kama binadamu yeyote huweza kuwa mwenye udhaifu au dosari fulani. Kwamba, baadhi ya vitendo vyao si mwafaka wala kamilifu kwa sababu, baadhi ya yale wanayoyatenda huenda si murwa. Kwa jicho

la upekuzi, baadhi ya wanajamii huona ya kwamba, kiongozi wao amepotoka kwa kiasi fulani na hustahili kutanabahishwa. Kwa hivyo, kiongozi asiye na busara humtuhumu aliyemkosoa kuwa adui ambaye hunyemelea kuuporomosha utawala uliopo. Mtazamo uliojitokeza ni kwamba, mawaidha yanayotolewa hustahili kuchukuliwa kwa nia njema kwa manufaa ya jamii. Iwapo kiongozi hatatilia maanani malalamishi ambayo hutolewa, huenda jamii ikawa haina imani na uongozi huo.

Kadhalika, kupitia kwa methali na maelezo yaliyotolewa, humbainika kuwa ingawa dhana ya 'kinyozi' imetumika, ichukuliwe kama ishara ya kuwezesha kutambua na kufumbua ujumbe fiche unaowasilishwa. Kwa kuzingatia uelekezo wa nadharia ya Semiotiki, dhana za kiisitiari huweza kupata uelekezi kwa maneno au kauli za kawaida ambazo huweza kufasirika kupitia kwa utamaduni wa watu (Scholes 1974). Kwa mfano maneno yaliyotumika katika methali ni *Muwerevu* na *Hajinyowi*. Maneno hayo yaliyotumika ni ya kawaida, lakini maana ambayo hukusudiwa huweza kufasirika kwa kuzingatia uhalisi wa maisha ya watu. Katika mazingira hayo, mtunzi ameweza kuuwasilisha ujumbe wake kimafumbo. Kwa hivyo, kinyozi si kinyozi wa kawaida katika uhalisi wake, bali huashiria mtu mwingine ambaye hutenda kama yeye. Hiyo ndiyo sababu ya kumnasibisha 'kinyozi' na yeyote aliye mamlakani katika jamii. Katika muktadha huu, mshairi humtaka msomaji kuizingatia na kuifasiri dhana ya 'kinyozi' kuwa ni kiongozi au mtu ambaye hutegemewa katika jamii.

Viongozi wenye kiburi katika jamii huchukuliwa kuwa hawana mwelekeo katika kuelekeza harakati za kimaendeleo katika jamii. Kupitia kwa matumizi ya methali,

mshairi ameweza kutoa ithibati ya viongozi walijifanya 'werevu' ambao waliweza kuangamia na kusahauliwa katika jamii (Karama 1996). Kwa hivyo, kiongozi mwenye busara huwa kipenzi, mashuhuri na hudumu katika kumbukumbu ya jamii. Aidha katika uwasilishaji wa mawazo, mshairi humtaka msomaji awabaini viongozi wasio na busara ili kuweza kutimuliwa au kufurushwa; iwapo jamii huhitaji kupiga makasia ya maendeleo. Kadhalika, msanii ameendeleza hoja kwamba, kiongozi hawezi kuwepo pasipo jamii. Vile vile, pande hizo mbili za watawala na watawaliwa hupaswa kushirikiana na kutegemeana kwa manufaa yao wenyewe. Katika muktadha huo, methali imesaidia kujenga isitiari ambapo kupitia kwazo jamii huweza kuelimishwa na kuzinduliwa.

3.1.2.3 Methali kama Mbinu ya Kusaili na Kutafakarisha

Mshairi ameitumia methali kama mbinu ya kumshirikisha kikamilifu msomaji katika utanuzi wa mawazo ya msingi yaliyowasilishwa. Kwa ambavyo mshairi hana muda mwingi wa kujieleza na kufafanua kwa undani mawazo hayo. Kwa hivyo, humshirikisha kwa ubunifu msomaji katika usaili na utafakari wa matumizi ya methali au kauli msingi zilizotumika katika uwasilishaji wa shairi.

Kadhalika, mshairi ametumia methali kama mfano sahili ambao umezowewa katika tajiriba ya jamii ili kuwa chemichemi ya kuupata ujumbe fiche uliowasilishwa. Ni kutokana na kujikuna kichwa au kupiga bongo ndipo msomaji huweza kuung'amua na kuubainisha ujumbe unaowasilishwa (Steen 1974). Mathalani, *mwerevu* ni mtu hujiona kuwa mjuaji na kufanya mambo kichinichini ambapo kijuujuu huonekana kama mwenye utu kumbe sivyo. Ni baada ya kufahamu vitimbi na ujanja uliotumika, ndipo msomaji

huweza kuupatanisha ukweli huo na uhalisi uliowasilishwa katika shairi. Kutokana na matumizi ya methali, mshairi ameweza kumdhibiti na kumshirikisha kikamilifu msomaji kuwa mhusika kamili na tendaji baadala ya kuwa tuli. Ingawa mshairi ndiye mchimuzi wa mawazo yaliyowasilishwa, huelewa kuwa msomaji wake si wa kubwagiwa tu mawazo bali pia huhitaji kupanua mawazo yayo hayo ili kuweza kumfaidi. Hiyo ndiyo sababu ambayo imemfanya mshairi kutumia kibwagizo kilichosheheni maelezo ya msingi yaliyochukuana na matumizi hayo ya methali.

Aidha, mshairi ametumia methali hiyo kama anwani katika shairi ili msomaji awe tayari kuianza safari ya kuduru na kusaili mawazo hutarajiwa kuwasilishwa kiisitiari na kimafumbo. Kwa mfano, msomaji huweza kujiuliza maswali yafuatayo:

- 'kinyozi' ambaye amezungumziwa huweza kupatanishwa na mtu au mwanajamii yeyote katika uhalisi wa maisha?
- Mshairi ametarajia kuwasilisha ujumbe wa aina gani?
- Methali ambayo imetumika huweza kufasiriwa vipi katika uhalisi wa maisha na utamaduni wa jamii?

Hayo ni baadhi ya mkururo wa maswali ambayo msomaji huweza kukumbana nayo wakati wa kupiga mbizi katika usomaji wa shairi. Hali hiyo imedhihirishwa kupitia kwa kibwagizo: *Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?* Swali hilo ni la kibalagha na limetumiwa kwa makusudi ili kujenga mazingira ya usaili na uhitaji wa jibu hata ingawa mtunzi au fanani haonekani.

3.1.2.4 Ujenzi wa Taharuki Kutokana na Matumizi ya Methali

Kwa ambavyo methali kusudiwa imetumiwa kama anwani katika shairi, imesaidia katika kujenga mandhari ya taharuki ya awali katika duru na utafakari wa msomaji. Punde tu msomaji anapokumbana na methali hiyo, humfanya kujiuliza kwa udadisi zaidi maswali mbalimbali ambayo husaidia katika ubainishaji wa ujumbe kitaharuki. Baadhi ya maswali ambayo huchochewa ni:

- Ni kwa nini 'kinyozi' *mwerevu* hawezi kujinyoa?
- Ni nini matokeo ya 'kinyozi' kujinyoa *mwenyewe*?
- Mshairi ana mawazo au mwelekeo gani kupitia kwa matumizi ya methali hyo?

Hayo ni baadhi ya maswali ambayo huweza kutunga katika akili ya msomaji anapokumbana na methali iliyotumika wakati wa kulidurusu shairi. Vile vile, mshairi hubaini kwamba, huenda msomaji asimaizi ufafanuzi wa mawazo yaliyowasilishwa ila pale anapokuwa mwenye subira ya kutaka kulisoma shairi zima. Aidha, mshairi ametumia kwa makusudi methali kuwa anwani katika shairi. Kwa hivyo, hata kabla ya msomaji kuanza safari ya kulidurusu, huwa amejengewa mazingira ya kudokezewa kwa uchochezi kuhusu ujumbe ambao hutarajiwa kuwasilishwa katika shairi.

Kadhalika, kupitia kwa methali, mshairi ameanza uwasilishaji wa mawazo kwa mshindo unaostahili na unaotafakarisha. Kwa mfano, mshairi ameanza ufaraguzi wa hisi na mawazo kwa kubainisha kuwa: *mwenye nacho wajishawasha, wajiona kama ndovu.* Huo ni mshororo wa awali ambao unapatikana katika ubeti wa mwanzo. Aidha, anapoendelea katika ufaraguzi wa mawazo hayo, ameukariri zaidi ujumbe wake kwamba, alichonacho

mtu kisimfanye kujawa kiburi. Katika muktadha huo, imefananishwa alichonacho mtu na *nguvu za povu*. Kwa hivyo, msomaji anapozingatia maelezo yaliyotolewa, hupata fununu kuwa mali au alichonacho mtu ni mazigazi yasiyodumu. Hoja hiyo pia imebainishwa katika shairi la'cheo' (Mnyampala 1965:23). Kwa mfano, imetongolewa ifuatavyo:

Inataka muungwana, muungwana wa upeo,
Yule asiyejivuna, akajivunia cheo,
Kwa tabia hiyo hana, ya majivuno na ndweo,
Cheo huwa ni kileo, kwa mtu wa kulimbuka (Ubeti wa 1)

Dondoo hilo limesisitiza umuhimu wa utu na maelewano mema katika jamii. Mathalani, watu ambao huweka matumaini na matarajio yao yote kwenye vitu walivyovihodhi kwa hila na udanganyifu, ni wapungufu wa utu na busara. Kutokana na maelezo hayo ya yaliyowasilishwa, huweza kumfanya msomaji kutaka kufahamishwa zaidi kuhusu majitwazo na kiburi cha wale walichonacho miongoni mwa jamii. Baadhi ya wahakiki wa kifasihi wameeleza kuwa: uzuri wa mashairi ya *Sauti ya Dhiki* ni kwamba, humuacha msomaji katika shauku ya kutaka kuyasoma zaidi (Matteru 1975:24). Kadhalika, matumizi ya methali na maelezo yaliyotolewa humchochea msomaji kuwa na nguvu mpya au ilihamu ya kutaka kuendelea kulisoma shairi zima ili aweze kufahamu zaidi ujumbe unaowasilishwa. Kwa mfano, kupata kitu hakupaswi kumfanya binadamu kuwa baradhuli au kujitenga na wanajamii wenzake. Kwa sababu, pande hizo mbili za watu hutegemeana katika jamii. Mshairi alipofikia ubeti wa nne alibainisha kwa uwazi kuhusu mwelekeo mbaya na makeke ambayo husababishwa na mali au uwezo alionao mtu. Ni katika hitimisho la shairi, ambapo mshairi ameonya kuhusu vitimbi na kiburi kinachosababishwa na mali au uwezo alionao mtu katika jamii. Hata baada ya kuhitimisha utungo, humtaka msomaji kujenga mazingira yaliyoibua isitiari ambayo

humfanya kutokidhi hamu ila kuendelea kutafakari na kufafanua zaidi ujumbe uliowasilishwa.

3.1.2.5 Methali kama Chombo cha Uzindushi na Uwasilishaji wa Maadili

Kiuchambuzi, matumizi ya methali hiyo imelifanya shairi kuwa lenye upeo mkubwa wa maudhui ya kiuzindushi na kimaadili. Kimsingi, mshairi ana wajibu muhimu sana katika kuielimisha jamii. Hata hivyo, jukumu lake si kusifu bali kuonya na kukosoa. Itikadi au mwongozo alionao msanii ni ule ni wa kujihusisha na maoni, mahitaji na matakwa ya walio wengi na hasa watu waliomo katika tabaka duni iwapo ni jamii ya kitabaka. Kwa hivyo, mshairi huwa na jukumu la kutetea na kuufafanua uhalisi na ukweli wa kijamii na kuuponda unafiki na uwongo katika jamii (King'ei na Kemoli 2001:8). Kutokana na tajiriba yake, mtunzi ameitumia methali kwa makusudi na kwa azma ya kukashifu na kukejeli baadhi ya matendo mabaya ya viongozi (vinyozi) katika jamii. Kadhalika, msanii haoni ni kwa nini baadhi ya viongozi waliopewa nyadhifa hizo; badala ya uihudumia jamii huvimbishwa kiburi huku wakiweka masilahi ya kibinafsi mbele. Viongozi wenye mielekeo hiyo hasi, husutwa kwa kuzingatia muktadha wa matumizi ya methali hiyo. Dhana ya baadhi ya viongozi kukataa kushauriwa imejitokeza pia katika shairi la'Ewe Sarahangi' (Mohamed 1980:2). Shairi hilo lenye ubeti mmoja umetoa uelekezi kwamba:

Ewe sarahangi, kizindukana, sikia, chombo chenda mrama
Manahodha wengi, wanazozana, pania, bado kungali mapema
Na upepo mwingi, tunagongana, balia, gharika inanguruma
Manahodha wengi, chombo chenda mrama

Katika ubeti huo, mtunzi amewataka wanaoshikilia hatamu za uongozi kusikia sauti ya watawaliwa. Kwa sababu, taifa au *chombo* ni cha wanajamii wote. Kadhalika, kupitia kwa methali *Manahodha wengi, chombo chenda mrama* ndipo ujumbe wa uzindushi na maadili hupitishwa. Kulingana na ujumbe katika shairi la 'Muwerevu Hajinyowi' ni kwamba, viongozi hawapaswi kuwasahau waliomkweza ambapo kwa wakati huo wakidharauliwa na wakinyanyaswa.

Kadhalika, mshairi humtaka msomaji kurejelea mifano halisi ya watu waliowahi kuangamia kutokana na kiburi kilichofungamanishwa na mali waliokuwa nayo. Kwa hivyo, kupitia kwa methali mshairi huweza kuwa kinywa au chombo cha kuwaonya watu wenye kiburi kuwa, wanavyotenda si mwafaka. Aidha, watu hao huhitaji kuwa wenye utu na maelewano mema katika jamii.

3.1.3 Shairi: Zindukani

Shairi hili ni la muundo wa tarbia na lina beti ishirini na nne. Aidha, limetumia methali mbili mahususi ambazo huchangiana na hukamilishana katika uwasilishaji wa ujumbe Katika shairi. Methali hizo ni: '*Ukipanda siku ya mvuwa, utakula siku ya juwa'* na *Kingoja kusaidiwa, tutakufa masikini.* Dhima ya methali hizo imebainishwa katika ufafanuzi ufuatao. Maudhui ambayo yamewasilishwa katika shairi ni kuhusu uzindushi zaidi na uhamasishaji wa jamii.

3.1.3.1 Ukipanda Siku ya Mvuwa, Utakula Siku ya Juwa

Methali ambayo imetumiwa inapatikana katika ubeti wa kumi na tatu. Maneno mahususi ambayo yameunda methali hiyo, yametawanyika katika mshororo wa tatu na wa nne. Mwangwi wa methali hiyo hueleweka pindi ubeti huo unaposomwa na kuzingatiwa. Kwa hivyo, imebainika kuwa, si lazima maneno yote kuweza kutokea kwa pamoja katika mfumo mmoja wa methali. Katika ubeti huo imetongolewa kuwa:

Si kwamba walikiiza, wenzenu kamanywi kuwa
Lakini wakijikaza, na kujinyima uluwa
Wao wakijihimiza, kupanda siku ya mvuwa
Kusudi siku ya juwa, waje kula kwa makini (Ubeti wa 13)

3.1.3.1.1 Methali kama Mbinu ya KujengeaUsuli au Dibaji

Methali hiyo imetumiwa kujenga mazingira ya usuli au dibaji kuhusu ujumbe ambao umetarajiwa kuwasilishwa. Katika beti wa kwanza hadi wa kumi na mbili, yaani kabla ya methali kutumiwa, mshairi ameweza kubainisha kwa kuyakinisha uhalisi wa maisha ya jamii. Katika muktadha wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli teule za kimapokeo huweza kutumiwa kuwa anwani au sentensi mahususi ambayo huelekeza uchimuzi wa ujumbe ambao huwasilishwa (Parry 1968). Ingawa methali iliyotumiwa haikujitokeza kama anwani au mwanzoni mwa shairi, matumizi hayo yameshirikisha mawazo ambayo tayari yamezingatiwa. Kadhalika, kwa ambavyo ni methali ya mwanzo; imekidhi haja hiyo. Katika jamii ya mshairi, baadhi ya watu wamekuwa wakilaza damu huku wakitarajia kufanikiwa maishani kutokana na kudura za mwenyezi Mungu. Hiyo ni itikadi ambayo haina mashiko. Kwa hivyo, mshairi haoni mwafaka wowote ambao huweza kupatikana kupitia kwa miujiza. Kulingana na mawazo ya baadhi ya jamii ya mtunzi ni kwamba, Mungu ndiye huwasaidia katika kunyanyua hali ya maisha katika

jamii. Kadhalika, kuna baadhi ya watu ambao wamebahatika kutokana na urithi walioachiwa na wavyele wao. Kundi hilo la watu hustahabu kuwa na mali hiyo, huku wakiionea fahari au kuwa kigezo cha ufanisi katika maisha. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, mawazo hayo ni potoshi. Kwa sababu, kile kilichorithiwa kisipoimarishwa na kustawishwa, kitadidimia huku wakiachwa fukara. Katika jamii ya mshairi, kuna wale ambao hujikakamua kila uchao kwa kujinyima ili kuututumua au kuimarisha uchumi wao. Walipokuja kufanikiwa maishani katika siku za usoni, wale waliokuwa wakilaza damu hujiuliza ni kwa nini wao wasifanikiwe kama wenzao!

Makundi hayo mawili yanapolinganishwa hubainisha kwamba, wale waliokuwa wakijitahidi wameweza kutononoka ilihali wenzao wana maisha yaliyodorora au duni. Kwa mfano, katika kibwagizo cha ubeti wa kumi imekaririwa kuwa:

Hawa kuwa kipumuwa, saa zote wa mbiyoni

Katika muktadha wa dondoo hilo, mtunzi ametaka kueleweka kuwa ukwasi na maendeleo katika jamii hayatokani kwa sadfa au kutegemea kudura za Mwenyezi Mungu bali kwa jitihada na juhudi za kibinafsi. Vile vile, mshairi amemwondolea lawama Mwenyezi Mungu kwamba, ni yule aliyejitahidi katika maisha ndiye hufanikiwa. Kwa kutumia methali hiyo, mshairi ameweza kuoanisha mawazo na mwelekeo alionao na utendakazi katika jamii. Kwamba, mwanajamii asipopanda wakati wa majira ya mvua ni muhali kutarajia miujiza ya kuvuna wakati wa jua. Kwa sababu, endapo mja hakufanya lolote, hawezi katu kutarajia kuvuna chochote siku za usoni. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, mtu kama huyo hustahili kulamiwa au kujilaumu mwenyewe badala ya kuwalaumu wenziwe kwa dhiki ambazo humwandama. Aidha, matumizi ya methali,

yamemfanya mshairi kuwa katika nafasi murwa ya kufahamisha kuhusu uhalisi wa maisha katika jamii kusudiwa. Methali hiyo ingeweza kutokea katika ubeti wa mwanzo, haidhuru pale ilipotokea. Kwa sababu, imekidhi mahitaji ya kutanguliza mawazo.

Kadhalika, matumizi ya methali hiyo imedokezea muhtasari wa ujumbe kimbele. Hata hivyo, shairi hili halitakamilika bila ya kufaragua au kufafanua baadhi ya maelezo ambayo yamefuatia baadaye. Hiyo ndiyo sababu ya kutumwa kwa methali nyingine ya *Kingoja kusaidiwa, tutakufa maskini*. Methali hiyo imesaidia katika kujenga mazingira ya kilele cha matukio katika shairi. Kwa hivyo, kila methali iliyotumika imeshikilia nafasi muhimu katika uwasilishaji wa ujumbe katika shairi.

3.1.3.1.2 Uibushaji wa Taswira Kutokana na Matumizi ya Methali

Mshairi ameitumia methali hiyo ili kumsaidia msomaji kutunga picha ya kimaono ambayo imechangia uwasilishaji wa ujumbe. Msomaji anapokumbana na methali hiyo, hushawishika kuunda picha kamili ya mkulima ambaye tayari ametayarisha shamba na mbegu zimepandwa au miche imesimikwa. Mwanajamii huyo, amefanya hivyo kwa shauku na matumaini kwamba, siku za usoni atapata mavuno yatakayomfaa na kumvusha wakati wa kiangazi au wa njaa. Kinyume na hayo, mtu aliyelaza damu wakati wa upanzi, hutatizika mno siku za usoni kwa sababu lishe yake itakuwa haba. Katika kufafanua zaidi wazo hilo, amesema:

Muzowele kubwagaza, na kungoja majaliwa
Viungo mumviviza, hamtaki jisumbuwa
Hamuna munaloweza, mwataka ya kufanyiwa
Daima tutapwelewa, jamani amshanani (Ubeti wa 2)

Kutokana na kauli ya *muzowele kubwagaza, kungoja majaliwa* imedhihirisha namna jamii hiyo ilivyoendekeza uzohali. Kwa kutumia methali, mshairi ameishawishi akili ya msomaji kuoanisha maono yaliyojengwa na ujumbe ulioibuliwa katika shairi. Mawazo ambayo hayo yamejikita katika kuwabainisha baadhi ya wanajamii ambao hawataki kujituma bali kutarajia miujiza ili iwaauni. Kadhalika, mshairi ameweza kushutumu na kukemea vitendo hasi ambavyo huendekezwa na baadhi ya wanajamii. Kwamba, si ajabu kwa watu ambao ni mazohali kushangazwa wakati hali zao za kimaisha zilipodorora ilihali wenzao walioshika mpini hapo awali, hawababaishwi. Hata hivyo, haoni ni kwa nini baadhi ya wanajamii hawawezi kujiuliza sababu ya hali zao za kiuchumi kudumaa daima ingawa kuna ithibati halisi ya watu walioimarisha uchumi wao katika jamii. Kwa mfano, kuna watu ambao wamejinyanyua na kuboresha uchumi wao kutokana na jasho lao kama ilivyoelezwa katika ubeti ufuatao:

Nyuso mlipogeuza, na mato kuyafumbuwa
Kuona walivyojaza, wale walofanikiwa
Haanzanyi kuuliza, waliyapataje hawa?
Kama bure kutolewa, au kwokotwa jaani (Ubeti wa 6)

Jambo jingine ambalo mshairi hapendezwi nalo katika jamii ni kwamba, baadhi ya watu walivyouchukulia urithi kemkem walioachiwa na wavyele wao. Badala ya kuimarisha fungu hilo, hulifuja katika anasa ili waonekane na kutambulika katika jamii kuwa ndio waliojiweza kiuchumi. Aidha, ubadhirifu huo hufanywa na baadhi ya wanajamii ili waweze kushehenezwa sifa ambapo kwa mtazamo wa mshairi ni bandia. Ujumbe wa mtunzi umepitishwa pia kwa taswira iliyojengwa. Kwa mfano, ubeti wa nne umekariri:

Lenu kubwa kujitwaza, na kupenda kusifiwa
Na kupenda kujijuza, mtu alivyozaliwa
Apitie akitangaza watu wapate mjuwa
Ili apate ambiwa, yu fulani wa fulani (Ubeti wa 4)

Kwa hivyo, mambo hayo huwafumba au huwatia kiwi macho ili wasitende murwa kulingana na mahitaji ya uhalisi wa maisha. Kutokana na matumizi ya methali, mshairi ameweza kuwasilisha wazo kwamba, baadhi ya wanajamii hujali ya wakati uliopo na kusahau ya siku za usoni. Katika kushadidia wazo hilo, ubeti wa kumi na mbili umebainisha kuwa:

Vyenu mulipovisoza, na kwa fujo kutumiwa
Wenzenu wakijikaza, matumbo kutopanuwa
Wakila na kubakiza, kwa ya kesho kutojuwa
Ndipo hi' leo wakawa, wako juu mukotini

Kupitia kwa dondoo hilo, hali halisi ya jamii imebainishwa na imedhihirishwa kitaswira. Hata hivyo, taswira iliyoibuliwa imefafanuliwa na imeshadidiwa zaidi kupitia kwa methali iliyotumika. Zaidi ya hayo, mshairi amekirihishwa kwa tabia ya baadhi ya wanajamii ambao, baada ya kurithi mali furifuri huamua kuoa wanawake wengi na kujiingiza katika hawaa za dunia kuwa ishara ya ukwasi walionao. Ubainishaji huo umejitokeza pia katika ubeti wa kumi na nne, hasa baada ya methali kutumiwa. Katika ubeti wa kumi na nne, imetongolewa:

Vyenu ngoma muliteza, na wake wingi kuowa
Mijana mukasambaza, musoweza watu kuwa
Raha mulitanguliza, nazo zikawapotowa
Mpaka mukaishiwa, ha mu nyingi ha mu nani (Ubeti wa 14)

Katika dondoo hilo, hawaa na anasa za baadhi ya watu zimedhirishwa. Kwa hivyo, hadhira huweza kuishuhudia kadhia hiyo kutokana na maelezo yaliyotolewa. Baada ya kuifuja mali yao, huweza kuelekeza kidole cha lawama kwa wenzao badala ya kujilaumu wao wenyewe.

Kulingana maelezo yaliyotolewa, watu hao hustahili kugeuza mielekeo na nyendo zao kwa manufaa yao wenyewe na kwa jamii nzima. Kwa hivyo, methali hiyo imetumiwa ili kuweza kuupitisha ujumbe kwamba, mtu asipopanda kwa wakati unaofaa, huambulia patupu. Hapa inapaswa kueleweka kwamba, waliofanikiwa katika jamii si kutokana na sadfa au miujiza. Shime, ni kwa wanajamii kujitahidi na kujinyima ili kuboresha uchumi wao badala ya kuzuzuliwa au kuzuzuana. Kutokana na vile baadhi wanajamii walivyothamini mno sifa bandia kutoka kwa jamii, hukuta uchumi wao umesambaratika na kuanza kutoa lawama zisizokuwa na msingi.

3.1.3.1.3 Methali kama Chombo cha Uzindushi

Kutokana na matumizi hayo ya methali, mshairi huwa ni mwalimu mwenye maono ambayo hupaswa kuwaelekeza wenzake katika jamii. Kwa ambavyo mshairi ni miongoni mwa wanajamii, hataki kamwe kuuficha ukweli wa mambo bali kuukabili na kuuwasilisha uhalisi huo mchungu. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mtunzi ni mwanajamii. Kwa hivyo, mazingira alimokulia na kulelewa ndiyo humwelekeza katika kuteua kauli ambazo hututumika (Wood 1971). Kwa kutumia methali hiyo, mshairi ameweza kuubainisha uzandiki na mwelekeo hasi uliofichama katika jamii. Kwa mfano, haoni ni kwa nini jamii hiyo kutegemea *majaliwa* ilihali haitaki *jisumbuwa* wala *kwandama zao hatuwa*. Kwa hivyo, watu hao waliorejelewa wana nguvu lakini kikwazo ni kwamba; kujitahidi kwao ni kama kujidhalilisha. Sauti shime ilikuwa imedokezewa hapo awali katika ubeti wa kwanza kuwa:

Sikuja weka baraza, au hadithi kutowa
Sikuja kuzungumza, maneno yaliyokuwa
Nakuja kuw'eleza, ambao yatu sumbuwa
Tuyatafutiye dawa, tuongokewe maishani (Ubeti wa 1)

Kupitia kwa dondoo hilo, mshairi hufahamu kuwa wanajamii hawaupendi ukweli lakini hasiti kuudhihirisha kwa ujasiri hata kama atasutwa na jamii. Katika muktadha wa matumizi ya methali, mshairi ameweza kuwaonya na kuwakemea baadhi ya wanajamii wenzake kwamba, wasipojitahidi kuukwamua uchumi wao, wasitarajie miujiza iwaauni. Vile vile, matumizi ya methali hiyoimesaidia kumbainisha mtunzi kama mzalendo ambaye huistahi na huithamini jamii. Aidha, hataki kuimba wimbo ambao hupendwa katika jamii bali alichokitaka ni kuipa jamii mtazamo na mwelekeo ambao ni wenye manufaa zaidi katika jamii. Hiyo ndiyo sababu huwaona baadhi ya watu waliolaza damu kama wanaojitakia nakama au maafa katika maisha yao ya baadaye. Waadhi ambao umeotolewa ni kwamba, wanajamii wenzake watakapositisha kuzuzuliwa kwa mali walioirithi au kujiona 'wangwana' kwa kutotoa jasho; ndipo uchumi wa jamii huweza kuimarika.

Kadhalika, mshairi hataki katu wenzake waje kujutia matendo na mielekeo yao ya wakati huu uliopo ilihali yeye mshairi yu macho. Kupitia kwa methali hiyo, msomaji hubainishiwa kwa undani mtazamo na mwelekeo wa mshairi kuhusu mambo ya msingi ambayo hupaswa kuzingatiwa ili maendeleo katika jamii yaweze kuimarika. Swala hilo la uzindushi limebainishwa pia katika shairi la 'Mtu Hachagui Kazi' (Mohamed 1980:23). Katika ubeti huo wa kwanza imetongolewa kuwa:

Naamba kazi ni kazi, vyovyote vile iwavyo
Madamu si ubazazi, kwa mwanadamu ndivyo
Kushona na upagazi, pia vile vyenginevyo
Kazi ni kitu azizi, wala vyenginevyo sivyo
Mtu hachagui kazi

Kwa kuzingatia dondoo hilo, kazi ni wajibu na ni msingi wa uhai katika jamii. Kwa hivyo, watu hupaswa kuanza au kuiendeleza kazi kwa manufaa ya mtu binafsi na jamii kwa ujumla.

3.1.3.2 Kingoja Kusaidiwa, Tutakufa Masikini

Methali hiyo imejitokeza baada ya ile ya awali ya: *ukipanda siku ya mvuwa, utakula siku ya juwa* na inapatikana katika ubeti wa ishirini hususa, kama kibwagizo katika shairi. Kwa pamoja methali hizo zimeshirikiana katika ubainishaji na uwasilishaji wa ujumbe katika shairi. Matumizi na utendakazi wake umechanganuliwa kama ifuatavyo.

3.1.3.2.1 Methali kama Mbinu ya Kuimarishia Zaidi Taharuki

Methali hiyo imetumiwa kama mbinu ya kufaragua na kupanua zaidi mawazo yaliyowasilishwa katika shairi. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, hoja iliyoibuliwa kwa kauli msingi huweza kuendelezwa na kufafanuliwa zaidi kupitia kwa kauli zingine ambazo pia zina uzito ulio sawia katika uwasilishaji wa ujumbe (Nagler 1967). Katika uwasilishaji wa utungo huo kuna methali mbili zilizotumiwa na zilizojitokeza kiawamu. Kadhalika, methali hiyo imechangia kwa ufundi busara au mawazo yaliyoibuliwa katika ile ya awali: *Ukipanda siku ya mvuwa, utakula siku ya juwa.* Kama vile ilivyokwisha kudokezewa hapo awali, methali ya awali imetumiwa kwa malengo ya kufunulia athari ya mwelekeo hasi katika jamii kuhusu utendakazi wa kazi na uendekezaji wa anasa miongoni mwa wanajamii.

Methali hiyo ya pili *Kingoja Kusaidiwa, tutakufa maskini*, imemwandaa msomaji kuupokea ufunuo zaidi kuhusu athari na madhara ambayo huweza kutokana na ubadhirifu wa mali katika jamii. Wanajamii hao, kama ilivyoelezwa, hawataki kufanya kazi na wale wenye mali waliyoirithi huifuja katika anasa huku wakitarajia miujiza au *majaliwa* ya Mwenyezi Mungu. Kupitia kwa methali iliyotumiwa, mshairi ameweza kufafanua zaidi kuhusu uzohali na ubadhirifu wa mali uliosakini katika jamii. Katika muktadha huo, haoni manufaa yoyote ambayo huweza kusababishwa kwa kuoa wanawake wengi. Kwa mfano, imetongolewa kuwa:

Vyenu ngoma mukiteza, na wake wengi kuowa
Nyana mukasambaza, musoweza watukuwa
Raha mulitanguliza, nazo zikawapotowa
Mpaka mukaishiwa, hum u nyinyi ha mu nani (Ubeti wa 14)

Dondoo hilo limewasilisha namna watu walivyotumia mali yao katika anasa na starehe ili waweze *sujudiwa*. Katika jamii ya mshairi, mtu aliporithi mali hutaka kudhihirisha utajiri alionao kwa kuoa wanawake wengi. Kadhalika, mshairi angependa msomaji kuweza kupata ufunuo zaidi kuhusu namna baadhi ya wanajamii walivyopotoka kutokana na mielekeo yao kuhusu utendakazi katika jamii. Kwa mfano, mtu aliporithi mali hajitutumui kuchangiza mali iliyopo, bali hujiingiza katika anasa na hawa za dunia. Zaidi ya hayo, huinadi raslimali waliyonayo hadi wanakuwa muflisi. Ni baada ya kuwa fukara, ndipo huanza kujuta na kusema kuwa *Pale pangu palikuwa*. Baadhi ya watu ambao walijitutumua katika utendakazi na kuimarisha uchumi wao ndiyo sasa huwa watajika na kula murua katika jamii. Kulingana na mawazo yaliyowasilishwa, ni muhali kwa wasionacho kulinganishwa na wenye nacho. Hali hiyo imetokana na ukweli kwamba, 'Ukiona vyaelea vimeundwa'. Hoja hiyo imekuzwa zaidi kama ifuatavyo:

Mukauza mukauza, na watu 'kivinunua
Mukawa mwavipunguza, kila juwa likituwa
Vyote mukavimaliza, mukawa 'mekaukiwa
Wenyewe mulijiuwa, mutamlaumu nani? (Ubeti wa 15)

Ubeti huo umetumika kabla ya methali ya pili, ambapo mtunzi amemtayarisha msomaji kwa ufunuo zaidi. Kwa hivyo, kutokana na methali iliyotumiwa, humtaka msomaji kuelewa sababu za msingi zilizowafanya baadhi ya wanajamii kutajika kwa wakati huu wa sasa. Kwamba, wenye nacho kwa wakati uliopo, walijitolea siku za kisogoni. Kamwe isichukuliwe kuwa, mafanikio na ukwasi walionao wakati uliopo umetokana na miujiza au majaliwa ya Mungu. Kwa hivyo, majitwazo na majisifu uliotokana na nasaba zao hauna manufaa yoyote ila kwa kufanya kazi kwa bidii na kujinyima. Kwa hivyo, methali imesaidia katika kuufafanua na kuupeleka mbele uwasilishaji wa matukio hadi upeo wa juu. Kadhalika, methali hiyo imemfanya mshairi kushuka matao ya chini huku ikitolewa suluhu ya masaibu ambayo huikumba na huipotezea mwelekeo jamii husika.

3.1.3.2.2 Methali kama Msingi wa Ujenzi wa Taswira

Kwa kutumia methali hiyo, mshairi ameweza kuwasilisha picha ya kimaono. Kutokana na methali iliyotumika, msomaji imeundiwa picha ya kimawazo inayomhusu mtu ambaye hajishughulishi katika harakati ya kuboresha hali ya maisha yake kiuchumi huku akistahabu kusubiri miujiza itokee au majaliwa iweze kutendeka. Mshairi ameshangazwa na vitendo hivyo vilivyokithiri miongoni mwa wanajamii. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, mtu ambaye husubiri miujiza au majaliwa ili aepukane na dhiki zilizomwandama. Huo ni mwelekeo wa kidhahania ambao haukujengeka katika msingi wa kihalisi. Kwa kuitumia methali hiyo, mlengwa huweza kujenga utafakari zaidi

kuhusu mtu ambaye hataki kufanya kazi bali kusubiri msaada kutoka mbinguni au kwa wenziwe katika jamii. Mshairi tayari amekwisha kutoa maelezo ya kina kuhusu hali hiyo iliyokithiri miongoni mwa watu. Kadhalika, ujumbe umeweza kuwasilishwa kwa kuzingatia maelezo ambayo yamesaidia kujenga picha ya kimawazo. Maelezo yaliyotolewa kuhusu ujumbe uliowasilishwa ni wa kina na huenda msomaji amepwelewa au amekanganyikiwa kutokana na mkururo wa mawazo. Kwa hivyo, methali imetumiwa kwa makusudi kuwasilisha ujumbe, siyo tu kwa kuzingatia maelezo pana yaliyotolewa bali pia kupitia kwa usawiri wa picha ya kimawazo. Katika muktadha huo, uibuaji wa taswira kumetokana na methali mabayo imetumiwa kama mbinu ya uwasilishaji wa mawazo yalitarajiwa. Ujumbe huo huweza kutasaki zaidi katika taamuli ya msomaji wa shairi. Aidha, taswira iliyoibuliwa kupitia kwa methali huwa ni mbinu ambayo huchangia uwasilishaji wa ujumbe. Katika kushadidia zaidi taswira ya kimaono iliyojengwa kupitia kwa methali. Kwa hivyo, kumetumiwa kauli za kibinafsi kama vile:

- *Petu tupate pakuza, kwa jasho letu kutowa* (ubeti wa 20)
- *Hapo tutahishimiwa, tuhisabike tu nani* (ubeti wa 21)
- *Iwapo tutapunguza, kupenda vyetu vifuwa* (ubeti 22)
- *Yauliza wangu moyo, wala hautanyamaza* (ubeti 24)

Kwa mfano, picha iliyowasilishwa kupitia kwa kauli za madondoo hayo imesaidia kujenga mawazo yaliyozingatiwa katika shairi. Hata hivyo, matumizi ya methali husaidia katika kukumbuka na kutafakari zaidi mifano na maelezo yaliyotolewa kuhusu ujumbe uliozingatiwa.

3.1.3.2.3 Methali kama Msingi wa Kuibulia Isitiari

Mshairi ametumia methali ili usawiri na uwasilishaji wa utungo kuweza kufasirika kimafumbo au kiisitiari. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, ujumbe ambao huwasilishwa katika tungo za kifasihi huwa ni wa kimaono na kimafumbo (Scholes 1982). Katika utungo huu kumetumika methali ili ujumbe kuweza kuwasilishwa na kufasirika kiisitiari. Kwa mfano, *Kingoja kusaidiwa* ni ile hali ya baadhi ya wanajamii ya kutotaka kutoa jasho na kustahabu majaliwa kuweza kutokea au kutendeka. Kwa kutumia methali, mshairi amejenga mazingira ambayo yamesaidia katika utafakari zaidi wa ujumbe ambao huweza kubainishwa zaidi nje ya muktadha wa maneno yaliyopatikana katika methali.

Katika muktadha huo, msomaji huweza kuizingatia kauli teule kama ishara ambayo huhitaji kufafanuliwa na kufasiriwa kwa kuihusisha na uhalisi wa maisha katika jamii (Pierce 1977). Kwa hivyo, mshairi amaekuwa akidokezea kuwa, baadhi ya wanajamii wamekuwa wakilaza damu ilihali ni msingi wa utu wao na ni uti wa mgongo wa uchumi katika jamii. Kwa mfano, wanajamii waliozingatiwa ni wenye siha na uwezo, lakini huchukulia kuwa, kufanya kazi ni kujidunisha na kujiumbua katika jamii. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, wale wanajamii ambao ni wajuzi wa ufujaji wa mali ndio husujudiwa na hutukuzwa kinyume na uhalisi wa mambo. Kwa hivyo, katika jamii hiyo kuna mwelekeo hasi wa kushindana katika kutokuzingatia kazi. Hali hiyo imefafanuliwa zaidi, kuwa:

> *Wenzenu lilowakweza, ni jasho walilotowa*
> *Si raha si miujiza, wala si majaliwa*
> *Na si kwa kujitukuza, wala kwa kwao kuzawa*
> *Hawakujiviza hawa, nasi natukazaneni* (Ubeti wa 18)

Sehemu ya pili ya methali hiyo: *tutakufa masikini* huweza kusaidia katika utafakari zaidi kuhusu dhiki ambazo huikumba jamii kutokana na uzohali au uzembe huo. Mathalani *kifo*, kulingana na jinsi dhana hiyo ilivyotumika, huweza kufasiriwa kuwa ni hali ya kuasi au kutoweza kuudhibiti uchumi wa jamii. Kadhalika, mshairi ameweza kuwafananisha watu ambao huusambaratisha uchumi wao kama watu wasiokuwa na manufaa yoyote katika jamii. Isitiari iliyoibuliwa kupitia kwa matumizi ya methali, huwa ni chemichemi mwafaka ya kutafakarisha ujumbe batini ambao umewasilishwa. Zaidi ya hayo, utafakari huo hupata nguvu kupitia kwa maelezo yaliyotolewa katika utungo.

3.1.3.2.4 Methali kama Mhimili wa Kuendeleza Mawazo

Kama ilivyoelezwa hapo awali katika utunzi na uwasilishaji, msanii ametumia kwa makusudi methali mbili. Methali zote mbili zimeshikilia nafasi muhimu katika uibushaji na ukuzaji wa mawazo na hisi za mshairi. Katika muktadha wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, uwasilishaji wa ujumbe katika utungo huzingatia utaratibu maalumu. Kwa mfano kuna kauli za kuutanguliza na zile za kuufaragua ujumbe (Parry 1968). Kwa ambavyo kuna methali mbili zilizotumiwa, ya mwanzo hujenga usuli au utangulizi. Methali ya pili hujenga muktadha wa kuufafanua zaidi ujumbe katika utungo. Kwa hivyo, methali ya mwanzo imesaidia katika kuyakinisha na kubainisha mielekeo hasi ya baadhi ya watu kuhusu uzembe na ubadhirifu wa mali katika jamii.

Kadhalika, mawazo yaliyoibuliwa kupitia kwa *ukipanda siku ya mvuwa, utakula siku ya juwa*, hujenga mazingira ya kumtayarisha au kumwandaa msomaji kuelewa msingi hasi wa kiuchumi katika jamii. Kwa kutumia methali ya pili *kingoja kusaidiwa, tutakufa*

masikini, imekuwa ni dira ya kuelekeza zaidi katika kuibulia hisi na maono kuhusu mielekeo ya utendakazi katika jamii. Kwa hivyo, mshairi ameweza kubainisha kuhusu uhalisi wa utendakazi miongoni mwa wanajamii. Kwa hivyo, methali imetumiwa kama mbinu ya kumshika mkono msomaji ili kuweza kumwongoza na kumfunulia zaidi msimamo kuhusu vitendo hivyo hasi katika jamii. Kwamba, ni muhimu kubadili mielekeo iliyopo ili maendeleo na uchumi wa jamii kuweza kustawi na kuimarika. Kulingana na mawazo yaliyowasilishwa, kazi ndio msingi na uti wa mgongo wa maendeleo katika jamii, kinyume na sifa walizoshehenezwa wale waliolaza damu.

Kadhalika, starehe, anasa na ubadhirifu wa mali kwa wakati uliopo huwa ni kikwazo cha uchumi katika siku za baadaye. Tayari mshairi amekwisha kubainisha mtazamo hasi wa wanajamii kupitia maelezo yaliyotolewa. Kulingana na muktadha uliojengwa, mweleko huo hauna nafasi katika maendeleo ya jamii. Ingawa anasa na ufujaji wa mali umekuwa ukitukuzwa na kupewa kipaumbele; mawazo hayo, ni tofauti na mwelekeo alionao mshairi. Kwa ambavyo mshairi amejidhihirisha kuwa yu miongoni mwa wanajamii. Kwa hivyo, amekuwa akikirihishwa na mielekeo hiyo wa baadhi ya watu walivyochukulia dhana ya utendakazi kuwa ni udhia. Kupitia kwa methali, mshairi ameweza kubainisha na kuwasilisha zaidi hisi zake huku akitoa mifano ya msingi ambayo hupaswa kuzingatiwa kwa manufaa ya jamii.

3.1.4 Shairi: Kutendana

Shairi hili ni la tarbia na limesawiriwa na kuwasilishwa kwa kushirikisha beti mia moja na sabini na sita. Kimsingi methali nne zimetumiwa katika uwasilishaji wa utungo.

Katika muktadha wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli teule za kimapokeo huweza kuwa zaidi ya moja ambapo huchangia na kuukoleza ujumbe unaowasilishwa (Nagler 1967). Kadhalika, kupitia kwa nadharia ya Semiotiki ujumbe hukolezwa kutokana na maana zilizoibuliwa katika ushirikiano wa kauli teule ambazo hutumika katika utungo (Mosha 2008). Kwa hivyo, utungo mrefu kama huo huhitaji kuwa na mada ndogo ndogo ambazo zimechangia katika ufafanuzi wa mada pana. Methali hizo zilizotumika katika shairi ni:

- *Mtu huwa hakutupa, amfaapo mwenziye* (ubeti wa kwanza)
- *Nyege ni kunyegezana* (ubeti wa pili)
- *Mjinga 'meerevuka, mwerevu u mashakani* (ubeti wa kumi na tatu)
- *Yaliyopita yamepita, si vyema kuyaregeza* (ubeti wa tisini na saba)

Methali tatu za mwanzo zimekaulishwa kwa wahusika. Kwa mfano, ya kwanza ni kauli ya Mwanamume; ya pili na ya tatu ni za Mwanamke; nayo ya nne ni ya mtunzi mwenyewe. Hapa ifahamike kuwa katika shairi hili kuna wahusika wawili: Mwanamume na Mwanamke. Kwa sababu, mshairi ametumia mbinu ya kimalumbano katika uwasilishaji wa shairi. Malumbano ni mbinu ambayo hutumika mno katika uwasilishaji wa tanzu za fasihi simulizi hususa, ushairi (Alembi 2002). Kwa kuzingatia ufundi alionao mtunzi, ushairi andishi huweza pia kuibua matumizi hayo (Njogu 2004). Methali hizo zilizotumiwa na Mwanamke ni: *Nyege ni kunyegezana* ambayo inapatikana katika ubeti wa pili katika shairi. Methali ya tatu ni *Mjinga 'merevuka, mwerevu u mashakani* ambayo inapatikana katika ubeti wa kumi na tatu katika shairi hili. Kadhalika, methali hizo zimejitokeza kama kibwagizo katika beti hizo. Kimsingi, zimechangiana na zimetegemeana katika uwasilishaji wa ujumbe katika shairi.

3.1.4.1. Mtu Huwa Hakutupa, Amfaapo Mwenzake

Mantiki ambayo huibuliwa kupitia kwa methali hiyo ni kwamba, mtu anapomsaidia mwenzake kwa kumpa kitu, ni jambo ambalo hutokana na utu alionao. Katika utamaduni wa mwafrika hususa jamii ya Waswahili, ni wajibu kwa watu kusaidiana wakati wa dhiki. Kadhalika, hakuna mja ambaye huweza kujitosheleza kwa kila kitu. Kwa hivyo, mtu huteseka kimawazo endapo ana kitu cha kumwondolea mwenzake dhiki hiyo. Mtu huyo aliyesaidia hukumbukwa daima kwa ukarimu alioutenda.

3.1.4.1.1 Methali kama Mbinu ya Kujengea Dibaji

Mshairi ametumia methali hiyo ili kumwandaa msomaji shairi kuupata usuli wa msingi unaozuliwa ili kujenga mgogoro wa kimahusiano baina ya wahusika: Mwanamume na Mwanamke. Kwa kutumia methali hiyo, mtunzi ameweza kubainisha hisi na mwelekeo wake kuhusu mahusiano hayo yaliyodorora baina ya Mwanamume na Mwanamke. Katika muktadha huo, imedhihirishwa hila zilizotumika na mhusika Mwanamume kumrai Mwanamke. Kwa mfano, Mwanamume tayari amefunga safari na kumjia Mwanamke kwa kusudi la kukidhi mchomo wa ashiki. Katika utangulizi, hasa kupitia kwa mhusika Mwanamume, imesawiriwa kuwa:

> *MWANAMUME*
> *Kama bure utanipa, nipa sinisumbuliye*
> *Kama hutaki 'takopa, nikulipe baadaye*
> *Hivi sasa cha kukupa, sina: kweli nikwambiye* (Ubeti wa 1)

Dondoo hilo limebainisha uhusiano uliopo baina ya Mwanamume na Mwanamke. Kutokana na matumizi ya methali kama kibwagizo katika ubeti huo wa kwanza,

humuwia rahisi msomaji kubaini na kung'amua kuwa hapo awali Mwanamume amekuwa akikidhiwa haja zake za kimapenzi bila pingamizi.

Kadhalika, msomaji huweza kubainikiwa kwamba, mambo aliyoyakuta Mwanamume kwa Mwanamke si shwari kama ilivyokuwa kawaida. Vile vile, mshairi humtaka msomaji aelewe kuwa Mwanamke huyu ana mkururo wa mchomo wa maswali ambayo huhitaji kujibiwa na *mwenzi* wake. Katika muktadha huo, mshairi tayari amemwandaa msomaji kutarajia ufunuo zaidi kupitia kwa kadhia na maelezo yaliyotarajiwa kuwasilishwa. Hiyo ndiyo sababu katika malumbano hayo, Mwanamke amejitokeza na kusema kuwa: *sina kila siku sina, sina kwako i maisha.* Kwa hivyo *Sina* hizo huhitaji kutolewa maelezo ya hapo baadaye.

3.1.4.1.2 Uibushaji wa Kinaya Kupitia kwa Methali

Matumizi ya methali yamelifanya shairi kuwa lenye mguso wa kinaya. Kupitia kwa nadharia ya Semiotiki, maana ya kauli teule huweza kubeuliwa ili kuichochea hadhira katika tafakuri (Jacobson 1960). Kwa sababu, msanii huwa hauwasilishi ujumbe moja kwa moja. Kwa mfano, katika uhalisi wa ujumbe wa methali ni kwamba: mwanajamii anapomfaa mwenziwe humfanya kukumbukwa kwa utu na wema aliotenda. Wanaohusika katika kitendo hicho cha utu hukumbukana na kustahiana daima. Kamwe watu hao hawawezi kutendeana mabaya kila wanapokutana. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, mhusika Mwanamume hajaonyesha utu uliostahiki kwa Mwanamke. Hapo awali mhusika Mwanamke amekuwa kimkidhia mwanamume haja hizo bila ubishi wala kinyongo. Moyoni alikuwa akimchukulia mwenzake kuwa mwenye utu kumbe sivyo.

Kinyume na matarajio ya Mwanamke, Mwanamume alikuwa akimkumbuka mwenziwe wakati alipopandwa na ashiki na wakati wa mwambo. Hiyo ndiyo sababu ya kusema kuwa, *Huna siku utanena: ninacho 'kanirambisha?* Wakati ambapo kibindo cha Mwanamume kilituna au kilifurika alimwambaa na aliwaendea wengine mitaani na vilabuni. Kabla ya Mwanamke kuchukua hatua hiyo madhubuti ya kuibana *dawa* stahiki ya kutuliza ashiki, alikuwa tayari amefanya utafiti kabambe mitaani na kugundua kuwa mwenziwe huwa na wengine ambao walimsaidia katika kuuzimua mwako huo na kuifuja mali yake. Kwa hivyo, Mwanamume ameitumia methali kama kauli ya kumrai, na kumghilibu Mwanamke. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, si kweli kuwa Mwanamke akiamua kurithi tena matakwa ya Mwamume atakuwa amesaidia katika kuyapembeja na kuyaboresha mahusiano yao.

Kilichobainika katika mahusiano yao, Mwanamume alitaka *shetani* wake apungwe halafu ajiendee zake. Endapo Mwanamke ataamua kumvua maradhi hayo kwa *dawa* hiyo tunu itamaanisha kuwa amekubali kujidhalilisha au kujiumbua. Kulingana na mawazo yaliyowasilishwa, Mwanamke akikubali tena kumpa Mwanamume mapenzi ya dhati atakuwa ametupa nyonda hizo kwa mtu asiyestahili.

3.1.4.1.3 Methali kama Mbinu ya Kuibushia Viona Nyuma na Mbele

Methali hiyo imetumika siyo tu kwa manufaa ya mtunzi bali pia kwa msomaji. Kwa hivyo, mshairi ameitumia methali kama nyenzo ya kusaidia katika kusawiri matukio yaliyopita kuhusu mahusiano baina ya Mwanamume na Mwanamke. Kadhalika, matumizi hiyo huweza kumfanya msomaji kurejelea kadhia zilizopita ili aweze kuelewa

msingi halisi wa kimahusiano ya hapo awali baina ya Mwanamke na Mwanamume. Kwa mfano, hapo awali Mwanamke alikuwa akimridhia Mwanamume haja zake zote kwa kumpa huba la dhati. Kwa sababu alikuwa akimchukulia mwenzi wake kuwa mwenye upendo, imani na utu. Baada ya utafiti aliofanywa na kuunganishwa moja na moja, aligunduliwa kuwa '*mwenzi*' wake alikuwa hamthamini wala kumstahi. Mhusika Mwanamume alikuwa akimkumbuka wakati ambapo hana chochote mfukoni na mwako wa ashiki ulipomba na umezidi. Hiyo ndiyo sababu ya kitendo cha Mwanamke kumnyima pendo. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, huba la dhati hupewa mtu ambaye hujitolea na mwenye nia ya kulidumisha. Mawazo hayo yamedhihishwa zaidi ifuatazo:

MWANAMUME
Laiti kwamba wajuwa, uhisivyo wangu moyo
Laiti ungetambuwa, niumiavyo mwenziyo
Kattu hungenisumbuwa, na kunifanyiya choyo
Ndiwe wa kuiyondowa, hii dhiki nilo nayo (Ubeti wa 5)
MWANAMKE
Na kama yatakuuwa, kufa kwa maradhi hayo (Ubeti wa 7)

Madondoo hayo mawili yamebainisha zaidi mahusiano ya wahusika hao. Kwa ambavyo, methali ya kwanza na ya pili zimetumiwa kwa karibu, yaani katika ubeti wa kwanza na wa pili, ujumbe ambao umewasilishwa umeweza kuelekezwa kupitia kwazo. Hata hivyo, maelezo ya kina yameweza kutolewa katika beti za hapo baadaye.

Hila zilizotumiwa na Mwanamume ni: kutafuna na kutema. Kwa hivyo alipokuwa na fedha, zilizitumiwa kama chambo cha kuwanasia warembo wengine mitaani ambao walijua kuchuma na kutumia. Baada ya kuzidaka hizo fedha walizozihitaji, walimtema na walimwambaa. Kinyume na wanawake wengine wa mitaani, mhusika Mwanamke

alithamini utu zaidi kuliko fedha alizonazo Mwanamume. Katika muktadha huo, kama Mwanamume angelithamini pendo la dhati, Mwanamke angejitolea kwa hali na mali ili kudumisha mahusiano yao. Ili kueleza kiini cha mgogoro wa kimahusiano baina ya Mwanamume na Mwanamke, imebidi mshairi kutumia mbinu ya viona nyuma kama ilivyodokezewa katika methali iliyopo katika shairi. Kwa mfano, baadhi ya maswali ambayo huweza kutunga katika akili ya msomaji baada ya kukumbana na methali hiyo ni kama yafuatayo:

- kwa nini mshairi ametumia methali hiyo kwa kumkaulisha mhusika Mwanamume?
- Ni ujumi gani uliowasilishwa kupitia kwa methali hiyo?

Ni bayana kwamba, msomaji hatafahamu mtafaruku wa kimahusiano baina ya Mwanamume na Mwanamke ila kwa kurejelea vitimbi na vituko ambavyo Mwanamume amekuwa akimtendea Mwanamke hapo awali. Kwa mfano, Mwanamume anaposema *sina*, ni kweli kwamba hana chochote mfukoni? Je, anapokuwa nacho amekuwa akiwaendea akina nani mitaani? Kulingana na maelezo yaliyotolewa, kwa wakati huu Mwanamke amezinduka na hataki tena kughilibiwa kwa maneno ya kumtoa nyoka pangoni. Kwa sababu vitendo vya Mwanamume vimedhihirisha kuwa hana chembe ya utu wala hisani kwa mwenzake.

3.1.4.1.4 Methali kama Mbinu ya Kujengea Upeo wa Juu

Kwa ambavyo methali hiyo imetokea mwanzoni, imemfanya mshairi kuanza uwasilishaji wa shairi kwa hatua ya wastani kabla ya uwasilishaji huo kuingia katika matao au upeo wa juu. Kwa sababu hiyo, methali imetumiwa ili kujenga maamwandazi ya kuibua

ilihamu ya kutaka kujijuvya zaidi. Kwa mfano, mtunzi ametarajia kumlea msomaji kwa kufahamisha mambo yalivyokuwa kabla ya mhusika Mwanamke kuwa na mtazamo tofauti kuhusu mahusiano hayo na Mwanamume. Kwa kutumia methali hiyo mwanzoni, mshairi amekuwa hana nia ya kumstua kwa ghafla msomaji kuhusu ghadhabu yake juu ya Mwanamume. Hata hivyo, utangulizi umekuwa wenye mshindo uliostahili kupitia kwa methali. Kwa mtazamo wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli msingi hutarajiwa kutumika mwanzoni mwa utunzi kama sentensi ya kutanguliza au anwani (Parry 1971). Katika uwasilishaji wa shairi, methali haikutumika mwanzoni bali imetokea katika ubeti wa kwanza kama kibwagizo. Hata hivyo, kwa kutumia methali kama kibwagizo imetekeleza dhima hiyo. Kwa sababu 'Kutendana' kama anwani imeweza kufafanuliwa kupitia kwa methali iliyotumiwa. Hiyo ndiyo sababu ya kusawiriwa na kuwasilishwa kwa kudokezea maelezo ya msingi kimbele ili msomaji kuweza kujenga fikira na mwelekeo wa Mwanamume dhidi ya Mwanamke.

Kadhalika, akili ya msomaji imechochewa kwa kujengewa mazingira ya kiamsha hamu ya kutaka kuelezewa zaidi kuhusu msimamo anaouchukua Mwanamke dhidi ya Mwanamume. Kwa mfano, baadhi ya maswali ambayo huweza kuibuliwa kutokana na methali hiyo ni:

- Mwanamke atakubali kurithi matakwa ya Mwanamume au la?
- Endapo atakataa, matokeo hayo yatakuwa nini?

Aidha, kutokana na uwasilishaji wa mawazo katika matao ya chini yameandaa katika ujenzi wa mgogoro kufikia kilele. Katika muktadha huo, isieleweke kuwa mawazo

yaliyowasilishwa kwayo hayana manufaa au ni ya kiwango cha chini. Kinyume na hayo, mshairi ameitumia methali hiyo kwa azma ya kumtaka msomaji kupata fununu ya mambo yaliyopita ili kung'amua undani wa ujumbe uliosawiriwa. Ni baada ya kufanya hivyo, ndipo ameendelea kujenga mgogoro hadi kufikia kilele katika shairi.

3.1.4.1.5 Uibushaji wa Isitiari Kutokana na Methali

Matumizi ya methali yameufanya uwasilishaji na ufasiri wa shairi kuwa wa kimaono zaidi na wa kiisitiari. Kwa hivyo, matumizi ya methali yamesaidia kuufumba ujumbe ambao huweza kufafanuliwa na kufasiriwa kwa kuzingatia miktadha mingine ya kitabaka, kiuchumi na kisiasa inayopatikana katika jamii. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, maana ya maneno au kauli teule huweza kuwa ishara ambazo huweza kupata mshabaha wa ufasiri katika muktadha wa utamaduni na uhalisi wa maisha ya watu (Culler 1975). Kwa mfano, mhusika Mwanamume huweza kumithilishwa na baadhi ya wanajamii ambao ni wa tabaka la juu ilihali Mwanamke huwasilisha tabaka la wachochole.

Kulingana na mawazo yaliyoibuliwa, watu wa tabaka la juu huwakumbuka watu wa tabaka la chini wakati wanapokuwa wahitaji, yaani wanapotaka kukidhiwa haja zao na baadaye husahau yote murua waliotendewa. Mathalani, Mwanamke amechukuliwa kama chombo cha kumpunga *pepo* alipompagaza Mwanamume na baada ya hapo husahau yote aliyotendewa. Katika muktadha huo, utu na heshima hazikutambuliwa kama mihimili muhimu ya mahusiano katika jamii. Kama vile mhusika Mwanamume alivyomtendea Mwanamke, tabaka la juu linapokuwa na uwezo huenda kufuja mali katika anasa na watu

'muhimu' wa tabaka juu. Fedha zilipowaishia ndipo hukumbuka pahali ambako huweza kuendea kwa hadaa ili mahitaji au *pepo* wao kuweza kupungwa.

Hata hivyo, mshairi haoni mwafaka wowote ambao huweza kupatikana katika mahusiano kizandiki baina ya wahusika haoa. Kwa mfano, Mwanamume amekuwa na mawazo kwamba, Mwanamke ni mtu ambaye huweza kupumbazwa na kurubuniwa kwa hadaa. Katika muktadha huu, mshairi ametumia isitiari iliyojengwa kupitia kwa methali mahususi aliyoteuliwa ili kusawiri siyo tu mawazo yanayowasilisha mahusiano ya kijamii, bali pia kama chombo cha kubainishia maswala ya kisiasa na kiuchumi ambayo hupatikana katika jamii. Vile vile, baadhi ya wanasiasa katika jamiii wamekuwa wakitenda kinyume cha yale waliyoyatamka. Aghalabu, kauli za wanasiasa huwa zina ushawishi mwingi kiasi cha kuibua hisi za imani na huruma kwa wale ambao huongoza au hutawala (Njogu 1988). Ili mwanajamii kuweza kutambua vitimbi na hadaa hizo, huhitaji akili pevu ya uzindushi ambapo huweza kumaizi uovu na uzandiki uliosakini katika jamii. Kwa hivyo, katika jamii watu huhitaji kuwatendea wenzao mema, la sivyo wao pia hubidi kupashwa ukweli mchungu uliostahili. Hiyo ndiyo sababu, Mwanamke amekataa katakata uongo na hadaa za Mwanamume ambao umemwathiri kwa muda mrefu.

3.1.4.2 Nyege ni Kunyegezana

Methali hiyo imetumiwa katika ubeti wa pili katika shairi. Maana ambayo hutokana na methali hiyo ni kwamba, mapenzi huhitaji ushirika wa dhati wa pande mbili. Mmoja

anapotenda visivyo basi mwafaka huo hautafikiwa. Katika shairi, methali imekuwa ni kigezo cha kutathmini uhusiano baina ya Mwanamume na Mwanamke.

3.1.4.2.1 Methali kama Msingi wa Kuzua na Kuendeleza Usemezano

Methali imetumika kuwa mbinu ya kuibua mjadala na kuendeleza zaidi mawazo yaliyowasilishwa kupitia kwa methali ya hapo awali ya *Mtu huwa hakutupa, amfaapo mwenziwe*. Kama ilivyoelezwa, methali ya awali imetumika kwa makusudi ili kumtayarisha msomaji kufahamu na kutafakari kuhusu mambo yalivyokuwa katika mahusiano baina ya Mwanamume na Mwanamke. Methali ya pili, *Nyege ni kunyegezana* imeendeleza usemezano na imechangia zaidi mawazo kuhusu kinaya kilichowasilishwa kupitia kwa methali ya mwanzo. Kwa ambavyo methali hiyo i katika ubeti wa pili, imeshikilia pia nafasi muhimu katika kusawiri na kuendeleza ujumbe wa mshairi. Kupitia kwa methali hiyo, mshairi humtaka msomaji kubaini mizungu au hila zilizotumika dhidi ya Mwanamke. Mwanamume alipotumia kauli kwamba, *Mtu hakutupa, amfaapo mwenziwe* haimaanishi kuwa amezingatia hayo bali ni uzandiki tu.

Kwa kutumia methali ya pili, mshairi humtaka msomaji abainikiwe kwamba Mwanamke alikuwa karimu na alikuwa akimtendea Mwanamume wema wote aujuao kabla ya kugundua hila alizokuwa akitendewa. Kwa mfano, imetongolewa:

MWANAMKE
N'lishakupeleleza, hata n'kakubaini
Muda pesa ukijaza, humo mwako mfukoni
Huanza kujikimbiza, na kunigura nyumbani
Ngapita kukuuliza, uliko hujulikani (Ubeti wa 8)

Mwelekeo ambao umebainishwa kupitia kwa dondoo hilo, ulihusu mahusiano baina ya mhusika Mwanamume na Mwanamke. Kwamba, watu hustahili kutendewa wema kutokana na wema alioutenda. Kinyume na hayo, Mwanamume amekuwa akimwendea Mwanamke ili apewe *dawa* ambayo huweza kutumika kumpunga *shetani* aliyempaza kichwani. Baada ya Mwanamume kutendewa yote yaliyo mema alimwambaa Mwanamke. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, Mwanamke alikuwa akikumbukwa vyema siku zake za mwambo hapo mbeleni, alipokuwa akimtimizia kwa utu yote aliyohitaji bila ya kutarajia chochote. Jambo la kustaajabisha ni kwamba, Mwanamume alipokuwa na fedha mfukoni aliwaendea wanawake wengine mtaani ili astarehe nao.

Hapo mwanzoni, Mwanamke hakumfahamu vyema *mwendani* wake lakini katika pita pita zake mitaani, anagundua kuwa '*mwenziwe*' ana wanawake wengine ambao huiramba na kuifuta asali ya Mwanamume. Wanawake hao wa mitaani walipotanabahi kuwa kibindo kimesinyaa au kimenyauka, humwambaa na wala hawataki kumpunga *pepo* wake. Kutokana na matumizi ya methali, imepitishwa wazo kwamba, Mwanamke amebadili mwelekeo wake na kamwe hataki kuendelea kuishi katika kaburi alimokuwa. Kwa hivyo, pendo lake amelibana kwa yule asiye na utu, hisani wala imani. Kwa kubainisha zaidi mawazo hayo, mshairi amesema:

> *MWANAMKE*
> *Rudi kuko utokako, siniletee udhiya*
> *Tafutiya mwako wako, ndiya ya kuutoleya* (Ubeti wa 4)

Mishororo hiyo imeibuliwa kutokana na methali ya pili. Ujumbe ambao umepitishwa hapo ni ule uliomdhihirisha Mwanamke kama kiumbe kipya. Mwanamke huyo hataki tena kudanganywa kutokana na mbwembwe zilizotumika. Kadhalika, kupitia kwa

methali, mshairi ameweza kumsawiri Mwanamke kama mwenye msimamo dhabiti usiotetereka. Katika muktadha huo, itikadi na mwelekeo wa mshairi pia umefumbwa vilivyo katika methali hiyo. Kwamba, si vyema kujizuzua au kuendelea na mahusiano yaliyojengeka katika misingi ya hadaa. Kwa hivyo, mchomo wa mshairi kuhusu vitendo vya Mwanamume dhidi ya Mwanamke ndivyo vilivyoibuliwa na kuwasilishwa zaidi kupitia kwa methali. Aidha, hisi hizo zimedhihirishwa zaidi kupitia kwa malumbano ya wahusika hao. Kwa ambavyo Mwanamke tayari amezinduka, ameweza kujiopoa kutoka kwa mahusiano ambayo hayakujengwa katika msingi wa utu.

3.1.4.2.2 Methali kama Mbinu ya Kubainishia Mwelekeo wa Mshairi

Kutokana na matumizi ya methali, mshairi ameweza kubainisha zaidi mwelekeo na itikadi hiyo kuhusu maswala ya kijamii hususa, mahusiano baina ya Mwanamume na Mwanamke. Katika matumizi hayo ya methali, mshairi ameongezea kishazi kwamba *'kwangu huba zinkwisha'*. Matumizi hayo yamedhirisha kuwa, methali yenyewe haikutosheleza uwasilishaji wa hisi za mtunzi. Kwa hivyo, imembidi aongeze uziada huo katika kauli iliyotolewa. Isitoshe, methali imetiliwa nguvu kupitia kwa kauli zilizobuniwa na kutumiwa kwa makusudi. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli teule za kimapokeo huweza kufanyiwa marekebisho ambayo hayaathiri maana kusudiwa (Nagler 1967). Kadhalika, hisi na mwelekeo wa mshairi umewasilishwa kwa mwafaka zaidi kupitia kwa methali iliyofanyiwa marekebisho ya kiasi. Kwa mfano, Mwanamume amekuwa akipenda vitu vya bwerere huku yeye hayuko tayari kuwajibika. Mwelekeo uliowasilishwa ni kwamba, mwanajamii ambaye hana utu huweza kupuuzwa. Walipozua mahusiano, Mwanamke aliamini kuwa mwenziwe yu mwenye utu lakini hakuwa na

fedha za kumtumilia. Ni baada ya Mwanamke kutafiti ndipo aligundua kuwa Mwanamume alikuwa akimtumia yeye kama chombo cha kuzimulia ashiki. Kihisia, Mwanamke hakuwepo moyoni mwake. Ukweli ulipobainishwa, aliamua kusitisha kiungwana mahusiano hayo. Kupitia kwa methali hiyo, msomaji amejengewa ufunuo au mwelekeo na msimamo uliomhusu Mwanamke na wale ambao hunyanyaswa katika jamii. Katika harakati za kujenga na kubainisha zaidi msimamo wa Mwanamke, mshairi amesawiri:

MWANAMKE
Kila mambo naelewa, yaliyo ndiyo na siyo (Ubeti wa 7)

Kupitia kwa dondoo hilo, ubaya wa mja ulipobainika, ulimpotezea au utimlia doa heshima na staha yake. Kadhalika, kupitia kwa methali hiyo, mshairi ameweza kuitukuza hatua madhubuti iliyochukuliwa na Mwanamke. Katika muktadha huo, Mwanamke amesawiriwa kama mwenye utu na kwamba, katika maisha mja huweza kufanya makosa na pindi anapobaini kosa ni vyema kuchukua hatua mwafaka ya kujinusuru au kujiopoa. Msanii ameaendeleza wazo hilo, kwa kusema kuwa:

MWANAMUME
Amma um'badilika, hu tena kama zamani
Waniona nadhikika, hutaki kuniauni
Mwenziyo nataabika, hunionei imani?
Hufanyi hafariyika, hatowa pepo kutwani? (Ubeti wa 10)

Kupitia kwa dondoo hilo, mshairi amemwasilisha Mwanamume kama mja ambaye hutenda yasiyo utu. Kwa hivyo, hakupaswa kutarajia kutendewa yaliyo mema kutokana na mienendo hiyo ya ubinafsi. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, Mwanamke hakupaswa kuelekezewa kidole cha lawama kutokana na hatua aliyoichukua. Kwa

sababu, amekuwa amejitolea kwa hali na mali ili kudumisha mahusiano hayoo, lakini mwenzake alikuwa ameuficha ubinafsi ndani yake.

3.1.4.2.3 Uwasilishaji wa Maadili Kutokana na Methali

Matumizi ya methali yamelifanya shairi kuwa msingi wa kuwasilisha maadili kwa msomaji. Maudhui ya kimaadili yameshughulikiwa na wasanii mbalimbali katika uwanja huo, na hasa kupitia kwa mashairi wa kimapokeo. Kwa mfano shairi la 'Wema' (Mnyampala 1965:39-40), limesawiri kuwa:

Siyo wema usemaji, tenda wema ndiyo wema,
Mtu mwema hutaraji, kutenda lenye huduma,
Saliti ni mvunjaji; usukani wa huruma,
Kila atendaye wema ni adui ya saliti. (Ubeti wa 1)

Katika ubeti huo, mtunzi ameusifu wema na utu katika jamii. Kadhalika, katika shairi la 'Kutendana', mshairi amempa kauli hiyo mhusika Mwanamke ili msomaji kuweza kuupata funzo la kimaadili kupitia kwayo. Kwa mfano, hapo awali katika ubeti wa kwanza Mwanamume kumetumiwa kauli kwamba, *Mtu huwa hakutupa, amfaapo mwenziwe*. Kauli hiyo inapozingatiwa, huweza hudhirisha ukweli ambao ni wenye manufaa kwa jamii. Hata hivyo, matendo ya Mwanamume hayakuoana na mshabaha wa methali hiyo. Kutokana na maelezo yaliyotolewa, Mwanamume alikuwa akimkumbuka Mwanamke wakati alipokuwa amepagazwa kwa *pepo kitwani* ilihali hana chochote mfukoni. Kimsingi, mahusiano hayo yamekuwa hayana manufaa yoyote. Kwa ambavyo ni Mwanamke ambaye amekuwa akimpunga au akimtoa *pepo kitwani*, Mwanamume hakuchukulia kuwa mwenziwe alikuwa akifanya hivyo kwa heshima na kwa matarajio ya kutendewa vivyo hivyo.

Baada ya kugundua ujanja na uzandiki wa Mwanamume, Mwanamke aliamua kumnyima *dawa*. Kulingana na mawazo ya mshairi ni kwamba, pendo la dhati huchipuza na hushamiri pale ambapo pande mbili husika hushiriki kikamilifu katika kulikuza pendo hilo. Uhalisi wa mambo katika shairi ni kwamba, maswala ya mapenzi ya dhati hushirikisha pande mbili na wala haulekezwi upande mmoja. Wito ambao umetolewa ni kwamba, watu wawili ambao hushiriki mapenzi ya dhati hutegemeana na hukamilishana.

Shairi hilo linaposomwa, huweza kumbaini Mwanamume kama mwenye mielekeo ya kibinafsi ilihali Mwanamke amekuwa akimstahi na kumthamini. Mwanamke amekua akimchukulia Mwanamume kama mwenye utu ndio sababu ya kuamua kutomnyima *dawa* ya kumpunga *pepo kitwani*. Kutokana matumizi ya methali, mshairi ameweza kujenga mazingira ya kufafanua na kutoa mifano kemkem kuhusu ukarimu wa Mwanamke ilihali Mwanamume alikuwa akifikiria kuwa amepata pa kuutua mzigo wake au pa kula vya bwerere. Vitendo vya Mwanamke ni ithibati tosha ya utu alionao. Ni baada ya kusutwa ndipo Mwanamume ameelewa na amekiri kuwa amekuwa akimtendea unyama mwenziwe. Hata hivyo, Mwanamume haonekani kama mtu ambaye ametubu kwa dhati makosa au matendo aliyokuwa akiyatenda. Hiyo ndiyo sababu ya Mwanamke kutotaka kusikiliza uhodari wa uneni wa Mwanamume ili asije kujikuta tena ametumbukia katika shimo alimokuwemo. Kutokana na matumizi ya methali, mtunzi ameweza pia kuukemea na kuupiga vita ulaghai wa Mwanamume. Kama Mwanamume angekuwa mtu aliyestahi utu wa Mwanamke angekuwa akikumbuka, kila wakati, utu na ukarimu aliokuwa akitendewa.

Kulingana na nasaha zilizotolewa, mtu huweza kuwa hana kitu na ikawa imechuliwa vivyo hivyo, lakini Mwanamune alipokuwa nacho hakuwa akimkumbuka yule alikuwa akimfaa wakati wa shida au dhiki. Jambo hilo si jema kutendewa mtu. Kwa sababu, huweza kuzua uhasama wa kimahusiano katika jamii. Kwa ambavyo, Mwanamume alikuwa mwenye mazoea hayo; Mwanamke amechoka na ameamua kusitisha mara moja mahusiano yao. Kwa hivyo, amekuwa akimhangaikia mno Mwanamume hadi kiwango cha kunadi vito na vyombo vyake vya muhimu ilimradi mwenziwe asipate dhiki. Jambo hilo limedhihirisha kupitia kwa maelezo yafuatayo:

MWANAMKE
Fadhila ungekumbuka, hayano usingenena
Kwako mno 'mesumbuka, tena kwa kila namna
Nikawa nakueleka, kana kwamba mbwangu mwana
Hayo usingetamka, lau wajua maana (Ubeti wa 23)

Kulingana hoja katika dondoo hilo, Mwanamke hakufanya makosa, kwa vile hakujua uhalisi wa mambo. Vile vile, ni makosa kwa mtu kutumia hila kumlaghai mwenzake katika jamii. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, mhusika Mwanamume alipokuwa amepata fedha, labda kwa kumhadaa Mwanamke, aliwaendea changu doa katika mitaa na vilabu vya starehe. Hata hivyo, Mwanamke amesawiriwa kama mtu ambaye tayari amezinduka na katu hataki kuendelea kujizika na kupumbazika kwa mahusiano hayo ya awali. Kwa hivyo, kupitia kwa methali, mshairi humtaka msomaji awe mweledi na mwangalifu ili ajiepushe na matendo ya kilaghai na ya kizandiki katika jamii.

3.1.4.2.4 Methali kama Msingi wa Kusawiri Mahusiano ya Wahusika

Shairi hili ni la kitengo cha malumbalo na lenye kuhusisha wahusika wawili muhimu: Mwanamume na Mwanamke katika uwasilishaji wa ujumbe. Kadhalika, mshairi

ametumia methali hiyo ya *Nyege ni kunyegezana* kama msingi wa kusawiri na kubainisha mahusiano ya wahusika hao. Kutokana na maelezo yaliyotolewa, mahusiano ya wahusika hao hayakujengwa katika misingi ya utu. Ni bayana Mwanamke alikuwa mwenye utu usiotetereka na alimpenda Mwanamume kwa dhati. Mwanamume kwa upande wake alielewa hayo, lakini kwa makusudi alitumia ulaghai na ubinafsi ili kuweza kujinufaisha. Haukupita muda mrefu, Mwanamke alitilia shaka mahusiano hayo na nyendo za Mwanamume. Hiyo ndiyo sababu ya kuamua kufanya utafiti ili aweze kufahamu mbichi na mbivu. Kwa hivyo, mekaririwa kuwa: *N'lishakupeleleza, hata n'kakubaini.*

Zaidi ya hayo, Mwanamke aliamua kumsubiri 'mwenzi' wake nyumbani kwake ili atakapofika ampashe ukweli mchungu. Mwanamke amesawiriwa kama mwenye utu na amezingatia subira. Mwanamume alipowasili kwa Mwanamke wakati amepandwa kwa *shetani* huku hana chochote mfukoni, hapati makaribisho ya ukarimu na bashasha kama ilivyokuwa mazoea. Mwanamke hakupoteza muda ila aliweza kumpasha ukweli kuwa *nyonda* zake zimemwisha. Kwa sababu, *Nyege ni kunyegezana* na vinginevyo sivyo. Ni kutokana na matumizi ya methali hiyo ndipo mshairi ameweza kumfafanulia zaidi msomaji wa shairi kuhusu malumbano muhimu yaliyojiri baina ya Mwanamume na Mwanamke. Kadhalika, ni kupitia kwa methali ndipo imeweza kufafanuliwa kuhusu kiini cha kuporomoka na kusambaratika kwa mahusiano hayo. Vile vile, matumizi hayo yaliyotolewa yamesaidia katika kubainisha na kufahamisha zaidi kuhusu nyendo hasi za Mwanamume na utu alionao Mwanamke.

3.1.4.3.1 Mjinga 'Meerevuka, Mwerevu u Mashakani

Methali hiyo imetumiwa kwenye ubeti wa kumi na tatu katika shairi hili. Maana iliyoibuliwa katika methali hiyo ni kwamba, mtu ambaye alikuwa akichukuliwa kuwa haelewi; sasa hufahamu. Kwa hivyo, yeye na yule aliyekuwa akijifanya mjuzi au mjuaji wako katika kiwango sawa au zaidi. Katika uwasilishaji wa shairi, mwerevu amejipata kuwa hakuweza kuthaminiwa kama ilivyokuwa hapo awali.

3.1.4.3.1 Uwasilishaji na Uibuaji wa Isitiari Kutokana na Methali

Matumizi ya methali hiyo umeyafanya mawazo kuwasilishwa na kufafanuliwa kiisitiari. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, kauli ambazo huibua isitiari huutajirisha zaidi utungo kwa upande wa uchambuzi (Hedley 1998 na Eco 1976). Isitoshe, hizo ni kauli ambazo hutumiwa katika uwasilishaji, huutafakarisha na huuwasilisha ujumbe kitaswira (Steen 1974). Katika utungo huu, methali huweza kufasirika kama isitiari ambapo maana hiyo hubainika zaidi katika uhalisi na utamaduni wa jamii. Kadhalika, mhusika Mwanamke amesawiriwa kama mtu aliyeghilibiwa kwa hila. Kwa upande wa Mwanamume, alikuwa akimchukulia Mwanamke kama mtu ambaye hana hisia na aliyeweza kuhadaiwa kwa urahisi. Kwa mfano imesawiriwa kuwa:

MWANAMUME
Zako sijaziafiki, jawabu za ukaidi
Ungazijibu sichoki, na wala nyuma sirudi
Kwa sababu n'na dhiki, nami kwako sina budi
Ni kweli kwamba hutaki, au ni yako inadi (Ubeti wa 16)

Kutokana na maelezo katika dondoo hilo, Mwanamke amekuwa mwenye utu na karimu kwa mwenzake hata ingawa uwezo wake ulikuwa kichele. Kwa hivyo, Mwanamume alipokuwa akisumbuliwa au akipandwa na *shetani* wa ashiki huku akiwa hana kitu

kibindoni, kimbilio la maliwazo lilikuwa kwa Mwanamke. Kitendo hicho kimekuwa kikifanywa kama ibada. Kwa sababu, alielewa kuwa atapewa *dawa* bila pingamizi yoyote. Kwa sababu ya wema uliomsukuma Mwanamke; amekuwa kiguu na njia ili akope au awekeshe rehani na kunadi vito vyake, ilimradi 'mwenzi' wake asipate shida moyoni. Katika kushadidia wazo hilo, imetongolewa kuwa:

MWANAMKE
Vyombo vya thamani tosha, rehani nikaviweka
Kimoja sikubakisha, dhahabu na kadhalika
Vyote n'kavisozesha, upate kusitirika
Vipi wanambiya kisha, tamaa innishika? (Ubeti wa 48)

Hayo yote, Mwanamke alikuwa akiyafanya ili mahusiano yao yaweze kuimarika. Hata hivyo, Mwanamke hakujua ujanja uliokuwa umejificha moyoni mwa mwenzake.

Kimsingi, Mwanamke hakuwa mjinga kama alivyofikiriwa au kudhaniwa na Mwanamume. Kwa sababu, Mwanamke hakutaka kutoa kauli za uvumi bila ya kuwa na ithibati mwafaka. Kutokana na usumbufu mwingi moyoni, ameamua kuzunguka huku na huko mitaani na vilabuni ili auzumbue mbichi na mbinu. Pilika pilika zake mitaani, zilizaa matunda na amebaini kuwa alimtumia yeye kama nyenzo ya kudumisha anasa na starehe hiyo vilabuni na mitaani. Baada ya kubaini uzandiki na ujanja uliotumiwa, ameamua kusitisha mahusiano hayoo na kumpasha mwenziwe ukweli uliostahili. Kwa hivyo, Mwanamke amechukua hatua hiyo ya kuibana *dawa* ya kumpunga *shetani* wa Mwanamume. Aidha, shetani huyo aliendelea kumsakama na kumtesa.

Kutokana na matumizi ya methali, imejengwa mazingira ya utafakari zaidi kuhusu jinsi Mwanamume alivyoathirika kutokana na vikwazo alivyowekewa. Ingawa mshairi

amezungumzia kuhusu mahusiano ya kimapenzi, kuna uwezekano kwamba maswala hayo huweza kueleweka na kufafanuliwa zaidi kwa kuzingatia maswala nyeti ya kijamii. Kwa mfano, msomaji huweza kutanua zaidi ufahamu kwa kuzingatia pia umuhimu wa mwanamke kwa mwanamume kama wanajamii wenzake. Katika muktadha uliojengwa katika shairi, Mwanamke alikuwa akitumiwa kama chombo bila kufahamu. Kwa hivyo, hakuwa mwelewa wa mambo hapo mwanzoni, lakini alipoelewa vitimbi hivyo; aliamua kubadili mawazo ya awali. Katika makabiliano hayo, Mwanamke alijifananisha na *nyuki* aliyejua makali aliyonayo au aliyechokozwa ambapo hana budi kuuma. Mwanamume naye alijifanya mjuaji, lakini ujanja wake uligota ukingoni baada ya ukweli kujulikana. Kwa hivyo, methali iliyotumiwa ilikuwa msingi wa kuelewa undani wa ujumbe ulioibuliwa kiisitiari.

3.1.4.3.2 Uundaji wa Taharuki Kutokana na Matumizi ya Methali

Matumizi ya methali ya 'Mjinga 'meerevuka, mwerevu umashakani', imesaidia katika kuwasilishia ujumbe kwa kujenga mazingira ya kuichochea na kuidhibiti hamu ya msomaji kutaka kuendelea zaidi kulisoma kwa tuo shairi. Kama ilivyoelezwa hapo awali kuwa, kabla ya kujitokeza kwa methali hiyo, mshairi tayari alikuwa ametumia methali nyingine mbili za msingi. Methali hizo za awali ni: *Mtu huwa hakutupa amfaapo mwenziye* na *Nyege ni Kunyegezana*. Methali hizo mbili za awali hazipaswi kudunishwa, kwa ambavyo ni mhimili muhimu katika kusawiri na kuwasilishia mawazo. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli msingi huchangiana na hukamilishana katika uwasilishaji wa ujumbe kwenye utungo (Whallon 1969). Hata hivyo, kauli hizo

zimetumiwa kiawamu ambapo kila moja imekuwa ni mbinu ya kueendeleza kipengele fulani cha hoja kilichowasilishwa katika shairi.

Kwa kutumia methali ya tatu ya *Mjinga 'meerevuka, mwerevu u mashakani*, mtunzi amepata fursa ya kufaragua na kuwasilisha mawazo mengine mapya ambayo huenda hakuyagusia hapo awali. Kwa mfano, hapo awali Mwanamke alikuwa akizunguka huko na huko ili mwenzi wake apate alichokitaka. Kadhalika aliyafanya hayo, kwa ambavyo hakuelewa mwelekeo wa *mwenzi* wake. Kwa wakati huo, Mwanamke ni kiumbe kipya ambaye amebadilika, si kama yule wa awali bali amezinduka, yaani ameerevuka kutokana na yale aliyoshuhudia na aliyoapata mitaani na vilabuni. Aidha, ni Mwanamume ambaye amejipata taabani kwa mwako wake wa ashiki ambao hautulizwi kwa *dawa* tarajiwa. Kwa sababu hiyo, hamu ya msomaji huchochewa na kudhibitiwa ili kutaka kuelewa zaidi kuhusu hatima ya mahusiano baina ya Mwanamke na Mwanamume.

Vile vile, kwa kutumia methali hiyo, mkondo wa uwasilishaji na athari ya mawazo yalichukua mwelekeo mwingine. Kwa mfano, mshairi ameweza kufafanua na kujibu baadhi ya maswali ambayo yaliibuliwa kwa matumizi ya methali hiyo. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, Mwanamke tayari hataki tena usuhuba na Mwamamume. Maswali ya msingi ambayo huweza kuibuka ni kama vile:

- Kwa nini Mwanamke hakutaka kuendelea na mahusiano hayo?
- Hatima ya Mwanamume kunyimwa dawa ni nini?

Kwa hivyo, muktadha wa mahusiano ya hapo awali yamebainishwa kupitia kwa ubeti ufuatao:

MWANAMUME
Tushakaa wewe nami, kwa siku tumbi nzima
Sijainua ulimi, kukueneza lawama
Baya kwako silisemi, la kukuudhi mtima
Bali hayano hamami, ya leo yannitoma (Ubeti wa 18)

Hata hivyo, Mwanamke hataki kabisa kujiingiza tena katika mtego wa Mwanamume ambaye alimdhikisha na alimzubaisha kwa muda mrefu hapo awali. Kutokana na matumizi ya methali hiyo, mshairi ameweza kuendeleza na kukuza kauli za wahusika hao wawili. Msomaji naye huweza kuupata ufunuo zaidi wa mkondo wa mahusiano baina ya Mwanamke na Mwanamume. Kwa mfano, Mwanamke amebainisha kwa uchungu dhiki alizozipitia hapo awali alipokuwa katika mahusiano bandia ya kimahaba. Hali hiyo, imedhihirishwa kupitia kwa kauli ya Mwanamke kuwa:

Mato unnifumbuwa, ya wazi sasa yaona
Hili kaa ukijuwa, kwako huba sina tena
Mizizi n'shangowa, hayawezi shikamana
Uwate kujisumbuwa, mi nawe tushatokana (Ubeti wa 24)

Kupitia kwa ubeti huo, msomaji huweza kujiuliza: Ni mambo gani yaliyokuwa yakimfumba macho Mwanamke? Katika mazingira hayo, msomaji hutarajia ufumbuzi zaidi kuhusu kadhia hiyo. Baadhi ya matatizo ambayo Mwanamke aliyoyapitia ni kama: kuzunguka huku na huko akibadilisha *duka baada ya duka* ili akopeshwe na; kufikishwa mbele ya *mashitaka* baada ya kushindwa kulipia madeni hayo. Kadhalika, Mwanamke aliweka rahani na kuuza vyombo vyake vya thamani kama vile *dhahabu* ili kuuridhisha na kuupoza moyo wa Mwanamume asiye utu. Kwa hivyo, matumizi ya methali yameweza kusaidia katika kujenga taharuki ya kulisoma shairi zima. Hali hiyo ya

taharuki imedhibitiwa zaidi kupitia methali ya nne ambayo ni: *Yalopita yashapita, si vyema kuyaregeza.*

3.1.4.3.3 Methali kama Mbinu ya Kujengea Viona Nyuma na Mbele

Kupitia kwa methali, mshairi ameweza kubulia uhalisia wa mambo yaliyopita katika mahusiano baina ya Mwanamke na Mwanamume. Kwa hivyo, mtunzi ametumia methali ya kwanza na ya pili ili msomaji kuweza kujifahamisha zaidi na mambo ya awali ambayo yamesababisha msukosuko huo katika mahusiano baina ya Mwanamke na Mwanamume. Kutokana na matumizi ya methali ya tatu ambayo ni: *Mjinga 'meerevuka, mwerevu u mashakani*, msomaji huweza kuchochewa zaidi kujiuliza baadhi ya maswali ya msingi kama vile:

- Kwa nini Mwanamke amejichukulia kuwa alikuwa *mjinga* hapo mwanzoni na sasa ni mwerevu?
- Kwa nini Mwanamume alikuwa *mwerevu* hapo awali na sasa ni *mjinga*?
- Wahusika hawa wawili walikuwa wenye mahusiano ya aina gani hapo awali?
- Kwa nini Mwanamke amechukua hatua ya dharura ya kusitisha mahusiano hayo kwa wakati huo?

Kadhalika, msomaji huweza kuzingatia uhalisi wa mambo yaliyomfanya Mwanamke kubadili nyendo za hapo awali. Kwa mfano, Mwanamke alikuwa akijitahidi kwa hali na mali ili kuhakikisha kuwa mahusiano hayo na Mwanamume yametengenea na yameimarika. Aidha, Mwanamke alikuwa yu radhi kuuza au kuwekeza rehani vyombo au raslimali aliyonayo ili 'mwenzi' wake aliwazike moyoni. Mambo hayo aliyokuwa

akiyafanya Mwanamke humdhihirisha kuwa karimu kwa mali aliyokuwa nayo na wala hakubakisha chochote ilimradi *mwenzi* wake hapati shida ya matumizi.

Mwanamume alipokitia kibindoni alichokichuma kutoka kwake, alikuwa akiwaendea wanawake wengine mitaani ili kuweza kujionyesha na kujishauwa kwa kustarehe nao. Katika fikira za Mwanamume alifurahia mno ujanja aliokuwa akiutumia kupata alichokitaka kutoka kwa Mwanamke. Kwa upande mwingine, Mwanamume alikuwa zuzu na wala hakuelewa kuwa wanawake hao wa mitaa walichotaka ni fedha alizokuwa nazo tu. Kupitia kwa methali hiyo, imejengwa mazingira ya kumhurumia Mwanamke ambaye alikuwa hajui kuwa 'mwenzi' wake alikuwa akitumia uzandiki na hadaa tupu. Kwamba, Mwanamke alikuwa akipumbazika huku mwenzake akipata nafasi ya kujitoma katika starehe na anasa kutokana na ukarimu alioupata.

Taswira ambayo imetokana na methali ilihusu Mwanamke alikuwa akitumiwa kama chombo ili kukidhi haja za kibinafsi za Mwanamume. Mahusiano ya awali baina ya Mwanamke na Mwanamume huweza kueleweka kwa kuzingatia methali iliyotumiwa katika kuibulia maelezo ya msingi yaliyotolewa katika shairi. Kwa mfano, msomaji huweza kufahamikiwa kuwa Mwanamke alijiingiza katika mahusiano hayo kwa nia njema lakini hakumwelewa fika 'mwenzi' wake. Aidha, maswali ambayo msomaji huweza kujiuliza ni kama yafuatayo:

- Mwanamke alipozinduka alichukua hatua gani?
- Mwanamume ameathirika kiasi gani kutokana na kuvunjika kwa mahusiano hayo na Mwanamke?

Mathalani, Mwanamke alipobaini kuwa alikuwa akichezewa shere, aliamua kusitisha mara moja mahusiano hayo. Kutokana na hali hiyo, Mwanamume amekuwa taabani kwa sababu *shetani* wake hapungwi na anasa hiyo mitaani imefikia ukingoni. Kwa kutumia methali, mshairi amepata nafasi ya kufahamisha kuwa, ni muhimu kuzingatia kila wakati; mahusiano baina ya Mwanamke na Mwanamume. Kwa kuzingatia hayo, hadhira huweza kubainishwa sababu za msingi zilizolisambaratisha uhusiano huo. Katika muktadha huo, isichukuliwe kuwa ukariri wa methali zaidi moja haina maana. Umuhimu wa kuitumia methali hiyo ni kuuendeleza zaidi ujumbe uliowasilishwa ili kuweza kusaki katika akili na tafakuri ya hadhira.

3.1.4.3.4 Methali kama Msingi wa Ujenzi wa Muundo

Kwa ambavyo, methali ni kauli ambayo imekamilika na imejisimamia, imetumika mahususi katika ujenzi wa kibwagizo kwenye ubeti wa kumi na tatu wa shairi. Kwa kuzingatia methali hiyo kama kibwagizo, mshairi ameweza kupata kwa urahisi mizani kumi na sita zilizohitajika katika muundo wa kila mshororo kwenye ubeti. Upatanisho wa urari wa vina katika ubeti huo pia umekamilika. Methali yenyewe imechukuliwa jinsi ilivyo na kuchopekwa kwa makusudi katika uundaji wa mshororo bila ya kufanyiwa marekebisho yoyote.

Katika uwasilishaji wa shairi, methali zote nne zimetumiwa kama kibwagizo. Kwa hivyo, mishororo iliyoibuliwa katika beti hizo mahususi imeafiki muundo wa methali zilizopo. Isitoshe, vina vimebadilika katika beti za shairi kutokana na uelekezo wa methali isipokuwa idadi ya mizani katika mishororo imedumishwa kwenye utungo.

Kimsingi, vina vya kati na vya mwisho katika mishororo ya awali huwa vimefanana. Kimuundo, jambo hilo huruhusiwa isipokuwa katika mshororo wa mwisho, ambapo kibwagizo huweza ama kuwa na kina kilichofanana au kilichotofautiana.

3.1.4.3.5 Methali kama Chombo cha Kubainishia Uzindushi wa Mwanamke

Mshairi ametumia methali kama msingi wa kudhihirisha uzindushi wa Mwanamke dhidi ya Mwanamume ambaye amekuwa akimlaghai na kumtesa kimawazo. Kwa mfano, *MWANAMUME* amekuwa akidhihirisha udanganyifu wake kwa kusema:

Kama bure utanipa, nipa sinisumbuliye
Kama hutaki 'takopa, nikulipe baadaye
Hivi sasa cha kukupa sina; kweli ni kwambiye
Mtu huwa hakutupa, amfaapo mwenziye (Ubeti wa 1)

Kwa kuzingatia ubeti huo, mshairi umebainisha ujanja ambao baadhi ya wanaume katika jamii wanaoutumia kama chambo. Kwa hivyo, methali iliyotumika imesaidia kuelewa mwelekeo wa Mwanamume kama tabaka nyanyasaji lisiloweza kutegemewa katika jamii. Kupitia kwa maelezo yaliyotolewa, Mwanamke alikuwa akimkidhia Mwanamume yote aliyohitaji bila ya kuuliza swali. Kwa sababu, hakuwa ameelewa hasa nia ya 'mwenzi' wake. Mwanamke alipogundua kuwa Mwanamume alikuwa kimtumia kama chombo cha kuzimua ashiki zake, aliamua kusitisha mahusiano hayo mara moja. Kwa hivyo, MWANAMKE amedhihirisha kimako chake kwa kusema:

'Sina' kila siku 'sina', 'sina' kwako i maisha
Huna siku utanena: ninacho 'kanirambisha?
Hiyo 'sina' yako Bwana, sasa ishanichokesha
Nyege ni kunyegezana, kwangu huba zinkwisha (Ubeti 2)

Katika dondoo hilo na hasa kupitia kwa methali iliyotumika, Mwanamke amebainishwa kuwa ni mwelewa na aliyestahili kupigiwa mfano katika jamii. Kwa sababu, tayari amebaini ujanja, kama ilivyoelezwa kupitia kwa kauli za Mwanamume katika ubeti wa kwanza. Baada ya kuelewa kwamba nyendo na hila zilizotumiwa zimegunduliwa, Mwanamume ametumia kauli mbalimbali za kumpembeja na kumrai Mwanamke. Kutokana na maelezo yaliyotolewa, Mwanamume ameambulia patupu. Hiyo imetokana na jinsi Mwanamke alivyokataa katakata kutumiwa kama chombo. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, Mwanamke ni sawa na mwanamume. Kwamba, hapo mbeleni Mwanamume alijichukulia kuwa mjanja lakini mbinu zilizokuwa zikitumiwa zilifahamika. Katika muktadha huo, MWANAMKE amekariri kuwa:

Usemayo ni hakika, si urongo aswilani
Ni kwa kuwa mmachoka, kukufanya muhisani
Ndipo n'kabadilika, hakutowa maanani
Mjinga 'meerevuka, mwerevu u mashakani (Ubeti wa 13)

Kupitia kwa matumizi ya methali hiyo, Mwanamke amekuwa akiitetea haki hiyo. Kwamba, katu hataweza kughilibiwa kwa janja za Mwanamume. Kwa kutumia methali, mshairi ameweza kubainisha kuwa, hatua iliyochukuliwa na Mwanamke ndiyo mwafaka zaidi kwa mtu mwenye utu. Mshairi haoni sababu ya kumfanya Mwanamke kuendelea na usububa ambao haumfaidi kwa njia yoyote ile. Kwa hivyo, amejenga mazingira ya kufamisha kuwa Mwanamke huyo amezinduka na tayari amekata kauli ya kusitisha mahusiano hayo ili asiweze kuendelea kuishi katika maisha ya kudanganywa kwa hila za Mwanamume.

Msimamo na mwelekeo ambao umedhihirishwa kupitia kwa methali ya nne ni kwamba; ni vyema kusahau yaliyopita na kuandama yaliyopo na yajayo badala ya kujisononesha na kujidhalilisha kutokana na yale yaliyokuwa yakimwathiri wakati uliopita. Kwa njia hiyo, Mwanamke amekuwa mwenye mwelekeo wenye matumaini makubwa katika maisha ya usoni. Wazo hilo limedhihirishwa pia kupitia kwa *MAELEZO* ya mtunzi, kuwa Mwanamume:

> *Tamaa hakuikata, akazidi bembeleza*
> *Akasema yalopita, ni bora kuyanyamaza*
> *Kuliko kuyafuwata, na kisasi kulipiza*
> *Yaliyopita yashapita, si vyema kuyaregeza* (Ubeti 97)

Hoja ambayo imepitishwa katika ubeti huo ni ya msingi, kwa kuwa imemdhihirisha Mwanamke kama mtu mwenye mwelekeo mwafaka na akili iliyotuama. Kwamba, hakuna haja ya kujidhikisha kwa yale yaliyopita. Kwa hivyo, msimamo wa kusitisha mahusiano hayo na Mwanamume ndiyo uliotumika kufafanua zaidi na kuwasilisha mwelekeo wa mshairi.

3.2 UCHANGANUZI WA USHAIRI WA K.H.A. AKILIMALI SNOW-WHITE: *USANIFU WA USHAIRI*

Diwani ya *Usanifu wa Ushairi* ilitungwa na ilichapishwa mwaka wa 1974 na Shirika la East Africa Literature Bureau. Diwani hii, ina jumla ya mashairi mia moja arobaini na moja. Ingawa mashairi hayo ni mengi, ni manne tu ndiyo yaliyochanganuliwa katika utafiti huu. Mashairi hayo ni:

i. Subira

ii. Alie kwenda kaenda

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

iii. Mganga Hatajiganga

iv. Umoja ni Ngome kuu

3.2.1 Shairi: Subira

Shairi hili ni la muundo wa tarbia na lina jumla ya beti saba. Katika uwasilishaji wake imetumika methali moja: *Subira huleta heri* ambayo imejitokeza katika ubeti wa awali hususa, mshororo wa tatu. Kadhalika, imejitokeza kama sehemu ya mshororo yaani, utao. Ingawa ni methali moja imetumika, mshairi ameweza kutimiza mambo mbalimbali katika utunzi na uwasilishaji kama ilivyoelezwa hapa.

3.2.1.1 Methali kama Dira Katika Utunzi na Uwasilishaji wa Mawazo

Mshairi ametumia methali hiyo ya *subira huleta heri* kama kichocheo cha kufafanulia na kuwasilisha mawazo katika utungo. Kwa kawaida, mshairi huwa ana mchomo au hisi ambazo angependa kuzisawiri na kuziwasilisha kwa hadhira. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, hisi ambazo huwailishwa hutokana na uhalisi wa mazingira na tajiriba za watu kuhusu maisha (Propp 1968). Kwa sababu hiyo, mshairi hupata ilihamu na msukumo wa kutunga na kuwasilisha hisi na mawazo kwa uelekezo wa methali iliyoteuliwa. Kwa hivyo, mawazo ambayo yamewasilishwa huwa yamejikita au yaweza kufafanuliwa katika muktadha wa kauli msingi ambayo ni, methali ya *subira huleta heri.* Hiyo ndiyo sababu ya shairi kupewa anwani ya *subira.* Kwa kutumia anwani hiyo, msomaji huweza kufahamu muktadha wa mawazo yaliyonuiwa kuibuliwa na kuwasilishwa katika shairi.

Kadhalika, mshairi hakuona haja ya kulipa shairi hili anwani ya methali kwa ukamilifu wake. Kwa vile huelewa kwamba, ndani ya shairi hilo hana budi kutumia methali hiyo kwa ukamilifu na kuitolea maelezo yaliyohitajika. Kama anwani, dhana ya 'subira' imetumiwa kama nyenzo ya kumdokezea msomaji kuhusu mawazo ambayo hutarajiwa kuwasilishwa. Katika muktadha huo, mshairi hapotezi muda wala kumkaviza msomaji kuhusu maswala ambayo yalipaswa kupewa kipaumbele. Aidha, kwa kutumia kidokezi cha methali ameweza kubainisha mwelekeo na mkondo wa mawazo yaliyopo. Kwa hivyo, uteuzi na matumizi ya methali yamewezesha kujenga msingi mwafaka wa kufafanua mawazo na mchomo wa hisi zilizomsakama msanii. Kwa mfano, ameona si vyema mtu kuwa na papara katika maisha hata kama jambo ambalo hutaka kulitimiza linamwathiri au kumuuma kiasi gani. Katika kudhihirisha wazo hilo, amesema:

Subira ni kitu chema, mwanadamu subiri,
Japo jambo la kuuma, na moyo walikasiri,
Subira ni kitu chema, subira huleta heri
Subira ni kitu chema, mwanadamu subiri (Ubeti wa 1)

Kwa kutumia methali iliyopatikana katika ubeti huo, mshairi amejenga mazingira ya kufahamu kuwa jambo ambalo hutendwa kwa haraka huwa halifanywi kwa utaratibu uliostahili. Kwa sababu, mtu ambaye huwa mwenye papara au haraka katika maisha hatadiriki kula tamu. Kwa hivyo, *Haraka itakunyima, mambo yaliyo mazuri* (Ubeti wa 2).

Kadhalika kwa kutumia methali, mshairi ameweza kufafanua zaidi dhima au utendakazi wa subira katika maisha ya watu katika jamii. Mfano ambao uliozingatiwa ni wa mtu ambaye hana *subira* alipoalikwa katika hafla au sherehe, alianza kujidhalilisha kwa

kufakamia vyakula visivyo vya muhimu. Katika kufafanua zaidi umuhimu wa *subira*, imetongolewa kuwa:

> *Subira ni kitu chema, mwanadamu subiri*
> *Kwa pupa huwezi chuma, au hajazo kujiri*
> *Mwenye pupa hali vyema, vinono au vizuri*
> *Subira ni kitu chema, mwanadamu subiri* (Ubeti wa 3)

Muktadha ambao umeibuliwa katika ubeti huo ni ule wa ulafi ambapo vyakula mahususi vilipoletwa kwa wageni, mtu huyo hatakuwa na nafasi baki tumboni. Kwa hivyo, kwa kutumia methali hiyo, mshairi ameweza pia kufaragua na kuelezea zaidi hoja zake kwa kutoa mifano mwafaka iliyo dhahiri katika jamii kuwa msingi wa kuthibitishia mawazo yaliyowasilishwa. Hiyo ndiyo sababu ya kutoa mifano kemkem iliyojikita katika mapisi ya jamii kwamba: watu ambao walitenda mambo yao bila haraka ndiyo sasa hula tamu na wenye *heshima* katika jamii.

Kutokana na matumizi ya methali hiyo, mshairi ametoa ushauri kwa baadhi ya watu ambao hutaka *kujiua kwa ari* au wamekata tamaa na kufadhaika kwa vile hawajafanikiwa katika maisha. Kwa sababu, kila kitu kina wakati wake na wakati wao wa kufanikiwa bado haujawadia. Kulingana na maelezo yaliyotolewa ni kwamba, wanajamii hawahitaji kujiingiza katika jaka au hangaiko la moyo kwa sababu ya kukosa. Kilicho cha muhimu ni uzima na *Mungu* ni mwenye uwezo wa kuwarehemu na kuwaneemesha pindi wakati unapowadia.

Kadhalika, mshairi ameweza kubainisha mwelekeo kwamba: mambo ya mwanadamu huwa hayafanikishwi kwa kutumia maguvu au kulazimishwa. Aidha, kupata na kukosa

ni kawaida na hutegemea utashi wa Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, matumizi ya methali yamesaidia katika kufaragulia na kuwasilishia mawazo ya msingi katika shairi.

3.2.1.2 Methali kama Msingi wa Kubainishia Falsafa na Itikadi ya Mshairi

Kwa kutumia methali, mshairi ameweza kubainisha kwa uwazi imani na mwelekeo alionao kuhusu *subira* katika jamii. Msomaji anapolidurusu shairi na kufikia pale ambapo methali ilipotumika, huweza kupata fununu kwamba: mshairi hajapendezwa na mielekeo ya baadhi ya watu ambao hutaka mambo yao kutendeka au kutimilika kwa haraka. Hapa ieleweke kuwa, mtunzi hupata kichocheo cha hoja ambazo huziwasilisha kupitia kwa yale aliyoyashuhudia katika jamii (Akporobaro 1994). Kwa hivyo, mshairi amewasilisha ujumbe wake kutokana na hisi au mwelekeo alionao. Kupitia kwa maelezo yaliyotokana na methali ni kwamba, mwanajamii ambaye hunufaika zaidi katika maisha ni yule mwenye akili iliyotuama au mwenye *subira.* Kadhalika, mwanajamii ambaye huendekeza zaidi papara au haraka huishilia kupata machungu katika maisha.

Kwa kufafanua zaidi ujumbe, imeelezwa kuwa mtu ambaye huheshimika zaidi katika jamii ni yule ambaye huzingatia *subira* katika utekelezaji wa mambo yake. Hiyo imetokana na sababu kwamba, mtu ambaye hana subira huwa mwenye wasiwasi na hufanya mambo hayo bila ya kuzingatia utaratibu unaofaa. Dosari ambayo hupatikana katika kutenda mambo haraka haraka, hukemewa na kukashifiwa na jamii. Jambo hilo pia limezungumziwa katika shairi la 'Intidhamu' (Mohamed 1980:38). Katika shairi hilo imesawiriwa kuwa:

Apendaye intidhamu hushika, huishika maalumu
Huwa yeye, enenda bila wahaka, huepuka na ugumu
Na mamboye, hakika hukamilika (Ubeti wa 3)

Kwa hivyo, kupitia kwa ubeti huo, mtunzi amemtaka mtu awe mwenye kupanga mambo vizuri bila ya haraka. Mawazo ambayo yameibuliwa na kuwasilishwa, yameafiki ya busara inayoibuliwa katika methali ya 'Subira huvuta heri'. Kwa sababu aliye makini huwa mwenye uhakika wa yale ambayo amezingatia.

Kulingana na maelezo ambayo yametolewa, si vyema mtu kukata tamaa kwa haraka bali ni vyema kuwa na moyo wa matumaini katika maisha kwa vile mipango ya Mungu haijulikani. Kwa hivyo, mshairi ametumia methali ili kupitisha ujumbe kwamba, kila mja ana wakati wake wa kufanikiwa na kama bado hajayashuhudia hayo, hupaswa kuwa na moyo wa kusubiri hadi pale atakapojaliwa na Mwenyezi Mungu. Majaliwa ambayo yamewasilishwa katika shairi hilo ni kinyume na mwelekeo uliochukuliwa na Abdalla (1973:69) katika shairi la *Zindukani.* Katika shairi lililozingatiwa, mshairi amehimiza jamii ichukue hatua ya kuboresha uchumi wao badala ya kusubiri majaliwa. Katika muktadha huo, washairi hao wamezungumzia swala la *subira* lakini kwa kuzingatia mielekeo tofauti tofauti. Mawazo hayo ni kwamba, wanajamii huhitaji kufanya kazi badala ya kuendekeza uzohali. Kadhalika katika shairi *subira*, mshairi huwataka watu wafanye kazi kwa makini na kwa uangalifu zaidi badala ya kutarajia mafanikio ya haraka katika maisha.

3.2.1.3 Uwasilishaji wa Maadili Kutokana na Methali

Mshairi alipotumia methali, amelifanya shairi kutoa mwelekezo na maadili katika jamii. Kadhalika, matumizi hayoe humfanya kuwa mwalimu na mwanafalsafa mwenye mtazamo pana kuhusu masuala ya maisha katika jamii. Zaidi ya kuibua hisi na kuburudisha au kuhuzunisha, shairi lina dhima ya kufunza miongozo mema katika jamii (Kuvuna, Mvati na Maliachi 1992:10 na Nabhany 1985:18). Kwa mfano, mtunzi haoni mwafaka wowote ambao huweza kutokana na kufanya mambo kwa papara katika maisha. Kimsingi, mtu mwenye subira, hufanikiwa kinyume na yule ambaye hutumia maguvu au kulazimisha mambo katika maisha.

Kutokana na tajiriba yake kuhusu maisha, mshairi huwaasa baadhi ya watu ambao hutaka kufanikisha mambo kwa kutumia kifua. Kwa mfano, imetongolewa kuwa:

Subira ni kitu chema, mwanadamu subiri
Falau upate homa, kukaa ukisubiri
Lika kuwa mzima, Mungu atakusitiri
Subira ni kitu chema, mwandamu subiri (Ubeti wa 6)

Katika ubeti huo, kumetumiwa neno *homa* kumaanisha shida au ugumu ambao huweza kumpata mtu. Kwa hivyo, zaidi ya kufanya papara ni kufahamu kuwa kuna mambo mengine ambayo ni muhimu katika maisha, kama vile afya. Katika muktadha wa uwasilishaji wa maadili, imetolewa ithibati ya baadhi ya wanajamii ambao wamefanikiwa na kuheshimiwa mno katika jamii kwa subira waliokuwa nayo. Kwa mfano, amesema kuwa watu hao ambao huzingatia *subira* ni *wenye heshima*. Kama mwalimu na mwanajamii, mshairi humtaka msomaji awe mwenye hadhari katika upangaji wa mambo hayo badala ya kutumia nguvu ili kulazimisha kwa haraka. Kwa mfano, imesailiwa

kwamba: kuna haja gani kwa mwanajamii kutumia papara ilihali hawezi kufanikisha mambo hayo vizuri katika maisha! Kwa kutumia methali, mshairi hapendi kuwaona baadhi ya watu katika jamii hiyo wakitatizika wakati suluhu ipo katika *subira.*

3.2.1.4 Methali kama Kichocheo cha Utafakari na Usaili

Mshairi ametumia methali hiyo kwa kwa makusudi ili iwe kichocheo cha kutafakarisha usomaji wa shairi. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, kauli au maneno teule ambayo hutumiwa katika mawasiliano ya jamii hujibainisha katika tamathali za usemi. Kwa hivyo, hizo ni dhana ambazo huhitaji kutolewa ufafanuzi kwa uzingativu wa utamaduni na tajiriba ya watu (Lackoff na Johnson 1980). Katika muktadha wa utungo, methali imetumika kama ishara iliyojengewa kisa. Kwa ambavyo hizo ni kauli teule na angavu, huweza kutambuliwa katika utungo. Mshairi ameitumia methali hiyo kwenye ubeti wa mwanzo, katika mshororo wa tatu kuwa kidokezo kamili cha kuchochea tafakuri ya msomaji.

Kadhalika, msomaji anapokumbana na methali hupiga bongo ili aweze kupata fasiri dhahiri kwanza, ndipo baadaye aweze kujiuliza sababu ya msingi ya kutumiwa kwayo. Katika muktadha huo, msomaji hushiriki siyo tu katika upokezi wa ujumbe bali pia katika kutafakari zaidi kuhusu umuhimu wa matumizi hayo katika uwasilishaji wa utungo. Kwa hivyo, imetumika mahususi kuwa mbinu ya kuuelekeza na kuuathiri mwendo wa uwasilishaji katika shairi. Kwamba, msomaji anapofikia kwenye matumizi hayo, husita kidogo au kwa kipindi kirefu ili ajipe fursa ya kutafakari mawazo amba yamewasilishwa. Kutokana na hali hiyo, mshairi ametoa kiliwazo cha kuudhibiti mwendo wa shairi na vile

vile kuukoleza zaidi ujumbe ambao umewasilishwa. Hiyo ndiyo sababu ya mshairi, kuamua kutumia ukariri wa makusudi kuhusu dhana ya *subira* aghalabu mara mbili katika kila ubeti. Endapo msomaji atapuuzia au atapitwa kwa maelezo ambayo yametolewa, bado hurejeshwa kwenye ujumbe ambao huwasilishwa kwa kuzingatia methali iliyotumika. Kwa kuzingatia methali hiyo, msomaji hupata chemichemi ambayo hujenga msingi wa ufafanuzi wa ujumbe ambao umewasilishwa.

3.2.2 Shairi: Alie Kwenda Kaenda

Shairi hili ni la muundo wa tarbia na lina jumla ya beti nane. Kadhalika, mtunzi ametumia methali moja mahususi: *Alie kwenda kaenda, si sawa na mja nyuma.* Sehemu ya awali ya methali imetumiwa kama anwani yaani *Alie kwenda kaenda.* Hata hivyo, methali imetumiwa kwa ukamilifu katika kibwagizo cha beti zote katika shairi. Kwa mfano, imetongolewa kuwa:

> *Alie kwenda hatuwa, si mwenzi si mshindani*
> *Midhali amenyanyuwa, mguu umo njiani*
> *Kwenda naye mwendo sawa, hili halipatikani*
> *Alie kwenda kaenda, si sawa na mja nyuma* (Ubeti wa 1)

3.2.2.1 Methali kama Kiunzi cha Utunzi na Uwasilishaji

Mshairi ametumia methali kama chanzo au msingi wa usawiri na uwasilishaji wa hisi kutokana na mchomo alionao na tajiriba yake katika maisha. Aidha, mshairi tayari ametunga hisi au mwelekeo fulani kuhusu nyendo za wanajamii. Kutokana na maelezo ambayo yametolewa, baadhi ya wanajamii ambao husitasita katika kufanya maamuzi ya msingi. Kadhalika, kuna wale ambao hufanya maamuzi na kuyatekeleza malengo au maamuzi hayo kivitendo mara moja. Kwa hivyo, mshairi amewawasilisha watu hao

wawili ambao wana mielekeo iliyotofautiana kuhusu utekelezaji wa maamuzi yao. Kwa mfano, imetongolewa kuwa:

> *Alie kwenda kaenda japo enda achechema,*
> *Japo ndege hakupanda, njia ameiandama,*
> *Mja nyuma hatashinda, japo tamfata hima,*
> *Alie kwenda kaenda, si sawa na mja nyuma* (Ubeti wa 2)

Kutokana mielekeo hiyo katika maisha, mshairi ameamua kuitumia methali hiyo kuwa mbinu ya kusawiri na kufafanulia mawazo. Mawazo yaliwasilishwa kupitia kwa methali, yamedhihirishwa kwa njia mbili: kama anwani na pia kama kibwagizo katika shairi. Kama anwani, imetumiwa sehemu ya kwanza ya methali na kama kibwagizo imetumiwa katika ukamilifu wake. Kwa kuzingatia sehemu ya mwanzo ya methali kama anwani, mshairi ameweza kudokezea kuhusu ujumbe uliotarajiwa. Kwa hivyo, methali ambayo imetumiwa imesaidia kumtayarisha msomaji kufahamu mkondo wa mwelekeo ambao umechukuliwa katika usawiri na uwasilishaji wa mawazo. Katika mkabala huo, mshairi amebainisha na amemrahisisha muktadha wa maswala ambayo yamezingatiwa.

Kadhalika, kama kibwagizo katika shairi: *Alie enda kaenda, si sawa na mja nyuma*, mshairi amejipa nafasi mwafaka ya kufaragua mawazo, mwelekezo wa hisi. Kwa njia hiyo, mshairi ameweza kupanga na kuwasilisha mawazo hayo kiawamu na kimantiki. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, hoja ambazo huwasilishwa hupaswa kujengewa mtiririko ufaao (Levi-Strauss 1955). Kwa kuzingatia utaratibu huo, shairi limefumwa kwa kujengewa muktadha wa kuupata ujumbe kwa urahisi. Kwa hivyo, mshairi humpiga makasia katika uwasilishaji wake kwa kuelezea kuwa mtu aliyefanya maamuzi na kuianza safari ya utekelezaji wa mradi wake si sawa na yule ambaye

hufuatia. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, watu hao wawili hawawezi katu kutembea kwa mwendo au hatua ambazo ni sawia; hata kama yule aliyetangulia alianza safari hiyo pole pole au kwa *kuchechema*. Kwa kuifafanua zaidi methali hiyo, ameelezwa kuwa *mja nyuma* hakuweza kumshinda yule *ambaye njia ameiandama*. Ijapokuwa *mja nyuma* amefika mwishoni mwa mkondo, amekuwa amechoka na hatakuwa na wasaa wa kupumzisha kiwiliwili chake. Kinyume na huyo aliyetangulia, amewahi kufika kule alikokuwa akienda na pia amepata wasaa wa kupumzisha akili na akili.

Kadhalika, mshairi amedhihirisha kuwa, maswala ya nani aliyefanya maamuzi mwafaka katika kuianza safari si jambo la mjadala. Kwa sababu, mwenye macho huweza kupambanua mbivu na mbichi. Sauti ya shime imetumiwa ili kudhihirishia hoja hiyo, kwamba:

> *Kutangulia ni hoja, kwa hili tusibishane,*
> *Mwanzo wa hesabu ni moja, ndipo uzipate nne* (Ubeti wa 4)

Endapo, watu hao wawili wamekutana njiani, huo hauwezi kutumika kuwa msingi wa kuwalinganisha. Kwa vile yule aliyetangulia, huwa amefika na yumo katika mapumziko. Aidha, aliyetangulia na kufika ukingoni mwa *safari* huwa na wakati wa kukabiliana na shughuli zingine za msingi ilihali *mja nyuma* huwa amefika huku akihema kwa machofu. Kutokana na matumizi ya methali, mshairi ameweza kuyasawiri na kuyafafanua zaidi mawazo. Kadhalika, maelezo na mifano hiyo imeibuliwa kutokana na matumizi ya methali ambayo imejenga uziada wa msingi ili umesaidia katika ufafanuzi wa ujumbe ambao umewasilishwa.

3.2.2.2 Uibushwaji wa Isitiari Kutokana na Methali

Matumizi ya methali yamelifanya shairi kuwasilishwa kiisitiari. Isitiari iliyoibuliwa, imechangia pakubwa taswira ya kimawazo iliyotumika. Kwa hivyo, mshairi alipoitumia methali katika uwasilishaji wa utungo, ameweza kujenga muktadha wa kuichochea akili na tafakuri ya msomaji. Matumizi hayo huweza kupanua zaidi mawazo ambayo yamewasilishwa kwa kuzingatia uhalisi na miktadha ya maisha katika jamii. Hiyo humaanisha kuwa, ujumbe wa msanii haudhihiriki tu katika utungo bali pia kwa kuzingatia upana wa uhalisi wa maisha katika (Momanyi 1998). Aidha, matumizi ya methali katika shairi huufanya uwasilishaji wake kuwa wenye uzito wa kimawazo na kimaono zaidi kuliko maneno ya kawaida yaliyotumika kama maelezo. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, kauli teule za kitamathali ambazo husaidia katika kubainisha umbuji wa msanii wa shairi ni zile zilizofumwa na kuwasilishwa kiisitiari (Jacobson 1960). Kwa hivyo, shairi ambalo huwasilishwa huwa lenye uzito wa kiuchambuzi, kiusaili na kiutafakari.

Aidha, msomaji huweza siyo tu kutunga picha ya wahusika wawili walisawiriwa bali pia kuzingatia kauli mahususi zilizotumika katika uwasilishaji wa utungo. Picha ya kimawazo ambayo imeibuliwa, imewasilisha maana ya kijuujuu ambayo hudhamiriwa kumshawishi msomaji kutafakari zaidi ujumbe wa msingi uliowasilishwa. Kwa njia hiyo, msomaji huweza kuibua miktadha mingine ya kijamii ambayo huweza kupatanishwa na methali iliyozingatiwa. Kuhusu safari, mtunzi wa shairi la 'Ndiya Panda' (Abdalla 1973:79-81) amesawiri kuwa:

Haitaki mlegevu, na ambaye ajipenda
Kwa mtu mtepetevu, 'wapo ndiya hiyo enda
Atafurikwa na povu, na pumzi kumpanda
Hapafiki ndiya panda (Ubeti wa 4)

Katika ubeti huo, mshairi amezungumzia kuhusu safari inayowafikisha wahusika katika *ndiya panda*. Hata hivyo, mtunzi ameuweka utungo katika misingi ya kisiasa. Kwa hivyo, dhana ya '*safari*' huweza kufasiriwa kama harakati na mikakati mbalimbali ambazo hufanywa na wanajamii wakati wanapoazimia kufikia malengo muhimu katika maisha. Kwa mfano, mwanajamii ambaye huamua kufanya jambo fulani ni vyema adhihirishe azma hiyo kivitendo mara moja. Kwa hivyo, mtu ambaye hutoa sababu mbalimbali za kusubirisha utekelezaji wa azma hiyo si sawa na yule ambaye tayari ameianza safari. Katika muktadha wa shairi, dhana ya *safari* huelekeza katika utafakari ili kuupata maana inayotokana na uhalisi wa maisha. Kimsingi, wahusika hao waliazimia kutekeleza azma hiyo, lakini kwa wakati tofauti tofauti. Yule ambaye ameyewahi kutenda tendo hapo awali huwa amepiga hatua zaidi ya yule ambaye bado hupoteza wakati katika kufikiria kulitenda tendo hilo wakati ujao.

Kulingana na mantiki iliyoibuliwa kupitia kwa methali hiyo, mshairi amesisitiza kwamba, ni vyema kuanza kutenda jambo hata kama ni pole pole badala ya kuairisha pasipo na sababu mwafaka. Kwa hivyo, mtu aambaye husubirisubiri huweza kutatanabahi kuwa ameachwa nyuma kimaendeleo. Zaidi ya hayo, mshairi ametahadharisha kwamba; mtu ambaye hutarajia kufanya mambo kwa haraka hawezi katu kumfikia yule ambaye tayari ameishaianza na ameitangulia safari. Vile vile, mtu aliyeamua kuanza shughuli fulani awali, huweza kuifanya shughuli hiyo kwa satuwa au utaratibu bila ya papara.

Kwa hivyo, mipango hiyo hukamilika vizuri na wala haiwi katu yenye dosari. Kama vile ilivyo kwa mtu aliyeianza safari mapema, huwa na wasaa wa kujipumzisha na akili ili kuweza kuingia katika duru ya kufikiria namna ambavyo huweza kukabiliana na shughuli zingine za baadaye ambazo pia muhimu. Kulingana na busara ya methali hiyo, mtu ambaye hutarajia kuianza safari si sawa na yule ambaye tayari amepiga hatua katika safari. Kadhalika, busara ambayo imeibuliwa kupitia kwa methali hiyo huwa ni kichocheo cha kuzingatia miktadha mingine katika jamii. Kwa hivyo, msomaji huweza kufahamu kuwa msingi au kigezo cha kuibulia maana au ujumbe unaokusudiwa ni kupitia kwayo.

3.2.2.3 Methali kama Msingi wa Kujengea Itikadi na Mwelekeo wa Mtunzi

Mshairi alipokuwa akilisawiri shairi, kwa kiwango fulani alikuwa mwenye mwelekeo na itikadi mahususi ambao ulichochewa kwa tajiriba na uhalisi wa maisha hayo katika jamii. Vivyo hivyo, mshairi ameitumia methali hiyo ya *Alie kwenda kaenda, si sawa na mja nyuma* ili kumfanya msomaji kupata hisi na mwelekeo ambao hutawala katika shairi. Kwa mfano, katika utungo huo msanii humtaka msomaji kufahamu kuwa, mtu aliyedhamiria au aliyekawia kuianza safari si sawa na yule ambaye tayari ameiandama *safari.*

Kulingana na mawazo yaliyowasilishwa, kilicho cha msingi katika safari ni kuianza na wala si busara kuikawiza safari kutokana na sababu zisizofaa. Katika mantiki hiyo, *Alie kwenda hatuwa, si mwenzi si mshindi.* Kwa hivyo, mhusika ambaye ametukuzwa zaidi katika shairi ni yule ambaye amekwisha kuianza safari; ingawa safari hiyo imeanzwa kwa

shida au polepole. Kulingana na mawazo ambayo yamewasilishwa, mtu aliyeianza safari ndiye mwenye mwelekeo wa busara kinyume na yule ambaye hajaianza. Kwa mfano, mshairi amesema kuwa:

Wa nyuma japo tafika, bali ipo walakini
Atafika amechoka, na mwili hoi tabani (Ubeti wa 3)

Kwa hivyo, taswira ambayo imesawiriwa na imeibuliwa imehusu *mja nyuma* ambaye ni mtu ambaye hana mwelekeo mwafaka katika maisha. Kwa sababu, mtu kama huyo hata kama huianza safari baadaye, huwa yenye walakini na atakuwa ameutumikisha mwili isivyopaswa. Katika muktadha huo, *mja nyuma* huenda akafanya haraka haraka mambo hayo na matokeo yatakuwa ni kujutia kutofanya maamuzi mapema.

3.2.2.4 Methali kama Kielekezo cha Kuudhibti Muundo

Mshairi ametumia methali kama mbinu ya msingi katika ujenzi wa muundo wa shairi. Kwa mfano, mshairi ameweza kupata ukwapi na kibwagizo katika shairi. Kwa kuzingatia sehemu ya mwanzo katika methali hiyo, mshairi ameweza kukamilisha ujenzi wa ukwapi kwenye ubeti wa pili; mizani nane abayo huhitajika katika kila kipande cha mshororo. Vile vile, mshairi ameweza kwa urahisi, kupata vina tarajiwa katika mishororo iliyozingatiwa. Ni muhimu kuelewa kuwa, kibwagizo kama mshororo ungetumika mwanzoni mwa ubeti ungekuwa kielekezo cha muundo katika shairi. Kwa ambavyo ametumia methali kama kibwagizo, mishororo ya awali imejengwa ili iafiki muundo wake. Kadhalika kwa kuitumia methali hiyo, mshairi ameweza kutimiza mahitaji kwa namna mbili: kuunda kibwagizo na kuukariri ujumbe katika shairi. Kibwagizo katika shairi hili kina mizani kumi na sita: mizani nane katika ukwapi na utao

mtawalia. Aidha, kumeweza kupatikana vina vya kati na vya nje katika beti kutokana methali hiyo mahususi. Kwa hivyo, mshairi ametumia methali hiyo kwa malengo ya kimuundo katika usawiri na uwasilishaji wa shairi.

3.2.3 Shairi: Mganga Hatajiganga

Shairi hili ni la muundo wa tarbia na lina jumla ya beti saba. Katika uwasilishaji, methali moja imetumika kwa namna mbili muhimu. Sehemu ya kwanza ya methali imetumika kama anwani kamili na pia imetumika kikamilifu kama kibwagizo. Huu ni mtindo ambao umejitokeza mno katika mashairi ya mtunzi huyu. Methali iliyotumika ni: *Mganga hatajiganga, ila ende kwa wenziwe.* Kwa hivyo, methali imetumiwa kuwa msingi wa kukidhi malengo maalumu kama ilivyobainishwa hapa.

3.2.3.1 Methali kama Kichocheo cha Kutungia Kisa

Kutokana na tajiriba yake katika jamii, mshairi ana mchomo wa hisi kuhusu matendo ambayo hutendwa na wanajamii, ambapo angependa kuyawasilisha. Kwa mfano, katika jamii *mganga* ni mtu ambaye ni mashuhuri na huheshimiwa kutokana na taaluma hiyo ya utabibu. Kwa hivyo, ni mtaalamu ambaye ana uwezo wa kuwatibu wagonjwa mbalimbali. Hata hivyo, anapokuwa mgonjwa hawezi katu kujiagua bali kwa kuwaendea wengine ambao huenda si mjuzi sana kama yeye. Katika muktadha huo, imetongolewa kuwa:

> *Awe bingwa wa kutibu, na maradhi kuaguwa,*
> *Ajua kila hijabu, ala hakupungukiwa,*
> *Kujiganga aghalabu, hatibu atatibiwa,*
> *Mganga hatajiganga, ilia ende kwa mwenziwe* (Ubeti wa 1)

Katika ubeti huo, tukio la *mganga* kutoweza kujitibu limesawiriwa. Jambo hili huweza kushuhudiwa kwa urahisi katika maisha ya watu. Kwa hivyo, mshairi ametumia sehemu ya awali ya methali kama anwani na pia kuwa kibwagizo katika beti za shairi. Sehemu ya awali huwa imedokezea zaidi kuhusu methali ambayo hurejelewa (Mlacha 1985). Kwa kutumia sehemu ya methali ameweza kulipa anwani mwafaka shairi hili.

Aidha matumizi ya methali kama anwani, imejenga mazingira ya kumdokezea kuhusu ujumbe ambao hutarajiwa kuwasilishwa. Kwa sababu hiyo, msomaji hapati shida ya kung'amua muktadha wa ujumbe ambao umesawiriwa na umewasilishwa. Kadhalika, mshairi ameitumia methali kabla kama anwani ili kuweza kumtayarisha msomaji wa shairi. Baada ya kulipa anwani shairi hili, ameamua kimakusudi kutumia methali nzima kama kibwagizo au mshororo mahususi katika beti. Kwa kufanya hivyo, ameweza kujenga msingi wa kuuendeleza, kuufaragua na kuukoleza zaidi ujumbe ambao umekusudiwa. Kwa mfano, ameanza kuelezea kinachomghasi na kumchachafya moyoni mwake. Kwamba, baadhi ya waganga ambao ni weledi katika taaluma yao ya utabibu, wanapokuwa wagonjwa huwa hawawezi kujiganga ila kuwaendea wengine ili waweze kuganguliwa.

Ingawa waganga ni mashuhuri katika taaluma hiyo, werevu wao huweza kufikia ukingoni hasa wanapokuwa hoi kwa uwele. Waganga hao, huweza kuwa ni magwiji katika utabibu lakini wanapokumbwa na maradhi madogo madogo kama vile kuwangwa *kichwa* au kuugua *mafua* au *jip,* hutatizika mno na afya yao huathirika vibaya. Magonjwa hayo madogo amekuwa akiyatibu kwa urahisi wakati wagonjwa walipomwendea kwa

matibabu. Jambo la kushangaza, kulingana na maelezo yametolewa na kupitia kwa methali iliyotumika, tabibu huyo hawezi kujitibu.

Kadhalika, mshairi ameelezea kuwa, *mganga* huyo huweza hata *kufa* kutokana na maradhi hayo madogo madogo. *Maafa* yanapomfika *mganga*, jamii hushangazwa mno kwa matukio hayo ambapo yeye mwenyewe alikuwa na maarifa ya kuyaagua na kuyagangua kwa wengine. Mshairi ameelezea zaidi kuhusu ujumbe huo kwa kusisitiza kuwa, mganga huyo mashuhuri hawezi katu kutumia ujuzi wake kujitibu ila kwa kuwaendea wenzake ambao ni wa taaluma hiyo. Endapo tabibu huyo huwa mbishi au kuona muhali kutaka ushauri au tiba kutoka kwa wale ambao amewapiku, maradhi hayo madogo huenda yakamwathiri vibaya na pia kumuua.

Msisitizo wa ujumbe huo umetokana na methali iliyotumiwa. Kwamba, ili *mganga* kuweza kupata uponyaji, ni sharti kunyenyekea kwa kuwaendea matabibu wenzake ambao huenda si magwiji wa taaluma hiyo. Kwa hivyo hoja hiyo, imesisitizwa kupitia kwa methali kuwa; hatua ya pekee iliyopo ya kumvua maradhi ni ile ya kuwaendea wengine katika jamii la sivyo huenda akaendelea kudhikishwa kwa maradhi hayo hafifu. Katika ubeti wa mwisho, mshairi amesifu hatua na vitendo vya kuwaendea wengine ambavyo huleta ufanisi na maendeleo katika jamii. Ni kupitia kwa methali, ndipo msanii ameweza kuuwasilisha ujumbe wa kumtaka mwanajamii kutotegemea tu uwezo alionao bali kushirikiana na wenzake katika utatuzi wa dhiki ambazo huzizonga jamii.

3.2.3.2 Uwasilishaji wa Mawazo Kiisitiari Kutokana na Matumizi ya Methali

Shairi hili limewasilishwa kimafumbo na kiisitiari kutokana na matumizi ya methali. Katika utungo huu, mshairi ameweza kuwasilisha ujumbe kwa kutoa maelezo ya kina kuhusiana na kiburi cha tabibu ambaye ameimaizi barabara taaluma hiyo. Kadhalika, methali imetumika ili kumfanya mpokezi kunoa bongo zaidi katika kuupokea ujumbe fiche ambao yamewasilishwa kiisitiari kupitia kwa maneno ya kawaida. Maneno hayo yaliyotumiwa ni, *Mganga hatajiganga.* Ingawa kauli iliyotumiwa ni ya kawaida, ni ishara ambayo hupaswa kuzingatiwa na kufasiriwa kuibuka katika akili ya msomaji, ni kama:

- Kwa nini *mganga* hawezi kujiganga?
- Je, *mganga* akiamua kujiganga, matokeo ni yapi?

Haya ni maswali ambayo hutarajiwa kuichochea akili ya hadhira. Majibu huweza kupatikana endapo maneno yaliyotumika katika methali yatazingatiwa. Katika muktadha huo, tabibu bingwa aliyesita kutilia maanani mawaidha aliyopewa, huenda akajikuta katika mateso, upweke au kubaguliwa na kuchukuliwa kuwa hayawani katika jamii. Kulingana na maelezo yalitolewa, tabibu hata awe mwenye uwezo wa kiasi gani hawezi katu kugundua dosari aliyonayo hadi pale anapotanabahishwa na wenzake. Kadhalika ikumbukwe kuwa mtu akiwa amewaendea wengine kwa ushauri isichukuliwe kama ni namna ya kujidunisha.

Kupitia kwa methali, mkataa ushauri hawezi katu kuheshimika katika jamii. Kwa sababu, hakuna mja ambaye huweza kujikosoa au kujiimarisha bila ya kusikiliza au kushirikisha mawaidha ya wenzake katika jamii. Kama vile *mganga* mwenye kiburi

hujichukulia kuwa mwerevu zaidi huku akiwapuuza wenzake huenda akaathirika zaidi kwa uwele au dhiki alizo nazo na hata pengine kujisababishia maafa yasiyotarajiwa. Msomaji anapokumbana na methali katika shairi, anatarajiwa kujitutumua na kupiga bongo ili apate ufafanuzi zaidi kuhusu ujumbe ambao umewasilishwa. Hiyo ni imetokana na sababu kwamba, mshairi hana muda mwingi wa kufaragua kwa kina hoja na mawazo hayo. Kwa hivyo, huteteua ishara au kauli ambazo hutumika katika kuashiria (Propp 1968). Ingawa mshairi amezungumzia kuhusu *Mganga* asiyeweza kujiganga, huweza kufasiriwa zaidi kuwa, ni uwasilishaji wa kijuujuu wa ujumbe unaohitaji upatanisho wayo kwa kuzingatia muktadha mpana wa utamaduni na uhalisi wa jamii. Wakati ambapo msomaji anapotafakari zaidi huweza kufasiri na kujifafanulia ujumbe fiche uliokusudiwa. Kwa mfano, mganga mashuhuri katika jamii huweza kuwa ni mmojawapo wa wanajamii ambaye hushikilia hatamu au wadhifa wa uongozi katika taasisi za kijamii. Shairi la 'Mamba' (Abdalla, 1973:10), ambalo limetumia dhana ya *mamba* kuwa ishara ambayo imeashiria kiongozi wa kimabavu ambaye hujigamba katika jamii.

Kwa kuzingatia methali, msomaji huweza kutanua zaidi mawazo au ujumbe ambao umewasilishwa. Kulingana na nadharia ya Semiotiki, kauli au maneno teule hutumika katika kutilia mkazo jambo linaloelezwa katika muktadha wa mawasiliano (Scholes 1982). Kwa hivyo, *mganga* huweza kuwa ni kiongozi katika jamii, huenda akawa ni mashuhuri au mweledi wa shughuli hiyo lakini jambo dogo huweza kumtatiza na kumwathiri. Suluhu ambayo imetolewa katika shairi hili ni kujadiliana miongoni mwa jamii ili tatizo liweze kurekebishwa au kutafutiwa tiba kabla halijaenda mrama. Endapo

kiongozi huyo atakuwa mwenye kiburi na kudharau ushauri wa wale walio chini yake, labda kwa kuwatisha au kuwanyima nafasi ya kumkosoa, huenda hatakuwa makini katika utendakazi wake katika jamii. Hiyo ndiyo sababu katika ubeti wa mwisho wa shairi hili, imedokezwa kwamba; *vitendo* (yaani mtu asiyependa kutafuta ushauri au usaidizi kwa wengine hata wale waliochini yao) ndiyo kiini cha kutojinyanyua au kutopata suluhu katika jamii. Katika muktadha huo, matumizi ya methali hulifanya shairi kuwasilishwa na kufasiriwa kimafumbo au kiisitiari. Kwamba, mshairi alipotumia maneno kama vile *mganga* na uganga huwa ni ishara mwafaka ambayo huweza kupatanishwa na kufasiriwa kisahihi kwa kuzingatia ishara ambazo hupatikana kwa urahisi katika jamii.

3.2.3.3 Methali kama Nguzo ya Kuwasilishia Mawazo ya Uzindushi na Utangamano

Kwa kutumia methali, shairi hili limekuwa msingi wa kuwasilishia uzindushi na utangamano ambao hujikita katika falsafa na utamaduni wa jamii. Kwa hivyo, matumizi ya methali huweza kusaidia katika uwasilishaji wa ujumbe ambao hupaswa kuzingatiwa na msomaji. Kwa mfano, mshairi amemsawiri *Mganga* stadi ambaye hawezi *kujivua* maradhi hayo kutokana na kiburi alichonacho. Kwa njia hiyo, amemsawiri na kumwasilisha mwanajamii mwenye kiburi na asiyeweza kujiauni kutokana na majitwezo yake. *Mganga* aliyewasilishwa ni mwenye uwezo mkubwa katika taaluma yake, lakini hawezi katu kujiganga ila kwa kuwaendea wenzake. Mtu kama huyo hujiona babe na muweza wa kila kitu. Kimsingi, jambo hilo halitakikani kuwepo katika jamii.

Kulingana na mawazo ambayo yamewasilishwa ni kwamba, *mganga* huyo hajatumia hekima. Aidha, huhitaji kubadili mtazamo wake kwa manufaa yake na kwa jamii. Hiyo

ndiyo sababu ya mshairi kuukejeli uwezo alionao mganga stadi katika muktadha wa methali iliyotumika. Kadhalika, mshairi haoni mwafaka wowote huweza kutokana na kuwadharau watu ambao ni wa viwango vya chini. Kwa sababu, hao pia ni watu ambao huweza kutoa mchango mdogo lakini wa muhimu katika jamii. Itikadi ya mshairi ni kwamba, mtu aliye juu huwa na nafasi hiyo kutokana na juhudi za walio wengi au walio chini. Kwa hivyo, watu kama hao hustahili kuheshimiwa na mawazo yao kuthaminiwa inavyostahili; la sivyo mambo huenda yasiwe shwari katika jamii. Endapo mambo yataenda segemnege, ni wote ambao huangamia. Aidha, mtu ambaye hudharau mawaidha ya wengine katika jamii huenda akajidhikisha au kujiangamiza yeye mwenyewe. Kulingana na mawazo yaliyowasilishwa, *mganga* kama huyo aliyekataa ushauri wa wenzake anakuwa hujichimbia kaburi lake mwenyewe. Kwa sababu, mawazo ya mtu mmoja huenda yawe yenye dosari au yasiwe mazuri. Busara ambayo imetokana na methali hiyo ni kwamba, watu katika jamii huhitaji kushirikiana kila wakati na anayepuuza umuhimu huo, hujikuta ameangamia kwa 'mwiba wa kujidunga usiohitaji waombolezaji'. Kwa mfano, imetongolewa kuwa:

Yakamkuta maafa ...
Wakashangaa kaifa, kushindwa kujivumbua (Ubeti wa 4)

Aidha, si busara kuchelea kutaka na kutafuta msaada kutoka kwa wengine katika jamii. Hilo lisichukuliwe kuwa ni namna ya kujifedhehesha kwa sababu, 'mficha uchi hazai' na vile vile 'mkamilifu ni mfu'. Kwa hivyo kutokana na methali imefahamishwa kuwa, mtu hawezi katu kubaini dosari aliyonayo ila huweza kugunduliwa kwa urahisi na wengine katika jamii. Aidha, hao waliogundua dosari ya dharura na kufahamisha hawapaswi kuchukuliwa kama hasidi, bali ni watu wenye utu na upendo mkuu katika jamii. Vile vile, *mganga* kama mwanajamii yeyote yule, huweza kujirekebisha siyo kwa mawazo au

uwezo wa kibinafsi bali, kutokana na mawazo ya wengine katika jamii. Kwa hivyo, matokeo ya kurekebishana miongoni mwao, ni msingi wa maendeleo, utangamano na mahusiano mema katika jamii.

3.2.3.3 Methali kama Chombo cha Kuwasilishia Muhtasari wa Ujumbe

Mshairi ametumia methali hiyo kwa makusudi ili kuwasilishia muhtasari wa ujumbe. Kwa sababu, methali ni fumbo ambalo limefumba ujumbe pana (Waihiga na Kagwa 2007 na Wamitila 2003). Katika shairi, mtunzi ametoa maelezo ya kina kuhusu vitimbi na kiburi cha *mganga* asiyetaka msaada kutoka kwa waganga wenzake. Isitoshe, maelezo na mifano mbalimbali imetolewa katika uwasilishaji wa ujumbe na ufafanuzi wa hoja za mshairi. Kadhalika, matumizi hayo ya methali hujenga muhtasari wa ujumbe ambao umewasilishwa. Kwa ambavyo, methali hiyo imetumiwa kama kibwagizo katika shairi, husaida kumrejesha msomaji kila wakati katika msingi wa mawazo ambayo huwasilishwa. Kwa mfano, tayari ameelezea kwa kina mawazo hayo kuhusu dhiki ambazo humwandama *mganga* mwenye kiburi.

Kadhalika maelezo yaliyotolewa, husaidia mno katika ujenzi wa mkururo wa mawazo yanayowasilishwa. Hata hivyo, mawazo hayo huweza kuwa ni mengi mno yenye mzunguko. Jambo hilo huweza kumfanya msomaji wa shairi asiweze kukumbuka yote yaliyoelezwa. Kwa kutumia methali, mawazo ya msingi hufumbwa na huwasilishwa kimuhtasari na kwa mwafaka zaidi. Hali hiyo haimaanishi kuwa msomaji hapaswi kuzingatia maelezo na mifano yaliyotolewa. Kwa kuzingatia methali, msomaji huweza kuchuja na kudondoa mawazo muhimu ambayo hupatikana katika shairi. Isitoshe,

msomaji huweza kuwa na kumbukumbu mwafaka ya mawazo ambayo yamewasilishwa katika shairi. Kwa kuikumbuka methali, msomaji huweza kujifafanulia uziada wa maelezo na mifano iliyotolewa kwa kudokezwa katika shairi. Zaidi ya hayo, msomaji huweza kujenga kumbukumbu mwafaka ya mawazo katika shairi linalowasilishwa. Hapa ieleweke kwamba, shairi la Kiswahili huwasilisha maelezo kwa ufupi kuhusu ujumbe. Kutumiwa kwa methali, mawazo huchujwa zaidi ili msomaji awe na dira ya hifadhi mwafaka ya mawazo hayo ambayo ni muhimu. Katika kufanya hivyo, hoja muhimu huhifadhiwa na ujumbe huwasilishwa kwa muhtasari.

3.2.4 Shairi: Umoja ni Ngome Kuu

Shairi hili ni la muundo wa tarbia na lina beti nane. Katika usawiri na uwasilishaji wa utungo, mshairi ametumia methali moja: *Umoja ni ngome kuu, utengano udhaifu.* Methali hiyo humaanisha kuwa, mtu anapofanya jambo fulani kibinafsi, huweza kuwa ni mchango mdogo unapolinganishwa na juhudi za watu wengi. Kadhalika, jambo gumu huweza kutatuliwa kwa urahisi endapo watu wengi wamechangia. Kwa hivyo, ujumbe ambao umesisitizwa katika shairi ni umuhimu wa ushirika wa watu. Sehemu ya awali ya methali imetumika mahususi kama anwani ya shairi. Zaidi ya hayo, imetumiwa kwa ukamilifu kama kibwagizo katika shairi. Kwa kutumia methali hiyo, mtunzi ameweza kutimiza mambo mbalimbali ya msingi kama inavyovyoelezwa.

3.2.4.1 Methali kama Kielekezo cha Kuibulia na Kuwasilisha Mawazo

Mshairi ametumia methali hiyo kama msingi wa utunzi na uwasilishaji wa mawazo katika shairi. Sehemu ya awali ya methali imetumiwa ili kulipa anwani: *umoja ni ngome*

kuu. Kwa hivyo, kama anwani imeweza kutanguliza na kudokezea kuhusu umuhimu na *umoja* unaotarajiwa kusawiriwa na kuwasilishwa katika shairi. Kwa njia hiyo, msomaji huweza kufahamu kwamba, mwelekeo ambao umechukuliwa katika uwasilishaji wa ujumbe ni ule uliofungamana moja kwa moja na methali iliyoteuliwa na illiyotumiwa. Kwa hivyo, msomaji anapolisoma shairi huelewa kuwa, hata mifano ambayo imeibuliwa na imetumiwa huwa imerejelea anwani ya shairi.

Katika muktadha huo, mshairi hatarajii msomaji kupata matatizo katika kuufasiri au kuuelewa ujumbe ambao umewasilishwa. Kutokana na tajiriba yake huibua na huuwasilisha ujumbe ambao huhusu umuhimu wa *umoja* na utangamano katika jamii. Kwa hivyo, mawazo yaliyowasilishwa yameweza kupata mwelekeo zaidi kupitia kwa methali iliyotumika. Aidha, mshairi alipotumia methali aliweza kupata msingi wa kuibulia na kufafanulia zaidi mawazo hasa kwa kutoa mifano maridhawa inayotolewa kama ithibati . Vile vile, kupitia kwa methali, mshairi amepata mwanya wa kufaragua na kuelezea kwa undani mawazo huku akidhihirisha namna jamii yenye *umoja* hunufaika kuliko ile ambayo imeshikilia ubinafsi katika utendakazi wa jamii. Msisitizo wa ujumbe ambao umedhihirishwa ni ule uliohusu *umoja* ambapo humkweza au humnyanyua mtu katika jamii. Kama ilivyotongolewa kuwa:

> *Umoja ni utukufu, mkubwa uso kifani*
> *Humkuza mtu dufu, kuwa juu kileleni*
> *Kutengana udhaifu, moja ya umasikini*
> *Umoja ni ngome kuu, kutengana udhaifu* (Ubeti wa 2)

Kwa kutumia methali, mshairi ameweza pia kuusifu *umoja* kwa kuufananisha na vito au *madini.* Kadhalika, methali imetumiwa kuibulia hisi au mwelekeo unaokemea ubinafsi

katika jamii. Kwamba, mtu ambaye hapendi kushirikiana na wenzake katika jamii huwa ni *punguani* au hayawani. Kwa mfano, imekaririwa kuwa:

Mkataa ushirika, umoja asitamani
Mtu huyo kalanika, na tena ni punguani
Kasha ni mwenda mahoka, si mtu hasa razini
Umoja ni ngome kuu, kutengana udhaifu (Ubeti wa 4)

Mshairi hakomei katika maelezo hayo, bali pia ameweza kurejelea mifano ya baadhi ya wadudu wadogo ambao hutenda mambo makubwa kutokana na utendakazi wa ushirika. Mfano wa kwanza uliozingatiwa ni wa *nyuki* ambao hushirikiana katika utendakazi wao wa kutayarisha *uki* huku wakiishi kwa *amani* na upendo mkuu. Katika kufafanua zaidi umhimu wa umoja, ametoa mfano mwingine wa *mchwa* ambao hutenda mambo ya ajabu katika kichuguu. *Mchwa* hao, kulingana na maelezo yanayotolewa ni kwamba, kila mmoja wao huwajibika kabisa katika shughuli zao ndogo ndogo katika himaya au ujenzi wa kichuguu. Isitoshe, katika kichuguu kuna wafanyikazi, walinda usalama, malkia na mfalme. Makundi hayo hushiriki matendo madogo madogo ambayo ni muhimu katika kichuguu. Kwa hivyo, ngome hiyo imeweza kudhibitiwa kutokana na umoja na ushirikiano katika utendakazi wao.

Kulingana na mshairi ni kwamba, katika jamii yao kuna mifano mingi ambayo hupaswa kuzingatiwa ili kuweza kuzinduliwa lakini wanajamii wamekuwa kama waliofumbwa macho ya kutoona manufaa hayo. Katika muktadha huo, imedhihirishwa kuwa jamii haiwezi katu kufanikiwa maishani kutokana na ubinafsi. Kwa mfano, imekaririwa kuwa:

Haya yote haya kwamba, umoja umkononi
Moyo hubi wameshiba, umoja wamethamini
Umoja ngome ya shaba, udhaifu utengani
Umoja ni ngome kuu, kutengana udhaifu (Ubeti wa 7)

Kwa hivyo, mawazo hayo hasi ambayo yaliendelezwa na baadhi ya watu ni yenye mwelekeo ambao hupaswa kutokomezwa katika kaburi la sahau iwapo watu hutarajia kupiga makasia ya kimaendeleo katika jamii yao. Kulingana na mshairi, watu ambao huendekeza ubinafsi hawapaswi tu kukemewa bali pia kulaniwa na Mwenyezi Mungu. Katika muktadha huo, matumizi ya methali yamekuwa ni dira ambayo iliongoza katika ufaraguzi wa mawazo na ubainishaji wa mwelekeo wa msanii kuhusu umuhimu wa *umoja*.

3.2.4.2 Methali kama Msingi wa Kuundia Taswira

Mshairi ameitumia methali ili ujumbe na mawazo yaweze kuwasilishwa kitaswira kwa msomaji. Kwa kuitumia, mshairi ameweza kuisawiri na kuiwasilisha picha ya watu ambao walishirikiana kwa umoja. Vile vile, ameweza kumwasilishia msomaji picha ya baadhi ya wanajamii ambao hutenda mambo yao kibinafsi. Kwa hivyo, mtu huyu ameabainishwa kama *punguani*. Kutokana na matumizi ya methali, mshairi huifanya hadhira wa shairi kutunga picha ya kimaono kuhusu wanajamii na utendakazi wao. Kwamba, wanajamii waliotenda kazi zao kwa ushirika hunufaika kwani *wamo katika faraja*.

Katika muktadha huo, mshairi amekuwa mwenye nafasi nzuri ya kuuwasilisha ujumbe wake kitaswira. Kilichobainika ni kwamba, taswira huweza pia kuwasilishwa kupitia kwa maelezo ya kibinafsi yaliyotolewa. Aidha, kwa kutumia methali, mshairi ameweza kupata upenu mwingine wa kusisitiza na kuwasilisha ujumbe kitaswira. Mwanajamii ambaye hapendi kushirikiana na wenzake katika utendakazi wao imedhihirishwa kwa

uwazi zaidi kupitia kwa mifano iliyopo. Kwa kuzingatia matumizi ya methali, ameibua hasira yake kwa baadhi ya wanajamii ambao hawauoni ushirika wa wadudu unaowanufaisha zaidi katika maisha yao ya kila siku. Katika muktadha wa matumizi ya methali, mshairi ameweza pia kujenga taswira ya *nyuki* na *mchwa* ambao kila wakati wamo katika harakati za kujiimarisha kimaisha huku wakiwa katika ushirika. Ni kutokana na matumizi ya methali ndipo ameweza kufafanua zaidi mifano iliyojenga taswira ya utendakazi wa wadudu hao wadogo.

Kulingana na maelezo yaliyotolewa, *nyuki* ni wadudu wadogo kimaumbile lakini wameweza kutengeneza *uki* mzingani kwa juhudi zao za ushirika. Kila *nyuki* hutoa mchango wa kuhakikisha kuwa viungo vyote vilivyotarajiwa katika utengenezaji wa *uki* vimepatikana kwa wakati ufaao. Taswira nyingine imejikita katika *mchwa* ambao huishi kwa *amani* huku wakishirikiana katika ngome yao isiyokuwa na mfano. Ingawa mchwa wana uwezo mdogo wa kibinafsi, mchango wao huweza kutenda mambo makubwa na ya ajabu, kama vile kujenga kichuguu. Kwa mfano, malkia na mfalme hawaonekani hivi hivi, lakini katika kichuguu *mchwa* hushirikiana katika utekelezaji wa shughuli zao muhimu. Kwa hivyo, kila mchwa huwa na umuhimu wake katika kichuguu. Kama vile nyuki, katika jamii ya mchwa kuna vibarua wa ujenzi kichuguu na pia kuna wanaoshika doria. Kwa upande mwingine, mfalme hukubaliwa kuwa kiongozi kwa kushirikiana na malkia kuhakikisha kwamba wameiendeleza jamii yao katika himaya hiyo.

Hata hivyo, ni vyema ieleweke kuwa taswira ya *nyuki* na *mchwa* zimeibuliwa kutokana na methali ambayo husaidia katika kuibua na kuzingatia mifano mingi mingine inayopatikana kwa urahisi katika mazingira ya jamii. Jambo la msingi hapa ni kwamba,

taswira hizo ndogo ndogo ambazo huhusu wadudu zimechangia mno taswira iliyoibuliwa kupitia kwa methali. Kwa kuzingatia taswira iliyoundwa, mshairi amepata upenu mwingine mwafaka ulioshadidia zaidi ujumbe uliojikita katika kudhihirishia umuhimu wa umoja katika jamii. Kwamba, watu hawapaswi kujitolea sababu zisizo kuwa za msingi kwa kutoshirikiana ilihali kuna mifano kemkem ambazo hupatikana kwa urahisi katika mazingiria yao. Iwapo mwanajamii hupata dhiki, dhiki hiyo hupaswa kutatuliwa na wanajamii wote. Kwa sababu hiyo, jamii itakuwa imepiga makasia ya maendeleo. Hiyo ndiyo picha ya kimaono ambayo imeundiwa hadhira.

3.2.4.3 Methali kama Mhimili wa Kuundia Isitiari

Katika uwasilishaji wa utungo huu, methali hiyo imetumiwa kiisitiari ili kuchochea tafakuri ya hadhira. Kutokana na isitiari iliyoibuliwa, msomaji huwa katika nafasi nzuri ya kuuelewa zaidi ujumbe ambao umewasilishwa katika shairi. Kwa kuzingatia nadharia ya Semiotiki, kauli au dhana teule zilizotumika katika uwasilishaji wa shairi, hujengeka katika tamathali za usemi. Hata hivyo, utamathali huo hugawanyika katika sehemu mbili: metonomia na taashiria (Jacobson 1960). Kwa ambayo ujumbe katika shairi hilo hauhitaji utafakari sana, umekuwa ni wa kimetonomia. Kwa sababu, tayari mtunzi ametoa ufafanuzi wa kina kuhusu ujumbe unaowasilishwa.

Kadhalika kwa kutumia methali, mshairi humtarajia msomaji kuzingatia maelezo yaliyotolewa ili ujumbe kuweza kubainishwa. Maelezo yaliyotolewa ni kwamba, umoja ni nguvu katika jamii. Katika hali hiyo, msomaji huweza kufahamu msukumo uliomchochea na uliomsukuma mshairi kutunga shairi. Kwa mfano, ametumia dhana ya

umoja kuwa ni *ngome kuu* na *utengano* kuwa ni *udhaifu.* Hizo ni dhana mbili zinazokinzana katika methali, lakini kutokana na ukinzano huo ndimo ujumbe unamojikita. Wakati msomaji anapokumbana na matumizi ya methali, hujiingiza katika usaili wa *ngome kuu* na *udhaifu* ili kuweza kuufahamu zaidi ujumbe uliowasilishwa. Kwa hivyo, msomaji huchochewa kufikiria zaidi manufaa ya umoja na pia kutafakari zaidi kuhusu ubaya wa utengano katika jamii. Kwa mfano, watu wanaposhirikiana katika utendaji wa kazi huweza kufaulisha kwa urahisi mambo ambayo ni magumu na mazito.

Katika jamii huwa kuna mambo ambayo ni magumu au yasiyowezekana yanapokabiliwa kibinafsi. Ugumu huo huweza kutatuliwa kwa wepesi na haraka endapo watu watakuwa wameamua kushirikiana. Kwa hivyo, mtunzi amefafanua mambo hayo kwa kuzingatia mifano halisi ambayo hupatikana katika jamii. Hiyo ndiyo sababu ya kuundwa kwa taswira ambayo hueleweka ambayo huelezea namna *nyuki* na *mchwa* hushirikiana katika utendaji kazi wao. Ingawa nyuki na *mchwa* ni wadudu wadogo, taswira yazo zimesaidia katika kuutilia nguvu na kuuelewa ujumbe huo uliohusu *umoja* katika jamii. Isitoshe, methali imetumwa kuwa ishara ambayo huhitaji kufafanuliwa na kupatanishwa na uhalisi wa jamii. Jambo hilo limerahisishwa kupitia kwa maelezo ya kina yaliyotolewa.

Kadhalika, msomaji huweza kutafakari zaidi harakati nyinginezo ambazo hutekelezwa katika jamii kwa kuzingatia uelekezi wa mifano iliyotolewa. Kwa ambavyo mshairi hana muda mwingi wa kufaragua mawazo, ametumia methali hiyo kuwa ishara ambayo humtafakarisha msomaji ili kuuelewa zaidi ujumbe katika shairi. Ishara hizo ni kama *nyuki* na *mchwa.* Kimsingi, umoja katika jamii ni muhimu mno na haliwezi kufasiriwa

kwa mwafaka bila ya kuzingatia uhalisi wa maisha na utamaduni wa jamii. Kwa mfano, katika jamii mbalimbali za Afrika, mtu ambaye hufanya mambo kwa manufaa ya kibinafsi huchukuliwa kuwa mchawi. Vile vile, alipolinganisha umuhimu wa *umoja* na *udhaifu* wa *utengano*, mshairi humtaka mpokezi kuzingatia zaidi madhara ambayo husababishwa na utengano katika utendakazi na maendeleo yao. Hiyo imemaanisha kuwa methali iliyotumika huweza kueleweka kwa kuzingatia miktadha mingine ambayo hupatikana katika jamii. Kwa hivyo, ujumbe uliowasilishwa huweza kupatanishwa na busara ambayo imeibuliwa kupitia kwa methali. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli teule zilizotumika katika uwasilishaji wa utungo ni zile ambazo hufahamika na hadhira (Lord 1960). Kwa hivyo, mshairi hamtaki msomaji awe hadhira tuli bali kuweza kuendelea kusaili na kutafakari zaidi upeo wa maelezo yaliyowasilishwa katika shairi.

3.2.4.4 Methali kama Mbinu ya Kuwasilishia Muhtasari wa Ujumbe

Mchango wa methali hiyo katika shairi ni kumsaida mshairi kusawiri na kuwasilisha ujumbe wake kwa muhtasari. Kama ilivyobainika katika uwasilishaji wa shairi hili, ujumbe uliohusu *umoja* katika jamii ni mpana mno. Kadhalika, mshairi ameweza kutoa maelezo na kuwasilisha mifano iliyofahamika ili kufafanulia hoja zake katika shairi. Kuna uwezekano kwamba, mshairi angetaka kufafanua zaidi mawazo hayo lakini kutokana na muda au nafasi iliyopo, hakuweza kufanya hivyo. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, ushairi hutarajiwa kutungwa kutokana na tukio la kijamii. Kwa hivyo, hutungwa na kuwasilishwa kimasimulizi. Mtunzi naye huwa hana muda mwingi wa matayarisho (Nagler 1967). Kwa sasa ushairi hutungwa na kuwasilishwa

kimasimulizi na kimaandishi. Katika muktadha huo, ushairi huweza kuwa mfupi au mrefu. Shairi hili la 'Umoja ni Ngome kuu' ni fupi ili kukidhi haja hizo mbili. Kadhalika, uwasilishaji huo umeelekezwa kwa methali iliyotumika.

Kwa sababu hiyo, mshairi ametumia methali hiyo: *Umoja ni ngome kuu,* utengano ni *udhaifu* ili kuufumba na kuuwasilisha jumbe kwa muhtasari. Aidha, msomaji hatarajiwi kukumbuka au kuhifadhi maelezo na mifano mbalimbali iliyotolewa. Kwa hivyo, matumizi ya methali katika shairi yamekuwa kama fupa ambalo huhitaji mnofu. Katika muktadha huo, msomaji hutarajiwa kujitolea mifano na maelezo pana wakati anapokumbana na methali iliyotumiwa katika shairi. Kwa sababu hiyo, mshairi ameamua kwa makusudi kutumia methali ambayo imesaidia kuuwasilisha ujumbe kwa muhtasari katika shairi.

Katika harakati uwasilishaji, mshairi ametoa ufafanuzi wa kijumla na wa kina kuhusu umuhimu wa umoja katika jamii. Vile vile, mshairi ameufananisha *umoja* na *madini* ambayo hupatikana katika mazingira na uhalisi wa maisha katika jamii. Katika kushadidia zaidi mawazo, ameibua pia taswira ya *nyuki* na *mchwa.* Taswira iliyoundwa imechangia kwa namna moja au nyingine katika kuukoleza na kuupeleka mbele ujumbe ambao umewasilishwa.

Kadhalika, mshairi ameushutumu ubinafsi ambao ni pingamizi au kikwazo katika maendeleo ya jamii. Mifano na ufafanuzi ambao umetolewa ni pana mno na hauwezi kukumbukika kwa urahisi katika taamuli na kumbukumbu ya hadhira. Kwa hivyo, ili

kusaidia katika kuupata muhtasari wa ujumbe ambao umewasilishwa, methali imetumiwa katika utungo. Methali hiyo imeufumba na kuuwasilisha ujumbe kwa namna ambavyo huwza kusaki katika akili ya hadhira. Ujumbe wa msingi wa mshairi ni kuwa, *umoja* ni muhimu na *utengano* hauna nafasi katika maendeleo ya jamii. Mifano na maelezo yote ambayo imetolewa ni ya kuukariri ujumbe ambao tayari umefumbwa katika methali iliyotumiwa.

3.2.4.5 Methali kama Nguzo ya Muundo

Mshairi ametumia methali ya *Umoja ni ngome kuu, kutengana udhaifu,* kuwa msingi wa kujengea baadhi ya mishororo katika shairi. Ni bayana kwamba, ametumia methali kama kibwagizo ili kuusisitiza zaidi ujumbe; lakini pia imetumiwa kama muhimili mwafaka wa muundo wa shairi. Kwa mfano, imetongolewa:

WATU wenye na umoja, siku zote duniani
Wamo katika faraja, ya fahari na thamani,
Na wale waso umoja, siku zote wao duni,
Umoja ni ngome kuu, kutengana udhaifu (Ubeti wa 1)

Kwa hivyo, kupitia kwa methali hiyo, mshairi ameweza kujenga kibwagizo. Hata hivyo, mshairi kwa kupachika silabi mbili yaani **[kuu],** anairefusha methali. Kwa mfano muundo wa methali hiyo ungekuwa: 'Umoja ni ngome, utengano ni udhaifu' au 'umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu'. Uchopekaji au urefushaji huu haudhuru ukamilifu wa mantiki katika methali yenyewe. Kimsingi, huo ni uhuru wa kishairi ambao hukubalika katika utunzi wa ushairi wa Kiswahili. Kwa malengo ya kupanua idadi ya mizani zilizohitajika katika mishororo ya shairi, methali imetumika. Kwa sababu hiyo, mshairi ameweza kupata jumla ya mizani kumi na sita kwenye mshororo ambayo ni sawia na

idadi ya mizani hupatikana katika mishororo mingine katika shairi. Kadhalika, matumizi ya methali yamesaidia katika kupata kina cha kati yaani [**u**] na kina cha mwisho yaani [**fu**] katika kibwagizo. Ujenzi wa muundo wa shairi umeweza kupatikana kwa urahisi kwa kuzingatia methali ambayo imetumiwa.

3.3 KIISHILIO

Sura hii imechanganua matumizi ya methali katika mkabala wa utunzi, usawiri na uwasilishaji wa ushairi andishi wa Kiswahili. Mashairi yaliyohakikiwa katika sura hii ni yale yaliyozingatia zaidi arudhi za kimapokeo katika uwasilishaji wake. Kilichobainishwa katika utafiti huu ni kwamba, matumizi ya methali hujitokeza mno katika utunzi na uwasilishaji wa mashairi hayo. Sababu ya msingi ni kwamba, kwa kiwango fulani, methali zina sifa za ufupi na za kishairi. Isitoshe, sifa za kiarudhi zimedhihirika katika ushairi wa kimapokeo hasa kupitia kwa muundo wake. Vile vile, methali zina uwezo wa kuibua muhtasari wa ujumbe ambao umewasilishwa kwa kuzingatia utamaduni wa jamii.

Uchanganuzi wa mashairi hayo umedhihirisha kuwa washairi wa kimapokeo hutumia methali kwa makusudi kama mbinu au kichocheo cha utunzi na uwasilishaji wa mawazo. Aidha, waliposhirikisha zaidi ya methali moja katika utunzi ni kwamba, huchangiana na hukamilishana katika ufaraguzi na uwasilishaji wa maudhui. Kadhalika, uhakiki wa mashairi hayo umebainisha kuwa, washairi wanapotumia methali, huweza siyo tu kufaulisha usimulizi na ufafanuzi ujumbe bali pia, kama msingi wa kufumba hisi na kuwasilishia muhtasari wa ujumbe. Katika muktadha huo, washairi hutambua kuwa

wapokezi wa ujumbe wana uwezo wa kutafakari, kufasiri na kufafanua zaidi methali au kauli msingi zilizotumiwa ili kuweza kuufahamu kikamilifu ujumbe uliowasilishwa. Pia, imebainishwa kuwa; kipengele cha taharuki na mvuto katika utungo huambatana na jinsi methali ilivyotumika. Ili msomaji kuweza kuendelea kulisoma shairi, hapana budi ndani yake muwe na nguvu fulani ya kumvuta na kumsukuma mbele hadi mwisho. Utekelezwaji huo huwezekana kupitia kwa methali iliyotumiwa au zilizotumiwa. Kwa hivyo, ujumbe katika mashairi hayo huwasilishwa kwa kuzingatia zaidi tamathali za usemi ambazo huundwa kutokana na uzoefu wa matumizi yake katika mawasiliano ya jamii.

Vile vile, katika uchanganuzi mashairi hayo, umedhihirisha kuwa uwasilishaji wake hushirikisha zaidi kauli za kimapokeo kama vile methali. Isitoshe, hizo ni kauli ambazo hujibainisha zaidi katika tamathali za usemi. Hiyo ndiyo sababu ya mawazo kuwasilishwa kimaono zaidi kwa kuzingatia tamathali za usemi kama vile taswira, taashira, kejeli, kinaya na tashihisi. Kadhalika, kauli za kibinafsi zilizotumika, husaidia katika kufafanulia dhima ya methali katika utungo. Kwa hivyo, kilichobainika katika mashairi ya Kiswahili ya kimapokeo ni kwamba, matumizi ya methali ni angavu zaidi siyo tu katika kudhihirisha mielekeo na itikadi za wasanii, bali pia kuwa msingi wa kuwasilisha maadili na maelekezo ambayo yamejikita katika utamaduni wa jamii. Katika muktadha huo, mashairi ya Kiswahili ya kimapokeo huwa ni hifadhi au kanzi angavu ya kuwasilishai utamaduni wa jamii.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI WA USHAIRI WA KATI KWA LENGO LA KUTATHMINI MATUMIZI YA METHALI

4.0 UTANGULIZI

Sura hii imetathmini matumizi ya methali katika baadhi ya mashairi ya sasa ambayo hayazingatii mno kaida za utunzi wa ushairi wa kimapokeo wala ushairi huru wa Kiswahili. Kutokana na hali hiyo, ushairi huo huweza kuchukuliwa kuwa wa kati. Licha ya kuwa mashairi hayo ya kati huitwa 'huru', mbinu ambazo humiwa katika uwasilishaji wake huwa si huru kabisa (Wamitila 2001). Kwa sababu, uwasilishaji huo huzingatia baadhi ya arudhi hizo za kimapokeo. Hata hivyo, kanuni hizo huwa si bayana. Katika muktadha huo, kuzingatiwa kwa arudhi hizo huwa si wa lazima. Aidha, katika kitengo hiki, kuna wasanii mashuhuri ambao wameuchangia ushairi huo. Miongoni mwa watunzi hao ni kama Alamin Mazrui, Said Ahmed Mohamed na Muhammed Seif Khatib. Ushairi huu wa kati ni daraja muhimu baina ya ushairi wa kimapokeo na ushairi huru. Diwani mahususi zilizochanganuliwa katika sura hii ni: *Chembe cha Moyo* (A. Mazrui) na *Jicho la Ndani* (S.A. Mohamed).

Kadhalika, katika uwasilishaji wa mashairi ambayo hupatikana katika diwani hizo, watunzi hao wamechanganya mbinu na mitindo ya mashairi yanayozingatia na yale yasiyozingatia sifa za arudhi za kimapokeo. Baadhi ya mashairi hayo yaliyozingatiwa huakisi kuwa, sanaa haiwezi kufungika mno kwenye kaida (Gromov 2006). Hiyo imetokana na sababu kwamba, sanaa si sugu bali mbinu za uwasilishaji huweza

kuzingatia ama mabadiliko machache au zaidi kulingana na mabadiliko ya kiwakati, kitamaduni na kijamii.

Kwa hivyo, sifa za msingi ambazo huubaainisha ushairi wa Kiswahili, hudhibitiwa na kuhifadhiwa. Mashairi yaliyomo katika diwani hizo yamebainisha uchache wa matumizi ya methali katika uwasilishaji wake kinyume na vile hali ilivyo katika ushairi ambao huzingatia mno katika arudi za kimapokeo.

Kwa hivyo, sura hii imechanganua matumizi ya methali kama kipengele cha uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili. Kadhalika, imebainishwa kwa kutoa ithibati kwamba, matumizi ya methali huweza kuwepo kwa uwazi au kutokuwepo bayana katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Vile vile, sura hii imezingatia kwamba, ingawa methali hutumiwa kama nyenzo ya kuwasilishia maadili katika ushairi wa kimapokeo, zinapotumika katika ushairi wa kati, huwa ni chombo muhimu cha uzindushi na ubainishaji wa uhalisi wa maisha katika jamii. Katika muktadha huo, matumizi ya methali yameangaziwa kama kigezo cha uainishaji wa ushairi wa Kiswahili.

4.1 UCHANGANUZI WA USHAIRI WA ALAMIN MAZRUI: *CHEMBE CHA MOYO*

Diwani hii ya *Chembe cha Moyo* imetungwa na Alamin Mazrui na ilichapishwa kwa mara ya kwanza, mwaka wa 1988 na Shirika la Heinemann (K) Limited. Kadhalika, diwani hii ina jumla ya tungo hamsini na tisa. Miongoni mwa mashairi hayo, ni matano tu ndiyo yaliyoshirikisha matumizi ya methali. Mashairi hayo ni: 'Usijangamize',

'Mkombozi', 'Hasira Hasara?', 'Mgongano' na 'Jana Leo na Kesho'. Hata hivyo, ni mashairi manne tu ndiyo yamechanganuliwa. Mashairi hayo mahususi ni:

(i) *Usijiangamize*

(ii) *Hasira Hasara*

(iii) *Mgongano*

(iv) *Kula Njama*

4.1.1 Shairi: Usijiangamize

Shairi hili lina beti saba. Kila ubeti una mishororo minne. Aidha, shairi hili limesawiri dhiki ambazo huzikumba mataifa ya bara la Afrika kwa wakati huu wa sasa. Kila mwanajamii huhisi mazonge ya dhiki hizo zilizosakini, lakini jamii hustahabu kuwa katika uhalisi huo bila ya kuzingatia mikakati yoyote ya kujikomboa. Kwa hivyo, imebainishwa kwamba, ukombozi wa jamii umo mikononi mwao na kilichohitajika ni kubadili mielekeo iliyopo la sivyo hakuna atakayelaumiwa. Mshairi ametumia kauli mbalimbali za lugha kuwa msingi wa uwasilishaji wa ujumbe. Katika shairi hilo, miongoni mwa kauli zilizotumika ni methali ya *Upatilize udongo, ungali na yake maji.* Kwa hivyo, dhima ya methali pamoja na baadhi ya kauli zingine za makusudi zilizotumika katika uwasilishaji, zimechanganuliwa ili kubainisha utendakazi wazo.

4.1.1.1 Methali kama Chombo cha Uwasilishaji wa Muhtasari wa Ujumbe

Mshairi angeitumia methali hiyo mwanzoni mwa shairi, uelekezi wa ufaraguzi wa mawazo ungekuwa bayana. Ingawa methali hiyo imejitokeza mwishoni mwa shairi, imekidhi mahitaji ya kuongoza katika kuibulia mawazo kiurejeleaji au kinyumenyume.

Kwa kuzingatia methali, mshairi ameweza kudokezea ujumbe kwa hadhira. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli teule ya kimapokeo huweza kutumiwa kama mbinu ya kuelekeza ujumbe ambao umeibuliwa na pia kuwa nyenzo ya kuibulia matukio yaliyowasilishwa (au dhana ya kufumbika muhtasari wa maudhui (Mulokozi 1986 na Fowler 1966). Katika uwasilishaji, mtunzi ametumia methali kama kauli mojawapo ya kimapokeo. Vile vile kwa kuirejelea nadharia ya Semiotiki, mtunzi wa fasihi hususa, ushairi ma nyimbo huzingatia kauli za kimapokeo ambazo hufasirika kupitia kwa vipengele vya utamaduni na uhalisi wa maisha ya watu (Mosha 2002 na Jacobson 1960). Kwa ufafanuzi zaidi wa ujumbe ambao umewasilishwa, msomaji huhitaji kurejelea maelezo na mifano ambayo imetolewa kuanzia mwanzo na kabla ya methali kujitokeza mwishoni mwa shairi. Kwa mfano, mshairi amebainsiha namna bara la Afrika lilivyoathirika na lilivyosambaratishwa kiuchumi, kisiasa na kijamii kutokana na msukumo wa nguvu zilizotoka nje. Mshairi ameitaka jamii ya Afrika isiwe *gizani* bali kuweza kufungua macho ili kung'amua mambo yaliyoisababishia kuathirika huko. Kwa sababu, maisha ya wenyeji yamekuwa ni vurugu na dhiki tupu.

Kulingana na maono yaliyosawiriwa, Afrika imedhikishwa kwa miaka mingi kiasi cha kuifanya *gutu* au mazoea ambayo huchukuliwa kuwa ni matukio ya kawaida. Aidha, matatizo hayo huweza kuhitimishwa iwapo jamii imeamua kukabiliana na hali hiyo kwa wakati wa sasa. Wenyeji wa bara la Afrika wamekuwa wakijitahidi katika kazi na shughuli za kijamii, kwa matarajio kuwa maisha yao yatakuwa nafuu; uwezekano huo haupo na afueni haijapatikani. Ingawa dhiki hizo zimeathiri pakubwa mfumo wa uchumi na maisha ya jamii, mshairi ameiona hali hiyo kuwa ni dalili tu ya maangamizi zaidi

ambayo huweza kujiri wakati wa usoni. Hiyo ndiyo sababu ya kuitaka jamii kufahamu kuwa, bara hilo limo katika lindi la masaibu ya hatari. Kwamba, Afrika imelemazwa kwa mielekeo hasi kutoka nje. Kwa hivyo, hakuna *jema* ambalo huweza kutokea katika bara la Afrika. Hayo ni baadhi ya mawazo ambayo huhitaji kutafakariwa na kufahamika ili Afrika kuweza kujikomboa kutoka kwa giza la maka na mikaka. Kwa hivyo, Afrika huhitaji kuwa na msimamo imara ambao ili kuweza kutambuliwa katika jumuiya ya ulimwengu kuhusu matakwa na kilio chake. Endapo jamii za Afrika zitastahabu kwa hali yake, kilio chake hakitasikizwa wala kujulikana. Kadhalika, Afrika kama jamii, hupaswa kuhoji kwa kudadisi kila jambo ambalo limekuwa kikwazo katika maendeleo yake kwa miaka mingi.

Ingawa mtunzi hakutumia methali kama anwani, maelezo ambayo ameyatoa yamefiki matumizi ya kauli msingi ambayo imejitokeza mwishoni mwa utungo. Hapa ifahamike kuwa, mtunzi huweza kutumia methali kama anwani, mwanzoni, katikati au mwishoni wa utungo. Kwa hivyo, umuhimu wa methali hutegemea zaidi pale ilipotumika. Aidha, mshairi amebainisha utaratibu na hatua ambazo hupaswa kuchukuliwa na jamii ili iweze kujinusuru kwa nakama hiyo. Hapa ibainike kuwa, ufaraguzi huo wa mawazo, umeweza kupitia kwa kauli zilizotumiwa kwa makusudi kama ilivyobainishwa. Kauli hizo zimesaidia katika kuishadidia methali iliyotumika katika shairi. Kwa kuzingatia methali iliyotumika, mshairi ameweza kuuwasilisha ujumbe kwa muhtasari.

Mshairi ameweza kukidhi haja hiyo kwa kuitumia methali kama kauli ya mwisho katika shairi. Endapo hadhira huhitaji ufafanuzi zaidi hubidi kurejelewa kwa uzingativu wa

mifano na maelezo ya hapo awali. Kwa mfano, mshairi alipotoa kauli kwamba, 'upatilize udongo, ungali na maji yake', ameweza kuufumba zaidi ujumbe uliowasilishwa. Kwamba, matatizo ambayo yamesakini katika bara la Afrika ni madogo na huhitaji kutafutiwa suluhu hivi sasa kabla hayajakithiri katika jamii. Kwa hivyo, matumizi ya methali yameunufaisha utungo huo kuwa chombo cha kuurejelea zaidi ujumbe uliofumbwa na uliowasilishwa kwa muhtasari na kwa utafakari.

4.1.1.2 Methali kama Kichocheo cha Kutafakarisha na Kuwasilisha Ujumbe

Katika utungo huo, ujumbe umewasilishwa kwa kauli za kimafumbo. Kwa hivyo, ujumbe huo huhitaji kufasiriwa na kusailiwa zaidi kwa uelekezo wa methali au kwa kauli mahususi zilizotumika. Isitoshe, usomaji haukamiliki pasi na kupata maana ambayo imewasilishwa katika shairi linalohusika. Shairi huweza kuwasilisha maana ya juu juu na maana ya ndani (Wamitila 2005). Ili msomaji kuweza kuelewa maana ya ndani, huhitaji kuzichambua tamathali za usemi zilizotumika, kuuchambua utata uliopo na kujaribu kuchunguza maana nasibishi za maneno, yaani maana nyingine ya ziada kuliko ile ya ambayo hueleweka kwa usahili.

Kwa ambavyo methali imetumiwa mwishoni mwa shairi, msomaji huwa katika hali ya kutafakari zaidi mawazo yaliyokwisha kuwasilishwa. Ingawa methali kama kauli imetumika kuashiria hitimisho la shairi, ingeweza pia kutokea popote pale katika shairi. Hapo awali, mshairi amezua mjadala wa msingi ambao umehusu masaibu yameikumba Afrika. Katika muktadha wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli ya msingi iliyotumiwa husaidia katika upataji wa dira ya kuufaragua ujumbe ambao huwasilishwa

katika utungo (Barthes 1981). Kwa mfano, mshairi amechukulia matatizo hayo ndiyo hasa chanzo cha dhiki barani Afrika. Kwa hivyo, Afrika bado imelala na wala haioni uhalisi uliopo. Hiyo ndiyo sababu ya mshairi kuitaka Afrika isiendelee *kuuangamiza utu* wake. Isitoshe, mshairi angependa jamii ya Afrika kuweza kutafakari na kusaili kuhusu hoja zilizoibuliwa. Vile vile, mshairi amekwisha kubainisha dhiki hizo kwa kutumia taashira za *kilema, tasa* na *chongo* kumaanisha kwamba, *mama* yu gizani. Suluhu iliyotolewa ni kwamba, Afrika inahitaji kutumia uwezo wake ili ijikomboe kutoka gizani na sauti hiyo isikike na jamii za kimataifa. Kimsingi, kauli au dhana teule ambazo hutumika zaidi katika tungo za ushairi ni zile zilizojengeka katika tamathali za usemi (Jacobson 1960). Kwa ambavyo mshairi hana muda mwingi wa kujieleza huchochea usaili na utafakari kupitia kauli za kiisitiari. Vile vile, dhana hizo hupata maana kwa kuzingatia utamaduni wa jamii. Kwa hivyo, maelezo ambayo yamewasilishwa yamesadifu katika kubainishia dhiki za Afrika. Aidha, msanii ameweza kueleza namna bara hilo huweza kujikwamua.

Katika muktadha wa matumizi ya methali, mshairi humtaka msomaji azingatie zaidi kuhusu mbinu mwafaka ambazo huhitajika ili Afrika isiweze kuendelea kuwa katika lindi hilo la masaibu hayo ambayo huirudishia nyuma maendeleo. Kwamba, matatizo hayo ya sasa ambayo yamesakini barani Afrika ni kama cheche za moto zifukazo. Cheche hizo huhitaji kuzimwa kabla ya moto haujawaka. Hiyo haimaanishi kuwa, matatizo ya Afrika ni madogo bali huhitaji kukabiliwa na jamii kwa hivi sasa la sivyo itakuja kujuta siku za usoni. Uhalisi wa mambo uliowasilishwa ni kwamba, kipindi ambacho jamii ya Afrika imekuwa katika matatizo hayo ni kifupi. Kwa sababu bara hilo limekuwepo, lipo na

litaendelea kuwepo kwa miaka na mikaka. Kwa hivyo, urekebishaji na usawazishaji wa dosari ziliyopo kwa wakati wa sasa, hustahili kufanyika mara moja kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Kadhalika, mshairi alipoitumia methali huweza kuchochea hadhira kujiuliza baadhi ya maswali, ambapo kwa pamoja, huwa msingi wa kufafanulia ujumbe ambao umewasilishwa katika shairi. Miongoni mwa maswali hayo ni kama:

- Matatizo ambayo huikumba Afrika ni ya kiwango gani?
- Ni hatua zipi ambazo hupaswa kuchukuliwa na jamii ili kuboresha hali hiyo?
- Hatua zitakazochukuliwa zitakuwa zenye manufaa gani kwa kizazi cha sasa na kijacho?

Maswali hayo huchochewa kutokana na uelekezo wa methali iliyotumiwa. Hiyo ni kwa sababu ya ufupi wa utungo huu na hoja sufufu ambazo huhitaji kuwasilishwa. Hata hivyo, ufupi wa shairi si kikwazo cha uwasilishaji wa ujumbe kikamilifu. Kwa mfano, kutokana na uibushwaji wa maswali hayo, hadhira huweza kuutanua zaidi ujumbe ambao umewasilishwa. Ingawa mshairi ameitumia methali mwishoni mwa utungo, huwa si mwisho wa kuutafakari na kuuendeleza ujumbe katika shairi. Kwa sababu, hadhira hurejeshwa kila wakati katika maelezo na mifano ya msingi iliyotumiwa katika uwasilishaji wa utungo. Kadhalika, maswali hayo, yaliyoibuliwa na kupitika katika akili ya hadhira, ni msingi wa kulifumbua fumbo lililofumbwa kupitia kwa methali.

4.1.1.3 Methali kama Mbinu ya Kuibulia Maudhui ya Uzindushi

Ingawa mshairi amebainisha matatizo ambayo yamesakini katika Afrika, uelekezo wa ujumbe uliowasilishwa umejikita katika kuibulia maudhui ya uzindushi wa jamii katika shairi. Mshairi ameiwasilisha Afrika kama ambayo bado *imelala* na katu haijafungua macho ili ione uhalisi wa chanzo cha masaibu yaliyopo. Kwa mfano, bara la Afrika limeungamiza *utu* wake na limo katika *kifo kisichokufa.* Kadhalika, bara hilo limedumazwa na limejilemaza kwa njia mbalimbali. Kulingana na mshairi, kiini cha matatizo ya kiuchumi na kijamii barani Afrika yamesababishwa na jamii yiyo hiyo. Kwa hivyo, suluhisho hupaswa kuzinduliwa katika jamii yiyo hiyo. Kwamba, jamii imekuwa na mielekeo isiyo ya msingi kuhusu namna ya kukabiliana na matatizo hayo. Kwa hivyo, mshairi ameshangaa kuiona Afrika kuwa imejilemaza ilihali ni bara lenye uwezo mkubwa wa rasilimali na utendakazi wa jamii si wa kupigiwa mfano. Mshairi ameashiria hayo, kwa kutongoa kuwa:

Umekuwa ni kilema
Kiwete tena u tasa
Kutozaa lilo jema
Wala dhuli kujiasa (Ubeti wa 5)

Kadhalika, maisha ya jamii na uchumi yamevurugwa kutokana na nguvu kutoka nje ya bara hili. Kulingana na mshairi ni kwamba, jamii ya bara la Afrika huhitaji kuzinduliwa na kuhamasishwa, la sivyo litabaki nyuma katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Sauti ya uzindushi pia imesikika kupitia kwa shairi la'Afrika na Watu Wake' (Kezilahabi 1974:19). Imesawiri kuwa:

Mimi naona mgonjwa
Bado amelala kitandani
Kama hatutamtoa miiba iliyobaki
Mgonjwa hataweka miguu yake chini
Ili kutembea bila kujiegemeza (Ubeti wa1)

Ujumbe huo pia umeashiriwa na kujitiokeza katika shairi la 'Usijiangamize'. Hayo ni masaibu ambayo huikumba na kuiyumbisha Afrika. Hata hivyo, hayo hayakupaswa kuwepo wala mwenyezi Mungu hakuleta majaliwa hayo bali yamesababishwa kutoka nje. Mshairi haoni mwafaka wowote wa Afrika kuendelea kubaki katika kaburi hilo la matatizo. Hiyo ndiyo sababu ya kusisitizwa kuwa:

> *Inuka mama inuka*
> *utoke mwako gizani* (Ubeti wa 6)

Katika muktadha wa dondoo hilo, jamii ya Afrika huhitaji kuzinduka ili ichukue hatua ya haraka ya kujinasua kutokana na matatizo hayo yanayoisakama. Endapo *mama* Afrika hatachukua hatua hiyo, basi huenda akabaki nyuma kimaendeleo. Kutokana na methali aliyotumiwa, mshairi ameweza pia kubainisha kiwango chake cha ufahamu wa matatizo ambayo yameizinga jamii. Katika harakati za kubainisha uhalisi wa maisha na kutoa suluhu, ushairi wa Kiswahili huwa ni chombo cha kuizindua jamii (Wamitila 2001 na Chacha 1987). Kwa hivyo, mshairi amekuwa ni mwalimu, tabibu na mzalendo ambaye hueelewa kiini cha matatizo ya bara la Afrika na aghalabu hupendekeza tiba mwafaka ya matatizo hayo. Kwamba, tiba ya maradhi hayo ya *Mama* hustahili kutoka ndani na wala si nje. Hiyo ndiyo sababu ya kusisitizwa kuwa, *mama* asijiangamize ilihali ana uwezo wa kujiopoa katika maangamizi yaliyotokana na athari za ukoloni-mamboleo.

Hapo awali na kabla ya kutumia methali hiyo ya *upalilize udongo ungali na maji yake*, tayari imebainishwa namna Afrika ilivyoathiriwa. Kwa njia hiyo, msomaji amekuwa amejengewa taswira ya masaibu hayo. Aidha, msomaji huweza kuelewa mbinu ambazo huhitaji kuchukuliwa ili jamii kuweza kubadilisha hali na mielekeo hasi iliyopo. Kwa

kutumia methali hiyo mwishoni, msanii ameweza kuukoleza zaidi ujumbe wa uzindushi. Kwamba, matatizo yaliyopo katika bara la Afrika, huhitaji kutafutiwa suluhu siyo kwa kusubiri bali wakati uliopo wa sasa. Aidha, jamii ikisitisha kuhoji au ikiamua kuridhi hali ilivyo haitakuwa imejitendea haki na matokeo yatakuwa ni kujidunisha na kukwamisha maendeleo ya msingi barani Afrika.

4.1.1.4 Methali kama Chombo cha Kubainishia Itikadi na Mwelekeo wa Mtunzi

Mshairi ametumia methali kuwa chombo cha kuyakinisha na kuwasilisha mwelekeo wake kuhusu matatizo ambao huinyonga na hukwamiza maendeleo ya jamii barani Afrika. Kwa hivyo, kama mwalimu na mwanafalsafa, amefahamu kiini cha matatizo hayo na tayari yameyabainishwa kwa maelezo yaliyotolewa katika shairi. Mtazamo ambao umewasilishwa ni kwamba, Afrika haijakuwa na mwamko mwafaka wa kisiasa wala kujenga mwelekeo chanya wa kuzindua hatua ambazo hupaswa kuchukuliwa ili kuukwamua uchumi. Kwamba, jamii ya Afrika haijui iwapo matatizo yaliyopo yameudunisha utu au maisha hayo. Mwelekeo wa mtunzi umejitokeza pia kupitia kwa *kifo kisichokufa*. Kulingana na mawazo na mwelekeo ambao umewasilishwa, jamii ya Afrika huhitaji kufahamu kuwa imejilemaza yenyewe kwa kukosa jicho angavu haliwezi kubaini matatizo hayo. Mwelekeo sawia na huo umejitokeza pia katika shairi la 'Jicho Geni' (Mohamed 2002:45) Kwa hivyo, matatizo yaliyopo ni dhahiri, lakini jamii haitaki kubaini hayo wala kuchukua hatua ya haraka za ukombozi.

Kulingana na nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli teule zilizotumika katika uwasilishaji wa tungo za kifasihi, ni zile ambazo hupatikana katika mapokeo ya jamii

(Parry 1971). Kwa hivyo, ujumbe ambao umewasilishwa umejikita katika busara inayoibuliwa na jamii. Kauli hizo zilizotumika huuweka ujumbe unaowasilishwa katika muktadha wa utamaduni wa jamii kwa hivyo hauwezi kuelekezewa kidole cha lawama (Mulokozi 1986). Kwa kuzingatia methali, mshairi haoni namna nyingine ya kukabiliana na matatizo hayo isipokuwa kujitolea kwa dhati ili kubadili na kurekebisha hali hiyo. Kwa hivyo, mshairi haridhishwi na mwelekeo wa jamii ya Afrika kwa kustahabu kuishi maisha ya *kifo* kisichostahili. Kimsingi, maisha hayo hayatoi mwanya wa kuututumua na kuendeleza uchumi uliopo. Kama ilivyotongolewa kuwa:

Ni kifo kisichokufa
kiishicho na miaka
kuzikwa haujafa
pasi nawe kuzikika (Ubeti wa 3)

Kutokana na kauli hiyo, mshairi amebainisha muktadha wa kukatisha tamaa. Kwa hivyo, mshairi haoni matumaini yoyote katika maisha ya jamii ya Afrika isipokuwa kwa kuchukua hatua ya dharura ya kuukomboa uchumi huo. Kadhalika, imani ya mshairi imejitokeza kupitia kwa kauli mahususi zilizotumiwa na hasa kupitia kwa methali, kwamba: matatizo hayo ya Afrika yamesababishwa na uzembe wa jamii na nguvu kutoka nje ya bara hili. Hiyo ndiyo sababu ya kusawiriwa kuwa:

Usiwe mwenye chongo
Kutoona, kutohoji (Ubeti wa 7)

Kwa hivyo, jamii ya Afrika hupaswa kufungua macho la ndani ili ijionee madhila na dhiki imepata au imepatishwa na huhitaji kutafuta dawa au mbinu za kukabiliana na hali hiyo. Kwa ambavyo Afrika imechukuliwa kuwa ni *chongo* na *kilema,* inamaanisha kuwa bado ina uhai na uwezo wake ungalipo. Aidha, jamii ya Afrika ina uwezo wa

kubadilisha hali ya uchumi na maisha hayo pindi itakapokuwa na ari ya kufanya hivyo. Kama ilivyosisitizwa kuwa:

Inuka mama inuka
utoke mwako gizani (Ubeti wa 6)

Taswira ambayo imejengwa katika dondoo hilo ni kuhusu jamii ya Afrika ambayo imeathirika vibaya. Jamii hiyo huhitaji kuzizoazoa na katu isikate tamaa ili iweze kujitoa katika matatizo yaliyopo. Kimsingi, jamii ya Afrika ina uwezo wa kuboresha maisha hayo. Kulingana na mshairi, matatizo hayo bado hayajaota mizizi sugu. Kwa hivyo, mizizi hiyo huweza kuchimbuliwa na kutupiliwa mbali ili jamii ya Afrika ipate ahueni. Kwa kutumia methali hiyo, msanii ameisawiri Afrika kama bara lisilojua athari ya matatizo yaliyopo wala mbinu zilizohitajika kutumika katika kusawazisha matatizo hayo. Kwa sababu, jamii ya Afrika ni kama ambayo huyaona matatizo hayo, kuwa ni majaliwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu na inapaswa kuishi nayo. Mwangwi wa mawazo hayo yamejitokeza pia katika shairi, 'Zindukani' (Abdalla 1973: 69-72)

Kinyume na mtazamo huo, mshairi ameyaona matatizo hayo kama yaliyosababishwa kuwepo kwake na huhitaji kuondolewa kwa juhudi zake pasi na kutarajia miujiza (Thiong'o 1986). Kwa hivyo, mshairi hataki au hapendi jamii iendelee kudhikishwa zaidi ilihali uwezo upo. Katika muktadha huo, baadhi ya maswali yafutayo huweza kuibuliwa:

- Ni haki jamii ya Afrika kuwa *kilema* au imelemazwa?
- Ni halali kwa jamii ya Afrika kuwa *gizani*?

- Ni hatua zipi hupaswa kuchukuliwa na jamii ili *wasiuangamize* na *kuudunisha* utu wao?

Majibu ya maswali hayo yamedokezewa kwa uelekezi wa methali iliyotumiwa mwishoni mwa shairi. Mshairi hakubaliani na mwelekeo hasi wa jamii ambayo haitendi lolote la manufaa katika kuboresha hali ya maisha. Kutokana na methali hiyo ya *upatilize udongo ungali na yake maji*, mshairi huitaka hadhira au jamii ya Afrika ibaini uhalisi wa maisha uliopinda ili ichukue hatua mwafaka yenye uelekezi, kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Kulingana na mshairi, jamii katika bara la Afrika imekuwa ikijiangamiza pasi kujua, sasa linahitaji kuwa macho na kuchukua hatua mwafaka kurekebisha dosari iliyopo kabla ya chombo hakijaenda mrama. Kwa hivyo, itikadi ambayo imepitishwa katika shairi ni kuwa, jamii ya Afrika ina uwezo lakini bado haijatambua. Kwa sababu hiyo zimeendelea kuwa nyuma kimaendeleo.

4.1.1.5 Methali kama Mbinu ya Ujenzi wa Upeo wa Juu

Shairi hili limesawiri matatizo mbalimbali ambayo yamelisakama bara la Afrika. Maelezo kuhusu swala hilo ni ya kina, kuanzia mwanzo hadi mwisho wa shairi. Kwa mfano, dhiki mbalimbali zimebainishwa. Mambo hayo yameusambaratisha mwafaka wa mfumo wa jamii na maendeleo ya kiuchumi barani Afrika. Kwa hivyo, hadhira haipati tatizo katika kuelewa usuli wa matatizo hayo kwa uzingativu wa mwelekeo wa mshairi.

Kadhalika, mshairi ameweza kuibua na kusuka vitushi hadi kufikia upeo wa juu katika shairi. Kwa mfano, ameeleza kwamba, jamii ya Afrika huhitaji kufungua macho ili ibaini *giza* katika uhalisi wa maisha na matatizo hayo, kama alivyosema kuwa: *Afrika macho*

angaza. Kauli hiyo, imedhihirisha na imebainisha kilio na matamanio kuhusu mwelekeo hasi wa jamii ya Afrika kuhusu namna hukakabiliana na matatizo hayo. Katika muktadha huo, mshairi ameilaumu na ameilekezea kidole cha kuisuta jamii ya Afrika. Kwamba, haijatambua mbinu mwafaka zilizohitajika kutumika katika ukombozi wa uchumi na uimarishaji wa maisha. Baada ya kufanya hivyo, ameitanabahisha jamii kuwa, kufanya hivyo ni *kuuangamiza utu*. Kulingana na mawazo ya mshairi ni kwamba, maisha hayo duni ni kama ... *kifo kisichokufa na kuzikwa hai hujafa*. Kwa hivyo, mshairi huitaka jamii ya Afrika ibaini kuwa *i kilema*, *kiwete* na *tasa*. Dhana hizo tatu zimewasilishwa kitaashira, ambapo mshairi hutarajia ujumbe uwe wa kimaono na kuitafakarisha zaidi hadhira yake. Wakati huo ndipo ufaraguzi wa ujumbe umefikia kilele. Kinachotarajiwa na msomaji, ni kuelezwa hatua au mwelekeo uliopaswa kuchukuliwa na jamii iliyosawiriwa.

Endapo mshairi angeishilia katika kauli au dhana hizo tatu, kiu ya msomaji ingekuwa bado haijakatika. Kwa mfano, katika muktadha huo hadhira huweza kuchochewa kujiuliza maswali yafuatayo:

- Jamii ya bara la Afrika itaendelea kustahabu kuwa vivyo hivyo daima dawamu?
- Jamii ya bara la Afrika itafanya nini baada ya kuzinduliwa?

Hayo ni baadhi ya maswali ambayo huweza kumpitikia msomaji kutokana na usawiri na ubainishaji wa maelezo yaliyodokezewa na yaliyotolewa. Hiyo ndiyo sababu ya kutolewa kwa kauli nyingine kuwa jibu la maswali hayo, kwamba:

inuka mama inuka
utoke mwako gizani (Ubeti wa 6)

Katika muktadha huo, mshairi huitaka jamii ya Afrika iwe yenye mwelekeo dhibiti usiotetereka na ijitoe muhanga ili kuyakabili matatizo yaliyopo. Kwa kufanya hivyo, ndipo kilio cha jamii ya Afrika kitasikika miongoni mwa mataifa ya ulimwengu.

Kadhalika, mshairi ametumia methali hiyo kuwa fingo la shairi na pia kuwa kienzo cha muhtasari wa ujumbe ambao umewasilishwa. Kwamba, matatizo yaliyopo katika jamii ya Afrika huhitaji kukabiliwa kwa wakati uliopo badala ya kungojea wakati ambapo yakawa sugu zaidi au makubwa yasiyowezekana. Ingawa, msomaji huachwa katika hali ya kutafakari, kufahamikiwa kuwa mshairi ameutamatisha ujumbe wake. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, uwasilishaji wa utungo hupaswa kuzingatia utaratibu maalumu kama vile utangulizi wenye mshindo, ufaraguzi wa vitushi na kuuhitimisha ujumbe ambao umewasilishwa kwa kutoa muhtasari au kwa kuielekeza hadhira kufahamu kuwa, hicho ndicho kiishilio (Propp 1968). Katika muktadha wa shairi, methali imetumika kama kauli ya kuhitimisha ambayo pia kuchochea zaidi usaili na utafakari. Kwa sababu hiyo, msomaji hulisoma shairi kwa utaratibu na kwa matao ya chini.

4.1.1.6 Ujenzi wa Usambamba Kutokana na Matumizi ya Methali

Katika shairi hili, mshairi ametumia methali kama mbinu msingi ya kuibulia kinyumenyume miundo mbalimbali ya lugha ambayo imeutawala na imeukariri ujumbe. Kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli msingi zinazotumika hupaswa kuudhibiti muundo au umbo la utungo wa shairi. Kauli kama hiyo huhitaji kutumika mwanzoni mwa utungo kama vile anwani au sentensi msingi.

Kwa kufanya hivyo, msomaji au msikilizaji huweza kujuatilizia mtiririko wa vitushi kwa urahisi (Whallon 1969). Ingawa mtindo huu umetumiwa, methali imezingatiwa kama kauli ya mwisho katika utungo. Hata hivyo, kwa kuzingatia mantiki ya nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, usambamba au ukariri wa ujumbe huelekezwa kutoka chini au mwishoni mwa utungo. Kwamba, msomaji huweza kuupata ukariri wa kauli zilizotumiwa katika uwasilishaji kutokana na methali iliyohusishwa. Kimuundo, jambo hilo hudhihirika mno katika ushairi ambao huzingatia arudhi.

Katika utungo huu, maudhui yamekaririwa kinyumenyume au kisa kinachowasilishwa kupitia kwa kauli msingi zilizoundwa kutokana na uwepo wa methali hiyo. Ingawa methali hiyo imetumiwa kama kauli ya kuhitimisha, mwangwi au athari hiyo huhisika katika shairi. Kimsingi, mshairi ameufafanua kwa kina ujumbe wake kuanzia mwanzo hadi mwisho wa shairi. Kwa mfano, katika beti nne za mwanzo mshairi amebainisha dhiki zilizosakini barani Afrika. Katika beti mbili za mwisho, msanii amefafanua zaidi mwelekeo na hatua ambazo hupaswa kuchukuliwa. Mawazo hayo yamewasilishwa kitaashira, kiisitiari na kwa kutumia mbinu ya usambamba. Kwa mfano, imesawiri kuwa:

(i) *Afrika macho angaza*
uwache kiwayowayo (Ubeti wa 1)

(ii) *Inuka mama inuka*
utoke mwako gizani
Inuka ukilimka
usikike hadharani (Ubeti wa 2)

(iii) *Usiwe ni mwenye chongo*
kutoona, kutohoji (Ubeti wa 3)

(iv) *Upatilize udongo*
ungali na yake maji (Ubeti wa 4)

Kwa hivyo, katika kauli hiyo ya (i), mshairi ameihimiza jamii ya bara la Afrika kuweza kufufungua macho ili ibaini uhalisi wa dhiki zilizopo na iache kunung'unika. Katika kauli ya (ii), ameisihi jamii ya Afrika kutumia nguvu na juhudi ya asili katika kujinasua kutokana na matatizo yaliyopo.

Vile vile, mshairi ameitaka jamii ya Afrika isinyamaze na kustahabu kwa matatizo hayo. Kwa sababu, mataifa mengine ya ulimwengu hayawezi kuhisi wala kuelewa shida za Afrika bila ya jamii hiyo kubainisha matamanio au kilio chake. Kwa hivyo, mshairi huitaka jamii ya Afrika kuelewa kuwa *i gizani* na inapotaka kupata mwangaza au maendeleo ya kiuchumi, ni sharti kuweza kujikakamua kwa wakati wa sasa na katu isingojengoje.

Kadhalika, katika kauli ya (iii) imeisawiri jamii ya Afrika kama iliyolemazwa, yaani, *i kilema* na *chongo* kwa sababu ya kutotaka kuhoji wala kusaili kiini cha matatizo yaliyopo. Kwa kuhitimisha mifano na maelezo yaliyotolewa, mshairi ametumia kauli (iv) ambayo ni methali. Hapa ieleweke kuwa, methali hiyo imetumiwa pia kama kauli ya msingi iliyofafanuliwa kwa kuzingatia baadhi ya miundo mingine ya lugha kama ile inavyodhihirika katika (i), (ii) na (iii). Kwa ambavyo imejitokeza mwishoni, huweza pia kuchukuliwa kiusambamba kuwa ni kauli mojawapo katika uwasilishaji wa utungo. Kwamba, kauli zilizotumiwa huenda zikawa zimeibulia na zimeukoleza ujumbe mmoja au kauli tofauti za kushadidia zaidi wazo kuu. Kwa sababu hiyo, mshairi amezipa kauli hizo zingine nafasi ya kuchangia dhima ya methali. Kwa hivyo, hadhira huweza kuichukulia kauli yoyote ile iliyoibuliwa katika shairi kuwa msingi wa ujenzi wa

usambamba katika shairi. Katika muktadha huo, mshairi humtaka msomaji kuzichukulia kauli hizo zote zilizotumika kama kunga za ukariri na kuudhihirisha zaidi ujumbe uliowasilishwa. Hata bivyo, methali iliyotumika huweza kujenga mazingira au kichocheo cha kuibulia kauli za kiusambamba katika shairi.

4.1.1.7 Methali kama Mhimili wa Muundo na Wizani

Mshairi ameitumia methali iliyopo kama nguzo mojawapo katika ujenzi wa muundo katika usawiri na uwasilishaji wa shairi hili. Kama mshairi angeitumia methali hiyo mwanzoni (ambapo si lazima katika muktadha uliopo), hadhira ingefahamikiwa kabla kuwa ni nyenzo ambayo imeongoza katika uibuaji wa muundo wa shairi. Katika uwasilishaji wa utungo huo, matumizi ya methali yamepewa nafasi muhimu katika unzi na uwasilishaji. Aidha, matumizi hayo huwa ni sawa na kauli ambazo hutumiwa kwa makusudi. Jambo hilo limeashiria kuwa kuna kauli zingine za lugha ambazo zimechangia methali katika kutekeleza jukumu hilo.

Kimuundo, mshairi hakuwa na shuruti yoyote ya kufanya hivyo ila kwa kuzingatia kwa makusudi uwasilishaji wa shairi hili kinyume nyume. Kwa ambavyo methali imetumiwa mwishoni mwa shairi; kimantiki imeweza kuongoza mshairi katika kuibulia mishororo ambayo imeafiki muundo wa methali katika utungo uliowasilishwa. Kwa hivyo, kimuundo matumizi ya methali si bayana, kimtindo imeshikilia nafasi muhimu katika shairi. Kama kielekezo cha utunzi, mshairi ametumia baadhi ya miundo sawia ya lugha kwa malengo ya kuafiki muundo wa methali hiyo iliyotumika. Kwa mfano katika shairi, mishororo iliyotumika ni ya mizani nane. Kwa hivyo, shairi lina idadi maalumu ya

mizani lakini halikugawanyika katika sehemu mbili: ukwapi na utao. Beti za shairi zinapopanguliwa hubainisha kuwa, mishororo imegawanyika katika sehemu hizo mbili muhimu. Kwa mfano, ubeti wa mwisho katika shairi huweza kupangwa ifuatavyo:

usiwe mwenye chongo, kutoona, kutohoji

upatilize udongo, ungali na yake maji

Katika kuzingatia mpangilio wa dondoo au ubeti huo, mshairi ameweza kupata mshororo kamili kutokana na methali ya:

Upatilize udongo, ungali na yake maji

Hapa ieleweke, kuwa neno *yake* limehamishwa kutoka mwishoni mwa mshororo ili shairi liwe na urari wa vina. Kwa hivyo, ubeti huo una kina cha ndani [*ngo*] na cha nje **[-*ji*]**. Kwa kuupangua muundo wa methali hiyo, mshairi amejipa uhuru wa kusarifu miundo ya lugha katika uwasilishaji wa shairi. Kwa ambavyo mshairi hakutumia kiakifishi **[,]** ili kubainisha mwisho wa ukwapi, hadhira nayo huweza kuhisi athari yake wakati wa usomaji wa shairi. Kwa kufanya hivyo, kumelipa shairi hili muundo ambao si sawia na ule wa kimapokeo. Kwa hivyo, shairi linalozingatiwa huweza kuwa la kati ya ushairi wa kimapokeo na ushairi huru.

4.1.2 Shairi: Hasira Hasara?

Utungo huu, ni miongoni mwa mashairi mafupi katika diwani hii ya *Chembe cha Moyo*. Shairi hilo lina beti mbili, ambapo ubeti wa kwanza una mishororo au mistari mitatu ilihali ubeti wa pili una mishororo saba. Shairi hilo limesawiri namna wanajamii wanavyohofu kuibua *hasira* kuwa chombo cha kutetea haki. Kwa sababu ya kuhofia madhara ambayo huweza kusababishwa na hasira. Kadhalika, wanajamii wamekuwa

wakitumia utu katika kukabiliana na mahasimu wao. Kulingana na mshairi ni kwamba, *hasira* huweza kutumiwa kuwa silaha au chombo cha jamii kinachotumiwa katika kusuluhishia matatizo hayo. Katika shairi hilo, mtunzi ametumia methali ya *Hasira Hasara?* na kunga zingine za lugha kuwa nyenzo ya kuwasilishia kama itakavyobainishwa hivi punde.

4.1.2.1 Methali kama Msingi wa Kuibulia na Kuwasilishia Mawazo

Mshairi ameitumia methali hapo mwanzoni kama anwani katika shairi. Zaidi ya hayo ametumia kiakifishi [?] mwishoni mwa methali. Kimsingi mshairi ameitaka methali hiyo kueleweka kama fumbo au swali ambalo huhitaji jibu. Kwa hivyo, mshairi amejenga malumbano au usemezano wa kinafsia na ule wa kusemezana na hadhira (Karama 1996 na Njogu 1993). Katika muktadha wa maisha ya watu, *hasira* ndiyo husababisha *hasara,* lakini mshairi amekuwa mwelekeo tofauti kuhusu dhana ya *hasira.* Kwa kuzingatia ubeuzi wa methali, mshairi ameweza kuibua na kufaragua mawazo katika muktadha huo. Matumizi ya kiakifishi [?] yamemfanya mtunzi kuipa miundo ya lugha iliyozowewa, mtazamo mpya (Zubkova-Bertoncini 2008 na Gromov 2006). Kwa hivyo, methali si sugu bali huweza kufanyiwa marekebisha madogo madogo kulingana na hisi za msanii. Mawazo ya mshairi ni kwamba, baadhi ya watu huwa na mwelekeo hasi dhidi ya *hasira.* Hata hivyo, mshairi haoni dosari yoyote kwa mtu kuzingatia *hasira* iwapo ametumia utu katika kuidai haki hiyo ilihali hakuna yeyote katika jamii ambaye humtilia maanani.

Kwa kuitumia methali hiyo kama anwani, mshairi ameweza kudokezea kabla mwelekeo ambao umechukuliwa katika uwasilishaji wa ujumbe katika shairi. Kwa hivyo, matumizi

hayo yamejenga mazingira yaa upokezi wa mawazo ambayo yanawasilishwa. Kwa mfano, mshairi ameukariri ujumbe kwa kusema:

Ayi, Hasira, uweje kwangu hasara
iwapo dhuli ndiyo yangu tijara
ilonishambulia ja simba marara
ikanichanachana kama tambara
Basi Hasira, kwangu uweje, Hasara?(Ubeti wa 1)

Kutokana na dondoo hilo, mshairi tayari amebainisha kuwa *hasira* haidhuru na wala haina ubaya wowote kwake. Kwa sababu ustahimilivu haujamfaidi kamwe katika maisha hayo. Kwa hivyo, methali hiyo imesaidia katika kufaragua na kusarifu zaidi mawazo yaliyohusu mambo mawili: *hasira* na *hasara.* Ni katika muktadha huo ndipo msanii amejenga kisa ambacho kimedhihirisha ukweli wa kauli aliyoitumiwa.

Kulingana na nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli teule za kimapokeo hutumiwa kuwa chombo cha kuibulia mawazo katika tungo (Mitchell na Naggy 2000). Kwa ambavyo mshairi ameitumia methali hiyo kabla kama anwani, hakupoteza muda bali ameingia moja kwa moja katika kuendeleza mawazo ambayo yanawasilishwa huku akizingatia mifano na maelezo mbalimbali iliyohitajika. Kwamba, kwa kipindi kirefu mshairi amekuwa akiathirika mno kutokana na uendekezaji wa utu na ungwana kama mbinu ya kusuluhisha matatizo hayo. Pia, hajawahi kupata manufaa yoyote katika kukabiliana na matatizo hayo kwa kuzingatia utu.

Kwa namna moja, mshairi ameitumia kauli hiyo kudhihirishia hisi alizonazo kutokana na tajiriba yake. Kwa hivyo, kauli ambazo hutumiwa katika tungo, huteuliwa kwa hadhari kubwa ili mawazo kuweza kuwasilishwa ipasavyo (Karama 1985). Hata hivyo, mshairi

ana mawazo kwamba, utu una manufaa hasa kwa mtu ambaye ni mstahimilivu na msikivu, lakini si kwa mtu ambaye hataki kutenda haki kama ilivyotarajiwa katika jamii. Kadhalika, mshairi hupata ilihamu ya kubainisha mwelekeo wake kuwa njia ya pekee ya kuidai haki dhidi ya yule au wale ambao hudhikisha. Kwa hivyo, njia mwafaka aliyoibua ni kwa kuzingatia *hasira* ili kuweza kusikika. Kwa kutumia kiashiria cha kiulizi **[?]**, mshairi huitaka hadhira ijaribu kufikiria na kutathmini zaidi kuhusu mwelekeo ambao huchukuliwa na baadhi ya wanajamii kuhusu *hasira*. Kwa mfano, mshairi amezua swala la msingi kuwa:

- 'Hasira' itakuwaje mbaya iwapo hapati mustakabali wake?

Kulingana na mshairi ni kwamba, *hasira* ndiyo itakayomwauni na hata kama haitamfaidi hataweza kupoteza chochote. Kwa hivyo, kama atapoteza kilichotarajiwa, hali ya maisha yake itakuwa ni ile ile tu. Hiyo ndiyo sababu ya kuisujudia *hasira* kwa kusisitiza kuwa:

Ndipo Hasira nikakusujudia
Hasira ya myaka nilokuvumbika
ulojaa hasira isoburudika
uje uongoe pa mwisho kufika
unipe mahali palipo laika
na kunizimia kiza cha miaka
Kiza cha maisha kilotapakaa (Ubeti wa 2)

Kutokana na methali mahususi ilivyotumiwa, mshairi amepitisha ujumbe kwamba, *hasira* ni silaha ya mwisho ambayo binadamu huweza kuitumia endapo hapana budi. Hapa ieleweke kuwa, mshairi kama mhusika katika shairi amekuwa akitumia busara na utu katika kuidai halali yake lakini hakuna chochote alichoambulia katika maisha. Kwa ambavyo matatizo yake hayajazimwa, ameamua kutumia hasira ambayo ameitarajia kuwa itampa mahali palipo laika na kumzimia *kiza cha miaka*.

Kwa kutumia kielekezi cha kiulizi katika methali, ujumbe unaowasilishwa unakuwa ni ubeuzi wa ule uliofumbwa katika busara ambayo hupatikana katika kauli hiyo. Msomaji kwa upande wake hutarajiwa kuufasiri ujumbe ambao umewasilishwa kwa kuzingatia ubeuo wa methali hiyo; vinginevyo sivyo. Kadhalika, methali imetumiwa kuwa dira mwafaka ya kuibulia na kufafanulia mifano na maelezo yaliyohitajika katika shairi. Isitoshe, maneno hayo yamerudiwa kwa makusudi katika uwasilishaji wa shairi. Ukariri huo, umemfanya mshairi kuubainisha ujumbe unaowasilishwa kujikita katika dhana ya maneno hayo mawili ya msingi: *hasira* na *hasara*. Kwa hivyo, ukariri huo wa maneno yayo hayo usichukuliwe kuwa mshairi amekuwa mufilisi au hajaudhibiti sawa sawa msamiati uliotarajiwa katika kuubainishia ujumbe uliokusudiwa. Katika muktadha wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi Parry (1971) amesisitiza kuwa, ukariri wa kauli maneno au sauti usichukuliwe kama udhaifu wa mtunzi bali ni mbinu ya kiuwasilishaji na ya kuibulia ujumi katika utungo. Kimsingi, mshairi ameutumia ukariri huo kama mbinu ya kuibulia ridhimu na mdundo mahususi uliostahiki katika uwasilishaji wa shairi. Isitoshe, matumizi ya methali hiyo umemfanya mshairi kuibulia mifano na maelezo ya msingi ambayo yamesaidia katika ukariri na ukolezaji wa ujumbe umewasilishwa. Katika muktadha huo, mshairi amesaili kwa ustadi kuwa:

Ni kwa nini *hasira* iwe kwake ni *hasara?*

Kimsingi, huo ni mwelekeo wa mawazo ambayo hushikiliwa kiholela na kuendelezwa pasi na kusailiwa katika jamii. Kwa kutumia methali kama msingi wa uwasilishaji, mshairi ameweza kuibulia kauli zingine ambazo zimechangia uzito wa kiuchambuzi

katika shairi. Kifasihi, marudio au ukariri huo hubaika kiusambamba (Senkoro 1988). Katika ubeti wa kwanza kuna kauli zifuatazo:

- *Ayi Hasira, kwangu uweje Hasira?*
- *Basi Hasira, kwangu uweje Hasira?*

Katika dondoo hilo, mshairi haoni ubaya wa hasira endapo stahamala na ushauri wa kiungwana hautiliwi maanani. Kadhalika, katika ubeti wa pili, mshairi ametilia mkazo hoja hiyo ya awali kuwa:

Ndipo Hasira nikakusudia
unipe mahali palipo laika
na kuuzimia kiza cha miaka (Ubeti wa 2)

Kupitia kwa dondoo hilo, mshairi amedhihirisha na ameyakinisha kuwa, *hasira* alikuwa nayo lakini hakuwa ameitumia kwa vile alielewa madhara yake katika jamii. Hata hivyo, mshairi kama mhusika ameitumia *hasira* kwa vile hana njia nyingine ya kuitetea na kuikomboa haki ambayo ni *laika* yake katika jamii. Kwa kuendekeza zaidi utuvu na staha, kumemkosesha murwa katika maisha yake. Kupitia kwa usambamba katika uwasilishaji wa mawazo, mshairi amejidhihirisha kuwa mweledi wa kuisarifu miundo ya lugha iliyomruhusu kujieleza na kujifaragua pasi kutindikiwa.

4.1.2.2 Methali kama Mbinu ya Kuibulia Usaili na Utafakari

Shairi hili limesawiriwa kiisitiari na kimafumbo kwa malengo ya kusaili na kuchochea utafakari katika akili ya hadhira. Kama anwani, methali imetumia alama ya kiulizi [?] mwishoni mwake. Kwa hivyo, mshairi ameikaulisha methali, ili iwe ya kibalagha. Kadhalika, mshairi ametumia alama hiyo ya kiakifishi katika mojawapo ya kauli kama ilivyodhihirishwa hapa:

Basi *Hasira,* kwangu uweje *Hasira?* (Ubeti wa 1)

Katika muktadha huo, mshairi ameitumia alama hiyo ya kiulizi kwa makusudi ili iwe dira ya kuongoza katika usomaji na upokezi wa ujumbe. Kwa hivyo, mshairi ametilia shaka busara ambayo huibuliwa kupitia kwa methali hiyo na pia kuifanya ieleweke hivyo kwa hadhira kusudiwa. Kwa kutumia alama hiyo, ameifanya kauli hiyo kuwa yenye kutekeleza mambo mawili katika shairi: uchimuzi wa mawazo na kubainisha zaidi mwelekeo wa hisi aliyonayo kuhusu tajiriba hayo katika maisha. Kauli hiyo huweza kuwa ni methali au ni zile ambazo huibuliwa na kutmika kwa makusudi katika shairi. Iwapo kauli hiyo imechukuliwa kuwa si ya kimethali, mantiki ambayo imeibuliwa imeukoleza zaidi ujumbe uliowasilishwa. Ingawa mshairi ameujenga ujumbe kwa kuzingatia ubeuzi wa mantiki ya methali ili kupanua upeo wa kiufasiri na kiupembuzi. Isitoshe, mshairi ameuzua mdahalo mkubwa wa kiusaili wa ndani kwa ndani baina yake na nafsi yake. Mdahalo huo umehusu *Hasira* na *Hasara* umebainishwa zaidi katika ubeti wa awali katika shairi. Kupitia kwa kauli hiyo, mshairi amesaili kuwa:

- *Hasira* huwezaje kuwa hasara kwake?
- Kwa nini *Hasara* imemwathiri ja *simba marara*?
- Kwa nini *Hasira* imemchanachana kama *tambara*?

Kupitia kwa maswali hayo, mshairi ameweza kuusaili moyo wake. Hata hivyo humtarajia msomaji kujiuliza baadhi ya maswali kama vile:

- *Hasira* ya mshairi itamfikisha vipi *mahali palipo laika*?
- *Hasira* ya mshairi itamzimia vipi *kiza cha miaka*?

Hayo ni baadhi ya maswali fiche ambayo yamezuliwa na yamewasilishwa kwa ubunifu ili yametumika kuwa kichocheo cha usaili na utafakari. Kwa ambavyo mshairi hataki hadhira ijikune kichwa zaidi, ametoa jibu katika ubeti wa pili katika shairi hili. Kwamba, kwa muda mrefu amekuwa akiizuia *hasira* lakini kwa sasa hana jingine. Kutokana na maelezo yaliyowasilishwa ni kwamba, *hasira* inapozingatiwa huenda ikamfaidi hata ingawa hufahamu fika madhara yake. Kwa sababu ya kutumia kauli ya usaili, msomaji au msikilizaji huwa ni hadhira tendi katika uwasilishaji wa ujumbe katika shairi. Kimsingi, hiyo ni mbinu ambayo hutumiwa zaidi katika uwasilishaji na upokezi wa baadhi ya tanzu za fasihi simulizi kama vile ngano (Njogu 2006). Ingawa shairi hili limeshirikisha beti mbili tu, ambazo kwa hakika ni chache, ujumbe uliwasilishwa ni mpana ambao huhitaji kufafanuliwa kwa kuzingatia mdokezo wa maswali yaliyoibuliwa kupitia kwa methali iliyotumiwa. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, utungo wa ushairi hushirikisha pande mbili; msimulizi na mpokezi (Barthes 1973). Baina ya pande hizo huwiana. Kwa sababu, kuna ujumbe ambao huwasilishwa kupitia kwa kauli teule. Kauli hizo huweza kuwa za kimapokeo kama vile methali. Ingawa methali hutumika mno katika uwasilishaji wa tanzu za fasihi simulizi hutumika pia kama matini za msingi katika uwasilishaji wa tanzu za fasihi andishi hususa, ushairi wa Kiswahili. Kadhalika, katika uwasilishaji na upokezi kuna mwingiliano unaounganisha pande hizo mbili (Mulokozi 1986). Pia kwa kuzingatia nadharia ya Semiotiki, maneno ambayo hutumika huweza kuwa ya kiisitiari, kitaashira au kitaswira ambapo hupaswa kufasiriwa kwa kuzingatia utamaduni na uhalisi wa maisha ya watu (Njogu 2004 na Mosha 2002). Kwa hivyo, maswali ambayo yameibuliwa katika utungo yamejengewa mazingira hayo kupitia kwa kauli ya methali iliyotumika.

4.1.3 Shairi: Mgongano

Shairi hili ni miongoni mwa mashairi mafupi katika diwani hiyo. Utungo huo una beti nane na kila mojawapo una mishororo miwili. Kadhalika, shairi hilo limezungumzia kuhusu sura mbili za uhalisi wa maisha ambazo huweza kutokea kutegemea mabadiliko ya kiwakati katika jamii. Aidha, nguvu ambazo hutumiwa na watawala, huenda zikadidimizwa na watawaliwa. Kwa hivyo, mabadiliko hayo ni ya lazima katika jamii ambapo, leo huwa hivi na kesho huwa vingine. Katika shairi hilo, imetumiwa methali ya *Maisha mwendo wa ngisi, mwendo wa nyuma na mbele.* Methali hiyo ina maana kwamba, kitu au kiumbe huweza kubadilika kulingana na mabadiliko yanayojiri katika jamii. Kwa hivyo, utabiri wake haujulikani. Methali hiyo imetumiwa katika muktadha wa kauli zingine kuwa msingi wa uwasilishaji katika shairi.

4.1.3.1 Methali kama Kichocheo cha Kuibulia na Uwasilishaji wa Mawazo

Katika usawiri na uwasilishaji wa mawazo, mshairi ameitumia methali. Kwa hivyo, anwani ya shairi si ya methali. Hata hivyo, imesaidia katika ubainishaji wa ujumbe ambao umewasilishwa. Kwa kufanya hivyo, methali hiyo imekuwa dira mwafaka zaidi ya kumwongoza katika uibuaji na uwasilishaji wa mawazo ya mshairi. Kwa mfano, mshairi amefananisha harakati mbalimbali zinazofanywa katika jamii na *mwendo wa ngisi*. Kutokana na taswira ya *ngisi* ni kwamba, maisha hayawezi kamwe kuwa yenye mdundo na mwendo wa aina moja katika jamii. Kadhalika, mshairi ameyakinisha kuwa maisha ya jamii huweza kubadilisha mkondo wake kutokana na mpito wa wakati. Kadhalika, maisha huwa katika mabadiliko. Kwa mfano, mtu huweza kuwa mchochole au fukara kwa wakati mmoja lakini baadaye huenda akatononoka na kuwa mkwasi wa

kutajika na kuheshimiwa katika jamii. Kama alivyokariri mshairi, mabadiliko ni ya kiwakati:

Huwavamia inasi
kuwafisha mageule
yakawafanya wakwasi
wakawa watu wateule. (Uk. wa 36)

Kwa hivyo, mabadiliko ya kiwakati huweza kuwafanya wale waliochukuliwa kuwa wanyonge katika jamii kuzinduka na kuidai haki yao ya kujitawala. Kadhalika, mwamko wa kisiasa na ushikamano wa kijamii huwasaidia wanyonge kupigania na kujinyakulia utawala wa jamii. Chambilecho mshairi, wanyonge katika jamii:

Husiniama mvutano
daraka kupiganiwa
wajaribupo wanono
haki yetu kuiuwa (Uk. wa 36)

Kulingana na mawazo yaliyowasilishwa ni kwamba, watawaliwa ambao huchukuliwa kuwa ni wanyonge, katu wasidharauliwe kutokana na hali yao duni. Kwa sababu, ya kesho hayajafichuliwa wala hayajulikani. Kwa hivyo, mivutano ambayo huzuka huigawanya jamii katika misingi ya kitabaka. Katika muktadha huo, watu wa tabaka la chini hujiona kuwa wamedharauliwa na wale wa tabaka la juu. Hiyo ndiyo sababu ya kuelezwa kuwa kuna uwezekano kwamba, wanajamii:

Wakasimama wakiwa
kuanza kuitetea. (Uk. wa 36)

Vile vile, wale ambao wamemiliki nyenzo za uzalishaji mali na utawala katika jamii huwa hawalali kwani wamekuwa wakitumia kila mbinu kuchonga hila fiche ili zitumike katika kuwanyanyasa zaidi wanyonge. Vitimbi hivyo, huweza kuhalishwa katika mfumo

huo dhalimu wa kiutawala. Hata hivyo maono yaliyowasilishwa ni kwamba, hali kama hiyo haitaendelea milele kwa sababu; wale ambao huhisi kunyanyaswa au kudhulumiwa huweza kuhimizana kwa kuzinduana huku wakipanga mikakati kabambe ya kukabiliana na udhalimu huo uliosakini katika jamii. Kama ilivyokaririwa kuhusu harakati hizo, ni kuwa:

Wajaribupo wanono
haki yetu kuiwa
wakasimama wakiwa
kuanza kuitetea (Uk. wa 36)

Kutokana na dondoo hilo, *wanono* yaani wanaowadhulumu na wanaowahini wanyonge, kuna wakati ambapo wahiniwa wataidai halali yao kwa kutumia nguvu. Kwa kutumia methali, mshairi ameweza siyo tu kuibulia mawazo yake bali pia kubainisha na kuwasilisha hisi na itikadi yake kuhusu uwezekano wa mabadiliko ya kiwakati katika maisha ya jamii. Itikadi na mwelekeo wa mshairi ni kwamba, wakati ambao umesetirika katika taamuli ya jamii huweza kubadilisha au kugeuza mkondo wa maisha katika jamii. Hiyo ndiyo sababu wanyonge na waliodhulumiwa katika jamii hupaswa kuwa na matumaini ya kupata stahiki yao, pindi kimbunga cha wakati kitakapowadia, kutoka kwa mahasimu wao. Kwa hivyo, mshairi ameitahadharisha jamii ya *wanono* kuwa hupaswa kubadili mielekeo na nyendo zao, la sivyo mabadiliko ya kiwakati yatawakumba na yatawafurusha hata kama si katika wakati uliopo. Kwa wanyonge, mshairi amewatia shime kuwa wawe macho na kuzinduana kwa vile *siku moja* harakati zao zitawafaidi na zitazaa matunda. Hali hiyo pia imebainishwa katika baadhi ya tungo za ushairi. Kwa mfano Abdalla (1973:21), ametongoa:

ALII
Kwa kuwa ni haki yangu, sitahayari kuidai
Tatumiya nguvu zangu, madhali ningali hai
Nipate fungu langu, japo kwa ghali bei
Nawe hapo uwe hoi (Ubeti wa 33)

Katika muktadha huo, itikadi na mwelekeo wa mshairi hubainisha kuwa matumaini katika mabadiliko ya maisha yapo, endapo nia ipo. Shime ni kwamba, jamii isiweze kukata tamaa.

4.1.3.2 Uibushaji na Uwasilishaji wa Ujumbe Kiisitiari Kutokana na Methali

Mshairi ameuwasilisha ujumbe kupitia kwa isitiari inayoibushwa kutokana na matumizi ya methali. Kama vile ilivyobainishwa, methali imetumiwa kama kauli muhimu katika kuutanguliza wa ujumbe wa shairi hili. Kadhalika, kauli hiyo ya methali imetumiwa mahususi ili kuufanya ujumbe wa shairi uweze kuwasilishwa na kufasiriwa kiisitiari.

Kwa hivyo, msomaji anapokutana na methali hiyo, hujaribu kutafakari ujumbe uliofumbwa huku akijenga taswira iliyokusudiwa. Kwa mfano, msomaji hujenga picha ya kimaono kuhusu uhalisi wa maisha katika jamii, ambayo hayana budi kubadilika kutokana na kiumbiumbi cha wakati. Kwamba, maisha kama *mwendo wa ngisi* hayawezi kutabirika moja kwa moja kwa sababu, hayafuati mkondo mmoja mahususi. Kutokana na uhalisi wa maisha, baadhi ya watu ambao walikuwa fukari wakati uliopita, hivi sasa wameza kujikweza na maisha yao yamekuwa ni bora zaidi. Kwa kutumia methali hiyo kuwa msingi wa kuusawiri na kuuwasilisha, mshairi ameufafanua zaidi ujumbe wake kwa kuibua isitiari ndogo ndogo katika shairi. Kulingana na mihimili ya nadharia ya Semiotiki, ujumbe katika utungo wa fasihi huwasilishwa kwa maono na utafakari zaidi kupitia kwa kauli zilizojenga isitiari (Scholes 1982 na Pierce 1977). Hata hivyo, isitiari

pana huibushwa na kubainishwa kupitia kwa isitiari ndogo ndogo zilizotumiwa. Kwa mfano, baada ya kutumia methali, mshairi amepiga kasi kwa kubainisha kuwa wakati:

Huwavamia inasi,
kuwafisha mageule
yakawafanya wakwasi,
wakawa watu wateule. (Ubeti wa 36)

Kupitia kwa dondoo hilo, mshairi ana mawazo kwamba, mabadiliko ya wakati huwa kama kimbunga ambapo hutokea au hujiri bila ya kutarajiwa katika jamii. Kwa hivyo, wale waliokuwa ni wachochole na waliokuwa wakidharauliwa katika jamii huweza kuwa wakwasi na kuweza kuheshimiwa. Kadhalika, wanyonge au waliotawaliwa kimabavu huweza kuungana pamoja na kuubwaga utawala huo dhalimu. Mshairi amebainisha hayo, kwa kusema kuwa:

wanyonge walo wawele, tawala kujipatia.

Harakati hizo za kiukombozi zimedokezewa na zimedhihirishwa kupitia kwa isitiari pana ya methali na kurutubishwa kwa kauli au maelezo ya kitaswira yaliyotolewa katika shairi. Kutokana na taswira zilizoibuliwa, mshairi ameweza pia kuuwasilisha na kuubainisha ujumbe wake kiisitiari. Katika muktadha huo, mshairi humtaka msomaji kutambua kuwa; methali hiyo imetumiwa kama isitiari pana ambayo imeweza kutolewa maelezo ya kina kutokana na tajiriba ya mshairi iliyojikita katika uhalisi na utamaduni wa jamii. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, ujumbe uliowasilishwa katika utungo ni ule ambao umejengwa katika utamaduni wa jamii (Wamitila 2003). Kwa hivyo, mshairi hakuzungumzia maswala ya kidhahania bali yale ambayo huweza kufasirika na kufafanuliwa kwa kuzingatia muktadha wajamii maalumu.

Hata hivyo, ujumbe ambao umewasilishwa si wa moja kwa moja bali kauli zilizotumiwa huwa ni chemichemi ya kuchochea utafakari na usaili katika usomaji wa shairi. Zaidi ya hayo, msomaji hawezi kuelewa undani wa ujumbe ambao umewasilishwa bila ya kuzingatia uelekezo wa methali, maelezo na ishara zilizotumika. Kwa mfano, hapo awali imebainishwa namna mabadiliko ya kiwakati huweza kuleta na kusababisha mabadiliko katika maisha ya jamii. Kwa hivyo, watawaliwa huweza kujipatia uhuru na haki yao hata kama si kwa wakati huu wa sasa.

Kadhalika, mshairi amewatia moyo *wanyonge* ambao wamekuwa wakidhulumiwa na *wanono.* Kwamba, wakiamua kusimama kidete na kuidai haki yao huenda wakaupata mustakabala wao siku za usoni. Katika uwasilishaji wa shairi, dhana ya *wanono* imetumiwa kitaashira na kiisitiari kumaanisha wale huendekeza dhuluma au hujitapa kutokana na madaraka waliyo nayo. Kwa hivyo, matumizi ya methali yamesaidia katika utunzi na uwasilishaji wa mawazo kimafumbo. Hapa ieleweke kuwa, matumizi ya mafumbo husaidia mno katika kuufundika ujumbe ambao huhitaji ufafanuzi mpana (Gibbe 1990). Ingawa shairi hili ni fupi, limefumba maudhui pana ambayo humtaka msomaji kupiga bongo na kujitolea maelezo ya kina. Isitoshe, matarajio ya mshairi ni kwamba, msomaji atalisoma shairi hilo kuanzia mwanzo hadi mwisho ili kuweza kuupata ujumbe ambao umekusudiwa. Kwa njia hiyo, mshairi ameweza kuitumia methali ili kuchochea tafakuri na kujengea taharuki katika akili ya msomaji.

Baada ya kulisoma shairi lote, msomaji huweza kuupata ujumbe wa msingi na pia huweza kujiundia baadhi ya maswali yafuatayo:

- Kwa nini mshairi ameitumia methali hiyo mwanzoni mwa shairi?
- Ni ujumbe gani uliofumbwa na kuwasilishwa kupitia kwa methali hiyo?
- Maelezo yaliyotolewa katika shairi yamechangia vipi katika kubainishia dhima ya methali hiyo?

Maswali hayo yaliyoibuliwa, huweza kumfanya msomaji kutaka kulisoma tena shairi hilo kwa tuo. Aidha, anapolidurusu kwa mara ya pili au zaidi, msomaji huweza kutua kidogo wakati anapokumbana na methali ili kuweza kutafakari zaidi kuhusu matumizi yake. Kadhalika, msomaji huwa na hamu ya kutaka kulisoma shairi zima huku akijaribu kutafakari zaidi isitiari ndogo ndogo zilizoibushwa kutokana na uelekezi wa methali. Isitiari hizo ndogo ambazo zimeibuliwa kupitia kwa matumizi ya methali ni kama vile:

- *Maisha ni mgongano*
- *Wajaribupo wanono*
  Haki yetu kuiuwa
- *Wakasimama wakiwa*
  Kuanza kuitetea (Uk. wa 36)

Kupitia kwa madondoo hayo na hasa kauli zilizopigiwa mstari, mshairi ameweza kuikuza isitiari pana ambayo imetokana na methali. Endapo msomaji atasitisha usomaji katika methali, basi hatafaidi uhondo wa ujumbe uliowasilishwa. Kwa hivyo, methali imetumiwa mahususi kama mbinu ya kuufumba na kuibulia mawazo muhimu yanayowasilishwa. Kadhalika, methali kama kichocheo cha isitiari na cha kutafakarisha, imetumiwa kwa makusudi ili kuipambanua hadhira: wasomaji wa dhati na wasomaji wa kijuujuu. Wasomaji wa dhati hupiga mbizi katika kutafakari isitiari iliyoundwa kwa uelekezi wa methali na wale wasio wa dhati hupata tija ya burudani kupitia kwa kauli teule zilizotumika katika shairi.

4.1.3.3 Methali kama Mbinu ya Kuibulia Usambamba

Katika usawiri na uwasilishaji wa shairi hili, mshairi ametumia takiriri ya vina vya ndani na nje, yaani katika ukwapi na utao. Jambo hilo si bainifu hadi pale umbo la shairi linapoweza kupanguliwa na kupangwa upya kama itakavyobainishwa hapo baadaye.

Kadhalika, matumizi ya methali yamesaidia katika kuusisitiza na kuukoleza zaidi ujumbe ambao umewasilishwa, hasa kwa kuzingatia mbinu ya usambamba iliyobuliwa kupitia kwa kauli zilizotumika kwa makusudi katika uwasilishaji wa shairi. Kwa kutumia methali hiyo, mshairi ameweza kubainisha ujumbe kwa kuzingatia mifano na maelezo tofauti tofauti iliyotumika. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, kauli teule zaidi ya moja huweza kutumiwa kuushadidia ujumbe mahususi katika utungo (Jilala 2008). Mshairi ameweza kufanya hivyo kwa manufaa yake mwenyewe na pia kwa hadhira yake. Hadhira inapozingatia methali iliyotumika hapo mwanzoni mwa shairi, huweza kuupata kwa ujumla ujumbe ambao huwasilishwa. Kwa sababu, methali ni kauli ambayo huhitaji kutolewa maelezo ya muhimu ili kuufafanua na kuubainisha zaidi ujumbe uliopo. Hali hiyo hutokana na pale ambapo mtunzi huhisi kuwa ujumbe unaowasilishwa si bayana au haujabainika vilivyo. Kwa ambavyo mshairi hataki ujumbe uwe wenye utata, huwasilishwa kwa kauli za makusudi au kupitia kwa miundo mbalimbali ya lugha. Kwa hivyo, methali imetumiwa kama msingi wa kuibulia na kujengea usambamba katika usawiri na uwasilishaji wa shairi. Katika mantiki hiyo, mifano na kauli zilizotolewa zimesaidia kushadidia zaidi ujumbe uo huo katika shairi. Kwa mfano, mageuko ya kiwakati huweza:

- *Huwavamia inasi*
  kuwafisha mageule

yakawafanya wakwasi
wakawa watu wateule

- *Wanyonge walo wawele*
  tawala kujipatia
- *Maisha ni mgongano*
  mudhili na mudhiliwa
- *Wajaribupo wanono*
  haki yetu kuiuwa
  wakasimama wakiwa
  kuanza kuitetea. (Uk. wa 36)

Kwa kutumia kauli zilizozingatiwa katika madondoo hayo, mshairi ameweza kujenga ukariri wa ujumbe kiusambamba, kwamba:

- *Maisha* huweza kuchukua mkondo mwingine ambao ni tofauti. Watu ambao walikuwa wachochole huweza kuwa *wakwasi.*
- Katika jamii huweza kuwa na migongano yenye mivutano baina ya *mudhili* na *mdhiliwa* au baina ya walichonacho na wasionacho.
- Baada ya kuzinduka au kutambua haki yao, wadhulumiwa huweza kuzua mikakati ya kuitetea halali yao.

Kadhalika, matumizi ya kauli ambazo hujenga usambamba, mshairi ameweza kuelekeza udurusu na kuufafanua zaidi ujumbe uliowasilishwa katika shairi. Kwa mfano, kauli hizo huwa ni kunga badilia katika usawiri na uwasilishaji wa ujumbe. Kwa sababu, mshairi hataki kuikifu wala kuichosha hadhira kwa kauli zenye miundo ya aina moja. Kwa kutumia methali, mshairi ameweza kujijengea msingi au chemichemi ya miundo mbalimbali ambayo huvutia hisi na huathiri zaidi upokezi wa ujumbe.

4.1.3.4 Methali kama Mhimili wa Muundo

Methali hiyo imetumiwa mwanzoni mwa shairi, siyo tu kama kauli ya kuelekeza na kufaragua ujumbe wa mshairi bali pia kama msingi wa kusawiri muundo, mahadhi na ridhimu katika shairi. Kimuundo, methali iliyotumika hushabihiana mno na miundo mingine ya kauli zilizotumika katika shairi. Kwa mfano, muundo wa sehemu ya mwanzo katika methali imemsaidia mshairi kuwa na mizani nane kwenye ukwapi. Kadhalika, sehemu ya pili ya methali imesaidia katika upataji wa mizani nane kwenye utao. Katika muundo wa nje, methali imejibainisha kama mishororo miwili katika shairi kama ifuatavyo:

Maisha mwendo wa ngisi
mwendo wa nyuma na mbele (Uk. wa 36)

Kwa hivyo, methali hiyo ina jumla ya mizani kumi na sita. Hata hivyo, mshairi ametumia uhuru wa kishairi kupanga maneno hayo ya methali katika mistari ya msharazo au mishororo miwili. Kimsingi, maneno ambayo yamepatikana katika kauli hiyo hujenga sentensi moja. Huo ni ukiushi wa kikaida katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi Kiswahili wa kimapokeo. Kimtindo, jambo hilo huweza kuwa ni njia mojawapo ya kuuondoa polepole ushairi huo kutoka kwa kaida za kiarudhi. Katika muunbo wa ndani hubainika kuwa, shairi hilo lina beti mbili za msingi zenye mishororo minne kwa kila mojawapo. Kwa hivyo, shairi kusudiwa huweza kupangwa hivi:

- *Maisha mwendo wa ngisi, mwendo wa nyuma na mbele*
  Huwavamia inasi, kuwafisha mageule
  Yakawafanya wakwasi, wakawa watu watule
  Wanyonge wao wawele, tawala kijipatia
- *Maisha ni mgongano, mudhili na mudhiliwa*
  Husimama mvutano, daraka kupiganiwa
  Wajaribupo wanono, haki yetu kuiuwa
  Wakasimama wakiwa, kuanza kuitetea. (Uk. wa 36)

Ingawa mshairi hakutaka kudhihirisha muundo huo kuwa ni wa tarbia, ni dhahiri kuwa utaratibu huo wa kiutunzi na uwasilishaji ni wa ushairi wa kimapokeo. Baadhi ya vipengele vya kiarudhi ambavyo hudhihirika katika shairi hili ni: mizani, urari wa vina vya ndani na nje, mishororo na kiishilio au kibwagizo. Kiumbiumbi mpangilio wa muundo wa ndani katika shairi hudhihirisha kuwa ubeti wa mwanzo una kina cha kati [-**si**] na kina cha nje [-**le**]. Katika kibwagizo, mshairi ametumia kina cha kati [-**le**] na kina cha nje [-**a**]. Kwa hivyo, ubeti huo wa mwanzo umeundwa kwa mishororo minne ambayo imegawanyika katika sehemu mbili: ukwapi na utao.

Kinyume na mwelekeo wa utunzi na uwasilishaji wa kimapokeo, mwendo na usomaji wa shairi hilo umeelekezwa kwa uzingativu wa ishara za uakifishi kama vile matumizi ya herufi kubwa mwanzoni mwa kila mstari na pia kwa matumizi ya kituo mwishoni mwa kauli zilizotumiwa. Katika muktadha huo, usomaji wa shairi hili huongozwa zaidi kwa misingi ya alama hizo. Kwa njia hiyo, mahadhi na ridhimu ya shairi yamedumishwa. Kwa kuzingatia uelekezo huo, shairi hilo huweza kuimbwa au kughaniwa bila ya kupoteza athari ya kiujumi na kiumbuji (Masinde 2007 na Wanyoike 1974). Kimsingi, muundo wa shairi hilo umechochewa na umeelekezwa kwa uzingativu wa methali iliyopo.

4.1.4 Shairi: Kula Njama

Shairi hili ni miongoni mwa mashairi marefu katika diwani hii ya *Chembe cha Moyo*. Isitoshe, idadi ya aya zilizopo si bayana. Aidha, shairi hili limesawiri maswala ya kisiasa na kiuchumi miongoni mwa mataifa huru barani Afrika. Ingawa mataifa hayo yamepata

uhuru, huegemea na huelekezwa kwa nguvu kutoka kwa mataifa 'yaliyoendelea'. Katika muktadha huo, mshairi ameeleza namna mfumo wa ukoloni unavyoendelezwa na unavyobainishwa kupitia kwa ukoloni-mamboleo. Ujumbe huo umewasilishwa kupitia kwa kauli teule zilizotumiwa kama ilivyobainishwa. Kadhalika, shairi hilo limetumia methali moja katika uwasilishaji wake. Methali hiyo ni: *Ukionacho sicho ukipatacho.* Maana ya methali hiyo ni kwamba, kile ambacho mtu hukiona au hulipwa kutokana na kazi aliyoifanya hakilingani na kazi iliyofanywa.

4.1.4.1 Uundaji wa Kinaya Kutokana na Methali

Methali hiyo imetumiwa kama mbinu ya kuibulia kinaya katika utunzi na uwasilishaji wa mawazo yaliyojikita katika mikinzano iliyohusu mawakala wa ukoloni mamboleo katika mataifa yanayoendelea. Katika shairi imebainishwa namna mataifa machanga ya Afrika hufanyiwa hila za kusambaratisha chumi zao. Kulingana na mawazo ya mshairi, *ukionacho sicho ukipatacho*. Kwa mfano, mabarakala wa mfumo wa ukoloni-mamboleo ni watu wanaoshirikiana na wengine wasioonekana kupanga mipango ya kufilisi mataifa hayo machanga. Katika muktadha hu, ukoloni-mamboleo huziletea dhiki kubwa mataifa hayo. Kwa ambavyo, hawataki siri zao zibainike, vikao vyao hupangwa na hufanywa kwa siri katika miji mikuu ya Ulaya, kama vile: *Washington, London* na *Geneva.*

Kimsingi, mawakala hao wa ukoloni-mamboleo huenda *kwao* kwa malengo ya *kupika na kupanga ili kutunyonya kila tone la damu yetu.* Kwa hivyo, imebainishwa kuwa *Wala Njama* ni maadui ambao hujificha miongoni mwa jamii huku wakidhaniwa kuwa ni watu wema kumbe sivyo. Vile vile, mshairi huitaka jamii ielewe kuwa mawazo na mipango ya

Wala Njama au mataifa nyonyaji haina manufaa yoyote katika mataifa yanayoendelea. Matatizo huzisibu jamiiau nchi zinazoendelea hayazingatiwi isipokuwa mahitaji yao ndiyo hupewa kipaumbele. Dhiki na masaibu hayo hushuhudiwa na hufahamika vyema katika jamii hizo zilizodhulumiwa na zilizonyanyaswa. Kulingana na nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mawazo ambayo huwasilishwa ndiyo hubainisha zaidi anwani katika utungo (Nagler 1967). Katika shairi hilo, ujumbe umebushwa kwa ulekezi wa anwani; matumizi ya methali husaidia katika ufafanuzi huo. Kadhalika, matumizi hayo hujenga muktadha wa usaili katika uwasilishaji wa utungo. Hiyo ndiyo sababu ya kusailiwa kuwa:

Tuna haja ya shaka, dada zangu?
Shaka hatuna haja nayo
Tuna haja ya utafiti ndugu zangu?
Utafiti hatuna haja nao. (Uk. wa 45)

Kutokana na dondoo hilo, jamii nyanyaswaji imeyashuhudia yote na ni ithibati tosha ya udhalimu unaotendwa. Kwa mfano, mazao adimu yenye thamani kubwa hukuzwa katika mataifa haya machanga na faida yote huenda kunufaisha mataifa ya *mabwana.* Matokeo ni kuwa, mataifa zalishi au kuzaji huwa katika ulitima au hali mbaya ya kisiasa na kiuchumi ilivyoathiri maisha ya wanajamii. Kwa mfano, imeelezwa kuwa:

Faida ikiwapandia 'fika mbinguni
sisi twala njaa kwetu mitaani (Uk. wa 45)

Katika muktadha huo, mshairi amesaili zaidi na kwa mshangao kuwa:

Basi ukionacho ndicho ukipatacho!
Au bado hujaamini? (Uk. wa 45)

Hapa ieleweke kuwa jambo la msingi ambalo limewasilishwa, ni kinyume na ndoto au matarajio ya jamii. Ni kutokana na utambuzi wa kinaya kilichosetiriwa katika methali iliyotumika ndipo ujumbe fiche katika shairi huweza kueleweka na kufasiriwa. Kulingana na nadharia ya Semiotiki, methali ni kauli zilizojengwa katika tamathali za usemi (Norvick 1985). Kwa hivyo, kauli hizo huhitaji kufasiriwa kwa uelekezo wa mtunzi au mtumiaji. Kwa mfano, jamii dhulumiwa huingiza fedha na faida hiyo kubwa. Hata hivyo, haiinufaishi kamwe bali hutoka mikononi mwake na kupelekwa kukidhi mahitaji ya mataifa nyanyasaji. Kutokana na mahusiano hayo ya kizandiki, mataifa zalishi hurudishwa nyuma maendeleo yake ilihali mataifa nyonyaji huneemesha chumi za mataifa yao. Zaidi ya hayo, mshairi amezitaka nchi hizo za Afrika huru au 'zinazoendelea' kuweza kufahamu kuwa, si fukara bali hali zao za kiuchumi zimesababishwa na *mabwana* wa kigeni. Kwa sababu hiyo, imebainishwa kwamba:

Si yale manoti
wala si mahundi
...
yapelekwayo mawindoni
ili kuwapandishia wala njama
faida iliyowashukia (Uk. wa 46).

Ujumbe ambao umeibuliwa katika dondoo hilo ni kwamba, mataifa hayo hupaswa kutambulika katika jumuiya ya mataifa kuwa ni *tajiri.* Kwa mfano, katika mataifa 'machanga' kuna milolongo ya watamba na njia ambapo hali hiyo haipaswi katu kuwepo. Katika muktadha huo, utajiri na rasilimali ipo lakini imefyonzwa na majitu ambayo ni *kama MAFUNZA chini ya mawe. Majitu* na *mafunza* hyoa hayafanyi lolote bali hunyemelea kwa siri na vilinge ili kuweza kuifyonza raslimali iliyopo katika mataifa hayo machanga. Kwa sababu hiyo, mshairi ana mawazo kwamba: kile ambacho wajamii

hukiona kuwa ni *faida nyingi* sicho ambacho hutarajiwa kukipata. Kwa kutumia methali hiyo, mshairi amedhihirisha wazo kwamba, japo jamii katika mataifa hayo huru hupata mapato, mapato hayo hayalingani kabisa na kile walichotarajiwa kukipata. Kwa hivyo, wakipatacho ni kifumba macho. Kwa sababu, mataifa hayo ndiyo zalishi lakini ambayo hufaidi zaidi ni yale ya kigeni. Katika mantiki ambayo imeibuliwa kwenye methali, mshairi huitaka jamii ing'amue uhalisi wa mambo hayo yaliyowasilishwa.

4.1.4.2 Methali kama Chombo cha Kubainishia Mwelekeo na Itikadi ya Mshairi

Mshairi ameitumia methali kama chombo cha kuwasilishia dhamira na pia kama mbinu ya kubainishia itikadi yake kuhusu ukoloni-mamboleo. Jambo la msingi lililobainishwa katika shairi ni kwamba, ukoloni-mamboleo umedumaza zaidi maendeleo katika mataifa hayo 'yanayoendelea'. Kwa mfano, mawakala wa mfumo huo dhalimu wa kiutawala na kiuchumi, si kwamba huishi nje ya mataifa hayo ambayo hudhikishwa, bali huishi na kujumuika miongoni mwa wanajamii huku wakitumia ujanja na udanganyifu ili wafaidi na waikamue zaidi au waifyonze rasilimali iliyopo. Kwa hivyo, mawakala wa ukoloni-mamboleo ni maadui wenye lengo moja kuu: kujinufaisha wao wenyewe na kuyanufaisha mataifa ya mabwana zao, kama ilivyotongolewa kuwa:

> *Kwa pumzi moja yakiungana*
> *Kwa shauri moja yakioana*
> *Kula-njama kula watu nyama* (Uk. wa 44)

Katika muktadha wa dondoo hilo, mawakala wa ukoloni-mamboleo wanapotamakani katika jamii hizo huwa ni wapelelezi na majasusi wenye nia ya kuuhujumu na kuufuja chumi za mataifa hayo 'machanga'. Kwa mfano, hupanga mipango kwa siri huku:

Wakipika na kupanga
Kunyonya kila tone la damu yetu? (Uk. wa 44)

Kulingana na mwelekeo uliochukuliwa, mipango hiyo dhalimu husetiriwa na huafikiwa kwa siri katika miji mikuu ya ughaibuni. Kwa ambavyo mipango hiyo hufanyika nje ya mataifa hayo, haizingatii hisi na mahitaji ya mataifa hayo yanayodhulumiwa. Maamuzi yanayoafikiwa na yanayoamuliwa, huja kutekelezwa kwa siri na mawakala hao wa ukoloni-mamboleo. Endapo jamii hutilia shaka nyendo hizo, mara moja kauli za kupumbaza hutolewa na mawakala wa ukoloni-mamboleo kuwa:

Kwamba mwenyewe Mungu Mwenyezi
amepanga kwa yake mapenzi
iwe vivi ilivyo katika yake enzi?
mwenye kupata apate
mwenye kupatwa apatwe?(Uk. wa 44)

Kulingana na mawazo ya mshairi, kauli hizo ni za kipuuzi na zenye *Dhamira chafu.* Kwa sababu, kazi za sulubu zinazofanywa na wanajamii haziwaletei tija yoyote isipokuwa mateso na dhiki chungu nzima. Aidha, mshairi amezihimiza jamii zinazoyanyaswa kuwa zinahitaji ziwe macho, kwamba:

Usiiwache hadaa yao ikule njama!
Risasi ile iliyokutoboa mwili mzima
tulipangiwa mimi na wewe
tangu mwanzo wa mfumo huu(Uk. wa 36)

Kwa hivyo, mshairi ana mwelekeo kwamba, matatizo ambayo huzizonga jamii za mataifa 'machanga' ya Afrika si faradhi au majaliwa bali yamesababishwa na hao *wala-njama.* Kwa kuzingatia nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli au dhana msingi za kimapokeo huweza kutumiwa katika utungo ili kuulekeza ujumbe unaowasilishwa (Nagler 1967). Kwa ambavyo ujumbe huo umeibuliwa kupitia kwa hisi za mtunzi, utungo huweza pia

kubainisha mwelekeo wa mtunzi. Kadhalika, kupitia kwa mihimili ya Semiotiki, dhana ya *kula-Njama* na *wala-njama* huweza kufasiriwa kwa kuzingatia historia, uhalisi wa maisha na utamaduni wa watu. Vile vile, mshairi amedhihirisha kuwa mataifa hayo 'machanga' ni tajiri, kwa ambavyo yana hazina kubwa ya migodi na rasilimali tosha lakini tatizo ni kwamba; hayana nyenzo na bei duni ya hazina yao hupangwa kwa vilinge na mataifa 'yaliyoendelea'.

Kulingana na maono ya mtunzi, wanajamii wa mataifa 'machanga' hudhulumiwa kwa njia tatu: hupangiwa bei ya mazao, ujira mdogo kwa vibarua na mazao hayo kupelekwa kwa mataifa ya kigeni. Kwa hivyo, ujira huwa mdogo na faida ambayo hutokana na jasho lao hairejeshewi katika mataifa hayo 'machanga'. Chambilecho mshairi:

- *Na ule mshahara uliokatiwa*
  mkato wa ndani-kwa-ndani
  uliopasua mifuko yote surualeni?
- *Bei ya dhahabu ikiwaendea chini*
  wenzetu wauawa kule migodini
- *Faida ikiwapandia 'fika mbinguni*
  sisi twala njaa kwetu mitaani (Ubeti wa 45)

Kutokana na madondoo hayo, jamii hizo zimekuwa zikidhikishwa ilihali zimebarikiwa kwa utajiri mkubwa. Kwa hivyo, taswira iliyowasilishwa kuhusu mfumo huo wa kisiasa na kiuchumi ni ile ambayo huwaingiza mamilioni ya watu katika shida na ulitima, kama ilivyobainishwa hapa:

> *Chakula chao mezani*
> *itakayowawekea kitandani*
> *moto wa njozi zisizo kifani*
> *za mwisho wa maisha yao*
> *hapa ulimwenguni.*(Ubeti wa 47)

Ili kushadidia zaidi dhamira na itikadi hiyo, imedokezwa kuwa:

Basi ukionacho ndicho ukipatacho! (Uk. wa 45)

Kwa kuzingatia busara ya methali, mshairi amejikaulisha mawazo yake kuhusu mfumo dhalimu wa ukoloni-mamboleo ambao hudhihirika katika mataifa 'machanga'. Vile vile, ametilia shaka yale ambayo hushuhudiwa katika uhalisi wa maisha ya watu. Msimamo ambao umebainishwa ni kwamba, *mataifa machanga* hayapasi kuchukuliwa kuwa fukara au maskini kwa mtazamo wa *mataifa yaliyoendelea* bali hali yao ni matokeo ya mfumo dhalimu wa ukoloni-mamboleo uliosakini katika mataifa hayo.

4.1.4.3 Methali kama Kauli ya Kubainishia Maudhui ya Ukoloni-Mamboleo na Uzindushi

Kimsingi, mshairi ametumia methali hiyo ya *ukionacho ndicho ukipacho* ili kuibulia na kuwasilisha maudhui ya ukoloni-mamboleo na uzindushi wa jamii. Kulingana na nadharia ya Semiotiki, mawazo au ujumbe ambao huwasilishwa hupata uelekezo zaidi kupitia kwa kauli mahususi zilizoteuliwa na kutumika. Kauli hizo ni zile ambazo hujibainisha katika tamathali za usemi (Eco 1981). Vile vile, msomaji hupaswa kuzingatia kauli zilizotumika kama ishara au chombo cha kuufasiri ujumbe unaowasilishwa (Djik 1977). Kwa hivyo, msomaji anapolisoma shairi hili, huweza kubainikiwa kuwa jamii ya mataifa 'yanayoendelea' *wanachokiona sicho wanachokipata.* Kwamba, ukoloni-mkongwe tayari umeishagura na kuuacha ukoloni-mamboleo ambao huhakikisha kuwa unaendeleza na kuudumisha ukoloni kwa sura nyingine. Uhalisi wa mambo ni kwamba, mkoloni hayupo na wala haonekani lakini bado mizizi na athari zake huweza kuhisika na kuendelezwa kupitia kwa nguvu au msukumo

na msisimko mpya wa kisiasa na kiuchumi. Kwa hivyo, mkoloni hayupo lakini kivuli chake bado kingalipo. Kwa mfano, mataifa 'machanga' tayari yamenyakua uhuru uliopaniwa, lakini jamii hizo bado hazijaudhibiti kikamilifu uchumi wake.

Katika muktadha wa utungo, viongozi wa mataifa haya si watu wanaoweza kujiamulia hatima ya jamii zao kwani lazima wapate maelekezo kutoka kwa 'mabwana' au *wala njama*. Hussein (1971:2), amesawiri pia tukio hilo kupitia kwa tamthilia ya *Mashetani* kama ifuatavyo:

SHETANI: *Unanicha?*
BINADAMU: *Ndiyo*
SHETANI: *Unaninyenyekea?*
BINADAMU: *Ndiyo*
SHETANI: *Mbona sini unyenyekevu wala uoga katika uso wako?*
BINADAMU: *Kipitacho moyoni si lazima kionekane usoni.*
SHETANI: *Sijali kipitacho moyoni. Ninajali kionekanacho usoni.*

Malumbano hayo yamedhihirisha uwezo na mamlaka ya *Shetani* katika ulimwengu wa akina *Binadamu*. Kwa hivyo, *Wala-Njama* ambao ni 'mashetani' au mawakala wa ukoloni-mamboleo ambao hupanga njama za kuufyonza uchumi wa jamii zao kwa kujipendekeza au kushirikiana na 'mabwana' wasiokuwepo katika mataifa hayo 'machanga'.

Kadhalika, njama hizo zilizopangwa huwa hazieleweki katika muktadha wa utamaduni wa mataifa hayo 'machanga'. Hapa ieleweke kuwa, kuimarika kwa chumi za mataifa 'yaliyoendelea' zimetokana na rasilimali zinazoibwa kutoka kwa mataifa hayo 'machanga'. Ili kuwafumba macho wanajamii, mawakala wa ukoloni-mamboleo wamekuwa wakiendeleza mawazo hayo, kuwa:

Kwamba mwenyewe Mungu Mwenyezi
amepanga kwa mapenzi
iwe vivi ilivyo, katika yake enzi?
Mwenye kupata apate,
Mwenye kupatwa apatwe? (Ubeti wa 44)

Uhalisi wa mambo ni kwamba, mataifa hayo 'machanga' hayana namna ya kupiga makasia ya maendeleo kutokana na vizingiti au vikwazo vya kiuchumi vilivyowekewa na 'mabwana' wa mataifa 'yaliyoendelea'. Ingawa mataifa 'machanga' yamebahatika kuwa na migodi yenye malighafi za kiuchumi, jamii hizo hutatizika mno kimaisha. Kwa kuzingatia methali iliyotumiwa, mshairi ameweza kuibua kiusanii maswali ya msingi. Baadhi ya maswali hayo, ni kama vile:

- Ni kweli kwamba, mataifa 'yanayoendelea' ni fukara au masikini? (Jibu ni, la)
- Mataifa 'yaliyoendelea' na ustawi wa uchumi wao ni kutokana na kudura au mipango ya Mwenyezi Mungu? (Jibu ni, la)

Hayo ni baadhi ya maswali ambayo huchochea na hujenga msingi wa uzindushi katika jamii za mataifa 'yanaendelea'. Kama ilivyobainika kupitia kwa mantiki ya methali inayotumia, mshairi hakubaliani na mwelekeo wa mawazo ambayo yanayoibuliwa kuwa *ukionacho ndicho ukipatacho*. Ili kuyakinisha zaidi mawazo ya uzindushi, ametumia kiakifishi cha mshangao [!] mwishoni mwa kauli kama ilivyodhihirishwa hapa:

Basi *ukionacho ndicho ukipatacho*! (Uk. wa 45)

Kutokana na uelekezo wa ishara ya mshangao, mshairi huitaka jamii itilie shaka dosari busara iliyoibuliwa katika methali hiyo. Vile vile, mshairi huitaka izinduke na ichukue hatua ya kusitisha dhiki na madhila iliyopatishwa na mfumo wa ukoloni-mamboleo.

Kwa hivyo, jamii inapobaini chanzo cha matatizo yake huhitaji ichukue hatua gani? Kwanza, mshairi amedhihirisha kuwa dhiki hizo ni dhahiri katika jamii na wala hakuna haja kutilia shaka wala kufanya *utafiti* wowote kama ilivyokaririwa kuwa:

Tuna haja ya shaka, dada zangu?
Shaka hatuna haja nayo.
Tuna haja ya utafiti, ndugu zangu?
Utafiti hatuna haja nao. (Uk. wa 45)

Kwa hivyo, mshairi amezitaka jumuiya za mataifa 'yanayoendelea' zielewe kuwa: zimekuwa zikidhikishwa kwa kipindi kirefu kutokana na uwepo wa mfumo dhalimu wa kiuchumi na kisiasa. Katika muktadha huo, mshairi amewachukulia mawakala au *mabwana* hao wa ukoloni-mamboleo kuwa ni *majitu* na *MAFUNZA* ambayo ni *manene* na *mazito yaliyojificha chini ya mawe* huku yakiotea rasilimali ya mataifa machanga. Kwa uelekezo wa nadharia ya Semiotiki, maneno na kauli teule zilizotumika katika uwasilishaji wa utungo ni za kitaashira, kitaswira na kiisitiari. Katika muktadha wa shairi, kauli hizo hutumiwa kwa makusudi ili kuchochea utafakari wa ujumbe uliowasilishwa. Vile vile, mtunzi amepata kauli zilizotumika katika kutunga na kuwasilisha ujumbe wa uzindushi. Kwa hivyo, *majitu* hayo huhitaji kufukuliwa na kutokomezwa ili mataifa hayo yapate ahueni. Kwa sababu, hupanga *kutumalizia maisha yetu* huku yakiwafanya wanajamii kuwa walala hoi wasio na mbele wala nyuma.

Sauti ya uzindushi ya mshairi imesikika na imebainishwa zaidi anapoyahimiza mataifa 'machanga' kuchukua hatua kabambe zitakazotumika kuutokomeza mfumo wa ukoloni-mamboleo. Katika kufafanua zaidi mawazo hayo, amehimiza kuwa:

Tuimbe nyimbo zetu,
zile nyimbo za unyago
Bwana kula-Njama katuletea muhogo.
Kwa sababu,
maadamu kuna majitu
kutumalizia maisha yetu. (Uk. wa 47)

Kutokana na dondoo hilo, mshairi ana imani na uwezo wa jamii hasa itakapozingatia mbinu zinazojikita katika uhalisi wa utamaduni wa jamii. Kwa hivyo, shime kwa jamii ya mataifa machanga inapopanga mikakati ya kukabiliana na ukoloni-mamboleo ni muhimu kutumia mbinu zilizopo za kitamaduni na wala si kwa kuzingatia mielekeo ya kigeni. Ingawa mshairi ametoa ufafanuzi wa kina kuhusu ukoloni-mamboleo na uzindushi wa jamii. Kimsingi, ameweza kuibua mawazo hayo kwa uelekezo wa methali iliyotumiwa.

4.1.4.4 Methali kama Mhimili wa Kuibulia na Kuwasilishia Muhtasari wa Mawazo

Methali ya *Ukionacho ndicho ukipatacho* imetumika kama chombo cha kuufumba muhtasari wa mawazo yaliyowasilishwa katika shairi. Kimsingi, methali imetumika katika kuwasilisha ujumbe kwamba; juhudi ya mtu hupata tija inayostahili bila ya kunyanyaswa. Hata hivyo, kinachobainika katika shairi ni dhuluma na unyanyaswaji wa watu. Kadhalika, mshairi ameuelekeza ujumbe kwa kuzingatia kiashiria cha mshangao. Kwa kuitumia methali, mtunzi ameweza siyo tu kujenga kisa, bali pia kuufundika na kuuwasilisha ujumbe kwa muhtasari. Kwa hivyo, mshairi tayari ametoa ufafanuzi wa kina kuhusu mfumo dhalimu wa kibepari unaoendelezwa na ukoloni-mamboleo. Hayo yamebainishwa kutokana na maelezo pamoja na mifano iliyotolewa katika utungo. Kwa

mfano, mataifa 'yanayoendelea' yamedhikishwa mno kutokana na njama ambazo hupangwa na mawakala wa ukoloni-mamboleo wa mataifa 'yaliyoendelea'.

Isitoshe, mshairi hakubaliani na dhana kwamba mataifa 'yanayoendelea' ni fukara, kwani ameona kuwa kuna mbinu za kijanja ambazo hutumika katika kusababishia hali hiyo. Kwa kutumia methali, mshairi ameweza kuufundika na kuuwasilisha ujumbe wake kwa muhtasari. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mshairi huwa hana muda mwingi wa kufaragua maelezo yaliyotolewa. Kwa hivyo, kauli teule za kimapokeo zilizotumika katika utungo huwa ni ishara ya uelekezi katika kuufundika zaidi ujumbe uliowasilishwa (Fowler 1966). Katika muktadha wa shairi, methali imetumika kutekeleza mambo mawili ya msingi: kuendeleza kisa na pia kuwa mbinu ya kuwasilishia muhtasari wa ujumbe.

Kadhalika, kwa upande mwingine msomaji huweza kuupata ujumbe uo huo kwa kutafakari busara inayoibushwa kupitia kwa methali katika muktadha wa shairi. Kwa mfano, hadhira inapokumbana na methali iliyopo katika shairi; mwendo wa usomaji hudhibitiwa ili kuweza kuutafakari na kuurejelea ujumbe ambao huwasilishwa. Zaidi ya kuudhibiti mwendo wa shairi, msomaji hujengewa taswira inayosaidia kusaili zaidi kuhusu ujumbe ambao umewasilishwa kupitia kwa methali. Kwa mfano, msomaji huweza kujiuliza maswali yafuatayo:

- Matumizi ya methali yametokea wapi katika uwasilishaji wa shairi?
- Mshairi anawasilisha ujumbe gani kupitia kwa methali iliyotumika katika shairi?
- Mshairi ana mwelekeo upi katika mawazo anayoyawasilisha kupitia kwa methali?

Hayo ni baadhi ya maswali ambayo huweza kumpitikia msomaji anapokumbana na methali hiyo iliyotumiwa katika shairi.

Katika uwasilishaji, mtunzi hufahamu kuwa msomaji wake huenda akawa amepuuzia baadhi ya ukariri wa maelezo na mifano iliyotolewa lakini matumizi ya methali huweza kumdhibiti na kumrejesha katika kiini cha ujumbe unaowasilishwa. Kwa kufanya hivyo, msomaji huweza kuupata muhtasari wa ujumbe unaowasilishwa ambapo, maelezo yaliyotolewa huweza kuufafanua zaidi ujumbe huo unaoibuliwa. Katika muktadha huo, isichukuliwe kiholela kwamba msomaji anapozingatia methali peke yake atakuwa ameupata ujumbe kikamilifu bali iwe ni njia mojawapo ya msingi ya kuupokea ujumbe kwa muhtasari.

Kwa ambavyo methali hiyo imetokea katikati ya shairi, humbidi msomaji kurejelea beti za nyuma na za mbele ili kumaizi hoja mbalimbali ambazo hujenga na huchangia ujumbe kusudiwa. Kwa mfano, kabla ya methali kutumika, kuna maelezo yaliyotolewa yameweza kubainisha mwelekeo hasi wa ukoloni-mamboleo na pia hatua ambazo hupaswa kuchukuliwa katika jamii za mataifa 'machanga' ili kuutokomeza mfumo huo dhalimu wa ukoloni-mamboleo. Kwa hivyo, matumizi ya methali huweza kuwa msingi wa kujengea muhtasari wa mawazo katika shairi. Katika uwasilishaji wa shairi la Kiswahili, aghalabu watunzi hutumia methali kama kauli ambayo hutokea mwishoni mwa utungo (Kandoro 1983). Kwa njia hiyo, huwa rahisi kuhusishwa na muhtasari wa mawazo ambayo tayari yamewasilishwa katika shairi. Kama mtindo, mtunzi ameitumia methali ndani ya shairi ili kuudhibiti muhtasari wa ujumbe.

4.1.4.5 Uibushaji wa Isitiari Kutokana na Methali

Mshairi ametumia methali kama mbinu ya kuibulia na kuwasilishia ujumbe kiisitiari. Aidha, matumizi ya methali katika shairi yamekuwa chombo mwafaka zaidi cha kuusetiri ujumbe na kumwingiza msomaji katika kutafakari. Kama vile ilivyoelezwa hapo awali, pale ambapo methali imetumiwa, humfanya msomaji kutua kidogo ili kutunga taswira na kutafakari zaidi kuhusu ujumbe uliowasilishwa. Vile vile, msomaji hufahamu kuwa mshairi haitumii methali kiholela bali kwa ustadi na kwa makusudi. Kwa kuzingatia nadharia ya Semiotiki, kauli teule zilizotumiwa katika uwasilishaji wa ushairi huwa ni za kitaashira au kiisitiari. Kwa hivyo, huweza kuhusishwa moja kwa moja kimetonomia au kimafumbo (Jacobson 1960). Kimsingi, methali iliyotumiwa katika uwasilishaji wa utungo huo huhitaji kufasiriwa kwa kuzingatia uhalisi wa maisha.

Katika muktadha huo, msomaji anapokumbana na methali huweza kusaili na kujiuliza baadhi ya maswali. Kwa hivyo, mshairi ametumia methali hiyo ya *Basi ukionacho ndicho ukipatacho!* ili kujenga mazingira ya kuibua maswali yafuatayo:

- Ni nini *wanachokiona* wanajamii katika mfumo wa ukoloni mamboleo?
- Ni kweli kwamba wanachokiona ndicho *wakipachokipatacho*?

Hayo ni baadhi ya maswali ambayo mshairi huyaundia hadhira iyatafakari zaidi. Zaidi ya hayo, mshairi amejenga mazingira ambayo huufanya usomaji wa methali kuweza kuelekezwa kwa alama ya mshangao (!) ambayo ipo mwishoni mwa kauli hiyo. Kwa kutumia dhana ya *Basi* na ishara ya mshangao, mshairi ameweza kujikaulisha methali hiyo na hadhira hupata uelekezo wa kufahamu kuwa, hiyo ni kauli ya mshairi.

Fauka ya hayo, anapotumia methali hiyo, mshairi huitaka hadhira yake ifikirie zaidi ya upeo wa maneno hayo yaliyotumika. Kwamba, mawakala wa ukoloni-mamboleo wametamakani miongoni mwa wanajamii lakini hawapaswi kuchukuliwa kuwa ni 'wenzi' wao, kwa vile:

- *hawashushi pumzi kwa mdundo mmoja* (Uk. wa 44)
- *... chombo walichotutilia*
  kimeshindwa kutunasa kihisia (Uk. wa 44)
- *Dhamira chafu ... nakueleza hayo* (Uk. wa 45)
- *Usiiwache hadaa yao ikule njama!*
  Risasi ile iliyokutoboa mwili mzima
  tulipangiwa mimi na wewe, (Uk. wa 45)

Kutokana na madondoo hayo, mshairi huitarajia hadhira kubaini kuwa mfumo wa ukoloni-mamboleo ni mbaya. Kwa hivyo, ujumbe unaowasilishwa si wa moja kwa moja bali vipengele vya maneno vimetumiwa kuwa ishara tosha ya kuutambulia na kuufafanua ujumbe unaowasilishwa katika shairi. Kwa mfano, mabarakala wa mfumo wa ukoloni-mamboleo *hawashushi pumzi kwa mdundo mmoja, wana dhamira chafu, wana hadaa* na *njama iliyokutoboa mwili mzima.* Katika muktadha wa kauli hizo, ujumbe huwa umewasilishwa kitaswira na huweza kueleweka kwa kufafanua taashira zilizotumiwa.

Kadhalika, kutokana na methali, mshairi ameweza kujenga isitiari ndogo ndogo ambazo huchangia katika uwasilishaji wa ujumbe katika shairi. Kwa mfano, utajiri unaotokana na rasilimali au migodi iliyopo hauwafaidi wanajamii kwani *sisi twala njaa kwetu mitaani* na ukosefu wa kazi umeshamiri katika jamii hizo. Kadhalika, wafanyikazi au vibarua wanapoongezewa ujira hawapewi nafasi ya kuzungumzia au kulijadili swala hilo kama ilivyokaririwa kuwa:

Watu kukutana kwa hiari
Kuongeza asili-mia kwa siri
Itakayowaondolea mamilioni
Chakula chao mezani. (Uk. wa 47)

Anachokieleza mshairi ni kwamba, mawakala hao hawaishirikishi jamii katika kufikia maamuzi mwafaka bali huipangia na kuiamulia. Kwa hivyo, maamuzi hayo hayaifaidi jamii bali huiongezea dhiki katika maisha.

Ingawa mshairi habainishi ujumbe wazi wazi, hutaka hadhira ijiulize kwamba:

- Ni kweli kwamba jamii zilistahili kutendewa dhuluma zote hizo?

Jibu la swali hilo ni: *La hasha*! Sababu ni kwamba, jamii zinajitolea kufanya kazi kwa bidii na utajiri wa madini upo! Matarajio ya jamii ni kuwa, itapata faida au tija kubwa kutokana na rasilimali iliyopo lakini imo katika lindi la dhiki kubwa isiyo kifani. Kwa mfano, katika kubainisha na kuitafakarisha zaidi hadhira, imekaririwa kuwa jamii hizo zimo katika *mathare za dunia* zenye *milolongo ya wasio-kazi*. Kadhalika, mipango hiyo ya kuinyonya na kuifilisi jamii hupangwa kwa siri huko *Washington, London na Geneva*. Hayo ni mataifa ambayo hayajali utu na maendeleo ya mataifa 'machanga' (Thiong'o 1993). Ili jamii hizo zipate halali yao ya *wakionacho*, hustahili kujikomboa kimawazo kwa kutumia mbinu zilizooana na utamaduni wao. Mshairi amedhihirisha uhamasishaji huo, kwa kuinasihi jamii kuwa:

Njoo basi, sogea kidogo
Tuimbe nyimbo zetu
Zile nyimbo za unyago
Bwana kula-Njama katuletea muhogo (Uk. wa 47)

Aidha, mfumo wa maneno yanayopatikana katika methali hiyo huhiaji kufasirika zaidi kiisitiari. Kwa hivyo, matumizi yake yamesaidia katika kujenga muktadha wa kuibulia na kuendeleza mawazo ya mshairi kuhusu ukoloni-mamboleo. Hapa ieleweke kuwa katika muktadha wa shairi, methali imetumiwa kama mojawapo za kauli ya kiisitiari zinazoukariri ujumbe unaowasilishwa. Hiyo imemaanisha kuwa, dhima ya methali hufafanuliwa zaidi kupitia kwa kauli muhimu zilizotumika katika kujengea usambamba wa maelezo au hoja kwenye shairi. Ingawa methali imejitokeza katika ubeti mojawapo, mwangwi wake huhisika kiisitiari katika shairi zima. Isitoshe, ufafanuzi wa isitiari inayoibuliwa katika methali huweza kupatikana pia kupitia kwa maelezo na mifano iliyotumiwa.

Kama vile ilivyoelezwa hapo awali, usomaji wa na shairi lote kwa ujumla, huelekezwa kwa viakifishi vilivyotumiwa. Kwa kutumia alama ya mshangao, mshairi ameweza kuchochea utafakuri katika usomaji wa shairi. Kwa hivyo, mshairi huitaka hadhira ipige bongo kila wakati inapokumbana na kauli teule iliyoibuliwa na kutumika katika shairi. Katika muktadha uliojengwa, hadhira haitarajiwi kuridhi kauli zilizotumika kiholela bali hupaswa kuzichukulia kama ishara muhimu ambazo huhitaji kufasirika na kupatanishwa na uhalisi katika utamaduni wa jamii.

4.1.4.6 Methali kama Mbinu ya Kuibulia Usemezano

Kwa kutumia methali, mshairi amejenga msingi wa usemezano katika usawiri na uwasilishaji wa shairi. Katika shairi, imebainishwa uhusika wa aina mbalimbali kama vile: fanani anayeuwasilisha ujumbe; mhusika anayejisemeza na msemezaji

anayewasemeza wahusika wengine. Kwa hivyo, kuna kurunzi ya wahusika wa aina tatu: mshairi kama msemeza, msemezwa na wasemezwa. Hapa ieleweke kuwa mjadala huo hutokea ndani ya nafsi ya mshairi. Kwa mfano, mshairi kama msemeza huwa ana mchomo wa hisi ambazo huziwasilisha kwa msemezwa au hadhira pana. Kwa hivyo, huichukulia hadhira yake kuwa *dada* na *ndugu* kama ilivyotongolewa kuwa:

> *Tuna haja ya shaka, dada zangu?*
> *Tuna haja ya utafiti, ndugu zangu?* (Uk. wa 45)

Ingawa mshairi ametumia maswali hayo ya kibalagha, huilenga hadhira pana. Kwa sababu, maswali hayo si lazima kuweza kutolewa majibu bayana bali huweza kujibiwa ndani kwa ndani na mshairi au hadhira kusudiwa (Bhaktin 1990). Kadhalika, kwa kukitumia kiambishi [*u*] cha nafsi ya umoja katika methali, mshairi huweza kulielekeza swali lake kwa mtu binafsi. Vile vile, mshairi ameweza kujisemeza yeye mwenyewe katika nafsi yake au kusemezana na hadhira. Hilo limetokea kwa kuzingatia uelekezi wa kiambishi hicho cha [*u*] kama ilivyobainika katika methali ya *Basi ukionacho ndicho ukipatacho*. Usemezano wa kinafsia, kama mbinu ya uwasilishaji hubainika pia katika baadhi ya tungo zingine za ushairi. Kwa mfano, katika shairi la 'Moyo Iwa na Subira' (Abdalla 1973:48), msanii ametongoa kuwa:

> *Usiliye moyo wangu, siliye moyo nyamaza*
> *Usijitie matungu, siliye 'tajiumiza*
> *Huno ndiwo ulimwengu, muna yasiyopendeza*
> *Kwa hivyo moyo nyamaza, zaidi kuwa na subira* (Ubeti wa 1)

Katika ubeti huo, mtunzi ameweza kusemezana na nafsi yake kutokana na machungu aliyonayo kwa uelekezo wa kiambishi [*u*] mwanzoni mwa mishororo miwili ya mwanzo. Kadhalika, methali haikutumiwa lakini kutokana na ujumbe ulioibuliwa, mwangwi wa

methali ya 'subira huvuta heri' hugonga ndipo. Kwa njia hiyo, mshairi hupata nafasi ya kuzua mjadala wa ndani kwa ndani ili kuweza kuuasa moyo wake. Kwa sababu, baina ya msemeza na msemezwa pana ujumbe ambao huunganisha pande hizo mbili.

Katika utungo unaochanganuliwa, chombo cha kupitishia ujumbe huo mahususi ni kiseme ambacho ni methali iliyotumika. Ushikamano katika mfumo wa mawasiliano hayo huhitaji mihimili hiyo yote miwili ya msemezaji na msemezwa. Kama mwanajamii, mshairi hajitengi na wenzake ambao hudhikishwa kwa kuathiriwa na mfumo huo wa ukoloni-mamboleo (Gibbe 1990). Kwa hivyo, kwa kutumia kiambishi [*Tu*] na kwa kusema *dada zangu* na *ndugu zangu*, mshairi hujinasibisha zaidi na jamii yake. Hata hivyo, ujumbe unaoibushwa na unaowasilishwa ndio wa msingi zaidi kwa hadhira pokezi. Ili kufahamikiwa zaidi kuhusu ujumbe uliowasilishwa, ni muhimu kwa msomaji kulisoma shairi lote kwa kuzingatia usaili na utafakari wa mfumo wa ukoloni-mamboleo na namna ilivyodhihirishwa. Zaidi ya kwamba mbinu ya usemezano ni muhimu iliyotumika katika utungo, imedhihirisha pia mizungu na umbuji wa mshairi katika usarifu wa lugha.

4.2 UCHANGANUZI WA USHAIRI WA SAID A. MOHAMED: *JICHO LA NDANI*

Diwani hii ya *Jicho la Ndani* ilitungwa na Said Ahmed Mohamed kwa mara ya kwanza mwaka wa 2002 na kuchapishwa na shirika la Longhorn Publishers (K) Limited. Diwani hii ni kusanyiko la mashairi tisini na sita. Kati ya mashairi hayo ni saba tu ambayo

yametumia methali. Mshairi hayo mahususi ni: 'Maisha yawa Bahari', 'Jicho la Ndani', 'Jicho Geni', 'Kesho', 'Mja', 'Donda Ndugu' na 'Nguvu Hazilei'.

Kama vile ilivyoelezwa kuhusu diwani ya *Chembe cha Moyo,* mashairi mengi yanayopatikana katika diwani hii hayakutumia methali kwa uwazi. Hali hiyo pia, hudhihirika katika diwani ya *Jicho la Ndani.* Ingawa hivyo, mashairi hayo yametumia kauli ambazo zinawiana na methali. Katika kutathmini dhima ya methali katika mashairi hayo ni manne tu ndiyo yamezingatiwa, nayo ni:

(i) Mara mia La!

(ii) Jicho Geni

(iii) Nguvu Hazilei

(iv) Kesho

4.2.1 Shairi: Mara Mia La!

Shairi hili lina beti nne ambapo kila ubeti una mishororo sita. Shairi limezungumzia kuhusu athari za kauli zilizotumika katika mawasiliano ya watu. Ingawa mtu huweza kutoa kauli ambazo si za kihisia, huweza kupokelewa na kufasiriwa vingine miongoni mwa watu. Kwa hivyo, ni vyema kutathmini kauli zilizotolewa badala ya kujipatiliza msimamo ambao huweza kuzuzua katika akili ya mpokezi wa ujumbe. Kwa sababu, huenda mtu huyo alikuwa ametoa maoni tu ya kuelekeza au kushauri ambapo haziambatishwi na hisia zozote. Isitoshe, ni muhimu mpokezi wa ujumbe awe mwenye subira katika utathmini wa kauli zilizotumika katika mawasiliano ya watu. Katika

kulisawiri shairi hili, mtunzi ametumia methali ya *Jambo usilolijua, kama Usiku wa kiza* na kauli zingine za makusudi ili kuwasilishia ujumbe kama ilivyobainishwa.

4.2.1.1 Methali kama Msingi wa Kuibulia na Kusawiria Mawazo

Methali hiyo imetumiwa kama dira ya kumwongoza mshairi katika kuibulia na kusawiria mawazo. Kwa ambavyo imetumika mwanzoni mwa utungo, humfanya mshairi kubainisha mwelekeo aliouchukuliwa katika mawazo yaliyowasilisha. Msomaji anapokumbana na methali hiyo, hufahamu kabla kuhusu mawazo yaliyotarajiwa kuwasilishwa kuwa: *Jambo* lisilojulikana ni kama *usiku wa kiza.*

Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mtunzi huwa ana mpekecho wa mawazo ambayo huelekezwa kupitia kwa tajiriba yake. Kwa hivyo, kauli msingi huweza kuwa kichocheo cha kuusawiri, kuufafanua na kuuwalisha ujumbe kwa hadhira (Whallon 1969). Ingawa msanii ametumia anwani ambayo si ya methali, ufafanuzi wa ujumbe hupata mwelekeo kupitia kwa methali iliyotumika.

Kwa uelekezo wa mantiki hiyo, mshairi hana haja ya kupoteza wakati bali kujitosa moja kwa moja katika kufaragua na kuwasilisha ujumbe wake kuhusu maswala ya kijamii, mathalani, usuhuba unaotarajiwa kuanzishwa. Kwamba, mtu anaposhikilia jambo ambalo limegubikwa katika siri na kuchukulia kuwa ameukata au amepata murwa; ni kama anayeishi katika njozi. Hiyo ndiyo sababu ya kukaririwa kuwa; hisani na nasaha zake nzuri zisifasiriwe kuwa ni ishara ya kutaka au kukubali kuanzishwa kwa mahusiano. Katika muktadha huo, amesema kuwa:

'sichukulie mfao *wa yangu njema kalima*
Na nafasi na kituo *n'lokupa kwa huruma*
Ukadhani ni funguo *kufungulia tuhuma* (Ubeti wa 2)

Katika muktadha wa dondoo hilo, dalili au ishara ya kauli au vitendo vya utu havipaswi kuchukuliwa kiholela. Kwa hivyo, dalili ngeni huzuzua na hueneza uvumi usiokuwa na msingi. Kwa kuukariri zaidi ujumbe, imetongolewa kuwa:

Ungengoja 'katamka *na ishara kutimiza*
Au ningehangaika *wewe kukubembeleza*
Lakini huna hakika *kama unampenda*
Sasa imebainika *hata chembe sijawaza*
Kwako sitaathirika *na moyo wanikataza*
Hasha, si mara moja *la, mara mia la!* (Ubeti wa 3)

Katika dondoo hilo, mshairi amedhihirisha msimamo wake kuwa hataki kabisa kutetereka au kujizuzua kwa mambo asiyokuwa na uhakika nayo. Kwa sababu, huelewa kuwa uvumi una hadaa na hauwezi katu kumfaidi. Hiyo ndiyo sababu ya msimamo thabiti kuchukuliwa kuwa:

Moyo wangu u kwengine *ambako umefungama*
Fumbua macho uone *pendo lilikogandama*
Usijitie swenene *kwenye raha nimefuma*
Tafuta mbinu nyingine *ya uzushi imekwama*
Hasha, si mara moja *la, mara mia la!* (Ubeti wa 4)

Kutokana na maelezo na mifano iliyotolewa ni dhihirisho kwamba, matumizi ya methali yamemsaidia katika kufaragua ujumbe uliowasilishwa kuhusu athari za uvumi. Kadhalika, mwelekeo alionao ndio uliomfanya kuukariri ujumbe kuwa: *Hasha, si mara moja la mara mia la*! Aidha, uvumi huwa *unapita ukizua na watu kuwapoteza.* Kwa hivyo, methali imetumiwa katika kuibulia na kutoa ufafanuzi wa kina ili kushadidia

ujumbe ambao umewasilishwa. Hadhira nayo inapokumbana methali hiyo hapo mwanzoni, huweza kupata fununu ya ujumbe uliotarajiwa kuwasilishwa katika shairi.

4.2.1.2 Methali kama Mbinu ya Kuibulia Usemezano

Katika shairi hili, mshairi ameuwasilisha ujumbe wake kiusemezano kutokana na uelekezo wa methali. Kwa upande mmoja, ameuasa moyo wake na kwa upande mwingine, amezua usemezano na hadhira yake. Kwa mfano, anapotumia kauli hiyo ya methali, ameweza kubainisha ubaya au madhara ya tamaa ambayo husababishwa na uvumi katika jamii. Kwa hivyo, ameuchukulia uvumi kama nafsi ambayo huweza kuathiri mkondo wa maisha yake na pia katika jamii. Katika muktadha wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli teule ambazo hutumiwa katika uwasilishaji wa tungo ni zile ambazo hufundika hekima na busara ya jamii (Barthes 1981). Katika kuielekeza hadhira, mshairi ametumia methali kupitishia ujumbe uliopo. Aidha, amebainisha kuwa, uvumi umemvunjia *murwa*. Kwamba, uvumi hupita mitaani *ukizua na watu kuwapoteza*. Hiyo ndio sababu ameibua mjadala wa nafsi kwamba, uvumi *unasema watambua kwako mimi nimeoza*.

Kwa hivyo, mshairi hataki kabisa kusukumwa wala kuathirika kutokana na tamaa au mahitaji ya kiwiliwili chake. Kwa kuwa anapodhani nafsi yake imepata murwa, *kumbe unajizuzua na tamaa imemcheza*. Kutokana na usemezano huo, ameitaka nafsi yake ibaini kuwa tamaa imekuwa ikimcheza shere na pia kuwazuzua baadhi ya watu katika jamii.

Kadhalika, mshairi ameitumia methali ili kujenga muktadha wa usemezano baina yake na hadhira. Kwa hivyo, anamwambia mhusika huyo kuwa:

Jambo usilolijua ni kama usiku wa kiza. (Ubeti wa 1)

Kama alivyoisemeza nafsi yake, amembainishia msomaji wake kuhusu madhara yanayoweza kusababishwa na msukumo huo. Kwamba, tamaa huweza kumvunjia *murua* na akabaki kujuta maishani. Kwa kuzingatia tamathali ya uhuishaji kupitia kwa neno wa *tamaa*, (kama mhusika halisi) hufahamu kuwa huba lake (kama mhusika katika shairi) haliwezi kutetereka au kubiuliwa kwa vile yupo aliyemjali. Kwa mfano imekririwa kuwa:

Ungengoja katamka *na ishara kutimiza*
Au ningehangaika *wewe kukubembeleza*
Lakini huna hakika *kama unanipendeza*
Sasa imebainika *hata chembe sijawaza*
Kwako sitaathirika *na moyo wanikataza*
Hasha, si mara moja *la, mara mia la!* (Ubeti wa 3)

Katika dondoo hilo, mshairi amekuwa kama mhusika anayezungumza na mwenzake ambaye ana mshawasha wa tamaa. Katika muktadha huo, mtunzi amebainisha kiufundi msimamo wake kuhusu tamaa na humsihi 'mwenzake' atafute pahali pengine pa kuutua mzigo wake. Kwa sababu, ujanja wa mwenzake tayari amekwisha ubaini. Katika hali hiyo, mshairi amebainisha kuwa:

Moyo wangu u kwengine *ambako umefungamana*
Fumbua macho uone *pendo lilikogandama*
Usijitie swenene *kunivuta kwa shutuma*
Siji kwako mavune *kwenye raha nimefuma* (Ubeti wa 4)

Kutokana na kauli anazozitumia mshairi, hadhira huweza kutunga au kubaini malumbano ya wahusika. Hapa ieleweke kuwa, usemezano huo umeongozwa au umeelekezwa kwa methali iliyotumika hapo awali. Katika kuukamilisha mjadala au usemezano kwenye shairi hili, mshairi ametoa kauli au silaha ya mwisho, kwamba:

Tafuta mbinu nyingine ya uzushi imekwama
Hasha, si mara moja la mara mia la! (Ubeti wa 4)

Kwa hivyo, mshairi hana nia ya kumsikiliza mtu au mhusika asiyetafakari kwanza kabla ya kufikia msimamo mwafaka unaotarajiwa katika uhalisi wa mambo.

4.2.1.3 Methali kama Kauli ya Kuwasilishia Uzindushi na Maadili

Katika shairi hili kuna ujumbe unaowasilishwa kwa azma ya kuizindua na kuiadilisha jamii kupitia kwa kauli anazozitumia. Kwa kuitumia methali, mshairi ameweza kuizindua nafsi yake na jamii kuhusu ubaya wa tamaa. Katika kufanya hivyo, huitaka nafsi yake na hadhira au jamii yake iwe yenye mwelekeo ufaao katika maisha. Kwa mfano, haoni mwafaka wowote ambao huweza kutokana na uzushi uliojikita katika tamaa.

Ingawa mjadala au mdahalo ulioumuliwa katika nafsi yake na mhusika mwenzake wa kidhahania, kimsingi, mshairi huitanabahisha jamii izinduke na ibadili mwenendo hasi kuhusu uelekezi wa tamaa zilizozuzua. Ujumbe wake unaowasilishwa ni kwamba: si busara kuendekezwa kwa jambo lisilojulikana, kwani ni *kama usiku wa kiza.* Kwa mfano, mtu aliyeelekezwa kwa tamaa na msukumo wa silika, huweza kumzuzua na kuipotezea mwelekeo jamii.

Zaidi ya kwamba ujumbe uliowasilishwa ni wa uzindushi, pia maadili yaliyoibuliwa hayaachwi nyuma. Kwa hivyo, ujumbe hupata mwelekeo kupitia kwa methali iliyotumika yaani: *Maskini akipata, matako hulia mbwata.* Aidha, mtu anapozungumza na mwenzake kwa taadhima na utu, isiwe ni kigezo cha kumfanya kufikiria kuwa huyo mwenzake amesalitika kimapenzi. Mshairi amenasihi kuwa:

'Sichukulie mfao *wa yangu njema kalima*
Na nafsi na kituo *n'lokupa kwa huruma*
Ukadhani ni funguo *kufungulia tuhuma*
Ni desturi ya vyuo *ya watu waliosoma*
Ucheshi na mchukuo *wa dhihaka na kusema* (Ubeti wa 2)

Kwa hivyo, kabla ya kufikia msimamo au kuyakinisha kauli zinazotolewa, ni vyema:

Ungengoja 'katamka *na ishara kutimiza*
Au ningehangaika *wewe kukubembeleza* (Ubeti wa 3)

Kwa hivyo, ni busara mtu kugeza aliyoambiwa ili uhakika kuweza kubainishwa, la sivyo huwa ni kujidhalilisha na kujidhikisha moyo bure. Kwa mfano, mshairi kama mhusika hushangazwa na msimamo wa 'mhusika' mwenzake wa kusalitika kimapenzi ingawa hana uhakika wa jambo hilo lililosetirika katika moyo wa mwingine. Hiyo ndiyo sababu imemfanya mshairi au 'mhusika' kumwambia 'mwenzake' kuwa:

Lakini huna hakika *kama unanipendeza*
Sasa imebainika *hata chembe sijawaza*
Kwako sitaathirika *na moyo wanikataza*
Hasha, si mara moja *la, mara mia la!* (Ubeti wa 3)

Kulingana na dondoo hilo, mtu huhitaji kuwa mwenye subira na busara katika kila hatua ya uamuzi ulioafiki, la sivyo hupata jaka la moyoni bila ya sababu ya msingi. Kwa sababu huenda mtu huyo aliyememuwaza kimapenzi, ilihali ana mwingine ambaye humtegemea na humpenda kwa dhati. Kwa hivyo, amemtarajia mwenzake afungue

macho ili ajibainishie kuwa moyoni mwake hana nafasi ya kumweka. Wazo hilo limedhihirishwa kuwa:

Moyo wangu u kwengine *ambako umefungamaza*
Fungua macho uone *pendo lilipogandama*
Usijitie swenene *kunivuta kwa shuhuma*
Siji kwako mavune *kwenye raha nimefuma* (Ubeti wa 4)

Kutokana na maelezo hayo yaliyoelekezwa kupitia kwa methali, mtu huhitaji kuwa na jicho la upembuzi badala ya kusukumwa kwa mielekeo inayoyumba kwa tamaa za kibinafsi. Kwa sababu hiyo, maadili yaliyowasilishwa yamefungamana na utamaduni wa jamii. Mshairi kama mwalimu mwenye taamuli, amebaninisha madhara ya tamaa ili jamii iweze iongoke kwa kuzingatia misingi ya uadilifu. Kwa sababu, watu hupoteza mwelekeo wa heshima na taadhima kwa kuendekeza zaidi tamaa na fikra potoshi huku wakijiaziri kwa wenzao. Kwa ambavyo mshairi ameitumia methali hiyo mwanzoni mwa utungo, imekuwa dira mwafaka ya kufaragulia maudhui au mawazo ya uzindushi na pia kuwasilishia maadili.

4.2.1.4 Methali kama Mbinu ya Kuundia Taswira

Ujumbe uliowasilishwa umeweza kufanikishwa kwa kuzingatia kauli za lugha zilizojenga taswira iliyoibuliwa. Taswira hiyo ni ya kimaono na kihisi. Kwa mfano, hadhira inapokumbana na methali hiyo mwanzoni, hujenga picha ya mtu ambaye hushikilia mawazo ambayo hana uhakika nayo. Ili kufafanua zaidi taswira hiyo iliyoundwa, mshairi amechora picha ya mwanamke au mwanamume ambaye anamwendea mtunzi (ambaye ni mhusika) kwa lengo la kutaka kuanzisha usuhuba wa kimapenzi. Hata hivyo, mhusika huyo amesumbuka mno kimawazo ingawa ameambulia patupu.

Kadhalika, taswira hiyo humfanya msomaji kuwaona watu ambao wanalumbana. Kwa mfano, mmoja kati ya wahusika hao (ambaye ni mshairi) huhoji kuwa:

Unasema watambua *kwako mimi nimeoza*
Kumbe unajizuzua *tamaa imekucheza*
Unapita ukizua *na watu kuwapoteza* (Ubeti wa 1)

Ingawa malumbano hayo huenda yanatokea katika akili au mawazoni mwa mshairi, ukweli ni kwamba husemezana na nafsi yake au mhusika mwingine katika shairi. Zaidi ya hayo, mhusika ana mwendani wake ambaye wameshibana kama ilivyobainishwa kuwa:

Moyo wangu u kwengine *ambako umefungama*
Fumbua macho uone *pendo lilikogandama*
Usijitie swenene *kunivuta kwa shuluma*
Siji kunako mavune *kwenye raha nimefuma* (Ubeti wa 4)

Kwa hivyo, kauli katika dondoo hilo, hudhihirisha kuwa taswira iliyosawiriwa ni ya watu wawili wanaolumbana: mshairi na mhusika mwingine wa kidhahania. Hata hivyo, hakuna ukakika unaobainisha jinsia ya mhusika huyo anayezungumza au mpokezi wa ujumbe huo. Kimsingi, mmoja kati ya wahusika hawa amemwendea mwenzake kwa jambo moja ambalo hana uhakika nalo: kumtaka awe mpenzi wake kutokana na tamaa aliyonayo. Hiyo imetokana na vile amekuwa akizungumziwa vizuri hapo awali huku akidhani kuwa chambo kitanasa. Kinyume na matarajio hayo, mhusika (ambaye ni mshairi) hana hisi wala nafasi ya kumweka akilini. Hiyo ndiyo sababu ya kutanabahisha, kuwa:

Lakini huna hakika *kama unanipendeza*
Sasa inabainika *hata chembe sijawaza*
Kwako sitaathirika *na moyo wanikataza* (Ubeti wa 3)

Kutokana na maelezo hayo, mhusika anayemwendea mshairi anaonekana kama mtu ambaye ana jaka au hangaiko la moyo. Kwa sababu, matilaba yake hayaridhiwi ingawa alikuwa na 'uhakika' wa kupata kile alichokitarajia. Kwa hivyo, kupitia kwa kauli zilizozitumika, msomaji huweza kubaini wasifu na mwelekeo wa mshairi kama mhusika. Kwamba, ni mtu ambaye ana mwelekeo au msimamo thabiti kuhusu uhalisi wa maisha na maswala ambayo huzuzua ilihali mwenziwe huelekezwa kwa silika na tamaa ya kihisia. Kwa mfano, imeonywa kuwa:

Ungengoja 'katamka *na ishara kutimiza*
Au ningehangaika *wewe kukubembeleza* (Ubeti wa 3)

Mhusika huyo angetilia maanani subira na stahamala ya kung'amua ukweli wa mambo angeweza kuenga msimamo usiotetereka. Zaidi ya ufafanuzi wa maelezo yaliyotolewa, methali iliyotumika imemfanya mshairi kuuthibiti uwasilishaji wa utungo kwa kujenga taswira ya kimaono kupitia kwayo. Kwa hivyo, methali imeweza kubainishwa zaidi kupitia kwa kauli zingine zilizotumika hushirikiana katika uwasilishaji wa ujumbe.

4.2.1.5 Methali kama Mhimili wa Muundo na Mahadhi

Methali hiyo imetumiwa siyo tu kama nyenzo au kichocheo cha kuibulia mawazo bali pia hushikilia nafasi muhimu katika muundo wa shairi. Kimsingi, muundo wa methali huwa umedhibitiwa katika misingi ya kisarufi (Babusa 2009 na Wamitila 2008). Kwa hivyo, huweza kuchukuliwa jinsi zilivyo na kuchopekwa katika mikarara ya mishororo katika shairi. Kwa ambavyo methali ni miongoni mwa kauli zilizokubalika katika mawasiliano ya jamii, imetumiwa mahususi kuumbia mojawapo ya mishororo katika shairi. Kwa mfano, mshairi ameweza kupata idadi kamili ya mizani zilizohitajika yaani mizani kumi

na sita au mizani nane kwa nane katika ukwapi na utao. Kadhalika, mshairi amepata kina cha ndani [α] na cha nje [za] katika ubeti wa mwanzo. Kwa hivyo, matumizi ya methali hiyo hulifanya shairi kuwa na ridhimu au mahadhi yaliyotawala. Kimsingi, ridhimu na mahadhi ya ushairi hutokana na mpangilio wa vipindi vya mapigo ya sauti. Kwa kuzingatia hayo, huweza kupunguza maudhi masikioni na vile vile kuwasilisha hisi za mtunzi (Kahigi na Mulokozi 1979, Leech 1969 na Nowottny 1968). Kwa hivyo, ujumi na mahadhi katika shairi yameweza kuwasilishwa kupitia kwa methali. Matumizi hayo ya methali yamelifanya shairi kujiweka katika mkabala wa mashairi ya kimapokeo ya Kiswahili. Kwa mfano, katika utunzi na uwasilishaji wa shairi, mizani na takriri ya vina ni baadhi ya mambo ambayo ni ya msingi (Noor 1988). Kwa ambavyo methali iliyotumika imejitokeza mwanzoni mwa shairi, huwa imejenga msingi wa kuibulia kauli zingine ambazo zimeshabihiana na muundo wa methali hiyo.

Katika muktadha wa shairi, ujumbe uliosawiriwa ni ule ambao umekaririwa kwa methali iliyotumika. Isitoshe matumizi hayo yamesaidia katika kujenga mishororo ambayo huhitajika katika muundo ambao hupata uelekezo kupitia kwa methali iliyotumika.

4.2.2.0 Shairi: Jicho Geni

Shairi hili lina beti nne. Vile vile, ni miongoni mwa mashairi mafupi yanayopatikana katika diwani hii. Kulingana na nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mtunzi wa ushairi hana muda mwingi wa kuelezea ujumbe kwa ukamilifu.Kwa hivyo huwasilishwa kwa kudokezwa (Parry 1971). Kadhalika, utungo wa ushairi huwasilishwa kwa kauli ambazo zimejengeka katika tamathali za usemi (Jacobson 1960). Kwa hivyo, ufupi wa utungo

haimaanishi kuwa ujumbe haujawasilishwa kikamilifu. Kila ubeti una mishororo mitatu. Katika shairi hili, mtunzi amezungumzia kuhusu dosari iliyopo katika kuzingatia mambo kijuujuu. Kwa mfano, mgeni anapofika pahali fulani, huenda akaona baadhi ya mambo yaliyopo na kuchukulia kuwa huo ndio uhalisi wa maisha. Kimsingi, uhalisi wa jamii huweza kuyakinishwa kwa mwafaka zaidi kupitia kwa yule ambaye ana tajiriba pana kuhusu mkondo wa maisha unaomzunguka. Katika uwasilishaji, kumetumiwa methali ya *Jicho geni si angavu ingawa nalo laona* na baadhi ya kauli zilizoibuliwa kwa makusudi katika uwasilishaji wa shairi kama ilivyobainishwa hapa.

4.2.2.1 Methali kama Msingi wa Kuibulia na Kuwasilishia Ujumbe

Katika muundo wa shairi, methali imetumiwa kama anwani na pia kauli ya msingi ya kutanguliza mawazo au ujumbe katika shairi. Mshairi ameitumia methali hiyo kwa makusudi. Mshairi amedokezea ujumbe wake kupitia kwa kauli *Jicho Geni* kuwa anwani kamili katika shairi. Aidha anwani hiyo imedokezea pia methali iliyotumiwa katika utungo. Kwa kufanya hivyo, mshairi ameweza kupata uelekezo mzuri wa kuibulia mawazo na pia kuelekeza usomaji wa shairi.

Isitoshe, mdokezo huo wa methali umekuwa ni mada msingi ambayo imepaswa kufafanuliwa kwa kina. Kadhalika, mshairi ameitumia methali hiyo kwa ukamilifu wake kama mshororo msingi katika utangulizi wa ubeti wa awali yaani *Jicho geni si angavu, ingawa nalo laona.* Kwa uelekezi wa methali imekuwa dira ambayo imeongoza katika kuibulia hisi na ufaraguzi wa mawazo. Katika mantiki hiyo, mshairi amezua mambo mbalimbali yanayohusu ugeni, kama ilivyodhihirishwa kuwa, *jicho geni*:

Daima hujaa kuvu *penye nuru kubwa sana*
Sababu lakosa nguvu *kuona vil'ofichama* (Ubeti wa 1)

Katika muktadha wa dondoo hilo, *jicho geni* ni zuri na linapendeza lakini kutokana na ugeni wake haliwezi kung'amua mambo mabaya yanayokithiri na yanayoiathiri jamii. Aidha, *jicho geni* huona tu mambo ambayo ni ya juu juu. Kwa sababu, mambo yaliyofichama huhitaji uzoefu na tajiriba pana ambapo halina uwezo huo. Jicho hilo linapotazama huwa na mwelekeo ambao huupotosha uhalisi wa mambo. Kama ilivyokarirriwa kuwa:

Jicho geni ni potovu *ingawa laona sana*
Hupaona patulivu *kumbe fujo nazo kuna*
Mbele yake tononovu *nyuma shida zaandama* (Ubeti wa 3)

Kulingana na mshairi, *jicho geni* haliwezi kuthaminiwa kama chombo cha kubainishia uhalisi wa jamii. Kadhalika, ametamani jicho badalia ambalo hutarajiwa kuwa pekuzi na penyevu. Jicho hilo ni lile lisiloweza kuwa na mwelekeo unaopotosha kutokana na mtazamo wa kijuujuu. Kama ilivyobainishwa kuhusu matarajio ya jicho hilo, ni kuwa:

Natamani li'kuzivu *iole vina kwa vina*
Ekisirei penyevu *liwe kikwazo halina*
Ela tamani ni povu *mara maji hulisukuma* (Ubeti wa 3)

Katika muktadha wa dondoo hilo, dhana kama vile: *Ekisirei penyevu*, *Ela ni povu* na *maji hulisukuma* zimetumiwa ili kuelekeza na kuendeleza ujumbe ambao umewasilishwa.

Kwa hivyo, *Jicho geni* ni *povu* ambalo *mara nyingi maji husukuma.* Katika msingi huu, methali iliyotumika huwa ni mhimili wa kujengea kisa na pia chombo cha kuibulia

mawazo ambayo yamewasilishwa. Vile vile, kutokana na matumizi hayo, hadhira imeweza kujengewa muktadha wa kuufasiri ujumbe kwa kurejelea methali iliyotumika.

4.2.2.2 Methali kama Chombo cha Kubainishia Mwelekeo wa Mshairi na Uzindushi

Kwa kutumia methali, mshairi ameweza kubainishia itikadi yake kuhusuya uzindushi wa jamii. Kwamba, *jicho geni* huwa lenya mtazamo finyu kuhusu dhiki zilizo katika jamii. Katika mantiki hiyo, mshairi halithamini jopo kazi hilo katika kubainisha matatizo ya jamii. Tathmini inayopatikana au inayotolewa hupumbazwa au kughilibiwa kwa mambo madogo madogo ambayo si ya msingi. Ili kuukariri ujumbe kuhusu swala hilo, imesisitizwa kuwa, *jicho geni*:

Daima hujaa kuvu *penye nuru kubwa sana*
Huona vishehenevu *lin'opasa kuviona*
Vya juu vielelevu *si vya chini vin'o kina* (Ubeti wa 1)

Kwa hivyo, maono ya *jicho geni* hayana mwelekeo anofaa kuhusu dhiki za jamii. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, *jicho geni* haliwezi kuwa na ithibati tosha kuhusu mambo ambayo yamefichama. Kwa sababu, mizani hizo huwa hazina mashiko. Kwa *sababu lakosa nguvu kuona vilofichama.* Msimamo wa mshairi ni kwamba, mgeni ambaye hajazama au hajaloa katika matatizo hayo ya jamii, Kwa hivyo, hawezi kamwe kuchukuliwa kama mwakilishi wa dhati wa jamii hiyo. Hilo limetokana na dhana kwamba, huyo ni mgeni. Kwa hivyo:

Hupaona patulivu *kumbe fujo kuna*
Mbele yake tononovu *nyuma shida zaandama* (Ubeti wa 3)

Katika muktadha wa dondoo hilo, ubainishaji wa matatizo katika jamii kupitia kwa *Jicho geni* yameekezwa kwa ishara potovu ambazo ni za kijuujuu. Kwa hivyo, mshairi hana

imani na watu ambao hujifanya kuwa wajuzi kumbe lengo lao ni kuupotosha uhalisi katika jamii. Mshairi anachokitarajia ni, jopo kazi la wazalendo ambalo lina nia ya kuibua uchafu wote uliosakini katika jamii. Watu hao ndio mshairi huchukuliwa kuwa wenye *jicho* pembuzi la *Ekisirei penyevu* ambalo ... *kikwazo halina.* Katika muktadha huo, watu ambao hawana nia ya kuibua na kurekebisha kiini cha matatizo sugu katika jamii ni wale ambao wana jicho geni ambalo *ni povu mara maji hulisukuma.* Katika muktadha huu, jamii haiwezi kujinasua kutokana na matatizo yanayoisakama.

Kutokana na kauli zilizozitumika, mshairi ameweza kubainisha mwelekeo wake kuhusu *jicho geni.* Ubainishaji huo wa udhaifu wa 'jicho geni,' zimesaidia katika kujengea mazingira ya sauti ya utetezi na ya uzindushi wa jamii. Katika hali hiyo, mshairi ameihamasisha jamii ili kuweza kuigeuza mielekeo yao kuhusu ugeni na kushirikisha mtazamo unaoibuliwa katika misingi ya utamaduni wao. Kulingana na mawazo yaliyowasilishwa, 'jicho geni' si la kuthaminiwa kama suluhishi la mtatizo katika jamii. Kwamba, 'jicho geni': *Daima hujaa kuvu penye nuru kubwa sana* na pia *lakosa nguvu kuona vil'ofichama.* Katika muktadha huo, mshairi ameitaka hadhira au jamii ibainikiwe na uhalisi huo huku ikijiuliza maswali kama:

- Kwa nini, wanajamii wakubali matatizo yao yatatuliwe
  kwa uzingatifu au mwelekeo wa mtazamo wa kigeni?
- kwani hakuna wazalendo ambao wanaweza kutoa mwangaza
  au mwelekeo wa kutatulia matatizo katika jamii yao?

Kwa hivyo, jamii imehimizwa ijiamini. Kwamba, matatizo hayo huweza kutatuliwa na wanajamii wenyewe. Kwa sababu, mgeni *Hupaona patulivu kumbe fujo nazo kuna.* Mshairi tayari hapo mwanzoni amekwisha kubainisha kuwa *Jicho geni si angavu ingawa nalo laona.* Kwa hivyo, swali ambalo huweza kuibuka katika akili ya msomaji ni: jamii inatarajiwa kufanya nini? Kulingana na mtazamo ambao umewasilishwa ni kwamba, jamii huhitaji kuwa na wazalendo ambao wana jicho la *Ekisirei penyevu liwe kikwazo halina.* Endapo jamii itakuwa na watu wa aina hiyo, ndipo itakapopiga hatua mwafaka katika maendeleo yake ya kiuchumi kisiasa na kijamii. Katika muktadha huo, mshairi huitaka jamii isitegemee wageni kutoka nje bali kutoka ndani; kwa vile hao ndio wanaofahamu fika matatizo yao. Hata hivyo, mshairi ametahadharisha kuwa watu hao teule wawe ni wale walio tayari kuihudumia jamii na kuweka pembeni masilahi yao ya kibinafsi. Hapa ieleweke kuwa, matumizi ya methali yameweza kujenga mazingira ya kubainishia mwelekeo uliotarajiwa kwa malengo ya kuihamasisha jamii.

4.2.2.3 Uundaji wa Kejeli Kutokana na Methali

Ujumbe katika shairi hili umejengeka katika kejeli inayoibuliwa kutokana na methali iliyotumiwa. Kimsingi, mshairi hana matumaini yoyote yanayoweza kutokana na *jicho geni.* Kwa hivyo, jicho ni jicho lakini uwezo na umakini huzidiana. Kwa kuzingatia maelezo yaliyotolewa *jicho geni,* hupumbazwa na mambo ya kijuujuu bila ya kutafakari kwa kina ili kubainisha undani wa matatizo katika jamii. Kupitia kwa methali, msanii ameweza muktadha wa kuibulia swali la utafakari kuwa:

- Kwa nini jamii ithamini *Jicho geni* ambalo si angavu?

Kulingana na mtazamo wa mtunzi *jicho* hilo *geni,* halioni na katu haliwezi kuwa lenye manufaa yoyote kwa jamii. Ingawa huliona *jicho geni* lina uwezo wa kutazama, halina uwezo mkubwa wa kubaini matatizo yaliyosakini katika jamii. Hiyo ndiyo sababu ya kukaririwa kuwa:

Jicho geni ni potovu *ingawa sana laona* (Ubeti wa 1)

Katika muktadha huo, mshairi huitaka jamii izingatie jicho la ndani au jingine ambalo lina uzoefu na tajiriba pana kuhusu uhalisi wa jamii kuliko *jicho geni.* Kwa hivyo, mshairi humtarajia msomaji kuufasiri ujumbe unaowasilishwa kwa kulikejeli na kulibeza hilo jicho geni. Kwa sababu, jicho hilo *huona vishehenevu linalopasa kuviona.* Hapa ieleweke kuwa, mshairi amekejeli uwezo wa jicho geni katika kubainisha maswala nyeti ya kijamii.

Kwa mfano, baadhi ya watu ambao hutoka nje hupewa wadhifa wa kubainisha na kuyatafutia suluhu matatizo sugu katika jamii. Matokeo ni kwamba, hawafanyi utafiti wa msingi kulingana na matarajio au matamanio ya watu. Kwa sababu, watu hao huzingatia mambo ya kijuujuu ambayo ni potofu pasi na yale yaliyofichama. Kwa hivyo, matatizo yaliyopo katika jamii huendelea kuwepo. Chambilecho mshairi, *jicho geni*:

Hupaona patulivu *kumbe fujo nazo kuna*
Mbele yake tononovu *nyuma shida zaandama* (Ubeti wa 3)

Kutokana na dondoo hilo, *jicho geni* huona lakini haliwezi kuchukuliwa na jamii kuwa chombo mwafaka katika ubainishaji wa matatizo ya jamii. Baadhi ya washairi pia wameweza kufafanua zaidi kuhusu jicho linalotarajiwa kama chombo cha kubainishia

matatizo ambayo huzizinga jamii za Afrika. Kwa mfano, katika shairi 'Kilio cha Afrika' (Mazrui 1988:30), jicho la ndani linapaswa kuona na kusema:

Tazameni miji ikinyongeka
Kwa magugu ya ubepari
Na madhila yakituzika
Yapita yakijikariri (Ubeti wa 3)

Hata hivyo, mshairi ametamani 'jicho la ndani' ambalo linaweza kuwa 'si geni' lakini liwe lile lenye uwezo wa kubainisha uhalisi wa ndani uliostahili, kama ilivyosisitizwa kuhusu matamanio hayo kuwa:

Natamani li'kuzivu *iole vina kwa vina*
Ekisirei penyevu *liwe kikwazo halina*
Ela tamani ni povu *mara maji husukuma* (Ubeti wa 4)

Kwa hivyo, mshairi ameitumia methali kuwa msingi wa kuibulia kejeli katika uwasilishaji wa ujumbe kwenye shairi. Jicho ambalo hupaswa kuzingatiwa si *jicho geni* bali *jicho la ndani.*

4.2.2.4 Methali kama Mbinu ya Kuibulia na Kuwasilishia Ujumbe Kitaharuki

Ujumbe katika shairi hili umewasilishwa kwa uelekezo unaostahili kuanzia mwanzo, kutokana na methali iliyotumiwa. Ingawa methali imetumiwa kama mbinu ya kuibulia mawazo, pia imetumiwa kama kichocheo cha kuidhibiti ilihamu ya usomaji. Hadhira inapokutana na methali hapo mwanzoni mwa shairi, huweza kupunguza kasi ya usomaji na kuanza, kutunga maswali mbalimbali ambayo huhitaji kujibiwa. Kwa mfano:

- Kwa nini *jicho geni* ambalo si angavu ingawa nalo laona?
- Mshairi ameitumia methali kuwasilishia mawazo yenye mwelekeo gani ya msingi?

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Kwa uelekezi wa maswali hayo, hadhira hushawishika zaidi kuendelea kusoma ili ikidhi hamu ambayo imechochewa. Katika mkabala wa nadharia ya Semiotiki, kauli teule zinazotumiwa katika uwasilishaji wa utungo ni zile huufanya ujumbe kuwasilishwa kitamathali. Kauli hizo, humtosa msomaji katika kupiga bongo ili aupate ujumbe batini unaokusudiwa (Kunemah 2008 na Gibbe 1990). Katika shairi, methaliimetumiwa kuwa kichocheo cha utafakari ili msomaji asisitishe usomaji wake. Kwa hivyo, methali -+ yenyewe huwa ni fumbo ambalo linahitaji kufumbuliwa. Kwa mfano, *jicho geni si angavu* kwa vipi? Ufumbuzi wa swali hilo umefafanuliwa kwa uangavu zaidi katika muktadha wa uwasilishaji wa shairi kutoka mwanzoni hadi mwishoni. Kwa hivyo, majibu ambayo yametolewa kuhusu *jicho geni* ni kuwa:

- *Daima hujaa kuvu* *penye nuru kubwa sana* (Ubeti wa 1)
- *Sababu lakosa nguvu* *kuona vilofichama* (Ubeti wa 1)
- *Huona vishehenevu* *lino'pasa kuviona* (Ubeti wa 2)
- *Vya juu vielelevu* *si vya chini vinokina* (Ubeti wa 2)
- *... ni potovu* *ingawa sana laona* (Ubeti wa 3)
- *Hupaona patulivu* *kumbe fujo nazo kuna* (Ubeti wa 3)
- *Mbele yake tononovu* *nyuma shida zaandama* (Ubeti wa 3)

Kutokana na madondoo hayo, *jicho geni* lina dosari na katu haliwezi kutegemewa kutoa mwelekeo mwafaka kuhusu matatizo yaliyosakini katika jamii. Katika mantiki hiyo hadhira huweza kujiuliza:

- Ikiwa mshairi huliona *jicho geni* kuwa na dosari, ni lipi analopendekeza kuwa msingi wa kubainisha matatizo hayo yaliyosakini katika jamii?

Jibu la swali hilo linapatikana katika ubeti wa mwisho katika shairi kuwa jicho hilo linapaswa liwe:

- *... likuzivu* *iole vina kwa vina* (Ubeti wa 4)
- *Ekisirei penyevu* *liwe kikwazo halina* (Ubeti wa 4)

Kwa hivyo, hadhira haiwezi kukidhi haja hiyo hadi inapolisoma shairi hili kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kutokana na methali, mshairi ameweza siyo tu kufaragua mawazo bali pia kuchochea ilhamu ya hadhira kutaka kulisoma shairi lote kwa usaili na utafakari zaidi.

Vile vile, hadhira imedhibitiwa vilivyo kwa kuwa haitaki kusitisha usomaji wake katika methali tu bali inahitaji kufahamishwa zaidi kuhusu ujumbe unaowasilishwa. Hiyo imetokana na dhana kwamba, ujumbe hukamilika katika fingo la ubeti wa mwisho. Katika muktadha wa shairi hili, mtunzi hapotezi muda bali ameingia moja kwa moja kuwasilisha ujumbe wake kwa kuichochea hadhira kudadisi zaidi kuhusu yale yanayowasilishwa. Kwa kutumia methali moja, ameweza kutekeleza mambo mawili ya msingi katika uwasilishaji: kubainisha ubaya wa *jicho geni* na pia kudhihirisha hatua inayopaswa kuchukuliwa kwa mtazamo mahususi unaokusudiwa. Hayo ni mambo ya msingi ambayo yamesaidia katika kuusukuma mbele ujumbe kwa uwepo na uchochezi wa methali iliyotumiwa.

4.2.2.5 Methali kama Mbinu ya Ujenzi wa Usambamba katika Uwasilishaji wa Mawazo

Mshairi ametumia methali kama mbinu ya kujengea usambamba katika utungo. Katika ubeti wa awali, imetumiwa methali ya *jicho geni si angavu ingawa nalo laona.* Kwa kufanya hivyo, tayari mshairi ameyakinisha mwelekeo ambao ameuchukua katika uwasilishaji wa ujumbe. Hata hivyo, haridhishwi na kauli hiyo tu. Kwa kutaka kuukariri zaidi ujumbe, ametumia maelezo yaliyojikita katika kauli au miundo tofauti ya lugha ili

kutomelea au kukoleza zaidi wazo lililoibuliwa kutokana na kauli hiyo ya methali. Msomaji anapoirejelea methali, huwa ana nafasi nzuri kuelewa mwelekeo uliouchukuwa kuhusu *jicho geni* kuwa *si angavu.* Swali ambalo limejenga muktadha wa utafakari ni:

- Iwapo mshairi huiona kauli hiyo ya methali haitoshi kufafanulia na kuwasilishia ujumbe wake, amefanya nini?

Mwelekeo wa kuzingatia ni kwamba, sharti atoe maelezo mengine ambayo huweza kuwa ni tofauti au yamefanana kwa kiwango fulani lakini hujengana na hukamilishana. Kwa hivyo, imebainishwa kuwa, *jicho geni*:

Daima hujaa kuvu penye nuru kubwa sana (Ubeti wa 1)

Kwa kutumia kauli ambazo hupatikana katika dondoo hilo, mtunzi amefafanua msingi wa mawazo kuwa, *jicho geni* lina ukungu unaosababisha kutoona vizuri. Kwa sababu:

Huona vishehenevu lino'pasa kuviona (Ubeti wa 2)

Jicho hilo lililorejelewa ni lile ambalo... *lakosa nguvu kuona vilo'fichama.* Isitoshe, *jicho geni* huona *vya juu vielelevu si vya chini vin'o kina.* Kwa hivyo, msimamo unaopendekezwa kwamba, ingawa *jicho geni* huona, halibainishi kwa uangavu kijini cha matatizo yanayosakini katika jamii. Zaidi ya hayo, mshairi amekoleza zaidi ujumbe kuhusu *jicho geni* kuwa:

Jicho geni ni potovu ingawa sana laona
Hupaona patulivu kumbe fujo nazo kuna
Mbele yake tononovu nyuma shida zaandama (Ubeti wa 3)

Katika ubeti huo, ujumbe umekaririwa kwa kuzingatia hoja tatu za msingi ambazo zimebuliwa kwa miundo tofauti ya lugha. Hapa ieleweke kuwa, ujumbe uliowasilishwa huweza kufanana ingawa kwa kutolewa maelezo au kauli tofauti. Hata hivyo, hoja

zilizowasilishwa zimesaidia katika kuibulia ujumbe katika shairi. Aidha, hoja hizo zichukuliwe kuwa ni mifano au maelezo ambayo huufafanua zaidi ujumbe kupitia kwa methali iliyotumika. Hiyo ndiyo sababu alipoona kwamba tayari mawazo ya awali yamebainishwa bila utata, ndipo msanii ameingia katika ubeti wa mwisho kwa kutoa suluhu kuwa uelekezo wa kushughulikia tatizo lililoibuliwa katika shairi.

4.2.3.0 Shairi: Kesho

Shairi hili lina beti mbili ambapo kila ubeti una mishororo sita. Utungo huu ni mfupi sawia na shairi la 'Jicho Geni'. Aidha, mshairi amedhihirisha jinsi jamii haipigi hatua katika kuuendeleza uchumi wake. Kwa sababu, jamii hiyo imekuwa ikitumia mbinu duni. Kwa hivyo, jamii imeshindwa kabisa kujiendeleza kimaisha. Mbinu za kijadi hazina nafasi yoyote katika kizazi cha sasa na kijacho. Katika msingi huo, mshairi ameitaka jamii kupata maendeleo. Katika kuliwasilisha shairi , mtunzi ametumia methali ya *Iwapo shida 'meganda, hazitoki kwa koleo* na kushadidiwa kwa baadhi ya kunga za katika kuibulia mawazo kama ilivyodhihirishwa hapa.

4.2.3.1 Methali kama Msingi wa Kuwasilishia Maudhui ya Uzindushi

Kutokana na matumizi ya methali hiyo, mshairi ameweza kufaragua na kuwasilisha mawazo yaliyojikita katika uzindushi wa jamii. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mawazo ambayo huibuliwa na huwasilishwa katika ushairi wa kimapokeo hupaswa kuzingatia maadili ya jamii (Propp 1968). Kwa hivyo, kutokana na maudhui ya uzindushi ambayo yameibuliwa, imebainisha kuwa ushairi huweza kuzingatia mojawapo ya ujumbe huo. Ujumbe ambao umewasilishwa kupitia kwa methali hiyo ni kwamba,

jamii haijikakamui ipasavyo. Kwa sababu, *shida meganda hazitoki kwa koleo.* Kupitia kwa kauli hiyo, mshairi amejichukulia kuwa yu miongoni mwa jamii. Kwa hivyo mwelekeo uliochukuliwa ni kwamba, iwapo chombo kitaangamia basi hata yeye ataathirika pakubwa. Kwa kujinasibisha zaidi na jamii yake, imekeririwa kuwa:

- *Iwapo dogo la shinda* *kubwa la**tu**piga ngeo* (Ubeti wa 1)
- *Iwapo yana**tu**pinda* *maisha tuyaishio* (Ubeti wa 2)

Kwa kutumia kiambishi [**-tu**], mshairi amejichukulia kuwa yu pamoja na wengine ambao huishi pamoja katika jamii. Ingawa yu miongoni mwa wanajamii, haridhishwi na mielekeo ya wenzake kuhusu utendakazi wao. Kwa hivyo, ni mwenye maono chanya zaidi kuliko wenzake katika jamii.

Isitoshe, jamii ya sasa imeharibu na imeyachafua mazingira badala ya kuyahifadhi kwa manufaa ya sasa na kwa kizazi kijacho. Hiyo ndiyo sababu ya kuchukua hatua ya kuhimiza kuwa:

- *Iwapo twa'cha kuvunda maziwa ya tegemeo*
  Kesho litakuwa lipi? (Ubeti wa 1)
- *Iwapo twa'cha kupanda kuimarisha vya leo*
  Na kesho vitakuwaje? (Ubeti wa 2)

Kilichobainishwa kupitia kwa madondoo hayo, ni uhalisi wa mambo ambayo yamekuwa yakichukuliwa kuwa ya kawaida. Kwa hivyo, msanii amezua mambo mawili ya msingi: uharibifu wa mazingira na jamii ambayo haitaki kujitahidi katika kilimo ambacho ni uti wa mgogo wa uchumi wao. Isitoshe, jamii iliyosawiriwa ni ile ambayo haina ari katika shughuli zao za msingi. Mambo hayo ni ya dharura na huhitaji kutiliwa maanani, la sivyo jamii itakuwa imedumaza uchumi na maendeleo yake. Katika muktadha huo,

ameizindua jamii yake itathmini mbinu huweza kutumiwa kwa kutozingatia mbinu duni ili maendeleo kuweza kupatikana. Matokeo ya kuzingatia mbinu hizo duni ni kwamba, jamii hupata: *maudhi* na *kwingi kukonda* ambayo ndiyo *tegemeo* lao la sasa na wakati ujao. Kutokana na maelezo yaliyowasilishwa, huenda jamii hufahamu au haifahamu uhalisi uliopo lakini haitaki kuchukua hatua kuboresha maisha.

Kwa kutumia methali hiyo, mshairi amejibainisha kuwa mwalimu, mwelewa na mwenye maono ya busara, ambapo jamii huhitaji igeuze nyendo katika harakati za kukabiliana na matatizo ambayo yameweza kuizinga na kuinyonga. Hiyo ndiyo sababu ya kushikiliwa kuwa:

Iwapo shida meganda hazitoki kwa koleo (Ubeti wa 1)

Ikiwa ni hivyo, vya *kesho vitakuwaje*? Katika kubainisha mbinu zinazopaswa kuzingatiwa na jamii kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Shairi la 'Ndoto na Swali' (Mulokozi na Kahigi 1979:89-91) limetoa uelekezo kuwa:

Na hii ndiyo sababu
Lazima tuchambue chanzo cha kisa
Na kutatua mkato wa mawimbi ya mwimbayo
Tuchambue mienendo kiini
Na kuota ndoto halisi
Inayoongozwa na taa ing'azayo ukweli
Tutalipata jibu

Katika dondoo hilo, wasanii hao wamemulika sababu ya wafanyikazi kutoimarisha hali zao za kimapato na kimaisha. Ili kupata jibu swali hilo, huhitaji kutambua kiini cha matatizo yao ili wayagange kwa manufaa yao ya sasa na kwa kizazi kijacho. Katika uwasilishaji wa ujumbe wametumia kauli kama vile: *Chanzo cha kisa, tuchambue mienendo kiini, ndoto ya haki* na *taa ing'azayo ukweli*. Ujumbe ambao umepitishwa

hapa ni sawa na ule umepatikana kwenye methali iliyotumiwa katika shairi linalozingatiwa.

Vile vile kwa kutumia methali, mtunzi amebainisha na amedhihirisha mwelekeo wake kuhusu maswala muhimu yanayohusu uchumi katika jamii. Kwamba, shida zilizopo kwa wakati wa sasa katika jamii zimeota mizizi sugu na wala haziwezi kundolewa kwa nyenzo au mbinu duni zinazomithilishwa kwa *koleo*. Kwa hivyo, maendeleo ya uchumi wa jamii yamebaki nyuma kila kuchao.Kwa sababu, jamii haitaki kuganga shina la matatizo hayo yanayoidumaza. Msimamo uliopendekezwa ni, jamii isitarajie msisimko au ustawi wa maendeleo kwa kung'ang'ania mbinu hizo duni. Kwa kuzingatia methali, mshairi ameweza kuibua maswali ya msingi kuwa:

- Mbinu duni ambazo huzingatiwa katika jamii zimefaidi nini kwa wakati wa sasa?
- Kizazi kijacho hupata tija gani kutokana na yale ambayo hufanywa wakati wa sasa?

Kimsingi, majibu ya maswali hayo ni ya kukatisha tamaa kwa kizazi cha sasa. Kwa hivyo, msimamo wa mshairi ni kwamba, jamii yake haijitahidi inavyopasa na wala haitoi mwelekeo unaofaa kwa kizazi cha sasa na kijacho.

4.2.3.2 Methali kama Msingi wa Kujengea Usambamba

Katika shairi hili, mtunzi ameuwasilisha ujumbe unaohusu dhiki zinazopatikana katika jamii. Matatizo hayo ni mazito, naye hachelei kuyabainisha katika uhalisi wake. Hata hivyo, jamii hiyo ni kana kwamba imeyazoea na hustahabu kuishi nayo kwa wakati wa

sasa. Kwa mfano, jamii haifahamu kuwa uharibifu wa mazingira umeathiri kilimo ambacho ni uti wa mgongo wa maendeleo ya uchumi wake. Kulingana na maelezo ambayo yametolewa, harakati ambazo hutumika kwa wakati wa sasa huwa ni vizingiti vya msingi wa maendeleo katika jamii. Kwa kutumia methali hiyo ya *iwapo shida 'meganda, hazitoki kwa koleo*, mshairi huitaka jamii yake ibadili au itathmini upya mwelekeo, la sivyo msingi wa uchumi utaporomoka. Kwa hivyo, ujumbe unaowasilishwa tayari umebainishwa lakini umeukaririwa zaidi kwa kutumia kauli mbalimbali ziliyoelekezwa kwa methali.

Kadhalika, methali imetumiwa kama kauli mojawapo ambayo imejitokeza kwa uwazi katika shairi yaani, kama mshororo wa pili kwenye ubeti wa awali. Kwa kufanya hivyo, mshairi huitarajia hadhira itilie uzito siyo tu katika methali na pia katika maelezo yaliyotokana na kauli zingine zilizotumiwa kwa makusudi. Mathalani, msomaji anapolisoma shairi hugundua kuwa, aghalabu mishororo yote imeibuliwa ili ichangae kwa namna moja au nyingine ubainishaji wa ujumbe. Kwa mfano, kauli zilizotumika katika uwasilishaji wa ujumbe hujengana na huibua usambamba kama ifuatavyo:

- *Iwapo leo 'mepinda* *la sawa tulitakalo* (Ubeti wa 1)
- *Iwapo dogo lashinda* *kubwa latupiga ngeo* (Ubeti wa 1)
- *Iwapo yanatupinda* *maisha tuyaishio* (Ubeti wa 2)
- *Iwapo yachondachonda* *maudhi na mengineo* (Ubeti wa 2)
- *Iwapo kwingi kukonda* *ndiko sasa tegemeo* (Ubeti wa 2)

Katika madondoo hayo, imesisitiza wazo moja lakini kwa kauli tofauti zilizotumiwa kwa makusudi. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, ukariri wa maneno au sauti katika utungo ni muhimu katika kushadidia ujumbe unaowasilishwa na pia kujengea mahadhi na ridhimu (Parry 1971). Kwa hivyo, isichukuliwe kuwa mtunzi si gwiji katika

usarifu wa lugha. Kadhalika, kisemiotiki kauli ambazo hutumika huweza kuwa tofauti lakini zinajenga ujumbe mmoja (Jacobson 1986). Kwa hivyo, msanii ana msimamo mmoja kwamba, hana matumaini na mbinu zilizotumiwa na wanajamii katika kuukwamua na kuustawisha uchumi wao. Kutokana na kutumiwa kwa matumizi ya methali, hutaka jamii itambue kuwa; matatizo ya kiuchumi katika jamii yao *'meganda* na wala *hazitoki kwa koleo*. Katika muktadha huo, dhana ya *koleo* imetumiwa kama taashira ya mbinu duni ambazo hutumiwa katika jamii. Kwa hivyo, kauli mbalimbali zilizotolewa zimesaidia katika kujenga usambamba. Kwa hivyo, ujumbe ambao umewasilishwa umekolezwa kwa uelekezo wa methali. Kwamba, mbinu mwafaka huhitajika ili kuukwamua uchumi katika jamii.

4.2.3.3 Methali kama Mbinu ya Kujengea Taharuki

Mshairi ametumia methali kama mbinu ya kutafakarisha na kuupeleka mbele ujumbe unaowasilishwa. Methali hiyo imejitokeza katika mshororo wa pili kwenye ubeti wa kwanza. Katika mshororo wa kwanza, tayari imemdokezwa kuhusu ujumbe ambao umetarajiwa kuwasilishwa kwamba:

Iwapo leo 'mepinda la sawa tulitakalo (Ubeti wa 1)

Kwa kurejelea dondoo hilo, *leo* ya jamii ina kasoro au dosari. Kwa kusisitiza zaidi ujumbe, imesawiriwa kuwa:

Iwapo shida 'meganda hazitoki kwa koleo (Ubeti wa 1)

Hiyo ni kauli ya nguvu ambayo imebainisha zaidi mawazo na hatua hupaswa kuchukuliwa na jamii. Kwamba, endapo *leo* ya jamii *imepinda* hutarajiwa ielewe kuwa *koleo* halitafaa katika kutatulia matatizo yao. Kwa kutumia methali, mtunzi huitaka hadhira yake izingatie zaidi taashira na isitiari ambazo zimeibuliwa. Kwa hivyo, msomaji hujiingiza katika kutafakari vikwazo vya maendeleo ya kiuchumi katika jamii yao. Hata hivyo, matatizo hayo ya kiuchumi yaliyodokezewa bado hayajabainishwa vilivyo. Ili msomaji aweze kufahamikiwa zaidi kuhusu ujumbe unaowasilishwa humbidi awe na subira ya kulisoma shairi lote. Kwa mfano, mshairi amepiga kasi ya kufafanua zaidi kuhusu dhiki zilizopo katika jamii. Kwa hivyo, mshairi amejenga mazingira yafuatayo:

- Siku zimekatika ilihali hakuna mwafaka au manufaa yoyote yaliyopatikana katika jamii.
- Iwapo mambo madogo yamewashinda wanajamii nayo yale makubwa ndio yatawadhikisha zaidi.

Hapa ieleweke kuwa, ubainishaji wa matatizo katika jamii umefafanuliwa punde tu baada ya methali kutumika. Kadhalika, mshairi ametoa mifano ili kuthibitishia mawazo yake. Kwa hivyo, baadhi ya matatizo yaliyopo katika jamii ni kama:

- Shughuli za kilimo haziifaidi jamii
- Wanajamii hawana mwelekeo mwafaka katika kukabiliana na matatizo yao ya kiuchumi na kisiasa.
- Shida zilizopo zimewaathiri mno wanajamii ingawa hawaelewi hayo.

Kwa hivyo, maelezo yaliyowasilishwa ndiyo yaliyopeleka kujenga maswali ya ukariri kuwa:

- *Kesho litakuwa lipi?* (Ubeti wa 1)
- *Na kesho vitakuwaje?* (Ubeti wa 2)

Katika muktadha huo, imebainishwa kuwa, methali iliyotumiwa imesaidia katika kufafanua zaidi ujumbe unaowasilishwa. Zaidi ya hayo, matumizi ya methali pamoja na maswali ya balagha yaliyoibuliwa, yamesaidia katika kujenga taharuki katika usomaji wa shairi. Kwa hivyo, matumizi ya methali huweza kuchukuliwa kuwa msingi unaoumua kauli zilizojenga taharuki katika shairi hili. Katika muktadha wa nadharia ya Semiotiki, kauli teule ambazo hutumika katika uwasilishaji wa ujumbe ni muhimu ingawa kuna zile ambao husaidia katika kufafanua zaidi dhima ya kauli hizo (Peck na Coyle 1984). Kwa hivyo, katika shairi hilo kuna methali kwa upande mmoja na kauli zingine zilizoibuliwa na kwa makusudi. Kwa hivyo, dhima ya taharuki huweza pia kuendelezwa kwa kauli zingine za lugha ambazo huchangia ile ya kauli ya msingi inayorejelewa. Kwa mfano, kichocheo cha usomaji huweza kukidhiwa kupitia kwa maswali yanayoibushwa na pia kupitia kwa maelezo yaliyowasilishwa. Kwa ambavyo methali imetumiwa katika mshororo wa pili wa ubeti wa kwanza, humwelekeza zaidi msomaji kubaini kuwa imeshikilia nafasi ya msingi. Kimsingi, kauli zote zilizotumika katika shairi zina umuhimu ambao huzidiana katika uwasilishaji wa ujumbe. Hata hivyo, methali kama kauli ni angavu zaidi kuliko miundo mingine ya lugha iliyotumika kwa makusudi katika uwasilishaji wa shairi.

4.2.4. Shairi: Nguvu Hazilei

Shairi hili lina beti tatu na kila ubeti una mishororo minne. Kadhalika, linasawiri upungufu wa matumizi ya nguvu katika mfumo wa utawala katika jamii. Kimsingi mawazo yanayowasilishwa ni kwamba, nguvu hazipasi kutumiwa katika kuwaelekeza wanajamii au watawaliwa. Kwa sababu zinapotumika, wanajamii huenda wakahisi kuwa wanakandamizwa na wanayanyaswa. Kwa hivyo, mfumo mwafaka wa kiutawala ni ule ambao huleta maridhiano mema katika jamii. Katika msingi huo, wanajamii hupaswa kuthaminiwa la sivyo huweza kutumia uwezo wao kuuporomosha utawala wanaouhisi kuwa dhalimu. Mtunzi ametumia mbinu mbalimbali za lugha kuuwasilisha ujumbe kama inavyobainishwa. Miongoni mwa kauli hizo zilizotumika ni methali.

4.2.4.1 Methali kama Msingi wa Kuibulia na Kuwasilishia Ujumbe

Katika shairi hili, methali imetumiwa kama kichocheo cha kufaragua na kuwasilishia mawazo ya mshairi. Katika mkabala wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli msingi huteuliwa na hutumiwa kwa hadhari kubwa na msanii. Kwa sababu, kauli hizo huubeba ujumbe unaochochewa kwa hisi za mtunzi (Mulokozi 1986). Kutokana na tajiriba yake, mshairi ana mawazo kwamba *nguvu* haziwezi katu kutumiwa kama chombo cha kusuluhishia matatizo. Kwa hivyo, ametumia methali kuwa dira ya kuwasilishia maono na ujumbe muhimu kwa hadhira. Kwa kutumia sehemu ya kwanza yaani *Nguvu Hazilei* kuwa anwani, mshairi pia ameweza kuidokezea hadhira yake kuhusu ujumbe unaotarajiwa kuwasilishwa. Kwa hivyo, msomaji huweza kupata mwelekeo au muktadha wa matukio yanayotarajiwa kwamba: *nguvu* hazifai kuwa chombo kisuluhishi.

Isitoshe, mshairi ameitumia methali kwa ukamilifu wake kama kauli ya utangulizi katika shairi hili kwamba: *Nguvu hazishiki yai zikishika hutumbuka.* Kwa hivyo, amekuwa mwenye nafasi nzuri ya kumtayarisha kimbele msomaji kwa kumbwagia methali hiyo. Katika muktadha huo imebainishwa kuwa, ameitumia methali kwa makusudi kuwa mwongozo wa kujengea na kuwasilishia mawazo yaliyotarajiwa. Kwa mfano, mtu anapotumia kifua au *nguvu* kama mbinu ya kusuluhishia matatizo katika jamii, huenda watu wakamtuhumu na kumchukulia vibaya hata ingawa mawazo yake huenda yalikuwa yenye manufaa.

Vile vile, katika harakati za kuielekeza na kuihamasisha jamii, *nguvu* katu hazipaswi kutumika. Sababu ni kuwa:

Waoga huwa washupavu
Wajinga huwa werevu!

Kulingana na maelezo yaliyotolewa katika dondoo hilo, *waoga* na *wajinga* ni wale ambao hawajaujua ukweli lakini wanaposhurutishwa huweza kusaili kila wanachokiona au wanachokihisi. Matokeo ya wale wanayoyaona na kutendewa ni, kufunguka macho na kuutambua udhalimu uliotumika au kutambua uhalisi wa mambo. Kwa hivyo, mabavu na ukatili unapotumika, hakuna mwafaka wowote unaoweza kupatikana. Aidha, matumizi ya mabavu katika jamii ni uharibifu wa murua uliokuwepo hapo awali. Kwa ambavyo baadhi ya wanajamii huwa wamekerwa na dhuluma wanazotendewa, hustahabu kusema uongo ambao huubatilisha ukweli, kama ilivyokaririwa:

Wakweli huwa waongo
La sawa huwa mipingo! (Ubeti wa 3)

Kutokana na dondoo hilo, wanajamii hawana hiari bali kuubatilisha uhalisi wa mambo ili kuweza kutuhumiwa kuwa waasi. Kwa hivyo, matumizi ya methali yamesaidia katika kubainishia zaidi hisi na mwelekeo wake kuhusu athari za matumizi ya kimabavu katika jamii. Ingawa mshairi amebainisha ubaya wa matumizi ya nguvu, pia kwa kutumia methali ameweza kuifanya jamii itathmini upya mbinu mwafaka zinazoweza kuwa msingi wa kujengea utangamano na maridhiano mema katika jamii.

4.2.4.2 Methali kama Mbinu ya Kubainishia Mwelekeo wa Mshairi

Mshairi ameitumia kwa makusudi methali kuwa kauli ya kuibulia na kuwasilishia itikadi na mwelekeo wake kuhusu maswala muhimu katika jamii. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, mtunzi ana hisi ambazo humwelekeza katika kuteua kauli anazozitumia (Jilala 2008 na Gibbs 1994). Hiyo hutokana na sababu kwamba, kauli mbili au zaidi huweza kutumika kudhihirishia ujumbe wa msingi. Kwa hivyo, methali imetumiwa kuwa ishara iliyoumua zaidi msimamo na mwelekeo wa mshairi kuhusu matumizi ya mabavu katika jamii.

Kulingana na maelezo yaliyoibuliwa kutokana na methali ni kwamba, *nguvu* au mabavu zinapotumika kama njia ya kukabiliana na matatizo katika jamii itaambulia patupu. Ingawa mtu huweza ana nia njema ya kuielekeza jamii, anapotumia mabavu huenda watu wakahisi kuwa wananyanyaswa na kudhulumiwa. Kwa hivyo, matumizi ya nguvu huweza kuzua cheche za upinzani na makabiliano makali baina ya pande mbili: watawala wemye nguvu na watawaliwa au wasiokuwa na uwezo.

Kimsingi nguvu zinapotumika, jamii hupoteza matumaini na mwelekeo katika maisha. Kwa mfano, jamii ya mshairi imekuwa ikiukubali mfumo wa utawala huo, lakini maguvu yanapokithiri, huweza kujenga mazingira ya kusaili kila tendo, kama ilivyoelezwa:

Twaa hugeuka sugu
Mpole huota gugu! (Ubeti wa 1)

Katika dondoo hilo, imedhihirishwa mwelekeo wa mtunzi kuwa, watawaliwa wanapohisi kuwa wamesukumwa ukingoni, hawataogopa kusaili mfumo huo. Vile vile, hata yule ambaye alikuwa akichukuliwa kuwa *mpole* hatakuwa akiogopa wala kujali chochote kitakachompata. Kwa hivyo, jamii ambayo imenyanyaswa kimabavu huwa imetoneshwa hisi zake kutokana na uhalisi wa mfumo huo. Ujumbe huo pia umebainishwa katika shairi la 'Siwati' (Abdalla 1973:9), ambapo imetongolewa kuwa:

Siwati ngaadhibiwa, adhabu kila mfano
Siwati ningaambiwa 'tapata kila kimono
Siwati lililo sawa silibanduwi mkono
Hata ningaumwa meno, mkono siubanduwi (Ubeti wa 2)

Zaidi ya ubeti huo na pia kupitia kwa ubeti wa kwanza katika shairi la 'Nguvu Hazilei', sauti ya shime imejitokeza ambapo mateso na dhiki haziondoi ari ya mapambano dhidi ya unyanyasaji katika jamii. Katika muktadha huo, mbegu za mapambano huchipuza ili kuutokomeza udhalimu huo. Kwa ambavyo nguvu zimetumiwa katika jamii, huwa ni mazoea hata kama baadhi ya wanajamii wataathirika au wanapatishwa mateso; kwao huwa ni mamoja.

Kulingana na mawazo ya mshairi ni kwamba, wanajamii wanahitaji kuelezwa kwa upole na upendo lakini kwa kutumia mabavu hayatasaidia. Mabavu yanapotumika hupalilia

werevu na kujenga ujasiri miongoni mwa wanajamii. Mtunzi ameendeleza wazo hili, kwa kusema:

Waoga huwa washupavu
Wajinga huwa werevu! (Ubeti wa 2)

Aidha, utawala wa kimabavu unapotumia nguvu, jamii haitakuwa na imani na mfumo huo wa utawala. Daima mawakala wa utawala huo, huchukuliwa kuwa ni maadui katika jamii. Kwa sababu, wanajamii wanashurutishwa kutoa ushuhuda fulani au kutoa mchango wao, husema uongo ili kukidhi haja za kibinafsi za watawala, kama ilivyodhihirishwa kuwa:

Wakweli huwa waongo
La sawa huwa mipingo! (Ubeti wa 3)

Kutokana na kauli hiyo, hali hiyo haiubainishi uhalisi wa mambo bali itaubeua. Kwa hivyo, matumizi ya methali yamesaidia zaidi katika kuibulia na kuwasilishia hisi, itikadi na mwelekeo wa mshairi kuhusu uendekezaji wa mabavu katika jamii. Ingawa mshairi amebainisha hayo, pia ameweza kutoa suluhu kuhusu utawala wa kimabavu kuwa, nguvu katu *hazilei* au hazifai kutumika kama suluhu ya matatizo katika jamii.

4.2.4.3 Ujenzi wa Taharuki Kutokana na Methali

Mshairi ameitumia methali kama chombo cha kuwasilishia mawazo na pia kama msingi mwafaka wa kuibulia taharuki katika usomaji. Msomaji anapokumbana na methali hiyo hapo mwanzoni, hamu ya kuendelea kulisoma shairi huchochewa zaidi. Kwa mfano, hadhira huweza kujiuliza kwamba:

- Mshairi amekusudia nini kwa kutumia methali hiyo?

Katika muktadha wa kauli hiyo, msomaji huwa amejengewa muktadha wa kuibulia hamu ya kulisoma shairi ili kuweza kufahamu mawazo yaliyoibuliwa. Kwa mfano, matumizi ya methali yamesaidia kubainisha mwelekeo wa mshairi lakini kwa kudokezewa tu na wala hajaelezwa kinaganaga kuhusu ujumbe wenyewe. Ili kuweza kufahamikiwa zaidi kuhusu ujumbe, humbidi kupiga mbizi kulisoma shairi kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Mbinu hiyo ya taharuki imekuzwa zaidi kupitia kwa usambamba uliotumika katika shairi. Kwa mfano, mshairi alipotumia methali ameweza kuusukuma mbele ujumbe kwa kuibua mifano na maelezo mengine ambayo yamesaidia kuifafanua zaidi methali iliyotumika. Kwa hivyo, ameanza ufaraguzi wa mawazo kwa kutumia kauli mahususi kuwa vianzo vya beti kama vile:

- *Nguvu katu hazilei zileapo hufujika* (Ubeti wa 1)
- *Nguvu hazishiki yai zikishika zinaruka* (Ubeti wa 2)
- *Nguvu kweli hazilei zileapo huharibu* (Ubeti wa 3)

Endapo msomaji angesitisha usomaji wake katika methali, hawezi kufahamikiwa zaidi kuhusu utawala wa kimabavu usiofaa katika jamii. Kwa hivyo, kutokana na matumizi ya methali, mshairi ameweza kumdhibiti zaidi msomaji kuanzia mwanzoni mwa shairi. Kwa mfano, katika ubeti wa kwanza mshairi ameanza ufaraguzi wa mawazo kwa matao ya chini lakini jambo hilo ni tofauti alipoingia katika ubeti wa tatu ambao ni hitimisho. Katika ubeti huo, mshairi amebainisha zaidi mwelekeo wake kuhusu matumizi ya mabavu kwamba:

Nguvu katu hazijui ila kwingi kuadhibu (Ubeti wa 3)

Kwa hivyo, matumizi ya methali yamemsaidia mtunzi kwa namna mbili: kubainisha au kuyanikisha mawazo na kudhihirisha msimamo au mwelekeo wake kuhusu utawala dhalimu wa kimabavu. Katika shairi, mawazo yamepangwa kwa utaratibu ambapo beti zote tatu zina umuhimu unaochangia uwasilishaji wa ujumbe. Hiyo ni mbinu ya ujenzi wa vitushi au mgogoro hadi kufikia upeo wa juu katika shairi. Endapo msomaji hatasoma beti hizo zote, basi huenda asiweze kuupata ujumbe kwa ukamilifu. Hapa ieleweke kuwa, mawazo yamewasilishwa kwa kuzingatia ishara elekezi ya methali ambayo yameufanya mawazo kuweza kukaririwa kiusambamba. Jambo hilo ni muhimu katika kujenga taharuki katika shairi.

4.2.4.4 Methali kama Msingi wa Kuudhibiti Muundo

Mshairi ameitumia methali ya: *Nguvu hazishiki yai zikishika hutumbuka* kuwa msingi wa kujengea muundo katika shairi. Kwa ambavyo methali ina mizani kumi na sita, imetumiwa katika ujenzi wa mshororo mmojawapo katika ubeti. Kwa hivyo, methali kama mshororo kamili, una ukwapi ambao una mizani nane na utao una mizani nane. Kadhalika, methali hiyo kama mshororo, una kina cha ndani [**i**] na cha nje [**ka**]. Kutokana na uelekezi huo, mishororo mingine katika shairi imefuata na imeelekezwa kwa utaratibu huo. Hata hivyo, hakutumia kikomo kwenye methali na hali hiyo imetawala katika mishororo yote inayopatikana katika shairi. Uwazi unaotenganisha sehemu ya kwanza na ya pili katika methali hukidhi haja hiyo.

Hapa ieleweke kuwa, mtuo katika methali na mishororo yote inayopatikana katika shairi huweza kubainika kwa kulisoma shairi kwa kuzingatia mdundo au ridhimu unayoibuliwa

kupitia kwa urari wa maneno teule yaliyotumika. Huo ni ukiushi wa kaida ambao ulizingatiwa katika muktadha wa utunzi wa mashairi ya Kiswahili ya kimapokeo. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kaida katika utunzi huweza kukiukwa kutokana na uelekezo wa hisi za mtunzi. Kwa hivyo, uhalisi huo unapotokea katika uwasilishaji wa utungo huweza kukaripiwa mwanzoni kisha baadaye ukakubaliwa pole pole (Nagler 1967). Katika muktadha huo, mshairi hataki kujifunga zaidi katika taratibu na arudhi zilizoshilikiwa sana na watunzi wa ushairi wa kimapokeo ambazo zilikuwa ni shuruti katika utunzi wa ushairi wa Kiswahili.

4.3 KIISHILIO

Sura hii imehakiki matumizi ya methali kama kipengele muhimu katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa kati wa Kiswahili. Katika muktadha wa mashairi yaliyozingatiwa, matumizi ya methali si angavu zaidi kama vile ilivyobainika katika ushairi wa kimapokeo. Kwa hivyo, methali zilipotumiwa katika ushairi huu huwa ni miongoni mwa kauli za msingi katika kuikemea na kuikashifu mienendo mibaya katika jamii. Kwa sababu, swala la kimaadili limeshughulikiwa kwa uwazi mno katika ushairi uliozingatia mno arudhi za kimapokeo. Hata hivyo, matumizi yake yamesetiriwa zaidi katika maudhui yanayowasilishwa. Pale ambapo methali haikutumika kwa uwazi, dhima yake huhisika kwa mwangwi kupitia kwa kauli zilizojenga maudhui katika utungo. Kwa ambavyo matumizi ya methali katika ushairi huu si ya wazi, huweza kudhihirisha uwezekano wa matokeo ya mabadiliko machache katika mbinu na mitindo ambayo huweza kutumika katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili.

Katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili hususa, katika miaka ya 1970 hapa Afrika ya Mashariki, kuliwahi kushuhudiwa mitazamo mbalimbali kuhusu mbinu zinazotumika katika utunzi na uwasilishaji wa utanzu huu. Kimsingi, tungo ambazo zilikuwa zikiwasilishwa kwa kuzingatia arudhi za kimapokeo zilikuwa tayari zimekubalika miongoni mwa wanajamii. Watunzi walipoanza kutunga na kuuwasilisha tungo kwa uzingativu wa kiasi wa mbinu hizo, washairi hao waliweza kukabiliwa na kupingwa kihisia na kimwelekeo. Kwa hivyo, matarajio ya watunzi wa ushairi wa kati ni kwamba, mabadiliko hayo yanayotokea hivi sasa kwenye utunzi na uwasilishaji katika ushairi wa Kiswahili huweza kuletwa polepole hadi pale ambapo ushairi wa kimapokeo na ushairi huru utakubaliwa kuwa sarafu moja kwa ya pili.

Utaratibu wa mabadiliko hayo, huweza kuyakinishwa pia kupitia kwa namna methali cheche zilivyotumiwa kwa uwazi katika muktadha wa ushairi uliozingatia arudhi za kimapokeo na ule ushairi huru. Mkondo huo wa matumizi machache ya methali huufanya ushairi wa kati usiweze kujibainisha bayana iwapo ni wa kitengo cha kimapokeo au huru. Hata hivyo, ushairi wa kati huwasilisha hisi na mawazo yaliyotokana na tajiriba iliyojikita katika utamaduni na uhalisi wa maisha ya jamii. li ya kutumiwa kwa methali chache katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi ni daraja ambayo huweza kuunganisha ushairi wa kimapokeo na ule ushairi huru.

SURA YA TANO

UCHANGANUZI WA USHAIRI HURU KWA LENGO LA KUTATHMINI MATUMIZI YA METHALI

5.0 UTANGULIZI

Sura hii imetathmini matumizi ya methali katika ushairi huru wa Kiswahili usiozingatia arudhi za kimapokeo. Katika kitengo hiki, kuna washairi wengi waliotunga na waliochapisha mashairi yao katika diwani mbalimbali. Baadhi ya watunzi hao mashuhuri ni kama Kulikoyela K. Kahigi, Mugyabuso M. Mulokozi, Ebraham Hussein, Euphrase Kezilahabi na Kithaka wa Mberia. Hata hivyo, ni watunzi wawili tu ndio wamezingatiwa katika sura hii kuwa kiwakilishi cha watunzi wengine mashuhuri wanaopatikana katika kundi hilo. Watunzi hao ni Euphrase Kezilahabi katika diwani ya *Kichomi* (1974) na Kithaka wa Mberia katika diwani ya *Bara Jingine* (2001). Watunzi hawa, kama inavyobainika katika watunzi wengine wasiozingatia arudhi za kimapokeo, wametumia methali chache mno na baadhi ya mashairi yao hayana kabisa ithibati ya matumizi hayo. Hata hivyo, tungo ambazo hazikutumia methali kwa uwazi zina uhusiano wa moja kwa moja na methali zinazopatikana katika jamii.

Mashairi ya watunzi hawa wawili yamechanganuliwa ili kubainisha dhima ya matumizi ya methali kwa kulinganisha na matumizi ya kauli zingine muhimu zinazoibuliwa na kutumiwa kwa makusudi na watunzi hao. Aidha, sura hiyo imechangaua utendakazi wa kauli hizo zilizotumiwa kwa makusudi kuwa msingi wa kuibulia mwangwi wa methali katika utunzi na uwasilishaji wa mashairi hayo. Katika ushairi uliozingatia arudhi za kimapokeo, methali zilizotumika humfanya mtunzi kuwasilishia mawazo kiisitiari, kitaswira na pia kuwa msingi wa kuibulia baadhi ya tamathali za usemi (Taz. Sura ya

Tatu na Nne). Kadhalika, sura hii imefafanua nafasi ya uhuru wa kishairi kama kigezo cha kutotumia methali kwa uwazi katika uwasilishaji wa tungo hizo. Kulingana na nadharia ya Semiotiki, maana au ujumbe huweza kuwasilishwa kupitia kwa kauli au miundo tofauti ya lugha. Katika muktadha wa utunzi na uwasilishaji wa mashairi yanayozingatia arudhi za kimapokeo, swala la kimaadili limepewa kipaumbele hasa ikilinganishwa na hali ilivyo katika mashairi yasiyozingatia arudhi. Maudhui ya kimaadili katika mashairi hayo huibushwa na kusisitizwa zaidi kutokana na bayana ya methali zilizoshirikishwa katika uwasilishaji wa tungo hizo (Mazungumzo na Nabhany tarehe 26.02.2011). Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, swala la kimaadili huweza kuwasilishwa kupitia kwa kauli za kimapokeo kama vile methali (Swingwood 1998). Kwa hivyo, jambo linalochochea uchanganuzi huu ni kwamba, iwapo swala la kimaadili halishughulikiwi mno kwa kalamu ya watunzi hawa, basi nafasi yake imechukuliwa na maswala gani ya kijamii?

Kimsingi, kauli mbalimbali zilizotumiwa na wasanii wa mrengo wa mashairi hayo, zina mwelekeo wa kibinafsi badala ya kijamii. Hata hivyo hoja kwamba, matumizi ya methali bado yapo ingawa si ya uwazi kama vile yalivyoshamiri katika ushairi wa kimapokeo. Kwa hivyo, dhima ya methali imetathminiwa ili kubainisha mchango na nafasi yake katika mkabala wa mabadiliko ya kiutunzi na uwasilishaji wa ushairi usiozingatia arudhi za kimapokeo.

5.1 UCHANGANUZI WA USHAIRI WA EUPHRASE KEZILAHABI: *KICHOMI*

Diwani ya *Kichomi* ilitungwa na kuchapishwa mwaka wa 1974 na Shirika la Heinemann Educational Books (E.A.) Ltd. Diwani hii ina jumla ya mashairi arobaini na mbili. Ingawa mashairi haya ni mengi, ni manne tu ndiyo yamezingatiwa katika sura hii. Mashairi hayo teule ni:

i. *Mafahali wapigana*
ii. *Nimechoka*
iii. *Kuchambua mchele*
iv. *Hadithi ya Mzee*

5.1.1 Shairi: Mafahali Wapigana

Katika shairi hili, mshairi amesawiri kinyang'anyiro cha kisiasa katika mataifa huru ya Afrika Mashariki hususa, Tanzania. Mataifa hayo tayari yamepata uhuru kutoka kwa utawala wa kikoloni mwanzoni mwa miaka ya 1960. Baada ya kujinyakulia uhuru, kipindi hiki kimeshuhudia viongozi mbalimbali ambao wana mielekeo na mirengo ya itikadi tofauti tofauti za kisiasa. Kila aliyewania wadhifa wa utawala hujiona simba au *fahali*. Baadhi ya viongozi huwa ni wa tabaka ambalo limemiliki nyenzo za uzalishaji mali na limejilimbikizia mali na mara kwa mara hutaka kudhihirisha uwezo wao hadharani. Kiongozi mtarajiwa aliposhinda kinyang'anyiro hicho, hujikita katika kuendeleza itikadi yake. Kwa watawaliwa huwa hawana ufahamu wa msingi kuhusu makabiliano hayo miongoni mwa 'viongozi'. Kwa ambavyo wamekuwa katika hali hiyo ya ukata au uhitaji, huchukulia kuwa hali yao imekuwa na yiyo hiyo: aliyeshinda na aliyeshindwa kwao ni mamoja.

Kulingana na mshairi, watawala hao husukumwa kwa mahitaji yao ya kibinafsi badala ya kuyapa kipaumbele masilahi ya umma. Kwa hivyo, watawala hao wamekuwa ni vizingiti wa mwafaka wa maendeleo katika baadhi ya mataifa hayo hata ingawa mkoloni tayari ameishagura. Katika kuusawiri na kuuwasilisha ujumbe wake, mshairi ametumia kauli mbalimbali kuwa msingi wa kutekelezea mradi wake.

5.1.1.1 Kauli Teule za Msanii kama Msingi wa Kuundia Taswira na Uwasilishaji Ujumbe

Katika shairi hili, mshairi ametumia kauli ambazo ni teule kuwa msingi wa kuibulia mbinu ya taswira katika usawiri na uwasilishaji wa ujumbe. Kwa kuzingatia uelekezaji wa anwani ya *mafahali wapigana*, mshairi ameweza kubainisha kwa ujumla ujumbe unaotarajiwa kuwasilishwa. Kadhalika, mshairi alipotumia anwani hiyo huwa amejijengea muktadha baadhi ya kauli nyinginezo za msingi zinazofafanua zaidi taswira ya mafahali hao wanaopigana.

Kutokana na kauli alizozitumia, mshairi huweza kujenga kwa ufundi picha ya kimawazo katika akili ya hadhira. Kwa mfano, picha ya kimaono ambayo hadhira huitunga ni ya *mafahali wanono* wanaopigana. Kwa hivyo, moja kwa moja hadhira hutunga taswira ya mifugo wawili waliopambania himaya ya uongozi. Kimsingi, mafahali hao si wa kawaida, kwa sababu si wahitaji wa lishe lakini wamo wanapigana. Vita vilivyosawiriwa ni vya hatari kubwa ambapo vinashangiliwa na *watazamaji wakondefu*. Kwa hivyo, hayo ni makundi mawili yaliyosawiriwa na kubainishwa kiusanii. Kwa upande wa mtunzi haoni sababu ya halaiki kufurahia kitendo hicho ili hali kimsingi wao ndio wahitaji.

Katika muktadha wa kauli zilizotumika, mshairi huielekeza hadhira yake kutunga taswira ya kuikejeli furaha ambayo zimedhihirika katika nyuso za watazamaji. Katika kuikoleza zaidi picha ya kimaono inayowasilishwa, amekariri kuwa halaiki *pole pole hawaoni kitu.* Zaidi ya hayo, fahali aliyeshindwa huamua kukimbilia usalama ili asije akajeruhiwa. Naye fahali mshindi amewasilishwa kama aliyefurahia zaidi ushindi au matokeo ya ushindi wake huku *akionyesha kidole kimoja* na wakati uo huo amejipweteka kwenye *kichuguu.* Isitoshe *mchwa ndo askari* wanashika doria ili kuihami himaya hiyo. Katika hali hiyo, fahali mshindi hustaajabia na hushangilia ushindi wake kwa kusema kuwa: *kilikuwa kivumbi hicho.* Hizo ni kauli ambazo zina uhusiano wa karibu na methali zinazojulikana katika jamii. Ingawa mshairi hakutumia methali yoyote kwa uwazi, ujumbe ulioibushwa huweza kuwasilishwa kupitia kwa methali kama vile: Mwenye nguvu mpishe; mafahali wanapopigana ni nyasi zinazoumia au mafali wawili hawakai zizi moja. Methali hizo hujulikana katika mawasiliano ya watu. Hata hivyo, mshairi ameiachia hadhira iupatanishe ujumbe unaoibuliwa na methali yoyote inayopatikana katika utamaduni wao. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki ni kwamba, ujumbe huweza kuwasilishwa kupitia kwa ishara zaidi ya moja (Pierce 1977 na Scholes 1974).

Baada ya vita hivyo kumalizika, sehemu hiyo inakuwa *tulivu.* Kutokana na maelezo ya mshairi ni kwamba, halaiki inamsifu na inampagaza sifa mbalimbali fahali mshindi. Kwa ambavyo fahali huyo ndiye anayeibuka mshindi, halaiki ndio inayempenda na inayemsherehekea. Hata hivyo, mshairi haoni hali hiyo kuwa shwari. kwa sababu, ametoa usiyahi wake ambao umekatisha tamaa kuhusu hali ilivyo katika jamii hiyo. Miongoni mwa halaiki hiyo iliyosawiriwa kuna wale ambao hawakuridhishwa kwa hali

hiyo. Kwa hivyo, hubidi wanyamazishwe. Katika hotuba ya mwanzo, fahali mshindi ametangaza kuwa jamii inapaswa kushirikiana ili *tujenge kichuguu na kuulainisha udongo.*

Kulingana na mshairi, huo si utulivu uliotarajiwa. Kwa hivyo, amesema *patulivu kweli!* na amekamilisha shairi hili kwa *Lakini!*. Taswira iliyoibuliwa katika shairi huweza kumfanya msomaji kuupokea ujumbe kimaono kutokana na kauli teule zilizoshirikishwa kwa makusudi. Kwa kufanya hivyo, huweza kuuathiri upokezi wa ujumbe kwa kuibua vionjo mbalimbali katika hadhira. Vionjo hivyo, vimepewa umbo kamili akilini (Senkoro 1988:117). Aidha, hadhira huwasilishiwa ujumbe na pia ameweza kuwaona mafahali walioshiba wakiwa vitani. Katika muktadha huo mshairi huweza kuibua hisi za huruma au hasira kwa hadhira. Kwa hivyo, mtunzi huteua matini ambazo huwiana na athari ambayo huitaka kuibua katika hadhira (Kahigi na Mulokozi 1979 na Nowottny 1968). Isitoshe, hadhira huwekwa katika nafasi nzuri ya kutathmini kiwango cha vita hivyo vinapoanza, vinapoendelea na vinapofikia ukingoni, hasa kwa kuzingatia uelekezo wa kauli mahususi zilizotumiwa. Kwa ustadi, mshairi ameweza kujenga taswira ya mawazo siyo tu kwa uzingatifu wa kifungu au sehemu moja ya kauli hizo bali kwa kuzingatia utendakazi na uwiano wake katika shairi zima.

5.1.1.2 Matumizi ya Viakifishi kama Mbinu ya Kujengea Usimulizi na Udhibiti wa Muundo

Mshairi ametumia mbinu ya usimulizi kwa uelekezi wa viakifishi ili kujengea muundo, ridhimu na mahadhi wakati wa kuwasilisha ujumbe. Kwa kutumia usimulizi, mshairi

ameweza kuufanya utungo usifungike katika idadi maalumu ya mizani, mistari na hata vina. Hata hivyo, shairi la namna hiyo huweza kughaniwa, kukaririwa kimoyomoyo au kusomwa kwa sauti (Wanyoike 1976 na Topan 1974).

Katika muktadha wa shairi la *Mafahali wapigana*, mshairi amejulisha kabla kuhusu ujumbe unaowasilishwa kwa kutumia kauli mbalimbali za nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu. Kwa kutumia nafsi ya kwanza, amejipa nafasi maalumu ya kuubinafsisha ujumbe na kuelezea tukio analolishuhudia kulingana na hisi zinazowasilishwa. Kauli ya mwanzo iliyozingatiwa yaani *Mafahali wanapigana,* imekuwa ya msingi zaidi na yenye kubainisha ni nani anayesimulia kadhia hiyo. Kadhalika, usimulizi kama mbinu ya uwasilishaji ni bayana katika kifungu au ubeti wa mwanzo na wa pili. Kwa kutumia mbinu hiyo, imemfanya mshairi kupanga na kuuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa mantiki iliyotarajiwa. Kimsingi, hiyo ni mbinu ambayo imemsaidia siyo tu katika kupanga na kufaragua mawazo, bali pia kulipa shairi muundo mahususi ambao umezingatia ridhimu na mahadhi maalumu. Matumizi hayo yamebainishwa na yamepata mwelekeo kupitia kwa uelekezo wa viakifishi. Kwa sababu, usimulizi katika wa ushairi huibua mdundo na mwendo unaotokana na viakifishi mbalimbali vilivyotumika (Gromov 2006:109). Mshairi ametumia viakifishi mbalimbali kama vile kituo [.], kikomo [,], nyota [*], kishangao [!], alama za kufungua na kufunga usemi [“ ”] na pia herufi kubwa. Hapa ifahamike kuwa, mshairi anapotumia viakifishi hivyo huutaka usomaji na upokezi wa ujumbe ubainike zaidi kwa kuzingatia uelekezi wa ishara hizo. Kwa hivyo, hadhira huweza kulisoma shairi kwa mwendo ulioafiki matarajio ya mshairi. Kwa mfano,

kuongeza au kupunguza kasi ya usomaji na pia kuipa hadhira wasaa wa kutafakari ujumbe uliyoibuliwa kwa uelekezi wa dhana au kauli zilizotumika katika shairi.

Isitoshe, mahadhi na ujumi umedumishwa kwa uelekezo huo wa viakifishi. Hayo ni mambo ya msingi ambayo huongoza katika uwasilishaji na upokezi wa ujumbe katika shairi. Kwa ambavyo shairi limewasilishwa kwa Kiswahili sanifu na kwa hadhira isiyoonekana, kama ilivyo katika uwasilishaji wa ushairi simulizi, imembidi mwasilishaji kutumia mbinu au kunga msingi za kisarufi ili kuifikia hadhira pana. Katika ufunguzi wa ujumbe, mshairi ameukaulisha usemi wa *mafahali wenye matumbo wanapigana* na pia kutumia kituo [.] mwishoni. Matumizi ya kituo humaanisha kuwa kauli hiyo imekamilika na humwezesha msomaji kujipumzisha na kutafakari kabla ya kukabiliana na kauli nyinginezo baadaye katika shairi. Katika kufaragua mawazo hayo, mshairi ameukariri na amekoleza zaidi ujumbe kwa mfululizo wa maneno yafuatayo:

> *Chini, chini, chini zaidi*
> *Mpaka vichwa vyao vinagusana* (Ubeti wa 1)

Katika dondoo hilo, mshairi ametumia herufi kubwa mwanzoni mwa kauli au mistari hiyo. Ingawa mshairi habainishi wazi kuwa anazungumzia dhana mbili zinazochangiana. herufi kubwa katika neno *chini* na *mpaka* hukidhi haja hiyo. Kadhalika, mahadhi na ridhimu yamekidhiwa zaidi kwa ukariri wa hoja zilizotumia vikomo [,] baina ya maneno yaliyotumika *katika chini, chini, chini zaidi.* Kwa ambavyo mshairi hakutumia kituo [.] humwelekeza msomaji kutosita bali afululize katika usomaji wake hadi atakapofikia kituo. Kadhalika, ametumia kiakifishi cha mshangao [!] katika kauli zifuatazo:

> *Haya! Haya! Machakulo* haya!* (Ubeti wa 1)

Isitoshe, matumizi ya kinyota [*] humwelekeza msomaji kutambua kuwa neno hilo *Machakulo* limetoholewa au ni neno ambalo huweza kueleweka kwa kuzingatia utamaduni wa jamii maalumu. Kwa hivyo hilo si neno la Kiswahili. Kwa uelekezi zaidi, mshairi huitaka hadhira izingatie maelezo au ufafanuzi uliotolewa mwishoni mwa utungo. Kwa mfano, huyo ni fahali mwenye siha na nguvu katika jamii ya mshairi. Katika muktadha wa dondoo hilo, maneno hayo yamekaririwa ili yawakilishe furaha waliyonayo watazamaji. Huo ni mfano wa kauli halisi za watazamaji au wahusika wanaoshuhudia kitendo cha makabiliano baina ya mafahali wawili.

Aidha, matumizi ya vishangao vimerutubisha zaidi mahadhi na ridhimu katika shairi. Kwa sababu, hadhira tayari imedhibitiwa ili kusoma kauli hizo kwa mwendo na athari ilivyotarajiwa. Kwa hivyo, mshairi amebainisha kwa uangavu namna mafahali wanavyopigana na hasa kupitia kwa viakifishi. Mwendo huo umeendelea hadi mwishoni mwa ubeti wa kwanza. Katika ubeti wa pili, amewasilisha hoja mpya kwa mshindo unaostahili. Kwamba, vita au sinema hiyo tayari imehitimishwa. Kwa hivyo, ameanza tena kwa herufi kubwa kuwa:

Kilikuwa kivumbi hicho. (Ubeti wa 2)

Kimsingi, hoja hiyo imewasilishwa kwa ukamilifu wake. Hiyo ni kauli ambayo hudhihirisha maelezo ya mtunzi na vile vile kuibua usiyahi wa halaiki ambayo imekuwa ikishuhudia mapambano hayo. Hata hivyo, usomaji wa ubeti wa pili umedhibitiwa na umeelekezwa kwa viakifishi vilivyotumika. Ridhimu na mahadhi katika aya ya pili imefikia kilele katika mstari wa mwisho. Kauli ambayo imetumika kukidhi haja hiyo ni:

Patulivu! Patulivu! Patulivu kweli! (Ubeti wa 4)

Kwa kuzingatia dondoo hilo imebainisha kuwa, hiyo ni sauti au kauli halisi ya msanii. Kwamba, hajaridhishwa kwa *utulivu* huo. Kadhalika, msomaji anaposoma kauli hiyo hutarajiwa kupandisha, kushusha sauti na pia mazingira ya mwendo usiwe wa kasi. Katika mazingira hayo hiyo, mshairi huitaka hadhira iisome kauli iliyokusudiwa kwa usaili na utafakari wa tukio linalowasilishwa.

Katika ubeti wa tatu, mshairi amemdhibiti zaidi msomaji wake katika kuanza kusoma kauli tangulizi kwa mshindo zaidi kama vile mtu mwenye mamlaka anavyohutubia halaiki ya watu. Kwa kutumia alama za kufungua na kufunga usemi au unukuzi [“ ”] amemwelekeza zaidi msomaji kufahamu kuwa, hiyo ni kauli ambayo imetolewa na mhusika mwingine ambapo si ya mshairi mwenyewe. Kwa hivyo, msomaji huweza kugeuza usomaji wake ili iwe sauti ya mhusika mwingine katika shairi. Kwa kumwelekeza zaidi msomaji, mshairi ametumia neno *anasema* mwishoni mwa unukuzi wa kauli halisi kama ifuatavyo:

“Basi kama mchwa
Tujenge kichuguu
Kama mchwa tuungane
Na kuulainisha udongo, anasema. (Ubeti wa 3)

Katika muktadha wa dondoo hilo, uwasilishaji wa kauli zilizotumiwa zimepewa uzito zaidi kutokana na alama hiyo ya kufungua na kufunga usemi [“ ”]. Kwa kudhihirisha sauti ya shime zaidi, msanii ametumia alama za kishangao [!] katika ubeti wa tamati. Kwa mfano, amedhihirisha usiyahi wa mshangao kwa kusema kuwa:

Patulivu! Patulivu! Patulivu!
Lakini! Lakini! Lakini! (Ubeti wa 4)

Mshairi katika dondoo hilo, ametumia maneno mawili kwa ukariri yaani *Patulivu* na *Lakini*. Kila moja ya maneno hayo yamerudiwa mara tatu. Katika mshororo wa kwanza, mshairi ameweza kuiga namna watazamaji wa vita vya mafali wanavyokuwa wakisema baada ya vita hivyo kwisha. Kwa sababu hiyo, mshairi ametilia shaka kauli za watazamaji au jamii kwa uelekezi wa neno *Lakini!*. Hapa ieleweke kuwa, maneno hayo hayakurudiwa tu kama mbinu ya ukariri bali pia kudhibiti na kujenga mahadhi na ridhimu inayohitajika katika shairi. Kinyume na muundo wa ushairi wa kimapokeo unaoibua mahadhi na ridhimu kwa kutumia vina na urari wa mizani, shairi hili limetumia kauli za kibinafsi na viakifishi katika kujengea mfumo mahususi wa mahadhi na muundo katika uwasilishaji wake (Masinde 2007:35). Katika muktadha huo, imebainishwa kuwa shairi la Kiswahili huweza kuwasilishwa kimahadhi na kiridhimu kwa uelekezi wa kauli za makusudi au kwa viakifishi vinavyotumiwa.

5.1.1.3 Matumizi ya Kauli Zinazofahamika kama Msingi wa Uwasilishaji

Kwa ambavyo mshairi huifahamu hadhira yake, ameamua kwa makusudi kutumia kauli za kawaida zinazofahamika katika jamii ili kujenga msingi wa kuwasiliana na hadhira yake. Kwa mfano, hadhira pokezi huweza kuwa finyu au pana. Hiyo ni hadhira ambayo mtunzi hawezi kuibainisha wazi. Kwa hivyo, ametumia kauli ambazo huweza kufahamika na kufasiriwa kwa kuzingatia uzoefu wa utamaduni na uhalisi wa maisha. Matumizi hayo hayamaanishi kuwa mshairi ametindikiwa kuuwasilisha ujumbe wake kwa ufasaha na kwa namna inayogusa au inavyoathiri hisi za wapokezi. Kwa mfano, mshairi ameamua kutumia kauli ya '*mafahali wanapigana*' ili kujenga taswira ambayo si ya dhahania bali iliyotokana na uhalisi wa shughuli wanazozifanya wanajamii. Katika

jamii ambazo hupatikana Tanzania au katika mataifa jirani ya Afrika Mashariki hufahamu vituko vya mifugo hususa mafahali (Mazungumzo na Masinde tarehe 18.11.2011). Hiyo ndiyo sababu ya mshairi kutumia kwa makusudi dhana ya *machakulo*. Kwa ambavyo mshairi amelenga ufinyu na upana wa hadhira, maelezo ya dhana ya *machakulo* yamewekewa kinyota [*] kama ilivyoelezwa hapo mwanzoni.

Katika muktadha wa uwasilishaji wa tanzu mbalimbali za fasihi simulizi, usawiri wa matukio hujikita katika mazingira, utamaduni na uhalisi wa maisha ya jamii (Indede 2008 na Njogu na Chimerah 1999). Kwa sababu hiyo, mshairi hataki hadhira yake ipate tatizo la kufasiri ujumbe au kutofuatilizia kadhia inayowasilishwa. Kwa hivyo, mshairi ameteua na ametumia miundo ya lugha ambayo hupatikana kwa urahisi katika mawasiliano ya jamii. Matumizi hayo yameweza kulipa shairi sura ya ukawaida katika uwasilishaji huku akidhihirisha ukweli au uhalisi fulani wa maisha yenye uasili wa Kiafrika (Kezilahabi 1977). Kwa kuzingatia uwasilishaji wa shairi hili, mshairi ametumia kauli za kawaida ambazo zimedhihirisha kuwa kitendo bado kinaendelea. Katika mantiki hiyo, mshairi ametumia kauli hizo sahili ambapo huitaka hadhira ichukulie kadhia iliyowasilishwa kuwa ni msingi wa kujengea chemichemi ya utafakari na ubainishaji wa ujumbe fiche. Kulingana na nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli teule zinazotumika katika uwasilishaji wa utanzu kama vile nyimbo au ushairi ni zile ambazo hueleweka katika mapokeo ya jamii (Fowler 1966). Kadhalika, katika muktadha wa kisemiotiki, kauli hizo zilizotumika katika uwasilishaji huweza kufasirika na kufafanuliwa kwa kuzingatia vipengele vya utamaduni na mazingira ya jamii mahususi (Imbosa 1990 na Hawkes 1977).

Vile vile, kutokana na upangaji wa maneno teule, shairi limepata muundo maalumu ambao hauwezi kupanguliwa. Katika uwasilishaji wa ushairi unaozingatia arudhi za kimapokeo, ni matumizi ya msamiati mgumu au wa zamani ambao huufanya utungo kuwa mgumu kufasirika ila kwa kikundi kidogo ambacho kina 'kipawa' au ujuzi mkubwa wa ufasiri (Mazungumzo yangu na Nabhany tarehe 26.2.2011). Katika utunzi na uwasilishaji wa shairi hili, isichukuliwe kuwa matumizi ya lugha ya kawaida ni ya kuufanya utungo huo kuwa chapwa. Kwa sababu kauli zilizotumika ni zile zile ambazo hupatikana katika mawasiliano ya jamii ambapo huufanya utungo kuwa wenye mahadhi na kivutio kwa hadhira.

Kimsingi, msanii angependa kuifikia hadhira pana: wasomaji ambao ni wazoefu au wataalamu wa fasihi na wale ambao hawana ujuzi mkubwa wa kiuchambuzi. Hata hivyo, ili kuupata ujumbe fiche ambao umewasilishwa huhitaji kujikuna kichwa. Katika muktadha huo, upokezi wa shairi hili umeshirikisha aina mbalimbali za hadhira ilihali ushairi unaozingatia arudhi za kimapokeo lina mwelekeo wa kuwachuja zaidi wasomaji.

5.1.1.4 Ujenzi wa Sitiari kama Msingi wa Kuitafakarisha Hadhira

Kutokana na matumizi ya kauli teule, mshairi ameweza kujenga sitiari kuwa mbinu mahususi ya utunzi na ya kuwasilishia mawazo. Kadhalika, sitiari iliyoibuliwa haikujifunga tu kwenye kauli zilizotumiwa bali pia kauli hizo hujengana na hutegemeana katika uwasilishaji wa shairi (Leech 1969). Kwa mfano, mtunzi ameeleza kuwa wanaopigana ni *mafahali wenye matumbo*. Hiyo ni kauli ya msingi inayochangia ile ya anwani ambapo kwa pamoja zimejenga taswira ya wanaohusika katika mapambano hayo

makali. Katika muktadha huo, kauli hizo huweza kufasirika kiisitiari kwa uelekezi wa taswira zilizoundwa. Kwa ambavyo mafahali hao ni *wanono* kutokana na shibe, hawana shida wanapolinganishwa na *watazamaji wakondefu* wanaoshangilia. Kimsingi, mshairi ameikejeli hali ya watazamaji ambao hawaufahamu dhiki zilizoko katika uhalisi wa maisha yao.

Kejeli inayoibuliwa humfanya mshairi kuichochea hadhira ili kuweza kujenga isitiari ambayo huweza kufasiriwa kwa upatanisho wa muktadha halisi wa maisha ya jamii. Kwa hivyo, hawa *mafahali* huweza kueleweka na kufasiriwa vizuri katika muktadha wa kinyang'anyiro cha kisiasa kinachotokea katika baadhi ya mataifa ya Afrika Mashariki na barani Afrika hasa baada uhuru kupatikana. Kwa hivyo, mtunzi huitaka hadhira ibaini kuwa *mafahali* wanohusika katika kinyang'anyiro cha kisiasa ni viongozi watarajiwa ambao wana mielekeo ya itikadi zinazohitilafiana. Hali hiyo pia imejitokeza katika baadhi ya mashairi ya Kiswahili kama vile 'Bara Jingine' (Mberia 2001:10-16 na 'Mnazi:Vuta N'kuvute' (Abdala 1973:17-22). Kutokana na itikadi tofauti za wanaohusika ndio umekuwa msingi wa kichocheo cha ugomvi wao. Kwa hivyo, mtunzi wa 'Mafahali Wapigana' ameuwasilisha ujumbe wake kitaswira au kimaono kwa kuzingatia uelekezo wa dhana au kauli ambazo ni za kiisitiari. Kwa ambavyo mshairi amewawasilisha watazamaji kuwa ni *wakondefu*, anachokitaka ni hadhira ielewe kuwa, umma haufaidi chochote kutokana na vita hivyo wasivyojua chanzo wala hatima yake.

Aidha, umma umekuwa katika lindi la dhiki ya muda mrefu na huzidi kuendelea kuwa katika hali hiyo. Katika muktadha huo, mshairi ameweza kusawiri makundi mawili ya

kitabaka ambapo: tabaka la juu linazozana ili kuwania utawala na udhibiti wa kiuchumi. Kwa *fahali* aliyeshinda hupata fursa ya kujenga himaya huku akihakikisha kuwa sauti yake husikika; kama asemavyo mshairi kuwa: *mshindi juu ya kichuguu amekaa* (Ubeti wa 1).

Katika muktadha wa shairi, dhana ya *kichuguu* huweza kufasirika na kueleweka kuwa ni himaya ambapo *fahali* mshindi ameshika hatamu za uongozi. Mshairi amemsawiri *fahali* huyu ambaye ni kiongozi, ambapo amekaa juu ya *kichuguu* huku *akionyesha kidole kimoja sasa*. Kabla ya hapo, *fahali* huyo alikuwa hana msukumo wa kutoa usemi lakini sasa ana uwezo wa kuushinikiza umma kumsikiliza. Katika kipindi hicho cha utawala, mtawala huyo ana *askari* ambao hushika doria ili kuhakikisha kuwa usalama wake umedumishwa. Aidha, kuwepo kwa *askari* hudhihirisha kuwa, mtawala hana uhakika wa usalama wake. Kwa hivyo, askari au wahudumu hao wana jukumu la kuhakikisha kuwa hakuna anayeukashifu utawala huo wakati wa *kuulainisha udongo*. Kutkana na kauli za kiisitiari zilizotumika, hadhira huweza kubaini mfumo wa utawala unaowasilishwa kuwa ni utawala wa kimabavu. Kwa hivyo, wale ambao huonyesha dalili za kuushuku utawala huo, hunyamazishwa kwa kiboko na rungu la askari.

Hata hivyo, mshairi haoni manufaaa yoyote ambayo huweza kutokana na kinyang'anyiro hicho cha kisiasa. Hiyo ndiyo sababu ya kusema kuwa:

> *Patulivu! Patulivu! Patulivu!*
> *Lakini! Lakini! Lakini!* (Ubeti wa 4)

Kulingana na nadharia ya Fomula ya kisimulizi, kauli teule zinazotumika ni kunga za kufaragulia zaidi ujumbe unaowasilishwa (Lord 1960). Vile vile, katika muktadha wa nadharia ya Semiotiki kauli hizo za kiisitiari huweza kufasirika kwa kuzingatia tajiriba ya jamii. Hata hivyo, mshairi ametilia shaka kuhusu utawala ambao umejengwa na fahali mshindi. Isitoshe, mshairi angependa ujumbe unaowasilishwa ufasiriwe kwa kuzingatia dhana au kauli za kiisitiari ambazo zimetamalaki katika shairi, kuanzia mwanzo hadi tamati.

5.1.1.5 Uibushaji wa Usaili Kutokana na Uelekezi wa Kauli Teule za Mshairi

Mshairi ametumia kauli za kawaida ambazo hazisababishi utata wowote katika utunzi na uwasilishaji wa shairi hili. Kauli zilizotumiwa ni sahili lakini kutokana na namna alivyozitumia, zimejenga kichocheo cha usaili wa ujumbe fiche uliowasilishwa. Zaidi ya usaili, kauli hizo zimesaidia katika ujenzi wa taswira ambayo huitafakarisha akili ya hadhira. Kwa kuzingatia kauli teule zilizotumika, usomaji wa hadhira hudhibitiwa kwa uelekezo wa maswali ya kutafakarisha kama vile:

- *Mafali wenye matumbo* wanapigania nini?
- Kwa nini watazamaji au halaiki inayoshangilia mapigano hayo, ni *wakondefu*?
- Kwa nini umma *umenyamaza* tuli?
- Kwa nini katika *kichuguu* si patulivu?

Kimsingi, mshairi ametumia kwa makusudi kauli za kawaida ili hadhira isipate ugumu katika usomaji wa shairi. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli ambazo hushirikishwa katika utunzi na uwasilishaji wa utungo ni zile ambazo hueleweka katika mawasiliano ya watu (Fowler 1966). Kadhalika, kwa kutumia kauli hizo za

kawaida, mshairi ameijengea hadhira muktadha mwafaka wa kutafakari na wa kufumbulia fumbo lililofumbwa. Hata hivyo, matumizi ya lugha ya kawaida huweza kuchukuliwa kuwa ni msingi wa kuitenganisha na vile vile kuishirikisha hadhira pana ya jamii. Hadhira hiyo, ni ile ya usomaji wa kijuujuu na ile ya dhati inayohitaji kujijuvya zaidi kiini cha ujumbe unaowasilishwa. Kwa wasomaji wa kijuujuu hufurahia uhondo wa lugha iliyo wazi na ile ya dhati huwa inajikuna kichwa.

Katika muktadha huo, mtunzi ameikusudia hadhira ya dhati ambayo huweza kuufasiri ujumbe uliofumbwa kwa uelekezi wa ishara dhahiri. Kwa kutumia vielekezi vya *mafahali wenye matumbo wanapigana*, msomaji hutambua kuwa wanaorejelewa ni wanasiasa ambao hapo awali wamejichumia kwa ulaghai; bado wana uchu wa kutaka kujilimbikizia kwa kuihodhi au kuifilisi mali ya jamii. Ubinafsi wa wanasiasa umebainishwa pia kupitia shairi la "Nchi Iwapo Kukutu" (Mohamed 1980:18-19). Katika shairi hilo, imekaririwa kuwa:

> *Vikaukapo visima, nafsi hujaa matu*
> *Mashimo ya toka zama, ndani yalalayo chatu*
> *Huchimbwa kwa nyingi hima, jembe mtu shepe mtu*
> *Nchi iwapo kukutu, hukimbiliwa mlimbi*

Katika ubeti huo, mshairi ametumia dhana ya *chatu* ili kuilekeza zaidi hadhira yake katika kuelewa ujumbe unaowasilishwa. Kwa kuwafananisha wanasiasa na *chatu* hadhira hupata fununu kuwahusu. Kwa hivyo, wanasiasa hao kama vile *mafahali* hupenda kuendelea kupigania nyadhifa za uongozi ili waweze kuimarisha nyenzo za kujinufaisha wenyewe. Kikundi hichoki cha jamii huwa kina ubinafsi na hakijali lolote litakalowapata wanajamii walio wengi, bora uchu wao wa mali hukidhiwa.

Kadhalika, katika mapambano ya kisiasa ni yule aliyeibuka mshindi ndiye anayefaidi na wala haelekezwi kwa hisi za utu wala huruma. Aidha, watazamaji ambao ni *wakondefu* huwakilisha kundi la watawaliwa ambao hawaelewi vitimbi vya wale wanaopigania kushika hatamuzi uongozi katika jamii. Kutokana na maelelezo yaliyotolewa, kundi hilo hufurahia kushuhudia sinema kwa wakati huo ingawa halijui kuwa watakuja kujuta siku za usoni.

Ni katika kutafakari zaidi viashiria vilivyotumiwa kupitia kwa kauli zinazotumika, ndipo hadhira huweza kuelewa kuwa kikundi cha watazamaji hakina upeo mkubwa kuhusu maswala ya siasa za nchi na maisha kwa ujumla. Kimsingi, mshairi hufumba uwasilishaji wake kupitia kwa kauli teule zilizoteuliwa kwa makusudi na hadhira hushiriki katika kufumbua fumbo (Gibbe 1990). Kama ilivyokwisha kuelezwa hapo awali, mshairi hana nia ya kubainisha wazi ujumbe wake. Kwa mfano, ametumia dhana mbalimbali za kutafakarisha na kusaili kama vile katika matumizi ya *mafahali*, *wakondefu*, *mchwa*, na *kichuguu*. Ingawa maneno hayo ni ya kawaida katika mawasiliano ya jamii yanahitaji kusailiwa na kutolewa ufafanuzi wa kina na hadhira.
Hata hivyo, ieleweke kuwa kauli zilizotumiwa kutoka mwanzo hadi mwisho, limelifanya shairi kuwa fumbo ambalo huhitaji kufasiriwa na kufumbuliwa ili ujumbe batini uweze kubainishwa. Aidha, kauli zilizotumika huhitaji kuzingatiwa na kufasiriwa kama ishara elekezi kwa kuzingatia muktadha wa shairi na uhalisi wa jamii kwa ujumla. Kwa mfano, dhana ya *kichuguu* huweza kufasiriwa kuwa nchi au taifa ambalo lina watawala na watawaliwa. Kadhalika, *mafahali* hao ni viongozi ambao hupigania uongozi katika mataifa ambayo tayari yamepata uhuru. Kwa *fahali* au kiongozi ambaye ameshinda

ndiye ameulazimisha mfumo wa uongozi kwa itikadi iliyomwongoza. Kulingana na mshairi ni kwamba, watawaliwa ni *wakondefu* na baada ya vita kumalizika wamenyamaza au wamenyamazishwa kupitia kwa virungu vya *askari*. Huenda wanajamii wamefanya hivyo kwa ukosefu wa uhuru wa kutoa maoni au kwa hofu ili wasije kutuhumiwa kuwa *wasaliti*.

Katika uwasilishaji wa utungo, mshairi ametumia dhana au kauli ambazo zinaelekezwa kwa viakifishi vya kishangao kama vile katika *patulivu kweli! Na lakini*!. Hapa ieleweke kuwa, kiakifishi cha mshangao [!] kimetumiwa kwa makusudi ili kumfanya msomaji kusaili zaidi ujumbe ambao umeibuliwa na umewasilishwa. Katika muktadha huo, msomaji hupata uelekezi wa kufahamu kuwa himaya hiyo inayosawiriwa ina amani ya kulazimishwa. Kwa kuzingatia uelekezi wa kauli teule zilizotumika, hadhira huhitaji kunoa zaidi usaili na utafakari ili kutambua ujumbe uliofumbwa kwenye shairi linalowasilishwa la sivyo huweza kutindikiwa kuung'amua ujumbe uliokusudiwa.

5.1.1.6 Kauli za Kibinafsi Katika Ujenzi wa Mwangwi wa Methali

Katika utunzi na uwasilishaji wa shairi hili, mshairi hakutumia methali au hakuwa na nia ya kufanya hivyo. Kwa kutafakari zaidi mawazo yanayoibuliwa, hadhira huweza kupata mshabaha wa methali ambazo huweza kuwiana na ujumbe unaowasilishwa. Methali kama vile *mafahali wawili hawakai zizi moja*, au *mafahali wanapopigana ni nyasi zinazoumia*. Methali hizo huweza kuhusishwa moja kwa moja katika utunzi na uwasilishaji wa utungo. Kwa mfano, *ni mafahali wenye matumbo* ndio waliopigana ili mshindi aweze kutambuliwa. Kila mmoja hujihisi babe au bora kuliko mwenziwe. Kwa

hivyo, mafahali hao hawawezi katu kuishi katika himaya au zizi moja. Hali hiyo imetokana na ukweli kwamba *mafahali* wawili huwa wenye mielekeo ambayo imetofautiana na matokeo ni ukinzani au upimanaji nguvu. Kwa yule fahali ambaye ameibuka mshindi ndiye aliyetoa sauti iliyosikika, na kwa yeyote ambaye huikaidi sauti hiyo hupatilizwa adhabu kali. Ili mshindi na mshinde apatikane ni lazima kuwepo na ushindani au upimanaji nguvu.

Katika uhalisi wa mambo, mafahali hao wawili wanapopigana ni nyasi ndizo huathirika kwa kukanyagwa. Mwelekeo huo huweza kuifanya hadhira kupata uelekezo wa methali yoyote waipendayo. Kwa hivyo, msomaji anapozingatia busara au mantiki iliyofumbwa na iliyoibuliwa kutokana na methali, huweza kutunga taswira ya kimaono na kuhisi namna watazamaji walivyo *wakondefu*. Katika muktadha wa uwasilishaji, nadharia ya Semiotiki huakisi kwamba, matini zilizotumika huwa ni ishara ambazo huweza hupata upatanisho wake siyo tu ndani ya utungo bali pia kwa kuzingatia miktadha ya jamii (Jacobson 1960). Katika muktadha wa shairi, hali hiyo ya watazamaji imesababishwa na matendo ya mafahali ao hao wanaopigana. Kwa sababu, maslahi ya jamii huwa hayatiliwi maanani kupitia kwa zogo la wanaowania uongozi. Kimsingi, watazamaji huwa hawaelewi asili ya vita hivyo, hujikuta katika mkumbo wa kuathirika kutokana na matukio hayo ya *mafahali*. Methali hizo zilizorejelewa zingeweza kutumika au kutotumiwa katika utunzi na uwasilishaji wa shairi. Swali hapa ni kwamba:

- Iwapo methali hazikutumiwa kwa uwazi katika utunzi na uwasilishaji wa shairi, ni kauli gani ambazo huibulia busara yake?

Ingawa katika shairi hili hakuna methali yoyote iliyotumiwa, kuna kauli mahususi zimeibuliwa kwa makusudi ili kuwasilishia ujumbe. Ni katika msingi huo, ndipo huweza kusailiwa iwapo matumizi ya wazi ya methali ni kichocheo cha pekee katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Endapo shairi la Kiswahili limeweza kuwasilishwa kupitia kwa kauli mahususi zilizobuniwa kibinafsi, humaanisha kuwa dhima ya methali katika ushairi wa Kiswahili huweza kufafanuliwa kupitia kwa maudhui yanayowasilishwa. Maudhui hayo yameweza kusawiriwa kupitia kwa kauli zilizotumiwa kwa makusudi katika uwasilishaji wa shairi. Kwa hivyo, utungo usiotumia methali huweza pia kupata nafasi katika ushairi wa Kiswahili.

Kwa ambavyo methali zimetumiwa mno katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili unaozingatia arudhi, shairi hili lisilozingatia arudhi huweza kuashiria mirengo miwili ya kiutunzi inayopatikana katika ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, kundi moja la washairi huweza kukinzana na kundi jingine la watunzi ambapo haipaswi kuwa hivyo. Katika muktadha huo, mgogoro wa ushairi huweza pia kuendelezwa kupitia kwa jinsi methali zilivyotumiwa. Kimsingi, makundi hayo mawili huchangiana na hukamilishana katika hali ya kuupeleka mbele ushairi wa Kiswahili.

5.1.1.7 Uibushaji wa Maudhui ya Kisiasa Kutokana na Matumizi ya Kauli Zilizokinzana

Katika usawiri na uwasilishaji wa maudhui ya kisiasa au utawala wa kimabavu, mshairi ametumia kauli zilizokinzana ili kuthibitishia wazo hilo. Katika mantiki hiyo, mshairi amejenga taswira ya utawala wa kimabavu katika jamii iliyowasilishwa, hasa kupitia kwa

maelezo ya kina kuhusu *mafahali wenye matumbo wanapigana.* Hata hivyo, msingi wa udhihirishaji wa mfumo huo wa kisiasa umeweza kuwasilishwa kwa kauli kinzani zinazoibuliwa kwa makusudi.

Katika shairi hili kuna makundi mawili yaliyozingatiwa: tabaka tawala na watawaliwa. Kwa mfano katika ubeti wa awali, mshairi amewadhihirisha *watazamaji* kuwa *wakondefu.* Kundi hilo limeshangilia kwa vifijo vita vya mafahali wawili ambao wamo katika mapambano. Kwa mfano, watazamaji wameweza kushangilia kwa kusema kuwa:

Haya! Haya! Machakulo haya!* (Ubeti wa 1)

Kadhalika, vita vilipochacha na vumbi kutimka, watazamaji hao hawaoni vizuri michakato ya vita hivyo. Kwa hivyo, hewani kunakuwa kiwingu chana vumbi, kama ilivyowasilishwa kuwa: *vumbi hewani, vumbi machoni*! Ni baada ya biwi hilo la vumbi kutoweka, ndipo watazamaji wametanabahi kuwa mafahali tayari wamekwisha kumaliza zogo na mshindi amekaa kwenye *kichuguu* huku *akionyesha kidole kimoja sasa.* Kimsingi, taswira iliyoundwa kuhusu afya ya watazamaji si ya kuridhisha ingawa wanafurahia hali wanayoiona. Kutokana na kauli zilizozitumiwa, mshairi huitaka hadhira yake ielewe kuwa watazamaji au watawaliwa hufurahia jambo wasilolijua mwanzo wala hatima yake. Aidha, mshairi huitaka hadhira kuweza kuisaili na kuitafakari zaidi hali za watawaliwa kuhusu maisha yao badala ya kupoteza wakati katika kufurahia utawala usiojali maslahi yao.

Kulingana na maelezo yaliyotolewa, *mafahali* hao wanapigania shibe yao na wala si kwa maslahi ya umma au jamii. Kwa hivyo, njia ya wokovu wa wanyonge katika jamii imebainishwa pia kupitia kwa shairi la 'Njia ya Damu' (Kahigi na Mulokozi 1976:23). Kwa mfano, wamesema:

Wito unaita: "Shikeni mikuki
mapanga na miundu na bunduki
mwende kwenye kituo cha uhaki"

Katika dondoo hilo, Kahigi na Mulokozi wametumia dhana kama vile *mikuki*, *mapanga*, *miundu* na *bunduki* ili kubainisha harakati za kifasiri zinazopaswa kuzingatiwa na wanyanyaswaji. Kilichodhihirishwa hapa ni hali ya jamii kutoridhirika kwa uhalisi uliopo. Kadhalika, wale ambao hugombea hatamu za uongozi ni watu ambao hawana shida za kiuchumi. Walichokitaka ni kuimiliki kwa kuihodhi rasilimali na nyenzo muhimu za uzalishaji mali katika jamii. Katika kuukariri mfumo dhalimu wa kiulawala, imetumiwa kauli kwamba:

Ambapo kutembeza midomo ndo kusikika
Kunyamaza ndo basi kudhaniwa. (Ubeti wa 2)

Kupitia kwa dondoo hilo, kundi la watawala hupenda mno kubwabwaja maneno ambayo hayana umuhimu wowote katika maendeleo ya jamii. Ingawa jamii hufahamu kuwa utawala huo una dosari, hawapati nafasi ya kuukosoa. Kwa sababu, mtu yeyote ambaye hujiweka katika mstari wa mbele kutoa kauli za kukashifu au kukosoa, huyatia maisha yake hatarini. Hata hivyo, katika jamii ya watawaliwa si wengi ambao hutambua haki yao bali huukubali mfumo wowote wa utawala ilimradi wanapumua. Kwa hivyo, hawajui jinsi ya kujiopoa kutoka kwa lindi hilo la nakama. Matokeo yake ni kwamba, hustahabu na hali iliyopo. Hiyo ndiyo sababu ya kutumiwa kauli za kiusaili kuhusu

dhihirisho la amani, utulivu na ushirika ulioshinikizwa katika jamii. Katika ubeti wa pili, imedokezewa kuhusu usaili huo kuwa: *patulivu! Patulivu! Patulivu kweli*! Kwa sauti ya shime, ameukariri usaili huo katika ubeti wa mwisho kuwa:

Patulivu! Patulivu! Patulivu!
Lakini! Lakini! Lakini! (Ubeti wa 4)

Kutokana na maelezo yaliyotolewa, mshairi ameugusia uzandiki na usalihina wa utawala huo wa kimabavu lakini hataki kubainisha wazi msimamo wake bali huitaka hadhira ifumbue fumbo hilo kwa kuzingatia uelekezo wa kauli zilizotumika. Kwa hivyo, hakubaliani na mawazo ya watawala kuwa jamii hiyo ni *tulivu* kwani, pana dosari. Hata hivyo, swali ambalo hadhira hupaswa kujiuliza ni kwamba: dosari hiyo inayowasilishwa na mshairi ni ipi? Kupitia kwa dosari iliyorejelewa, mshairi imedokezewa katika ubeti wa awali kuwa, *fahali* mshindi hakuupata ushindi huo kwa kuteuliwa bali kwa kutumia nguvu kujipweteka hatamuni. Kadhalika, jamii haipewi uhuru wa kutoa maoni au maelekezo kuhusu utawala uliopo na kwamba, mtawala wa kimabavu hupewa ulinzi mkali na *askari*.

Katika shairi hili, dhana au kauli ya *mchwa ndio askari*, imetumiwa kwa makusudi ili kuashiria wingi wa makachero ambao wametumika kuwa chombo cha kuwanyamazisha wote wnaotilia shaka sera ya utawala wa kimabavu. Kwa sababu hiyo, kundi la jamii ambalo hukubali bila ya kusaili mfumo huo, huchukuliwa kuwa ni kundi jema au tiifu ambapo ni kinyume na kikundi ambacho hukashifu huchukuliwa kuwa kinapanga njama za kiusaliti. Matumizi hayo huifanya hadhira kupanua utafakari wa ujumbe ambao

umewasilishwa. Kwa hivyo, mshairi ameweza kuibua na kusawiri maudhui ya kisiasa kupitia kwa kauli kinzani zilizotumiwa katika uwasilishaji wa shairi.

5.1.2 Shairi: Nimechoka

Shairi hili ni miongoni mwa mashairi marefu katika diwani ya *Kichomi*. Shairi hili lina beti nane ambapo kila aya moja ina mistari au kauli msingi saba. Katika utungo, mshairi amefafanua kuwa: maisha ni makali au magumu, na daima binadamu wako mbioni kuyawania. Kadhalika binadamu amewasilishwa kama kiumbe ambaye hana uwezo wa kujinusuru au kubadili mkondo wa maisha yake. Kwa hivyo, mkondo huo ni wenye hatima moja: maangamizi au kifo. Ingawa binadamu yu hai kwa wakati wa sasa, siku moja atatoweka katika uso wa dunia ili akajumuike na wenzake waliomtangulia. Katika utunzi na uwasilishaji, mshairi ameibua matumizi maalumu ya lugha ili kubainisha kwa usanii kuhusu harakati za maisha kwamba: maisha hayana maana yoyote kwa mwanadamu.

5.1.2.1 Usawiri na Uwasilishaji wa Ujumbe Kutokana na Kauli Zinazojenga Taswira

Kwa kuzingatia kauli teule, mshairi ameweza kuusawiri na kuwasilisha ujumbe wake katika utungo huo. Kwa ambavyo isitiari zilizoundwa huweza kufasiriwa, mshairi amepata dira ya kuongoza katika kuupanga, kuufaragua na kuuwasilisha ujumbe. Kwa mfano, imesawiriwa katika ubeti wa awali kama ifuatavyo:

Nilipofikishwa hapa, na juu kupandishwa.
Na kwa hila gani, au, zilizopangwa
Ncha za waya hii ngumu ya maisha, sijui.
Lakini najiona nimeninginia kama ndege

Aliyenaswa na mtego wa mtoto mdogo.
Mimi, lakini, ni mwanadamu na akili zangu
Timamu. Ninaweza kudondoka kama nikipenda. (Ubeti wa 1)

Jambo ambalo limebainishwa hapa ni tukio ambalo limeshudiwa. Kwa hivyo,amejenga mazingira ya kuuelekeza ujumbe katika shairi. Vilie vile, kabla ya kuanza kuwasilisha mawazo hayo ya msingi katika ubeti wa mwanzo, tayari mshairi amekwisha kutumia neno *Nimechoka* kuwa anwani. Neno hilo limekuwa ni kidokezo cha msingi kuhusu ujumbe uliotarajiwa kuwasilishwa kiisitiari. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, anwani katika utungo ni dira ambayo huelekeza uteuzi wa kauli ambazo hupaswa kushirikishwa katika usawiri na matukio (Mitchell na Naggy 2000). Ingawa kauli hizo ni za kimapokeo, huweza pia kuwa ni za kawaida au zile ambazo huibuliwa na kutumiwa kwa makusudi na wasanii wa ushairi. Hali hiyo huweza kujenga mazingira ambayo huruhusu matumizi mengi ya kauli za kibinafsi katika ushairi wa sasa wa Kiswahili. Kwa hivyo, msomaji huwa ameandaliwa kabla kuhusu kiini cha ujumbe. Katika muktadha huo, mshairi ameingia moja kwa moja katika ufaraguzi wa ujumbe kupitia kauli teule ambazo huweweza kufasirika kwa kuzingatia tajiriba ya hadhira katika utamaduni na uhalisi wa maisha yao. Kwa mfano, mshairi ametumia kauli kwamba:

Ncha za waya hii ngumu ya maisha, sijui (Ubeti wa 1)

Vile vile, ni katika *waya* huo ndipo mhusika amejipata *ameningia*. Kimsingi, maneno yaliyotumiwa katika kauli hiyo ni ya kawaida, lakini muundo wake hauwezi kupanguliwa na ufasiri wake huweza kuwa ni wa kiisitiari. Zaidi ya hayo, mshairi huelewa fika jambo ambalo hutaka kuliwasilisha kwa hadhira. Kwa hivyo, ugumu wa *maisha* umemithilishwa kiisitiari na *waya* ngumu unaoweza kumkata au kumjeruhi. Kwa kutumia kauli hiyo,

mshairi ameweza kulipa shairi mwelekeo na kuwasilisha hisi tarajiwa. Kwa kuzingatia uelekezi wa taashira ya *ncha ya waya*, mshairi amejipa nafasi nzuri ya kuufumba na kuusawiri ujumbe. Kwamba, maisha ni vurugu, mateso na dhiki tupu. Kama ilivyoelezwa hapo awali, mawazo ya mtunzi yameweza kuwasilishwa kitaswira. Kadhalika, taswira iliyojengwa imesaidia pia katika ujenzi wa sitiari katika ubeti wa mwanzo na kwamba, mwangwi wake umetamalaki katika shairi zima. Ni kutokana na uelekezo huo wa sitiari iliyoibuliwa ndipo amepata msingi wa kujengea kisa au mawazo yaliyokusudiwa. Kadhalika, sitiari kama ishara za kisemiotiki zimeweza kujengewa kisa na kufasiriwa kwa njia tofauti tofauti. Kwa hivyo kauli msingi zilizotumiwa katika shairi haziwezi kufasiriwa kwa namna moja.

Katika msingi huu, mshairi ameweza kufafanua na kusisitiza zaidi ujumbe wake na pia kuibulia sitiari zingine ndogo ndogo katika beti zilizofuatia. Kwa mfano mshairi ameukariri zaidi ujumbe, kwa kusema:

> *Lakini ninaogopa chini yangu naona miti*
> *Iliyochongwa ikifuata usawa wa waya hii*
> *Ikingoja kwa hamu, kama mshikaki kunichoma,*
> *Kunitoboa na kufurahia kimya kimya* (Ubeti wa 2)

Katika dondoo hilo mshairi ametumia dhana muhimu kama vile: *miti iliyochongowa* inayongoja kwa furaha *kunichoma* na *kunitoboa*. Ni kutokana na ushirika wa dhana au kauli hizo ndipo mshairi amewezeshwa kuusukuma mbele ujumbe wake. Kwa hivyo, mshairi ameashiria kuwa kama binadamu yeyote ni sharti atapata au atapitia dhiki kubwa kama hiyo katika maisha. Kadhalika, dhana ya *miti iliyochongoka* ilitarajia *kunichoma* imeunda taashira ya ugumu na masaibu yanayopatikana katika uhalisi wa maisha.

Mshairi hatosheki kwa kauli hizo zilizotumiwa, bali amezidi kubainisha ujumbe kwa kauli za kiisitiari ambazo zimeibuliwa kwa makusudi. Kwa mfano, amesema:

> *Mikono inauma, na waya imekwisha kata vidole.*
> *Damu imetiririka hadi kwapani; kujipangusa siwezi.*
> *Nimechoka.* (Ubeti wa 3)

Kutokana na dondoo hilo na hasa kwa kuzingatia dhana ya *mikono inauma, na waya imekwisha kata vidole*, mshairi amewasilisha kiisitiari ugumu wa maisha ambao humwathiri binadamu. Kwa hivyo, kwa kutumia kauli hizo, ameweza kuwasilisha ujumbe wake kwa namna mbili; kujenga taswira na pia kuibua isitiari katika shairi. Zaidi ya hayo, mshairi humtarajia msomaji kuzingatia maneno yaliyotumika kama ishara ambazo huweza kufasirika kutokana na uhalisi wa utamaduni wa jamii. Katika kusawiri na kuelezea zaidi kuhusu hali ya kutokujali kuhusu maswala ya maisha, mshairi amesema kuwa: *wanadamu wameinama.* Taswira iliyoibuliwa ni ya waumini ambao wamo katika kipindi cha ibada lakini kiisitiari ni kwamba, amewawasilisha binadamu wasiokuwa na utu au moyo wa huruma kwa wenzao ambao wamo katika hali ya mateso. Katika muktadha huo, mshairi ametumia dhana ya binadamu walioinama ili wasomaji kuweza kufasiri mawazo ambayo yamewasilishwa kiisitiari. Kwamba, binadamu hapigwi mshipa na dhiki au yale yanayowatendekea waja wenzao. Ingawa mshairi kama mhusika, ameathirika vibaya na waya au maisha anaanza *pole pole ... kutabasamu.* Kihalisia ni kwamba, mtu hutabasamu anapofurahia hali anamojikuta. Hata hivyo, msomaji anapoifasiri kauli hiyo kama isitiari, ndipo falsafa na mwelekeo wa kidhanishi hubainishwa. Katika muktadha huo, shairi limeweza kutungwa na kuwasilishwa kutokana na uelekezo wa dhana za kiisitiari ambazo huweza kufasiriwa katika tajiriba na uhalisi wa maisha ya jamii.

Aidha, kupitia kwa dhana hizo za kiisitiari, mshairi ameweza kuupitisha ujumbe kuhusu kukata tamaa katika maisha na kwamba, binadamu hustahabu kuendelea kuishi kama kikaragosi hadi siku zake za mauko zitakapowadia (Musau 1985). Hiyo ndiyo sababu ya kutumiwa kwa kauli:

Sijafikia hatua ya kucheka; maana nimechoka,
Kichomi kimenipata na sijadondoka. (Ubeti wa 8)

Kutokana na maelezo yaliyotolewa, binadamu huyo amepata mateso chungu nzima lakini amepania kuendelea katika hali hiyo. Kama alivyojikaulisha yeye mshairi ni kwamba, angetaka angeweza kujidondosha lakini hataki kuchukua hatua hiyo. Kwa hivyo, ufasiri wa isitiari imetekelezwa kupitia kwa kauli zilizotumiwa. Kwamba, maisha ni vurugu na dhiki tupu kwa binadamu na katu hana njia nyingine aijuayo.

5.1.2.2 Matumizi ya Mbinu ya Usimulizi na Uakifishi katika Kuibulia Msuko wa Vitushi

Mshairi ametumia kiambishi cha nafsi ya kwanza '**ni**' pamoja na alama za kufungua na kufunga usemi [" "] kuwa mbinu ya kuubinafsisha ujumbe unaowasilishwa katika utungo. Matumizi hayo yameufanya utungo kuwasilishwa kimasimulizi kwa uelekezo wa viakifishi. Katika anwani, mshairi ametumia dhana ya kuchoka kwa kuibinafsisha kauli hiyo yaani *Nimechoka.* Kiambishi '**ni**' kimetamalaki katika kauli nyinginezo zinazopatikana katika shairi. Kwa kufanya hivyo, mshairi ameweza kutunga na kufaragua ujumbe ambao umemhusu mwehyewe kama mtu binafsi. Katika ufaraguzi wa vitushi, amebainisha tukio lililomsibu na mwelekeo wa msingi anaouchukua katika maisha yake. Katika muktadha huo, mshairi amesema:

Nilipofikishwa hapa, na juu kupandishwa.
Na kwa hila gani, au, zilipofungwa
Ncha za waya huu mgumu ya maisha, sijui. (Ubeti wa 1)

Kwa kuzingatia dondoo hilo, mshairi ameweza kubainisha hisi zake na vitimbi anavyofanyiwa kutokana na nguvu au msukumo fulani asioufahamu vizuri. Kwa hivyo, kauli zilizozitumiwa hueleweka kwa msomaji kuwa za kimasimulizi ambapo zina mshabaha wake katika mbinu za utambaji zilizotumika kuwa mianzo ya msingi kwenye masimulizi ya ngano au hadithi za fasihi simulizi (Wamitila, 2002 na Finnegan, 1977). Kadhalika, mshairi alipokuwa akifaragua zaidi mawazo alitumia viambishi '*ni*' na '*mimi*' kama ilivyodhihirishwa katika kauli zifuatazo:

- *Lakini najiona nimeninginia kama ndege* (Ubeti wa 1)
- *Mimi, lakini, ni binadamu na akili zangu* (Ubeti wa 1)
- *Lakini ninaogopa chini yangu naona miti* (Ubeti wa 2)
- *Ikingoja kwa hamu, kama mshikaki kunichoma* (Ubeti wa 2)
- *Lazima nishike kwa nguvu nisianguke kama kifurush* (Ubeti wa 2)
- *Mikono inaniuma, na waya imenikata vidole* (Ubeti wa 3)
- *Ninatazama huku na huko kuwatafuta wenye huruma* (Ubeti wa 3)
- *Ninaendelea kuning'inia kama picha iliyotundikwa* (Ubeti wa 4)
- *Machozi yananitoka, kujipangusa siwezi* (Ubeti wa 4)
- *Ninashangaa zaidi kusikia sauti ya baba* (Ubeti wa 5)
- *Ninaendelea kuning'inia. Nimechoka* (Ubeti wa 8)
- *Mikono inaniuma* (Ubeti wa 8)
- *Mimi bado nimening'inia na vitimbo having'oki* (Ubeti wa 8)
- *Lakini pole pole ninaanza kutabasamu* (Ubeti wa 8)

- *Kichomi kimenipata na sijadondoka.* (Ubeti wa 8)

Kauli hizo zilizotapakaa katika shairi zimemfanya mshairi kuwa na dira mwafaka zilizomwongoza katika kusuka vitushi na kuwasilishia kimasimulizi ujumbe uliotajiwa. Katika muktadha wa matumizi ya kauli hizo, huwa ni msingi wa kimasimulizi wa kupanga, kuwasilisha na kufafanulia ujumbe. Vile vile, ujumbe ungeweza pia kupitishwa kwa methali ambazo hupatikana katika mawasiliano ya jamii, lakini kwa ambavyo kauli hizi zimekaulishwa zimekuwa ni chombo cha kuwasilishia hisi na mchomo wa mtu binafsi. Kwa sababu, methali ni mali ya jamii ilihali kauli za mshairi huweza kuwa ni mali ya kibinafsi. Kwa hivyo, kauli za mshairi huweza kuwa za aina mbili: zilizosimamia mawazo na mielekeo ya kibinafsi na zile ambazo huwakilisha mtazamo wa jamii. Tofauti iliyopo hapa ni ndogo mno. Kwa sababu, kauli hizo hutumika katika miktadha ya jamii. Hata hivyo, kauli za kibinafsi zimesaidia katika kuibulia na kujenga mwangwi wa methali katika uwasilishaji wa maudhui katika shairi.

Katika ujenzi wa vitushi, matumizi hayo yameurutubisha uwasilishaji wenye mwelekeo wa kimasimulizi. Kadhalika, mshairi ametumia kauli halisi kwa uelekezi wa viakifishi vya kufungua na kufunga usemi [“ ”]. Kauli hizo ni kama vile:

- *“Jamanie! Nisaidie! Ng'oeni hivyo vitimbo!”* (Ubeti wa 4)
- *“Mnaliona hilo! Joga!”* (Ubeti wa 6)
- *“Ninyi nyote hamna akili! Mnaniudhi Hamwoni hali yangu!”* (Ubeti wa 6)
- *“Najua utafika wakati itakulazimu kudondoka,*
  Lakini endelea kushikilia hiyo waya
  kama unazo nguvu bado, na usikate tamaa
  ila usietegemee kusifiwa au kusaidiwa;

Vichwa vyote hivi vilidondoka kutoka umbali huo,
Nawe kudondoka utadondoka!" (Ubeti wa 7)

Kutokana na madondoo hayo, mshairi ameweza kujenga vitushi katika shairi kwa kuzingatia aina mbili za kauli: kauli za mshairi kama mhusika na sauti ya watazamaji wa kadhia hiyo inayowasilishwa. Kwa njia hiyo, kauli huakisi usemezano wa wahusika katika shairi (Karama 1996, Njogu 1993). Kwa hivyo shairi, ingawa haibainiki wazi, limewasilishwa kwa kuzingatia malumbano ya wahusika. Kadhalika, kwa kutumia kauli zilizopatikana katika makundi hayo mawili: ya msemeza na wasemezwa, mshairi ameweza kuupeleka mbele ufunuo wa vitushi na ujumbe uliowasilishwa.

5.1.2.3 Uendelezaji wa Mawazo na Ujenzi wa Taharuki Kutokana na Kauli Elekezi

Katika shairi hili, mshairi amebainisha mchomo wa dhiki anazozipata yeye kama mhusika kutokana na ugumu wa maisha. Aidha, taswira iliyoundwa ni ile ya kujipata amening'inizwa kama *ndege aliyenaswa na mtego wa mtoto.* Kutokana na maelezo aliyoyatoa mshairi ni kwamba, amechoka kiwiliwili na akili huku asiweze kufahamu la kufanya. Vile vile, kilio chake hakiibui huruma miongoni mwa wanajamii. Katika kuyaendeleza mawazo, mshairi amewasilisha mawazo kwa kuzingatia mbinu ya taharuki. Hata hivyo, kauli za makusudi zilizoibuliwa zina nafasi muhimu katika shairi, kwa ambavyo husaidia kujenga taharuki kwa kuzingatia pahali ambapo zimetumiwa.

Katika ubeti wa kwanza hadi ya pili, mshairi ameanza uwasilishaji wake kwa matao ya chini ili kujenga upeo wa juu. Kwa hivyo, hadhira huweza kusoma beti za mwanzo ili

kuweza kubainikiwa na hali ambayo mshairi alimojikuta. Katika kuusukuma mbele ujumbe kitaharuki imetongolewa:

Ninatazama huku na huko kuwatafuta wenye huruma
Lakini wanadamu wote wazima wanainamisha vichwa
Chini kama kwamba hawanijui; hata jamaa zangu! (Ubeti wa 3)

Katika muktadha wa dondoo hilo, msomaji huchochewa zaidi kutaka kujua: Kwa nini binadamu *wote wazima wameinamisha vichwa* ilihali kuna mtu ambaye hutaka msaada wao? Kadhalika, kwa nini jamii ya mhasiriwa imejifanya kuwa haimjui hata ingawa kuna jamaa zake wa karibu? Kwa kutumia kauli zinazozua maswali, mshairi huweza kuifanya hadhira yake iwe yenye hamu ya kutaka kuendelea kulisoma shairi hasa kwa uelekezo wa kauli zilizotumiwa. Kwa upande mwingine, amepata nafasi ya kuibua hoja nyingine mpya. Kwa njia hiyo, amejifunulia mwanya mwingine wa kukuza mawazo yake. Kwa mfano, imesawiriwa kuwa:

Nitaendelea kuning'inia kama picha iliyotundikwa
Katika shamba la mawele, na mwenye shamba
Huvuta waya kutoka nyumbani itingishike kuwatisha ndege
Machozi yananitoka, kuyapangusa siwezi. (Ubeti wa 4)

Katika muktadha wa ubeti huo, mshairi tayari amekwisha kuwasilisha hali aliyonayo katika beti za awali lakini kupitia kwa dondoo hili ameng'ang'ania kuendeleza kwa mshindo mawazo yake. Kwa hivyo, amejifananisha na kinyago kinachovutwa huku na huko na *mwenye shamba la mawele*. Kwa kutumia kauli hizo, imejengwa picha nyingine ya kiakili kuhusu masaibu hayo. Jambo la msingi linalowasilishwa ni kuwa, yeye kama mhusika ni kama kikaragosi kinachoyumbishwa kwa nguvu ambazo hawezi kuzidhibiti. Kwa kuukoleza na kuufafanua zaidi ujumbe uliowasilishwa, mshairi amechopeka ukwenzi na kilio cha uhitaji, kwa kusema kuwa:

"Jamani e! Nisaidie! Ngoeni hivyo vitimbo"
Lakini wanadamu wameinama. Wanaanza sasa kusali. (Ubeti wa 4)

Kwa kuzingatia dondoo hilo, mshairi huitarajia hadhira itambue kuwa kuna watu wanaoshuhudia masaibu anaoyapata. Kutokana na kauli zilizotumika kwa makusudi katika dondoo hilo, hadhira huweza kutunga maswali ya kujenga utafakari kama vile:

- Kwa nini mhusika huyo ametoa kilio cha kutaka msaada ilihali binadamu wenye akili zao hawaitikii wito wa mwenzao?
- Je, ni masaibu gani zaidi ambayo yatamtokea mhusika huyo?
- Usemezano baina ya mhusika (mshairi) na watazamaji utaendelea vipi?
- Anayeathirika atachukua hatua gani au atafanya nini?

Hayo ni baadhi ya maswali ambayo hujenga mazingira ya kumstua na kumdhibiti msomaji ili kuweza kushawishika kuendelea kulisoma shairi; ubeti hadi ubeti . Endapo hadhira itasitisha usomaji wake itakuwa haijitendei haki. Kwa sababu, haitaupata kwa ukamilifu mfululizo wa mawazo yaliyowasilishwa. Kwa kuidhibiti zaidi hadhira, amejenga taswira ya kimaono kama ifuatavyo:

Kati ya vitimbo, vichwa vyeupe vimezuka ardhini.
Ukweli wa maisha unakuwa kama ndoto ya uwongo
Kichwa kimoja kinasema kwa sauti "mnaliona Hilo!"
Halafu vichwa vyote vinacheka. Ninashangaa.
Ninashangaa zaidi kusikia sauti ya baba
Ikicheka miongoni mwa vichwa hivyo vyeupe.
Sijaamini macho, siyaamini masikio, sikiamini kichwa. (Ubeti wa 5)

Katika kauli zilizotumika, mshairi amechopeka kwa makusudi sauti ya wahenga ambapo miongoni mwao ni baba yake mzazi ambaye ameshiriki katika kumzomea: *Mnaliona Hilo*! Hayo ni maneno ambayo hayampi matumaini yoyote mhusika anayedhikika na

kuzomewa. Katika hali hiyo, mshairi amewasilisha na ameelezea zaidi hisi na mchomo alionao. Kwa mfano, amesema:

> *"Ninyi nyote hamna akili! Mnaniudhi!*
> *Hamwoni hali yangu!"* (Ubeti wa 6)

Kauli hizo zilizotumiwa, hukusudiwa kuibua malumbano baina ya mhasiriwa na wanaomtazama ambapo baba yake mzazi yu miongoni mwao. Kwa hivyo, msomaji hutarajia kuelezwa zaidi kuhusu malumbano hayo. Hiyo ndiyo sababu ya kutongolewa kwa sauti nyingine ambapo baba yake mzazi amesema:

> *"Najua utafika wakati itakulazimu kudondoka*
> *Lakini endelea kushikilia hiyo waya*
> *Kama unazo nguvu bado, na usikate tamaa,*
> *Ila usitegemee kusifiwa au kusaidiwa,*
> *Vichwa vyote hivi vilidondoka kutoka umbali huo,*
> *Nawe kudondoka, utadondoka!"* (Ubeti wa 7)

Tukio kama hilo lililosawiriwa halitarajiwi kumhusisha jamaa wa karibu wa mhusika aliye taabani. Kwa hivyo, kupitia kwa mhusika ambaye ni baba yake, imewasilishwa ujumbe kwamba; hakuna msaada au tegemeo lolote lililoweza kutarajiwa kutoka kwa jamii. Kwa hivyo, duru ya akili ya msomaji huchochewa kuibua maswali ya utafakari ambayo huhitaji kujibiwa au kutolewa maelezo ya kina. Baadhi ya maswali ambayo huweza kuibuka au kutunga katika akili ya msomaji ni kama:

- Mshairi kama mhusika atachukua hatua gani?
- Iwapo hatachukua hatua yoyote, hali yake itakuwa vipi?
- Watu hao wanaomkebehi na kumcheka huashiria nini?
- Ni nini matokeo ya tukio linalosawiriwa na mshairi?
- Mawazo yaliyoibuliwa hudhihirisha nini kuhusu itikadi au mwelekeo wa mshairi?

Kwa ambavyo mshairi ameelewa kuwa hadhira hutarajia jibu kwa hamu, amesema:

Nitendelea kuning'inia. Nimechoka. Mikono
Inauma; hatari ya vitimbo. Vinacheka. Wanasali
Sasa wanaimba. Sitaki nyimbo zao; maana
Mimi bado nimening'inia na vitimbo havingoki
Lakini pole pole ninaanza kutabasamu.
Sijafikia hatua ya kucheka; maana nimechoka
Kichomi kimenipata na sijadondoka (Ubeti wa 8)

Kwa kurejelea kauli zilizomo katika dondoo, mshairi haoni haja ya kuendelea zaidi kulirefusha shairi. Hata mahadhi na mwendo wa shairi umebadilishwa na hadhira hutarajiwa kuusoma ubeti kwa matao ya chini. Hiyo imetokana na ukweli kwamba, kilele cha mgogoro wa vitushi tayari umefikiwa, kilichosalia ni kuhitimishwa. Ingawa mshairi amefikia kikomo katika ubeti wa mwisho, ukweli ni kwamba, hadhira bado imejengewa mazingira ya kutafakari zaidi mawazo yaliyoibuliwa ili kuweza kupatanishwa na miktadha ya utamaduni na uhalisi wa maisha katika jamii.

5.1.2.4 Ujenzi wa Usaili na Utafakari Kutokana na Matumizi ya Kauli za Makusudi

Kimsingi, wa usaili na utafakari katika shairi umetokana na kauli za makusudi zilizotumiwa katika shairi. Mshairi tangu hapo awali amelipa shairi hili anwani ya *Nimechoka*. Kutokana na anwani, ameweza kujenga muktadha wa matukio na mawazo yaliyoshughulikiwa. Kwa hivyo, hata kabla ya kuzama katika usomaji wa shairi, msomaji huchochewa kwa kujengewa vidokezo vya utafakari. Aidha, kuwepo kwa anwani kumesaidia kuibulia maswali ya usaili kama yafuatayo:

- Ni nani ambaye amechoka?
- Ni kwa nini mhusika huyo amechoka?
- Kuchoka huko kumesababishwa kwa misingi gani?

- Ni nini matokeo ya kuchoka huko?

Zaidi ya kwamba maswali hayo huweza kuibua taharuki, huichochea na huingiza hadhira katika utafakari zaidi wa maswala yaliyowasilishwa. Kimsingi, dhana ya *Nimechoka* imemfanya mshairi kuzingatia baadhi ya kauli na msamiati ambao huweza kuibulia mawazo yaliyowasilishwa. Hiyo ndiyo sababu ya mshairi kuamua kuanza uwasilishaji, kwa kusema kuwa:

> *Nilipofikishwa hapa, na juu kupandishwa*
> *Na kwa hila gani, au, zilipofungwa*
> *Ncha za waya hii ngumu ya maisha, sijui*
> *Lakini najiona nimening'inia kama ndege*
> *Aliyenaswa na mtego wa mtoto mdogo*
> *Mimi, lakini, ni mwanadamu na akili zangu*
> *Timamu. Ninaweza kudondoka, kama nikipenda* (Ubeti wa 1)

Katika ubeti huo, mshairi ametumia baadhi ya kauli na maneno teule ambayo kwa pamoja yamejenga msingi ambao umechochea utafakari katika akili ya hadhira. Katika muktadha wa nadharia ya Semiotiki, kauli ambazo hutumika zaidi katika tungo za kifasihi huwa ni zile ambazo huchochea usaili na utafakari (Imbosa 1990 na Hawkes 1977). Kadhalika, kauli hizo teule hupata nguvu kwa kuzingatia uwiano wavyo na kauli zingine ambazo huibuliwa kibinafsi na kutumiwa kwa makusudi (Barthes 1981). Kwa mfano, mshairi ameelezea kuhusu tukio ambalo limesikitisha kuwa; alivyojikuta ameninginia kwenye waya huo wa maisha, hawezi kutambua ni nguvu gani zilizotumiwa. Katika hali ya upanda alimojikuta, mshairi ameweza kujenga kitendawili au fumbo kwa hadhira. Katika muktadha huo, huweza kusailiwa kuwa:

- Ni nguvu gani, zilizomfanya mshairi au mhusika katika shairi kuning'inia kwenye *waya hiyo ngumu ya maisha?*

- Ni kwa nini mshairi ameamua kwa makusudi kujifananisha na *ndege aliyenaswa na mtego wa mtoto mdogo?*
- Je, mhusika huyo aliyesawiriwa huweza *kudondoka* kwa hiari na akiamua kufanya hivyo, matokeo yatakuwa nini?

Katika ubeti wa pili, mshairi ametoa jibu la fumbo hilo lakini kwa hadhari kubwa, kuwa *ninaogopa*, kwa vile chini ya waya hiyo ngumu ameona *miti iliyochongwa ... ikingoja kwa hamu kunichoma* pindi anapodondoka. Kwa kutumia dhana ya *ninaogopa*, kunaichochea hadhira kufikiria zaidi hali na mazingira ambayo yamemzunguka mhusika huyo katika shairi. Muktadha ambao umejengwa ndiyo umesababisha kukaririwa kuwa:

> *Ninatazama huku na huko kuwatafuta wenye huruma*
> *Lakini wanadamu wote wazima wameinamisha vichwa*
> *Chini kama kwamba hawanijui; hata jamaa zangu!* (Ubeti wa 3)

Katika dondoo hilo, mshairi ametumia kauli huielekeza hadhira kufahamu madhila ambayo yamempata mhusika. Kwa kujenga usaili zaidi, hadhira huweza kujiuliza kuwa:

- Wanaoshuhudia mateso ya mhusika kama mwanajamii mwenzao, wana hisia au mielekeo gani kuhusu utangamano wao katika jamii?

Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi ni kwamba, mtunzi wa ushairi huwa hana muda mwingi wa kufafanua hoja kwa kina.Kwa hivyo, hudokezea mawazo ambayo hupaswa kuzingatiwa (Parry 1971). Kwa ambavyo, mshairi hana muda mwingi wa kujieleza, huitaka hadhira ijitahidi na ijitwishe mzigo wa kuyaendeleza mawazo ambayo yamewasilishwa kwa kuitathmini mielekeo ya jamii kuhusu swala la maisha katika jamii.

Mshairi haishilii hapo tu, bali ameendelea kuidhibiti zaidi hadhira kwa kuitaka itafakari kuhusu tukio, hali na muktadha ambao umesawiriwa. Kwa mfano, mshairi ametumia kwa makusudi kauli kuwa:

> *Nitaendelea kuning'inia kama picha iliyotundikwa*
> *Katika shamba la mawele, na mwenye shamba*
> *Huvuta waya kutoka nyumbani, itingishike kuwatisha ndege* (Ubeti wa 4)

Katika dondoo hilo, mshairi ametumia kauli mbalimbali ambazo zimejenga taswira ya mhasiriwa. Kwa mfano, hapo awali mhusika aliyetundikwa kwenye waya alikuwa akijitapa kuwa, kwa utashi wake angeweza kujiopoa au kujidondosha lakini jambo hilo halijawezekana. Katika mawazo ya hadhira, huyo ni mhusika ambaye hawezi kujinasua kwa nguvu alizonazo. Kwa hivyo, amesawiriwa kama kikaragosi tu kinachoweza kuyumbishwa kwa nguvu ambazo ziko nje ya uwezo wake. Hiyo ndiyo sababu ya jamaa walioshuhudia, hawataki kujiingiza katika mambo wasiyoyajua mwanzo wake lakini wametambua hatima yake. Kwa mfano, mhusika amehitaji msaada wa dharura *lakini wanadamu wameinama wanaanza kusali.* Katika muktadha huo, msomaji ameandaliwa mazingira ya kujiuliza baadhi ya maswali ya kutafakarisha kama vile:

- Maisha huwa na maana gani kwa mwanajamii?
- Mwanajamii huweza kupata msaada kutoka kwa wanajamii wenzake?

Kwa kuitafakarisha zaidi hadhira, mshairi amesawiri kuhusu mielekeo ya wale waliokuwa wakishuhudia tukio hilo, kuwa:

> *Kichwa kimoja kinasema kwa sauti "mnaliona Hilo!"*
> *Halafu vichwa vyote vyeupe vinacheka. Ninashangaa.*
> *Ninashangaa zaidi kusikia sauti ya baba*
> *Ikicheka miongoni mwa vichwa hivyo vyeupe*(Ubeti wa 5)

Kwa kuzingatia dondoo hilo, mshairi huichochea hadhira ili iweze kutafakari kuhusu tukio la *vichwa vyote vyeupe vinacheka.* Swali ambalo msomaji huweza kujiuliza zaidi kutokana na tukio hilo ni: kwa nini, wahenga wameshiriki katika kumcheka huyo anayepata dhiki? Baada ya kutafakari, msomaji huweza kufumbua fumbo hilo. Kwamba, hizo ni harakati mbalimbali zinazofanywa katika maisha ilihali hatima ni moja: maangamizi au kifo (Musau 1985). Kulingana na mshairi ni kwamba, haoni ni kwa nini mja hujiingiza katika hawaa za dunia na matokeo yake ni kujiangamiza yeye mwenyewe. Aidha, kupitia kwa kauli zilizotumiwa, mshairi huitaka hadhira kujenga mazingira ya kugutuka na ifahamu kuwa, dhiki za maisha kwa mja ni jambo ambalo ni la kawaida. Katika kuukoleza zaidi ujumbe huo, amesema:

> *"Nyinyi nyote hamna akili! Mnaniudhi!*
> *Hamwoni hali yangu!" napiga kelele. Lakini vichwa*
> *Havitishiki, na wanadamu hawatingishiki*(Ubeti wa 6)

Kupitia kwa dondoo hilo, huitaka hadhira ifahamu kuwa si binadamu walio hai tu bali pia wafu hufurahia dhiki ambazo humpata mja katika maisha. Kwa kauli moja, vikundi hivyo viwili, waliopo na waliotoweka: hushangilia mateso ambayo humkumba mja katika harakati za kupania hawaa za dunia. Kutokana na maelezo yaliyotolewa, mja huwa hana uwezo wa kufahamu kuwa maisha ni hadaa hadi pale anapotoweka katika uso wa dunia. Hiyo ndiyo sababu ya kukaririwa kuwa:

> *Vichwa vyote hivi vilidondoka kutoka umbali huo,*
> *Nawe kudondoka, utadondoka!* (Ubeti wa 7)

Kutokana na kauli ziliazopatikana katika dondoo hilo, mshairi amebainisha kimafumbo itikadi yake kuhusu maisha na ameitaka hadhira ilinganishe hoja zilizopo katika aya za awali na zile zimebainishwa katika ubeti wa saba ili kupata ufunuo wa msimamo

uliowasilishwa. Kwamba, maisha hayana maana au matumaini yoyote ila dhiki tupu ambazo humfurahisha mja aliye hai. Swali ambalo huweza kumpitikia msomaji kwa kuzingatia kauli zilizotumiwa katika uwasilishaji wa ujumbe ni kwamba: maisha yana maana gani? Hilo ni swali ambalo mshairi amelielekezea hadhira ili kuumua usaili na utafakari katika muktadha wa shairi na pia katika uhalisi wa maisha. Mazingira ya uchimuzi wa swali hilo umetawala katika kauli mbalimbali zilizotumiwa katika shairi zima. Hata hivyo, uchimuzi huo umedhibitiwa zaidi katika ubeti wa mwisho, kwamba:

> *Nitendelea kuning'inia. Nimechoka. Mikono*
> *Inaniuma; hatari ya vitimbo. Vinacheka. Wanasali*
> *Sasa wanaimba. Sitaki nyimbo zao; maana*
> *Mimi bado nimening'inia na vitimbo having'oki.*
> *Lakini polepole ninaanza kutabasamu.*
> *Sijafikia hatua ya kucheka; maana nimechoka,*
> *Kichomi kimepata na sijadondoka.* (Ubeti wa 8)

Katika muktadha wa ubeti huo, imetumiwa kauli mahususi ambazo huweza kumfanya msomaji kufikiria zaidi kuhusu ujumbe ambao umewasilishwa. Baadhi ya maswali hayo ambayo yameibuliwa ni kama:

- Kwa nini, mshairi (au mhusika) amepania kuendelea kuning'inia *kwenye waya ngumu* hata ingawa amechoka?
- Kwa nini, mshairi (au mhusika) ameanza *pole pole kutabasamu?*

Hayo ni baadhi ya maswali ambayo yamesaidia kujenga fumbo ambalo huhitaji kufumbuliwa katika shairi.

5.1.2.5 Matumizi ya Viakifishi na Uradidi wa Maneno kama Mbinu ya Kujengea Muundo, Ridhimu na Mahadhi

Mtunzi ametumia viakifishi na uradidi wa maneno kama msingi wa kujengea muundo na kuibulia siyo tu ridhimu bali pia mahadhi katika utungo unaowasilishwa. Kimsingi, viakifishi vinavyotumiwa katika uwasilishaji wa matini huafiki au huzingatia kanuni za kisarufi (Kitsao, 1995 na Nkwera 1978). Kadhalika, mbinu hyoi imetumiwa kwa makusudi katika harakati za uwasilishaji wa shairi. Matumizi ya uradidi wa kauli au maneno hupatikana zaidi katika uwasilishaji wa tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kama vile nyimbo na ushairi (Mitchell na Naggy 2000). Mshairi ametumiakwa ustadi mbinu zote mbili kuwa msingi wa uwasilishaji. Mathalani, **[,]** na kituo na **[;]** zimetumiwa kuwa mtuo mdogo ndani ya sentensi au katika kauli ili kutenganisha mawazo mawili yanayozuliwa kwa pamoja au kuashiria mtuo kabla ya msomaji kuendelea katika usomaji. Kwa mfano, imetumiwa kauli kwamba:

Nilipofikishwa hapa, na juu kupandishwa
Na kwa hila gani, au, zilizopangwa
Ncha za waya hii ngumu ya maisha, sijui(Ubeti wa 1)

Kwa kuzingatia dondoo hilo imebainishwa kuwa, kauli teule zilizotumiwa katika uwasilishwaji haziwezi katu kujisimamia pasi na uelekezo wa viakifishi. Kupitia kwa matumizi ya viakifishi, mtunzi ameweza kuudhibiti mwendo na mahadhi katika usomaji wa shairi. Zaidi ya hayo, ametumia herufi kubwa kwa namna mbili: Kama mianzo ya mishororo na pia kama mbinu ya kudokezea hoja mpya katika shairi. Kwa mfano, mianzo yote katika mistari ya shairi imetumiwa herufi kubwa. Kwa mfano, imesawiriwa kuwa:

Mimi, lakini, ni mwanadamu na akili zangu
Timamu. Ninaweza kudondoka, kama nikipenda (Ubeti wa 1)

Kutokana na kauli zilizotumiwa, imebainishwa kwamba; mshairi ametumia herufi kubwa ili kuielekeza zaidi hadhira. Kwa hivyo, matumizi ya herufi kubwa yametumiwa kuwa kidokezo cha mianzo ya kauli ngeni na pia kuwa mianzo ya sentensi. Kwa sababu hiyo, ameielekeza zaidi hadhira kuzingatia usomaji wa kauli kwa mahadhi yaliyotarajiwa na vile vile kujengea muundo na ridhimu katika uwasilishaji. Kwa ambavyo ana hoja mbali mbali ambazo ameziwasilisha, ameamua kwa makusudi kutumia viakifishi ambavyo si vya aina moja ili kuibua kauli ambazo husaidia kufafanulia ujumbe ambao umeangazia miktadha tofauti. Kwa mfano, ametumia kituo na kikomo **[;]** ili kuunganishia na kushirikisha hoja mbili ambazo zimehusiana, kama ifuatavyo:

> *Mikono inaniuma, na waya imekwisha kata vidole*
> *Damu imetiririka hadi kwapani; kujipangusa siwezi ...*
> *Lakini wanadamu wote wazima wanainamisha vichwa*
> *Chini kama kwamba hawanijui; hata jamaa zangu!* (Ubeti wa 3)

Kwa kutumia kiakifishi cha kituo na **[;]**, mshairi anawezeshwa kuunganisha hoja zinazokinzana lakini zenye uhusiano. Kadhalika, kwa kutumia kiakifishi hicho, huitaka hadhira ipate wasaa wa kutua kidogo ili kuweza kutafakari hoja mpya ambayo inawasilishwa katika shairi. Katika ubeti mbili za mwanzo, mshairi ametoa ufafanuzi wa kina kuhusu *Kichomi* cha maisha ambacho humwandama mhusika. Zaidi ya hayo, kauli ambazo hupatikana katika mshororo wa mwisho katika ubeti wa tatu, mshairi amebainisha zaidi usiyahi alionao kwa kutumia kiakifishi cha mshangao [!]. Usiyahi huo, umeibuliwa ili kumwathiri msomaji wa shairi na umejitokeza zaidi katika ubeti ufuatao:

> *Machozi yananitoka, kujipangusa siwezi.*
> *Najitahidi kutoa sauti kwa nguvu:*
> *"Jamani e! Nisaidie! Ng'oeni hivyo vitimbo!"*
> *Lakini wanadamu wanainama. Wanaanza sasa kusali.* (Ubeti wa 4)

Katika uwasilishaji wa mawazo ambayo yamepatikana katika beti mbili za awali, mshairi amekuwa akielezea namna alivyoteseka, lakini alipofikia ubeti wa tatu amedokezea zaidi kuajabishwa kwake na malimwengu. Hata hivyo, muumano wa usiyahi umeudhihirishwa zaidi katika ubeti wa nne hadi ubeti wa saba. Kwa hivyo, kilio na kustaajabu kwake kumedhibitiwa na kuwasilishwa kwa hadhira kupitia kwa uelekezi wa matumizi ya kiakifishi cha kishangao ambacho kimeshirikiana na viakifishi vingine katika shairi. Hapa ikumbukwe kuwa, matumizi ya vishangao ni vya msingi katika uelekezaji wa usomaji katika shairi andishi. Kwa sababu, ridhimu na mahadhi hubadilika badilika kutoka kwa kauli au ubeti moja hadi nyingine. Vile vile, katika uwasilishaji wa ujumbe, mshairi ametumia mbinu ya usemezaji na usemezwaji. Kauli za msemeza zimetolewa kimaelezo lakini kwa kushirikisha kauli za wasemezwa katika shairi. Malumbano hayo yamejitokeza zaidi katika ubeti wa nne hadi aya ya saba. Mifano hiyo ni kama:

"Mnaliona Hilo!" (Ubeti wa 5)
"Mnaliona Hilo! Joga!' (Ubeti wa 6)

Katika kudhihirisha zaidi dhima ya usemezano, mshairi ametumia kauli halisi. Kwa mfano:

"Nyinyi nyote hamna akili! Mnaniudhi!
Hamwoni hali yangu!" (Ubeti wa 6)

Alama hizo za kufungua na kufunga usemi [“”] zimetumiwa kwa namna mbili: kudhihirisha kauli za wasemezwaji na za msemezaji. Katika muktadha huo, msomaji huelekezwa ili kubainisha kauli hizo kutokana na msingi ya uakifishaji. Kwa hivyo, mshairi ametumia sauti yake mwenyewe na wale aliolumbana nao ingawa hawaonekani. Katika kuelekeza zaidi matumizi hayo, imetolewa kauli kwa sauti nyingine, kwa kusema:

"Najua utafika wakati itakulazimu kudondoka,
Lakini endelea kushikilia hiyo waya
Ila usitegemee kusifiwa au kusaidiwa;
Vichwa vyote hivi vilidondoka kutoka umbali huo,
Nawe kudondoka, utadondoka!" (Ubeti wa 7)

Dondoo lililorejelewa ni refu lakini haliikifu hadhira. Kwa vile, mahadhi au ridhimu iliyoibuliwa imedhibitiwa kwa uelekezi wa viakifishi vya kufungua na kufunga usemi vinavyotumiwa katika uwasilishaji wa shairi. Kadhalika, viakifishi mbalimbali katika utungo vimetumiwa kwa makusudi ili kuuvunja mfululizo wa kauli au ujumbe unaowasilishwa. Katika hitimisho, mshairi amebainisha zaidi mwelekeo wake kwa kauli za kimaelezo ambazo zimesadifu muktadha wa kujenga matao ya chini kwenye shairi. Katika muktadha huo, uwasilishaji na upokezi wa ujumbe huwa umedhibitiwa kutoka mwanzo hadi tamati kutokana na matumizi ya makusudi ya viakifishi.

5.1.3 Shairi: Kuchambua Mchele

Hili ni mojawapo ya mashairi mafupi yanayopatikana katika diwani ya *Kichomi.* Beti tatu za awali zina mishororo au mistari minne na ubeti wa mwisho una mstari au mshororo mmoja. Ingawa shairi hili ni fupi, limesheheni na limefumba kwa ukamilifu mawazo kuhusu matarajio ya jamii na utekelezwaji wa Azimio la Arusha la Mwaka wa 1967. Kadhalika, mshairi ametumia mbinu mbalimbali za lugha kuwa msingi wa utunzi na uwasilishaji wa ujumbe katika shairi.

5.1.3.1 Matumizi ya Taswira na Isitiari kama Mbinu ya Kusawiri na Kuibushia Mawazo

Kutokana na vipengele mbalimbali vya lugha vilivyowekewa pamoja, mshairi ameweza kuunda taswira ya kimaono kuhusu ujumbe ambao umewasilishwa katika shairi. Kwa mfano, mshairi ametumia dhana ya *Kuchambua Mchele* kama anwani na pia kama dira ya kuongoza katika uwasilishaji ujumbe. Ni kutokana na mazingira yaliyojengwa ndipo mtunzi amepata nguzo mwafaka ya kuibulia taswira pana iliyohitajika katika ubainishaji wa mawazo yaliyowasilishwa katika shairi. Kwa uelekezo wa shughuli muhimu ya kijamii, mshairi amesema kuwa:

Habari zilifika kutoka Arusha
Tukaanza kuchambua mchele wa ujamaa (Ubeti wa 1)

Kutokana na shughuli au harakati hizo za kijamii, mshairi ameweza kutathmini iwapo malengo ya Azimio la Arusha yaliafikiwa au la. Kwa hivyo, mshairi ameweza kubainisha kuwa mfumo huo wa kisiasa ulianza rasmi mwaka wa 1967 baada ya Azimio la Arusha kutangazwa katika taifa la Tanzania. Baada ya hapo, serikali pamoja na jamii ilianza kutathmini iwapo maazimio hayo yalikuwa yenye manufaa katika jamii. Katika muktadha uliojengwa na maelezo yaliyotolewa, hadhira imewasilishiwa harakati hizo katika misingi ya taswira iliyoundwa. Katika utathmini huo, wanajamii au wale waliopewa majukumu hayo walikuwa makini na wala hawakupuuzia jambo lolote la muhimu. Katika muktadha huo, imebaishwa kuwa:

Macho mbele, macho pembeni, tukatoa mchanga
Tukafanya kaburi dogo la mchanga (Ubeti wa 1)

Shughuli hiyo ya uchambuzi au utathmini, ilijumuisha jamii ambayo ilikuwa yenye maono na mwamko wa kizalendo. Matokeo ya utathmini huo ni *kaburi dogo la mchanga*. Kupitia kwa kauli mahususi zilizozitumiwa, jamii husika bado haijaudhibiti mfumo wa ujamaa kama ilivyopitishwa katika Azimio la Arusha. Kwa mfano, ni baada ya shughuli ngumu ya kujitolea kwa uaminifu ndipo chenga na uchafu uliomo katika mchele umeweza kupambanuliwa. Hiyo ilikuwa ni kazi ngumu kwa wanajamii waliotwishwa jukumu hilo. Hiyo ndiyo sababu ya kukaririwa kuwa:

> *Vidole vikaanza kazi kama cherahani*
> *Usiku na mchana; macho yakauma.*
> *Tukafanya kichuguu kidogo cheupe* (Ubeti wa 2)

Katika dondoo hilo mshairi amedhihirisha kuwa, hiyo shughuli hiyo iliwapambanua waliouvaa ujamaa ambapo: walikuwa ujamaa walikuwa ni wachache mno na wengi wao ni wale wanaoupinga mfumo huo. Kutokana na kauli zilizotumika, hadhira huweza kujenga taswira ya kimaono na kihisia. Kwamba, kazi hiyo ilikuwa ngumu, ya kuchosha na ya kukatisha tamaa. Kwa mfano, matokeo ya harakati hiyo ilijenga *kichuguu kidogo cheupe* cha mchele. Swali ambalo limeweza kujengewa au kumpitikia msomaji, ni kwamba:

- Mfumo wa ujamaa katika Jamhuri ya Tanzania ulifanikiwa kweli?

Jibu hapa ni: la. Vile vile, hadhira inaposoma kwa uelekezo wa kauli hizo huweza kuupata ujumbe kitaswira na pia kuwaonea huruma wale wachache ambao wana msukumo wa dhati wa kujenga mfumo wa kijamaa katika jamii hiyo inayowasilishwa. Katika jamii hiyo, pana makundi mawili yaliyokinzana: wale wa *kaburi dogo la mchanga* na *wale wa kichuguu kidogo cheupe*. Hayo ndiyo makundi ambayo msanii angependa

hadhira kuweza kuyatafakari na kuyaelewa. Kadhalika, jambo la kukatisha tamaa zaidi, ni kwamba:

Chenga na chenga vikawa vingi sana.
Tukapika baada ya muda mrefu wa kazi.
Tukaanza kula,
Tukakuta bado mchanga na chenga! (Ubeti wa 3)

Katika muktadha huo, imewasilishwa hoja ya kukatisha tamaa kuhusu juhudi hizo za ujenzi wa jamii mpya. Kwamba, hata baada ya kujitolea katika harakati na juhudi zao za ujenzi wa jamii mpya kwa kuzingatia mfumo wa ujamaa bado *mchele* ulikuwa na *mchanga* na *chenga* nyingi sana. Kwa njia hiyo, mshairi ameitaka hadhira ifahamu kuwa ingawa mfumo huo wa ujamaa ulikuwa wenye matarajio ya manufaa, mwafaka huo haujafikiwa katika kizazi cha sasa. Ujumbe huo umewasilishwa kwa kuzingatia taswira iliyoundwa kwamba, mchele uliotayarishwa bado una *chenga* na *mchanga*. Kwa hivyo wali uliopikwa haukuweza kulika. Katika kuhitimisha shairi, mshairi ameuliza:

Lini tutaula bila mchanga, bila chenga? (Ubeti wa 4)

Kimsingi, swali ambalo limeulizwa huweza kuifanya hadhira kujenga taswira ya kukata tamaa kuhusu, ni lini ambapo jamiiitaweza kuula wali ambao hauna *chenga* wala *mchanga*. Kwa hivyo, imedhihirishwa kuwa; ingawa mfumo huo ulikuwa wenye manufaa. Hata hivyo, kuna baadhi ya watu ambao wamekuwa vikwazo au vizingiti vya kushuhudiwa kwa mwafaka huo.

Katika muktadha huo, taswira iliyoundwa imewakilisha ujumbe kwa udhahiri na wakati uo huo hadhira hutarajiwa kujenga usaili na kupiga bongo ili ujumbe uliofumbwa uweze kufumbuliwa. Kwa hivyo, ujumbe ambao umekusudiwa katika shairi ni ule uliofumbwa

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kwenye kauli zilizotumiwa kwa makusudi katika uwasilishaji huo. Kwa mfano, anwani ya shairi imeashiria *kuchambua mchele* ili kutenga mchele uliohitajika na *chenga* au *mchanga* usiohitajika. Hata hivyo, mshairi ameitumia anwani hiyo kwa makusudi ili kuitafakarisha zaidi hadhira. Kwamba, baada ya Azimio la Arusha kupitishwa rasmi mnamo mwaka wa 1967, jamii ya Tanzania ilitarajiwa kujengwa katika misingi ya ujamaa na baadaye ilitaka kutathmini iwapo malengo ya azimio yamefikiwa ua la. Kwa mfano, baada ya Azimio hilo kupitishwa, wanajamii wa Tanzania walitarajiwa kukata mirija ya ubepari na ukupe wa ukabaila ili kuuvaa mfumo wa ujamaa katika nyanja zote za maisha (Babu 1981). Kwa hivyo, muktadha ambao umejengwa katika shairi ni ule wa jamii ya Tanzania baada ya uhuru na hasa baada ya Azimio la Arusha kutangazwa rasmi. Baadhi ya maswali ambayo mshairi angependa kuibusha katika utafakari wa hadhira ni:

- Jamhuri ya Tanzania imefanya nini kuhusiana na mfumo huo kupitishwa rasmi na serikali?
- Mfumo wa ujamaa umekuwa wenye manufaa yoyote kwa jamii ya Tanzania?

Hayo ni baadhi ya maswali ya msingi ambayo yameshughulikiwa na yamewasilishwa kiisitiari kuanzia mwanzo hadi mwisho wa shairi. Kwa hivyo, harakati za jamii zimeshughulikiwa na zimewasilishwa kiisitiari. Kwa mfano, imesawiriwa kuwa:

> *Habari zilipofika kutoka Arusha*
> *Tukaanza kuchambua mchele wa ujamaa* (Ubeti wa 1)

Katika anwani, mshairi amedokezea kuwa jambo ambalo ametaka kulishughulikia ni *kuchambua mchele*. Ili kuyakinisha zaidi mawazo hayo, ameibua hoja zake katika katika muktadha maalumu wa kihistoria. Katika muktadha huo uliosawiriwa, hadhira

imejengewa mazingira ya kutambua kuwa kuchambuliwa huko kwa mchele umepaswa kuhusishwa na mfumo wa ujamaa katika jamii hiyo ya mwandishi. Kadhalika, katika akili ya hadhira imejengewa vidokezo vya kufahamu kuwa, mchele uliokusudiwa si mchele wa kawaida bali ni utathmini wa mfumo wa ujamaa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na taswira ya kimaono kuhusu waliohusika ni kwamba, wamo:

Macho mbele, macho pembeni, tukitoa mchanga (Ubeti wa 1)

Kupitia kwa kauli hiyo, jamii ya Tanzania imo katika shughuli muhimu ya kutathmini mafanikiyo ya mfumo wa ujamaa. Mfumo huo uliasisiwa na kiongozi mashuhuri wa wakati huo, Julius Kambarage Nyerere (Kitogo 2002). Mshairi hakutaka kuwasilisha mafanikio au kutokufanikiwa huko kwa mfumo huo kupitia matumizi ya lugha bayana au sahili, bali kwa kauli zilizoufumba kiufundi ujumbe uliowasilishwa. Kijuujuu, ujumbe huo huweza kuashiria shughuli halisi za uchambuaji wa mchele. Hadhira ya dhati hutarajiwa kupiga mbizi na kukuna bongo ili kuweza kuupata ujumbe wa ndani uliowasilishwa. Kwa mfano, mshairi ameunda isitiari katika muktadha wa kauli zilizotumiwa:

Vidole vikaanza kazi kama cherehani
Usiku na mchana, macho yakauma
Tukafanya kichuguu kidogo cheupe (Ubeti wa 2)

Katika muktadha wa dondoo hilo, medhihirishwa kuwa, baadhi ya wanajamii waliukumbatia kwa hamu mfumo huo wa ujamaa hasa kwa wale wasio nacho. Wale ambao walikuwa makabila na mabepari walikuwa na mawazo tofauti kuhusu mfumo huo. Kwao, waliuchukulia mfumo huo kuwa hatari kwa rasilimali yao ambayo ingeweza kutaifishwa au kugawanywa katika jamii. Ingawa kikundi hicho cha jamii kilikuwa kilijifanya kuwa mfumo huo ni wa manufaa mchana; usiku walikuwa wakiendeleza

mambo yao kwa ubinafsi na kwa usiri mkubwa. Kwa hivyo, uchambuaji huo wa dhati uliweza kuwabaini kwa jicho pekuzi la kizalendo. Kwa mfano, imedhihirishwa kuwa:

- *Tukaanza kutoa chenga, moja moja* (Ubeti wa 1)
- *Vidole vikaanza kazi kama cherahani* (Ubeti wa 2)
- *Macho yakauma* (Ubeti wa 2)
- *Tukafanya kichuguu kidogo cheupe* (Ubeti wa 2)

Kauli hizo zilizodondolewa zimesaidia katika kuukoleza zaidi ujumbe uliowasilishwa kiisitiari kuhusu harakati za jamii zilizoazimia kutathmini mfumo wa ujamaa, Tanzania. Zaidi ya hayo, kauli hizo zimebainisha kuwa bado kuna kundi la watu ambalo ni la kizandiki. Kundi hilo dogo ni lile ambalo limekuwa likijiweza, limekuwa kikwazo kikuu katika harakati ya chama cha T.A.N.U. na serikali iliyokuwepo Tanzania. Kwamba, serikali ya Muungano wa Tanzania ilipanga mikakati ya mfumo wa ujamaa kwa manufaa ya walio wengi katika jamii, mwafaka huo ulibeuliwa na kundi hilo dogo la mabepari na makabaila. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, kikundi hicho kimekuwa ni kizingiti katika maendeleo ya ushirika na ugavi sawa wa rasilimali katika jamii. Hiyo ndiyo sababu ya kuwasilishwa ujumbe kiisitiari kwa kuzingatia kauli zifuatazo:

- *Chenga na mchanga vikawa vingi sana* (Ubeti wa 3)
- *Tukaanza kula* (Ubeti wa 3)
- *Tukakuta bado mchanga na chenga* (Ubeti wa 3)

Ingawa kauli hizo zimechangia katika kujenga na uwasilishaji wa taswira ya wali ulio na chenga. Kwa kufanya hivyo, mshairi ameweza kubainisha na kuuwasilisha ujumbe kiisitiari. Kwamba, mapambano hayo bado yalihitaji kuendelezwa na wala hayajafikia kikomo. Swali ambalo huweza kuipitikia akili ya hadhira, ni kwamba:

- Shughuli hiyo ya mapambano dhidi ya wahujumu wa mfumo wa ujamaa utaendelea hadi lini?

Katika kujenga na kushadidia zaidi usaili huo, imeulizwa katika ubeti wa mwisho kuwa:

Lini tutaula bila mchanga, bila chenga? (Ubeti wa 4)

Swali hilo ni la msingi ambapo, mshairi amelibwaga kwa hadhira ili itafakari zaidi kuhusu isitiari ulioibushwa katika uwasilishaji wa utungo. Kwamba, katika kizazi cha sasa; mwafaka huo uliotarajiwa haukuweza kufikiwa labda kwa kuwepo na kizazi kingine. Isitiari ambayo imeibuliwa katika shairi ni ile ya kutokuwa na matumaini katika kizazi cha sasa kuhusu mfumo wa ujamaa. Kadhalika, ubinafsi ni swala ambalo limekuwa likikaripiwa kupitia kwa baadhi ya methali zilizopo katika jamii. Kwa hivyo, methali mbalimbali huweza kutumiwa katika kuwasilisha ujumbe huo, kama vile: 'Mchoyo ni kama Mchawi' au 'Binadamu wote ni Sawa'. Methali kama hizo hupatikana kwa urahisi katika mawasiliano ya jamii zingeweza kutumiwa kuibulia taswira na isitiari katika utungo huo ili kubainishia umuhimu wa ujamaa. Hata hivyo, mawazo hayo yameweza kubainishwa na kufasiriwa kwa sitiari ambazo hupata uelekezo wa msingi katika muktadha wa utamaduni, uhalisi wa kihistoria.

5.1.3.2 Matumizi ya Usimulizi kama Msingi wa Kuibulia Hisi

Mshairi amesawiri na amewasilisha mawazo kimasimulizi na wakati uo huo kuibua hisi zake katika shairi (Momanyi 1998, Masinde 2003, Senkoro 1988, Mulokozi na Kahigi 1979). Kimsingi, mshairi ana mawazo ambayo huyawasilisha kulingana na tajiriba yake katika maisha ya jamii. Katika shairi, ujumbe umeibuliwa kutokana na mchomo alionao au mambo aliyoyashuhudia kuhusu mfumo wa ujamaa na jinsi ulivyotekelezwa katika

jamii. Katika kuwasilisha mawazo, ametumia kwa makusudi kauli mbalimbali ambazo zimedhihirishwa kwa mbinu ya usimulizi katika shairi. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli zilizotumiwa katika uwasilishaji wa utungo kama vile ushairi au nyimbo, huwa ni zile ambazo hujenga mazingira ya kuchochea hamu ya kuupata ujumbe uliotarajiwa (Ezeliora 2009). Katika muktadha huo, mshairi ameanza uwasilishaji kwa kwa kujenga mazingira ya usimulizi.

Isitoshe, mshairi amechagua kwa hiari kulipa shairi hili anwani ya *Kuchambua Mchele*. Katika msingi huo, ameweza kusawiri, kufumba na kuibua maswala ya kihistoria kwa kuzingatia mbinu ya viona mbele na nyuma. Hiyo ndiyo sababu kukaririwa kwamba:

> *Habari zilifika kutoka Arusha*
> *Tukaanza kuchambua mchele wa ujamaa* (Ubeti wa 1)

Kutokana na anwani pamoja na kauli ambazo zipo katika dondoo hilo, tayari mshairi amelipa utungo mwelekeo wa kisimulizi. Kwa hivyo, dondoo hilo limejenga muktadha wa dibaji ya usimulizi uliotarajiwa. Katika mantiki hiyo, mshairi huitaka hadhira irejelee maazimio ya Arusha ya mwaka wa 1967. Kwa kutumia kauli zilizopo katika dondoo hilo, mshairi alielewa kuwa hadhira ilifahamu maazimio ya mfumo huo wa ujamaa. Kwa sababu, vipengele vya lugha kama ishara hupata ufasiri wake kupitia kwa tajiriba za jamii (Esthope 1992). Kwa hivyo, mshairi ameweza kujenga muktadha wa kimasimulizi kuhusu jambo ambalo limemghasi na limemkirihisha. Muktadha huo umeweza kuibuliwa kupitia kwa matumizi ya kiambishi cha nafsi ya kwanza yaani ***'tu'***. Matumizi hayo yametamalaki kwenye mianzo yote ya vitenzi katika beti zote zilizounda utungo. Aidha, mshairi ametumia uelekezo wa viakifishi katika ujenzi wa usimulizi. Ingawa mshairi

amevyaza mfululizo wa matukio, mfululizo huo umevunjwa na umedhibitiwa kwa viakifishi vilivyotumiwa. Kwa mfano, ufaraguzi huo umewasilishwa ifuatavyo:

> *Macho mbele, macho pembeni, tukitoa mchanga*
> *Tukafanya kaburi dogo la mchanga* (Ubeti wa 1)

Kutokana na kauli zilizotumiwa katika dondoo hilo, mshairi ameudhibiti kwa ukamilifu usomaji au udurusu wa hadhira. Kadhalika, ameamua kwa makusudi kutotumia kituo mwishoni mwa aya kauli. Ameweza kufanya hivyo mwishoni mwa beti zake ili kulekeza kwamba, kuna uhitaji katika kufululiza katika udurusu na wala si kuishilia hapo. Katika muktadha huo, hadhira hulisoma shairi hilo siyo tu kwa kuzingatia kauli zilizotumiwa katika mshororo bali kwa uelekezo wa ishara za viakifishi ambavyo vipo ndani ya beti. Vile vile, mshairi ametumia viakifishi kwa malengo ya kuielekeza hadhira yake na pia kutolea hisi. Kwa mfano, imetumiwa kauli zifuatazo:

- *Tukakuta bado mchanga na chenga!* (Ubeti wa 3)
- *Lini tutaula bila mchanga, bila chenga?* (Ubeti wa 4)

Kwa kuzingatia kauli hizo, mshairi ameweza kutolea mchomo wa hisi na mshangao alionao kuhusu matukio ambayo yamewasilishwa. Kadhalika, ametumia kauli hiyo ya pili yaani *Lini tutaula bila mchanga, bila chenga?*. Kauli hiyo imesaidia kujengea msingi wa ubalagha na pia kama mbinu ya kuibulia utafakari katika shairi. Hapa huweza kueleweka kuwa, mshairi amekoleza zaidi usimulizi kama mbinu ya uwasilishaji kwa kutumia matukio ya kawaida yaliyofahamika ili kuibulia na kusawiri uhalisi wa maisha ya jamii.

Hata hivyo, kauli za kawaida zilizotumiwa zisichukuliwe kuwa ni kikwazo katika uwasisilishaji wa mawazo na hisi za mtunzi, bali kuwa ni msingi wa usimulizi ambao

umejengwa katika shairi. Kutokana na mfululizo wa usimulizi, ameweza kuudhibiti usomaji kuanzia mwanzo hadi tamati. Kadhalika, kwa kutumia kauli ya *Lini tutaula bila mchanga, bila chenga*?, ameweza siyo tu kuashiria tamati bali kujenga utafakari wa ujumbe uliowasilishwa.

5.1.4 Shairi: Hadithi ya Mzee

Shairi hili limejikita katika kuwasilisha historia ya jamii. Kwa hivyo, linadhihirisha namna baadhi ya jamii za Afrika zilivyokuwa zikiishi kwa amani na ushirikiano kabla ya maajilio ya mfumo wa ukoloni. Kwamba, ukoloni ulipokuja, jamii ziliupokea kwa shauku na matamanio makubwa. Hata hivyo, haikuchukua kipindi kirefu, jamii hizo ziligundua kuwa miundo msingi ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni imevurugwa. Baadhi ya wanajamii walipong'amua uhalisi huo, waliamua kwa pamoja kuwafurusha. Hata hivyo, imebainika kuwa miongoni mwa wanajamii tayari walikuwa wamekwisha kuuvaa na kuukumbatia utamaduni huo wa kigeni. Kwa hivyo, ilikuwa vigumu kuurejesha msingi wa maisha kama ulivyokuwa hapo awali.

Katika muktadha huo, mshairi hana matumaini yoyote katika kizazi hiki cha sasa na kwamba, jamii hizo zimegawanyika katika makundi mawili ya kimielekeo: wale waliouthamini mfumo wa utamaduni wa mwafrika na wale waliouabudu utamaduni wa kigeni. Katika muktadha wa uwasilishaji, hili ni shairi refu ambalo huweza kuwekwa katika muktadha sawia wa utunzi wa utenzi wa Kiswahili. Hata hivyo, mpangilio wa beti na mishororo ambayo hupatikana katika shairi hili haina idadi maalumu ya silabi.

Mshairi ametumia mitindo na kauli mbalimbali katika kuusawiri na kuuwasilisha ujumbe kama ilivyobainishwa.

5.1.4.1 Utambaji kama Mbinu ya Utunzi na Uwasilishaji katika Shairi

Kama ilivyokwisha kuelezwa, hili ni shairi refu ambalo limefumba na kuwasilisha mambo muhimu yaliyohusu historia na uhalisi wa maisha ya jamii. Kwa sababu hiyo, mshairi ameamua kwa makusudi kuwasilisha hoja zake kwa kuzingatia mbinu ya usimulizi. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, uwasilishaji wa shairi hupaswa kuzingatia siyo tu mpangilio mahususi wa vipashio bali pia maudhui huweza kuwasilishwa kiutambaji (Levi-Strauss 1955).

Kimsingi, shairi hili limegawanyika katika sehemu tatu: utangulizi, ujenzi wa vitushi au ufaraguzi wa ujumbe na hitimisho. Mbinu ya utambaji na usimulizi zilizotumiwa katika uwasilishaji wa utungo huu, hufanana na zile ambazo hupatikana katika ngano za fasihi simulizi (Finnegan 1977). Aidha, kuna viukundi viwili vya wahusika vilivyotumiwa katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. Kwa mfano, maelezo yaliyowasilishwa yametengwa ili kujenga mandhari au muktadha wa masimulizi. Katika kuuweka utungo huo katika mazingira ya utambaji, mshairi ametoa maelezo kuwa:

Ilikuwa siku ya Jumapili
Wakati kila mtu
Alikuwa amekwenda kusali
Watoto walipomzunguka
Mzee na kumwambia
"Tusimulie hadithi!
Hadithi tusimulie!
Babu tusimulie!" (Ubeti wa 1)

Kutokana na dondoo hilo, mandhari au mazingira ambayo yamejenga uhitaji wa usimulizi wa hadithi yamebainishwa. Katika mukadha wa fasihi simulizi, ni hadhira ya watoto ndio waliotambiwa hadithi na watu wazima au wazee hususa, babu au nyanya. Mandhari hayo yaliyojengwa humfanya msomaji kufahamu kabla kwamba, kilichotarajiwa ni uwasilishaji wa hadithi katika uhalisi wake. Kwa kufafanua zaidi mandhari hayo, mshairi amemleta fanani katika uwasilishaji wa utungo, kwamba:

Mzee alikohoa
Akacheka kidogo
Akafukuza inzi
Kwa mkia wa n'gombe (Ubeti wa 2)

Katika muktadha huo, mshairi ameweza kumtengea fanani nafasi yake na pia kudhihirisha namna utambaji huo ulivyoendelea baina ya *babu* na *wajukuu* wake kuwa:

"Mnataka nini?"
"Hadithi" walijibu
"Hadithi gani?"
"Nzige! Nzige! Nzige!" (Ubeti wa 2)

Ingawa hadithi hiyo imejikita katika *Nzige*, kimsingi matumizi hapo yameufafanua zaidi ujumbe kwa kujengewa muktadha wa uhai ambao umeshirikisha wahusika (mzee na wajukuu) katika uwasilishaji wa utungo. Hata hivyo, mshairi hajitoi kabisa katika kujishirikisha. Kwa sababu, hapa na pale katika shairi amejipa mwanya wa kudokezea na kuuelezea zaidi ujumbe unaowasilishwa. Kwa ambavyo wajukuu hujibu kwa pamoja kuwa walitaka kusimuliwa hadithi ya *Nzige*, ni dhahiri kuwa hapo awali walikuwa wamewahi kusikia au kudokezewa kuhusu kadhia ya wadudu au wageni hao.

Katika mazingira ya utambaji wa ngano za hurafa, wadudu, wanyama na hata miamba hutumiwa kama wahusika. Aidha, wahusika hao huwakilisha mienendo na vitendo vya binadamu (Ngure 2003). Kwa hivyo, wajukuu wametarajia kusikia kwa hamu ufafanuzi zaidi kuhusu kisa hicho. Mshairi ameupa utambaji huo lugha cheshi na pia kwa kuzingatia dhana au mambo ambayo hueleweka kwa urahisi katika utafakari wa mazingira ya hadhira. Kwa hivyo, mshairi ametumia dhana ya *Nzige* na *vimatu* ambao hupatikana katika mazingira ya jamii husika. Kupitia kwa *mzee*, imetongolewa:

> "... *Kwamba huko pwani*
> *Kumefika wadudu*
> *Wadudu wenye pua ndefu* ..." (Ubeti wa 4)

Katika muktadha wa dondoo hilo, na pia kupitia kwa fanani, imesawiriwa kwa ubunifu matukio muhimu ya kihistoria katika jamii. Kwamba, katika kipindi maalumu cha kihistoria, wazungu au wageni walipofika sehemu hizo za Afrika Mashariki na waliweza kuharibu na kuvuruga uchumi na kuuathiri utamaduni wa jamii. Katika usimulizi huo, ametumia nyimbo kama mbinu ya kuibulia burudani na pia kuishirikisha hadhira kushiriki kivitendo katika uwasilishaji wa matukio. Kwa mfano, fanani ameiga wimbo ambao jamii ilifunzwa na wageni hao kama alivyoendeleza kuwa:

> *Wakatufundisha na wimbo*
> *Wimbo wao ndio huu*
> *"Kuleni majani yoho!*
> *Kuleni majani yahoo!*
> *Vya chini tuachieni!*
> *Kuleni majani yahoo!*
> *Kuleni majani yahoo!*
> *Mazao tuachieni!"* (Ubeti wa 19)

Wimbo huo umeshikilia nafasi muhimu siyo tu kama njia ya kuishirikisha hadhira sikizaji, bali pia kama mbinu mwafaka ya kuitumbuiza na kuipunguzia machofu hadhira

katika usomaji wa shairi. Kwa njia hiyo, mshairi ameweza kuufanya ushairi kusomeka kwa mahadhi na ridhimu ambayo huiathiri hadhira. Kimsingi, uwasilishaji huo umetamalaki katika shairi zima na kila ubeti huweza kusomwa kwa mahadhi tofauti tofauti. Katika ubeti wa mwisho, imetumiwa kauli kwamba:

"Huu ndio mwisho
Mwisho wa hadithi yangu" (Ubeti wa 24)

Katika hatua hiyo, imeashiriwa kuwa masimulizi ya hadithi yamefikia ukingoni. Kwa hivyo, mshairi ametumia mbinu ya usimulizi kuwa kunga ya utunzi na uwasilishaji wa matukio katika muktadha wa utamaduni na uhalisi wa jamii.

5.1.4.2 Ujenzi wa Taswira kama Mbinu ya Usawiri na Uwasilishaji wa Ujumbe

Kauli ambazo zimetumiwa katika uwasilishaji wa ujumbe, zimesaidia katika kuibulia taswira ya kimaono katika uwasilishaji wa shairi. Kwa mfano, maelezo ya awali yaliyotolewa yamesaidia katika kujengea mandhari ya usimulizi na ya wahusika ambao hushiriki. Kwa njia hiyo, mshairi ameweza kutoa maelezo ya muhimu ambayo hutarajiwa katika upokezi wa ujumbe. Kwa hivyo, akili ya msomaji imedhibitiwa ili kuweza kuwaona washiriki walivyojiandaa na walivyoupokea hadithi iliyotambwa. Kwa mfano, imebainishwa kuwa:

Ilikuwa siku ya Jumapili
Wakati kila mtu
Alikuwa amekwenda kusali
Watoto walipomzunguka
Mzee ... (Ubeti wa 1)

Katika muktadha huo, msomaji huweza kufahamu kuwa siku hiyo ya masimulizi ilikuwa tulivu na wahusika walikuwa katika hali ya mapumziko. Aidha, kumejengewa mazingira

ya kuwaona *wajukuu* walimwendea *babu* ili awasimulie hadithi. Vile vile, *Mzee* amesawiriwa jinsi alivyojiandaa katika kukidhi matakwa au haja ya wajukuu ambao walikuwa na nia ya kusimuliwa hadithi. Mshairi tayari ameelezea namna *nzige* walivyofika huko *pwani* na uharibifu ambao waliufanya. Kadhalika, kauli mahususi zimetumiwa katika kujenga taswira ya wavamizi hao, kwamba:

- *Kumefika wadudu*

  Wadudu wenye pua ndefu (Ubeti wa 4)

- *Wengine walisema ni wekundu*

  Wengine walisema ni weupe

  Wengine walisema ni walafi (Ubeti wa 5)

- *Wengine walisema*

  Wanazungumza

  Lugha isiyoeleweka (Ubeti wa 5)

- *Lakini sisi tuliokuwa bara*

  Hatukuamini (Ubeti wa 5)

Taswira iliyoibuliwa katika muktadha wa madondoo hayo ni kwamba, *Nzige* hao walikuwa tayari wamefika pwani na wamo njiani kuselelea bara. Tetesi za maajilio zilienea huko bara kwamba: *walikuwa wenye pua ndefu, weupe, wekundu* na *wanakula kila jani bichi*. Kupitia kwa kauli au dhana hizo, mshairi ameweza kujenga picha ya kimaono kuhusu wavamizi hao ambao si nzige wa kawaida, bali ni wazungu au wageni waliovamia na kutamalaki katika janibu za makazi ya wenyeji wa mwambao kisha wakaelekea bara. Katika muktadha huo uliobainishwa, shairi limeweza kuwekwa katika mazingira ya uhalisi wa kihistoria. Kwa hivyo, baadhi ya wenyeji walioshuhudia kadhia

hiyo bado wangali wapo au matukio hayo yamehifadhiwa katika kumbukumbu ya watu katika jamii. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli teule ambazo hutumika katika uwasilishaji wa utungo ni zile ambazo hueleweka katika utamaduni na mapokeo ya jamii. Aidha, kauli hizo teule huweza kufasirika kwa urahisi katika muktadha wa utamaduni na tajiriba ya maisha katika jamii maalumu (Parry 1971). Mshairi amezitumia baadhi ya kauli hizo ili kuwasilishia ujumbe kwa uelekezo wa hisi zilizotarajiwa. Maelezo yaliyotolewa ni kwamba, wanajamii au wenyeji hawakuweza kuwafurusha *nzige* hao kama ilivyobainishwa hapa:

Kwamba kulikuwa na vita
Kati ya nzige na wanadamu
Kwamba nzige walishinda.
Na damu ya mwanadamu
Nyingi chini ilimwagika (Ubeti wa 8)

Picha ambayo imejengwa na kuwasilishwa ni ile ya kitalu cha mapambano makali yaliyojiri ambapo *nzige* au wazungu ambao walikuwa wakitumia silaha bora. Katika kubainisha mshindi na mshinde, imeelezwa kuwa:

Mikuki haikufaa
Mishale haikufaa
Maana silaha yao
Mikuwa ni kupumbaza
Miguu ilikufa ganzi
Sauti zilitukauka
Tukabaki kuduwaa
Kuwatazama wanyonyaji (Ubeti wa 13)

Kutokana na dondoo hilo, hadhira huweza kuunda taswira ya kimaono kuhusu mapambano yaliyojiri baina ya nzige na binadamu. Baada ya *nzige* kuwashinda na kuwanyazisha wenyeji; walibaki wakila shibe yao bila tashwishi. Katika muktadha wa kauli zilizotumiwa, hadhira huweza kuibua hisi za huruma kwa jamii hiyo kutokana na

uvamizi huo. Zaidi ya hayo, hadhira huelekezwa kutunga taswira ya wadhulumu na wadhulumiwa kiasi cha kuwachukia wanaodhumu.

Kadhalika, *nzige* walipomaliza kula usiku mzima bila ya kubakisha, wanaamua kujiondokea wenyewe. Baadaye, kundi kubwa la nzige lilitua na kuanza kula na kuwafundisha baadhi ya wenyeji lugha na utamaduni wao kama ifuatavyo:

Wakatufunza na kula
Kula kama nzige
Yaani bila kushiba.
Halafu maajabu yakatokea
Tukaotesha mbawa
Tukaanza kuruka
Kuruka huko hewani
Kimawazo kama nzige. (Ubeti wa 17)

Kupitia kwa kauli zilizotumiwa katika dondoo hilo, mshairi ameupatia nguvu na ameusogeza mbele ujumbe uliowasilishwa kuwa, wenyeji walianza kuiga matendo ya *nzige* na hata kuzungumza lugha ya kigeni. Aidha, wenyeji walipogundua na kubaini ubaya au athari za nzige, walianza kupanga mikakati ya kuwafurusha kwa kuzingatia misingi ya utu, heshima, umoja na amani. Mbinu hizo zilijikita katika utamaduni wa jamii. Mshairi amewasilisha ujumbe kwa kauli zilizojenga taswira ambazo zimesaidia mno katika kubainisha harakati za jamii, kuwa:

Kuzindukana
Tukawafukuza
Wakaenda na yao shibe
Sisi sote tukafurahi
Tukatunga na wimbo wetu
Wimbo ngao ya Afrika
Tutataja misingi ya utu
Heshima, Umoja na Amani. (Ubeti wa 20)

Kwa hivyo, *nzige* sasa tayari wametimuliwa na wenyeji. Katika akili ya hadhira ni kwamba, kuna hinikizo la vigelegele na vifijo vya kufurahia kuondoka kwa nzige hao. Hata hivyo, wazo hilo haliingii akilini mwa mshairi. Hiyo ndiyo sababu ya kutolewa kauli, kwamba:

Mara tukaona vimatu weusi
Wengi wanarukaruka
Kumbe wale nzige
Waliacha mayai mchangani!
Au ni watoto wetu! (Ubeti wa 21)

Taswira hiyo imeibuliwa kwa azma ya kuishirikisha na kuitafakarisha hadhira. Kwa sababu, *vimatu* walioanguliwa walikuwa wenye sura zilizoshabihiana na za wenyeji. Jambo hilo huweza kuibua hisi za kukereka miongoni mwa wasomaji. Kwa sababu, tayari nzige wamefurushwa lakini miongoni mwa jamii kuna wale walioendelea kutenda na kuendeleza mienendo ya nzige. Katika kuifuatiliza kwa karibu hoja hiyo, kumeibuliwa upanda wa kimawazo. Kwa hivyo, imesawiriwa kuwa:

- *Hao watoto wa nzige*
  Au ni watoto wetu! (Ubeti wa 21)

- *Tukashindwa kuwaua*
  Mana kusema kweli
  Walifufuka majumbani
  Majumbani mwetu kabisa
  Tukaanza kuwalea
  Lakini kimawazo
  Hatukupatana nao
  Mambo yakawa magumu. (Ubeti wa 23)

Kutokana na kauli zilizowasilishwa katika dondoo hilo, mshairi ameibua taswira ya hisi ambayo imesaidia kujenga utata ulitarajiwa katika shairi. Kwamba, hao *vimatu* walioanguliwa ni wana kindakindaki katika jamii. Kwa sababu, wao pia ni wanajamii na

katu hawakuweza kufurushwa ingawa walihitilafiana kimawazo na kimwelekeo. Kwa hivyo, kupitia kwa kauli hizo, hadhira huweza kutunga picha ya ugumu katika kutatua matatizo ya kijamii. Katika hatua hiyo, fingo la taswira katika shairi limefikia ukingoni huku hadhira ikiachiwa utafakari wa ujumbe uliowasilishwa.

5.1.4.3 Kauli za Makusudi kama Msingi wa Kuibulia Taharuki na Kuendeleza Mawazo

Shairi hili limewasilishwa kwa kuzingatia kunga za usimulizi wa ngano ambazo hupatikana katika fasihi simulizi. Mshairi ametumia kauli za makusudi kuwa msingi wa uibuaji na ukuzaji wa vitushi katika shairi. *Mzee* ambaye ni fanani, ameitikia wito wa kuwasimulia wajukuu ngano. Hadithi yenyewe ilihusu *Nzige*. Wajukuu ambao ni hadhira ya fanani wameshiriki katika upokezi wa masimulizi hayo. Hali hiyo ingeweza pia ingeweza kudhihirishwa kupitia kwa matumizi ya methali ambapo ingekuwa kichocheo cha kuishirikisha hadhira katika utafakari au upokeaji wa ujumbe (Kunemah 2008). Hata hivyo, methali mahususi haikutumika bali kumetumiwa mbinu za utambaji. Kwa hivyo, msimulizi ameiuliza hadhira maswali yafuatayo:

> *"Mnataka nini?"*
> *"Hadithi!" walijibu*
> *"Hadithi gani?"*
> *"Nzige Nzige Nzige!"* (Ubeti wa 2)

Kutokana na kauli katika dondoo hilo, mshairi amezingatia mbinu za uwasilishaji wa kisimulizi. Aidha, msomaji huweza kutunga taswira ya masimulizi hayo na pia kutambua kuwa hadithi iliyotarajiwa kusimuliwa ilihusu *Nzige*. Kimsingi, *nzige* ni wadudu wadogo ambao hupatikana katika mazingira ya jamii, lakini hadhira ya mshairi huweza kutaka

kujua zaidi kuhusu mwelekeo ambao ulichukuliwa kupitia kwa kauli za fanani. Kauli zilizotumiwa zimejenga msingi wa utangulizi katika uwasilishaji wa hadithi. Baada ya hapo, kumejenga mwanya wa kufaragua na kuendeleza zaidi mawazo kwa kumfanya fanani kuwa kinywa cha masimulizi hayo, kama ifuatavyo:

"*Kwanza zilifika habari*
Habari zisizoaminika
Kwamba huko pwani
Kumefika wadudu
Wadudu wenye pua ndefu
Na walao kila wakati." (Ubeti wa 4)
Wengine walisema ni
Wekundu
Wengine walisema ni weupe
Wengine walisema ni walafi
Wengine walisema
Wanazungumza
Lugha isiyoeleweka
Lakini sisi tuliokuwa bara
Hatukuamini (Ubeti wa 5)

Kauli zilizotumiwa katika dondoo hilo, zimesaidia katika kuwabainisha zaidi wavamizi hao. Kwa hivyo, hadhira huweza kufahamu kuwa, *nzige* hao walikuwa *wekundu, weupe walafi* na *huzungumza lugha isiyoeleweka*. Kimsingi, kauli ambazo zimetumiwa katika kuwabainisha nzige hao, zimeweza pia kujenga na kuibua taharuki katika shairi. Mbinu hiyo imekolezwa zaidi kwa ambavyo hao *nzige* wamepewa uwezo wa kuzungumza *lugha isiyoeleweka*. Kwa kuzingatia kauli zilizotumiwa katika uwasilishaji, hadhira huweza kujengewa swali la kiusaili, kama vile:

- Kwa nini, wale walio bara hawakuamini tukio hilo?

Kwa kutumia dhana ya *Hatukuamini*, kumeweza kujenga muktadha wa uhitaji wa maelezo zaidi. Kwa ambavyo hadhira hutaka kuikidhi haja hiyo ya tetesi kuhusu wavamizi hao, imedhihirishwa kuwa, *Nzige:*

> *"Ni wadudu wa ajabu!"*
> *Sisi tulikuwa bara*
> *Tukajiweka tayari!* (Ubeti wa 6)

Kutokana na kauli hiyo, swali ambalo huweza kuchochewa katika akili ya hadhira ni kama:

- Watu wa bara walijitayarisha vipi kukabiliana na *nzige* hao?

Hata hivyo, kabla ya kukamilisha matayarisho ya msingi, *Nzige* walikaribia katika makazi yao na wasiwasi ulianza kuhisika miongoni mwa wanajamii. Kwa kuzingatia mbinu ya taharuki, haielezwi namna *nzige* hao walivyojihami au mbinu zilizozitumiwa katika ushindi wa vita dhidi ya jamii ya pwani. Kwa hivyo, mshairi tayari amewasilisha hoja kwamba, *nzige* hao ni wadudu hatari kwa jamii. Kwa kurejelea habari hizo kutoka pwani, mshairi amejenga mazingira ya usaili kama ifuatavyo:

- Wakazi wa bara walikuwa na wasiwasi wa kiasi gani?
- Mikakati iliyopangwa na wakazi wa bara ilikuwa ipi?

Kwa hivyo, hadhira huweza kuwekwa katika hali ya kutarajia maelezo zaidi. Kulingana na nadharia ya Semiotiki, kauli ambazo hutumika zaidi katika uwasilishaji wa ushairi ni za kiisitiari ambapo kuna uhitaji wa ufafanuzi au maelezo. (Mutembei 2001). Sawia na methali zilizotumiwa; kauli zilizoshirikishwa katika utungo huhitaji ufafanuzi zaidi. Ili kujibu maswali hayo, mshairi amejitwika mzigo huo kupitia kwa kauli za *mzee* kwa kusema kuwa:

Tukaamua kwa pamoja
Mikuki kuitengeneza
Ngao na zana zingine.
Kisha tukapeana zamu
Ya kulinda mipaka
Usiku na mchana
Tu macho hatulali
Kwa kuwaogopa nzige. (Ubeti wa 10)

Katika muktadha wa dondoo hilo, wenyeji wa bara tayari wamejiandaa kwa silaha na pia kwa kushika doria. Wakati uo huo wenyeji walikuwa wenye wasiwasi mwingi. Muda si mrefu, *wingu jeusi la nzige* lilitanda angani na likatua katika eneo la wenyeji wa bara. Matukio hayo hujenga mazingira ya swali ambalo huweza pia kumpitikia msomaji, kwamba:

- Je, silaha na mbinu walizozitumia wenyeji ziliwafaa katika kukabiliana na nzige hao hatari?

Kama silaha au mbinu ya uwasilishaji, mshairi habainishi jibu la swali hilo bali huitaka hadhira iwe yenye subira katika usomaji wa utungo. Hata hivyo, imetumiwa baadhi ya hoja ambazo huweza kuisaidia hadhira kupata uelekezo wa ufasiri mwafaka wa ujumbe kuwa:

Mikuki haikufaa
Mishale haikufaa
Maana silaha yao
Ilikuwa ni kupumbaza
Miguu ilikufa ganzi
Sauti zilitukauka
Tukabakia kuduwaa
Kuwatazama wanyonyaji (Ubeti wa 13)

Kauli zilizotumiwa katika dondoo hilo zimebainisha historia jami. Kwamba, huko bara watu hawakuwa na la kufanya ila kuwatazama *nzige* walivyokula shibe yao. Katika

mawazo ya wenyeji, kundi hilo hatari litakapoondoka mambo yatakuwa shwari. Hata hivyo, swali ambalo huweza kuitafarisha zaidi akili ya hadhira, ni kwamba:

- Kwa nini wenyeji wa bara hawakuendelea na maisha yao ya kawaida hata baada ya kundi hilo la nzige kugura?

Ili kujibu swali hilo, mshairi amedokezea kuwa:

Kulikuja kundi jingine
Tena kubwa zaidi
Hili likakaa
Likatufundisha lugha
Lugha hiyo ya nzige
Wanadamu tukaimudu
Tukawaona wazuri (Ubeti wa 16)

Katika muktadha huo uliorejelewa ni kwamba, lile kundi la kwanza la nzige lilileta maafa makubwa katika jamii. Hata hivyo, jambo ambalo huweza kuigusa na kuishangaza hadhira ni kwamba:

- Kwa nini kundi la pili lilikubaliwa kuwa *wazuri* ingawa wote ni nzige?
- Wenyeji wa bara watakapobaini kuwa utamaduni wa hao *nzige* hauna nafasi katika maisha ya jamii, watachukua hatua gani?

Kimsingi, maswali hayo yamesaidia katika kubulia muktadha wa taharuki. Kupitia kwa maswali hayo, hadhira imeweza kudhibitiwa zaidi, kwa ubeti ufuatao:

Kuzindukana
Tukawafukuza
Wakaenda na yao shibe
Sisi sote tukafurahi
Tukatunga na wimbo wetu
Wimbo ngao ya Afrika
Tukataja misingi ya utu
Heshima, Umoja na Amani (Ubeti wa 20)

Mpaka hatua hiyo, kauli zilizotumiwa zimesadia kubainisha kuwa wanajamii waliweza kulisanzua au kulifurusha kundi hilo la pili la *nzige* katika jamii. Aidha, muktadha ulijengwa ni ule wa kufurahia kuondoka kwa nzige. Kauli za makusudi zimetumiwa ili kuibulia taharuki katika mashairi ya Kiswahili. Kwa mfano katika shairi 'Vuteni Makasia' (Kahigi na Mulokozi 1976:3), imeelezwa kuwa:

Wakapiga yowe wakifurahika
"Hakika kweli sasa tumeokoka"
Na kila mmoja akafikiria
Vipi mke wake atakapotokea

Hata hivyo, furaha hiyo ya uhuru ilikuwa ni ya muda mfupi na ya kujidanganya. Swali ambalo msomaji huweza kujiuliza zaidi ni:

- Kwa nini furaha hiyo iwe ni ya muda mfupi na ukweli ni kwamba kundi hili la nzige tayari limefurushwa au limeishajiondokea?

Mshairi kwa upande wake amefahamu haja ya hadhira. Hiyo ndiyo sababu ya kutumiwa kwa hoja au kauli, kwamba:

Mara tukaona vimatu weusi
Wengi wanarukaruka
Kumbe wale nzige
Waliacha mayai mchangani!
Vimatu wanafufuka
Kutoka mchangani
Hao watoto wa nzige
Au ni watoto wetu! (Ubeti wa 21)

Katika muktadha huo, mshairi amezua hoja mpya, hasa kwa kuzingatia dhana zifuatazo: *mayai mchangani*, *kuanguliwa kwa vimatu* na ni *watoto wetu*. Matumizi ya makusudi ya dhana hizo, huchochea hisi ya mshituko katika akili ya msomaji. Katika mazingira hayo yaliyowaslishwa, msomaji huweza kujengewa hamu ya kutaka kujifahamisha zaidi

kuhusu kadhia ambayo imewasilishwa. Katika mantiki hiyo, mshairi tayari amekamilisha uwasilishaji kwamba, *nzige* walipokuja na walipofurushwa waliacha athari zao katika utamaduni na maisha ya jamii. Kwa hivyo, ieleweke kuwa ushikamano na uendelezwaji wa vitushi umedhibitiwa kupitia kwa kauli teule ambazo zimetumiwa kuibulia taharuki katika usomaji wa shairi.

5.1.4.4 Matumizi ya Kauli Teule za Makusudi katika Usawiri na Ubainishaji wa Maudhui ya Ukoloni-Mamboleo

Swala ambalo mshairi amelishughulikia katika utungo huu ni ubainishaji wa maudhui ya ukoloni-mamboleo katika jamii za Afrika Mashariki. Katika kuendeleza hoja zilizowasilishwa, mtunzi ametumia kauli za makusudi kuwa kunga ya kufafanulia kiini cha ukoloni-mamboleo ulivyotamalaki katika jamii. Kwa mfano, kumetumiwa dhana ya *Nzige* ili kuibulia taashira ya wakala wa ukoloni na ukoloni-mamboleo. Katika muktadha wa nadharia ya Fomula ya Usimulizi, neno au dhana huweza kutumika kuibulia mawazo muhimu katika tungo za fasihi. Neno teule lililotumiwa huweza kujenga kichocheo cha kusawiri vitushi au mgogoro katika utungo (Mulokozi 1986 na Blake 1984).

Kwa mfano, mawakala wa ukoloni walikuja katika maeneo ya Afrika Mashariki kwa awamu: kama majasusi na baadaye kujenga himaya zao. Kama alivyodhihirishwa, nia yao haikuwa mwambao au pwani tu bali pia kutamakani katika mataifa yote ya Afrika Mashariki. Kama vile *nzige*, wakoloni walivamia kwa mshindo na vitimbi janibu hizo za Afrika. Kadhalika, wakoloni hawakukuta upinzani au vikwazo vya haja; pindi upinzani

ulipozuka ulizimwa kwa mitutu ya bunduki. Baada ya kutamakani na kujenga himaya zao, waliweza kueneza utamaduni wao. Kwa mfano, wakoloni kama *nzige*:

- *Likatufundisha lugha*
- *Lugha hiyo ya nzige* (Ubeti wa 16)
- *Wakatufunza na kula*
  Kula kama nzige
  Yaani bila kushiba
  Halafu maajabu yakatokea
  Tukaotesha mbawa
  Tukaanza kuruka
  Kuruka huko hewani
  Kimawazo kama nzige. (Ubeti wa 17)

Kutokana na maelezo hayo ni kwamba, polepole bila ya kuelewa nia yao, wenyeji waliwakubali wakoloni na wakashirikiana nao kama marafiki. Kwa hivyo, wanajamii wakawa wajuzi katika utamaduni wa *nzige* au wakoloni. Jamii za mataifa hayo ya Afrika zilipotathmini na zilipozinduka, ziliamua kupanga mikakati ya kuwafurusha wakoloni na kuung'oa utamaduni wao kama ilivyobainishwa hapa:

Kuzindukana
Tukawafukuza
Wakaenda na yao shibe
Sisi sote tukafurahi
Tukatunga na wimbo wetu
Wimbo ngao ya Afrika
Tukataja misingi ya utu
Heshima, Umoja na Amani. (Ubeti wa 21)

Kulingana na maelezo yaliyotolewa, wanajamii walianza kuzinguana na kuhamasishana katika misingi ya utu na utamaduni wao. Wakati huo ndipo mataifa ya Afrika yalipojinyakulia au yalipopewa uhuru. Mataifa hayo yaliingia katika tafrija na sherehe mbalimbali kama njia ya kuadhimisha ushindi wao (Thiong'o 1986). Uhuru huo,

kulingana na mshairi, haukuwa kamili bali ni wa kujihadaa. Kwamba, baadhi ya wanajamii tayari wamejifunza vitendo na kuuvaa utamaduni wa *nzige* au wakoloni. Mshairi ametahadharisha kuwa, mfumo wa ukoloni haukung'olewa kwa mizizi yake. Hiyo ndiyo sababu ya kutumiwa kwa kauli kwamba:

Mara tukaona vimatu weusi
Wengi wanarukaruka
Kumbe wale nzige
Waliacha mayai mchangani!
Vimatu wakafufuka
Kutoka mchangani
Hao watoto wa nzige
Au ni watoto wetu! (Ubeti wa 21)

Ingawa mataifa ya Afrika Mashariki yalipata uhuru na kuufurahia, mshairi ametumia kauli mahususi ambazo huweza kuisaidia kufahamisha kuwa, jamii inahitaji kutathmini upya uhuru wao. Kulingana na mawazo yaliyowasilishwa, wakoloni hao waliamua kujiondokea baada ya malengo yao kutimilika. Hata hivyo, waliacha athari zao zikiendelea kustawishwa na kutamalaki kupitia kwa mfumo mwingine wa ukoloni. Kwa mfano, wakoloni walipoondoka waliacha *mayai ya nzige* ambayo yaliweza kuanguliwa kwa *vimatu*. Vimatu hao baadaye, walikomaa na kuwa *nzige* kamili. Zaidi ya hayo, miongoni mwa vimatu hao walikuwepo *vimatu weusi* ambao walishabihiana na watoto halisi wa wenyeji. Kwa kuzingatia dhana za msingi na maelezo yaliyotolewa katika shairi yameashiria athari za ukoloni-mkongwe katika mataifa huru ya Afrika Mashariki, hususa, taifa la Tanzania. Kwamba, mfumo wa ukoloni haukutoweka kabisa katika jamii. Kulingana na kauli zilizotumiwa katika uwasilishaji, mfumo wa ukoloni- mkongwe umeaendelezwa kwa kivuli chao kupitia kwa *wana* au kizazi cha wenyeji. Kwa kukariri zaidi mawazo hayo imeelezwa kuwa, *vimatu*:

Walifufuka majumbani
Majumbani mwetu kabisa
Tutaanza kuwalea
Lakini kimawazo
Hatukupatana nao
Mambo yakawa magumu. (Ubeti wa 23)

Kwa hivyo, *vimatu weusi* ndiyo waliotarajiwa kuwa wawakilishi wa mfumo wa ukoloni-mkongwe. Hiyo ni tanzia ya uhuru uliosalitiwa na baadhi ya viongozi ambao wamejitenga na kuwasahau wananchi waliopigania uhuru huo (Senkoro 1988:113). Kadhalika, mshairi hana matumaini na uhuru wa bendera ambao hufurahiwa katika mataifa haya baada ya mkoloni kung'atuka. Matarajio yaliyopo ni kwamba, ukoloni-mamboleo huweza kungolewa kwa dhati wakati ambapo kizazi kipya kitakapozaliwa; kizazi ambacho kitaukataa ukoloni na sura zake mbalimbali katika jamii. Hata hivyo, mwafaka huo hauweza kupatikana. Kwa sababu, waliouendeleza mfumo wa ukoloni katika jamii ni wanajamii wenyewe ambao wana 'ngozi nyeusi'.

5.1.4.5 Matumizi ya Isitiari kama Chombo cha Kuibulia Utafakari wa Mawazo

Kutokana na kauli mahususi zinazotumika, zimemsaidia mshairi kuibulia na kuwasilisha mawazo kiisitiari. Kwa mfano, dhana ya *nzige* imekuwa dira ya kusawiri, kufaragua na kuwasilisha mawazo. Kama taashira, dhana ya *nzige* hujenga mazingiraya usaili kuwa:

- Nzige katika muktadha shairi huwakilisha nini katika jamii ya mshairi?

Kwa ambavyo imedokezewa kuwa, *nzige* hao walifikia pwani ya Afrika Mashariki na baadaye waliselelea bara. *Nzige* kama ishara, umemwelekeza msomaji kupatanisha ujumbe uliowasilishwa kwa kuzingatia uhalisi wa kihistoria wa Afrika Mashariki.

Kimsingi, *nzige* hao ni wakoloni waliokuja na kutamakani katika janibu za Afrika Mashariki. Katika mantiki hiyo, mshairi amejenga mazingira ya utafakari na ya kufafanulia dhana ya *nzige* kwa kuzingatia namna wakoloni walivyokuwa hapa Afrika Mashariki katika awamu tatu: kabla, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni au wakati wa uhuru. Baadhi ya kauli ambazo huweza kuichochea utafakari kuhusu ujumbe ambao umewasilishwa ni kama: *Nzige wenye pua ndefu, wekundu, weupe* na *waliozungumza lugha isiyoeleweka.* Kadhalika, habari za nzige hao zilitokea *huko pwani.* Kupitia kwa dhana hizo za kitaashira, msomaji huweza kuzipatanisha na kujenga isitiari pana inayoweza kutambulika na kufasirika kwa kurejelea historia na utamaduni wa jamii. Kwa sababu, hakuna maajilio na uvamizi wowote wa wageni uliowahi kuvuruga uchumi, mfumo wa utamaduni wa jamii isipokuwa ule wa ukoloni wa Majerumani au Waingereza uliokithiri mno hapa Afrika Mashariki. Zaidi ya hayo, jamii ilipozinduka ilipanga mikakati ya kuwafurusha wakoloni na wakaupata uhuru. Watu walifurahia mno uhuru huo kwa nyimbo wa kuusifu ushindi au ushujaa wao. Kwa mfano, mshairi amerejelea shamra shamra hizo za sherehe, kwa kusema:

Tukataja misingi ya utu
Heshima, Umoja na Amani (Ubeti wa 20)

Kulingana na kauli zilizotumiwa, kumejengwa taswira ambayo huweza kutumiwa katika utathmini wa furaha hizo katika kipindi cha uhuru hapa Afrika Mashariki. Kadhalika, kumezuliwa dhana nyingine ya *vimatu weusi* ambayo huchochea zaidi utafakari kama ilivyobainishwa hapa:

Mara tukaona vimatu weusi
Wengi wanarukaruka
Kumbe wale nzige
Waliacha mayai mchangani!

Wao watoto wa nzige
Au ni watoto wetu! (Ubeti wa 21)

Katika dondoo hilo, kumetumiwa dhana au kauli tatu za msingi ambazo zimemsaidia katika ujenzi wa isitiari. Dhana hizo ni *vimatu weusi, mayai mchangani* na *watoto wetu.* Dhana hizo ni za kitaashira ambazo kuufanya ujumbe katika utungo kufasirika kwa kuzingatia uhalisi wa kihistoria na utamaduni wa jamii. Kimsingi, hadhira huweza kuutafakari na kuupata uhalisi wa mambo unaosawiriwa na mshairi. Kwa mfano, wakoloni waliokuja hapa Afrika Mashariki waliweza kuulazimisha mfumo wa utawala wao dhalimu kwa wanajamii. Hata hivyo, utawala huo uliweza kufurushwa au kwa hiari yao waliweza kutoweka hapa Afrika Mashariki. Baadhi ya maswali ambayo huweza pia kujengwa katika akili ya hadhira ni kama:

- *Mayai* ya *nzige* yaliachwa nyuma kwa misingi gani?
- Kwa nini *vimatu* hao ni weusi ilihali *nzige* wenyewe walikuwa ni *weupe* au *wekundu*?
- Kwa nini *vimatu* hao wanachukuliwa kuwa *watoto wetu*?

Maswali hayo ndiyo yamesaidia katika uwasilishaji wa fumbo katika shairi. Katika mantiki hiyo, kauli hizo huashiria kuwa ingawa ukoloni ulifurushwa au uliondolewa, athari yake imeendelea kupata uhai na imestawishwa kupitia kwa wale ambao waliouvaa na waliouenzi utamaduni huo. Kwa hivyo, kupitia kwa kauli zilizotumiwa, huambainikia msomaji kwamba; mfumo wa ukoloni utazidi kuendelezwa ingawa kwa sura nyingine. Kwa sababu hiyo, jamii za Afrika Mashariki na Tanzania ikiwemo, bado hazijaupata uhuru uliotarajiwa ingawa zilipiga vigelegele na kusherekea kifo cha ukoloni mkongwe (Hussein 1971). Katika muktadha huo, hata baada ya mshairi kuhitimisha utungo, hadhira huweza kuendelea kujiuliza kuwa:

- Mfumo huo mpya wa ukoloni-mamboleo utatokomezwa lini katika kaburi la sahau?

Kulingana na mtazamo ambao umewasilishwa, mshairi hana kabisa matumaini katika harakati au mikakati zinatumiwa na kizazi cha sasa.

5.2. UCHANGANUZI WA USHAIRI WA KITHAKA WA MBERIA: *BARA JINGINE*

Diwani ya *Bara Jingine* ilitungwa na Kithaka wa Mberia na ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 2001 na Shirika la Marimba Publication Ltd. Diwani hiyo, ina jumla ya mashairi sabini na tisa. Kati ya mashairi hayo, ni mashairi manne tu ndiyo yamechanganuliwa. Mashairi hayo ni:

i. Hatujaaga Ndoto
ii. Bara Jingine
iii. Mruko wa Nyuki
iv. Nakumbuka Ulivyokuwa

5.2.1 Shairi: Hatujaaga Ndoto

Shairi hili ni la aya au ubeti mmoja tu lakini refu. Mshairi amefafanua hali halisi ya maisha ya wanajamii ambapo matumaini au ndoto yao ya ujenzi wa jamii mpya bado haijatimilika. Kwa mfano, wanajamii walipokuwa wakipigania na wakiwania uhuru, walikuwa na matarajio makubwa kwamba, watakapoupata watakuwa na unafuu wa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kulingana na mawazo yameibuliwa, mambo ambayo hutendeka katika jamii hayakidhi matamanio na matarajio hayo. Kwa sababu, jamii

ilitaka kuutokomeza ufukara, ufisadi na utawala wa kimabavu. Uhalisi unaobainika katika mataifa hayo ni kwamba, hali iliyokuwepo wakati wa ukoloni-mkongwe bado imeendelezwa na imewakereketa kupitia kwa mfumo mwingine wa ukoloni-mamboleo. Hata hivyo, mshairi ameona kuwa hivi sasa hali ya maisha ni duni lakini uhalisi huo hautaua matarajio ya msingi waliyokuwa nayo. Kilichobainishwa ni kwamba, matumaini au ndoto ya jamii haitatimilika kupitia kwa kizazi cha sasa bali kupitia kwa kizazi kipya au kijacho kitakachokuwa kimejengwa kwa misingi ya uzalendo inayotarajiwa kuleta maendeleo na ustawi katika jamii. Katika uwasilishaji wa mawazo, kumetumiwa kauli na mbinu mbalimbali za msingi zilizojengana na zilizokamilishana katika uwasilishaji wa shairi.

5.2.1.1 Matumizi ya Kauli au Matini za makusudi kama Kichocheo cha Utunzi na Uwasilishaji

Kimsingi, mtunzi wa shairi hili ana ujumbe mahususi ambao anauwasilisha kulingana na mchomo wa hisi aliyonayo. Kwa hivyo, kumeteuliwa kauli mahususi kuwa msingi wa kuibulia, kusawiria na kuwasilishia mawazo au ujumbe. Hiyo ndiyo sababu ya kutumiwa kauli ya *Hatujaaga Ndoto* kuwa anwani. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, matumizi ya anwani, shairi hupata mwelekeo wa kuibulia kauli msingi katika kusawiri na kufaragua hoja mbalimbali zilizowiana katika harakati za kubainishia ujumbe ambao huwasilishwa (Fowler 1966). Baada ya kupata anwani hiyo, mshairi hapotezi muda bali ameingia moja kwa moja katika ufaraguzi wa maswala ya msingi ambayo mshairi amekabiliana nayo, kama vile:

- Ndoto msingi ya wanajamii ilikuwa ipi katika kipindi cha kupigania uhuru wao?

- Wakati wa sasa ambapo uhuru umepatikana, ndoto hiyo imetimilika au la?
- Ni harakati gani huhitajika ili kufikia malengo ya ndoto hiyo ya awali katika jamii?

Maswali kama hayo ndiyo yamesaidia katika kujenga msingi wa kuibulia vitushi au matukio katika utungo. Kwa mfano, mataifa ya Afrika Mashariki Kenya ikiwemo, yaling'ang'ania uhuru wao kwa matarajio ya: kuutokomeza ufukara, ujinga na ufisadi. Kutokana na maelezo yaliyotolewa, ndoto ya mataifa hayo bado haijatimilika hata baada ya kupata uhuru wa kisiasa. Ujumbe huo pia hupatikana katika baadhi ya mashairi ya Kiswahili kama vile: katika shairi la 'Vinyago' (Mazrui 1988:30) na 'Mnazi: Vuta N'kuvute' (Abdalla 1973:17). Washairi hao hawaoni mwafaka wowote kutokana na uhuru uliopatikana katika jamii. Katika kuendeleza zaidi wazo hilo lililohusu maisha ya baada ya ukoloni, mshairi amekariri kuwa:

- *Uhalisi mwekundu*
  Unaotisha macho
- *Meno ya ufukara*
  Yanararua watoto
- *Kichaa cha ufisadi*
  Kimesambaa kote
- *Bretton Woods na wenza*
  Wanatunyonya damu (Ubeti wa 4)

Katika muktadha wa kauli hizo, kumeweza kubainisha *ndoto* au matarajio ya jamii ilikuwa ni kujenga utu, maelewano mema na kuimarisha chumi zao. Hata hivyo, mwafaka huo haujafikiwa. Kwa sababu, dhiki katika jamii ni zile zile zilizokuwepo wakati wa ukoloni na tiba bado haijapatikana. Kama ilivyoelezwa, watawala au walio kalia kwenye enzi wameidhikisha jamii, kwa vile:

Wametuzungusha seng'enge
Kama mateka wa vita (Ubeti wa 4)

Kwa hivyo, kupitia kwa kauli hiyo, mshairi amebainisha muktadha wa dhiki ambazo hukumba jamii wakati huu wa sasa. Kimsingi, hiyo siyo *ndoto* ambayo iliwapa wanajamii msukumo wa kupigania uhuru wao. Kwa sababu, jamii za Afrika Mashariki hususa, Kenya hazikutarajia kujiopoa na kujizika katika shimo la dhiki. Kutokana na hayo, mshairi ameweza kuibua kauli zingine za msingi katika kufafanulia zaidi mawazo. Ili kukariri ujumbe huo uliowasilishwa na pia kuubainishia msimamo wake, amesema:

Sisi watoto wa Afrika
Tumekataa kuaga ndoto
Ewe ndoto ya dhahabu
Ndoto ya kesho (Ubeti wa 4)

Kutokana na dondoo hilo, imedhihirishwa kwa sauti ya shime kwamba: bado mapambano huendelea ili kukabiliana na mfumo ambo unaowadhulumu na unaowanyanyasa katika jamii. Mshairi ametumia dhana ya *dhahabu* kama njia ya kuisifu *ndoto* hiyo ya jamii. Kwa hivyo, mshairi ana matarajio kuwa, ndoto hiyo italimilika wakati wa baadaye, ambapo:

Mamba wanaoota jua
Juu ya mazuka mekundu
Watakuwa hadithi (Ubeti wa 4-5)

Katika muktadha huo, *ndoto* ya wanajamii itafikiwa wakati watawala ambao huuendeleza mfumo wa ukoloni-mamboleo watakapokataliwa kwa dhati katika jamii. Katika jamii hiyo mpya, *teknolojia* ya kisayansi itatumika kuwa msingi wa kuleta na kuendeleza chumi za bara la Afrika. Kutokana na hayo, *watoto wa Afrika* watapata lishe bora na

dhiki za magonjwa zitatokomezwa katika kaburi la sahau. Katika kuendeleza mwafaka huo imekaririwa kuwa:

Watoto watatembea vijijini
Bila kutafunwa njiani
Na ukambi au kifaduro (Ubeti wa 5)

Kwa sababu ya mwafaka huo wa amani na utulivu unaotarajiwa katika jamii, wana wa Afrika watapata fursa ya kunoa, kuendeleza fikra, mwelekeo na maarifa yao. Kauli hizo zimebainisha kwamba, hali hiyo itakapozumbuliwa na itakapoimarishwa, ndipo jamii za Afrika huweza kusema kuwa maono au matarajio yao yamefikiwa na zimepiga makasia ya maendeleo.

Aidha, mataifa hayo yataweza kuimarisha mbinu zinazotumika katika kilimo cha sasa. Kwa sababu, nguzo kuu katika mataifa hayo hutegemea kilimo ingawa mapato yake yamekuwa ni duni miaka nenda, miaka rudi. Isitoshe, mshairi ameendeleza mawazo kuhusu *ndoto* tarajiwa kwa kukariri kuwa jamii za Afrika huhitaji kujenga maendeleo katika misingi ya utamaduni wake na pia kupuuzilia mbali uelekezi wa mambo kupitia kwa kioo cha mataifa nyanyasaji ya kigeni. Kwa ambavyo mshairi ametaka kuuhitimisha utungo huo na kwa kujenga uelekezo zaidi, imetumiwa kauli ifuatayo:

Tutupe katika pipa la taka
Huu mkebe, ambao
Kwa aibu inayonuka
Tunazungusha duniani
Tukiomba makombo (Ubeti wa 5)

Kulingana na kauli ambazo zimezitumiwa katika uwasilishaji, ameweza kuibua na kubainisha kwa ubunifu masuala nyeti katika jamii. Kwamba, *ndoto* tarajiwa

itakapotimilika, mataifa ya Afrika yataweza kujiondolea aibu ya kuombaomba au kujidhalilisha kwa kujijengea ngome imara ya kiuchumi na kujitegemea. Kimsingi, hilo ndilo ombi na matarajio ya mshairi katika jamii yake.

5.2.1.2 Matumizi ya Kauli za Kibinafsi kama Mbinu ya Kuundia Taswira na Isitiari

Katika utunzi, mshairi ameunda taswira na isitiari kama mbinu ya kuibushia na kuwasilishia mawazo. Kwa mfano, alipotumia anwani ya *Hatutaaga ndoto*, tayari hadhira yake imeweza kutunga taswira ya kimaono kuhusu mawazo yanayotarajiwa kuwasilishwa kiubunifu. Kutokana na kauli za kibinafsi zilizotumika kwa makusudi, hadhira huweza hujiingiza katika utafakari wa kijumla kuhusu swala la *ndoto* inayotarajiwa. Kwa mfano, baada ya kutafakari taswira iliyoundwa, hadhira huweza kujiuliza kwa usaili, kwamba:

- Kwa nini mshairi pamoja na jamii hupania kuwa haiko tayari kuididimiza *ndoto* yao ya awali?

Ni kutokana na uelekezo wa anwani iliyotumika ndipo mshairi ameingia moja kwa moja katika harakati ya kudhihirisha mwelekeo wa *ndoto* hiyo. Kauli za awali ambazo zimetumiwa, zimebainisha mawazo kuwa:

Uhalisi mwekundu
Unaotisha macho
Na kubabaisha fahamu
Kama jinamizi la manane (Ubeti wa 4)

Kwa kuzingatia kauli katika dondoo hilo, mshairi ameubainisha zaidi uhalisi wa maisha katika mataifa ya Afrika. Kwamba, *uhalisi mwekundu* unaoshuhudiwa katika mataifa huru ya Afrika. Kwa ambavyo huo ni *uhalisi mwekundu* ameashiria hatari au hali mbaya

ambayo imetamakani katika jamii inayosawiriwa. Kwa hivyo, huo si uhalisi ambao ulitarajiwa kujenga msingi wa *ndoto* ya jamii. Vilevile, mambo ambayo hutendeka katika jamii ya sasa hayakujengwa katika minimili ya utu. Katika kuendeleza mawazo kitaswira na kiisitiari, imeelezwa kuwa:

Meno ya ufukara
Yanararua watoto
Kama mbwa-mwitu
Yakirarua kondoo (Ubeti wa 4)

Kauli hizo zimewasilisha dhiki ambazo huzikumba jamii za Afrika. Hata hivyo, mshairi haoni kuwa mwafaka wa ndoto yao itafutika. Kwa sababu, hapo mwanzoni katika harakati za kupigania uhuru wao walikuwa na malengo dhabiti ambapo uhalisi wa mambo umeubeua msingi wa *ndoto* yao. Kupitia kwa kauli hizo, hadhira huweza kuunda taswira ya kimaono kuhusu namna jamii hizo zilivyodhikika kutokana na *ufukara* ulioshamiri.

Kadhalika, mshairi huitarajia hadhira kuchukulia taswira hiyo iliyoundwa kuwa msingi wa utafakari wa ujumbe unaowasilishwa kiisitiari. Dhana za kiisitiari ni kama *meno ya ufukara* na *mbwa-mwitu* anayerarua *kondoo*. Kauli hizo zimetumiwa ili kuipa hadhira vidokezi vya utafakari kwa kuufananisha mkereketo wa *ufukara* na jinsi *mbwa-mwitu* anavyoshambulia na anavyowararua kondoo wasiokuwa na hatia. Isitoshe, mshairi amebainisha kwa uwazi kuathirika kwa jamii ambao hutokana na kutofahamu au kutozinduka kwao. Ili kuikoleza zaidi hoja iliyowasilishwa, imeibuliwa kwa makusudi kauli kwamba:

Sumu ya kutojua
Imefunika vijiji

Kama ukungu wa moshi
Kwenye njia ya msafiri (Ubeti wa 4)

Katika muktadha wa dondoo hilo, imeundwa picha ya watu ambao si wafahamu wa uhalisi wa mambo. Kutokana na dhana ya *sumu*, hadhira huweza kutafakari zaidi ili kuelewa athari ya ujinga katika jamii iliyosawiriwa. Ni katika kuzingatia zaidi 'sumu' hiyo, hadhira huweza kufahamu zaidi kuhusu ujumbe wa ndani uliokusudiwa katika shairi. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, dhana za kiisitiari kama vile inavyobainika katika matumizi ya methali huwa ni kichocheo cha ufasiri wa ujumbe batini unaowasilishwa (Trench 2003 na Akporobaro 1994). Zaidi ya hayo, imeelezwa hoja kuhusu ukithiri wa ufisadi ambao huendelezwa katika mataifa machanga ya Afrika katika muktadha wa mfumo wa ukoloni-mamboleo. Ingawa haijaelezwa kwa uwazi kuhusu mataifa hayo nyonyaji, kauli zilizotumiwa zimewasilisha hoja hiyo lakini kwa kuzingatia taswira na sitiari zilizoibuliwa. Kwa mfano, imeelezwa kuwa:

Bretton Woods na wenza
Wanatunyonya damu
Mithili kupe milioni
Na hao mazimwi wajeuri
Waliokalia kwenye enzi
Wanatuzungusha seng'enge
Kama mateka wa vita (Ubeti wa 4)

Kupitia kwa ubeti huo, amewasilisha taswira ya vikundi viwili vya wadhalimu: utawala unaotumia nguvu kutoka nje na pia utawala wa ndani wa mtu mweusi. Hata hivyo, ujumbe ambao umewaslishwa huweza kufafanuliwa kwa kuzingatia dhana za kiisitiari zilizotumiwa katika shairi.

Kwa mfano, mawakala wa mashirika ya *Bretton Woods* wamelinyanyasa bara la Afrika kupitia kwa vikwazo vya kiuchumi ambavyo huwekewa matafa 'yanayoendelea'. Kadhalika, mawakala hao pamoja na watawala wa mataifa 'yaliyoendelea' wamefananishwa na *mazimwi wajeuri.* Katika akili ya msomaji, picha ambayo imeundwa ni ile ya kukatisha tamaa iliyotokana na tawala hizo mbili. Katika muktadha huo, hadhira huweza kuibua hisi za huruma kwa jamii husawiriwa na msanii (Senkoro 1987). Kulingana na mawazo yaliyosawiriwa, mataifa hayo hayawezi katu kupiga hatua za maendeleo kutokana na msukumo kutoka nje na ndani. Kwa sababu, jasho lao hufaidi mataifa bepari ilihali uchumi wao umedhibitiwa na *mazimwi waliokalia kwenye enzi.* Kwa hivyo, kupitia kwa kauli zilizotumika, mshairi ameweza kuijengea hadhira vipengele vya kiisitiari ambavyo huweza kubainishwa na kufasiriwa vyema kupitia kwa utamaduni na uhalisi wa maisha katika jamii.

Kadhalika, viongozi waliosawiriwa katika shairi wamekuwa vikwazo vya ustawi na maendeleo katika jamii hizo. Kimsingi, watawala hao dhalimu huwazugazuga wanajamii ili kuugubika uhalisi huo. Kutokana na isitiari iliyoibuliwa, wanajamii wamekuwa kama *mateka wa vita* ambao hawana uhuru wowote. Hiyo siyo *ndoto* ambayo ilitarajiwa na wanajamii. Kwa hivyo, mshairi hajasita kuisifu *ndoto* ya msingi kuwa ni, *ndoto ya dhahabu.* Kiisitiari, *ndoto* au matamanio ya jamii yalikuwa yenye thamani kubwa. Hiyo ndiyo sababu ya kuimithilishwa kwa *ndoto* yao na *dhahabu.* Katika muktadha huo, hadhira hupata mwelekeo wa kuufasiri ujumbe ambao umewasilishwa. Katika hali hiyo, mshairi ameusawiri na ameuwasilisha uhalisi wa kisiasa katika jamii za sasa za Afrika, kwa kusema:

Mamba wanaoota juu
Juu ya mazulia mekundu
Watakuwa hadithi (Ubeti wa 4-5)

Kutokana na dondoo hilo, hadhira huweza kujenga taswira ya viongozi dhalimu ambao hustarehe kwa uwezo na mali waliyoihodhi kwa udanganyifu katika jamii. Hata hivyo, mshairi ana maono kwamba; starehe hizo zitawatoka puani pindi ndoto ya ujenzi wa jamii mpya haitatengenea. Dhana ya 'Mamba' kama taashira ya uongozi wa kimabavu imetumika pia katika shairi la 'Mamba' (Abdalla 1993:10). Katika shairi, msanii ameweza kusawiri starehe na hawa za baadhi ya viongozi katika wakati wa sasa. Kadhalika, katika shairi la 'Hatujaaga Ndoto' dhana ya *mamba wanaoota juu* imedhihirishwa kitaswira, namna viongozi hao wamejichukulia kuwa wamefikia kilele cha ufanisi. Kwa hivyo, matarajio ya ndoto ya maendeleo katika jamii imeelezwa kitaswira:

Teknolojia ya kilimo
Itabusu mashamba
Yazae kiazi kikuu
Kikubwa kuliko Afrika (Ubeti wa 5)

Katika muktadha wa dondoo hilo, kumetumiwa dhana au kauli ambazo zimeibulia tamathali ya tashihisi kama vile, *itabusu na yazae*. Dhana hizo zimejenga mazingira ya kuuwasilisha ujumbe kitaswira na kiisitiari. Kwa sababu, msomaji anapozingatia dhana zilizotumika hujiingiza katika kuupatanisha ujumbe ulioibushwa na uhalisi wa utamaduni wa jamii. Vile vile, katika kuhimisha ujumbe uliohusu ujenzi wa jamii mpya, mtunzi ameisihi jamii kuwa:

Tutupe katika pipa la taka
Huu mkebe, ambao
Tunauzungusha duniani
Tukiomba makombo (Ubeti wa 5)

Kwa kuzingatia kauli zilizotumiwa, mshairi ameweza kuukoleza zaidi ujumbe unaowasilishwa kiisitiari. Kwa mfano, kama mwanafalsafa na mzalendo, huisihi jamii kuwa iwapo inahitaji kupiga hatua za kamaendeleo inahitaji kutupa *Huu mkebe* ambao umekuwa ukitumiwa kuomba *makombo* kutoka kwa mataifa nyonyaji au 'yaliyostawi'. Ingawa ameweza kuchora taswira halisi ya utegemezi wa mataifa 'yanayoendelea', kimsingi hadhira hupata vidokezi vya kuufasiria isitiari zilizotumika katika ujumbe unaowasilishwa. Kutokana na isitiari iliyoundwa na kupitia kwa kauli zilizotumiwa ni kwamba, ili ukoloni-mamboleo na sura zake kuweza kutokomezwa katika kaburi la sahau, hubidi mataifa hayo ya Afrika kujitegemea badala ya kujiingiza katika uombaji wa misaada ambao inaudhalilisha utu, heshima na maendeleo ya kiuchumi katika jamii hizo. Baada ya mwafaka huo kupatikana, *ndoto* hiyo itatimilika na mataifa hayo yataweza kujivunia uhuru wa dhati.

5.2.1.3 Ujenzi wa Muundo, Mahadhi na Ridhimu Kutokana na Matumizi ya Kauli za Makusudi

Shairi hili ni refu na limewasilisha ujumbe unaohusu harakati za ujenzi wa jamii mpya. Ujumbe umesawirishwa na umewasilishwa kupitia kwa kauli za makusudi. Kauli ambazo zilizoteuliwa, zilitumiwa ili kuufanya utungo kuwa wenye muundo uliodhibitiwa kwa ridhimu na mahadhi. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, uwasilishaji wa utungo hupaswa kuzingatia mbinu za usimulizi. Kwa kufanya hivyo, utungo huwa huburudisha na wakati uo huo huwasilisha ujumbe ulikusudiwa katika shairi (Parry 1971).

Matumizi ya kauli hizo yametamalaki katika shairi zima. Kwa mfano, mstari wa kwanza na wa pili huwa umeshirikiana katika kuwasilishia hoja mahususi imesaidia katika kudhihirishia uhalisi wa mambo ambayo hutendeka katika jamii ya sasa. Aidha, mshairi ametumia viakifishi mbalimbali kuwa dira ya kuongoza katika usomaji wa shairi. Kwa kufanya hivyo, usomaji wa shairi umekuwa wenye mwendo na mahadhi yaliyotarajiwa. Kwa hivyo, mstari wa kwanza unapozingatiwa bila ya kuhusisha mstari wa pili, hoja hiyo iliyowasilishwa huwa haijakamilika. Kadhalika, shairi hilo limezingatia mtindo wa umithilishaji kuwa mbinu ya kuukariri ujumbe au hoja zilizowasilishwa.

Isitoshe, mbinu hizo zimesaidia zaidi kujenga na kuibulia ridhimu mahususi zilizohitajika katika uwasilishaji wa shairi. Kwa mfano, katika uwasilishaji wa utungo mshairi ametumia kauli zifuatazo:

- *Na kubabaisha fahamu*
  Kama jinamizi la manane
- *Imefunika vijiji*
  Kama ukungu au moshi
- *Kimesambaa kote*
  Mithili viini vya kichocho
- *Wanatunyonya damu*
  Mithili kupe milioni
- *Wametuzungusha sengenge*
  Kama mateka wa vita (Ubeti wa 4-5)

Kupitia kwa kauli ambazo zimepigiwa mstari, mshairi ameweza siyo tu kudhihirisha ukamilifu wa hoja ambazo zimewasilishwa bali pia kuhakikisha kuwa mahadhi na muundo mahususi umedumishwa.

Mbinu hiyo ya umithilishaji hubainika pia katika mtumizi ya methali katika mawasiliano watu na pia katika tungo za kifasihi. Kwa hivyo, mstari wa kwanza unaposomwa, hadhira huelewa kuwa kauli hiyo haijakamilika. Vile vile hadhira hupata fursa ya kutua au kupumua kidogo kabla ya kufululiza au kuingilia mistari inaofuata unaoanza kwa: *kama* au *mithili*. Kadhalika, mistari hiyo miwili imechangiana na imekamilishana katika ubainishaji na uwasilishaji wa ujumbe kuhusu uhalisi wa mfumo wa ukoloni-mamboleo. Katika muktadha huo, mshairi pia amejijengea mwanya wa kufafanua harakati mbalimbali ambazo hupaswa kuzingatiwa ili *ndoto* ya ujenzi wa jamii mpya kuweza kutimilika. Kutokana na mtindo huo, shairi limekuwa na muundo wa aya moja lakini lenye kushirikisha hoja au mawazo ya aina mbili. Ili kutekeleza mradi huo, ametumia kwa makusudi neno *Bali*. Kimsingi, neno hilo limetumiwa kiusanii ili kutenganisha na kushirikisha dhana mbili za hoja zilizokinzana katika uwasilishaji wa utungo.

Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, utungo huweza kuwa wenye hoja mbalimbali zenye uhitaji wa ushikamano wa matini katika uwasilishaji wavyo (Lindfors 1977 na Liyong 1972). Jambo hilo hudhihirika zaidi katika uwasilishaji wa ushairi simulizi. Katika ushairi andishi, mtunzi hubainisha matumizi hayo kupitia kwa maneno teule ambayo hujitokeza mwanzoni mwa kauli msingi katika ubeti. Katika muktadha huo, hadhira inaposoma kauli na kufikia pale ambapo neno teule lilipotumika. Kadhalika, hadhira hujengewa mazingira ya kupunguza kasi na kuweza kutua zaidi kabla ya kuingilia hoja au mawazo ya aina ya pili ambayo yamewasilishwa. Katika uwasilishaji wa mawazo au hoja mpya, mshairi amedumisha kiusanii mahadhi na ridhimu. Kwa hivyo, kunakuwa na ushikamano wa mawazo na uwasilishaji wa kimantiki. Zaidi ya

hayo, mshairi ametumia kauli nyingine ambayo ni ngeni ili kushikamanisha mawazo yaliyoibushwa. Kauli hiyo ni, *kesho ambapo* imekuwa kuwa mbinu ya kuibulia mahadhi na kuidhibiti zaidi hadhira kama ifuatavyo:

- *Kesho ambapo*
  Mamba wanaoota jua
  Juu ya mazulia mekundu
  Watakuwa hadithi
- *Kesho ambapo*
  Maktaba na maabara
  Zitamulika mabonde
  Na vilima vya Afrika
- *Kesho ambapo*
  Watoto watatembea vijijini
  Bila kutafunwa njiani
  Na ukambi au kifaduro
- *Kesho ambapo*
  Watoto watakweza akili
  Hadi vilele vya mikalatusi
  Bila kuvutwa chini na ufukara
- *Kesho ambapo*
  Teknolojia ya kilimo
  Itabusu mashamba
  Yazae kiazi-kikuu
  Kikubwa kuliko Afrika (Ubeti wa 4-5)

Katika muktadha huo, kauli ya *kesho ambapo* ni ya msingi wa kuelekeza usomaji wa shairi. Kwa sababu, msomaji hutarajiwa kusoma kauli hiyo kwa sauti ya juu na kwa msisitizo zaidi kuliko kauli za kimaelezo zilizofuatia. Kadhalika, kauli hizo zimesaidia katika kumwelekeza zaidi msomaji katika kuzingatia kiini cha ujumbe uliowasilishwa.

Vile vile, kauli hizo za makusudi zimeendelezwa kwa herufi kubwa mwanzoni mwa kila mstari isipokuwa pale jina mahususi la *Afrika* linaporejelewa. Matumizi ya herufi kubwa mwanzoni mwa mistari pia ni muhimu katika kuibulia mahadhi na ridhimu tarajiwa. Msanii ametumia herufi kubwa ili kuelekeza zaidi usomaji wa shairi. Kinyume na utunzi

wa ushairi wa kimapokeo ambapo huzingatia zaidi idadi maalumu ya mizani na vina, utunzi na uwasilishaji wa ushairi huru hupata uelekezi wa kimahadhi na kiridhimu kutokana na matumizi ya kauli teule na alama za uakifishaji. Katika msingi huo, shairi haliwezi kusomwa vinginevyo pasi na kuboronga mahadhi.

Kadhalika, mshairi ametumia alama mbili za uakifishaji katika uwasilishaji wa shairi hili ambazo ni kituo [,] na kikomo [.]. Ishara hizo za uakifishaji zina mchango muhimu katika uelekezaji wa usomaji. Kwa mfano, kituo kimetumiwa kwa makusudi ili kutenga hoja kuu na maelezo yaliyotolewa. Isitoshe alama ya kikomo imetumiwa mara moja tu kuwa ishara ya kumfahamisha msomaji kuwa huo ndiyo mwisho wa shairi.

5.2.2. Shairi: Bara Jingine

Shairi hili ni miongoni mwa tungo ndefu zinazopatikana katika diwani ya *Bara Jingine* na limegawinyika katika sehemu nne za msingi. Kadhalika, anwani ya shairi hili ni kama ile iliyopewa diwani hii ya *Bara Jingine*. Katika shairi hili, mshairi amebainisha zaidi ndoto na matamanio ya jamii mpya. Kwa sababu hiyo, mataifa ya sasa katika Afrika yatafikia kilele cha ufanisi. Kulingana na maono yaliyozingatiwa katika shairi ni kwamba, ufanisi wa mataifa hayo hautatokani kupitia kwa na kizazi cha sasa bali kupitia kwa kizazi kipya ambacho kitakuwa na mwelekeo tofauti na ule unaodhihirika au ule unaoshuhudiwa wakati wa sasa. Katika uwasilishaji wa hoja au mawazo, msanii ametumia miundo mbalimbali za lugha kama ilivyobainishwa.

5.2.2.1 Matumizi ya Kauli za Kibinafsi kama Msingi wa Kuibua, Kusawiri na Kuwasilisha Ujumbe Kuhusu Ujenzi wa Jamii Mpya

Katika shairi hili, mshairi amefafanua na ameendeleza swala la ujenzi wa jamii mpya kama ilivyodokezwa hapo mwanzoni kwenye shairi la *Hatutaaga Ndoto*. Kwa hivyo, amepitisha ujumbe kwamba, *Bara* la sasa litapisha kuundwa kwa *Bara Jingine*. Kutokana na mwelekeo huo, amelipa shairi hili anwani ya *Bara Jingine*. Kwa uelekezo wa anwani, ameweza kuzua kauli za makusudi ili kufafanulia ujumbe kuhusu ndoto ya *Bara Jingine* kama ilivyobainishwa hapa:

Ndoto yangu
Ni tamu
Kama asali,
Kijani
Kama majani ya mtango
Angavu
Kama jua la asubuhi (Ubeti wa 10)

Kauli ambazo zimepatikana katika dondoo hilo, zimeteuliwa na zimetumiwa kwa makusudi ili kubainishia maono kuhusu sifa ambazo hutarajiwa kuwepo katika *bara jingine*. Kupitia kwa kauli hizo, bara hilo tarajiwa litakuwa ni 'pepo' kwa jamii. Aidha, mshairi ameweza kuibulia mifano mbalimbali ambayo imesaidia katika usawiri wa *bara* hilo. Kwa mfano amesema:

- *Bunge*
  Halitakuwa ukumbi
  Wa genge la nzige
  Munga
  Wa kupigia yowe katadole
  Jukwaa
  La vikaragosi bila sura
- *"Usalama wa taifa"*
  Hautakuwa ngozi
  Ya kulinda mamba wa ikulu
  Bakora

Ya kudumisha miungu - wa - kinamo
Vizuizi
Na jela
Haziakua vinu
Vya kusagia utu
Mlango
Wa kuingia kaburini (Ubeti wa 10-11)

Katika muktadha dondoo hilo, mshairi ameweza kutumia kwa makusudi kauli za kibinafsi kuwa njia ya kuibulia na kuwasilishia ujumbe kuhusu maswala ya kisiasa katika jamii. Sawia na Kezilahabi katika mashairi ya 'Kuchambua Mchele' na 'Hadithi ya Mzee' ambayo hupatikana katika diwani ya *Kichomi* (1974: 63 na 69-72 mtawalia), mshairi ameitaka jamii iwe macho katika kuwatambua wahujumu wa uchumi na maendeleo. Kadhalika, msanii ameuona mfumo huo wa utawala katika jamii ambapo umeshirikisha viongozi ambao wamelifanya bara hili kuwa *nyumbani* au mbuga:

Ambamo nyati
Amekumbwa na ghadhabu
Mbwa-mwitu
Wanateketezwa na kichaa
Swila
Amefurisha shingo (Ubeti wa 11)

Muktadha uliojengwa kupitia kauli hizo zilizotumika, bara hilo si pahali pema pa kuishi wala hakuna usalama wowote. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, kauli zilizotumika katika tungo za kishairi ni za kitaashira na kiisitiari ambapo huhitaji kufasiriwa kwa kuzingatia utamaduni na mazingira ya jamii (Mutembei 2001 na Buhler 1985). Kwa sababu, baadhi ya viongozi hujifanya miungu ya kuwanyanyasa na kuwatatiza watu katika nyanja zote za maisha. Kulingana na maono ya mshairi kupitia kwa kauli zliizotumiwa, katika *bara jingine* hapatakuwa na ubinafsi wala ufisadi uliokithiri katika jamii ya sasa. Hiyo ndiyo sababu ya kubainishwa kuwa:

- *Ulafi*
  Na ufisadi
  Hazitanyesha kutoka juu
- *Urongo rasmi*
  Hautapaa angani
- *Ubaguzi wa kikabila*
  Hautakuwa ukungu
- *Katika ikulu*
  Hakutapinda mamba
  Bali kuketi binadamu
  Watu wenye damu
  Na fahamu (Ubeti wa 11-12)

Kufikia hatua hiyo, hadhira imejengewa muktadha wa kufahamu matarajio ya msanii kuhusu masuala ya kisiasa na kijamii katika bara hilo jingine. Kadhalika, katika sehemu ya II ya shairi, imebainishwa zaidi kuhusu umuhimu wa *sayansi* na *teknolojia* katika bara hilo jingine. Kwamba, *bara* hilo litakuwa lenye:

- *Teknolojia ya habari*
  Haitabakia juu angani
  Mbali na mkono wetu
  Bali itakuwa kurunzi kiganjani
  Ya kumulikia njia ya safari
- *Cheche za sayansi*
  Zitahimizwa
  Hadi ziwe mwako
  Mche wa teknolojia
  Utapaliliwa
  Hadi uwe gogo la mti
- *Utafiti wetu*
  Utakuwa makombora
  Dhidi ya malaria na ukambi
  Vifaru dhidi ya sotoka na baka
- *Wakulima*
  Wataimba nyimbo
  ...
  Kusifia kwa ukunjufu
  Siyo majani chai na kakao
  Siyo kahawa na tumbako
  Bali viazi
  Vikubwa kuliko njaa
  Mbaazi

Zitakuwa bila kinyongo
Mboga na matunda
- *Na jua na mito*

...
Wimbo wa umeme
Wa kuendesha mitambo
...
Na kumulika nyumba (Ubeti wa 12-13)

Kutokana na madondoo hayo, imebainishwa zaidi kuhusu umuhimu wa utendakazi wa *sayansi* na *teknolojia* ambao hutarajiwa kushuhudiwa katika bara hilo jingine. Kwa hivyo, katika sehemu ya III ya shairi, imeangaziwa maswala kuhusu ushirikiano na utangamano unaotarajiwa kuwepo katika bara hilo. Ili kushadidia zaidi hoja, imeibuliwa kauli za makusudi kwamba:

Badala ya harufu
Cameroon na Nigeria
Wakirushiana uzushi,
Badala ya miguno
Kenya na Tanzania
Wakitafunana neva,
Badala ya vitivo
Ethiopia na Eritrea
Wakikaangana jangwani,
Barabara na reli
Zitavuka mipaka
Kama mishipa ya damu
...
Barua na simu
Zitafika kijiji
Bila kupitia London
Bila kwenda Paris,
Noti za benki
Hazitageuka karatasi
Bara ambapo
Johari za utafiti
Zenye rangi ya Afrika,
Bidhaa za viwandani
Zenye nembo ya Afrika,
Zitapitana njiani
Kama pistoni
Zikiendesha mitambo. (Ubeti wa 14-15)

Katika dondoo hilo, mshairi amelipa mwelekeo shairi kwa uzingativu wa kauli zilizopigiwa mstari. Kupitia kwa kauli hizo, msomaji amejengewa vipengele muhimu ambavyo ni ishara mwafaka ya kuupokea ujumbe uliowasilishwa. Kwa hivyo, uadui na tuhuma miongoni mataifa hazitakuwepo tena katika bara hilo jingine.

Baada ya kubainisha ushirikiano utakavyoendelezwa, imejengwa mazingira ya uthamini wa utamanduni wa mwafrika katika bara hilo jingine. Kwa sababu hiyo, zimetumiwa kauli za kuelekeza katika sehemu ya IV kuwa:

- *Ngozi nyeusi*
  Itakuwa dhahabu
  Katika macho ya akili
- *Lugha za Kiafrika*
  Zitakuwa wimbo wa nyonza
  Katika masikio
- *Sanaa ya Mwafrika*
  Itakuwa dira
  Katika jahazi la utamaduni,
- *Shughuli kuu*
  Haitakuwa utafutaji mbinu
  Za kukaza vizuri fundo
  Katika tanzi hatari
  La kamba ya Bretton Woods
  Bali kutengeneza tupa
  Ya kukata minyororo
  Inayotufunga miguuni
  Katika barabara ya maisha (Ubeti wa 15-16)

Katika kauli hizo, mtunzi amekamilisha uwasilishaji wa ujumbe kuhusu ujenzi wa jamii mpya ambao umetarajiwa. Endapo mambo hayo yamezingatiwa kwa dhati, ndoto ya jamii kuhusu *bara jingine* itakuwa imetimilika.

5.2.2.2 Ujenzi wa Taswira na Isitiari Kutokana na Kauli za makusudi Zilizotumika

Katika shairi hili, mtunzi ametumia taswira na isitiari kuwa msingi wa kuusawiri na kuuwasilisha ujumbe. Kutokana na yale ambayo hutendeka wakati huu wa sasa katika mataifa mbalimbali ya Afrika, haoni kama matarajio ya jamii yametimilika. Kwa sababu hiyo, ndoto kuu ya mwafrika huweza kutengenea katika *bara jingine* ambalo si la kizazi cha sasa. Ili kuwasilisha ujumbe wake wa kimaono, mshairi amejenga taswira na isitiari zilizoweza kufafanulia na kufasiria hoja zilizoibuliwa kwa kuzingatia uhalisi wa maisha ya jamii za Afrika.

Kwa kutumia anwani ya *Bara Jingine*, msanii ameweza kujenga taswira ya kijumla kuhusu jamii nyingine ya kidhahania. Kwamba, wakati wa sasa pana bara halisi ambalo silo alilolishughulikia bali matarajio hayo yamejikita katika *bara jingine*. Hiyo ndiyo sababu ya kuundwa kwa kauli:

> *Ndoto yangu*
> *Ni tamu*
> *Kama asali* (Ubeti wa 10)

Katika dondoo hilo, mshairi ametumia kauli ya *asali* ambayo huichochea akili ya hadhira kuibulia taswira ya kuonja na kimaono kwa umithilishaji. Kadhalika, hadhira huweza kufasiri utamu huo kuwa ni mwafaka au manufaa ambayo jamii hutarajiwa kuupata pindi *ndoto* hiyo itakapotimilika. Kutokana na mantiki hiyo, ameingia moja kwa moja kufaragua ujumbe kwa kuibua kauli ambazo zina mwelekeo wa kuibulia ndoto aliyonayo kuhusu *bara jipya*, kwamba:

- *Bunge,*
  Halitakuwa ukumbi
  Wa genge la nzige,

- *"Usalama wa taifa"*
  Halitakuwa ngozi
  Ya kulinda mamba wa ikulu,
- *Vizuizi*
  Na jela
  Hazitakuwa vinu
  Vya kusagia utu
  Mlango
  Wa kuingia kaburini,
- *Akili azizi*
  Hazitashtuka
  Na kuangusha vifaa (Ubeti wa 10-11)

Kupitia kwa kauli hizo zilizopigiwa mstari, mshairi ameweza kuibainisha na kuiwasilisha ujumbe wake kitaswira na kiisitiari. Katika muktadha huo, hadhira huweza kuuona kwa uwazi mfumo dhalimu wa utawala katika bara hilo jingine litakavyoshughulikiwa na wenye mielekeo ya uzalendo. Kwa mfano, dhima ya *bunge*, *jela* na *akili* ya jamii zitakuwa zimejengwa katika misingi iliyothamini utu.

Kadhalika, mshairi ametumia taashira mahususi kama vile: *genge la nzige*, *mamba wa ikulu*, *jela hazitakuwa vinu vya kusagia utu.* Kwa kuzingatia kauli hizo zilizoibuliwa, hadhira inachochewa kupiga bongo ili taashira hizo kuweza kufafanuliwa na kupatanishwa na uhalisi wa maisha ya jamii (Buchbinder 1991). Kwa hivyo, hadhira huweza kufahamikiwa kuwa viongozi watakaopata nyadhifa katika *bara jingine* wataihudumia jamii kwa kuzingatia misingi ya uzalendo, amani, ukarimu na utu. Katika harakati hizo za ufafanuzi zaidi wa ujumbe, amesema:

- *Kwani majumbani*
  Kumegeuka mbuga
- *Ambamo nyati*
  Amekumbwa na ghadhabu,
- *Mbwa-mwitu*
  Wanateketezwa na kichaa,

- *Swila amefurisha shingo* (Ubeti wa 11)

Katika muktadha wa kauli zilizotumiwa, hadhira huweza kuunda taswira ya kimaono kuhusu bara hili la Afrika katika kipindi cha sasa. Kwa mfano, mshairi amejenga taswira ya mataifa ya Afrika kuwa *mbuga* ambamo kuna *nyati mwenye ghadhabu, mbwa-mwitu mwenye kichaa* na *swila* ambaye amejitayarisha kutema sumu. Mazingira ambayo yamesawiriwa, yamejenga picha ambayo ni ya hatari kubwa kwa waliomo ndani ya nyumba au waliomo katika mataifa hayo ya Afrika. Hali hiyo pia imebainishwa katika shairi la 'Joho la Maisha' (Mvungi 1986:31-32), amesema:

Shamba akilifilisi, na jingine atapewa,
Yeye hakosi nafasi, wenzake wanamjuwa,
Je, wanyonge wanahisi? nani anayewajuwa?
Shamba hili nalisema, ni mfano maridhawa

Shairi hilo limejenga mazingira ambayo ni ya kukatisha tamaa katika mataifa ya sasa barani Afrika ambapo pana maongozi yaziyofaa.

Kimsingi, ujumbe uliofumbwa kupitia kwa dhana za isitiari hizo unahusu vurugu ambalo husababishwa na viongozi wa kisiasa kwa wakati uliopo. Kwa ambavyo mtunzi hana upeo wa kutathmini uwezo wa kiuchambuzi na kiufasiri wa hadhira, ametoa maelezo yaliyowasilishwa kupitia kwa taswira na isitiari zilizoundwa kwa makusudi. Taswira na isitiari ambazo zimejengwa katika utungo ni zile zilizotokana na tajiriba za jamii (Imbosa 1990 na Chacha 1987). Kwa hivyo, kauli ambazo zimeundwa baadaye ni za kufafanulia uhalisi wa maisha katika bara hilo jingine, kwamba:

- *Ulafi*
  Na ufisadi
  Hazitanyesha kutoka juu
  Kama sumu

Ikinyunyizwa kutoka helikopta,

- *Urongo hautapita angani*
  Kama uzishi wa nyegere,
- *Ubaguzi wa kikabila*
  Hautakuwa ukungu
  Unaoshambulia macho
- *Katika mamba*
  Bali kuketi binadamu
  Watu wenye damu
  Na fahamu (Ubeti wa 11-12)

Kutokana na kauli hizo zilizojengwa kupitia kwa tamathali za usemi kama vile tashihisi, uhuishaji na tashbihi, zimesaidia kuwasilisha maelezo ya kijuujuu ambayo ni msingi wa kuelewa ujumbe fiche uliowasilishwa.

Katika sehemu ya II, mshairi ametumia kauli za makusudi kuwa kifariji au kitulizo cha moyo kwa hadhira. Kwamba, katika bara hilo jingine taaluma ya sayansi na *teknolojia* itakuwa imedhibitiwa kwa manufaa ya jamii. Kwa hivyo, imedhihirishwa kuwa:

- *Teknolojia ya habari*
  Haitabakia juu angani
  Mbali na mkono wetu
  Bali itakuwa kurunzi kiganjani
  Ya kumulikia njia ya safari
- *Ugunduzi wetu*
  Utakuwa makombora
  Dhidi ya malaria na ukambi
  Vifaru
  Dhidi ya sotoka na baka
- *Wakulima*
  Wataimba nyimbo
  Washairi
  Watakariri mashairi
  Kusifia kwa ukunjufu
  Siyo tu majani-chai na kakao
  Siyo kahawa na tumbako
  Bali viazi –
  Vikubwa kuliko njaa,
  Mbaazi
  Zinazokuwa bila kinyongo

Mboga na matunda
Yanayozomea adui shambani – (Ubeti wa 12-13)

Katika muktadha huo, hoja hizo zimebainishwa na kuwasilishwa kwa kuzingatia dhana za kitaswira na kiisitiari. Kupitia kwa kauli hizo, hadhira huweza kutunga picha mahususi zilizohusu manufaa ya utendakazi wa teknolojia ya kisayansi katika jamii hiyo mpya ambayo imetarajiwa.

Katika sehemu ya III, mshairi amewasilisha mafanikio yanayotarajiwa kutokana na harakati za jamii kuhusu ndoto ya *Bara jingine*. Kwa hivyo, ametumia dhana au kauli za kibinafsi katika kulisifu bara hilo jingine. Kwa mfano, amesema kuwa:

- *Nyota unayemwesamwesa*
  Katika majira ya gizagiza,
- *Kupitia kwa huu moshi*
  Wa moto wa ufukara
- *Kupitia hili wingu*
  La sumu ya utengano,
  Nakuita kwa sauti thabiti
  Njoo ewe bara jipya
- *Badala ya harufu*
  Cameroon na Nigeria
  Wakurushiana uzushi,
  Badala ya miguno
  Kenya na Tanzania
  Wakitafunana neva
- *Barabara na reli*
  Zitavuka mipaka
  Kama mishipa ya damu
- *Barua na simu*
  Zitafika kijiji jirani
  Bila kupitia London
  Bila kwenda Paris,
- *Johari za utafiti*
  Zenye rangi ya Afrika,
  Bidhaa za viwandani
  Zenye nembo za Afrika,
  Zitapitana njiani

Kama pistoni
Zinazoendesha mitambo (Ubeti wa 14-15)

Katika muktadha wa madondoo hayo, imefafanuliwa namna jamii zitakavyoshirikiana ili kuinua maendeleo na hadhi ya bara hilo tarajiwa. Kwa uelekezo wa nadharia ya Semiotiki, kauli ambazo hujenga taswira, huufanya ujumbe wa ndani kuweza kuwasilishwa na kufasiriwa kwa kuzichukulia dhana au kauli hizo kuwa ni vipengele muhimu vya kubainishia isitiari zilizoundwa katika shairi.

Kadhalika, mshairi huenda ameona kuwa taswira aliyoijenga katika sehemu hizo tatu kwenye shairi bado haijakamilika. Kwa hivyo, ameingia katika sehemu ya IV kwa kutumia kauli ambazo zimechangia katika uwasilishaji wa *ndoto* ambayo ni maono ya jamii. Kauli zilizotumika huweza kufasirika kwa kuhusisha vipengele mahususiambavyo hupatikana katika utamaduni wa jamii. Kauli hizo zilizotumika katika uwasilishaji wa ujumbe, ni kama zifuatazo:

- *Ngozi nyeusi*
  Itakuwa dhahabu
  Katika macho ya akili,
- *Lugha ya Kiafrika*
  Zitakuwa wimbo wa nyonza
  Katika masikio,
- *Sanaa ya mwafrika*
  Itakuwa dira
  Katika jahazi la utamaduni,
- *Shughuli kuu*
  Haitakuwa utafutaji mbinu
  Za kukaza vizuri fundo
  Katika tanzi hatari
  La kamba ya Bretton Woods
  Bali kutengeneza tupa
  Ya kukata minyororo
  Inayotufunga miguuni
  Katika barabara ya maisha (Ubeti wa 15-16)

Dhana au kauli zilizopigiwa mstari zimetumiwa kuumulia na kuwasilishia ujumbe kitaswira na kiisitiari. Kwa hivyo, mshairi amejijengea mwanya wa kuubainisha zaidi ujumbe siyo tu kwa kuzingatia maelezo bali pia kupitia taswira na isitiari zilizoundwa.

5.2.2.3 Kauli za Kibinafsi kama Msingi wa Kuibulia na Kubainishia Itikadi ya Mshairi

Katika shairi hili, mshairi amesawiri matukio mbalimbali yanayoshuhudiwa katika jamii za Afrika wakati wa sasa, ambapo jamii hizo zimejitawala baada ya uhuru. Ujumbe unaowasilishwa umejikita katika utathmini wa kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na umuhimu wa *teknolojia* ya sayansi katika jamii hizo. Katika muktadha huo, mawazo yaliyoibuliwa ni kwamba, bara la wakati huu wa sasa limeshindwa kufikia malengo ya *ndoto* yao kuu. Kwa hivyo, mshairi ameuona mwafaka huo kama unaoweza kupatikana katika *bara jingine*. Kadhalika, shairi limepewa anwani ya *Bara Jingine* kuwa msingi wa kujengea na kuwasilishia mawazo. Vile vile, katika kutanguliza uwasilishaji wa mawazo hayo, amesema:

> *Ndoto yangu*
> *Ni tamu*
> *Kama asali,* (Ubeti wa 10)

Kupitia kwa kauli hiyo, mshairi amedokezea mwelekeo wake kuhusu bara hili la sasa kwamba, hana imani nalo. Kwa hivyo, ndoto inayohusu ujenzi wa *bara jingine* ni kuwa, *bara* hili la sasa limeshindwa katika kufikia maazimio ya msingi yaliyojenga ari na hamasa za kuiondoa himaya ya mkoloni. Katika muktadha huo, mshairi amedhihirisha maono yake kuhusu *bara* hilo *jingine*.

Kwa kutumia nafsi ya kwanza katika *ndoto yangu* humbainikia msomaji kwamba, ujumbe uliowasilishwa umejikita katika mchomo na hisi za mshairi. Hata hivyo, hana nia ya kutoa maelezo ya kina yaliyohusiana na bara la sasa. Kwa sababu, huenda msomaji huyaelewa matatizo yaliyopo kwa ambavyo mpokezi huyashuhudia matizo yaliyopo katika jamii. Kwa hivyo, mshairi ameanza moja kwa moja kwa kujenga taswira ya kukatisha tamaa kuhusu mfumo wa utawala katika jamii hizo za Afrika. Katika mazingira hayo, ametongolewa kuwa:

Bunge
Haliktakuwa ukumbi
Wa genge la nzige (Ubeti wa 10)
Bara ambapo
Ngozi nyeusi
Itakuwa dhahabu (Ubeti wa 15)

Zaidi ya dhana au maneno yaliyotumika, itikadi na mwelekeo wa mshairi umeendelezwa kupitia kwa kauli za kitashibihi ambapo hoja fulani hutumiwa kuwa msingi wa umithilishaji. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mshairi huusawiri utungo kwa kuzingatia tajiriba na hisi alizonazo (Propp 1968 na Nagler 1967). Kwa hivyo, huweza kuishawishi hadhira kwa ubunifu ili ikubali yale ambayo yamewasilishwa. Matumizi ya kauli za nafsi ya kwanza ambazo zimetapakaa na zimejitokeza katika shairi, zimeibua na kuukoleza zaidi mwelekeo wa mshairi. Kwa mfano, imetumiwa kauli kama vile:

Utafiti <u>wetu</u>
Ugunduzi <u>wetu</u> (Ubeti wa 12)

Katika dondoo hilo kumetumiwa kauli za nafsi ya tatu. Amefanya hivyo kwa makusudi ili kuyakinisha zaidi namna jamii hizo zitakavyonufaika katika *bara* hilo *jingine*. Katika muktadha huo, huitaka hadhira itathmini jinsi bara la sasa lilivyoshindwa katika kufikia

matarajio au *ndoto* iliyokuwepo. Kwa hivyo mshairi amelisherehekea bara hilo, kwa kukariri kuwa:

Wakulima
Wataimba nyimbo
Washairi
Watakariri mashairi (Ubeti wa 13)

Katika sehemu ya III mshairi ametumia kauli ambazo ni za kulisifu zaidi *bara* hilo *jingine*. Kauli hizo zilizotumiwa ni za uhuishaji ambapo amelisheheneza sifa kwa kulisifu bara hilo *jipya,* kwa kusema:

Ewe bara jipya
Nyota inayomwesa mwesa
Katika majira ya gizagiza (Ubeti wa 14)

Katika muktadha wa dondoo hilo, mshairi amekariri hisi na mwelekeo alionao kuhusu *bara* hilo. Matumaini ya *ndoto* hiyo, yamedhihirishwa kupitia kwa kauli ambazo zimetapakaa katika sehemu ya IV. Hiyo ndiyo sababu ya kutumiwa kwa kauli kuwa:

- *Nakulilia, ewe bara jingine*
  Bara ambapo
  Ngozi nyeusi
  Itakuwa dhahabu
- *Lugha za Kiafrika*
  Zitakuwa nyimbo za nyonza
- *Sanaa ya Mwafrika*
  Itakuwa dira
  Katika jahazi la utamaduni (Ubeti wa 15)

Kulingana na kauli hizo mahususi, wakati utafika ambapo *bara* hilo litajiri. Hata hivyo, mshairi ana maono kwamba hakuna njia nyingine ya kufikia mwafaka huo isipokuwa pale ambapo jamii itazinduka na kuelewa kiini cha dhiki zilizopo. Katika uwasilishaji wa shairi limesheheni kauli za makusudi au za kibinafsi ambazo kwa pamoja

zimebainisha zaidi mwelekeo wa mshairi kuhusu bara lililopo na matamanio ambayo huhusu *bara jingine* lililowasilishwa.

5.2.2.4 Mbinu ya Usambamba kama Msingi wa Kuukoleza Uwasilishaji wa Ujumbe

Katika uwasilishaji, mawazo ya mshairi yamepata mwelekeo na yamebainishwa kupitia kwa uundaji wa usambamba katika utungo. Katika kuisifu na kuisheheneza ndoto hiyo, mshairi hatosheki kuwasilisha mawazo ya msingi kwa kauli aumiundo ya aina moja ya lugha. Kwa hivyo katika ufafanuzi wa hoja zilizowasilishwa, amesema:

- *Ndoto yangu*
  Ni tamu
  Kama asali
- *Kijani*
  Kama majani ya mtango
- *Angavu*
  Kama jua la asubuhi
- *Pendezi*
  Kama bustani ya mawaridi, (Ubeti wa 10)

Katika madondoo hayo, mshairi amejenga dhana moja ya msingi kuhusu *ndoto* yake. Kauli za makusudi zilizozitumiwa zimekaribiana kimaana lakini zimetofautiana kimuundo. Kwamba, ndoto hiyo *tamu, kijani, angavu* na *pendezi*. Hapa ieleweke kuwa, takriri hiyo ya maneno imetumiwa kwa makusudi ili kuwa msingi wa kuukoleza na kuuendeleza zaidi ujumbe kwa namna tofauti tofauti.

Kadhalika, matumizi tofauti ya uwasilishaji huifanya hadhira isichoke katika udurusu wa shairi na pia kuwa mbinu ya kuukariri ujumbe uliowasilishwa. Isitoshe, dhana hizo zilizoibuliwa huwa bayana katika muktadha wa sentensi au kauli za kitashibiha zilizotumika. Mshairi pia ametumia maneno ambayo yana maana tofauti ambayo

yamesaidia katika kushadidia mawazo yaliyowasilishwa kwa mizungu tofauti tofauti. Kwa mfano, ametumia ishara au dhana kama vile: *Bunge, unga, jukwaa, bakora, vizuizi,* na *mlango*. Kwa mujibu wa nadharia ya Semiotiki, dhana au kauli teule ambazo hutumika, huhitaji ufafanuzi uliojikita katika tajiriba za watu (Wamitila 1999). Kimsingi, dhana hizo zimetumiwa ili kuchochea na kuchangia uumuaji wa mawazo kuhusu taasisi dhalimu zilizopo katika Afrika ya sasa. Mawazo hayo yamejitokeza zaidi kupitia kwa kauli teule za kitaashira, kama vile:

Kwani nyumbani
Kumegeuka mbuga
Ambamo nyati
Amekumbwa na ghadhabu,
Mbwa-mwitu
Wanatekelezwa na kichaa,
Swila
Amefurisha shingo (Ubeti wa 11)

Kupitia kwa taashira ya wanyama wa mbugani ambao ni hatari, mshairi ameweza kujenga taswira na isitiari, kwa uelekezo wa usambamba ulioibuliwa. Wanyama hao hatari ni *nyati, mbwa-mwitu* na *swila*. Kama ilivyoelezwa hapo awali, dhana hizo zimesaidia katika kujenga na kuendeleza swala moja la msingi kuwa: bara Afrika la sasa si pahali pema pa kuishi kwani kumejaa nakama chungu nzima. Kwa hivyo, mshairi ana maono kwamba, *ikulu* ya bara hilo jingine:

Hatutapinda mamba
Bali kuketi binadamu,
Watu wenye damu
Na fahamu (Ubeti wa 11-12)

Zaidi ya hayo, katika sehemu ya II ya utungo, mshairi ametumia kauli ambazo zimewasilisha utendakazi wa *teknolojia* ya sayansi katika bara hilo tarajiwa kuwa:

KENYATTA UNIVERSITY LIBR

- *Teknolojia ya habari*
  Haitabakia juu angani
- *Bali itakuwa kurunzi kiganjani*
  Ya kumulikia njia ya safari
- *Mche wa teknolojia*
  Utapaliliwa
  Hadi uwe gogola mti
- *Utafiti wetu*
  Ugunduzi wetu
  Utakuwa makombora
  Dhidi ya malaria na ukambi (Ubeti wa 12)

Katika muktadha wa madondoo hayo, msanii ametumia kauli za kiusambamba ili kufafanulia zaidi mambo ambayo huweza kutekelezwa kupitia mbinu za sasa ambazo hutokana na *teknolojia* ya sayansi. Katika kuufafanua zaidi ujumbe kuhusu athari ya *teknolojia* ya sayansi katika jamii hiyo mpya, imekaririwa kuwa:

- *Siyo majani-chai na kakao*
  Siyo kahawa na tumbako
- *Bali vianzi –*
  Vikubwa kuliko njaa
  Mbaazi
  Zinazokua bila kinyongo,
  Mboga na matunda
  Yanayozomea adui shambani
- *Akili na mikomo*
  Zitakutana haraka
  Na jua na mito
  Na kwa mahadhi matamu
  Kuimba wimbo adhimu
  Wimbo wa umeme
  Wa kuendeshea mitambo
  Na ndoto,
  Ya kumulika nyumba (Ubeti wa 13)

Kwa kuzingatia kauli katika madondoo hayo, mtunzi ameweza kupanga na kuwasilisha hoja kimantiki na kwa udhahiri zaidi. Aidha, ameangazia *ndoto* yake kuwa bara hilo: *jipya* litakuwa limejengwa katika misingi ya amani, utangamano na matumaini makubwa. Ili kuyakinisha mawazo hayo, ametoa mifano ambayo huibulia utuvu na ushirikiano

katika mataifa ya Kiafrika. Kulingana na mawazo hayo, mataifa ya Afrika hayapigi hatua za kimaendeleo kutokana na uhasimu uliokithiri. Mataifa hayo, ni kama vile *Cameroon* na *Nigeria*, *Kenya* na *Tanzania*, *Ethiopia* na *Eritrea*. Maono zaidi kuhusu *bara jipya* au *jingine* ni kwamba, mataifa hayo huhitaji ushirikiano wa kijamii badala ya kujenga chuki miongoni mwao. Kimsingi, mataifa hayo yamejenga *bara* moja na huhitaji kushirikiana na kuoneana imani kama jamii moja ya Afrika.

Aidha, kutokana na tuhuma miongoni mwao, mawasiliano baina ya taifa na taifa hupitia *London* na *Paris*. Kwa hivyo, imekaririwa zaidi kuhusu uzingativu wa uzalendo na utamaduni wa Mwafrika, kwamba:

- *Ngozi nyeusi*
  Itakuwa dhahabu
- *Lugha za Kiafrika*
  Zitakuwa wimbo wa nyonza
- *Sanaa ya Mwafrika*
  Itakuwa dira
- *Shughuli kuu*
  Haitakuwa utafutaji mbinu
  Za kukaza vizuri fundo
  Katika tanzi hatari
  La kamba ya Bretton Woods
  Bali kutengeneza tupa
  Ya kukata minyororo
  Iliyotufunga miguuni
  Katika barabara ya maisha (Ubeti wa 15-16)

Katika uwasilishaji wa hoja kuhusu ndoto ya *bara jingine*, mshairi ameibua kauli mbalimbali ili kuukariria zaidi ujumbe huo. Kimsingi, ukariri huo hauendelezwi kwa mdundo mmoja. Kupitia kwa usambamba, dhana na mawazo yaliyoibuliwa, huwa ni kunga za kuukoleza zaidi ujumbe uliowasilishwa. Aidha usambamba uliotumika, umeutilia nguvu uwasilishaji wa ujumbe katika shairi.

5.2.2.5 Ujenzi wa Muundo, Mahadhi na Ridhimu Kutokana na Uelekezo wa Viakifishi

Katika usawiri na uwasilishaji wa shairi hili, mtunzi ametumia viakifishi kuwa mbinu ya kuibulia na kujengea muundo, mahadhi na ridhimu. Kama vile ilivyokwisha kuelezwa hapo awali, shairi hilo ni refu lakini mshairi amewasilisha ujumbe uliozingatiwa katika awamu nne: I, II, III na IV. Kwa kufanya hivyo, shairi limepata umbo na muundo maalumu.

Kadhalika, mshairi ameweza kuibulia hoja nne ambazo ni tofauti lakini zimechangiana na zimekamilishana katika uwasilishaji wa shauiri. Kwa hivyo, kila hoja imeshughulikiwa katika sehemu maalumu ili kukidhi dhamira ya mtunzi. Zaidi ya kuligawanya shairi hilo, ametumia ukariri wa baadhi ya kauli teule ili utungo uweze kusomeka kwa mahadhi na ridhimu iliyokusudiwa. Kauli zilizotumika ni zile ambazo hupatikana katika ufunguzi au dibaji ya kila sehemu husika, kama vile:

- *Ndoto yangu*
  Ni tamu [I]
- *Kama chozi*
  Juu ya ua [II]
- *Ewe bara jipya*
  Nyota inayomwesamwesa [III]
- *Nakulilia, ewe bara jingine* [IV]

Ingawa mshairi ametumia kauli hizo kujengea mazingira ya ufunguzi, zimetumiwa pia kama mbinu ya kulipa shairi mahadhi na ridhimu katika usomaji wake. Kwa sababu hadhira inapolisoma, huweza kupata fursa ya kupumua au kutua kidogo inapofikia mwishoni mwa kila sehemu kabla ya kutumia pumzi nyingi katika kauli za kutanguliza sehemu au hoja nyingine mpya. Mifano iliyotumiwa ni kama vile:

- *Ndoto ya bara jipya* (Ubeti wa 10)
  Bara ambapo (Ubeti wa 10)
- *"Usalama wa taifa"* (Ubeti wa 10)
- *Juu ya bara jipya* (Ubeti wa 12)
- *Njoo, ewe bara jipya* (Ubeti wa 14)

Katika uwasilishaji wa shairi, kauli zimekaririwa mno siyo kwa sababu ya ukosefu wa msamiati bali kuwa mbinu ya kujengea muundo na kuufanya utungo huu uweze kudumisha mahadhi yaliyotarajiwa. Kwa kuzitumia, usomaji huwa umedhibitiwa kwa uelekezo wa mshairi. Aidha, tashibihi zilizobuliwa na zimetumiwa ili mawazo yaliyowasilishwa kuweza kujenga utaratibu maalumu katika uwasiliashaji. Katika muktadha huo, kumetumiwa kiunganishi *kama* kuwa chanzo katika mishororo au kauli msingi kwenye utungo. Matumizi mahususi ya neno *kama* yamekithiri mno katika sehemu ya I, II na III. Mahadhi katika sehemu ya IV yameweza kudumishwa kupitia kwa tashihisi iliyoibuliwa katika shairi. Mifano iliyotumiwa, ni kama vile:

- *Ngozi nyeusi*
  Itakuwa dhahabu
- *Lugha za Kiafrika*
  Zitakuwa wimbo wa nyonza
- *Sanaa ya mwafrika*
  Itakuwa dira
  Katika jahazi la utamaduni, (Ubeti wa 15)

Kadhalika, muundo na mwendo katika shairi umechochewa kupitia kwa kushirikisha matumizi mbalimbali ya viakifishi. Kwa hivyo, msomaji anapolisoma shairi hukumbana na ishara za uakifishi kama [,], [" "], [.] na matumizi ya herufi kubwa mwanzoni mwa kila mshororo. Kwa mfano, msomaji anapokutana na ishara ya [,] hutambua kuwa, ni sharti apunguze kidogo kasi katika usomaji wake. Mwendo wa usomaji hugeuka pindi anapokumbana na ishara ya [.] ambapo husaidia siyo tu kujenga mazingira ya mtuo zaidi bali pia kutambua kuwa shairi limefikia kitengo maalumu.

Kwa ambavyo muundo wa shairi umegawanyika katika sehemu nne za msingi, hitimisho la kila kifungu limedhibitiwa kwa kituo [.]. Kimsingi, utungo umetumia mara nne kiakifishi cha kituo. Kimetumiwa mahususi kumwelekeza msomaji kuwa kuna vifungu vinne katika uwasilishaji wa shairi. Vile vile, mshairi ametumia ishara ya kufungua na kufunga usemi [“ ”] kwa lengo la kuelekeza zaidi kuwa huo ni unukuzi wa kauli za watu wengine au pengine huonyesha kutokubaliana kwake na hoja hiyo inayowasilishwa. Kwa hivyo, msomaji hutarajiwa kusoma kauli hizo kwa uelekezi uliokusudiwa. Kwa ujumla, matumizi ya kauli na kwa ushirika wa vipengele vya uakifishaji husaidia katika kuibua na kudumisha muundo na mahadhi katika shairi.

5.2.3. Shairi: Mruko wa Nyuki

Katika shairi hili, mshairi amebainisha namna utangamano, uchumi na utamaduni asilia wa jamii ulivyovurugwa kutokana na maajilio ya utawala wa kikoloni. Wakoloni hao walipofika katika barani Afrika, walitaka kunyakua na kujitajirisha kutokana na rasilimali waliyoikuta (Rodney 1989). Matokeo ya mfumo huo wa utawala, ulisambaratisha uchumi na kuiyumbisha zaidi jamii kimaisha. Kabla ya maajilio ya wageni hao, wenyeji walikuwa wakiishi kwa ushirika, amani na upendo, lakini kuwepo kwa wageni kuliutingisha na kuuathiri mwafaka huo. Kwa sababu, baadhi ya wanajamii waliukubali na kuuvaa utamaduni na kuuendeleza mfumo huo katika jamii. Hata hivyo, baadhi ya wanajamii ambao walikuwa na cheche za uzalendo walihamasishana kwa malengo ya kujenga umoja kwa kuzingatia misingi ya utamaduni wao.

Kwa ambavyo baadhi ya wanajamii tayari walikuwa wameukubali utamaduni wa kigeni, jitihada hizo zikigota pingamizi. Ni baada ya wanajamii kukubaliana kushirikiana kimwelekeo na kimaono, ndipo walipoweza kuwatimua wakoloni na kupiga makasia ya kimaendeleo katika jamii. Kulingana na mawazo yaliyoibuliwa katika shairi: umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. Katika muktadha wa shairi, kumetumiwa kauli na miundo mbalimbali ya lugha katika uwasilishaji kama ilivyodhihirishwa hapa.

5.2.3.1 Ufumbaji na Ufumbuaji wa Fumbo kwa Kuzingatia Mwangwi wa Methali

Katika uwasilishaji wa shairi, mshairi hakutumia kwa uwazi methali yoyote mahususi. Hata hivyo, mawazo yaliyoibuliwa yameweza kupata uelekezi kutokana na urejeleaji wa methali zilizopo katika mawasiliano ya jamii. Baada ya kuhitimisha usomaji au udurusu wa utungo ndipo msomaji huweza kubaini kwa ujumla mawazo yaliyoibuliwa.

Kimsingi, mawazo hayo huweza kupata mshabaha wake kupitia kwa methali sufufu zinazotumika katika mawasiliano ya jamii. Hata hivyo, ieleweke kuwa hadhira huweza kujenga mtazamo wao kwa uelekezo wa mwangwi wa methali. Katika muktadha huo, hadhira huweza kutumia methali mahususi ili kujenga muhtasari wa ujumbe uliowasilishwa. Kwa mfano, msomaji anapolipitia shairi hugundua kuwa *nyuki* (au wanajamii) wamevurugiwa amani na hivyo, wameamua kuruka au kupaa angani. Kwa hivyo, maisha yao hayapati mwelekeo mmoja kwa sababu kila mmoja ameandama njia yake. Matokeo ni kwamba, mihimili ya jamii iliathirika na iliporomoka. Kwa sababu, kila mmoja hakuweza kushirikiana na mwenziwe katika utafutaji wa *tiba ya safari*.

Hata hivyo, baada ya kushindwa kupata mwafaka huo uliotokana na ubinafsi wao, jamii iligundua kuwa: 'umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu'. Ingawa mshairi hakutaja au hakutumia methali ambayo imerejelewa, mawazo yaliyowasilishwa katika shairi husadifu busara inayoibuliwa. Katika ufasiri wa mawazo yaliyoibuliwa, uelekezo wa methali ni muhimu. Ni katika hatua hiyo ndipo hadhira hufahamikiwa kuwa *nyuki,* (au jamii ya Afrika) hawakuweza kupata mwafaka huo kwa kuendekeza ubinafsi kama ilivyodhihirishwa kwa taswira iliyoundwa na kupitia kwa maelezo yafuatayo:

Njia
Moja

iliingia *kulia*
nyingine *ikapitia*
kushoto *baadhi*
yetu *tulisafiria*
kushoto *wengine*
walifuata *kulia* (Ubeti wa 23)

Katika msingi wa taswira iliyoundwa, utafakari na upokezi wa ujumbe katika shairi huweza kufikiwa kwa mwafaka zaidi. Kwa hivyo, mshairi ameuwasilisha ujumbe katika taswira na kuiachia hadhira kutafuta methali au tamathali ya usemi ambayo huweza kupatanishwa moja kwa moja na ujumbe huu mahususi. Katika muktadha wa nadharia ya Semiotiki, ujumbe huweza kuwasilishwa kupitia kwa kauli msingi ambazo ni tofauti tofauti. Kadhalika kauli hizo, huweza kujenga taswira ya kimono (Akporobaro 2001). Kwa kufanya hivyo, mshairi hana dhamira wowote wa kutumia methali kwa uwazi lakini hiyo si sababu ya msingi ya kushikilia kuwa utungo hunapuuzia umuhimu wa methali.

Kutotumiwa kwa methali kwa uwazi katika mashairi ya Kiswahili, ni mbinu ya chemsha bongo au utafakari ambayo huachiwa hadhira. Katika muktadha huo, ni vyema kutaja

kuwa katika utamaduni wa mawasiliano ya watu, kuna chungu nzima ya methali ambazo huweza kutumiwa kwa uwazi au kujenga mwangwi wa mawazo yanayowasilishwa katika utanzu wowote wa fasihi hususa, ushairi wa Kiswahili. Huenda hiyo ndiyo sababu ya msingi iliyomfanya mshairi kutotumia methali yoyote mahususi katika uwasilishaji wa shairi. Kwa hivyo, kutotumiwa kwa methali haimaanishi kuwa kauli hizo zimepitwa na wakati bali ni mtindo katika mawasiliano ya jamii na pia katika utunzi na uwasilishaji wa tungo za kifasihi. Kadhalika, kutumiwa methali huweza kuwa ni kigezo cha kuuweka ushairi wa Kiswahili katika muktadha wa jamii.

5.2.3.2 Matumizi ya Kauli Teule kama Msingi wa Kusawiri na Kuwasilishia Maadili

Shairi lolote linapotungwa, huwa linawasilisha ujumbe ambao huelekezwa kwa kauli teule zilizotumiwa. Ujumbe huo huwa na lengo la kuielekeza, kuikosoa na kuionya jamii katika muktadha wa uhalisi wa utamaduni mahususi. Kulingana na nadharia ya Fomula ya Kisimulizi na kwa ambavyo ushairi huwasilishiwa jamii, hupaswa kuzingatia kauli ambazo huufumba ujumbe ambao huakisi utamaduni wa watu (Levi-Strauss 1966). Katika mantiki hiyo, shairi la *Mvuko wa Nyuki*, limetumia kauli mahususi ambazo zimegubika na zimewasilisha maadili ambayo hutarajiwa kuiongoa na kuielekeza jamii. Kama ilivyoelezwa hapo awali, ushairi wa kimapokeo na wa kati, maadili hufumbwa na kuwasilishwa kwa uwazi kupitia kwa methali ambazo hupatikana kwa urahisi katika mawasiliano ya jamii.

Kadhalika, maadili katika shairi huweza kuwasilishwa kwa hadhira kwa kuzingatia kauli teule zilizojenga mwangwi wa methali. Kwa hivyo kauli zilizotumika, huwa ni za makusudi ili kuweza kufafanua dhima methali ya kupitishia maadili katika shairi. Kwa mfano, mshairi amewasawiri *nyuki* walivyoruka kutokana na mshutuko wa ghafla. *Nyuki*, kulingana na maelezo yaliyotolewa, ni jamii ya Afrika ambayo *iliarithirika* mno kutokana na maajilio na utamaduni wa ukoloni. Vilevile, imeelezwa kuwa vurugu lililoletwa na wageni liliwapotezea mwelekeo wenyeji wa Afrika kama ilivyotongolewa:

kuvurugwa
na
wageni,
sisi
nyuki
wa
afrika,
tulipitia
nyanda
tata, (Ubeti wa 20)

Katika muktadha wa dondoo hilo, hadhira huweza kupata fununu kuwa amani na utangamano wa jamii husika umesambaratika kutokana na athari zilizoletwa na wageni. Kwa hivyo, umoja na ushirika uliokuwa ukisherehekewa haukuwepo tena. Dhiki iliyoletwa na wageni iliwafanya wanajamii kujiingiza katika *safari* ya kutafuta *tiba* ya matatizo. Katika uwasilishaji wa hoja hiyo, mshairi amesema:

tulikalamua
akili
zikajiri
ndoto
jamala,
ndoto
za
tiba,
tulikakamua
mabawa

ya
safari,
safari
ya
tiba; (Ubeti wa 21)

Kulingana na mshairi, *safari* ya wanajamii ya kutafuta *tiba* haikuandamwa kwa umoja au kwa ushirika. Kwa sababu, wanajamii walikuwa wamegawanyika katika makundi mawili: baadhi yao walifuata mrengo wa kulia na wengine waliandama kushoto. Isitoshe ujumbe unaopitishwa huweza pia kuwasilishwa kupitia kwa methali kama vile: 'Nyumba iliyogawanyika, haiwezi kusimama'. Katika muktadha huo, *safari* ya wanajamii ilikuwa yenye vikwazo vingi vya kimwelekeo katika kufikia malengo ya *ndoto* hiyo.

Aidha, wanajamii walipong'amua kuwa juhudi zao za kibinafsi hazkuifua dafu ndipo waliamua kwa pamoja kuungana ili kuiandama njia moja ya *kulia*. Matokeo ya ushirika huo ndiyo utakaofanikisha ndoto tarajiwa. Mshairi amekariri kuwa:

wakajiunga
na
njia
ya
kulia,
pamoja
kwa
nguvu
za
akili
nguvu
za
misuli
tulijizatiti
na
kufikia
mti
wa
tiba (Ubeti wa 23-24)

Kwa kuzingatia uelekezi wa kauli zilizozitumiwa, mshairi ameweza kupitisha maadili ambayo huielekeza jamii kuhusu dhima ya umoja na utendakazi wake.

Kupitia kwa kauli teule zilizotumiwa, mshairi amepata chombo cha kufundika ujumbe wa kimaadili na kuupitisha kwa hadhira. Kwa hivyo, amekuwa mwalimu mwenye busara katika kuionya, kuishutumu mienendo ya jamii na kutoa mwelekeo unaopaswa kuzingatiwa katika jamii. Katika mantiki hiyo, methali zimekuwazikitekeleza dhima ya msingi ya kuptishia maadili katika jamii kama vile ilivyo katika uwasilishaji wa ushairi wa kimapokeo na wa kati. Katika ushairi huru, dhima yake imesetiwa na imetekelezwa kupitia kwa kauli za kibinafsi ambazo hujenga mwangwi wake katika maudhui yaliyowasilishwa.

5.2.3.3 Ujenzi wa Muundo na Mahadhi Kutokana na Kauli Mahususi Zinazotumika kwa Uelekezo wa Viakifishi

Kupitia kwa uelekezo wa viakifishi, mshairi ameweza kulifanya shairi kuwasilishwa kwa umbo, muundo na mahadhi mahususi. Kauli zilizotumiwa katika shairi zimejenga taswira ya kusambaratika kwa umoja na ushirikiano katika jamii. Kadhalika, jamii baadaye iliamua kuuzika ubinafsi uliokuwepo na kutumikiza ushirikiano.

Katika kuwasilisha hoja hiyo ya ubinafsi na ushirika katika jamii, mshairi ametumia siyo tu kauli mahususi bali pia kuzipanga kwima ili kujenga taswira ya umoja wa wanajamii kabla ya maajilio ya wageni katika makazi hayo. Wageni au wakoloni hao walipofika na kujenga himaya yao katika janibu za bara la Afrika, mambo yaliwaendea segemnege. Hiyo ndiyo sababu ya kudhihirishwa kwa kuporomoka kwa miundo msingi katika jamii.

Kwa uzingativu wa kuporomoka huko, mshairi amejenga utege huo kupitia kwa mpangilio wa silabi za maneno kwenye neno *iliporomoka* kama ilivyodhihirishwa ifuatavyo:

i *po*

li *ro* *ka*

mo (Ubeti wa 23)

Zaidi ya hayo, imebainishwa taswira ya utengano wa wanajamii. Jambo hili limedhibitiwakwa kupanga maneno yaliyounda mistari miwili iliyokando au katika utege ambao umeungana hapo mwanzoni na mwishoni mwa shairi. Isitoshe, mshairi amewasilisha ushirikiano wa wanajamii kwa kupanga kauli au maneno katika upanda wa kulia wa utungo. Sehemu ya kushoto ya upanda huo umeachwa kapa kwa makusudi. Kwa kufanya hivyo, ameweza kutekeleza mambo mawili ya msingi: kutoa maelezo ya ujumbe unaowasilishwa na pia kujenga taswira ya kimaono kuhusu umoja na utengano uliokuwepo katika jamii.

Kimsingi, usomaji wa shairi hutoka kushoto kuenda kulia, kwa hivyo uelekezo huo hauna utata. Kwa kuzingatia mpangilio huo wa maneno, mshairi huisaidia hadhira kuunda picha ya jamii iliyosawiriwa kwa upande mmoja pasi na kuzingatia maelezo yaliyotolewa. Katika muktadha huo, shairi limeweza kupata umbo na muundo maalumu. Kinyume na shairi la Kiswahili lililotumia methali kwa uwazi, umbo na muundo katika utungo umeweza kupata msingi wake kutokana na mjengo wa maneno yaliyotumiwa kwa makusudi.

Katika shairi hilo, muundo hutegemea mpangilio wa maneno kwa kuzingatia taswira ya kimaono inayoibushwa (Zubkova-Bertoncini 2008). Hata hivyo, haimaanishi kuwa methali haziwezi kutumiwa; huweza kutumiwa kiulalo au kiusharazi ili kuibua muundo unaotarajiwa. Hata hivyo hilo hutegemea utashi wa mtunzi na mtindo unaotumika. Kadhalika, msomaji huelekezwa kuzingatia usomaji wa sauti, kimoyomoyo na pia kiutazamaji. Kama ilivyobainishwa hapo awali, silabi za neno *iliporomoka* zimepangwa kiupanguzi ili kudhihirishia mpomoko katika jamii (Gromov 2006). Kwa hivyo, mawazo ya msingi yamewasilishwa kimaono.

Isitoshe, mshairi amekariri kwa makusudi baadhi ya maneno yaliyotumika ili kuibua ridhimu na mahadhi katika shairi. Kwa mfano, amerudia zaidi ya mara moja matumizi ya maneno kama vile: *ndoto, safari, kitambo, panda, matunda* na *jua*. Ukariri huo wa makusudi yameurutubisha utungo kwa namna mbili: kuifanya hadhira kutambua na kuzingatia hoja mpya inayowasilishwa na kujenga mahadhi au ridhimu. Jambo hilo ni la msingi katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi huru wa Kiswahili. Kwamba, utungo huhitaji kuwa wenye mdundo ambao huathiri masikizi ya hadhira kama inavyodhihirika katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi simulizi wa Kiswahili ambao huzingatia au usiozingatia arudhi. Hata hivyo, ushairi huru wa Kiswahili hurutubishwa zaidi kwa kunga ambazo hushirikishwa katika uwasilishaji huo.

Aidha, dhana ya uakifishaji ni ya msingi katika kuelekeza usomaji na pia katika kulipa muundo mahadhi na ridhimu mahususi shairi. Kwa mfano, mtunzi ametumia viakifishi mbalimbali kama vile: koloni [:], kikomo [,], kistari [-], na semi koloni [;]. Katika

uwasilishaji, mshairi hakutumia herufi kubwa au kituo [.]. Herufi kubwa imetumiwa katika kauli ya anwani: *Mruko* na *Nyuki*. Kwa hivyo, msomaji anapolisoma shairi, huweza kumbainikiwa kuwa, utungo huo ni wa sentensi au kauli moja ambayo haijakamilika. Kwa sababu, haina matumizi ya herufi kubwa katika neno la mwanzo au matumizi ya kituo katika hitimisho. Hata hivyo, usomaji wake umedhibitiwa kwa uelekezi wa viakifishi vilivyotumiwa ndani kwa ndani. Katika muktadha huo, shairi huweza kusomwa bila utata kwa kuzingatia mpangilio wa maneno, matumizi mbalimbali ya viakifishi na ukariri wa makusudi wa kauli au maneno. Kwa ujumla, mambo hayo ni ya msingi katika kulipa shairi muundo na mahadhi yaliyokusudiwa.

5.2.4 Shairi: Nakumbuka Ulivyokuwa

Shairi hili limewasilisha dhiki zilizompata mhusika mwanamke ambaye yu mahututi, ingawa anaendelea kupata matibabu. Mwanamke huyo, amejikuta yu katika lindi la dhiki kutokana na msukumo wake wa kibinafsi na ule unaosababishwa na mwanamume. Hapo awali, mwanamke kama mhusika, alikuwa akiishi maisha ya ukata na alipokumbana na mwanamume aliyeukata alizuzuka kwa mali aliyoitarajia kuipata. Kwa hivyo, mwanamke alikubali kuishi na mwanamume bila ya kuelewa fika lengo lake. Mwanamke alipotanabahi alijikuta tayari amefumwa na ameambukizwa maradhi ya Ukimwi. Kimsingi, mwanamume alikuwa *amefunga ndoa* na ana familia iliyoangamia kutokana na maradhi hayo. Kwa hivyo, mhasiriwa amekuwa katika majuta huku akilaani matendo na maamuzi yake ya awali. Katika muktadha huo, mshairi ametumia kauli mbalimbali kuwa msingi wa kuibulia na kuwasilishia ujumbe kama ilivyofafanuliwa.

5.2.4.1 Utunzi Kutokana na Uelekezo wa Anwani na Kauli Teule Zinazoibuliwa Kibinafsi

Kutokana na anwani iliyotumiwa, mshairi ameweza kusawiri na kufafanua zaidi ujumbe unaowasilishwa. Kwa hivyo, anwani ya *Nakumbuka Ulivyokuwa* katika shairi imekuwa ni dira iliyoongoza katika kuteua kauli mbazo zilishirikishwa katika upitishaji wa ujumbe. Katika kutumia kauli hiyo mahususi kuwa anwani, mshairi ameweza kujenga muktadha ambao umesadifu busara ya methali iliyotumika ndani ya shairi. Katika mantiki hiyo, mshairi amefanya uteuzi wa dhana, maneno au kauli kuwa msingi wa kuibulia na kujengea kisa katika shairi. Kwa ustadi, mshairi ametumia kauli kama vile:

- *Mwili dhaifu* (Ubeti wa 1)
- *Alama za sindano*
  za ulishaji wa mpira
  zikikumbusha wembamba (Ubeti wa 1)
- *Ukoko mweupe*
  Ulidhahirisha wazi
  Kwamba eksirei
  Ulikutembelea
  Ili kukujulia hali (Ubeti wa 2)
- *Kabla ya ugunduzi*
  Kukukaba koo (Ubeti wa 3)
- *Kupiga mbizi kali*
  Katika bwawa la huzuni
  Ngozi na mifupa
  Mashaka na dhiki (Ubeti wa 3)
- *Huku matone ya machozi*
  Yakidondoka ndo! Ndo! Ndo! (Ubeti wa 4)
- *Basi matumaini ya pete*
  Yakakulainisha moyo
  Na kukulegeza maungo (Ubeti wa 5)
- *Ukimtembeza*
  Kwenye upinde wa mvua (Ubeti wa 5)
- *Katika chumba cha hospitali*
  Ukirejea taratibu
  Kwenye ukumbi wa maisha
  Katika lango
  La kaburi. (Ubeti wa 5)

Madondoo hayo yamesaidia kujenga muktadha wa ufaraguzi wa ujumbe uliowasilishwa. Hata hivyo, ni muhimu kuelewa kuwa kauli hizo zimeibuliwa kwa uelekezo wa anwani iliyotumiwa na kushadidiwa na methali iliyopo. Kwa mfano, Ukimwi umekuwa ukiendelezwa na baadhi ya wanajamii wasiowajibika au wahasiriwa ambao hutumia kile walichonacho kibindoni kuwa chambo au kivutio cha kuwateka wale ambao wana tajiriba finyu kuhusu uhalisi wa maisha. Kwa mfano, imesawiriwa kuwa mwanamke ambaye hajaolewa aghalabu huwa mwenye:

... *matumaini ya pete* (Ubeti wa 5)

Baada ya kupendekezewa kwa hadaa kuhusu ndoa, baadhi ya wahusika huwa wenye kiwi machoni na kuwafanya wasitambue mbichi wala mbivu hadi pale mambo yalipotumbukia nyongo. Kutokana na kauli ya anwani, ni mwanamke ambaye ameelekezewa kidole cha lawama ambapo sivyo ilivyostahili. Hata hivyo, mshairi ana mtazamo kwamba mwanamume pia hawezi kuepukana na lawama hizo. Kwa sababu, huwa na wajibu wa kutoa tahadhari ya hali yake ya kiafya na pia kuwatahadharisha wenziwe kuwa yu katika kifungo cha ndoa.

Aidha, mshairi ameyakinisha kuwa mwanamke na mwanamume kama watu waliohitaji kuelekezwa kwa hisi za utu katika mahusiano ya kijamii. Kwa hivyo, matatizo yaliyowapata yametokana na mielekeo ya kibinafsi iliyosetirika katika nyoyo zao. Kwa ambavyo anwani imetumiwa katika kuibulia kauli nyinginezo za makusudi au za kibinafsi, ni bayana kuwa mshairi anamsemeza mhusika mwanamke. Kwa wakati huo, yu hospitalini akipata matibabu ya kupunguza makali ya ndwele hiyo.

Katika utungo huo, kuna wahusika wawili ambao wamerejelewa: mwanamke na mwanamume. Mwanamke yu hoi *katika chumba cha hospitali huku akirejea taratibu kwenye ukumbi wa maisha.* Katika muktadha wa kauli hiyo, mshairi ametarajia kumpa mhusika huyo matumaini na kutoa nafasi nyingine ili aweze kurekebisha nyendo zake za awali kwa kuchukua tahadhari kubwa katika kukabiliana na maisha. Kwa sababu, mwanamke alikuwa amefanya kosa hapo mwanzoni lakini kulingana na mshairi, kosa si kosa ila kurudia kosa ni kosa. Isitoshe, usawiri na uwasilishaji wa ujumbe umetokana na anwani pamoja na kauli zingine zilizotumiwa kwa makusudi katika shairi. Kadhalika, mtunzi amemsawiri mwanamume kama kiumbe asiyeweza kutegemewa katika jamii. Kwa mfano, imesawiriwa kuwa:

Katika nyumba ya ambaye
Daima, alipapasa ndoto zako
...
Hadi siku ambapo
Ukweli ulilipuka
Alikuwa na mke
Aliyeozwa kwa arusi
Alikuwa na watoto
Aliopata kwa jasho! (Ubeti wa 5)

Kwa ujumla anwani, ni kauli muhimu ambayo imetumiwa katika kuuelekeza ujumbe uliowasilishwa katika shairi. Kwa hivyo, mtunzi ameirejelea katika kuvyaza kauli za makusudi katika harakati ya kuufaragua ujumbe katika shairi.

5.2.4.2 Ujenzi wa Taswira kama Mbinu ya Kuwasilishia Ujumbe

Mawazo ya mshairi yamewasilishwa kitaswira kupitia kwa tamathali za usemi zilizoundwa, kama vile tashbiha, tashihisi na isitiari. Kimbele ningependa kutaja kuwa, methali kama kauli imetumiwa katika kujengea taswira ya kimaono na kihisi katika

uwasilishaji wa shairi. Aidha, mshairi amemsawiri mwanamke kabla ya kuolewa, wakati ameolewa na maafa au majuto yaliyomwandama.

Katika muktadha huo na kupitia kwa methali iliyotumiwa, msomaji hupata taswira ya mwanamke anayerejelewa. Zaidi ya hayo, kuna kauli zilizoteuliwa na kutumiwa kwa makusudi katika shairi. Fauka ya methali, ametumia kauli ambazo zimechangia katika kumsawiri mwanamke na kuupeleka mbele ujumbe. Kwa mfano, mshauri amesema kuwa:

- *Nakumbuka ulivyokuwa*
  Mwili dhaifu
  Hamu hafifu
  Kama maji ya mtungi
  Ulikuwa tuli
  Katika kitanda,
- *Kwamba eksirei*
  Ilikutembelea
  Ili kukujulia hali
- *Nakumbuka ulivyokuwa*
  Kabla ya ugunduzi
  Kukukaba koo
- *Katika nyumba ya ambaye*
  Daima, alipapasa ndoto zako
  Kwa vidole vya lugha laini
- *Basi matumaini ya pete*
  Yakakulainisha moyo
  Na kukulegeza maungo
  ...
  Ukimtembeza
  Kwenye upinde wa mvua
  Hadi siku ambapo
  Ukweli ulilipuka
- *Nakumbuka ulivyokuwa*
  ...
  Ukirejea taratibu
  Kwenye ukumbi wa maisha
  Katoka langoni
  La kaburi (Ubeti wa 1)

Kwa kutumia kauli zilizopigiwa mistari, mtunzi ameweza kujenga taswira iliyotumika katika uwasilishaji wa mawazo katika shairi. Kwa mfano, imedhihirishwa kuwa mwanamke yu katika kitanda cha hospitali na ametulia kama *maji ya mtungi.* Kwa hivyo, lengo la mtunzi ni kuonyesha kwa uwazi namna mhasiriwa huyo asivyojiweza kwa uwele alio nao. Mgonjwa huyo yupo katika kiwiliwili lakini hana matumaini ya maisha. Vile vile, katika kauli ya *eksirei ilikutembelea ili kukujulia hali* ni kwamba, imeitumiwa kujenga na kuibua tashihisi katika shairi. Kadhalika, mtunzi ameihuisha dhana ya *eksirei* kuwa yenye uwezo wa kutenda jambo. Kwa kuzingatia uelekezo wa kauli hiyo, mshairi ameijengea taswira ya matatizo ambayo husababishwa na Ukimwi au *eksirei* katika jamii. Mshairi ameweza pia kufafanua na kuuwasilisha ujumbe kitaswira kuwa mwanamume aliyemuoa *alipapasa ndoto zako kwa vidole vya lugha laini.* Kimsingi, *vidole* havina uwezo wa kupapasa ndoto bali huweza kuhisika tu. Hata hivyo, nia ya mtunzi ni kuupitisha ujumbe kwa ukamilifu zaidi kupitia kwa taswira iliyoibuliwa kitashihisi.

Katika kudhihirisha hatari kubwa ya mwanamke kumkubali mwanamume katika maisha ya ndoa, ametumia kauli kama vile: *ukimtembeza kwenye upinde wa mvua* na *ukweli ulilipuka.* Kauli hizo kwa pamoja, zimechangia pakubwa katika kubainisha zaidi hatari ambayo imemfuma mwanamke bila ya kutarajia. Hata hivyo, jambo la kufahamisha ni kwamba, mtu habembelezwi katika *upinde wa mvua* wala ukweli hauwezi katu kulipuka ila msanii ameutilia nguvu uwasilishaji ujumbe ili kuweza kuchochea na kufungulia milango ya fahamu.

Katika kuhitimisha taswira aliyoijenga, msanii ameitaka hadhira ipate msingi wa kuelewa fika matatizo yaliyomkumba mwanamke ambaye yu katika hali ya majuto lakini amenusurika kifo na kuendelea kuishi katika *ukumbi wa maisha*. Katika muktadha wa maelezo yaliyojenga taswira, mshairi amebainisha mazingira ya kutambua kuwa mwanamke kama mhusika katika shairi amepewa nafasi nyingine ya kurejea katika uhalisi wa maisha yenye bughudha.

Ingawa msanii ametumia tamathali mbalimbali za usemi katika kujenga taswira, jambo la msingi ambalo limewasilishwa ni onyo kwa hadhira ili iwe yenye hadhari katika kukabiliana na maisha. Kama vile ilivyobainishwa katika sura ya tatu na ya nne, methali ambazo hutumika katika uwasilishaji wa tungo za fasihi huwa ni fani mahususi zinazobainisha maadili kwa kuielekeza jamii katika misingi ya utu (Mlacha 1989). Katika muktadha wa shairi, mtunzi ameitumia methali kama kauli muhimu katika kujenga taswira iliyoshadidiwa kwa kauli nyinginezo ambazo zimeibuliwa na kutumiwa kwa makusudi.

5.2.4.3 Muundo na Mahadhi Kutokana na Kauli za Kibinafsi

Shairi hili limesawiriwa na kuwasilishwa kwa miundo mahususi kupitia kwa kauli zilizobuniwa kibinafsi na kutumiwa kwa makusudi. Hali hiyo ni tofauti na vile ilivyodhihirishwa katika uwasilishaji wa tungo za kimapokeo ambapo muundo wa ushairi hupata uelekezo wa arudhi zinazozingatiwa. Kwa hivyo katika ushairi wa kimapokeo, muundo huweza kuwa bayana kutokana na uwepo wa methali ambazo zimetumiwa katika jamii. Katika utunzi na uwasilishaji wa utungo, mshairi ametumia methali moja:

Majuto ni mjukuu
Huja baadaye (Ubeti wa 4)

Hapa ifahamike kuwa methali hiyo imetumiwa kama mojawapo ya kauli muhimu. Kwa ambavyo imetumika katikati ya shairi, imeweza kuhusishwa zaidi na maudhui yanayoibushwa lakini katika muktadha wa muundo wa shairi ina nafasi ndogo. Mtunzi ameshirikisha kauli nyinginezo kuwa nyenzo ya kujengea muundo katika utungo. Aidha, ametumia ukariri wa kauli kuwa mbinu mojawapo ya kuwasilishia muundo wa shairi. Kwa mfano, ukariri huo umetumiwa katika kubainishia umbo na muundo wa ubeti kama ilivyohusishwa kauli ifuatayo:

Nakumbuka ulivyokuwa (Ubeti wa 3)

Kauli hiyo imetumiwa mwanzoni mwa ubeti kama anwani na pia imekaririwa mara nne katika baadhi ya beti katika shairi. Kwa kufanya hivyo, ameweza kubainisha na kuudhibiti muundo na mpangilio wa vitushi katika utungo. Kwa mfano, ametoa usuli wa ujumbe mpya uliotarajiwa kuwasilishwa kutokana na matumizi ya awali ya kauli hiyo. Baada ya hapo, kauli iyo hiyo imetumiwa kama mbinu ya uelekezaji wa usomaji. Matumizi ya mwisho ya kauli hiyo, yamekuwa ni mbinu ya kuhitimisha uwasilishaji wa mawazo. Kwa hivyo, matumizi hayo yameweza kuashiria mwanzo wa mawazo mapya yaliyowasilishwa katika shairi.

Kadhalika, ametumia ukariri au marudio ya silabi katika neno ili kujenga takiriri au muwala wa kauli zilizotolewa katika shairi. Kwa mfano:

- *Mwili dhaifu*
  Hamu hafifu (Ubeti wa 1)
- *Ukimtumbuiza*
  Ukimbembeleza (Ubeti wa 5)

Maneno hayo yana silabi za mwisho zinazoendelezwa kwa urari au mfumo mmoja. Kimsingi, ameibua urari huo ili kudumisha mahadhi na ridhimu katika baadhi ya aya. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, ukariri wa neno, kauli au silabi si udhaifu wa kiuwasilishaji katika tuno za kifasihi (Parry 1971 na Fowler 1966). Mtindo huo umetumika zaidi katika uwasilishaji wa ushairi unaozingatia arudhi za kimapokeo. Katika uwasilishaji wa utungo, kumetumiwa kwa makusudi kauli au maneno ambayo yamedhihirisha ukinzani wa hoja kama vile:

Kwenye mkono wa kulia
Kwenye mkono wa kushoto (Ubeti wa 1)

Maneno yaliyotumiwa katika kauli hizo, hufanana kimuundo isipokuwa katika maneno tamati kama vile: *kulia* na *kushoto*. Hata hivyo, matumizi hayo yamesaidia katika kujenga mahadhi na ridhimu katika kauli zilizotumika katika muktadha wa uwasilishaji wa shairi. Matumizi hayo ni ya msingi, siyo tu katika kudumisha ujumi wa mahadhi bali pia kama mbinu ya kuwasilishia mawazo katika utungo. Isitoshe, uwasilishaji wa usambamba wa ukinzani umejitokeza pia katika kauli zifuatazo:

- *Yakakulainisha moyo*
  Na kukulegeza maungo
- *Ukimtumbuiza*
  Ukimbembeleza (Ubeti wa 5)

Katika wa dondoo hilo, hoja inayowasilishwa ni moja isipokuwa imeendelezwa kwa muundo wa kauli mbili zilizotofautiana. Kwa kufanya hivyo, mshairi ameupa utungo muundo maalumu kwa mahadhi ambayo yametarajiwa.

Kwa kuzingatia kauli zilizotumiwa, imebainika kuwa mshairi ametenganisha beti kwa kuacha ukapa au uwazi baina ya ubeti mmoja hadi mwingine. Kwa hivyo, utungo una lina beti au kauli tano ambazo hulibainisha umbo la shairi hilo.

Aidha, shairi limejengwa kwa kauli au sentensi moja ndefu. Hata hivyo, ametumia uelekezi wa ishara za uakifishi kuwa msingi wa kujengea muundo unliotarajiwa. Kwa mfano, kistari kidogo [-] kimetumiwa kama mbinu ya kutenganisha au kuunganisha dhana mbili tofauti zenye uwiano. Nayo semi koloni [;] imetumiwa kuunganisha hoja mbili zilizowiana ilihali alama ya kikomo [,] imetumiwa kwa makusudi ili kuashiria hoja inayofafanuliwa kwa maelezo. Katika muktadha wa shairi, ishara hiyo imetumiwa ndani na mwishoni mwa mishororo au mistari. Jambo la msingi ambalo limeelekeza au limetenganisha hoja moja na nyingine ni kutotumia ishara yoyote ya uakifishi bali kuacha uwazi au ukapa baina ya beti zilizopo. Aidha, katika kuibulia na kuwasilisha mshangao imetumiwa ishara ya mshangao [!].

Kimsingi, mshairi ametumia isharo hizo za viakifishi ili kuelekeza katika usomaji wa shairi. Ushairi simulizi hudhibitiwa zaidi kwa matumizi ya kimihemko, kimako, kupandisha au kushusha vidatu vya sauti katika utamkaji wa maneno wakati wa uwasilishaji (Gromov 2006 na Nowottny 1968). Kama ilivyokwisha kuelezwa hapo awali, shairi hilo ni la kauli au sentensi moja lakini mshairi ameashiria hitimisho kwa kuchopeka kituo [.] mwishoni mwa utungo. Kwa hivyo, usomaji wake umedhibitiwa pia kwa ishara za viakifishi. Kwa mfano, hadhira inapolisoma shairi hilo huanza kwa mshindo ambapo hapa na pale hupunguza kasi na inapofikia karibu na mwisho hushuka

kwa matao ya chini. Katika na uwasilishaji wa shairi andishi ambalo huzingatia arudhi za kimapokeo muundo, mwendo na mahadhi hudumishwa na hudhibitiwa kwa uzingativu wa idadi maalumu ya mizani, vina na kwa kiasi fulani kwa kuzingatia viakifishi vilivyotumiwa katika uwasilishaji wake. Ushairi wa Kiswahili usiozingatia arudhi hutumia zaidi uelekezo wa viakifishi katika uwasilishaji wake kwa malengo ya kuelekeza usomaji na pia kulipa shairi muundo na mahadhi mahususi.

5.3 KIISHILIO

Sura hii imetathmini matumizi ya methali katika muktadha wa uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili usiozingatia arudhi za kimapokeo. Mashairi manne kutoka kwa diwani ya Euphrase Kezilahabi *Kichomi* na Kithaki wa Mberia *Bara Jingine* ndiyo yaliyotumiwa kama vielelezo vya mashairi mengine maarufu yanayopatikana katika kitengo hiki.

Katika uwasilishaji wa mashairi haya imebainika kuwa methali zilizotumiwa ni chache mno ikilinganishwa na ushairi wa Kiswahili ambao huzingatia arudhi za kimapokeo. Endapo methali zimetumiwa, huwa zimepewa nafasi finyu kuwa chanzo cha kuibulia muundo lakini ni tajiri katika udhibiti wa maudhui yaliyowasilishwa. Jambo hilo limebainishwa kupitia kwa mashairi teule katika sura hii. Ingawa si mashairi yote yaliyozingatiwa, baadhi ya tungo katika diwani ya *Kichomi*, ni mashairi matano ndiyo yaliyotumia methali. Methali hizo ni kama vile: *Yaliyopita yamepita* (Shairi la: 'Mto Nili'), *Nyoka akimbiapo shimoni huanzisha kichwa* (Shairi la: 'Barua ya Mkata kwa Rehema'), *Kamba isiyoonekana haikatiki* (Shairi la: 'Dhamiri Yangu'), *Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka* (Shairi la: 'Kumbukumbu 2') na *Pilipili Usiyoila*

yakuwashiani (Shairi la: 'Uliza Wanaojua'). Kadhalika, Kithaka wa Mberia katika diwani ya *Bara Jingine* ni mashairi mawili tu ndiyo yaliyotumia kwa uwazi methali. Mashairi hayo ni kama vile 'Machozi ya Damu' na 'Nakumbuka Ulivyokuwa'. Vile vile, ni methali moja ya *Majuto ni mjukuu* ndiyo iliyotumika katika muktadha wa mashairi hayo.

Ingawa methali zimetumiwa katika ushairi huu, imebainishwa kuwa hakuna ulazima wa kushirikisha kwa uwazi matumizi yake. Hata hivyo, zinapotumika hujenga taswira na isitiari. Kwa sababu, mantiki au busara ya methali hudhibitiwa na husetiriwa katika ujumbe uliowasilishwa.

Katika mantiki hiyo, mawazo huwasilishwa zaidi kimafumbo, kitaswira na kiisitiari katika muktadha wa tamathali za usemi zilizoundwa. Kwa ambavyo mtunzi hana ulazima wowote wa kutumia kwa uwazi methali, huwa amejikomboa kutoka kwa mazonge ya mikatale ya arudhi au sharuti za kimapokeo. Kwa hivyo, mshairi huweza kuusawiri ushairi kwa kuchochea mwelekeo na hisi alizotaka kuziwasilisha.

Katika kitengo hicho, mshairi huzingatia zaidi uzindushi wa jamii. Kwa sababu, maswala ya kimaadili huwa tayari yameshughulikiwa kwa kina katika mashairi ya kimapokeo. Kwa mfano, ushairi huo umezingatia mno swala la ujenzi wa jamii mpya kwa kuitaka hadhira au jamii itathmini upya mielekeo iliyopo na kuchukua hatua zinazofaa ili malengo ya ndoto zao kuweza kufikiwa.

Hata hivyo, methali ambazo hutumiwa katika ushairi wa Kiswahili huweza kuwa za masuto au mawaidha (Mlacha 1985). Methali ambazo huibua mawaidha ndizo zimekuwa zikitumiwa kwa uwazi zaidi katika uwasilishaji wa ushairi wa kimapokeo kwa kuhofia kukaripia au kukemea. Katika ushairi huru wa Kiswahili huweza kutumia ama methali au kauli za kibinafsi ili kushutumu, kukaripia na hata kukemea baadhi ya vitendo visivyofaa katika jamii. Endapo pana ulazima wa kutumia methali, basi zinazotumiwa mno kwa uwazi ni zile za masuto. Kadhalika, matumizi ya methali katika utungo huo husetiriwa katika maudhui yaliyowasilishwa. Vile vile, watunzi wa ushairi huu ni wataalamu au wasomi waliobobea katika taaluma ya fasihi hususa ushairi wa kilimwengu (Masinde 2007 na Senkoro 1988). Kwa hivyo, kauli mbalimbali huweza kuibuliwa na kutumiwa kwa makusudi na kwa utaalumu kama chombo cha kuwasilishia ujumbe kimafumbo au kimzunguko katika ushairi wa Kiswahili.

Kadhalika, kutumiwa au kutotumia methali ni swala ambalo huweza kuibua na kuendeleza mgogoro katika ushairi wa Kiswahili. Kimtindo, matumizi ya methali huufanya ushairi wa Kiswahili kuwa wenye sura mbili za sarafu moja ambazo hujengana na hukamilishana. Kwa hivyo, watunzi wa ushairi wa Kiswahili hawana ulazima kutumia methali kwa uwazi, lakini pale ambapo shairi halina matumizi hayo, mwangwi huhisika na hutawala.

SURA YA SITA

AINISHO LA USHAIRI WA KISWAHILI KWA KUZINGATIA MATUMIZI YA METHALI

6.0 UTANGULIZI

Sura hii imependekeza kigezo mbadala ambacho huweza kutumika katika uainishaji wa ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia kipengele cha methali. Kimsingi, ushairi wa Kiswahili umepitia mabadiliko mbalimbali ya kihistoria, kitamaduni na kijamii hadi kufikia hali yake ya sasa. Kwa mfano, hapo awali ushairi wa Kiswahili ulikuwa ni utanzu maarufu miongoni mwa Waswahili kama jamii. Kutokana na maenezi ya lugha ya Kiswahili kutoka Pwani ya Afrika Mashariki hadi bara, ushairi wa Kiswahili umeweza pia kupea na kupata umaarufu miongoni mwa jamii. Kwa hivyo, watunzi huweza kutunga tungo ambazo hushirikisha utamaduni mpana wa Afrika Mashariki kutokana na maenezi ya lugha ya Kiswahili.

Katika muktadha wa Afrika Mashariki, ushairi wa Kiswahili ulitungwa kwa kuzingatia zaidi arudhi za kimapokeo kama vile uzingativu wa mizani, mishororo, vina na vibwagizo. Mwishoni mwa miaka ya 1960 na hasa kuanzia miaka ya 1970, baadhi ya washairi waliweza kujitupa ugani na kutunga tungo zao bila ya kuzingatia zaidi arudhi za kimapokeo kama ilivyobainishwa katika sura ya nne na ya tano katika tasnifu hii. Kwa wakati huu wa sasa, ushairi wa Kiswahili unawakilisha tungo zinazozingatia zaidi arudhi za kimapokeo, zile zisizozingatia sana arudhi na zile zisizozingatia kabisa arudhi hizo katika uwasilishaji. Hata hivyo, hizo ni tanzu za ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, sura

hii imefafanua jinsi matumizi ya methali huweza kutumiwa kama kipengele muhimu cha kuainishia ushairi wa Kiswahili.

6.1 Uainishaji wa Awali wa Ushairi wa Kiswahili

Mpaka sasa ushairi wa Kiswahili umeweza kuainishwa na baadhi ya wahakiki na waandishi wa kifasihi kwa kuzingatia mitazamo tofauti tofauti. Maainisho hayo yametokana na tafiti zilizofanywa na kauli mbalimbali zilizotolewa kuhusu utanzu huu. Miongoni mwa wainishaji hao ni Babusa (2005), Masinde (2003), Kimani na Chimerah (1999), Sanka (1995), Mazrui (1994), Noor (1988), Senkoro (1988), Kandoro (1983), Kahigi na Mulokozi (1979), Kezilahabi (1974)na Abedi (1954).

Kwa mfano Masinde (Keshatajwa), ameuainisha ushairi kwa kuzingatia kipengele cha mabadiliko ya maudhui katika muktadha wa kihistoria. Kwa kufanya hivyo, ameweza kuyaweka mashairi ya Kiswahili katika vipindi mahususi vya kihistoria. Kimsingi, ushairi wa Kiswahili una tungo anuwai zenye kuwasilisha mada mbalimbali zinazotokana. na utamaduni na uhalisi wa maisha ya watu. Katika uwasilishaji wa sanaa hiyo, kuna matumizi ya kauli mahususi ambazo hubuniwa kibinafsi, hutumiwa kwa makusudi ili kuuathiri moyo na kuchochea tafakuri ya msomaji.

Kwa kuzingatia kauli hizo teule, mshairi huweza kuibua maswala ambayo huweza kuuchoma au kuuzindua moyo kupitia kwa taswira na isitiari zilizoundwa. Kwa hivyo, uainishaji wa ushairi haupo tu katika kiwango cha maudhui, bali pia kwa kuzingatia vipengele vya fani kama vile miundo, maumbo, lugha na usanii kwa jumla. Kulingana na

nadharia ya Semiotiki, mada au maudhui yale yale huweza kusawiriwa upya kwa kuzingatia miundo mbalimbali ya lugha. Zaidi ya maudhui katika mkabala huo, Masinde amependekeza kuwa ushairi wa Kiswahili huweza kuainishwa kimakundi kama ifuatavyo:

i. Ushairi wa Kiswahili kabla ya kuja kwa wakoloni.

ii. Ushairi wa Kiswahili wakati wa utawala wa kiarabu.

iii. Ushairi wa Kiswahili wakati wa utawala wa kizungu.

iv. Ushairi wa Kiswahili baada ya uhuru.

v. Kuzingatia kipengele cha muundo.

vi. Kuzingatia kipengele cha mtindo.

vii. Kuzingatia utendakazi wake.

Uhakiki wa Masinde umebainisha kuwa ushairi wa Kiswahili huweza kuainishwa kimakundi kwa kuzingatia maudhui ambayo huibuliwa katika miktadha mbalimbali ya kiwakati au kihistoria. Mwelekeo huo umejitokeza wazi katika makundi manne ya kihistoria (Taz. Vipengele i, ii, iii na iv) ambapo, amevitolea ufafanuzi wa kina kurejelea vipindi hivyo mahususi. Hata hivyo, uainishaji huo umegusia pia vipengele muhimu kama vile umuundo, mtindo na utendakazi wa ushairi (Taz. Vipengele v, vi na vii). Vipengele hivyo vitatu vimechukuliwa kuwa vya muhimu na vinavyohitaji kutolewa maelezo na kufanyiwa utafiti wa kina.

Kwa ambavyo hayo (vipengele v, vi na vii) ni mapendekezo yaliyohusu vigezo vya kijumla ambavyo huweza kuzingatiwa, Masinde hakuvitolea ufafanuzi wala kueleza jinsi vinavyoweza kutumiwa katika uainishaji wa ushairi wa Kiswahili.

Kwa kurejelea mwelekeo na mapendekezo ya Masinde, Babusa (2005) ameyaainisha mashairi ya Kiswahili kimaudhui na pia kudhihirisha kwa kiwango fulani kuwa, kipengele cha muundo huweza kutumika katika uainishaji wa mashairi hayo. Kwa kuzingatia kipengele cha muundo, Babusa amebainisha sura mbalimbali zinazoibuka na ameyaweka mashairi hayo katika maumbo au bahari mbalimbali za ushairi. Kwa kuzingatia bahari hizo, ushairi wa Kiswahili huwakilishwa kwa miundo maalumu ya lugha kama vile uzingativu wa msamiati teule, sajili za lugha na lahaja. Hata hivyo, kilichobainika ni kwamba, umbo au muundo katika ushairi wa Kiswahili hujibainisha zaidi kupitia kwa mtindo ambao huzingatiwa katika uwasilishaji wake.

Naye Kezilahabi (1973), ameonyesha jinsi ushairi wa Kiswahili unavyoweza kuainishwa kwa kuzingatia nyakati tatu maalumu za urasimi kama ifuatavo:

i. Wakati wa urasimi-mkongwe (1728-1885)

ii. Wakati wa urasimi-mpya (1945-1960)

iii. Wakati wa usasa (1967 hadi sasa)

Kulingana na Kezilahabi, urasimi ni wakati ambapo misingi maalumu ya kazi za sanaa huwekwa na kukubalika kuwa vipimo bora vya kazi nyinginezo za kisanaa. Katika

muktadha wa Waswahili, ushairi ulipaswa kutungwa na kuwasilishwa kwa uelekezi wa baadhi ya vipengele vifuatavyo:

i. Idadi maalumu ya mizani

ii. Urari wa vina

iii. Umbo

iv. Maudhui yaliyojikita katika maadili

v. Lugha isiyo na utusani

vi. Mtiririko au ushikamano wa mawazo kutoka ubeti hadi ubeti

vii. Kuimbika kutokana na matumizi ya vina na mizani

viii. Utaratibu wa uwasilishaji: mwanzo, kati na mwisho.

Vipengele hivyo viliidhinishwa na vilichukuliwa kuwa 'roho' ya ushairi wa Kiswahili katika kipindi cha urasimi. Mashairi ambayo yalikiuka utaratibu huo yalikemewa na kupuuzwa (Kandoro 1983 na Abedi 1954). Kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1960 na hasa katika miaka ya 1970 hapa Afrika ya Mashariki, baadhi ya watunzi kutoka bara pia waliweza kuwasilisha tungo zao kwa kuziasi baadhi ya kaida hizo (Senkoro 1988 na Kahigi na Mulokozi 1979). Huo ulichukuliwa na baadhi ya washairi wa kimapokeo kuwa ni dosari na uchafuzi wa ushairi wa Kiswahili uliokuwepo. Mwelekeo huo pia umeweza kupata uelekezi kupitia kwa mihimili ya nadharia ya Fomula ya Kisimulizi ambapo kilichopendekezwa ni uzingativu wa kauli teule za kimapokeo na maudhui yaliyojikita katika uhalisi na utamaduni wa jamii (Fowler 1966). Kuhusu ukiushi wa kaida hizo, nadharia ya Semiotiki imetoa mwelekeo kwamba, kazi ya fasihi huweza

kuwasilishwa kwa mitindo tofauti tofauti ilimradi ujumbe umefasiriwa kwa uzingativu wa utamaduni wa jamii (Barthes 1981 na Eco 1976).

Hapo awali, Kiswahili kilikuwa ni lugha ya pwani ya Afrika Mashariki na baadaye kuenea bara, nao ushairi wa Kiswahili umeweza kuwekwa katika makundi mawili mahususi: ushairi ambao huwasilishwa katika mazingira ya pwani na ushairi ambao huzingatia mazingira ya bara. Mwelekeo huo unapozingatiwa hauwezi kuuchukulia ushairi wa Kiswahili kwa upana wake. Kwa sababu, kwa wakati wa sasa, utanzu huu hushirikisha tungo ambazo hutungwa na jamii pana ya Afrika Mashariki na popote pale ambapo Kiswahili hutumika kama chombo cha mawasiliano. Vile vile, kutokana na kiumbiumbi cha mgogoro wa ushairi kuhusu kutumia au kutotumia baadhi ya arudhi za kimapokeo kama vile vina na urari wa mizani; ushairi wa Kiswahili umeweza kuwekwa katika matapo mawili: ushairi ambao huzingatia arudhi za kimapokeo na ule usiozingatia arudhi hizo katika utunzi na uwasilishaji wake (Sanka 1995, Gibbe 1990 na Senkoro 1988).

Pia, ushairi wa Kiswahili umeainishwa kwa kuzingatia idadi maalumu ya mishororo katika beti (Noor 1988, Kandoro 1983 na Abedi 1954). Zaidi ya kuzingatia idadi mahususi ya mishororo, mizani na urari wa vina katika ubeti, ushairi wa Kiswahili uliainishwa katika bahari mbalimbali kutokana na:

i. Urari wa vina katika mistari au mishororo katika beti.

ii. Mpangilio wa maneno katika mistari au mishoro katika beti.

iii. Idadi ya vipande katika mistari au mishororo katika beti.

iv. Idadi maalumu ya mizani katika mistari au mishororo katika beti.

Katika muktadha wa vipengele hivyo vine; muundo na maumbo ya ushairi uliweza pia kuainishwa zaidi kama ifuatavyo:

i) Tathnitha - shairi ambalo lina mishororo miwili katika kila beti.

ii) Tathlitha - shairi ambalo lina mishororo mitatu katika kila beti.

iii) Tarbia - shairi ambalo lina mishororo minne katika kila beti.

iv) Takhmisa - shairi ambalo lina mishororo minne katika kila beti.

v) Tashlita - shairi ambalo lina mishororo sita katika kila beti.

vi) Ushairi ambao una mishororo kumi kwa kila ubeti

vii) Masivina - shairi ambalo lina mlingano wa mizani katika mishororo lakini si urari wa vina.

viii) Ukawafi - shairi ambalo lina vipande vitatu katika kila mshororo.

ix) Msuko - shairi ambalo lina kibwagizo kifupi.

x) Sakarani - shairi ambalo linashirikisha bahari mbalimbali.

xi) Kikwamba - shairi ambalo linarudia neno moja katika kila mwanzo wa beti.

Kulingana na Wafula na Njogu (2007) na Mohamed (1990) ni kwamba, katika kipindi cha urasimi mpya katika fasihi ya Kiswahili ambapo palizuka istilahi maalumu za kuelezea dhana mbalimbali za ushairi wa Kiswahili. Istilahi hizo zilizotumika zaidi ni kama:

i) Mshororo - ambao ni mstari katika shairi

ii) Mwanzo - mstari au mshororo wa kwanza katika ubeti

iii) Mloto - mstari au mshororo wa pili katika ueti

iv) Mleo - Mstari au mshororo wa tatu katika ubeti

v) Kipokeo - Mstari au mshororo wa mwisho katika ubeti

vi) Ukwapi - Sehemu ya kwanza katika mshororo

vii) Utao - Sehemu ya pili kaitka mshororo

viii) Mwandamizi - Sehemu ya tatu katika mshororo

ix) Tabdila - Kifupisho cha sauti kaitka neno linalotumika katika mshororo bila ya kubadilisha maana ya msingi.

x) Inkisari - Kunga ya kufupisha maneno katika mshororo

xi) Mazida - Kunga ya kurefusha neno bila ya kupotosha maana ya asili.

Istilahi hizo zilitumiwa kwa makusudi, kwa malengo ya kuutambulisha ushairi wa Kiswahili. Katika muktadha wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, uwepo wa bahari na istilahi maalumu zilizotumika katika ushairi, ni njia mojawapo ya kubainisha tanzu za ushairi kwa ujumla. Uainishaji huo ulizingatia zaidi ushairi uliotungwa katika muktadha wa arudhi za kimapokeo (King'ei na Kemoli 2001). Hata hivyo, imebainishwa kuwa ushairi wa Kiswahili usiozingatia arudhi katika uwasilishaji haushirikishwa katika uainishaji huo.

Zaidi ya hayo, utafiti huu umependekeza matumizi ya methali kama kipengele cha kuainishia mabadiliko ya kiutunzi ambayo hubainika katika ushairi wa Kiswahili. Kwa sababu, katika wakati wa sasa kuna mashairi ambayo yamezingatia zaidi arudhi za

kimapokeo, yale ambayo hayakuzingatia mno arudhi hizo na yale ambayo hakuzingati kabisa arudhi za kimapokeo katika utunzi na uwasilishaji wake.

Makundi hayo matatu katika ushairi wa Kiswahili yamedhihirisha kuwa:

i. Ushairi wa kimapokeo ambao umejitenga kwa kiasi fulani na ushairi hu lakini una ukuruba na ushairi wa kati.

ii. Ushairi wa kati ambao huzingatia kwa kiasi mbinu za utunzi zinazopatika katika ushairi wa kimapokeo na ule wa ushairi huru.

iii. Ushairi huru ambao umejitenga zaidi na ushairi wa kimapokeo kwa upan wa umuundo na kiumbo.

Kwa hivyo, ushairi wa Kiswahili una tanzu zake ambazo huwiana katika utunzi uwasilishaji wake. Hata hivyo, tofauti ambazo hubanika si za msingi kuweza kuzifany tanzu hizo kutalikiana. Kwa mfano, tungo hizo huzingatia lugha ya kimafumb kitaashira, kiisitiari, kitashbihi, kitashihisi miongoni mwa kunga zingine za uwasilisha Kauli za muhimu ambazo hutumiwa mno katika uwasilishaji, ni zile ambazo hujibainis zaidi katika tamathali za usemi.

Kwa mujibu wa mtafiti, dhima ya methali inapozingatiwa, ushairi wa Kiswahili huwe kuainishwa kwa mwafaka zaidi. Imebainishwa hapo awali kuwa, ushairi wa Kiswahi umepitia mabadiliko mbalimbali hadi kufikia hali yake ya sasa (Kimaro 2008 na Sank 1995). Aidha, ushairi wa Kiswahili huweza kutumia methali nyingi, chache am kutotumia kabisa katika utunzi na uwasilishaji wake kutegemea mahitaji ya kimtindo mwelekeo wa mtunzi. Katika msingi huo, ushairi wa Kiswahili umekuwa wenye kurun

tatu (ushairi wa kimapokeo, kati na huru). Kimuundo, ushairi umeweza pia kuainishwa kwa kuzingatia namna methali zilivyotumiwa katika uwasilishaji wa utungo.

6.2 Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili Unaopendekezwa

Kulingana na utafiti huu dhima ya methali inapozingatiwa, ushairi wa Kiswahili huweza kuainishwa zaidi kama ifuatavyo:

i. Ushairi wa Kiswahili unaotumia methali kama anwani

ii. Ushairi wa Kiswahili unaotumia methali moja

iii. Ushairi wa Kiswahili unaotumia methali nusu

iv. Ushairi wa Kiswahili unaotumia methali mbili (au zaidi)

v. Ushairi wa Kiswahili unaotumia methali kama kauli

vi. Ushairi wa Kiswahili unaotumia methali kama kibwagizo (au kiishilio)

vii. Ushairi wa Kiswahili unaotumia methali kama mwangwi

Zaidi ya hayo, kila kikundi cha ushairi kimependekezewa jina mahususi kuwa kitambulisho chake. Mbinu iliyotumiwa katika uundaji wa istilahi hizo za majina ni ile ya kuunganisha viambishi awali vya maneno yanayopatikana katika kila kikundi. Majina ambayo yamependekezwa ni kama yafuatayo:

i. **Ukimea** - Ushairi wa **Ki**swahili unaotumia **me**thali kama **a**nwani.

ii. **Ukimemo** - Ushairi wa **Ki**swahili unaotumia **me**thali moja.

iii. **Ukimenu** - Ushairi wa **Ki**swahili unaotumia **me**thali **nu**su.

iv. **Ukimembi** - Ushairi wa **Ki**swahili unaotumia **me**thali mbili (au zaidi).

v. **Ukimeka** - Ushairi wa **Ki**swahili unaotumia **me**thali kama **ka**uli.

vi. **Ukimeki** - **U**shairi wa **Ki**swahili unaotumia **m** **ki**bwagizo (au **ki**ishilio).

vii. **Ukimemwa** - **U**shairi wa **Ki**swhaili unaotumia **me**thali kama **mwa**ngwi.

Kwa uelekezo wa mihimili ya nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, uainishaji huo umezingatia kwamba, uwasilishaji wa ushairi hushirikisha kauli teule zinazopatikana katika mawasiliano ya jamii (Propp 1968). Vile vile, kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Semiotiki, methali kama ishara mahususi zinazotumika katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili huweza kubadilika kulingana na mabadiliko ya utamaduni wa jamii. Katika muktadha huo, methali kama ishara zinazotumika katika ushairi huu huweza kufasiriwa au kufafanuliwa katika miktadha mahususi ya utamaduni wa jamii. Kwa hivyo, matumizi ya methali katika ushairi wa Kiswahili huweza kutekeleza dhima mbalimbali.

Dhima ambazo huweza kutekelezwa kwa kuzingatia matumizi ya methali katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili ni pamoja na:

i. Udhibiti wa muundo wa ushairi

ii. Uwasilishaji wa maudhui au ujumbe unaoibushwa katika shairi

iii. Uashiriaji wa kimtindo katika shairi

iv. Ubainishaji wa mwelekeo au itikadi ya mtunzi katika shairi

v. Uhifadhi wa utamaduni wa jamii katika shairi

vi. Udhihirishaji wa mabadiliko ya kimtindo katika utunzi wa ushairi

vii. Ubainishaji wa mazingira au muktadha wa jamii katika shairi

Ni katika utambuzi wa dhima na utendakazi wa methali ndipo uwiano wa sura mbalimbali za ushairi wa Kiswahili huweza kubainishwa.

6.2.1 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali kama Anwani

Kitengo hiki kinashirikisha ushairi ambao unatumia methali kama anwani. Katika utungo huo, mashairi ambayo huwasilishwa aghalabu hutumia sehemu au methali nzima kuwa anwani kamili ya shairi. Kwa kufanya hivyo, methali huweza kuwa ni kielekezo au chanzo cha utunzi, uibuaji na upangaji wa mawazo ambayo huwasilishwa. Aidha, ushairi wa *Ukimea* huweza kushirikisha methali moja au zaidi katika uwasilishaji wake.

Hata hivyo, kilicho cha msingi ni kuwa, methali zingine zinazoshirikishwa huibuliwa kwa uelekezi wa anwani. Kwa hivyo, methali hizo huweza kujitokeza miongoni mwa mishororo katika beti. Endapo methali imetumiwa kama kibwagizo, kibwagizo hicho hakitakuwa na ulazima wa kutiririshwa kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa ubeti wa mwisho. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mtunzi hupata uelekezo wa kufaragua mawazo katika utungo (Parry 1971). Aidha, uwasilishaji huo hutokana na mchomo kuhusu tukio au swala ambalo limemkera au limempa msanii nyombolezo ambayo yamesababishwa na yale aliyoyahisi, yaliyomwathiri au aliyoyashuhudia katika uhalisi wa maisha ya jamii (Mulokozi 1995 na Kahigi na Mulokozi 1979). Kwa hivyo, mshairi huamua kwa makusudi kuteua na kutumia kauli au methali mojawapo ambayo huweza kusaidia katika kubainisha hisi na mawazo kwa utaratibu unaoeleweka kwa hadhira.

Katika muktadha huo, mtunzi huwa mwenye udhibiti wa dira mwafaka inayoongoza katika uchimuzi wa hisi huku akiitilia maanani hadhira kusudiwa. Hali hiyo hutokana na sababu kwamba, methali ni matini au ishara ya lugha ambayo hupaswa kueleweka na kufasirika bila utata katika tajiriba na uzoefu wa wapokezi (Mlacha 1989 na Mohamed 1986). Kwa hivyo, methali inayotumiwa zaidi katika anwani ni ile iliyojengeka kwa maneno machache. Endapo methali hiyo imesheheni maneno mengi, humbidi yapunguzwe kwa ustadi au itumiwe sehemu ya awali. Kwa sababu, sehemu ya mwanzo katika muundo wa methali ndiyo ya msingi zaidi (Gesero 2009, Wamitila 2008 na Khatib 1999). Vile vile, methali iliyotumiwa kama anwani, humfanya mtunzi kujenga muktadha wa jumla ambamo ujumbe tarajiwa huweza kufumbwa. Kwa hivyo, tukio lililosawiriwa huweza kuwa la kihalisi au la kidhahania. Hilo hutegemea ujumbe ambao umeibuliwa kwa uelekezo wa methali kama anwani.

Kimsingi, methali ni miongoni mwa kauli maarufu ambazo zimekuwa zikitumika mno katika mawasiliano ya jamii na pia zimesheheni tajiriba ya jamii husika. Kimaudhui, methali hutumika katika kuibulia na kuwasilishia maadili na masuto ambayo hufungamana na uhalisi wa utamaduni wa jamii. Kwa sababu fasihi na ushairi ukiwemo, ni sehemu ya utamaduni wa jamii na vile vile ni tokeo la mivutano ya kijamii (Mulokozi na Kahigi 1979). Kwa hivyo, matumizi ya methali huifanya hadhira kupata uelekezo wa mwelekeo uliochukuliwa. Kimatumizi, mtunzi huwa amejitahidi kutafuta mifano ya mishororo au kauli ambazo huweza kushirikishwa katika uwasilishaji wa ujumbe ambao umefungamana na methali iliyotumiwa kama anwani katika utungo. Katika shairi la 'Muwerevu Hajinyoi' (Abdalla 1973:27), mshairi ameumua na ameendeleza mawazo

yake kupitia kwa kauli au mishororo iliyotumiwa. Kwa mfano, katika ubeti wa kwanza imetongolewa kuwa:

Mwenye nacho wajishasha, wajiona kama ndovu
Kitu kimekulewesha, huu tambui uovu
Ngoma yako itakesha, au ni nguvu za povu?
Tangu lini mwerevu, akajinyowa mwenyewe? (Ubeti wa 1)

Ubeti huo, umefafanua zaidi ujumbe ambao umeibuliwa kwa uelekezi wa methali iliyotumika kama anwani. Ujumbe ambao umewasilishwa umehusu mtu ambaye ameukata katika maisha na kuwadharau wale ambao hawajanafasika. Kadhalika, adili ambalo limewasilishwa kupitia kwa anwani, hubainishwa zaidi kupitia kwa mishororo ya ubeti.

Zaidi ya hayo, methali teule huwa ni kipengele muhimu katika kujengea kidokezo au kiashiria cha yale yaliyotarajiwa kuwasilishwa katika ushairi. Kwa hivyo, methali iliyotumiwa kuwa anwani huweza kuruhusu ama kwa kutoa ufafanuzi wa kimaelezo au kwa kujenga taswira ya picha ambayo huibua na huuwasilisha ujumbe kimafumbo. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), kuna taswira za aina mbili kuu: taswira ya kimaelezo na taswira ya kiishara. Kimsingi, methali hujengeka ndani ya tamathali za usemi ambazo humwongoza mtunzi katika usawiri na uwasilishaji wa maudhui katika utungo. Kwa misingi hiyo, methali inapotumiwa kama anwani huweza kujenga au kuibulia mafumbo, taswira na jazanda zilizoundwa hushadidia zaidi ufafanuzi wake. Kwa sababu, methali hujibainisha zaidi katika tamathali za usemi. Aghalabu, methali huweza kujenga mazingira ya kuibulia na kurejelea historia, utamaduni na mielekeo ya jamii.

Kimatumizi, methali huweza kuwa kielekezo cha ujumbe ambao unawasilishwa na humrejesha kila mara msomaji katika anwani iliyotumiaa. Vile vile, ufasiri wa ujumbe ambao huibuliwa hupaswa kurejelea kauli au ishara inayotumiwa katika anwani ambayo huweza kuwa ni methali. Kwa njia hiyo, mshairi humdhibiti msomaji kuzingatia maelezo ambayo yamefungamanishwa kiufundi na methali hiyo. Kwa ambavyo, methali husheheni hekima, busara na amali za jamii. Kwa hivyo, inapoitumiwa kama anwani huufanya utungo kuwa kitengo mahususi cha kuhifadhi utamaduni wa jamii husika. Isitoshe, methali huwa na maana dhahiri na batini katika uwasilishaji wa ujumbe (Wafula 1994). Baadhi ya mashairi ya Kiswahili, yameusawiri na yameuwasilisha ujumbe kwa kuzingatia maana dhahiri na batini. Jambo hilo huwa limepata mwelekeo kutokana na methali iliyotumiwa.

Katika Abdalla (1973:17) kuna shairi la 'Mnazi: Vuta N'kuvute'. Methali iliyotumika kama anwani ni:Vuta N'kuvute. Anwani iliyotumiwa katika shairi hili hudhihirisha maana dhahiri na vile vile maana batini. Kwa mfano, maana dhahiri ambayo imeibuliwa huwa ni mvutano baina ya wahusika wawili yaani *ALII* na *BADI.* Wahusika hao hawana maelewano mazuri. Hiyo ni maana ya kijuujuu ambayo huashiria maana fiche iliyowasilishwa. Kupitia kwa methali iliyotumika, mshairi huitaka hadhira ibaini mivutano ya kiuchumi na matokeo yake. Hapa ieleweke kwamba, mnazi ni mti ambao hupatikana katika sehemu za pwani. Mti huo huenziwa kutokana na matunda yake ambayo ni nazi. Nazi hutegemewa mo katika lishe la jamii. Kwa ambavyo *Badi* hataki kushuka chini, anamhini *Badi* kupata *nazi.* Kwa hivyo, mshairi ametumia mshororo wenye maneno kama vile '*wafanya ni masikani, mustarehe 'mekaa*'. Kwa kuzingatia

maneno ambayo yamepatikana katika mshororo huo, mshairi ameufafanua zaidi ujumbe ambao umewasilishwa. Hali hiyo pia imebainishwa katika baadhi ya tungo za Mohamed (2002). Mifano hiyo ya mashairi ni kama 'Jicho Geni' (Uk. 43) na 'Nguvu Hazilei' (Uk. 138). Kwa kutumia methali kama anwani, mshairi hupata uelekezo wa kuusarifu utungo ili kuweza kuwasilisha maudhui mazito au mepesi.

Kimsingi, swala hilo lihusulo uwasilishaji wa maudhui kimafumbo au kiusaili hutegemea mno kiwango cha ufasiri cha hadhira iliyokusudiwa. Kiusahili, mawazo ya mshairi katika utungo huo huweza kufafanuliwa kwa kutolea mifano na maelezo ya kina yanayoeleweka miongoni mwa hadhira. Ingawa mshairi humdokezea na humwelekeza kimbele msomaji katika anwani, maelezo ambayo yametolewa huweza kutamba kwingi kadri ya uelekezo wa upeo ulitarajiwa. Katika muktadha wa mihimili ya nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mtunzi huwa na kichocheo ambacho humfanya kutunga mawazo fulani kichwani mwake. Kutokana na mawazo aliyonayo, mtunzi huanza kuyawasilisha mawazo kwa intidhamu. Kwa uelekezo wa anwani ambayo ni mada msingi, msanii huanza kwa utangulizi, ufaraguzi wa mawazo na baadaye kumalizia utungo.

Kadhalika, methali iliyotumiwa katika ushairi huu huashiria viwango vya mawazo ambayo yamefundikwa katika itikadi na mwelekeo wa mshairi. Kwa kiwango fulani cha kimuundo, ushairi huo wa *Ukimea* una mwelekeo wa kuzingatia au kutozingatia matumizi ya vina na urari wa mizani katika usawiri na uwasilishaji wake. Hiyo imetokana na sababu kuwa, anwani katika shairi haitarajiwi iwe na idadi kubwa ya maneno. Kwa hivyo, iwapo methali ina maneno mengi baadhi ya maneno yasiyokuwa ya

msingi zaidi huweza kuachwa kwa makusudi ili yabaki yale ya msingi (Frolova 2008 na Wanyoike 1976). Aidha, ushairi huo huweza kuwa ule unaozingatia arudhi za kimapokeo kutegemea uelekezi wa muundo kamilifu wa methali inayotumiwa. Kwa mujibu wa M'ngaruthi (2007) na Mazrui na Syambo (1992), methali pia huwa yenye mwelekeo wa muundo wa kishairi, ambapo pana mahadhi ya kimziki na mara kwa mara hujitokeza katika mashairi ya Kiswahili ili kutosheleza mahitaji ya vina na mizani. Katika mantiki hiyo, ushairi huweza kuwa wenye mahadhi na ridhimu unaposomwa au unapoghaniwa. Jambo hilo limedhihirika mno katika uwasilishaji wa tungo za ushairi simulizi (Wamitila 2001). Hata hivyo, uwepo wa uwezekano au kutokuwezekana huko hutegemea aina ya methali iliyotumika kama anwani. Kutokana na maelezo au tathmini hiyo kuhusu matumizi ya methali kama anwani, ushairi wa *Ukimea* huweza kuwa na sifa za kijumla zifuatazo:

i. Matumizi ya urari wa vina na mizani huweza kuhusishwa au kutohusishwa katika utunzi na uwasilishaji.

ii. Maudhui huwasilishwa kupitia kwa miundo maalumu ya lugha.

iii. Mwelekeo na dhamira ya mtunzi hubainika.

iv. Mtindo kama mbinu ya uwasilishaji katika utungo huwa bayana.

v. Muktadha na mazingira ambayo huibua usawiri wa tukio au mawazo huwa dhahiri.

vi. Mahadhi ya ridhimu na mdundo hudumishwa.

vii. Kauli mahususi kama vile methali huwa ni chombo cha kuwasilishia mabadiliko ya kimtindo na maudhui.

Kwa kuzingatia mashairi katika diwani teule katika utafiti huu, sifa za ushairi wa *Ukimea* zimedhihirishwa kupitia kwa mashairi yafuatayo:

- Diwani ya **Sauti ya Dhiki**
  - (i) Shairi la 'Mnazi: Vuta N'kuvute' (uk. 17-22)
  - (ii) Shairi la 'Mwerevu Hajinyowi' (uk. 27)
- Diwani ya **Jicho La Ndani**
  - (i) Shairi la 'Jicho Geni' (uk. 45)
  - (ii) Shairi la 'Nguvu Hazilei' (uk. 138)

6.2.2 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali Moja

Mashairi ambayo hutarajiwa kupatikana katika kitengo hiki cha *Ukimemo* ni yale hutumia methali moja kama kauli au mshororo kamili katika utunzi na uwasilishaji. Kadhalika, utungo huu ni ule ambao anwani iliyotumika si ya methali au huweza kuwa ni kauli yenye mwangwi wa methali. Methali mradi iwe ni moja, huweza kutumiwa popote katika muktadha wa shairi: mwanzoni mwa shairi, miongoni mwa ubeti au kama mojawapo ya mishororo au mistari katika shairi.

Katika uwasilishaji wa ushairi wa *Ukimemo*, mtunzi huwa ana hoja mbalimbali ambazo huziwasilisha kwa hadhira. Kwa kutumia methali moja, huifafanua hoja moja mahususi iliyoizingatia miongoni mwa hoja zingine zinazowasilishwa. Hapa ieleweke kwamba, mtunzi huweza pia kuwa na hoja moja ambayo hujenga maudhui yanayowasilishwa katika utungo. Hoja hiyo huweza kuelekezwa kupitia kwa methali iliyotumika, ingawaje umuhimu wake hutegemea zaidi pale ambapo imejitokeza katika utungo. Kwa mfano,

inapotumiwa mwanzoni mwa shairi, yaani katika ufunguzi wa ubeti wa awali, huwa ya msingi zaidi kuliko inapotokea katikati au ndani ya ubeti. Kwa sababu, muundo wa shairi huelekezwa kupitia kwa kauli hiyo.

Katika ushairi usiozingatia zaidi arudhi za kimapokeo, methali hiyo huwa ni miongoni mwa kauli zilizotumiwa. Aidha, matumizi yake huweza pia kujitokeza mwishoni mwa utungo kama vile ilivyo katika ushairi wa *Ukimeki*. Tofauti ni kwamba, katika ushairi wa *Ukimeki*, methali hiyo moja hutumiwa kwa makusudi ili kuufumba zaidi muhtasari wa mawazo yaliyowasilishwa na inapotumika mwishoni huendeleza mawazo ya mshairi au kuashiria hitimisho katika utungo.

Kimsingi, matumizi ya methali huakisi mawazo ya mwasilishaji ambayo huweza kutolewa kwa uwazi. Kwa msikilizaji au msomaji, matumizi ya methali huimarisha zaidi fikra za kupima na kuchambua au kufasiria ujumbe uliokusudiwa kwa kupatanisha ujumbe au maana ya methali na ukweli uliopo katika maisha (Mtesigwa 1989 na Mlacha 1985). Kimaudhui, methali hiyo huweza pia kutumika katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi kwa:

i. Uzingativu wa maana ya ishara za maneno yaliyotumika kwa kulinganisha na ukweli unaokusudiwa na maneno hayo.
ii. Uzingativu wa mshabaha wa maana iliyoibuliwa kutokana na maneno hayo na kuivika maana pana ya kijumla.
iii. Uzingativu wa malengo au mwelekeo wa mtunzi kulingana na muktadha wa mazingira au hali iliyozungumzwa wakati huo.

Kwa hivyo, matumizi ya methali huweza kusaidia katika uibushaji na uwasilishaji wa hoja maalumu na pia kumfanya mpokezi kuufasiri ujumbe uliowasilishwa. Katika muktadha huo, matumizi hayo ya methali husaidia zaidi katika kuubainisha ujumbe mahususi ambao umesawiriwa na umewasilishwa (King'ei na Kemoli 2001). Matumizi hayo huibuliwa kutokana na uelekezo wa anwani katika shairi. Zaidi ya hayo, matumizi hayo ya methali huashiria mwelekeo ambao huchukuliwa na mtunzi.

Isitoshe, methali iliyotumiwa mwanzoni huwa imejenga dibaji au mwanzo wa shairi ambapo hutumika kama ishara ambayo huchochea zaidi taharuki miongoni mwa hadhira. Kwa hivyo, matumizi hayo huweza kujenga msingi wa kuutanguliza utungo na kwa mshindo uliostahili. Kutokana na matumizi hayo, hadhira hushawishika kulisoma shairi kwa usaili na utafakari zaidi. Kwa hivyo, hadhira hulikabili kwa shauku na kutaka kujua zaidi yatakayojiri baadaye kwa kuzingatia kauli zilizoibuliwa. Hiyo ni mbinu ya taharuki ambayo hutumiwa katika kuwasilishia utungo. Hapa ieleweke kuwa taharuki ni mbinu ya awali hujenga na huumua ilihamu ya usomaji katika hadhira kusudiwa (Wamitila 2003, Mulokozi na Kahigi 1979).

Methali ambazo hujitokeza katika beti zilizofuatia, zaidi ya ile ya awali, huwa imetumiwa kuwa mbinu ya kiurejelezi ili kuikumbusha hadhira mambo ambayo tayari yamekwisha kudokezewa au kuzungumziwa kwa kina katika beti za awali. Kwa mfano, katika Mazrui (1988) *Chembe cha Moyo*, kuna shairi la 'Mgongano' (Uk. 36). Katika shairi hilo, mtunzi ametumia methali moja katika uwasilishaji. Methali hiyo ni: *Maisha mwendo wa ngisi, mwendo wa nyuma na mbele*. Uibushwaji wa matumizi ya methali hiyo imetokana

na mawazo yaliyowasilishwa hasa kwa uelekezo wa anwani katika shairi. Kwa hivyo, ufasiri wa ujumbe uliofumbwa katika methali humfanya msomaji kuzingatia muktadha wa matumizi yake katika ubeti au aya iliyopo. Kwa ambavyo mshairi tayari amejenga taharuki kutokana na matumizi ya methali hiyo, humfanya kuwa na mwau au mwanya ambao huhitaji kujalizwa. Kwa hivyo, mshairi hupiga makasia katika ufaraguzi zaidi wa maelezo au kutoa mifano ambayo huweza kusaidia katika ubainishaji wa ujumbe katika shairi. Katika mantiki hiyo, matumizi ya methali huwa ni kiunzi cha kuunganisha mawazo ya awali na yale ambayo yamefuatia au yale ambayo hutarajiwa.

Matumizi ya methali iliyotokea mwishoni mwa utungo, huashiria kwa ustadi hitimisho la shairi. Kwa hivyo, mshairi huzingatia methali iliyotumiwa ili kuwa mbinu ya kujenga au kuibulia msimamo wake. Katika mazingira hiyo, hupunguza kasi au mwendo wa shairi na kuufanya utungo huo kuweza kusomwa aste aste au kwa matao ya chini. Usomaji wa aina hiyo, huifanya hadhira siyo tu kutafakari bali pia kuzingatia kiini cha ujumbe ambao umewasilishwa katika shairi. Kimtindo, methali iliyotumiwa mwanzoni, hulipa shairi uelekezo wa ridhimu na mahadhi ambayo huafiki muundo wa methali hiyo.

Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mtunzi hufanya uteuzi wa kauli alizozitumia kutokana na zile ambazo tayari zimekubaliwa kuwa kito au muhimu katika mawasiliano ya jamii (Kandoro 1974 na Lord 1960). Kwa ambavyo methali zimejengeka katika muundo maalumu, ushairi wa *Ukimemo* hupata uelekezo wa kiumbo na kimtindo ambapo aghalabu mtunzi huwajibika kuzingatia mbinu za uwasilishaji kama vile idadi

maalumu ya mizani na urari wa vina. Dhima hiyo, hutekelezwa zaidi kupitia kwa methali ambayo imetumiwa au imejitokeza mwanzoni mwa shairi.

Kwa kuzingatia maswala ya kimuundo, baadhi ya watunzi na wahakiki wa awali wa fasihi wamechukulia kuwa vina na mizani ni uti katika utunzi na uwasilishaji wa utungo huu (Knappert 1979 na Harries 1963). Mtazamo huo, kwa kiwango fulani huweza kubainishwa kupitia kwa matumizi ya methali ambayo imetumika awali au kimbele katika beti za shairi. Hata hivyo, mawazo hayo ya kushikilia vina na mizani kuwa uti wa ushairi wa Kiswahili yameweza kupingwa na baadhi ya watunzi wa ushairi na wahakiki wa kifasihi (Senkoro 1988 na Mulokozi na Kahigi 1979). Kwa hivyo, uelekezo wa muundo katika shairi la Kiswahili huweza kudhihirishwa kutokana na uzingativu wa pahali mahususi ambapo methali imetumiwa na hasa mwanzoni mwa utungo.

Utendakazi wa methali moja, haujifungi katika muundo wa shairi bali pia katika uibuaji wa mawazo kulingana na utashi au mwelekeo wa mtunzi. Kwa sababu, huweza kutumiwa mwanzoni, katikati au mwishoni katika uwasilishaji wa utungo. Kadhalika, ufasiri wa ujumbe ambao huwasilishwa huweza kuzingatia methali iliyotumiwa kuwa ishara ya ufafanuzi wa ujumbe huo katika muktadha wa utamaduni uliyoibua matumizi hayo. Kulingana na nadharia ya Semiotiki, methali kama ishara huweza kufarika au kueleweka zaidi katika muktadha wa ishara au matini zingine zilizotumiwa. Isitoshe, methali yenyewe huwa haina maana yoyote hadi pale imetumiwa katika muktadha wa uwasilishaji wa ujumbe (Maitaria 2008, Waihiga na Kagwa 2007 na Ndalu na King'ei 1997). Kwa hivyo, matumizi ya methali na ufafanuzi wa ujumbe uliomo hupata kiashiria

chake katika muktadha wa utamaduni na uhalisi wa maisha katika jamii. Kutokana na matumizi hayo ya methali, ushairi huwa ni kiwakilishi au kiashiria cha amali na mali ya jamii.

Kadhalika, kwa kutumia methali kama mshororo au kauli kamili katika uwasilishaji wa utungo, huweza kuibulia na kuendeleza mawazo kiusambamba. Matumizi ya methali ambayo yamebainisha mtazamo huo ni kama vile shairi la 'Mara Mia La!' (Mohamed 2002:43). Methali iliyotumiwa katika shairi hilo ni: *Jambo usil'olijua kama usiku wa kiza.* Ubeti ambao umezingatia methali na ulioibua usambamba ni kama:

1. *Jambo usil'olijua kama usiku wa kiza*
   Hukuvunjia murua kupita kujitukuza
   Unasema watambua kupita kujitukuza
   Kumbe unajizuzua tamaa imekucheza
   Unapita ukizua na watu uwapoteza
   Hasha, si mara moja la, mara mia la! (Ubeti wa 1)

Kutokana na methali iliyotumika, ujumbe ambao umeibuliwa umemithilisha '*jambo lisolojulikana*' vizuri na '*usiku wa kiza*'. Kwa kuufafanua zaidi ujumbe, imeundwa mistari mingine ambayo pia imeshadidia zaidi mawazo yayo hayo yaliyowasilishwa. Kwa mfano, msanii ametumia mishororo ifuatayo:

- *Hukuvunjia murua kupita kujitukuza*
- *Unapita ukizua na watu kuwapoteza* (Ubeti wa 1)

Kupitia kwa mishororo hiyo katika ubeti, ufafanuzi wa ujumbe umekaririwa na umebainishwa kiusambamba. Jambo hilo pia limeendelezwa zaidi katika baadhi ya mishororo ya beti zilizofuatia. Baadhi ya mishororo hiyo ni kama:

Ubeti wa 2: *ukadhani ni funguo kufungulia tuhuma* (mshororo 2)

Ubeti wa 3: *ungengoja 'katamka na ishara kutimiza* (mshororo 1)

Ubeti wa 3: *Fumbua macho uone pendo lilikogandama* (mshororo 2)

Kwa hivyo, kauli na miundo ya lugha iliyotumiwa katika uwasilishaji wa shairi huweza kutofautiana lakini ujumbe ambao huwasilishwa, hukolezwa zaidi kwa kuzingatia mbinu ya usambamba.

Mbinu ya usambamba katika fasihi hutumia kauli ambazo zina miundo iliyofanana au iliyotofautiana katika kukoleza na kuendeleza mawazo ya aina moja ya msanii (Wamitila 2002, Senkoro 1988 na Mulokozi na Kahigi 1979). Kwa kutumia methali mahususi, mshairi huweza kuibua kauli au miundo mingine teule ambayo husaidia katika kushadidia na kufafanua zaidi ujumbe wa msingi katika shairi. Kutokana na matumizi ya methali moja, utungo huo huweza kuwa na sifa za kijumla zifuatazo:

i. Uzingativu wa miundo ya lugha ambayo huweza kuibua ruwaza ya mipangilio maalumu ya mizani na urari wa vina.

ii. Uzingativu wa miktadha ya utamaduni wa jamii katika ufasiri na ufafanuzi wa ujumbe unaowasilishwa.

iii. Uwasilishaji wa ujumbe kitaharuki, kiutafakari na kiusaili.

iv. Ujenzi wa ukariri wa ujumbe kiusambamba.

v. Uzingativu wa mtindo au mbinu mahususi katika uibuaji, ufaraguzi na uwasilishaji wa mawazo.

vi. Mawazo yanayowasilishwa huwa yanajikita katika tamathali za usemi.

Kwa kuzingatia mashairi katika diwani zilizoteuliwa katika utafiti huu, sifa za ushairi wa *Ukimemo* zimebainika kupitia kwa mashairi yafuatayo:

- Diwani ya **Chembe cha Moyo**

  (i) Shairi la 'Mgongano' (Uk. 36)

- Diwani ya **Jicho La Ndani**

  (i) Shairi la 'Mara Mia La!' (Uk. 43)

6.2.3 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali Nusu

Katika kikundi hiki imependekezwa kwamba, mashairi ambayo yatajumuishwa hapa ni yale ambayo hututumia sehemu ya mwanzo ya methali. Katika ushairi wa *Ukimenu*, ushairi huweza kutumia anwani ya methali au kauli mahususi kuwa anwani. Endapo methali imetumiwa, basi huwa si ya msingi katika uwasilishaji au udhibiti wa maudhui ambayo yamewasilishwa. Kwa hivyo, mtunzi hutumia baadhi ya maneno hayo katika kujenga utafakari au kejeli au kuzua maswali ya mjadala katika utungo. Kadhalika, katika mawasiliano ya jamii, aghalabu wahusika hutumia kauli bate bate ambazo si kamilifu. Hata pale ilipochopeka methali katika mazungumzo ya ana kwa ana katika jamii, huzingatia mno sehemu ya mwanzo ambayo ni ya msingi (King'ei na Kisovi 2005 na Wafula 1994). Kwa hivyo, sehemu ya mwanzo ya methali huwa ni kiashiria au kidokezo mwafaka cha kauli hiyo.

Katika muktadha wa mihimili ya nadharia ya Semiotiki, utunzi na uwasilishaji wa shairi, si lazima mtunzi aitumie methali katika ukamilifu wake. Kwa vile, matumizi yake huwa tayari yameeleweka kutokana na sehemu ya awali. Mbali na hayo, mshairi huwa na kibali cha kuzingatia sehemu ya methali na pia kutozingatia utaratibu wa kisarufi. Matumizi hayo, huifanya kauli iliyotumika kutofautiana kidogo na ile methali ya kawaida

iliyozoweleka katika jamii. Vile vile, mshairi huwa ana ruhusa ya kukata kata maneno kwa kuondoa herufi, viunganishi, sauti, sialabi au hata viambishi fulani katika kauli za msingi zinazotumika. Kadhalika, huweza kutumia uhuru huo kupunguza au kuondoa vishazi au sehemu ya methali mradi asiipoteze au asiivize maana iliyokusudiwa (Gibbe 1998 na Mazrui na Syambo 1992). Kwa ambavyo mtunzi wa ushairi wa Kiswahili huchuja maneno ili yabaki yale ya msingi ambapo ujumbe huibushwa na huwasilishwa.

Matumizi ya sehemu ya methali au methali nusu yaliweza kubainishwa kwa kuzingatia shairi la '*Hasira Hasara?*' linalopatikana katika Mazrui (1988:21) *Chembe cha Moyo*. Kwanza, mtunzi ametumia anwani ya 'Hasira Hasara?' ambapo ni methali iliyojisimamia ingawa amedondosha kiunganishi '**ni**' kwa makusudi au kutokana na uhuru wa kishairi. Pia katika anwani, mshairi ameongezea kiakifishi cha kiulizi. Katika mazingira hayo, ameibinafsisha methali kuwa kauli. Udondoshaji wa kiunganishi na uchopekaji wa kiakifishi hakuiathiri methali iliyotumika. Kwa uelekezo wa methali, mshairi ameamua kutumia ustadi wa kiumbuji katika kuibulia mizungu ya sehemu za msingi katika kauli hiyo. Kwa hivyo, mshairi amejenga dhana au sehemu mbili ambazo zimetumiwa katika uwasilishaji wa utungo: *Hasira* na *Hasara*. Mfano wa ubate wa kauli uliotumika umeweza kubainishwa kwa kuzingatia ubeti wa kwanza katika shairi hilo la 'Hasira Hasara?' Kwa hivyo, mshairi amesawiri kuwa:

> A*yi <u>Hasira</u>, uweje kwangu <u>Hasara</u>*
> *Iwapo dhuli ndiyo yangu tijara*
> *ilonishambulia ja samba marara*
> *Ikanichanachana kama tabara*
> *Basi <u>Hasira</u>, kwangu uweje <u>Hasira</u>?* (Ubeti wa 21)

Katika mtazamo huo wa kimtindo, mshairi amejibainisha kuwa mweledi katika kuisarifu lugha ili kuweza kumtumikia. Aidha, maneno katika methali yametawanywa ndani ya

ubeti na katika shairi zima kwa ujumla. Kwa hivyo, hadhira hutakiwa kutumia ujuzi ili kuweza kuyaleta maneno hayo pamoja. Kadhalika ametumia weledi wake kwa kuiwasilisha methali hiyo kibalagha, kitashihisi na pia kuipa hulka ya uhusika. Upunguzaji wa maneno katika methali na kutumiwa katika uwasilishaji wa utungo huu hukidhi haja hiyo. Mtindo huo pia hutumiwa katika kuumba na kuwasilishia mishororo au kauli msingi katika baadhi ya mashairi ya Kiswahili.

Kama vile ilivyokwisha kuelezwa hapo awali (Taz. Sura ya Nne), mtindo huo hutumiwa mno katika anwani za ushairi wa Kiswahili. Katika utungo wa *Ukimenu*, ubate huo wa methali hujitokeza zaidi katika baadhi ya mishororo. Hata hivyo, huweza kutumiwa kwa ukamilifu katika utungo huu ingawa jambo hilo si la shuruti. Kimuundo, sehemu hiyo ya awali ya methali huwa ni ya msingi mno ikilinganishwa na sehemu ya pili (Andambi na Murono 2005 na Ligami na Barasa 2001).

Kwa hivyo, utendakazi au dhima ya methali huwa ni matini shirikishi ikiwa imetumika ndani kwa ndani katika uwaislishaji wa ujumbe katika shairi. Katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa *Ukimenu*, mshairi huamua kwa makusudi au kwa hiari kutumia sehemu ya methali ili kuweza kuwa matini ndani ya matini. Matumizi hayo huafiki mtazamo wa mhimili wa nadharia ya Fomula ya Kisimuizi kuwa, mtunzi wa ushairi huwa hana muda mwingi wa kueleza au kufaragua mawazo. Kwa hivyo, matumizi hayo ya methali huwa ni ishara au kidokezo cha msingi kinachomfanya mtunzi kuitumia hadhira kuwa tendi au katika kujaliza maelezo yaliyoachwa kiustadi hivi kwamba, hadhira ya mshairi hupaswa kushirikishwa vilivyo katika uendelezaji wa

mawazo yanayowasilishwa. Kwa mfano, hadhira inapozingatia shairi la 'Hasira Hasara?' (Mazrui 1988:21) hujenga mazingira ya kulisoma shairi kwa nafsi mbili za wahusika: 'Hasira' na 'Hasara'. Kadhalika, hadhira huwa makini katika kulisoma shairi huku ikitafakari dhima au utendakazi wa kauli hizo msingi.

Kadhalika, maneno au kauli zilizotumiwa huwa zimedhamiria kuchochea tafakuri ya hadhira ili kuweza kuubainisha zaidi ujumbe ambao umekusudiwa (Wanyoike 1976). Kwa hivyo, mshairi alipotumia sehemu ya methali hujenga mazingira ya usaili, utafakari ili hadhira ibaini kiini cha ujumbe. Matumizi ya baadhi au sehemu ya maneno katika methali ni mbinu ambayo hutumiwa mno katika uwasilishaji wa baadhi ya tanzu za fasihi simulizi hususa, ushairi simulizi ambapo hadhira huwa si tuli bali hushiriki kikamilifu katika usaili na upokezi wa ujumbe (Matteru 1987, Kipury 1985 na Finnegan 1970). Kupitia kwa matumizi hayo ya methali katika uwasilishaji, hubainisha kwamba ushairi andishi wa Kiswahili huweza kuwa ni hifadhi ya ushairi simulizi. Vile vile, imedhihirishwa kuwa kuna ukuruba kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi (Njogu 2004 na Mulokozi na Kahigi 1988). Kwa hivyo, kwa matumizi ya methali nusu kama mbinu ya utunzi na uwasilishaji, msanii hataki kujifunga kabisa katika kauli ambazo zimeeleweka kwa urahisi katika jamii. Katika msingi huo, methali humtumikia zaidi msanii katika kujengea muktadha wa kuibulia hisi. Aidha, matumizi hayo yametamalaki kwingi katika baadhi ya ushairi wa Kiswahili ambao huzingatia zaidi arudhi za kimapokeo kama vile katika mpangilio wa mizani na wa vina. Kwa hivyo, mtunzi wa ushairi huu hudai uhuru na huwa nahodha wa ubunifu.

Isitoshe, kutokana na matumizi ya methali isiyokamilika, mtunzi huwa amejijengea mwanya wa kujaliza maelezo ambayo huibua mawazo kulingana na utashi wake. Katika muktadha wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, kauli kama ishara husaidia katika kutanua kunga za uwasilishaji hususa, usarifu wa muundo katika utanzu wa ushairi. Kwa hivyo, uhuru wa kishairi humfanya mtunzi kuusarifu utungo kwa uelekezo wa hisi au mchomo alionao. Hiyo ndiyo sababu ya methali iliyotumika huwa haijakamilika kimuundo.

Katika muktadha wa utunzi na uwasilishaji, manufaa ya kutumia sehemu au kipande cha methali huweza kumfanya mtunzi kukidhi mahitaji yafuatayo:

i. Kauli hiyo mahususi iliyotumika ni ya msingi katika uwasilishaji wa shairi. Kwa sababu, katika kauli hiyo bate bate ya methali kuna maelezo mapya ambayo huizindua akili ya hadhira.

ii. Kauli hiyo hutoa mwau au upenu kwa mshairi ili kuzingatia mambo mawili katika kauli moja. Aidha, kauli hiyo huafiki mawazo ambayo yamejikita katika utamaduni wa jamii na sehemu ya pili huwa ni nyongeza ya mawazo kwa kuzingatia mwelekeo wa mshairi.

iii. Kauli hiyo huwa ni kiungo muhimu baina ya mtunzi au fanani na hadhira.

Kutokana na matumizi hayo ya methali, mshairi huufanya utungo, kwa kiasi fulani uwe ni mali ya kibinafsi badala ya kuwa zaidi mali ya jamii. Kimsingi, ushairi huo wa *Ukimenu* huweza kuwasilisha mawazo ambayo huwa yenye uelekezo mwafaka wa kibinafsi. Huo ni upenu ambapo mtunzi hutoa kiufundi ushairi wa Kiswahili kutoka kwa

urasimi wa arudhi za kimapokeo. Kwa sababu, mtunzi wa ushairi huu huhofia kuwa akiunasua utungo kwa mshindo kutoka kwa arudhi za kimapokeo huenda akashutumiwa au kukemewa na baadhi ya watunzi ambao hushikilia zaidi matumizi ya arudhi hizo katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili (King'ei 2000). Kwa kiasi fulani, shairi hilo huweza kuchukua kina au mizani yoyote na wakati uo huo likakubaliwa kuwa ni utungo wa ushairi wa Kiswahili.

Kutokana na ujuzi au ufundi wake, mshairi huweza kupachika nusu nyingine iliyosalia ya methali katika sehemu yoyote katika shairi. Kimtindo, matumizi hayo huifanya lugha iliyotumiwa katika uwasilishaji wa utungo kuwa yenye mwingiliano wa matini, ambapo methali kama ishara hupata ukamilifu wake kwa uzingativu wa ruwaza ya ishara zingine zinazotumika (Eco 1984 na Scholes 1982). Vipande hivyo vya methali huweza kuhusiana au visihusiane moja kwa moja katika kuendeleza wazo linaloibuliwa na linalowalishwa. Katika muktadha wa matumizi hayo ya methali, hadhira hupaswa kulisoma shairi lote ili kuupata kwa ukamilifu ujumbe uliowasilishwa (Senkoro 1988 na Wanyoike 1976). Kutokana na matumizi ya methali nusu katika utunzi na uwasilishaji, huweza kufanya utungo wa *Ukimenu* kuwa na sifa zifuatazo:

i. Uwasilishaji wa mawazo huwa wa kiisitiari, kitaswira na kiistiara kwa uelekezo wa kauli zilizotumiwa.

ii. Ujengaji wa uwiano kati ya matumizi ya methali na matini au kauli zingine zilizoibuliwa kibinafsi.

iii. Utungo huweza ama kuzingatia au kutozingatia mizani na urari wa vina mahususi katika utunzi na uwasilishaji.

iv. Uwasilishaji wa mawazo hupata uelekezo wa mdundo au ridhimu na mahadhi mahususi.

v. Ushairi uliowasilishwa huweza kuwa ni mali ya jamii na vile vile kuwa mali ya mtu binafsi.

vi. Utungo hushirikisha kikamilifu usaili wa hadhira katika upokezi wa ujumbe.

vii. Matumizi ya lugha ya mkato hutumika zaidi katika uwasilishaji wa utungo. Kwa hivyo, idadi ndogo ya maneno huufumba ujumbe pana.

Kwa kuzingatia mashairi katika diwani teule katika utafiti huu, sifa za ushairi wa *Ukimenu* zimebainika zaidi katika shairi lifuatalo:

- Diwani ya **Chembe cha Moyo**

  (i) Shairi la 'Hasira Hasara?' (Uk. 23)

6.2.4 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali Mbili au Zaidi

Kikundi hicho cha ushairi kimeshirikisha tungo ambazo hutumia methali zaidi ya moja katika uwasilishaji wake. Katika ushairi wa *Ukimembi*, matumizi ya methali mbili au zaidi ndani ya utungo hutokana kwa uelekezo wa anwani ambayo si methali. Ushairi huu hutofautiana na ule wa *Ukimea* kwa ambavyo hautumii methali kama anwani.

Aidha, matumizi ya methali mbili au zaidi katika ushairi wa *Ukimembi* hujitokeza kiawamu au kwa kuzingatia mantiki mahususi kulingana na mahitaji ya mtunzi wa ushairi: mwanzoni (ya kwanza) katikati (ya pili, ya tatu au yoyote ile). Matumizi ya methali ya pili huweza pia kuchukuliwa kuwa ya mwisho. Hata hivyo, methali ya

mwisho huweza pia kuwa ya pili kutegemea mfuatano wa kujitokeza kwayo katika uwasilishaji wa utungo. Methali ya mwanzo hujitokeza katika ubeti wa awali au katika beti za mwanzo endapo mshairi ameshughulikia hoja zaidi ya moja. Methali ya pili huweza kujitokeza katikati ya shairi au katika mojawapo ya beti za katikati endapo mshairi ametumia kwa makusudi methali mbili au zaidi. Kwa hivyo, utungo huweza kuwa na idadi yoyote ya methali katika uwasilishaji wake.

Baadhi ya mashairi ya Kiswahili yamesawiriwa na yamewasilishwa kwa methali zaidi ya moja. Shairi la Abdalla (1973:89-110) 'Kutendana', katika *Sauti ya Dhiki* limebainisha mazingira hayo:

MWANAMUME
kama bure utanipa, nipa sinisumbuliye
kama hutaki 'takopa, nikulipe baadaye
Hivi sasa cha kukupa, sina; kweli nikwambiye
Mtu huwa hakutupa, amfaapo mwenziye (methali ya kwanza)

MWANAMKE
'Sina' kila siku 'sina', kwako I maisha
Huna siku utanena: ninacho 'kanirambisha?
Hiyo 'sina' yako Bwana, sasa ishanichokesha
Nyege ni kunyegezana, kwangu huba zinkwisha (methali ya pili)

MWANAMKE
Usemayo ni hakika, si urongo aswilani
Ni kwa kuwa nnachoka, kukufanyaa muhisani
Ndipo n'kabadilika, hakutowa maanani
Mjinga 'meerevuka, mwerevu u mashakani (methali ya tatu)
MAELEZO
Tamaa hakuitaka, akazidi bembeleza
Akasema yalopita, ni bora kunyamaza
Kuliko kuyafuata, na kisasi kulipiza
Yalopita yashapita, si vyema kuyaregeza (methali ya nne)

Ujumbe ambao umewasilishwa katika shairi hilo la 'kutendana' umehitaji kufafanuliwa kwa kuzingatia hoja mbalimbali. Hata hivyo, kinachobainika ni kwamba methali hizo

hushirikiana katika kuibua na kuendeleza zaidi ujumbe ambao umewasilishwa. Kwa mfano, mzozano uliopo baina ya mhusika Mwanamume na Mwanamke umepitia matukio mbalimbali hadi kufikia hali ya sasa. Hiyo ndiyo sababu ambayo imemfanya mtunzi kutumia methali zaidi ya moja, ambapo kila moja imeshikilia nafasi muhimu katika uchimuzi na udhihirishaji wa matukio. Katika methali ya mwisho, mshairi amejipa nafasi ya kutoa suluhisho la mgogoro uliopo.

Isitoshe, shairi hilo lina methali ambazo huweza kuainishwa kuwa ya awali, ya ndani na ya mwisho. Muktadha huo huweza kubainika katika uwasilishaji wa utungo iwapo mtunzi ametumia methali zaidi ya mbili. Ikiwa msanii ametumia methali mbili, basi ile ya kwanza huwa ya awali na ya pili huwa ya mwisho. Kilichodhihirika katika matumizi hayo ni kwamba, methali hizo hushikilia nafasi tofauti tofauti lakini zilizoshirikiana na zilizochangiana katika mtindo uliozingatiwa katika uwasilishaji wa shairi.

Methali ya kwanza iliyojitokeza, huwa ni ishara ya kuutanguliza ujumbe kwa matao ya chini. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mtunzi wa ushairi simulizi huuwasilisha utungo kwa ufahamu kuwa, kauli zilizoshirikishwa hutumiwa kiawamu kama silaha ili mawazo yaliyowasilishwa kuweza kutiririshwa kimantiki kuanzia mwanzo hadi mwisho (Propp 1968 na Lord 1960). Huo ni urasimi ambao pia ulioshirikishwa katika uwasilishaji wa tungo za ushairi wa Kiswahili ambao huzingatia arudhi za kimapokeo. Aidha, matumizi hayo humfanya mtunzi kupata mwau wa kujenga mandhari au muktadha wa kijumla katika uwasilishaji wa utungo. Mathalani, muktadha ambao huibuliwa huweza pia kuwa wa kihistoria au wa kijamii kulingana na uelekezo wa

anwani. Kwa mantiki hiyo, mshairi hana ulazima wa kutumia anwani yenye mwelekeo wa methali. Kwa hivyo, methali iliyotumiwa huwa ni kielekezo mwafaka kwa hadhira.

Kimsingi idadi ya methali zilizotumiwa katika utunzi na uwasilishaji, hutegemea idadi ya hoja au maudhui yaliyosawiriwa. Katika muktadha huo, hadhira hupata usuli wa mawazo ambayo huwasilishwa katika shairi. Zaidi ya hayo, muundo wake huweza kuibuliwa na kuelekezwa kupitia kwa methali iliyotumika. Kwa ambavyo, methali imejitokeza mwanzoni, huwa ni kauli au sentensi ya msingi zaidi katika uwasilishaji wa utungo. Kadhalika, mshairi huwa na hadhari kubwa katika uteuzi wa methali iliyotumiwa. Vile vile, methali ni ishara au matini mahususi ambayo hutawaliwa au imejikita katika kanuni za kimuundo. Kisemiotiki, matumizi ya ishara ya msingi ya lugha sharti ihusishwe na muktadha ambao umeibuliwa na umewasilishwa kwa wanaoshiriki mawasiliano (Scholes 1982 na Culler 1982). Kwa mujibu wa mtafiti, methali ya awali ndiyo huumua zaidi ilihamu ya hadhira ili kuanza au kuendelea kulisoma shairi linalowasilishwa.

Isitoshe, shairi linapokuwa na matumizi ya methali mbili, basi methali mojawapo huwa ya awali na nyingine inayotokea baadaye huwa ya tamati. Sawia na mwelekeo huo, mshairi aliyetumia zaidi ya methali moja basi methali hizo huweza kujitokeza kwa awamu kama vile ya awali, ya kati na ya mwisho. Kama ilivyokwisha kuelezwa hapo awali, shairi huweza kuwa na methali zaidi ya moja kutegemea idadi ya mawazo au hoja zinazowasilishwa. Kwa hivyo, si lazima shairi ambalo lina matumizi ya methali mbili liwe na matarajio ya uwepo wa methali ya tatu au zaidi.

Katika muktadha huo, shairi linapokuwa na methali mbili basi ya mwanzo hujitokez awali na nyingine huwa ni kauli ya kuhitimisha katika utungo. Kwa hivyo, endapo shair lina methali mbili katika uwasilishaji, basi ile ya pili hujenga msingi wa kuendeleza waz lililoibuliwa kwa methali ya awali au wakati mwingine huweza kuibua hoja mpy ambayo huchangia zaidi hoja ya awali. Katika kiwango hicho, methali ya pili (au methal ambazo hupatikana baada ya ile ya awali) humfanya mtunzi kujenga msuko wa vitush ambao huibuliwa kitaharuki hadi kufikia kilele cha mgogoro. Endapo kumetumiw methali zaidi baada ya ile ya pili, methali hizo za baadaye hutenda kazi sawia na ile y pili lakini kwa kuendeleza na kufaragua zaidi kiini cha ujumbe ambao umewasilishw kabla ya ile ya tamati.

Kadhalika, methali ya pili au ya tatu inapotumiwa mwishoni mwa beti za mwish mwisho wa shairi, utendakazi wake huwa ni kuhitimisha, kutoa suluhisho, kuielekeza n kuifanya hadhira kutafakari zaidi hoja muhimu zilizokwisha kuwasilishwa hap mwanzoni. Kwa mtazamo wa mtafiti, methali ya awali na ya tamati ndizo za msing zaidi katika uwasilishaji wa utungo. Kwa sababu, mojawapo huutanguliza ujumbe n nyingine huutamatisha mjadala katika utungo. Zaidi ya hayo, methali ya pili katik muktadha wa matumizi ya methali zingine hujenga msingi wa taharuki wa kuusukum mbele ujumbe ambao huwasilishwa katika shairi.

Aidha, methali ya au za kati husaidia katika ubainishaji wa mkondo au mwelekeo wa mawazo yaliyoibuliwa. Mwelekeo ambao hucchukuliwa na mtunzi aghalabu hujitokeza kwa uwazi zaidi katika kauli msingi zipatikanazo katika beti za mwisho mwisho katik

shairi. Kwa hivyo, taharuki ambayo hujengewa huwa imechochewa kwa kuzingatia usaili na ufasiri (Gibbe 1995). Isitoshe, kwa kuzingatia matumizi hayo, mshairi hataki hadhira isitishe usomaji wake mwanzoni au katikati (pahali ambapo methali imetumiwa) bali hujengewa uchochezi wa hamu ili kuweza kuendelea kulisoma shairi lote ama kwa mwendo au udhibiti unaostahili. Matumizi ya methali ya pili iliyotokea katikati ya shairi humfunulia mwau msanii ili kuweza kuvyaza wazo, hoja mpya au kuendeleza na kukuza kwa makusudi mawazo ambayo tayari yalikwisha kuwasilishwa hapo awali. Kwa kutumia mifano tofauti tofauti iliyotofautiana lakini iliyopatikana au zilizopatikana katikati baina ya ile ya awali na ya mwisho husaidia zaidi katika kujenga na kuendeleza mawazo yaliyoibuliwa. Aghalabu, shairi huwasilishwa kwa zaidi ya methali moja huwa ni utungo mrefu ambao hushirikisha vitushi mbalimbali. Kwa mfano, mtunzi huenda ana ujumbe au maudhui changamano ambayo huhitaji kutolewa maelezo ya kina au pana. Kwa hivyo methali zilizotumiwa, husaidia katika kujenga ushikamano wa mawazo tofauti tofauti na kuyawasilisha kwa mtiririko au utaratibu uliostahili.

Kwa ambavyo mawazo ambayo huwasilishwa katika utungo mrefu ni mengi au changamano, huenda hadhira isiweze kufuatilizia kwa urahisi mkururo wa mawazo yaliyoibuliwa. Aidha, mshairi huyawasilisha mawazo hayo kiawamu huku akizingatia kauli teule ambazo hushikamanisha mawazo na kulifanya shairi kuwa na mtiririko usio chosha. Kwa hivyo, methali ya kati huteuliwa na hutumiwa kwa ustadi mkubwa siyo tu kama mbinu ya kuuthibiti usomaji bali pia kama mbinu ya kuudhibiti mwendo wa kimahadhi katika shairi. Katika muktadha huo, methali ya kati huifanya hadhira kuwa na kipindi au vipindi vya kuliajiri bongo ili kutafakari mawazo yaliyoibuliwa na pia

kujiweka tayari kupokea mawazo mapya. Huo ni ujenzi wa utafakari ambao huifanya hadhira kusaili kila kauli msingi ambayo imetumiwa katika uwasilishaji utungo kwa uelekezi wa methali iliyopo au zilizopo. Katika muktadha huo, mtunzi huweza kutumia mshabaha wa miundo ya methali ya awali au kwa kuzingatia miundo ya kauli za methali zilizofuatia.

Mtazamo wa mtafiti ni kwamba, shairi huweza kuwa refu na lenye beti au aya ambazo ambazo hufanana au hutofautiana kimuundo na kiumbo. Sawia na uwasilishaji wa utenzi, shairi hili husawiri maudhui ya kina na kwa uzingativu wa miundo tofauti tofauti ya lugha kulingana na tajiriba, ufundi au utashi wa mtunzi. Nayo methali ya mwisho, aghalabu hutokea kama kauli ya kulimatisha shairi. Kwa hivyo, si lazima matumizi hayo ya methali kutokea kama kibwagizo au kiishilio.

Methali ambayo imejitokeza mwishoni mwa shairi hutekeleza dhima ya kubainisha msimamo au mwelekeo wa mtunzi. Aidha, matumizi ya methali huufundika na huibulia muhtasari wa ujumbe ambao tayari umewasilishwa na umefafanuliwa kwa kina katika shairi kwa ujumla. Vile vile, matumizi yake huifanya hadhira kupata ishara au dira ya uelekezi na utafakari wa kijumla kuhusu mawazo yaliyowasilishwa hasa kwa kuyapatanishwa na tajiriba ya maisha katika jamii. Kwa njia hiyo, mawazo ambayo yamewasilishwa husaki na huacha athari kubwa katika akili ya msomaji wa shairi.
Kutokana na maelezo hayo kuhusu matumizi ya methali zaidi ya moja katika uwasilishaji wa ushairi wa *Ukimembi*, utungo huu huweza kuwa wenye sifa za kijumla zifuatazo:

i. Matumizi ya methali zaidi ya moja huweza kutumika katika utunzi na uwasilishaji. Kwa sababu, utungo huweza kuwa na dhamira au maudhui kuu na ndogo ndogo.

ii. Ushairi wa Kiswahili huweza kushirikisha sajili au miundo mbalimbali ya lugha hutegemea uelekezo wa kauli teule zilizotumika katika utunzi na uwasilishaji wake.

iii. Mawazo ya mtunzi husawiriwa na huwasilishwa kwa kuzingatia mbinu ya taharuki.

iv. Ushairi wa Kiswahili huwasilishwa kwa kuzingatia mtiririko au utaratibu maalumu ambapo kuna mwanzo, kati au ufaraguzi zaidi wa ujumbe na hitimisho.

v. Mawazo ya mshairi, ambayo ni ya kichangamano, huweza kusawiriwa na kuwasilishwa kwa kina kwa kuzingatia shairi refu.

vi. Mwendo, ridhimu na mahadhi huthibitiwa katika uwasilishaji wa shairi.

vii. Uwasilishaji wa ujumbe hujenga uhusiano wa karibu kati ya mtunzi na hadhira.

viii. Utunzi na ufaraguzi wa mawazo hupata mwelekeo kutokana na kauli teule za kimapokeo zilizotumiwa katika uwasilishaji.

ix. Muundo wa mizani na urari wa mizani huweza kubadilika kutegemea uelekezo wa kauli teule zilizotumika.

x. Uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili huzingatia fomula au mbinu za kisimulizi.

Kwa kuzingatia mashairi mahususi katika diwani zilizoteuliwa katika utafiti huu, sifa za ushairi wa *Ukimembi* zimeweza kubainishwa katika mashairi yafuatayo:

- Diwani ya **Sauti ya Dhiki**
  - (i) Shairi la 'Zindukani; (uk. 69-72)
  - (ii) Shairi la 'Kutendana' (uk. 89-110)

6.2.5 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali kama Kauli

Ushairi wa kitengo cha *Ukimeka* umejumuisha tungo ambazo hutumia methali kam kauli au kama mshororo mmojawapo kwenye beti au aya za utungo. Kimuundo, metha huwa zimekamilika kama ilivyodhihirishwa katika ushairi wa *Ukimemo* na *Ukimembi* a katika mawasiliano ya jamii. Kwa sababu hiyo, methali ambayo hutumika kama kau huweza kutajwa au isitajwe na mtunzi.

Kutokana na mashairi teule yaliyozingatiwa katika utafiti huu, matumizi ya methali kam kauli imeweza kudhihirishwa kupitia shairi la 'Nakumbuka Ulivyokuwa' katika diwa ya *Bara Jingine* (wa Mberia 2001:76-78). Kwa mfano, ubeti mojawapo katika shairi hil limewasilishwa ifuatavyo:

Nakumbuka ulivyohadithia
Huku matone ya machozi
Yakidondoka ndo! Ndo! Ndo
Kama kwamba yalikuwa yakikariri methali
Majuto ni mjukuu
Huja baadaye (Ubeti wa 77)

Kutokana na methali iliyotumika katika aya hiyo, hudhihirisha mwelekeo kwamb methali ni miongoni mwa kauli zingine zilizoibuliwa. Ingawa imetumiwa kushadid

ujumbe ulioibuliwa, matumizi yake yameweza kutekelezwa kupitia kwa kauli zingine zilizopo katika utungo. Kwa hivyo, hadhira haipaswi tu kuzingatia methali mahususi bali pia kauli zingine zilizotumika. Aidha, matumizi hayo huweza kuwasilishwa kwa uelekezo wa anwani iliyotumika. Matumizi hayo pia yamedhihirika kupitia kwa shairi la 'Kula Njama' katika *Chembe cha Moyo* (Mazrui 1988: 44-47) na shairi la 'Kesho' *Jicho La Ndani* (Mohamed 2002:74).

Katika muktadha wa ushairi huu, methali huweza kutumiwa jinsi zilivyo au kuongezewa maneno ya ziada, labda mwanzoni au mwishoni mwa kauli. Kwa hivyo, methali zilizoshirikishwa huwa zimeibuliwa kwa uelekezo wa anwani ambapo huweza kuwa ya methali au la. Methali zitumikazo katika utungo wa *Ukimeka* humfanya utungo kuwasilisha mawazo kiusambamba. Sawia na kauli au mishororo mingine katika ubeti au aya, matumizi ya methali huchangia katika kuibulia na kubainishia mawazo ya msingi kwa kuzingatia usambamba (Wamitila 2007 na Njogu 2004). Kauli ambazo hutumika katika usawiri na uwasilishaji wa ushairi huwa zimeteuliwa kwa ustadi mkubwa. Katika mantiki hiyo, kauli zote zilizotumika huwa ni za msingi na hushikilia nafasi muhimu katika shairi (Mutembei 2001 na Wanyoike 1976). Kwa hivyo, katika muktadha wa uwasilishaji wa utungo wa *Ukimeka*, mshairi huitarajia hadhira isizingatie tu methali hiyo iliyotumika bali izingatie pia kauli zingine muhimu zilizotumika katika harakati za ufasiri wa ujumbe ambao umewasilishwa.

Mtazamo wa mtafiti ni kwamba, methali ni miongoni mwa kauli za muhimu katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Kwa sababu dhima yazo huweza kusetiriwa na

kutekelezwa kupitia kwa maudhui yaliyowasilishwa. Kauli zingine zilizotumiwa katika uwasilishaji wa utungo, husaidia katika kubainisha zaidi dhima ya methali. Kadhalika, kauli teule zilizoshirikishwa katika uwasilishaji wa utungo huo hujengeka katika tamathali za usemi. Kulingana na mihimili ya nadharia ya Semiotiki, mtunzi huwa hana ulazima wa kuzingatia kutumia arudhi zilizoruhusu urari wa vina na mizani katika uwasilishaji wa shairi kama zilivyoendelezwa na wanamapokeo wa ushairi wa Kiswahili (Sanka 1995). Kwa hivyo, methali huweza kutumiwa au zisitumiwe kwa uwazi katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili.

Isitoshe, methali ni miongoni mwa matini ambazo hutumika zaidi katika mawasiliano ya jamii. Kimatumizi, dhana moja huweza kuwasilishwa kupitia kwa ishara nyingine ya lugha kwa uzingativu wa mwelekeo na utashi wa msanii (Mosha 2002, Hawkes 1977 na Culler 1975). Kwa sababu, matumizi ya methali huweza yasiwe angavu lakini busara yake hudhihirishwa kupitia kwa maudhui yaliyoibuliwa katika utungo. Kwa hivyo, kauli zingine zilizobuniwa kibinafsi na kwa makusudi huwa ni za msingi katika ubainishaji wa maudhui kwenye tungo za ushairi. Kimtindo, methali ambazo hutumiwa katika muktadha wa uwasilishaji wa ushairi, hadhira hutarajiwa kurejelea na kutafakari kauli ambazo tayari zimeashirikishwa hapo awali au za baadaye ili ujumbe kuweza kubainishwa kwa uwazi zaidi. Kwa sababu, baadhi ya kauli hizo huweza pia kuwa za msingi katika uwasilishaji wa ujumbe katika ushairi wa Kiswahili (Mulokozi 1989 na Senkoro 1988).

Kutokana na matumizi hayo ya methali kama kauli, ushairi huo wa *Ukimeka* huweza kuwa na sifa zifuatazo:

i. Ujumbe huwasilishwa kiusambamba kwa kuzingatia miundo changizi au kauli zingine za lugha katika shairi.

ii. Kauli za kibnafsi huchangia katika ubuaji wa busara ya methali. Kwa hivyo, kauli zinazotumika katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi hazipaswi katu kupuuzwa.

iii. Mawazo huibuliwa kwa kuzingatia hisi za msanii na kwa mwelekeo wa mchomo alionao.

iv. Ufasiri, usaili na utafakari wa ujumbe uliowasilishwa huzingatia ushirika wa kauli zote za msingi zilizotumiwa katika shairi.

v. Matumizi ya kauli teule huwa ni msingi wa kubainisha mwelekeo na mtindo katika shairi.

vi. Kimtindo, kunga za utunzi na uwasilishaji wa shairi hubainishwa kwa uwazi zaidi. Kwa hivyo, ushairi kama utanzu ulio hai huweza kukuzwa ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ambayo hushuhuidiwa katika jamii.

Kwa kuzingatia diwani teule katika utafiti huu, sifa za ushairi wa *Ukimeka* zimebainishwa katika mashairi yafuatayo:

- Diwani ya **Chembe cha Moyo**
  i. Shairi la 'Kula Njama' (uk. 44-47)
- Diwani ya **Jicho La Ndani**
  i. Shairi la 'Kesho' (uk. 79)

- Diwani ya **Bara Jingine**

  i. Shairi la 'Nakumbuka Ulivyokuwa' (uk. 76-78)

6.2.6 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali kama Kibwagizo au Kiishilio

Kundi hili la ushairi limejumuisha tungo ambazo hutumia methali kama kibwagizo katika beti zake au kama kauli mwishoni katika shairi. Kibwagizo ni mshororo wa mwisho katika ubeti. Mshororo huo hukaririwa au hurudiwarudiwa katika miisho ya beti zote katika uwasilishaji wa shairi. Baadhi ya mashairi ya Kiswahili hutungwa kwa kuzingatia arudhi za kimapokeo ambapo kigwagizo ni mojawapo ya vipengele hivyo. Kwa mfano, shairi la 'Alie kwenda kaenda' (Snow-White 1974:11-12) limewasilishwa kwa beti nane. Kibwagizo kinachotamalaki katika shairi hilo ni *Alie enda kaenda, si sawa na mja nyuma*. Ubeti wa kwanza umebainisha jambo hilo muktadha huo, kuwa:

> *Alie kwenda hatuwa, si mwenzi si mshindani,*
> *Midhali amenyanyuwa, mguu umo njiani,*
> *Kwenda naye mwendo sawa, hili halipatikani*
> *Aliye kwenda kaenda, si sawa na mja nyuma* (Kibwagizo)

Kimsingi, kibwagizo huukariri zaidi ujumbe uliowasilishwa na pia kuhakikisha kuwa utungo unazingatia kaida za arudhi. Katika muktadha huo, shairi ambalo huwasilishwa huweza kubainishwa kwa muundo au bahari maalumu.

Hata hivyo, kuna baadhi ya mashairi ambayo hudhihirisha kubadilika kwa kibwagizo katika beti za utungo. Jambo la kuzingatiwa katika ushairi wa *Ukimeki* ni kwamba, utungo uwe na kibwagizo ambacho hutiririshwa kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. Tofauti na kibwagizo, kiishilio huwa ni mstari au kauli ya tamati katika ubeti au

kauli ya tamati katika utungo wa ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, kiishilio kama kauli huweza kubadilika badilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Kama ilivyopendekezwa katika muktadha wa uwasilishaji wa ushairi wa *Ukimembi*, methali zilizotumika huweza kujitokeza kama mshororo wa mwisho katika beti au kama kauli ya mwisho katika shairi ambalo limewasilishwa.

Kuna tofauti mbayo hujitokeza kati ya ushairi huu wa *Ukimeki* na mashairi ya *Ukimea*, *Ukimemo* na *Ukimembi*. Kwa mfano, katika ushairi wa *Ukimea* kuna matumizi ya methali moja au zaidi ambapo si lazima kuwe na mtiririko wa matumizi yake au yazo. Kadhalika katika ushairi wa *Ukimemo*, kuna matumizi ya methali moja ambapo huweza kutumiwa popote katika muktadha wa utungo uliowasilishwa. Aidha, anwani iliyotumika si lazima iwe ya methali. Katika ushairi wa *Ukimembi* huwa kuna matumizi ya methali zaidi ya moja ambazo huchangiana na hukamilishana. Kwa kutumia methali kama mtindo wa uwasilishaji katika utungo wa *Ukimeki*, mshairi hubainisha kiufundi viishilio vya beti au viishilio vya ushairi ili kuukariri zaidi ujumbe uliowasilishwa. Kwa hivyo, mawazo ambayo huwasilishwa hupata mwelekeo na ushikamano wa hoja zizoibuliwa na pia hudhihirika kwa uwazi zaidi.

Vilevile, matumizi hayo ya methali huuthibiti uwasilishaji na usomaji wa shairi kimdundo, kiridhimu na kimahadhi. Kwa hivyo, baadhi ya mashairi ya Kiswahili huweza kuimbika kwa kuzingatia mpangilio maalumu wa mizani na urari wa vina (Noor 1988 na Kandoro 1982). Kwa sababu, dhima kuu katika ushairi wa Kiswahili ni kuburudisha na wakati uo huo huwasilisha ujumbe adhimu kwa hadhira (Abdallah 1990,

Knappert 1979 na Allen 1971). Katika muktadha huo, shairi hujengewa ukariri ambao hulifanya kuweza kuimbika, kughaniwa na kusomwa kwa sauti au kimoyomoyo.

Isitoshe, shairi ambalo husawiriwa na kuwasilishwa kimaandishi, hunuiwa kusomwa kwa sauti ili mahadhi na ujumi wa lugha kuweza kudhihirika (Mwamzandi 2002 na Wanyoike 1976). Hiyo hutokana na mpangilio mahususi wa mishororo, urari wa vina au kauli teule zilizotumika katika uwasilishaji wa utungo. Kwa kiasi fulani, matumizi hayo husaidia kuthibiti umbo na muundo wa shairi. Kwa ambavyo methali zina miundo mahususi, baadhi ya mishororo iliyoshirikishwa katika utungo, husaidia katika kuzingatia mpangilio wa mizani na urari wa vina. Kwa sababu ya kushirikishwa kwa matumizi ya methali, baadhi ya mashairi huweza kuwa na miundo na maumbo maalumu. Katika muktadha huo, mashairi hayo huweza kuainishwa zaidi kimakundi kwa kuzingatia maumbo au bahari katika uwasilishaji wake (Babusa 2005).

Kadhalika, miundo ya mishororo au kauli teule zilizotumiwa katika uwasilishaji wa ushairi huweza kuelekezwa kinyumenyume kutokana na uwepo wa methali kama kibwagizo au kiishilio (Mazungumzo yangu na Rocha Chimerah, tarehe 19.11.2010). kimuundo kipengele cha kibwagizo ndiyo cha msingi zaidi kuliko kiishilio. Katika muktadha huo, matumizi hayo ya methali husaidia katika kujenga mikarara ya mishororo au kuibua mistari ambayo ina mshabaha wake katika muundo wa methali na inayotumika kama kibwagizo. Methali itumikayo kama kiishilio huuficha zaidi muundo wa shairi. Kwa sababu, humbidi msomaji awe wa kiwango cha juu katika kupangua na kupanga

upya mishororo inayopatikana katika beti za shairi. Kwa hivyo, mashairi haya ya *Ukimeki* huweza kuwa na anwani ambayo ina mshabaha wake katika methali iliyotumika.

Kwa uelekezo wa nadharia ya Semiotiki, methali ni dhana au ishara inayohitaji ufafanuzi kwa kuzingatia kifasiri cha ishara ambazo hupatikana katika utamaduni na uhalisi wa maisha ya jamii (Gesero 2009 na Wamitila 2008). Kwa sababu hiyo, ufasiri wa ujumbe uliowasilishwa katika shairi hurahisishwa kwa hadhira kupitia kwa uelekezo na urejeleaji wa methali iliyotumika. Aidha, msanii hujipa nafasi ya kutoa mifano tarajiwa katika ufafanuzi wa ujumbe au huweza kuiachia hadhira ifanye hivyo. Hata hivyo, hakuna ulazima wowote wa kutoa ufafanuzi a kina kuhusu ujumbe ambao umewasilishwa. Kwa sababu, hadhira hufahamu dhima na matumizi ya methali zilizoshirikishwa. Kwa hivyo, uwasilishaji na ufasiri wa ujumbe haupaswi kuwa wenye utata wowote kwa hadhira. Ingawa utata huo huweza kujitokeza katika uwasilishaji wa utungo kimafumbo, matumizi yake huchukuliwa kuwa ni mbinu ya kutoubainisha wazi ujumbe unaowasilishwa (Gibbe 1990). Kadhalika, falsafa na mwelekeo wa mtunzi hujikita katika mizungu ya matumizi ya methali hiyo katika mshororo wa mwisho wa ubeti au mwishoni mwa shairi.

Kama vile ilivyokwisha kuelezwa hapo awali, mshairi huweza kuitumia methali siyo tu kama kibwagizo bali pia kama kiishilio katika shairi. Mshairi anapofanya hivyo, huashiria kikomo au hitimisho katika uwasilishaji wa utungo. Isitoshe, kwa kutumia methali kama kiishilio; hitimisho la shairi huwa katika matao ya chini kiuwasilishaji. Hata hivyo, matumizi ya methali kama kauli msingi ya tamati hurutubisha na hukoleza muhtasari wa mawazo yaliyowasilishwa katika utungo. Kwa sababu, hapo awali mshairi

tayari amefafanua kwa kina mawazo ambayo yanahitajika. Katika muktadha huo, methali ambayo hutumiwa mwishoni mwa shairi husaidia zaidi katika kubainisha kiini cha ujumbe. Isitoshe, falsafa na msimamo wa mtunzi hubainika kupitia kwa kibwagizo au kimalizio. Hilo ndilo jambo ambalo kuutafautisha ushairi wa *Ukimeki* na ushairi wa *Ukimemo*. Kwa sababu, matumizi ya kibwagizo au kiishilio huacha athari kubwa katika akili ya hadhira.

Katika muktadha wa utunzi, methali iliyotumiwa huwa ni kielekezo mwafaka kilichoufumba muhtasari wa maudhui ambayo huibuliwa na huwaislishwa. Zaidi ya hayo, mshairi hupata fursa ya kuichochea akili ya hadhira ili itafakari zaidi ujumbe uliowasilishwa kwa kupatanisha na miktadha halisi ambayo hupatikana katika jamii. Kwa mujibu wa Kelly (2006) ni kwamba, matumizi ya methali na ufasiri wake hujikita katika miktadha mahususi ya utamaduni wa jamii ulizoziibua. Vile vile, nadharia ya Semiotiki huakisi kwamba, methali ni ishara ambayo ina maana nasibishi (Herafeld 1980 na Olsen 1973). Kwa hivyo, dhima ya methali huweza kufafanuliwa kwa kuzingatia miktadha ya utamaduni na uhalisi wa maisha katika jamii ya mtunzi. Kwa sababu, methali ni mojawapo ya vipengele muhimu katika utamaduni wa jamii (Maitaria 2008 na Wamitila 2005).

Kadhalika, matumizi hayo ya methali huufanya ujumbe uliowasilishwa kusaki katika tafakuri ya hadhira, siyo tu kwa wakati uliopo bali pia kuwa kauli rejelezi kwa wakati ujao. Kimsingi, ni vigumu hadhira kukumbuka mifano na maelezo yote muhimu yaliyotolewa lakini ugumu huo hurahisishwa zaidi kwa kuzingatia methali inayojitokeza

kama kibwagizo au kiishilio. Chambilecho Senkoro (1988), ushairi hutumia lugha ya mkato yenye kuelezea maudhui kwa muhtasari, na aghalabu huyaficha maudhui hayo ndani ya taswira na ishara. Kwa hivyo, methali kama kauli tamati husaidia katika kujenga mbinu ya viona nyuma ili kuifanya akili ya mpokezi kuupatanisha ujumbe uliowasilishwa na miktadha mbalimbali ambayo hupatikana katika utamaduni wa jamii.

Kwa kuzingatia mashairi teule yaliyochanganuliwa katika utafiti huu, matumizi ya methali kama kiishilio huweza kubainishwa kupitia kwa shairi la 'Usijiangamize' (Mazrui 1988:9). Katika shairi hilo, methali imetumika kama kauli ya mwisho katika utungo kama ifuatavyo:

Usiwe ni mwenye chongo,
Kutoona, kutohoji
Upatilize udongo
Ungali na maji yake

Katika muktadha wa matumizi ya methali hiyo, mshairi amebainisha kwa uwazi mwisho wa shairi na vile vile, kutoa muhtasari wa ujumbe katika utungo unliowasilishwa. Isitoshe, methali hutumiwa kama mbinu ya kuitafakarisha zaidi hadhira. Kimaudhui, matumizi hayo katika muktadha wa ushairi wa *Ukimeki* huwa ni njia mojawapo ya kuutoa ushairi wa Kiswahili katika ufinyu wa kimaono na kiuchambuzi wa kimaudhui ili utungo kuweza kushirikisha mtazamo mpana uliojengeka katika tajiriba ya utamaduni na uhalisi wa jamii.

Kutokana na uelekezo huo, ushairi wa kitengo cha *Ukimeki* huweza kushirikisha sifa bainifu zifuatazo:

i. Methali kama ishara au matini muhimu, huwa ni ya msingi katika utunzi na pia huwa ni kichocheo cha kuitafakarisha hadhira.

ii. Maudhui yaliyoibuliwa na yaliyowasilishwa huweza hupatanishwa na utamaduni na uhalisi wa maisha katika jamii.

iii. Ufasiri wa ujumbe uliowasilishwa hupata uelekezo kupitia kwa ishara mahususi zilizoteuliwa kwa uzingativu tajiriba ya hadhira.

iv. Matumizi ya methali ni angavu zaidi kuliko kauli zingine zilizotumiwa katika uwasilishaji wa utungo. Kwa hivyo, matumizi hayo huwa ni kurunzi ya uelekaji wa mawazo muhimu ambayo huwasilishwa.

v. Ujumbe wa mshairi hukumbukwa na huhifadhika kwa urahisi zaidi katika taamuli ya hadhira.

vi. Kimuundo, utungo huwasilishwa kwa kuzingatia mahadhi na ridhimu kutokana na uwepo wa methali.

vii. Umbo mahususi la utungo hudumishwa hasa kwa kuzingatia kibwagizo.

Kwa kuzingatia mashairi katika diwani zilizoteuliwa katika utafiti huu, sifa za ushairi wa *Ukimeki* hudhihirika kupitia kwa mashairi yafuatayo:

- Diwani ya **Usanifu wa Ushairi**
  - (i) Shairi la 'Subira' (Uk. 6 – 7)
  - (ii) Shairi la 'Alie Kwenda Kaenda' (Uk. 11 – 12)
  - (iii) Shairi la 'Mganga Hatajiganga' (Uk. 53 – 54)
  - (iv) Shairi la 'Umoja Ni Ngome Kuu' (Uk. 111 – 112)
- Diwani ya **Chembe cha Moyo**

(i) Shairi la 'Usijiangamize' (Uk. 9)

6.2.7 Ushairi wa Kiswahili Unaotumia Methali kama Mwangwi

Imependekezwa kuwa kitengo hicho cha ushairi wa Kiswhaili kijumuishe tungo ambazo hazina kabisa matumizi ya methali katika uwasilishaji wake. Kama ilivyokwisha kuelezwa hapo awali kuwa, 'mgogoro' katika ushairi wa Kiswahili uliweza kuendelezwa rasmi wakati ambapo baadhi ya watunzi wa ushairi walipoanza kutunga tungo ambazo hazikujikita zaidi katika arudhi za kimapokeo. Kwa mfano, mwishoni mwa miaka ya 1960 na hasa mwanzoni mwa miaka ya 1970, walitokea 'watundu' watatu: Hussein (1970), Kezilahabi (1974) na Angira (1970). Baadaye kikundi hiki kilipata wafuasi wengine kama vile: Mulokozi na Kahigi (1973), Mutiso (1986) na Mberia (1997). Hawa walitunga na kuwasilisha kimaandishi tungo zao bila kujali au kuzingatia arudhi za kimapokeo ambazo zilichukuliwa kuwa ni 'roho au uti wa mgongo' katika ushairi wa Kiswahili (Njogu na Chimerah 1999 na Senkoro 1988). Mgogoro huo ulijikita katika kutumia au kutotumia vipengele vya arudhi za kimapokeo kama vile mizani na urari wa vina kuwa ni uti mgongo katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili (Walibora 2007, Njogu 1998 na Senkoro 1988). Kwa sababu, baadhi ya wahakiki wa fasihi katika wakati wa sasa wana mwelekeo kuwa ushairi wa Kiswahili haukupaswa kuelekezwa kwa uzingativu wa vina na mizani maalumu katika utungo. Kulingana na mawazo hayo ni kwamba, kuna hatari ya kuudumaza utungo huo.

Mawazo hayo yaliweza kuibua hisi na mielekeo tofauti tofauti miongoni mwa baadhi ya watunzi na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili. Kadhalika mitazamo hiyo ilibua mirengo

miwili ya kimwelekeo: wale walioshikilia mno na wale wasioshikilia zaidi kuwa urari wa vina na idadi maalumu ya mizani ni mambo ya lazima katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Kila kikundi cha washairi kilishikilia msimamo wake (Kimaro 2008, Sanka 1995, Mulokozi na Kahigi 1979). Kwa wakati wa sasa, mashairi yaliyotungwa kwa mitindo na mitazamo hiyo miwili yamekubalika kuwa ni tanzu za ushairi wa Kiswahili. Kulingana na Babusa (2005) na Gibbe (1998), tungo hizo ni tanzu za ushairi wa Kiswahili.

Kwa mujibu wa mtafiti, tungo hizo ni sura mbili za sarafu moja ambazo hujengana na hukamilishana, ingawa kwa uzingativu wa mitindo na sajili tofauti tofauti. Kimsingi, hii leo Kiswahili si lugha ya Waswahili kama jamii ya pwani tu kama ilivyokuwa katika karne mbili zilizopita ila matumizi hayo yameimarishwa na kuwa chombo cha kuwasilishia utamaduni wa jamii ya Afrika Mashariki kwa ujumla (Kimaro 2008 na Kahigi na Mulokozi 1979). Kwa hivyo, mabadiliko hayo pia yaliweza kuwa yenye athari kubwa katika utunzi na uwasilishaji wa tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiswahili hususa, ushairi wa Kiswahili (Wafula na Njogu 2007 na Chacha 1987). Katika muktadha huo, ushairi wa Kiswahili ni utungo wa jamii ya Afrika Mashariki na kwa jamii zote zilizotumia Kiswahili kama chombo cha mawasiliano miongoni mwao. Ingawa kwa sasa makabiliano hayo si makali au huendelezwa kichinichini, ushairi huru umekubalika na umeendelea kuzishughulisha kalamu za watunzi wa pwani na hata bara. Kama chombo kisuluhishi, methali huweza kutumika kama kipengele cha kushirikishia mielekeo hiyo miwili katika ushairi wa Kiswahili. Katika muktadha wa nadharia ya Semiotiki, dhima ya ishara moja huweza kupata mshabaha au utekelezwaji wake kupitia kwa ishara

nyingine zinazopatikana kwa urahisi katika jamii (Hawkes 1977). Kadhalika, kutumiwa kwa uwazi au mwangwi wa methali katika uwasilishaji wa utungo huweza pia kuzua na kuendeleza mgogoro katika muktadha mpana wa ushairi wa Kiswahili.

Kulingana na mtazamo wa mtafiti, na uwasilishaji wa mashairi huweza kuwa yenye maumbo na miundo iliyotofautiana lakini yenye kutekeleza dhima sawa ya kuuimarisha na kuustawisha utanzu huo wa fasihi. Hoja hiyo ina mshabaha wake katika maelezo ya King'ei (2007) na Khan (1975) kwamba, mshairi anapotunga shairi la Kiswahili huwa na lengo la kumvutia msomaji wake. Kwa hivyo, mshairi huwa mwenye hadhari zaidi katika kuteua kauli za lugha ambazo huzishirikisha ili shairi lisije likakinaisha. Kwamba, mshairi anapokabiliwa na hatari hiyo ya kuichosha hadhira, huanza kulipamba shairi kwa kutumia kunga mbalimbali za lugha ambazo hutokana na tamathali za usemi. Katika muktadha huo, huweza kwa hiari kutotumia kwa uwazi methali na kuibua matumizi ya kauli zingine mahususi za lugha ambazo hujibainisha pia katika tamathali za usemi.

Matumizi ya kauli hizo zilizoibuliwa kibinafsi huweza pia kujenga msingi wa kuuwasilishia tungo kijazanda, kiisitiari, kitaashira, kitaswira na kimafumbo (Akporobaro 1994 na Gibbe 1990). Kwa sababu, uwasilishaji wa ujumbe katika utanzu wa fasihi hususa, ule wa ushairi huwa hauna fasiri moja. Kama ilivyoelezwa katika sura ya pili ya tasnifu hii, matumizi ya methali huwa yenye maana ya kijuujuu na batini. Hata hivyo, maana mahususi ambayo imekusudiwa huweza kubainishwa zaidi kupitia kwa muktadha mahususi ulioibuliwa na mtunzi. Kwa hivyo, ufasiri huo hutegemea jinsi mtunzi alivyoufumba ujumbe na jinsi mpokezi alivyolikabili shairi hilo tangu mwanzo; mradi tu

kuweza kuthibitishia hoja zake kwa mifano dhahiri iliyotokana na miktadha halisi katika utamaduni wa jamii. Kwa hivyo, ushairi wa Kiswahili huweza kuwasilishwa kupitia kwa kauli au miundo tofauti tofauti ya lugha ambazo hushadidia dhima ya methali. Isitoshe, usomaji wa ushairi wa Kiswahili haukamiliki pasipo hadhira ya kuupokea ujumbe au maana inayokusudiwa. Kwa sababu, kauli teule ambazo hutumika katika uwasilishaji wa ushairi, huifinya au huipanua maana ambayo imewasilishwa.

Baadhi ya watunzi wa ushairi huru wa Kiswahili wamekuwa na mawazo kwamba, lugha ambayo hutumika katika uwasilishaji wa tungo zao huwa ni ya 'kawaida' kwa azma ya kuuleta ushairi karibu na watu wa kawaida katika jamii (Kezilahabi 1974). Dhana ya 'kawaida' hapa kama ilivyotumiwa na baadhi ya watunzi na wahakiki wa kifasihi ina utata. Kwa sababu, baadhi ya mashairi ambayo yametungwa na 'watundu' au 'wanamabadiliko'hao yana kiwango fulani cha ugumu na ufasiri. Kimsingi, mashairi hayo hukusudiwa kusomwa na tabaka la wasomi hususa, wanafunzi wa vyuo vikuu au wenye uwezo wa juu wa kiufasiri. Kimatumizi, mpangilio usio wa kawaida ni kivutio cha udadisi zaidi kuliko lugha ya kawaida (Mulokozi 2008). Hilo hutokana na hoja kwamba, kauli zilizoteuliwa na kutumiwa katika mawasiliano ya jamii husisitiza zaidi vipengele fulani vya hisi na mawazo ya mwasilishaji (Parker 1974). Katika muktadha wa shairi, ujumbe ambao huwasilishwa si wa kidhahania bali pia kauli zilizotumiwa hubainisha hisi za mtunzi kuhusu yale aliyoathirika nayo katika uhalisi wa maisha.

Ushairi uliotumia methali huuweka ujumbe ambao umewasilishwa katika muktadha wa utamaduni uliozoeleka katika jamii. Kwa sababu, methali zilizotumiwa katika

uwasilishaji wa ushairi, ni kauli ambazo zimesheheni hekima na busara ya jamii. Kama alivyo mtunzi mahiri wa fasihi, mshairi asiyetumia methali huwa haridhiki katika kutumia miundo ya lugha ambayo imekuwepo tu katika mapokeo ya jamii (mazungumzo yangu na Chimerah, tarehe 19.11.2010). Kwa hivyo, mshairi huhiari kuibua na kushirikisha miundo mipya na kwa uelekezo wa hisi zake ili kuutoa utungo huu kutoka kwa miundo ya lugha iliyozowewa. Kwa kufanya hivyo, huupa utungo upya wa kiuchambuzi, kimaono na kimtazamo katika uwasilishaji wake.

Kwa mujibu wa mtafiti, miundo ya lugha iliyozoweleka katika jamii huweza kuwa chakavu, ambapo kimawasiliano hupuuzwa au huweza kuvyazwa upya ili iwe yenye uhai unaostahili. Jambo la muhimu lipaswalo kuzingatiwa kwa watunzi na wahakiki wa ushairi huru wa Kiswahili ni kubainisha zaidi sifa za kimsingi katika uwasilishaji wa utungo wake. Kwa mfano, ushairi wa kimapokeo una sifa zake zinazoubainisha kinyume na hali ilivyo katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi huru. Swali ambalo huweza kuulizwa ni kwamba:

- Iwapo mtunzi wa ushairi huuwasilisha utungo wake pasi na kuzingatia arudhi za kimapokeo ni ushairi huru?

Kimsingi, ushairi kama utanzu wa fasihi ni sanaa iliyo hai. Kadhalika, mabadiliko ya kijamii huweza kudhiri madhiri yanajibuliwa na fani zinaytumika katika uwasilishaji wa utanzu huo. Hata hivyo, ugumu au wepesi wa uwasilishaji na ufasiri katika ushairi wa Kiswahili hutegemea kauli mahususi zilizotumiwa. Katika muktadha huo, ushairi huweza ama kutumia au kutotumia kwa uwazi methali na wakati uo huo

ujumbe huwasilishwa kwa mwafaka uliostahili (mazungumzo yangu na Chimerah, tarehe 19.112010 na Ogolla, tarehe 22.11.2010). Isitoshe, uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili usiotumia methali, hutumia kauli teule za lugha ambazo husaidia kuusetiri ujumbe ambao huweza kupatanishwa na methali yoyote inayopatikana katika jamii.

Sawia na matumizi ya methali katika utungo na uwasilishaji wa ushairi wa *Ukimemwa*, ujumbe ambao huibuliwa huweza kufasiriwa kwa uzingativu wa utamaduni na uhalisi wa maisha katika jamii husika. Kwa sababu, ujumbe ambao huwasilishwa huakisi mojawapo ya methali zilizopo katika jamii. Vilevile, lugha ya ushairi hutumia vipengele ambavyo hujenga na huchochea usaili na utafakari katika akili ya hadhira. Mtazamo wa mtafiti ni kwamba, japokuwa utungo wa *Ukimemwa* hautumii methali yoyote mahususi, maudhui ambayo huibuliwa huweza kuwa yenye mwangwi wa methali uliotawala na uliohisika (Mazungumzo yangu na Senkoro, tarehe 23.09.2010). Aidha, hadhira huachiwa jukumu la kuupatanisha ujumbe ambao huwasilishwa na methali yoyote waipendayo. Hata hivyo, methali hiyo lazima iwe imepatanishwa vizuri na ujumbe kusudiwa.

Kwa mfano, shairi la 'Mruko wa Nyuki' katika *Bara Jingine* (Mberia 2001:20-25) limejenga muktadha huo wa mwangwi wa methali. Kwa hivyo, shairi hilo halina matumizi ya wazi ya methali, labda kutokana na muundo na mtindo wa kiuwasilishaji au kutokana na utashi wa mtunzi. Hata hivyo, mwangwi huo umetawala katika uwasilishaji wa maudhui. Shairi hilo limewasilishwa kimchoro, ambapo taswira ya kimaono iliyoibuliwa ni ile ya jamii ambayo hapo awali ilikuwa yenye ushikamano na ushirikiano.

Baadaye, ushikamano huo uliathirika na kusambaratika kutokana na utamaduni wa kigeni. Hatimaye, wanajamii walihamasishana na kuurejelea msingi wa utamaduni wao wa awali. Katika hali hiyo, mshairi amedhihirisha swala hilo kwa uelekezo wa mchoro na pia kupitia kwa jinsi alivyobainisha utege katika baadhi ya maneno yaliyotumiwa (Taz. Sura ya tano kwa maelezo zaidi). Kupitia kwa maelezo yaliyowasilishwa, hadhira huweza kujenga mwelekeo fulani kwa kurejelea methali yoyote ambayo hustahiki. Kwa mfano, methali kama: 'Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu' au 'kidole kimoja hakivunji chawa', huweza kusadifu katika kuupatanisha ujumbe uliowasilishwa. Hata hivyo, upatanisho huo huhitaji utafakari na uzingativu wa methali zilizopo katika utamaduni wa jamii. Kwa njia hiyo, hadhira hushirikishwa kiustadi katika upokezi wa ujumbe.

Kwa ambavyo methali ni kauli ambazo zimezoweleka katika jamii, huweza kutumika pia katika utunzi na uwasilishaji wa mashairi mengi ya Kiswahili ya hapo awali na hata ya sasa. Mtunzi wa ushairi wa *Ukimemwa* humwachia msomaji kuupatanisha ujumbe ulioibuliwa na methali yoyote maarufu anayoitaka. Hiyo ni demokrasia au uhuru ambao hadhira hujengewa. Katika muktadha huo, msomaji hushirikishwa kikamilifu katika harakati za upokezi wa ujumbe. Isitoshe, methali ni misemo au kauli fupi yenye hekima fulani na hudhihirisha mkusanyiko na mafunzo waliyoyapata watu wa vizazi vingi vya jumuiya fulani katika maisha yao (Ndungo 1998). Kwa mintarafu hiyo, methali huwa ni sehemu moja ya lugha ambayo huweza kusawiri na kubaini falsafa na matamanio ya jamii kuhusu maisha kwa jumla. Hadhira nayo, huweza kuichopoa yoyote na kuipatanisha na ujumbe ambao umewasilishwa.

Kimaudhui, methali zimesheheni tajiriba ya jamii ambapo kila tamko au tendo linaloshuhudiwa katika jamii huweza kupatanishwa na kauli mahususi ya methali (Wafula 1994). Uhalisi huo hudhihirisha kuwa, uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili huweza kuzingatia au kutozingatia baadhi ya kauli ambazo zimekuwa zikirithishwa kimapokeo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa hivyo si shuruti kwamba, ushairi wa Kiswahili kuweza kuwasilishwa kwa maumbo, miundo na mitindo ya lugha ile ile ya miaka nenda miaka rudi. Kadhalika, kauli ambazo zimekuwepo katika mawasiliano ya jamii kwa muda mrefu huweza kuwa chakavu na kushosha. Kwa sababu hiyo, kizazi cha sasa na hasa vijana hupendelea mno kauli ngeni ambazo huweza kuwasilishia mawazo mapya yenye mshabaha katika tajiriba zao za maisha. Kwa hivyo, mshairi huweza kuzua mtindo au mizungu ya uwasilishaji ili kuipa au kuzipa methali sura mpya.

Kando na hayo, busara katika ushairi wa Kiswahili huweza kuwasilishwa kupitia kwa kauli nyinginezo za msingi zilizobuniwa kibinafsi na watunzi kulingana na hisi au mchomo walionao katika uelekezo wa uhalisi wa maisha yao. Kwa sababu, dhana ya busara au hekima huwa katika mabadiliko ambayo huathiri mielekeo ya jamii hususa, katika ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, ushairi wa *Ukimemwa,* hudhihirisha mwelekeo kwamba; hakuna ulazima wa kutumia methali kwa uwazi katika uwasilishaji wake. Kama ilivyo katika sanaa yoyote ya fasihi, utungo au ushairi huelekezwa kwanza kwa hisi au mchomo wa msanii; baadaye hufanyiwa uteuzi wa fani mahususi ili kujenga mwafaka wa kuwasiliana na hadhira (Jilala 2008 na Njogu na Chimerah 1999). Katika muktadha wa uwasilishaji, utungo wa *Ukimemwa* huweza kuimarisha zaidi baadhi ya

vipengele vya lugha au kauli ambazo zimekuwa zikithaminiwa mno katika mapokeo ya jamii.

Endapo baadhi ya matumizi hayo ya miundo, mitindo au kauli za lugha zilizozoweleka zimefifia, zile maarufu zilizobuniwa kibinafsi na kwa makusudi kwa wakati wa sasa, zitastawishwa na zitatumiwa zaidi katika uwasilishaji wa tungo za kifasihi hususa, ushairi wa Kiswahili. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mbinu au fani mahususi ambazo hututumika katika uwasilishaji wa utanzu wa fasihi huweza kubadilika kwa kiwango fulani. Mwanzoni mabadiliko hayo ya kimtindo huweza kukabiliwa vikali na baadaye huzowewa pole pole na kukubalika (Woods 1971, Whallon 1969 na Nagler 1967). Kwa mfano, ushairi ambao huzingatia mno arudhi za kimapokeo umekuwa ukitumia methali kwa uwazi lakini ushairi huru husetiri matumizi hayo katika maudhui yaliyowasilishwa. Hayo ni mabadiliko ambayo hushuhudiwa kwa wakati wa sasa katika ushairi wa Kiswahili. Swali ambalo huweza kuulizwa ni kwamba: Hadhira ya sasa huupenda ushairi upi?

Sawia na kutotumiwa kwa methali kwa uwazi katika na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili kunaashiria mabadiliko ya kimtindo. Hivi sasa mashairi huru ya Kiswahili yamekubalika. Hiyo ndiyo sababu, hapo awali katika miaka ya sabini hapa Afrika Mashariki, ushairi huru wa Kiswahili ulichukuliwa kuwa ni utungo wenye mikiki na usiofaa. Ingawa kwa sasa 'mgogoro' huo haupo, huweza kuendelezwa chini kwa chini kwa kiwango fulani. Mtazamo wa mtafiti ni kwamba, 'mgogoro' pia huweza kutokana na mwelekeo finyu kuhusu kauli za kimapokeo. Aidha, ushairi wa Kiswahili si sugu na

hauna budi kubadilika kifani na kimaudhui. Kwa hivyo, mitindo mbalimbali ya uwasilishaji huweza kuzuka ili ikabiliane na mabadiliko hayo ya kijamii. Katika mkabala huo, ushairi wa *Ukimemwa* huweza pia kuwasilisha maudhui ambayo ni ya kidhahania lakini yenye chemichemi ya ufasiri katika utamaduni wa jamii.

Kutokana na maelezo hayo, ushairi wa *Ukimemwa* huweza kuwa na sifa zifuatazo:

i. Mbinu au fani za uwasilishaji si sugu, bali huweza kubadilika kulingana na mabadiliko ya mfumo wa utamaduni na maisha ya jamii.

ii. Mabadiliko ya kimtindo huweza kuiathiri mitazamo ya watunzi kuhusu kauli au matini zinazotumika katika uwasilishaji wa ujumbe katika ushairi.

iii. Hakuna ulazimu wa kutumia fani moja au kauli mahususi kama vile methali katika uwasilishaji wa ushairi. Hiyo ni kwa sababu, baadhi ya kauli msingi ambazo hueleweka katika jamii, huweza kujengewa mwangwi wake katika shairi.

iv. Sura au vijitanzu vya ushairi huweza kuwa ni njia mojawapo ya kubainisha mitindo mbalimbali ya sajili ya lugha ambayo hutumika katika na uwasilishaji.

v. Matumizi ya kauli za lugha zilizozoweleka katika jamii huweza kuvyazwa upya katika uwasilishaji wa shairi.

vi. Usaili na utafakari huwa ni nyenzo muhimu katika uwasilishaji na upokezi wa ujumbe.

vii. Hakuna njia moja mahususi ambayo huweza kutumika katika kuwasilisha hisi na mchomo wa msanii.

Kwa kuzingatia mashairi katika teule diwani zilizoteuliwa katika utafiti huu, sifa za *Ukimemwa* huweza hubainika katika mashairi yafuatayo:

- Diwani ya **Kichomi**
  - (i) Shairi la 'Mafahali Wapigana' (uk. 5)
  - (ii) Shairi la 'Nimechoka' (uk. 34 – 35)
  - (iii) Shairi la 'Kuchambua Mchele' (uk. 63)
  - (iv) Shairi la 'Hadithi ya Mzee' (Uk. 69 – 72)
- Diwani ya **Bara Jingine**
  - (i) Shairi la 'Hatujaaga Ndoto' (Uk. 4 – 5)
  - (ii) Shairi la 'Bara Jingine' (Uk. 10 – 16)
  - (iii) Shairi la 'Mruko wa Nyuki' (Uk. 20 – 25)

6.3 JEDWALI LINALOWASILISHA RUWAZA YA MATUMIZI YA METHALI KATIKA USHAIRI WA KISWAHILI

Lifuatalo ni jedwali ambalo limewasilisha ruwaza ya uainishaji wa ushairi wa Kiswahili. Uanishaji huo umezingatia dhima ya methali katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Mashairi hayo mahususi ni yale yaliyochanganuliwa katika utafiti huu.

	DIWANI YA *SAUTI YA DHIKI*	DIWANI YA *USANIFU WA USHAIRI*	DIWANI YA *CHEMBE CHA MOYO*	DIWANI YA *JICHO LA NDANI*	DIWANI YA *KICHOMI*	DIWANI YA *BARA JINGINE*
USHAIRI WA **UKIMEA**	2	-	-	2	-	-
USHAIRI WA **UKIMEMO**	-	-	1	1	-	-
USHAIRI WA **UKIMENU**	-	-	1	-	-	-
USHAIRI WA **UKIMEMBI**	2	-	-	-	-	-
USHAIRI WA **UKIMEKA**	-	-	-	1	1	1
USHAIRI WA **UKIMEKI**	-	4	1	-	-	-
USHAIRI WA **UKIMEMWA**	-	-	-	-	4	3

Kwa kuzingatia takwimu ya data za mashairi mahususi yaliyotokana na diwani sita za Kiswahili zilizochanganuliwa katika utafiti huu, ruwaza ambayo imejitokeza kupitia kwa jedwali hilo ni kama ifuatavyo:

(i) Ushairi wa *Ukimemwa* una asilimia 29%

(ii) Ushairi wa *Ukimeki* una asilimia 21%

(iii) Ushairi wa *Ukimea* una asilimia 17%

(iv) Ushairi wa *Ukimeka* una asilimia 13%

(v) Ushairi wa *Ukimemo* una asilimia 08%

(vi) Ushairi wa *Ukimembi* una asilimia 08%

(vii) Ushairi wa *Ukimenu* una asilimia 04%

Kwa hivyo, ruwaza ambayo imebainika kutokana na uchanganuzi mashairi yaliyozingatiwa ni kwamba, ushairi ambao huzingatia arudhi za kimapokeo ndiyo

ulioshirikisha zaidi matumizi ya methali kuliko ushairi ambao hauzingatii arudhi hizo. Katika muktadha huo, baadhi ya tanzu za ushairi wa Kiswahili zina upekee na sifa jumuifu katika utunzi na uwasilishaji wake. Hiyo ndiyo sababu ya kuwepo kwa ushairi ambao umezingatia mno methali nyingi, chache na ule ambao umezingatia chache zaidi. Hata hivyo, vijitanzu hivyo ni sura mbalimbali za ushairi wa Kiswahili.

6.4 KIISHILIO

Sura hii imebainisha kuwa ushairi wa Kiswahili umebadilika mno kwa upande wa kauli zilizotumiwa na maudhui yaliyowasilishwa. Kutokana na maenezi ya lugha ya Kiswahili kutoka pwani hadi bara, ushairi wa Kiswahili umekuwa ukitungwa na jamii mbalimbali za Afrika Mashariki na kwingineko. Kwa ambavyo utungo huo umestawishwa na umeimarishwa zaidi kimatumizi, umeweza kushirikisha mitindo mbalimbali katika utunzi na uwasilishaji wake.

Kadhalika katika sura hii, ushairi wa Kiswahili umeweza kupendekezewa kigezo cha kuuainishia kwa kuzingatia dhima ya methali. Isitoshe, katika uchanganuzi wa mashairi teule umebainisha kuwa matumizi ya methali bado yana nafasi muhimu katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi. Kwamba, matumizi ya methali huweza kuwa angavu zaidi au matumizi hayo hudhihirika kama mwangwi wa kurejelea. Kwa kuzingatia matumizi ya methali kama mbinu ya uwasilishaji katika mkabala wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi na ya Semiotiki, mashairi yaliyopatikana katika diwani sita zilizoteuliwa yameweza kuwekwa katika makundi matatu:

i. Ushairi wa Kiswahili unaotumia methali nyingi katika uwasilishaji wake.

ii. Ushairi wa Kiswahili unaotumia methali chache katika uwasilishaji wake.

iii. Ushairi wa Kiswahili unaotumia methali chache mno au usiotumia kabisa methali katika uwasilishaji wake.

Vile vile, kwa kuzingatia matumizi ya methali katika muktadha wa ushairi wa Kiswahili, utungo huo umeweza kuainishwa zaidi katika makundi saba mahususi.

Kwa mujibu wa mtafiti, kigezo cha methali kimetumika katika uainishaji wa makundi hayo ya mashairi ili kushirikisha maudhui yaliyoibuliwa, miundo, maumbo na mitindo ya utunzi, vipengele vya utamaduni vilivyorejelewa katika ufasiri wa ujumbe na mabadiliko ya kiwakati ambayo hushuhudiwa katika jamii. Kwa hivyo, matumizi ya methali yameweza kuuanisha ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia fani iliyotumika katika uwasilishaji na maudhui yaliyoibuliwa. Aidha, majina mahususi yametumika kuwa kitambulisho cha kila kikundi kama tanzu za ushairi wa Kiswahili. Ingawa ushairi wa Kiswahili umekuwa ukitungwa na kuwasilishwa kwa mitindo tofauti tofauti, mitazamo hiyo hupaswa kuchukuliwa kuwa yenye kujengana na kukamilishana.

Kuhusiana na mashairi yaliyojitoa nje ya arudhi za kimapokeo, si kwamba tungo hizo ndiyo bora zaidi. Kile kinachofanyika ni kuutoa utungo wa ushairi katika mazoea ambayo yana mwelekeo wa kuichosha hadhira. Vile vile, mitindo iliyotumika katika uwasilishaji huwa ni upenu wa kuukuza zaidi ushairi; la sivyo kizazi cha sasa na kijacho kitakuwa na mwelekeo finyu kuhusu ruwaza nzima ya sanaa hiyo ya Kiswahili. Kulingana na nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, ushairi wa Kiswahili umedhibitiwa zaidi kwa arudhi za kimapokeo. Hata hivyo, kwa kuzingatia nadharia ya Semiotiki, ushairi wa Kiswahili haujanyimwa uhuru ambao huruhusu mitindo mipya kushirikishwa. Pamoja na

kwamba ukale (ushairi unaozingatia arudhi za kimapokeo) una uzuri wake; huru (ushairi usiozingatia arudhi za kimapokeo) haupaswi kudharauliwa.

Jambo la muhimu ni kwamba, hadhira ya sasa isiudharau ushairi wa Kiswahili ambao huzingatia arudhi kimapokeo, kwani una historia ndefu iliyojikita katika misingi ya utamaduni na uhalisi wa maisha katika jamii. Aidha, wanaotunga kwa kuzingatia arudhi hawapaswi kushikilia kuwa ushairi wa Kiswahili haujaathiriwa na mabadiliko ya kimtindo katika uwasilishaji wake. Kwamba, watunzi wa ushairi huathiriwa kwa mazingira na kiumbiumbi cha wakati. Hilo si jambo geni kwa waandishi au watunzi wa ushairi wa Kiswahili, bali pia kwa wanadau wote ulimwenguni. Jambo lililo la muhimu ni: kwa nini watunzi wamezuka kwa mitindo mbalimbali katika uwasilishaji wa utungo huu? Aidha, methali ni tagaa muhimu katika uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili. Isitoshe, imedhihirishwa kwamba, matumizi ya methali hayajapitwa na wakati. Kiumbuji, matumizi hayo huweza kustawishwa na kuimarishwa kutokana na athari za mabadiliko ambayo hutokea katika utamaduni wa jamii. Kwa hivyo, ushairi wa Kiswahili ni kanzi ya matini teule za lugha na kunga mbalimbali ambazo hutumika katika uwasilishaji wake. Kwa hivyo, methali kama ishara au matini huwa zenye dhima kubwa katika muktadha wa utungo huu.

SURA YA SABA

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

7.0 UTANGULIZI

Sura hii imewasilisha hitimisho na muhtasari wa mambo muhimu yaliyozingatiwa katika utafiti huu. Matokeo ya utafiti pia yamefafanuliwa na yamebainishwa kwa kuzingatia maswali na madhumuni ya utafiti. Kadhalika, sura hiyo imetoa mapendekezo ambayo huweza kuwa kichocheo cha utafiti zaidi. Kwa sababu, ushairi wa Kiswahili una historia ndefu na ni utanzu mpana ambapo kuna mambo ya msingi yanayohusiana na utunzi na uwasilishaji wake.

7.1 Hitimisho na Matokeo ya Utafiti

Malengo ya utafiti yalikuwa ni kubainisha na kutathmini dhima ya methali katika uainishaji ushairi wa Kiswahili. Katika kutekeleza malengo hayo, mashairi teule ya Kiswahili yalichanganuliwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Fomula ya Kisimulizi na ya Semiotiki. Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi ilitumiwa katika kuelezea jinsi watunzi walivyotumia methali kama kipengele cha uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili. Nayo nadharia ya Semiotiki, ilitumiwa kufafanulia matini teule zilizotumiwa katika upokezi na ufasiri wa ujumbe uliowasilishwa katika tungo hizo.

Mashairi mahususi yaliyochanganuliwa katika utafiti huu ni yale yaliyopatikana katika hifadhi za diwani sita maarufu za ushairi wa Kiswahili ambazo zilitungwa hapa Afrika Mashariki kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1970 hadi wakati wa sasa. Katika kipindi hicho, mashairi mbalimbali yaliweza kutungwa ama kwa kuzingatia au kutozingatia

arudhi za kimapokeo. Katika muktadha wa maswali na madhumuni ya utafiti, tathmini ya data zilizochanganuliwa zimedhihirisha kuwa:

- Methali hutumika katika ushairi wa Kiswahili kama dira ya kuibulia hisi na uwasilishaji wa maudhui.
- Mashairi yasiyobainisha kwa uwazi matumizi ya methali huwa ni mbinu ya uwasilishaji ambapo dhima yazo husetiriwa katika maudhui yaliyoibuliwa. Kadhalika, hadhira hupewa nafasi ya kuuhusisha ujumbe uliowasilishwa na methali inayo au zinazosadifu. Huo ni mtindo ambao umetamalaki katika ushairi usiozingatia zaidi arudhi za kimapokeo.
- Kauli ambazo hubuiniwa kibinafsi au kwa makusudi husaidia katika ufafanuzi wa dhima ya methali katika mashairi ya Kiswahili. Aidha, husaidia kujenga mwangwi wa methali katika maudhui yaliyowasilishwa.
- Methali huweza kutumika katika uainishaji wa ushairi wa Kiswahili.
- Matumizi ya methali huufanya ushairi wa Kiswahili kuweza kufasirika katika muktadha wa utamaduni na uhalisi wa maisha ya watu.

Kadhalika katika utafiti huu imebainishwa kuwa, methali zimekuwa zikitumiwa mno katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Hata hivyo, dhima yazo huweza kuufanya utungo huu kuwa wenye mielekeo tofauti tofauti katika wakati wa sasa.

Katika kutathmini dhima ya methali, mashairi teule yaliweza kuchanganuliwa. Kwa hivyo, mashairi hayo yamewakilisha tungo zingine maarufu zinazopatikana katika kipindi kilichozingatiwa. Sura ya kwanza, imebainisha maswali ya utafiti na madhumuni na pia kudhihirisha jinsi mkondo wa utafiti ulivyofanywa. Sura ya pili, imefafanua baadhi ya

mambo ya muhimu yanayowaelekeza watunzi kutumia methali katika uwasilishaji wa tungo hizo. Jambo la msingi lililodhihirika ni kuwa miktadha, mchomo wa hisi za watunzi na uhalisi wa utamaduni wa jamii huchangia pakubwa katika uteuzi wa methali ambazo hututumiwa katika usawiri na uwasilishaji wake. Aidha, kutokana na matumizi mbalimbali ya methali zilizohusishwa, ushairi wa Kiswahili umeweza kugawanywa katika makundi matatu muhimu: ushairi unaotumia methali nyingi, ushairi unaotumia methali chache na ushairi unaotumia methali chache zaidi au usiotumia kabisa methali katika uwasilishaji wake.

Uchanganuzi wa mashairi teule katika sura ya tatu umebainisha kwamba, methali hutumiwa mno katika ushairi wa Kiswahili unaozingatia zaidi arudhi za kimapokeo. Kitengo hicho cha watunzi kimewakilishwa na mashairi mahususi yaliyopatikana katika diwani za *Sauti ya Dhiki* (A. Abdalla) na diwani ya *Usanifu wa Ushairi* (K.H.A Snow-White). Kilichotambuliwa ni kuwa, hali hiyo imetokana na uzingativu wa matumizi angavu ya kauli teule za kimapokeo ambazo hurithirishwa kimapokeo kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kutumiwa mno katika mawasiliano katika jamii.

Kutokana na umaarufu huo, kauli hizo zimeweza pia kutumiwa na washairi kuwa fomula ya upangaji na uwasilishaji wa mawazo. Kadhalika, kauli hizo zinazotumika ni pamoja na methali ambazo huwafanya watunzi kusawiri na kuwasilisha mawazo na pia kama kunga za kuudhibiti muundo na ridhinu katika sanaa hiyo. Kwa sababu hiyo, ushairi wa Kiswahili umekuwa ni hifadhi mwafaka ya utamaduni na falsafa ya jamii. Kwa hivyo, mtunzi huwa ni mwasilishaji wa mambo adimu ambayo hutokea au hushuhudiwa katika

jamii. Katika muktadha huo, methali huwa ni kauli muhimu katika uchimuzi na uwasilishaji wa hisi, maono na mawazo ya mtunzi.

Isitoshe, uchanganuzi wa mashairi hayo umedhihirisha kuwa methali katika tungo hizo huweza kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kujenga na kuibua kauli za kitamathali kama vile isitiari au taswira katika uwasilishaji wa mawazo yaliyofungamana kabisa na hisi zilizoibuliwa.
- Muundo wa shairi huweza kuzingatia arudhi za kimapokeo kama vile mishororo, beti, kibwagizo, idadi maalumu ya mizani na urari wa vina.
- Methali iliyotumika huwa ni kauli au mada ya msingi ambayo huwa ni dira au kurunzi ya uelekezaji wa ufaraguzi na upangaji wa matukio yanayowasilishwa.
- Huuweka utungo katika muktadha wa utamaduni na uhalisi wa maisha ya jamii.
- Mawazo huweza kuwasilishwa kwa kuchochea na kuibua taharuki.
- Shairi huwa na anwani iliyotokana na kauli ya methali.
- Maelezo na utafakari wa hoja hudhibitiwa zaidi kwa mbinu ya usambamba.
- Ujumbe au maudhui huwasilishwa kwa muhtasari, endapo methali imetumika kama kibwagizo au kiishilio.
- Hubainisha na hudhihirisha maono, falsafa au mwelekeo wa mtunzi.

Kimsingi, utekelezwaji huo hutokana na ufungamano wa maana iliyoibuliwa kwa uelekezo wa methali husika katika muktadha wa uwasilishaji wa ushairi. Aidha, uchanganuzi wa mashairi umebainisha kuwa, mtunzi huweza kushirikisha zaidi ya methali moja katika uwasilishaji wa utungo. Kwa hivyo, endapo mshairi ana mseto wa

mawazo humbidi kutmia methali zaidi ya moja. Hali hiyo, ndiyo husababisha kuwepo kwa tungo za ushairi ambazo hutumia methali zaidi ya moja. Vilevile, mtunzi anapotumia zaidi ya methali moja, kila moja hutekeleza dhima muhimu katika umbuji na uibushaji au uendelezaji wa mawazo yaliyoibuliwa. Hoja hiyo huafiki nadharia ya Semiotiki kwamba, utungo ambao hushirikisha kauli teule zaidi ya moja kama vile matumizi ya methali mbili au zaidi, husaidia katika kupata dira ya kuibulia, kushadidia na kuendeleza mawazo ambayo huwasilishwa.

Zaidi uendelezaji wa maudhui katika ushairi, maudhui hayo huchochewa kupitia kwa methali iliyo au zilizotumiwa hapo mwanzoni kama kidokezo cha hoja ambayo tayari imegusiwa au imewasilishwa. Isitoshe, katika utafiti huu imebainishwa kuwa, maudhui ambayo huibuliwa hukolezwa zaidi kupitia kwa matumizi ya methali ya pili au ile ya tatu ambazo huwiana na hushirikiana. Kwa hivyo, methali hizo huwa ni zile za ndani katika shairi. Kwa sababu, ile ya mwisho huashiria hitimisho katika shairi. Kadhalika, katika muktadha huo, matumizi ya methali moja huwa haikidhi mahitaji ya mtunzi. Kwa sababu, huenda msanii ana hoja mbalimbali zilizokinzana lakini kwa namna moja huchangiana katika uwasilishaji wa dhamira. Pia imetambuliwa kuwa, matumizi ya methali zaidi ya moja katika uwasilishaji wa ushairi ni mbinu ya kudhihirishia umahiri au uhodari wa usarifu wa lugha alionao mshairi.

Sura ya nne imedahili kuwa, methali ni miongoni mwa kauli muhimu katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Kwa sababu, ushairi wa kati hauzingatii mno arudhi za kimapokeo. Kwa hivyo, matumizi ya methali huweza kuibua kiwango fulani cha

muundo katika utungo. Vile vile, ushairi huo hunasibishwa na kunga zilizotumiwa katika uwasilishaji wake. Kwa hivyo, matumizi ya methali huweza ama kudhihirishwa kwa uwazi au dhima yazo kusetiriwa katika maudhui yaliyowasilishwa. Mwelekeo huo umedhihirika kupitia kwa mashairi mengi ambayo yamepatikana katika ya diwani za *Chembe cha Moyo* (A. Mazrui) na diwani ya *Jicho la Ndani* (S.A. Mohamed).

Isitoshe, utafiti huu umebainisha kwamba, baadhi ya watunzi hao huotea kwa mbali au hawataki kuziasi kabisa arudhi hizo za kimapokeo. Katika muktadha huo, watunzi huhiari kushirikisha kwa kiasi fulani arudhi hizo. Katika mantiki hiyo, huwa vigumu kutambua mwelekeo wa watunzi hao iwapo ni wa mrengo wa kimapokeo au huru. Isitoshe imetambuliwa kuwa, jambo hilo huwafanya watunzi hao kutokuwa na mwelekeo dhahiri wa kubainisha tungo zao.

Kadhalika, utunzi wa ushairi huo wa kati huwa na ithibati ndogo ya methali, hata pale ambapo methali zimepotumika, matumizi hayo si angavu kama ilivyobainishwa katika ushairi wa kimapokeo. Kwa hivyo, ushairi wa kati huwa ni daraja au dhihirisho la mabadiliko ya kimtindo katika ushairi wa Kiswahili ambapo si ya mshindo kama vile ilivyobainishwa katika ushairi huru.

Katika uchanganuzi wa mashairi teule yaliyopatikana katika diwani hizo, imetambuliwa kuwa methali ni miongoni mwa kauli muhimu zilizojengeka katika tamathali za usemi. Kwa hivyo, methali huweza kutumika sako kwa bako na kauli zingine. Katika muktadha huo, methali zilizotumiwa hupewa nafasi sawa na kauli zingine zilizoibuliwa kwa

makusudi katika uwasilishaji wa mashairi hayo. Kwa hivyo, utungo huweza kuzingatia au kutozingatia arudhi za kimapokeo katika uwasilishaji wake.

Sura ya tano, imetathmini dhima ya methali katika baadhi ya ushairi wa Kiswahili usiozingatia kabisa arudhi za kimapokeo. Mashairi mahususi yaliyozingatiwa ni yale ambayo yaliyopatikana katika diwani za *Kichomi* (E. Kezilahabi) na *Bara Jingine* (K. wa Mberia). Katika uchanganuzi wa mashairi hayo, imebainishwa kuwa matumizi bayana ya methali hayana ulazima. Aidha, methali hazitumiwi kwa makusudi bali dhima yazo husetiriwa katika ujumbe ambao huwasilishwa. Kwa sababu, mtunzi huitaka hadhira ipige mbizi katika usaili na utafakari wa ujumbe batini. Isitoshe, hiyo ni mbinu ambayo huhitaji umahiri wa kunga za uwasilishaji katika utungo. Hata hivyo zinapotumiwa, huzitokeza kama kauli miongono mwa zingine. Mwelekeo uliojitokeza katika ushairi huo ni kwamba, utungo uliotumia methali chache mno au usiotumia kabisa methali, haujatindikiwa katika uwasilishaji wa ujumbe wa muhimu uliokusudiwa. Kwa hivyo, mashairi hayo hayana dosari yoyote kwa upande wa uwasilishaji, tofauti zilizodhihirika ni za kimtindo na kimuundo na wala si za kimaudhui.

Kadhalika, katika utunzi na uwasilishaji wa mashairi hayo ni kwamba, kauli teule zilizobuniwa kibinafsi na kwa makusudi, ndizo hujenga kiumbiumbi cha kusetiri dhima ya methali. Hali hiyo, kwa kiwango fulani, ni tofauti na vile ilivyobainishwa katika sura ya tatu na ya nne kwamba, ushairi wa kimapokeo na wa kati hubainisha matumizi bayana ya kauli hizo za kimapokeo ambapo ni pamoja na methali. Hata hivyo, kauli hizo zilizotumiwa huwa ni zile ambazo hujibainisha zaidi katika tamathali za usemi ambapo

kiutendakazi ni sawa na matumizi ya methali. Kwa kuzingatia nadharia ya Semiotiki, kauli teule zitumikazo katika uwasilishaji wa ujumbe muhimu husaidia katika kujenga mafumbo, isitiari na taswira. Kwa hivyo, katika muktadha wa utunzi wa ushairi huru, matini ambazo husherekewa zaidi ni zile ambazo huumua ujumbe batini (kauli za kiisitiari) na wala si zile dhahiri zibainishazo kwa uwazi ujumbe (kauli za kimetonomia). Isitoshe, kauli hizo zilizotumiwa, huufanya utungo kuufumba zaidi ujumbe uliowasilishwa ili kuweza kufasirika tu kwa hadhira ya dhati.

Utafiti huu pia umethibitisha kuwa matumizi ya kauli zilizoibuliwa kibinafsi au kwa makusudi huchangia katika uumuaji wa mwangwi wa methali katika uwasilishaji wa ushairi huo. Katika muktadha huo, matumizi hayo ni mbinu mojawapo ya kuunasua ushairi kutoka katika kuimarisha zaidi kunga au mitindo ya uwasilishaji katika ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, dhima ya methali huimarishwa zaidi katika mizungu ya uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili na katu isichukuliwe kuwa hiyo ni njia ya kufifilisha matumizi ya methali katika utungo. Kwa sababu, methali zimekuwa zikichukuliwa kiholela kuwa ni vito vya kuibulia hekima au busara katika mawasiliano ya watu. Kwa kiwango fulani, hiyo ni dhima sahili ya methali. Kwa hivyo, utungo huo hubainisha zaidi mizungu ya methali katika ushairi wa Kiswahili. Kauli zilizobuniwa kibinafsi husaidia katika kuibulia mwangwi wa methali. Kwa hivyo, hutajirisha mno tambo la umbuji katika ushairi wa Kiswahili kwa upande wa isitiari na taswira zilizojengwa. Katika mantiki hiyo, huufanya ushairi uliowasilishwa kutajirika zaidi kimaono, kiuchambuzi na kiufasiri.

Kimsingi, matini ambazo hutumika katika uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili, kwa kiwango fulani, huweza kuwa ni za kimapokeo. Hata hivyo, matumizi hayo hayawi ya shuruti, kwa ambavyo mtunzi ana uhuru wa kubuni kauli za makusudi na pia huweza kuivyaza upya miundo iliyopo ili ili kuweza kutumika katika uwasilishaji wa utungo. Katika muktadha huo, mtunzi hulazimika kuteua na kutumia maneno au kauli kwa hadhari ili kuelekeza hisi na athari ambazo huibuliwa katika uwasilishaji wa utungo. Aidha matumizi ya kauli hizo, huufafanya ushairi kupata dira au beramu ambayo huongoza katika upangaji na ufaraguzi wa mawazo katika shairi. Kwa hivyo, mawazo huibuliwa kutokana na mchomo wa mtunzi. Kwa sababu hiyo, maudhui yaliyoibuliwa hufungamana siyo tu na miktadha ya mazingira bali pia na utamaduni uliomzaa, uliomlea na uliomkuza.

Vile vile, utafiti huu umeafiki hoja kuwa, methali na kauli nyinginezo zilizoibuliwa kibinafsi huwa ni ishara za uashiriaji wa vipengele muhimu katika utamaduni wa jamii. Kwa hivyo, kauli hizo hutekeleza dhima tofauti ambapo huchangiana katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Katika mazingira hayo, huweza kutumiwa pamoja na methali au kwa kuubeba ujumbe uliojikita katika utamaduni wa jamii. Mwelekeo huo ndiyo huwachochea au huwasukuma baadhi ya washairi wa Kiswahili kushirikisha kwa ubunifu kauli za kibinafsi katika uwasilishaji wa tungo zao.

Kadhalika, kauli hizo zinazobuniwa kibinafsi hujibainisha katika tamathali za usemi. Kupitia kwa matumizi hayo, hadhira hupata kielekezo cha kuufasiri ujumbe kiumithilishaji. Ingawa mtunzi wa ushairi wa Kiswahili huweza kuzitumia kauli hizo, ni

muhimu kuelewa kuwa husaidia katika kujenga na kufafanua mazingira yaliyoibua mwangwi wa methali kwenye utungo. Jambo hilo limedhihirishwa katika sura mbalimbali za tasnifu hii.

Aidha, imedhihirishwa kuwa, kuna mashairi ambayo yamejikita au hayajajikita katika arudhi za kimapokeo, ambapo hayakutumia kabisa methali. Mashairi mengi ya aina hiyo hupatikana zaidi katika kitengo cha ushairi huru wa Kiswahili. Hata hivyo, maudhui ambayo huwasilishwa, hutilia nguvu dhima na mwangwi wa methali katika shairi. Kwa hivyo, isichukuliwe kuwa watunzi wa ushairi wa Kiswahili wasiotumia methali huwa hawataki kutambua dhima ya methali katika tungo zao. Ingawa kauli hizo hazijibainishi wazi kuwa za kimethali kama zinavyofahamika katika jamii; zina sifa za umethali ndani yake. Hiyo ndiyo sababu mojawapo ambayo huwafanya baadhi ya watunzi wa ushairi huru kama vile Kezilahabi, Kahigi, Mulokozi, Hussein, Kinene wa Mutiso na Kithaka wa Mberia kutumia kwa makusudi kauli za kibinafsi ili iwe mizungu ya kuibulia dhima ya methali katika tungo zao.

Kinyume na ushairi wa kimapokeo na ushairi wa kati, kimtindo ushairi huru hupaswa kuchukuliwa kuwa utanzu ambao huulea na huukuza zaidi wa ushairi wa Kiswahili. Katika muktadha huo, baadhi ya watunzi wa ushairi huamua kwa makusudi kutotumia methali kwa uangavu katika uwasilishaji wa mashairi hayo. Aidha, maudhui ambayo yaliyowasilishwa huwa si ya moja kwa moja. Kwa mfano ushairi kama huo, humhitaji msomaji kutafakari na kusaili zaidi ili kuupata ujumbe uliowasilishwa kupitia methali ambayo haijadokezewa waziwazi. Kwa hivyo, watunzi hao hawataki hadhira iwe tuli

bali huitaka iwe tendi. Kwamba, wasomaji wa ushairi hupaswa kujitahidi katika kunoa bongo na kutafuta methali yeyote ambayo huafiki ujumbe uliowasilishwa.

Isitoshe, matumizi ya kauli za kibinafsi hupata umaarufu wake katika kipindi maalumu katika jamii; kipindi hicho kinapopita, hupisha kauli ambazo ni ngeni. Hali hiyo huuimarisha na huuweka ushairi wa Kiswahili katika muktadha wa sasa. Kwa hivyo, ushairi wa Kiswahili usiozingatia arudhi za kimapokeo au ushairi huru; kama ulivyojulikana, hauna wafuasi wengi wa kiutunzi na kiusomaji. Zaidi ya hayo, walengwa wa ushairi huru hutarajiwa wawe wenye uwezo mkubwa wa kiutafakari na kiuchambuzi wa matini. Kadhalika, hadhira kubwa ya ushairi huo huwa ni wataalamu au wasomi wa ngazi za juu kama vile wahadhiri na wanafunzi wa vyuo vikuu. Kadhalika watunzi na hadhira kubwa ya ushairi wa sasa wa Kiswahili hujinasibisha zaidi na tungo ambazo huzingatia arudhi za kimapokeo. Kwa sababu, ushairi wa kimapokeo umekuwa maarufu katika jamii za Afrika Mashariki na pia umekuwa ukitumiwa kwa kipindi kirefu hadi wakati wa sasa. Vile vile, ushairi huru ni kanzi ya mafumbo, taashira na isitiari. Kwa hivyo, hadhira huwa ni ile ambayo imemakinika katika stadi za isimu ya lugha na uchambuzi wa matini.

Mwishoni mwa miaka ya 1960 na mwanzoni mwa miaka ya 1970, ushairi huru wa Kiswahili ulipojitokeza, ulizua taharuki, mgogoro na malumbano makali kuhusu maana ya ushairi. Kadhalika, utungo huo ulibezwa na kupachikwa majina ya kashfa kama vile mauve, umasivina, ushairi wa kinathari, ushairi huru, ushairi guni miongoni mwa mengine. Pole pole mashairi hayo yalianza kukubalika shingo upande. Ingawa kwa sasa

utungo huo umekubalika kuwa utanzu wa ushairi wa Kiswahili, bado una safari ndefu hadi pale wapokezi watakapouzoea na kuukubali kwa dhati. Hata katika machapisho mengi ya magazeti ya Kiswahili ambayo hupatikana nchini Kenya na Tanzania kama vile, Taifa Leo na Taifa Jumapili (Kenya), Uhuru, Mzalendo, Nipashe na Kasheshe (Tanzania) huwa yenye ithibati kubwa ya ushairi ambao huzingatia zaidi arudhi za kimapokeo. Kwa hivi sasa, ni watunzi wachache mno ambao hutunga mashairi hayo. Kwa sababu, ule mshawasha uliokuwepo hapo awali wa kutunga tungo hizo, sasa umedidimia au umefifia. Kadhalika, vijana ambao wangeututumua na kuupeleka mbele utungo huo hawakujengewa msingi imara katika utunzi wala uwasilishaji wake. Kwa hivyo, watunzi ambao hutunga tungo hizo ni wale wale waanzilishi, ambapo kwa sasa, ni wazee au ni kikundi kidogo cha washairi. Kimsingi, mashairi hayo ni mazuri kiumbuji. Kwa sababu hayaendelezwi sana kwa wakati wa sasa; umaarufu wake huenda umefifia (Mazungumzo yangu na Chimerah, tarehe, 24.11.2011). Endapo kuna machapisho yoyote ya ushairi huru huwa ni machache mno; hata hadhira hiyo huwa ni finyu zaidi.

Vile vile, katika hafla mbalimbali za kijamii, kama vile sherehe za kitaifa au za kijamii, mashairi ambayo huwasilishwa na hughaniwa ni yale yaliyozingatia zaidi arudhi za kimapokeo. Kwa mfano, wiki ya Tamasha za Utamaduni wa Waswahili katika kisiwa cha Lamu (Kenya) kuanzia tarehe 24 hadi 28 Novemba 2010, ziliadhimishwa mno kwa mashindano ya ushairi. Kadhalika, jambo hilo lilishuhudiwa katika sherehe za maulidi huko Malindi tarehe 27 Februari 2011. Mashairi yaliyowasilishwa ni yale yaliyotungwa kwa uzingativu wa arudhi za kimapokeo. Pia, kilichoshuhudiwa ni kuwa, mashairi hayo yalishirikisha zaidi methali na kauli za kimapokeo katika uwasilishaji wake. Kwa sababu

mashairi hayo yamezoweleka, matokeo ni umaarufu wake miongoni mwa jamii. Kadhalika, katika eneo bunge la Kinondoni (Tanzania) baadhi ya wagombeaji eneo bunge na waliohudhuria walitumbuizwa kwa mashairi ya Kiswahili. Baadhi ya mashairi yaliyowasilishwa ni yale yaliyozingatia mno arudhi za kimapokeo (Haya yalishuhudiwa katika mojawapo ya kitongoji jijini Dar es Salaam, mnamo tarehe 16, Septemba 2010). Katika misingi huo, ushairi wa kimapokeo umejijengea sifa za umaarufu kuliko ushairi huru kutokana na kunga au kauli teule za kimapokeo zilizotumiwa katika uwasilishaji wake.

Hapo mwanzoni, mtafiti alikuwa na mawazo kwamba, ushairi huru wa Kiswahili hauna ithibati yoyote ya matumizi ya methali. Katika udurusu wa kina wa mashairi hayo, umebainisha kuwa kuna ithibati ndogo ya methali zilizotumiwa. Pia, katika uchanganuzi wa mashairi teule, imedhihirika kuwa matumizi ya methali yana nafasi kubwa katika muktadha wa kuibua umbuji wa maudhui. Kadhalika, udhibiti wa muundo ulijibainisha zaidi katika ushairi uliozingatia mno arudhi za kimapokeo. Pale ambapo methali zilitumiwa katika uwasilishaji, shairi huru huwa halibainishi athari kubwa katika uthibiti wa muundo. Muundo katika ushairi huru hudhibitiwa zaidi kupitia kwa viwango mbalimbali vya kiisimu kama vile mofolojia, fonolojia, sintaksia, semantiki, mpangilio wa maneno, michoro, taswira na viakifishi vilivyozingatiwa. Kwa kiasi fulani, vipengele hivyo hudhihirika pia katika mashairi ya kimapokeo. Mambo hayo ni ya msingi katika uelekezaji wa mahadhi na ridhimu katika uwasilishaji wa mashairi. Kwa hivyo, shairi la Kiswahili huwa lina umbo, muundo na pia sajili maalumu ambazo hutumika katika uwasilishaji wake.

Kama vile ilivyokwisha kuelezwa katika sura za awali na kukaririwa hapa ni kwamba, kutotumiwa bayana kwa methali katika mashairi huru haimaanishi kuwa watunzi hao maarufu hawafahamu au wamepuuzia umuhimu wa dhima yazo katika kuibulia na kuwasilishia maudhui. Kwanza, baadhi ya watunzi hao ni wakwasi katika taaluma ya isimu na lugha na pia ni wahakiki wasifika wa fasihi. Pili, washairi hao, ni hodari au magwiji katika udhibiti wa mbinu za utunzi na uwasilishaji, siyo tu katika ushairi wa Kiswahili bali pia katika ushairi mpana wa kilimwengu. Huo ni ushuhuda kutokana na ithibati ya tungo zao za ushairi ambazo hutungwa kwa ufanifu mkubwa wa kiumbuji. Tatu, watunzi hao wamekuwa na ujasiri mkubwa katika kuthibitisha kwa utaalamu kuwa, ushairi huru ni utungo kindakindaki ambao hustawisha na huendeleza ushairi wa Kiswahili.

Katika tasnifu hii imedhihirishwa kuwa, watunzi wengi wa ushairi huru wa Kiswahili hawatumii methali kiholela bali kwa makusudi. Kwa kufanya hivyo, hujipa uhuru wa kishairi na hujijengea mwau wa kujieleza kimafumbo, kiisitiri na kitaswira. Kadhalika, watunzi hao huipa hadhira fursa ya kunoa bongo zao ili kuweza kuhusisha maudhui na methali yoyote waitakayo ilimradi imefungamana vyema na ujumbe uliowasilishwa. Katika muktadha huo, ujumbe uliowasilishwa ndiyo huwa msingi wa utafakari na wa kujengea mwangwi wa methali katika mashairi hayo. Kwa hivyo, dhima ya methali huwa imesetiriwa katika kunga na maudhui ambayo huwasilishwa. Zaidi ya hayo, hadhira ya dhati haipati shida kung'amua tambo hilo la kiuchambuzi na kimtindo. Katika mantiki hiyo, baadhi ya mashairi ya Kiswahili yaliyotumia methali kwa uwazi huwasilisha maudhui kiusahili au kijuujuu zaidi hasa yanapolinganishwa na yale

yasiodhihirisha kwa uwazi matumizi ya methali. Kimsingi mashairi ambayo hutumia wazi methali, huilenga hadhira pana katika jamii: wale wenye ujuzi mkubwa wa kiuchambuzi na wale wenye ujuzi wa kadri; wote huuenzi utungo huo. Hata hivyo, kuna baadhi ya washairi hodari ambao huzingatia arudhi za kimapokeo. Kwa hivyo, huteua na hutumia methali kwa hadhari katika tungo zao. Matumizi hayo huhakikisha kuwa shairi huwasilishwa kitaashira, kitaswira na kiisitiari ili ujumbe. Kwa hivyo, ujumbe ambao huwasilishwa huweza kusetiwa na kufumbwa ndani ya methali hizo.

Katika historia ya ushairi wa Kiswahili kuna watunzi mashuhuri kama vile Muyaka wa Muhaji, Shaaban Robert, Ahmed Nassir na Abdilatif Abdalla miongoni mwa wengine. Watunzi hao, wametumia methali kwa ustadi mkubwa katika uwasilishaji wa tungo zao. Tungo hizo, ni ushuhuda wa kazi bora za ushairi wa Kiswahili. Nao watunzi wa ushairi huru hutunga tungo zao kwa ustadi mkubwa ambapo kimatumizi, methali huwa ni kipengele muhimu lakini kudhihirika kwazo kunahitaji kujikuna kichwa na jicho pekuzi. Kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Semiotiki, tungo za kifasihi huweza kuwasilishwa kwa mitindo na miundo mbalimbali ya lugha. Katika muktadha huo, imedhihirishwa kuwa hakuna njia moja mahususi ambayo hupaswa kuzingatiwa katika uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili.

Kadhalika, kujitokeza kwa ushairi huru katika ushairi wa Kiswahili umewafanya watunzi ambao huzingatia arudhi na kauli za kimapokeo kama vile methali, kunoa na kupanua mtazamo wao kuhusu mitindo na kauli msingi inayopaswa kuzingatiwa katika uwasilishaji wa tungo hizo. Kwa hivyo, hata pale ambapo hutumia methali, huzitumia

kwa ustadi mkubwa zaidi kuliko vile zilivyotumiwa hapo awali. Kwa sababu, huelewa kuwa wanapotumia kauli hizo kiholela, watasutwa na watunzi hodari wa ushairi huru. Dhihirisho hilo ni la manufaa. Kwa vile, huhakikisha kuwa viwango vya ubora katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili hustawishwa na hudumishwa. Isitoshe, matumizi ya methali hayapaswi kupuuzwa. Kwa sababu, zinapotumiwa vizuri huchochea utafakari na kujenga usaili katika kuupata ujumbe batini unaowasilishwa katika shairi. Katika muktadha huo, uwaslishaji wa ushairi huru wa Kiswahili hujitambulisha zaidi katika matumizi ya kauli mahususi zinazoibuliwa na kutumiwa kwa makusudi. Kauli hizo pia hujengwa na hudhihirika katika tamathali za usemi. Kadhalika kauli hizo, hufafanua zaidi dhima ya methali katika tungo hizo. Katika mantiki hiyo ridhimu, mahadhi na mwendo katika uwasilishaji wa ushairi hudhibitiwa kwa uzingativu wa kauli zilizotumiwa kwa makusudi.

Kutokana na uchanganuzi wa mashairi teule na kwa uelekezo wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi ile ya Semiotiki, kutotumiwa kwa methali katika ushairi huru wa Kiswahili huweza kudhihirisha mwelekeo kwamba:

- Dhima ya methali katika huendelezwa kupitia kwa miundo au kauli mahususi ambazo huibuliwa na hutumiwa kwa makusudi.
- Mabadiliko ya kimtindo katika kiutunzi na kiuwasilishaji huweza kustawisha zaidi dhima ya methali katika uchambuzi wake.
- Ushairi wa Kiswahili huweza kutumia au kutotumia methali kwa uwazi katika uwasilishaji wake.

- Ushairi kama utanzu wowote wa fasihi u hai na hubadilika kila uchao kutegemea mabadiliko yaliyojiri katika utamaduni na uhalisi wa maisha katika jamii.
- Ushairi huweza kuwa ni mali ya jamii au ya kibinafsi kutokana na kauli teule zilizotumiwa katika uwasilishaji wake.
- Hisi za watunzi ndiyo dira elekezi ya kuibulia miundo na mitindo mahususi iliyoshirikishwa katika uwasilishaji wake.

Kwa hivyo uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili, hisi na michomo ya washairi ndiyo dira ambayo huwaelekeza watunzi katika kuteua kauli mahususi katika kuibulia miundo na mitindo katika harakati za uwasilishaji wa mawazo. Katika muktadha huo wa kiuwasilishaji, kutotumiwa kwa methali katika tungo za ushairi hupaswa kuchukuliwa kuwa ni mtindo wa kuibulia sura mpya ushairi wa Kiswahili.

Majaribio mbalimbali ya kiutunzi katika ushairi wa Kiswahili yaliweza kujitokeza mwishoni mwa miaka ya 1960 na kuendeleza zaidi katika miaka ya 1970 hapa Afrika ya Mashariki na matunda hayo yamedhihirika na yamestawishwa katika wakati wa sasa. Aidha, kutumiwa na kutotumiwa kwa methali katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili huweza kuwa ni makutano ya ushairi wa kimapokeo, ushairi wa kati na ushairi huru wa Kiswahili. Kadhalika, tungo ambazo hutungwa kwa mitindo tofauti ya kiuwasilishaji ni sura mbalimbali zishuhudiwazo, ambapo huchangiana na hukamilishana katika ushairi wa Kiswahili.

Katika mkabala wa kutumiwa au kutotumiwa kwa methali, ushairi wa Kiswahili umeshuhudia mabadiliko makubwa ya kimuundo, kimtindo na kiuwasilishaji katika wakati wa sasa; siyo tu hapa Afrika Mashariki bali pia kwengineko kunakotumiwa Kiswahili kama chombo cha mawasiliano miongoni mwa jamii. Aidha, utafiti huu umedhihirishwa kwamba, ushairi wa Kiswahili kwa wakati wa sasa huendelea kutungwa na hustawishwa kwa mitindo mbalimbali. Kutokana na dhima ya methali, ushairi wa Kiswahili umeweza kupendekezewa uainishaji wa makundi saba mahususi kuwa viwakilishi vya vijitanzu vyake, kama ilivyobainishwa katika sura ya sita ya tasnifu hii.

7.2 Matatizo

Tatizo kuu lililobainika katika utafiti huu ni kuhusu uanishaji wa tungo za ushairi wa Kiswahili. Kwa mfano, ushairi wa kati huhusisha mbinu za uwasilishaji ambazo huzingatiwa katika utunzi wa ushairi wa kimapokeo na zile ambazo huzingatiwa katika ushairi huru. Kwa hivyo, ushairi huo haujibainishi wazi. Aidha, ilikuwa vigumu kuuzungumzia utanzu huu bila ya kugusia sifa msingi zilizotumiwa katika tanzu hizo mbili. Pia, imekuwa vigumu kuzungumzia umbo la ushairi wa kati na huru. Kwa mfano, baadhi ya tungo hizo hazina mipaka ya beti. Je hizo ni aya, sentensi, mistari au beti?

Kadhalika, baadhi ya wa washairi wa kimapokeo hawakutaka kabisa kusikia ushairi huru ukitajwa. Kwa kiasi fulani watunzi wa ushairi huru hukubali ushairi wa kimapokeo lakini si katika misingi ya kiumbo na kimuundo. Vile vile, watunzi wa ushairi huru hawakutaka kusikia kuwa tungo zao si maarufu. Jambo hilo lilitatiza zaidi katika kuuzungumzia tanzu hizo mbili katika muktadha mpana wa ushairi wa Kiswahili.

Isitoshe, inapozungumziwa kususu umaarufu na ustawi wa ushairi wa Kiswahili katika Afrika Mashariki, aghalabu ushairi ambao huzingatiwa ni ule ambao umetungwa katika mataifa ya Kenya na Tanzania. Isitoshe nchini Uganda, kwa sababu Kiswahili hakijaimarishwa vilivyo, hakuna watunzi wasifika wa ushairi wa Kiswahili; kama wapo ni wachache.

7.3 Mapendekezo

Katika utafiti huu, imebainishwa kuwa methali ni kauli muhimu zilizojengeka katika tamathali za usemi. Aidha, ni kauli ambazo hutumika mno katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Vile vile imedahiliwa kwamba, methali ni kauli za kimapokeo ambazo ni maarufu katika mawasiliano ya jamii. Hata hivyo, kuna kauli zingine mahususi ambazo pia hutumiwa katika uwasilishaji wa utungo huu. Miongoni mwa kauli hizo ni kama vile vitendawili, semi, misimu, misemo na nahau ambazo pia zimejengeka katika tamathali za usemi.

Kadhalika, utafiti huu umedhihirisha kuwa, katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili kuna kauli mahususi ambazo hubuniwa kibinafsi na hutumika kwa makusudi. Kauli hizo, zina umuhimu wake katika uwasilishaji wa ushairi. Katika mkabala huo, ushairi wa Kiswahili hujibainisha kuwa ni kanzi ya matini za kitamathali. Kwa hivyo, imependekezwa kuwa, utafiti zaidi unaweza kuendelezwa ili kushughulikia maswala ambayo hayakufafanuliwa kwa uketo katika tasnifu hii. Kwa mfano, utafiti zaidi unaweza kuendelezwa kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Uhusiano uliopo baina ya matumizi ya methali na kauli nyinginezo za lugha ambazo huibuliwa kibinafsi na kwa makusudi kama kunga au mtindo katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili.
- Uwezekano wa methali kutumiwa kama chombo cha kuhifadhi mabadiliko ya utamaduni na uhalisi mpana wa maisha ya jamii za Afrika Mashariki katika muktadha wa ushairi wa Kiswhaili. Kimsingi, mabadiliko ya kihistoria kuhusu utamaduni wa jamii yameweza kushuhudiwa katika Afrika Mashariki ambapo Kiswahili ni lugha maarufu na fasihi yake hutumiwa kama kitambulisho au chombo cha kuendeleza ushirikiano na uhusiano mwema miongoni mwa mataifa hayo husika.
- Kudahili ushairi wa Kiswahili kama utanzu wa fasihi ambao huweza kudhoofisha matumizi ya methali au kustawisha na kuimarisha matumizi ya kauli zingine ambazo hujibainisha pia katika tamathali za usemi.
- Kulinganisha na kulinganua dhima ya methali katika ushairi simulizi na ushairi andishi wa Kiswahili. Kwa sababu, kwa wakati huu wa sasa ushairi wa Kiswahili huwasilishwa kimasimulizi na kimaandishi.
- Kuchunguza iwapo miundo ya methali hubadilika au huweza kuvyazwa upya kulingana na mabadiliko ya kijamii. Kwa mfano, vijana wa sasa huzalisha miisho ya methali zilizoko kama vile: Mwenda tezi na omo, huenda kufua nguo au Kupanda mchongoma, kushuka ni Bungoma.

MAREJELEO
MAKALA

Abdalla, A. (1973): "Ushairi wa Kiswahili na Uhuishwe Usiuliwe", katika *Zinduko.* Dar es Salaam: Jarida la Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

_____(1978): "Wajibu wa Mshairi wa Kiswahili katika Jamii yake", katika *Zinduko.* Dar es Salaam: Jarida la Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Abedi, A. (1971): "Utangulizi", katika *Waadhi wa Ushairi.* Nairobi: East African Literature Bureau.

Achebe, C. (1973): "The Novelist as a Teacher", katika Killan, G. D. (Mh.) *Africa Writers on African Writing.* London: Heinemann.

Angira, J. (1970): "Tungo Zake", katika *GHALA Vol VII.* Jarida la Chama cha Kiswahili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Barthes, R. (1981): "Theory of the Text", Ian Macleod (Mt.), katika Young, R. (Mh.) *Untying the Text.* London: Routledge.

Black M. (1979): "More about Metaphor", katika Ortony, A. (Mh.) *Metaphor and Thought.* Cambridge: Cambridge University Press.

Boyd, A. (1986): "The Music of the Waswahili of Lamu, Kenya", katika *Bulletin of Folkways Records.* New York: Folkways Corporation.

Buhler, K. (1985): "The Key Principle: The Sign Character of Language", katika Innis, R. (Mh.) *Semiotics.* London: Indiana University Press.

Chacha, C. N. (1987): "History and Literature: Reflections on Historical Issues in Swahili Literature", katika *Trans African Journal of History, Juzuu la 16.*

_____(1994): "The Social Structure of the Waswahili of East Africa," katika *Maseno Journal of Educational and Social Sciences Vol. 1 na Vol. 2.*

Chiraghdin, S. na Nabhany, A. (1975): "Tarehe ya Ushairi wa Kiswahili", katika *MULIKA Na. 7.* Dar es Salaam: TUKI.

Chiraghdin, S. (1971): "Utangulizi", katika *Malenga wa Mvita.* Nairobi: Oxford University Press.

Culler, J. (2003): "Structuralism and Literature", katika Keesey, D. (Mh.) *Contexts of Criticism.* London: Mayfield Publishing Company.

Ezeliora, O. (2009): "Colonial Discourse, Poetic Language and the Igbo Masquerading Culture in Ezenwa Ohaetos: The Voice of the Night Masquerade", katika *Journal of African Cultural Studies, Juzuu 21 na 1.* London: SOAS.

Fowler, R. (1966): "The Formalaic Theory and its Application to English Alliterative Poetry", katika Fowler, R. (Mh.), *Essays on Style and Language.* London: Routledge & Kegan.

Frolova, N. (2008): "Mazungumzo ya Washairi wa Mapokeo na wa Kisasa: Mabishano au Majadiliano?" Ogechi, N. C., Shitemi, N. K. na Simala, S. K. (Wah.), katika *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.* Eldoret: Moi University Press.

Gibbe, A. G. (1978): "Fasihi na Jamii: Baadhi ya Washairi wa Kiswahili, 1960-77", katika *KISWAHILI Juzuu 48/1* Dar es Salaam: TUKI.

_____ (1990): "Ufumbaji katika Ushairi wa Kiswahili", katika Gibbe, A. G. (Mh.), *Jarida la KISWAHILI, Juzuu 1.* Dar es Salaam: Education Services Centre.

_____ (1998): "Sajili ya Ushairi", katika Gibbe, A. G. (Mh.), *Mwongozo wa Ushairi Na. 1. Mashairi ya Taria.* Eldoret: SEKUKI.

Gromov, M. D. (2006): "The Question of Kiswahili Style Again? The Poetry of Kithaka wa Mberia", katika *KISWAHILI Juzuu 69.* Dar es Salaam: TUKI.

Hall, S. (1999): "Encoding and Decoding", katika During, S. (Mh.), *The Cultural Studies Reader 2nd Edition.* London: Routledge.

Hichens, W. (1963): "Swahili Prosody", katika *SWAHILI Juzuu 33/1.* Dar as Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Indede, F. N. (2008): "Mabadiliko katika Umbo la Ushairi na Athari zake katika Ushairi wa Kiswahili", katika *SWAHILI FORUM 15.*

Jacobson, J. W. (1960): "Concluding Statement: Linguistics and Poetics", katika Seboek, J. (Mh.), *Style and Language.* Cambridge: MIT.

Johnson, J. W. (2006): "Orality, Literacy and Somali Oral Poetry", Katika *Journal of African Cultural Studies, Juzuu 18.* London: Routledge Taylor and Francis Group.

Kahigi, K. K. (1975): "Ushairi: Mtazamo wa Kisayansi", katika *KISWAHILI, Juzuu 45/1.* Dar es Salaam: TUKI.

Kandoro, S. A. (1983): "Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Shairi la Kiswahili", katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III, Fasihi.* Dar es Salaam: TUKI.

Kezilahabi, E. (1973): "Diwani ya Massamba", katika *MULIKA Na. 13.* Dar es Salaam: TUKI.

_____ (1973): "The Development of Swahili Poetry 18th – 20th Century", katika *KISWAHILI Juzuu 42/2, 43/1.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

_____1977): "Mashairi ya Kiswahili", katika Topan F.M. (Mh.), *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili* (Kitabu cha Pili). Dar es Salaam: Oxford University Press.

_____ (1983): "Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili", katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III, Fasihi.* Dar es Salaam: TUKI.

Khatib, M. S. (1999): "Tamathali za Usemi", katika *MULIKA Na. 25.* Dar es Salaam: TUKI.

Kimaro, K. (2008): "Washairi huru Wamefilisika kimawazo na kisanaa", katika *Taifa Leo* Novemba 10, 2008 Uk. 21. Nairobi: Nation Media Group.

King'ei, G. K. (1994): "Swahili Taarab as a Medium of Political Expression in Kenya", katika *Writers Forum: A Journal of the Writers' Association of Kenya.* Nairobi. The Jomo Kenyatta Foundation Publishers and Printers.

_____ (2000) "Stunted Growth of Kiswahili Literature: Causes and Remedy", katika *KISWAHILI Juzuu 63.* Dar es Salaam: TUKI.

_____ (2007): "Athari za Washairi Wakongwe juu ya Washairi wa Kisasa: Mfano wa Muyaka bin Haji na Ahmed Nassir", katika *Kioo cha Lugha,* Juzuu 5. Dar es Salaam: TUKI.

Knappert, J. (1974): "The Appreciation of Kiswahili Poetry", katika *KISWAHILI Juzuu Na. 44/2.* Dar es Salaam: TUKI.

Ligami, P. na Barasa, S. (2001): "Tahakiki ya Methali za Kiswahili", katika Njogu, K., Momanyi, C. na Mathooko, M. (Wah.) *Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Nairobi: Taweza Communications.

Lord, A. (1951): "Composition by Theme in Homer", katika *Transactions of the American Philosophical Association 82.*

Magoun, F. P. (1953): "Oral Formulaic Character of Anglo-Saxon Narrative Poetry", katika *Speculum 28.*

Maitaria, J. N. (2008): "Methali za Kiswahili kama Kielelezo cha Ujenzi wa Umoja na Utangamano katika Jamii", Makala yaliyowasilishwa katika Kongamano La CHAKITA, Agosti 7, 2008. Mombasa: RISSEA.

_____ (2011): "Ushairi wa Kiswahili katika Njia Panda: Kutumia au Kutotumia Methali", Makala yaliyowasilishwa katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. Septemba 28,2011.

Maitaria, J. N. na Maina, R. W. (2011): "Fasihi ya Kiswahili kama Mbinu ya Kufunzia na Uelimishaji wa Jamii kuhusu Katiba: Mfano wa Ushairi wa Kiswahili", Makala yaliyowasilishwa katika Kongamano la BAWAKI tarehe 28 April 2011, Nairobi: CUEA.

Massamba, D. P. B (1983): "Utunzi wa Kiswahili", katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi.* Dar es Salaam: TUKI.

Matteru, M. (1975): "Sauti ya Dhiki", katika *MULIKA Na. 7.* Dar es Salaam: TUKI.

_____ (1987): "Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi", katika *MULIKA Na. 19.* Dar es Salaam: TUKI.

Matundura, E. (2001): "What Ails Kiswahili Literature", Katika *Sunday nation*, Juni 12, 2011.

Mayoka, J. (1977): "Vina na Mizani ni Uti wa Mgongo wa Ushairi", katika *MULIKA Na. 11.* Dar es Salaam: TUKI.

Mazrui, A. na Noor, S. I. (1976): "A Note on Kiswahili Poetry", katika *KISWAHILI Juzuu 46/1.* Dar es Salaam: TUKI.

Mbaga, N.O. (1978): "Dhima ya Ushairi Katika Kuhifadhi Historia ya Jamii", katika *MULIKA Na. 14.* Dar es Salaam. TUKI.

Mbatiah, M. (1990): "Umbo la Mashairi", katika *Mwamko Toleo la 5.* Nairobi. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Michiri, M.N. (2000): "Gendered Memory through Proverbs among the Agikuyu Tribe in Kenya", Makala yaliyowasilishwa katika Kongamano la International Society for Folk Narrative Research Conference, Tarehe 17-22 Julai 2000, Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mlacha, S. A. K. (1985): "Dhima ya Methali katika Malezi", katika *KISWAHILI Juzuu 51/1* na *52/2.* Dar es Salaam: TUKI.

Mohammed, S. A. (1977): "Fani katika Sauti ya Dhiki", katika *MULIKA Na. 11.* Dar es Salaam: TUKI.

_____ (1986): "Tamathali za Semi za Kiswahili", katika *MULIKA Na. 18.* Dar es Salaam: TUKI.

Momanyi, C. (2001): "Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaaban Robert", katika *KISWAHILI Juzuu 64.* Dar es Salaam: TUKI.

_____ (2006): "Dhima na Utendakazi wa Vitendawili katika Jamii", katika Njogu, K., Momanyi, C., na Mathooko, M. (Wah.) *Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Nairobi: Twaweza Communications.

Mtesigwa, P. C. K. (1990): "Methali ni Nini?", katika *KISWAHILI Juzuu Na. 2.* Dar es Salaam. TUKI.

Mulokozi, M. M. (1974): "Mapitio ya Sauti ya Dhiki", katika *UMMA Tol. 5 Na. 2.* Dar es Salaam: Idara ya Fasihi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

_____ (1975): "Revolution and Reaction in Kiswahili Poetry", katika *KISWAHILI Juzuu Na. 45/2.* Dar es Salaam: TUKI.

_____ (1978): "Ushairi wa Ukasuku", katika *Kioo cha Lugha.* Dar es Salaam. Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

_____ (1982): "Protest and Resistance in Swahili Poetry: 1600 – 1885", *KISWAHILI Juzuu Na. 49/1.* Dar es Salaam: TUKI.

_____ (1989): "Tanzu za Fasihi Simulizi", katika *MULIKA Na. 21.* Dar es Salaam. TUKI.

_____ (2008): "Nadharia ya Jadi ya Ushairi wa Kiswahili: Je Upo?", katika Ogechi N.O, Shitemi, N.L. na Simala, K.I. (Wah.) *Nadharia ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.* Eldoret: Moi University Press.

Mwamzandi I. Y. (2011): "Changing Face(s) of the Extended Metaphorical Frame of Taarab Lyrics", katika Makokha, J.K. S., Kabaji, E. na Dipio, D. (Wah.), *East African Literature: Essay on Written and Oral Tradition.* Berlin: Verlag Berlin GMBH.

_____ (2002): "Majadiliano ya Tanzu katika Ushairi wa Kiswahili", katika Ogechi N.O., Shitemi, N.K. na Simala K.I. (Wah), *Utafiti wa Kiswahili.* Eldoret: Moi University Press.

Nassir, A. J. B. (1977): "Muyaka wa Muhaji na Ushairi wa Kiswahili", katika *MULIKA Na. 10.* Dar es Salaam: TUKI.

Ndulute, C. L. (1987): "Shaaban Robert's Poetic Landscape from Ethnicism to Nationalism", *KISWAHILI Juzuu Na. 54/1 na 54/2.* Dar es Salaam: TUKI.

Njogu, K. (1996): "Kiswahili Metapoetry on Prosody", Makala yaliyowasilishwa katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

_____ (2006): "Fasihi Simulizi na Nadharia ya Fasihi ya Kiafrika", katika Njogu, K., Momanyi, C. na Mathooko, M. (Wah.), *Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Nairobi. Twaweza Communications.

Notopolous, J. A. (1951): "Continuity and Interconnections in Homeric Oral Composition", katika TAPA 82.

Ohly, R. (1973): "Historical Approach to Swahili Literature. As Here to Fore an Open Question", katika *KISWAHILI Juzuu Na. 43/2.* Dar es Salaam: TUKI.

_____ (1974): "A Review of Abdilatif's Abdalla *Sauti ya Dhiki*", katika *KISWAHILI Juzuu Na. 44/2.* Dar es Salaam: TUKI.

Omari, S. (2006): "Mtindo na Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya", katika *KISWAHILI Na. Juzuu 69.* Dar es Salaam. TUKI.

Ponella, C. (1995): "Matumizi ya Kiswahili katika Kanda ya Nchi Zinazotumia Kiswahili", katika *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki.* Dar es Salaam: TUKI.

Ramadhan, J. (1973): "Ushairi", katika *MULIKA Na. 3.* Dar es Salaam: TUKI.

Robert, S. (1958): "Hotuba Juu ya Ushairi", katika *Journal of the East African Swahili Committee Na. 28/1.* Dar es Salaam: Institute of Swahili Research.

Ruo, K. R. (1979): "The Place of Language in Literature", Makala ya Semina 102/1As, Idara ya Kiswahili Na Isimu, Chuo Kikuu cha Nairobi.

_____ (1983): "Suala la Ushairi wa Kiswahili', katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: FASIHI.* Dar es Salaam: TUKI.

Sanka, S. M. (1995): "Umapokeo na Usasa katika Ushairi wa Kiswahili", katika *Kioo cha Lugha, Juzuu Na. 1.* Dar es Salaam: TUKI.

Thorn, R. (1985): "From the Symbol to the Icon", katika Innis, R. (Mh.), *Semiotics.* London: Indiana University Press.

Topan, F. (1970): "Swahili Textual Variations", katika *SWAHILI Juzuu Na.40/1.* Dar es Salaam: TUKI.

_____ (1973): "Utangulizi", katika Kezilalabi, E., *Kichomi,* London: Heinemann.

Vasquez, A. S. (1992): "Semiotics", katika Bright W. (Mh.), *International Encyclopedia of Linguistics Vol 3.* New York: Oxford University Press.

Wafula, R. M. (1994): "Uainisho wa Methali", katika *Writers Forum, A Journal of the Writers' Association of Kenya.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation Publishers and Printers.

Wamitila, K. W. (1999): "A Rhetorical Study of Kiswahili Classical Poetry. An Investigation into the Nature and Role of Repetition", katika *Research in African Literatures.* Indian University Press.

_____ (2004): "Utangulizi", katika Mohamed S. A. (2002) *Jicho la Ndani.* Nairobi: Longhorn (Kenya) Ltd.

_____ (2007): "Narrative and Metaphor: Towards a New Aesthetics of the Kiswahili Novel", katika *KISWAHILI Juzuu 70.* Dar es Salaam: TUKI.

Wanyoike, E. N. (1976): "The Use of Language in Poetry", katika Oluoch A. L., Wanyoike, E. N. na Classen, A. (Wah), *LUGHA: A Journal for Language Teachers in Kenya, Vol 5. No. 1.* Nairobi: Kenya Language Association.

Zubkova-Bertoncini, E. (2008): "Some Remarks on Kithaka wa Mberia's Poetry", Makala yaliyowasilishwa katika Kongamano la 21st Century Swahili-Kolloquium, Chuo Kikuu cha Bayreuth.

TASNIFU

Alembi, E. (1992): "An Analysis of the Style and Social Significance of the Abanyole Children's Oral Poetry", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

_____ (2002): "The Construction of the Abanyole Perception of Death Through Oral Funeral Poetry", Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu cha Helsinki. (Haijachapishwa)

Babusa, H. O. (2005): "Vigezo badilia kuhusu uanishaji wa Mashairi ya Kiswahili", Tasnifu ya M. A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Bhab, A. J. (1976): "Muyaka wa Muhaji na Ushairi wa Kiswahili", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa)

Chacha, C. N. (1980): "Ushairi wa Abdilatif Abdalla", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

_____ (1987): "Meaning and Interpretation of Swahili Poetry: A Portrayal of Changing Society", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Yale. (Haijachapishwa)

Chacha, L. M. (1997): "Majigambo ya Kikuria: Mtazamo wa Kiisimu", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Gibbe, A. G. (1995): "Inkishafi: Uhakiki wa Kidayakronia", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa)

Gicuku, M. (2011): "Usawiri wa Maudhui ya Ndoa katika Mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Kithaka wa Mberia", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haichapishwa)

Habwe, J. W. (1999): "Discourse Analysis of Swahili Political Speeches", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Imbosa, R. (1990): "Jazanda katika Ushairi wa Muyaka", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Jilala, H. (2008): "The Artistic Uses of Metaphors in Constructing Meaning and Messages in New Generation Songs in Tanzania". Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.(Haijachapishwa)

Kabaji, E. (1991): "The Maragoli Folktale: Its Meaning and Aesthetics", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Karama, M. R. (1996): "Al-Inkishafi: Ushahidi wa Usemezo katika Ushairi wa Kiswahili", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Kazungu, K. (1982): "Deriviation and Foregrounding in Chosen Swahili Texts", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

King'ei, G. K. (1982): "Uhakiki wa *Nthimo* (Methali) za Kikamba kwa Kufuatisha Misingi ya Methali za Kiswahili", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kitsao, J. (1975): "A Stylistic Approach Adopted for the Study of Written Kiswahili Prose Texts", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Maitaria, J. N. (1991): "Matumizi ya Methali kama Chombo cha Mawasiliano: Mtazamo wa Kiisimu Jamii", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Masinde, E. (1992) "Ushairi Huru: Uchambuzi wa Dhamria na Maudhui", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

_____ (2003): "Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Mbughuni, P. (1978): "From Oral to Written Literature: The Politicization of Kiswahili Literature", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Indiana. (Haijachapishwa)

Mbugua, W. K. (2005): "A Critical Analysis of Conformity and Subversion in Gikuyu Children's Oral Poetry", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

M'ngaruthi, T. K. (2007): "Usawiri wa Wahusika katika *Dafina ya Umalenga* (H. M. Mbega) na *Jicho la Ndani* (S.A. Mohamed)", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Momanyi, C. (1991): "Matumizi ya Taswira kama Kielelezo cha Uhalisia katika Utenzi wa Al-Inkishafi", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

_____ (1998): "Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika Jamii ya Waswahili kama Inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Mosha, E.S. (2002): "The Use of Metaphors in Chaga Folktales and Oral Poetry", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa)

Mulokozi, M. M. (1975): "Ushairi wa Kiswahili na Ubantu hadi 1700", Tasnifu ya Mwaka wa Tatu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

_____ (1986): "The Nanga Epic of the Bahaya: A Case Study in African Epic Characteristics", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa)

Musau, P. M. (1985): "Euphrase Kezilahabi: Mwandishi Aliyekata Tamaa", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachaipishwa)

Musungu, J. J. (2005): "An Analysis of the Context and Meaning of the Poetry within the Babukusu Khuswala Kumse Ritual", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Mutembei, K.A. (1993): "A Phonological Aspect of Foregrounding in Kiswahili Poetry", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa)

Mwai, W. (1988): "New Trends in Ushairi", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Mwamzandi, I. Y. (2002): "Usemezano katika Malenga wa Kiswahili: Mfano wa Taarab", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa)

Nagy, W. (1974): "Figurative Patterns and Redundancy in the Lexicon", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha San California. (Haijachapishwa)

Nchebere, C. M. (2009): "Maudhui katika Msimu wa Tisa ya Kithaka wa Mberia", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Ndungo, C. (1985): "Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

_____ (1998): "Image of Women in African Oral Literature: A Case of Gikuyu and Swahili Proverbs", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Njogu, K.(1993): "Dialogic Poetry: Contestation and Social Challenge in East African Poetic Genres", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Yale. (Haijachapishwa)

Noor, I. S. (1983): "Functions of Dialogue in Swahili Society", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha New Jersey. (Haijachapishwa)

Nyanchama, M. B. (2004): "Matumizi ya Taswira na Istiara katika *Sauti ya Dhiki*", Tasnifu ya M. A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Nzuki, P. K. (2002): "Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Osiemo, D.O. (1997) "Fani katika Ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega: Uhakiki wa Upisho wa Umalenga na Dafina ya Umalenga", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Parker, C. A. (1970): "Iwapo Nia kuna Njia: A Case Study of the Content and Context of Proverbs in Swahili", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Washington. (Haijachapishwa)

_____ (1974): "Aspects of A Theory of Proverb", Tasnifu ya Ph.D, Chuo Kikuu cha Washington. (Haijachapishwa)

Saavedra, A. J. (2002): "Swahili Poetry as Historical Source: Utenzi, War poems and the German Conquest of East Africa", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha London. (Haijachapishwa)

Sanka, S. M. (1994): "Semantic Deviation in Iraqw Oral Poetry", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa)

Seitel, P. (1972): "Proverbs and Structures of Metaphors among the Bahaya of Tanzania", Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Pennsylvania. (Haijachapishwa)

Wafula, R. (1989): "The Use of Allegory in Shaaban Robert's Prose Works", Tasnifu ya M. A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

_____ (2003): "Performing and Hybridity: A Dialogue and Semiotic Study of Twentieth Century from Africa and the Africans Diaspora", Tasnifu ya Ph.D, Chuo Kikuu cha Indiana (Haijachapishwa)

Wekesa, A. (2008): "Matumizi ya Taswira katika Ushairi Huru wa Kiswahili", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

VITABU

Abdalla, A. (1973): *Sauti ya Dhiki.* Nairobi: Oxford University Press.

_____ (1977) (Mh.): *Mashairi ya Miaka Kumi ya Azimio la Arusha.* Dar es Salaam: UKUTA.

Abdulaziz, H. M. (1979): *Muyaka: 19th Century Popular Poetry.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Abedi, A. (1954): *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri.* Nairobi: East African Literature Bureau.

Abrams, M. H. (1993): *A Glossary of Literary Terms.* New York: Harcort and Brace.

Abudu, M. na Baruwa, A. (1981): *Methali za Kiswahili: Maana na Matumizi.* Nairobi: Shungwaya Publishers Ltd.

Adagala, K. na Kabira, W. (1985) (Wah.): *Kenyan Oral Narratives.* Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Akivaga, K. na Odaga, B. (1982): *Oral Literature: A School Cerfiticate Course.* Nairobi: Heinemann.

Akporobaro, F. B. O. na Emovon, J. A. (1994): *Nigerian Proverbs: Meaning and Relevance Today.* Lagos: Department of Culture.

_____ (2001): *Introduction to African Oral Literature.* Lagos: William Wilberforce Institute and Lighthouse Publishers.

Akporobaro, F. B. O. (1994): *Understanding Poetry: Its Language, Its Forms, Its Functions.* Lagos: DMODUS Publishers.

Allen, J. W. T. (1971): *Tendi.* London: Heinemann Educational Books Ltd.

Amana, B. (1982): *Malenga wa Vumba.* Nairobi: Oxford University Press.

Andambi A. na Murono, E. (2005): *Muundo Mpya wa Methali za Kiswhaili.* Nairobi: Mvule Africa Publishers.

Aoron, D. (1995): *Hands Full of Meaning.* Clarendon Press

Arnold, S. (1985): *African Literary Studies: The Present State.* Washington, D. C.: Three Continents Press.

Austin, J. (1962): *How to do Things with Words.* Clarendon: Oxford University Press.

Babcock, C. R. (1975): *Levi-Strauss: Structuralism and Sociological Theory.* London: Hutchinson.

Babusa, H. O. (2009): *A Dictionary of English and Swahili Equivalent Proverbs.* Saarbrucken: VDM Verlag Dr. Muller Aktiengeuschaft and Co. KG.

Babu, A. M. (1981): *African Socialism or Socialist Africa?* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Ba Schiera, A. (2003): *Euphrase Kezilahabi: Profiles.* London: The African Centre.

Barthes, R. (1973): *Mythologies.* London: Paladina.

Behn, R. and Twichell, C. (1992): *The Practice of Poetry.* New York: Harper-Collins Publishers.

Bennet, A. (1995)(Mh.): *Reader and Reading.* London: Longman.

Bernth, L. (1977): *Forms of Folklore in Africa.* Austin: University of Texas.

Bertens, H. (2001): *Literary Theory: The Basics.* London: Routledge.

Bhaktin, M. M. (1990): *Art and Answerbility.* Austin: University of Texas Press.

Biersterker, A. (19960: *Kujibizana: Questions of Language and Power in 19th and 20th Century Poetry in Kiswahili.* East Lansing: Michigan State University Press.

Birch, D. (1989): *Language, Literature and Critical Practice.* London: Routledge.

Black, M. (1973): *Meaning and Intention. An Examination of Grice's View: New Literary History.* Harvard: Harvard University Press.

Black, W. (1984): *How to Read a Poem.* Chicago: Penguin Groups.

Blamires, H. (1979): *A History of Literary Criticism: Post Structuralism or Deconstruction.* London: Macmillan Press Limited.

Bloom, H. (1976): *Poetry and Repression.* New Haven: Yale University Press.

Booker, M. K. (1996): *A Practical Introduction to Literary Theory and Criticism.* London: USA Publishers.

Brett, E. A. (1973): *Colonialism and Development in East Africa.* Nairobi: Heinemann Educational Books.

Buchbinder, D. (1991): *Contemporary Literary Theory and the Reading of Poetry.* Melbourne: Macmillan Educational Austria PTY Ltd.

Butcher, S. H. (1961): *Aristotle's Poetics.* New York: Hills and Wang.

Bukenya, A. S., Gachanja, M. na Nandwa, J. (1997): *Oral Literature: A Senior Course.* Nairobi: Longhorn.

Burnham, J. (1971): *The Structure of Art.* New York: Bariller.

Cane, M. (1962): *Making of a Poem: An Enquiry into Creative Process.* New York: Harcort Brace.

Chacha, C. N. (1992): *Ushairi wa Abdilatif Abdalla: Sauti ya Utetezi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Chiraghdin, S. (1987): *Malenga wa Karne Moja.* Nairobi: Longman.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977): *Historia ya Kiswahili.* Nairobi: Oxford University Press.

Ciardi, J. (1960): *How Does a Poem Mean?* Boston: Houghton Mifflin.

Cobley, P. na Jansz, I. (1997): *Semiotics for Beginners.* Cambridge: Icon Books.

Cohen, R. (1974) (Mh.): *The New Directions in Literary History.* London: Routledge and Kegan Paul.

Colebrook, C. (2004): *Irony.* London: Routeledge.

Conforth, M. (1962): *Dialectical Materialism, Vol. 2: Historical Materialism.* London: Lawrence and Wishard.

Cuddon, J. A. (1997): *A Dictionary of Literary Terms and Literary Theory.* Oxford: Blackwell Publishers.

Culler, J. (1975): *Structuralist Poetics: Structuralism, Linguistics and the Study of Literature.* New York: Cornell University Press.

_____ (1981): *The Pursuit of Signs: Semiotics, Literature and Deconstruction.* London: Routledge and Kegan Ltd.

Daiches, D. (1981): *Critical Approaches to Literature.* London: Longman.

Danesi, M. (1994): *Messages and Meanings: An Introduction to Semiotics.* Toronto: Canadian Scholars Press.

Darvin, D. na Wamuhu (1994): *Enjoying Poetry.* London: The Macmillan Press.

Djik, T. (1977): *Text and Content. Exploration in Semantics and Pragmatics of Discourse.* London: Longman.

Dorsch, S. T. (1965)(Mh.): *Aristotle/Horace/Longinus: Classical Literary Criticism.* Harmandsworth: Penguin.

Eagleton, T. (1991): *Ideology: An Introduction.* London: Verso.

Easthope, A. (1983): *Poetry as Discourse.* London: Methen.

Eco, U. (1976): *A Theory of Semiotics.* Bloomington: Indiana University Press.

_____ (1981): *The Role of the Reader: Explorations in the Semiotics of the Text.* London: Hutchinson.

_____ (1984): *Semiotics and the Philosophy of Language.* London: Macmillan Press Limited.

Egudu, R. na Nwoga, D. (1973): *Igbo Traditional Verse.* London: Heinemann.

Eschbach, A. (1983): *Foundations of Semiotics.* Amsterdam: John Benjamin's Publishing Company.

Esthope, A. (1992): *The Archaelogy of Knowledge and the Discourse of Language.* New York: Pantheon Books Ltd.

Fairclough, N. (1989): *Language and Power.* London: Longman.

Fanon, F. (1967): *Black Skins, White Masks.* New York: Grove Press.

Faucault, M. (1997): *The Order of Things.* London: Routeledge and Kegan Ltd.

Fergussson, P. (1983): *Dictionary of Proverbs.* London: Penguin Books Ltd.

Finnegan, R. (1970): *Oral Literature in Africa.* Nairobi: Oxford University Press.

_____ (1977): *Oral Literature: Its Nature, Significance and Oral Context.* Cambridge: Cambridge University Press.

Fish, S. (1980): *Is there a Text in this Class? The Authority of Interpretive Communities.* Cambridge: Harvan University Press.

Finke, J. (1990): *Introduction to Communication Studies.* London: Routledge.

Fokkema, D. na Ibsch, E. (1995): *Theories of Literature in the Twentieth Century.* London: Hurst and Company.

Foley, J. M. (1981) (Mh.): *Oral Traditional Literature A. Festschrift for Albert Lord.* Ohio: Slavica Publishers.

Forster, T. C. (2003): *How to Read Literature Like a Professor.* New York: Harper Collins Publishers.

Fowler, R. (1996): *Linguistic Criticism.* Oxford University Press.

Frye, N. (1963): *Fables of Identity: Studies in Poetic Mythology.* New York: Harbinger.

Gavins, J. (2007): *Text World Theory: An Introduction.* Edinburgh: Edinburgh University Press.

Gerald, A. (1981): *African Language Literatures.* Essex: Longman.

Gesero, W. C. (2009): *Methali za Kiswahili Afrika Mashariki na Kati.* Dar es Salaam: Absit Co.

Gibbe, A. G. (1980): *Shaaban Robert: Mshairi.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Gibbe, A. G. na Mvungi, T. A. (1987): *Fasihi kwa Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: Standard Publishing Company.

Gibbs, R. W. (1994): *The Poetics of Mind: Figurative Thought, Language and Understanding.* Cambridge: Cambridge University Press.

Goody, J. (1987): *The Interface Between Written and the Oral.* New York: Cambridge University Press.

Graham, D. (1968): *Introduction to Poetry.* London: Oxford University Press.

Greenway, J. (1964): *Literature among the Primitives.* Pennsylvania: Hatboro.

Guiraund, P. (1975): *Semiology.* London: Routledge and Kegan Paul.

Hainworth, J. B. (1968): *The Flexibility of the Homeric Formula.* Oxford: Oxford University Press.

Halliday, M. A. K. (1978): *Language as Social Semiotics: The Interpretation of Language and Meaning.* London: Edward Arnold.

Halliday, M. A. K. na Hassan, R. (1989): *Language, Context and Text.* New York: Oxford University Press.

Hann, C. M. (1993): *Socialism: Ideals, Ideologies and Local Practice.* London: Routeledge.

Harland, R. (1999): *Literary Theory from Plato to Barthes: An Introductory History.* New York: St. Martins Press.

Harries, L. (1962): *Swahili Poetry.* Oxford: The Claredon Press.

_____ (1966): *Poems from Kenya.* London: University of Winconsin Press.

Hawkes, T. (1977): *The Structuralism and Semiotics.* London: Methuen.

Hayhoe, M. na Parker, S. (1990): *Reading and Response.* Philadelphia: Open University Press.

Hedley, J. (1998): *Power in Verse: Metaphor and Metonymy in the Renaissance Lyric.* London: The Pennsylvania State University Press.

Henige, D. P. (1974): *The Chronology of Oral Tradition.* Oxford: Clarendon Press.

Herzfeld, M. D. (1980): *Semiotics.* New York: Plenum Press.

Hichens, W. (1972): *Inkishafi: The Soul Awakening.* Nairobi: Oxford University Press.

Hirsch, E. (1976): *The Aims of Interpretation.* Chicago: University of Chicago Press.

Holman, C. H. (1975): *A Handbook of Literature.* Indianapolis: Odyssey.

Honero, L. N., Sengo. T. S. Y na Ngole, S. Y. (1980): *Matunda ya Azimio.* Dar es Salaam: TUKI.

Horchman, B. (1985): *Character in Literature.* Ithaca: Cornell University Press.

Howthorn, J. (1987): *Unlocking the Text: Fundamental Issues in Literary Theory.* London: Edward Arnold.

Howthorn, J. (1994): *A Concise Glossary of Contemporary Literary Theory.* London: Edward Arnold.

Hudson, R. (1995): *Word Meaning.* London: Routledge.

Hughes, G. (19880: *Words in Time.* Oxford: Blackwell.

Hussein, E. N. (1971): *Mashetani.* Nairobi: Oxford University Press.

_____ (1976): *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi.* Nairobi: Oxford University Press.

Hyden, G. (1988): *Beyond Ujamaa in Tanzania: Underdevelopment and Uncaptured Peasantry.* Los Angeles: University of California Press.

Hyden, G. na Bratton, M. (1992): *Governance and Politics in Africa.* Riener: Boulder Co. Lynne.

Innis, R. E. (1985): *Semiotics.* London: Indiana University Press.

Irele, A. (1981): *The African Experience in Literature and Ideology.* Bloomington: Indiana University Press.

Iser, W. (1974): *The Implied Reader.* Baltimore: John Hopkins University Press.

_____ (1978): *The Act of Reading.* London: Routeledge and Kegan Paul.

Jahadhmy, S. H. (1975): *Kusanyiko la Mashairi.* Nairobi: Heinemann.

Johnson, M. (1977) (Mh.): *Philosophical Perspectives on Metaphor.* Mineapolis: University of Minnesota Press.

Jones, E. D. (1983): *Africa Literature Today. No. 13.* London: Heinemann.

Kandoro, S. A. (1974): *Ushairi wa Kiswahili.* Dar es Salaam. Longman.

_____ (1978): *Ushahidi wa Mashairi ya Kiswahili na Lugha Yake.* Dar es Salaam: Longman.

_____ (1972): *Mashairi ya Saadan.* Dar es Salaam: Mwananchi Publishing.

Karama, S. (1985a): *Sanaa ya Umalenga.* Nairobi: Heinemann Educational Books.

_____ (1985b): *Urembo wa Kiswahili.* London: Evans Brothers Ltd.

Karama, S. na Saidi, M. (1983): *Maelezo ya Methali za Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Kariana, J. na Kitonga, E. (1976): *An Introduction to East African Poetry.* Nairobi: Oxford University.

Kesteloot, L. (1972): *Intellectual Origins of the African Civilization.* Washington, D. C. Black Orpheus Press.

Kezilahabi, E. (1974): *Kichomi.* Nairobi: Heinemann Educational Books Ltd.

_____ (1976): *Ushairi wa Shaaban Robert.* Nairobi: East Africa Literature Bureau.

_____ (1988): *Karibu Ndani.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

_____ (2008): *Dhifa.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Khamis, S. A. M. (1980): *Methali za Tashbiha.* Dar es Salaam: Longman.

Khan, M. K. (1981): *Mashairi Yetu.* Nairobi: East African Publishers House.

Khatib, M. S. (2003): *Wasakatonge.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Kiango, S. D. na Sengo, T. S. Y. (1975): *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Longman.

King'ei, G. K. (2000): *Miale ya Uzalendo.* Nairobi: Phoenix Publishers.

King'ei, G. K. na Kemoli, A. (2001): *Taaluma za Ushairi.* Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

King'ei, G. K. na Kisovi, C. M. (2005): *Msingi wa Fasihi Simulizi.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kipury, N. (1983): *Oral Literature of the Maasai.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Kirk, G. S. (1964) (Mh.): *The Language and Background of Homer.* Cambridge: Cambridge University Press.

Kirumbi, P.S. (1975): *Misingi ya Fasihi Simulizi.* Nairobi: Shungwaya Publishers.

Kisia, A. na Mwarandani, B. (2007): *Uketo wa Ushairi kwa Shule za Upili Ukijumlisha Utungo wa Diwani Yetu.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Knappert, J. (1967): *Traditional Swahili Poetry.* Leiden: G. J. Brill.

_____ (1972): *A Choice of Flowers: An Anthology of Swahili Love Poetry.* London: Heinemann.

_____ (1979): *Four Centuries of Swahili Verse: A Literary History and Anthology.* London: Heinemann.

Krishna, R. (1987): *Text and Sub-Text: Suggestion in Literature.* London: Edward Arnold.

Kristeva, J. (1984): *Revolution in Poetic Language.* New York: Columbia University Press.

Kuhenga, C. (1977): *Tamathali za Usemi.* Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Kunemah, A. S. K. (2008): *Misemo na Methali katika Ushairi.* Dar es Salaam: TUKI

Kunene, D. P. (1971): *Heroic Poetry of the Basatho.* Oxford: Clarendon.

Lackoff, G. na Johnson, M. (1980): *Metaphors we Live By.* Chicago: Chicago University.

Lanham, R. A. (1991): *A Handbook of Rhetorical Terms.* London: University of Califonia Press.

Lattimore, R. (1960): *The Iliad of Homer.* Chicago: The University of Chicago Press.

Leavis, F. R. (1979): *New Bearings in English Poetry.* London: Penguin Books Ltd.

Leech, G. N. (1969): *A Linguistic Guide to the English Poetry.* New York: Longman Group Ltd.

_____ (2008): *Language and Literature: Style and Foregrounding.* London: Pearson Education Ltd.

Leger, L. (1990): *Creating Unforgetable Characters.* New York: Henry Holt and Company.

Levi-Strauss, L. (1955) *The Structural Study of Myth.* Journal of American Folklore 68.

_____ (1966): *The Savage Mind.* London: Weidenfeld and Nicholson.

Lindfors, B. (1977) (Mh.): *Forms of Folklore in Africa.* Austin: Texas University Press.

Lo Liyong, T. (1972): *Popular Culture of East Africa.* Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Lodge, O. (1970): *20th Century Criticism.* London: Longman.

Lord, A.B. (1960): *The Singer of Tales.* Cambridge: Harvard University Press.

Lotman, J. (1977): *The Structure of the Artistic Text.* Ann Arbor: The: University of Michigan.

Lukacs, G. (1962): *Meaning of Contemporary Realism.* London: Merlin Press Ltd.

Lyndon, H. (1962): *Swahili Poetry.* Oxford: Clarendon Press.

Mwalimu, H.M. (1984): *Dafina ya Umalenga.* Nairobi: Longman Ltd.

Madumulla, J.S. (1995): *Proverbs and Sayings: Theory and Practice*: Dar es Salaam:

Makward, E. (1972): *Contemporary African Literature.* New York: Random House.

Manya, A. B. (2006): *Semi: Maana na Matumizi.* Dar es Salaam: TUKI.

Masinde, E. W. (2007): *Ufundishaji wa Ushairi katika Shule za Upili na Vyuo.* Eldoret: Taaluma Publishers.

Massamba, D. P. B. (1976): *Diwani ya Massamba.* Nairobi: Nelson Africa Ltd.

Matejka, L. na Pomorska, K. (1971): *Reading in Russian Poetics:* Cambridge MIT.

Mayoka, J. (1986): *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mazrui, A. (1981): *Kilio cha Haki.* Nairobi: Longman Kenya Ltd.

_____ (1988): *Chembe cha Moyo.* Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.

Mazrui, A. na Tidy, M. (1984): *Nationalism and New States in Africa From about 1935 to the Present.* Nairobi: Heinemann.

Mazrui na Syambo, B.K. (1992): *Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbaabu, I. (1985): *Utamaduni wa Kiswahili.* Nairobi: Kenya Publishing and book Marketing Co. Ltd.

_____ (1996): *Language Policy in East Africa.* Nairobi. Educational Research and Publications.

Mbatiah, M. (2001): *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mberia, K. wa (1997): *Natala.* Nairobi: Marimba Publications Ltd.

_____ (2001): *Bara Jingine.* Nairobi: Marimba Publications Ltd.

_____ (2011): *Another Continent: An Anthrology of Poetry.* (Tafsiri pamoja na Wafula, R. M). Nairobi: Marimba Publications Ltd.

McGann, J. (1985): *Historical Studies and Literary Criticism.* Madison: University of Wisconsin.

Meema, E. (1975): *Misemo.* (Kitabu cha Kwanza A – E), Nairobi: Trans Africa Publishers Ltd.

Middleton, J. (1992): *The World of the Swahili.* New Haven: Yale University Press.

Mieder, W. (2004): *Proverbs are the best policy: Wisdom and American Politics.* Logan: Utah State University Press.

Mieder, W. na Janet Sobieski, J. (2003): *Proverbs and their Sciences: An Anointed International Bibliography:* Bolimannsueler. Schchneider Verlag Hohengehren.

Milner, A. (1995): *Contemporary Critical Theory.* London: UCLA Press.

Miruka, O. (1999): *Studying Oral Literature.* Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Mitchell, S. na Naggy, G. (2000): *The Singer of Tales – Albert B. Lord. 2nd Edition.* London: Harvard University Press.

Mlacha, S. A. K. na Hurskainen, A. (1985): *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Dar es Salaam. TUKI.

Mnyampala, M. (1965): *Waadhi wa Ushairi.* Nairobi: East African Literature Bureau.

Mohamed, S.A. (1973): *Vito Vya Hekima, Simo na Maneno ya Mshangao.* Nairobi: Longman Ltd.

_____ (1980): *Sikate Tamaa.* Nairobi: Longman.

_____ (1984): *Kina cha Maisha.* Nairobi: Longman Ltd.

_____ (1990): *Mbinu na Mazoezi ya Ushairi.* Nairobi: Evans Brothers (Kenya) Ltd.

_____ (2002): *Jicho la Ndani.* Nairobi: Longhorn Publishes (K) Ltd.

Momanyi, C. (2001): *Tamathali katika Vitendawili.* Nairobi: Didaxis.

Msokile, M. (1992): *Kunga za Fasihi na Lugha.* Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors Ltd.

_____ (1993): *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mugo, M. (1978): *Visions of Africa.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mukaravksy, J. (1964): *Standard Language and Poetic Language.* Washington D.C: Georgeton University Press.

Mulokozi, M. M. (1990) (Mh.): *Tenzi Tatu za Kale.* Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M.M. na Kahigi, K. K. (1973): *Mashairi ya Kisasa.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

_____ (1976): *Malenga wa Bara.* Nairobi: East African Literature Bureau.

_____ (1982): *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mulokozi, M.M. na Sengo, T.S.Y. (1995): *History of Kiswahili Poetry.* Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Murray, P. (19780: *Literary Criticism. A Glossary of Major Terms.* New York: Longman.

Musau, P.M. & Ngugi, P.Y. (1999): *Kunga za Kiswahili.* Nairobi: Didaxis Resources and Services.

Mutembei, A. K. (2009): *Ukimwi katika Fasihi ya Kiswahili 1982 – 2006.* Dar es Salaam: TUKI.

_____ (2001): *Poetry and AIDS in Tanzania. Changing Metaphors and Metonymies in Haya Oral Traditions.* Leiden: Leiden University.

Mutiso, K. wa (1986): *Mizani Yangu.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mvati, M., Maliachi, P.A na Kuvuna, S. (1992): *Nuru ya Ushairi wa Kiswahili.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mvungi, T. (1982): *Raha Karaha.* Dar es Salaam: Continental Publishers Ltd.

Mwangi, R. (1970): *Kikuyu Folktales.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mwinyihatibu, M. (1977): *Malenga wa Mrima.* London: Oxford University Press.

Mzenga, M. na Hijazy, S. O. (1977): *Tujifunze Mashairi.* Nairobi: Macmillan.

Nabhany, A. S. (1985): *Umbuji wa Kiwandeo.* Nairobi: East Africa Publishing House.

Nagler, M.N. (1967): *Towards a Generative View of Formula.* TAPA 98.

_____ (1974): *Spontaneity and Tradition. A Study in the Oral Art of Homer.* Berkeley: University of California Press.

Nassir, A. (1971): *Malenga wa Mvita.* Nairobi: Oxford University Press.

Ndalu, A. na King'ei, G. K. (1989): *Kamusi ya Methali za Kiswahili.* Nairobi: Heinemann.

Nestor, H.A. (1978): *500 Haya Proverbs.* Arusha: East African Literature Bureau.

New, C. (1999): *Philosophy of Language.* London: Routledge.

Newton, K. M. (1990): *Interpreting the Text: A Critical Introduction to the Theory and Practice of Literary Interpretation.* London: Harvester.

Ngure, A. (2003): *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Njogu, K. (2004): *Reading Poetry as Dialogue* . Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999:) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkwera, F.M.V. (1978): *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam Tanzania Publishing House.

Noor, I.S. (1988): *Tungo Zetu.* New Jersey: The Red Sea Press Inc.

Norvick, N. (1985): *How Proverbs Mean.* Berlin: Mouton.

Nowottny, W. (1968): *The Language Poets Use.* New York: Oxford University Press.

Nyamaume, K. A. (1976): *Diwani ya Ustadi Nyamaume.* Nairobi: Shungwaya Publishers Ltd.

Nyerere, J. K. (1968): *Ujamaa.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

_____ (1973): *Freedom from Development.* Nairobi: Oxford University Press.

_____ (1974): *Binadamu na Maendeleo.* Nairobi: Oxford University Press.

Obiechina, E. (1990): *Language and Theme: Essays on Africa Literature.* Washington DC: Howard University Press.

Odaga, B. (1984): *Yesterday's Todays: The Study of Oral Literature.* Kisumu: Lake Publishers and Enterprises Ltd.

Odinga, O. (1967): *Not yet Uhuru.* London: Heinemann.

Okpewho, I. (1992): *African Oral Literature. Backgrounds Character and Continuity.* Bloomington: Indiana University Press.

Olsen, S .N. (1973): *The Structure of Literary Understanding.* Cambridge: Cambridge University Press.

Ombuge, R. na Kisia, A. (1999): *Uchambuzi wa Mashairi.* Nairobi: Standard Textbooks, Graphics and Publishing.

Ong, W. (1982): *Orality and Lite*racy: New York; Methuen.

Oyugi, W. O. (1994): *Politics and Administration in East Africa.* Nairobi: English Press.

P'Bitek, O. (1973): *African's Cultural Revolution.* Nairobi: Macmillan.

_____ (1978): *Wimbo wa Lawino.* Nairobi: East African Publishing House.

Parry, A. (1971): *The Making of the Homeric Verse: The Collected Papers of Milman Parry.* Oxford: Clarendon.

Peck, J. na Coyle, M. (1984): *How to Study Literature, Literary terms and Criticisms.* London: Macmillan Educational Books Ltd.

Perry, J. E. (1965) (Mh.): *Approaches to the Poem: Modern Essays in the Analysis and Interpretation of Poetry.* San Franscisco: Chandler Publishing Company.

Pierce, C. (1977): *Semiotics and Significs.* Bloomington: Indiana University Press.

Preminger, A. na Brogan, T.V. (1997): *The New Princeton Encyclopedia of Poetry and Poetics.* Princeton: Princeton University Press.

Prins, H. H. J. (1967): *The Swahili Speaking People's of Zanzibar and the East African Coast.* London: I. A. Institute.

Propp, V. (1968): *Morphology of the Folktale.* Austin: University of Texas Press.

Richards, I. A. (1936): *The Philosophy of Rhetoric.* Oxford: Oxford University Press.

Rieu, E. V. (Taf.) (1950): *Homer: The Illiad.* London: Penguin Books.

Robert, S. (1961): *Mwafrika Aimba.* London: Nelson.

_____ (1969): *Koja la Lugha.* London: Oxford University Press.

_____ (1972): *Almasi za Afrika.* London: Nelson.

_____ (1972): *Sanaa ya Ushairi.* London: Nelson.

Roberts, E. V. (1978): *Thinking and Writing About Literature.* Englewood: Prentice Hall.

Roberts, P. D. (1988): *How Poetry Works.* London: Penguin Books.

Rodney, W. (1989): *How Europe Underdeveloped Africa.* Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Ruo, K. R. (1984): *Nguzo za Ushairi wa Kiswahili.* Nairobi Macmillan Publishers Ltd.

Sacks, S. (1979) (Mh.): *On Metaphor.* Chicago: The Chicago University Press.

Saussure, F. de. (1966): *Course in General Linguistics.* Wade Baskin (Mt.). New York: McGraw Hill.

Scholes, R. na Kellogg, R. (1966): *The Nature of Narrative.* New York: Oxford University Press.

Scholes, R. (1974): *Structuralism in Literature: An Introduction.* New Haven: Yale University Press.

_____ (1982): *Semiotics and Interpretation.* New Haven: Yale University Press.

Scully, J. (1966): *Modern Poets on Modern Poetry.* London: Fontana.

Sengo, T. S. Y. (1975): *Shaaban Robert: Uhakiki wa Maandishi Yake.* Nairobi: Longman.

Senkoro, F. E. M. (1984): *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

_____ (1987): *Fasihi na Jamii.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

_____ (1988): *Ushairi, Nadharia na Tahakiki.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

_____ (2007): (Mh.) *Lugha na Fasihi ya Kiswahili Afrika Mashariki.* Dar es Salaam: Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki.

Simiyu, W. F. (2011): *Kitovu cha Fasihi Simulizi.* Mwanza: Serengeti Bookshop.

Simpson, P. (1997): *Language Through Literature: An Introduction.* London: Routledge.

Snow-White, K.H.A. (1974): *Usanifu wa Ushairi.* Nairobi: East African Literature Bureau.

Soyinka, W. (1976): *Myth, Literature and the African World.* Cambridge: Cambridge University Press.

Steen, G. (1974): *Understanding Metaphor in Literature: An Empirical Approach.* London: Longman.

Sternberg, M. (1978): *Expositional Modes and Temporal Ordering in Fiction.* Bloomington: Indiana University Press.

Stolz, B. A. na Shannon, R. S. (1976): *Oral Literature and the Formula.* Michigan: Centre for Coordination of Ancient and Modern Studies: University of Michigan.

Swingwood, A. (1998): *Cultural Theory and the Problem of Modernity.* London: Macmillan Press.

Taylor, A. (1962): *The Proverb and Index to the Proverb.* Copenhagen: Rosenkilde and Bagger.

Thiong'o, N. wa. (1986): *Decolonizing the Mind: The Politics of Language in African Literature.* Nairobi: Heinemann.

_____ (1993): *Moving to the Centre.* London: James Carvey.

Todorov, T. (1977): *The Poetics of Prose.* New York: Cornell University Press.

_____ (1983): *Symbolism and Interpretation.* London: Routledge and Kegan Paul.

Tomlinson, C. na Lynch – Brown, C. (2007): *Essential of Young Adult Literature.* Boston: Pearson.

Tompkins, J. (Mh.) (1980): *Reader Response Criticism: From Formalism to Post-Structuralism.* Baltimore: John Hopkins.

Toolan, M. (2004): *Language in Literature: An Introduction to Stylistics.* London. Arnold.

Topan, F. (1975): (Mh.) *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*, (Katika kitabu cha pili), Nairobi: Oxford University Press.

Trench, R. C. (2003): *Proverbs and Their Lessons.* Burlington: Queen City Printers.

Trudgill, P. (1974): *Sociolinguistics: An Introduction.* London: Penguin Books Ltd.

Unspensky, B. (1973): *Poetics of Composition.* Berkeley: University of California Press.

Uvetie, E. (1983): *Utamu wa Lugha.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Vansina, J. (19850: *Oral Tradition as History.* Nairobi: Heinemann.

Wade-Grey, H. J. (1952): *The Poet of the Iliad.* Cambridge: Cambridge University Press.

Wafula, R.M. na Njogu (2007): *Nadharia na Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Waihiga, C. na Kagwa, F.M. (2007): *Kamusi ya Changanuzi ya Methali.* Nairobi: Macmillan Publishers Ltd.

Walibora, K. (2007): *Malenga wa Karne Mpya.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wallah, N.J. (1988): *Malenga wa Ziwa Kuu.* Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.

Wamitila, K. W. (2001): Archetypal Criticism of Kiswahili Poetry. Bayreuth: Bayreuth African Studies Series 57.

_____(2002): *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

_____ (2003a): *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Books.

_____ (2003b): *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Books

_____ (2004) (Mh.): *Tamthilia ya Maisha.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

_____ (2006a): *Kamusi ya Methali.* Nairobi: Longhorn Publishers.

_____ (2006b): *Kamusi ya Ushairi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

_____ (2008): *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wanjohi, G.J. (1997): *The Wisdom and Philosophy of African Proverbs.* Nairobi: Paulch Publications Africa.

Wats, A. C. (1969): *The Lyre and the Harp. A Comparative Construction of Oral Tradition in Homeric and Old English Epic Poetry.* New Haven: Yale University Press.

Wellek, R. and Warren, A. (1985): *Theory of Literature*. Harmondsworth: Penguin Books Ltd.

Wetherill, P. M. (1974): *The Literary Text: An Examination of Critical Methods.* Los Angeles: University of California Press.

Whallon, W. (1969): *Formula, character and Context: Studies in Homeric, Old English and Old Testament Poetry*. Cambridge: Cambridge University Press.

Whiteley, W.H. (1969): *Swahili: The Rise of a National Language*. London: Methuen and Co. Ltd.

Whitman, C. H. (19580: *Homer and the Homeric Tradition.* Cambridge: Cambridge University Press.

Whorf, B.L. (1958): *Language, Thought and Reality*. New York: John Wiley and Sons Ltd.

Wood, R. (1971): *An Essay on the Original genus and Writing of Homer*. New York: Garland Publishing.

Yule, G. (1985): *The Study of Language.* New York: Cambridge University Press.

Yule, P. na Levinson, S. (1987): *Politeness: Some Universals in Language Use.* Cambridge: Cambridge University Press.

Zakwany, A. S. (1979): *Diwani ya Jinamizi.* Nairobi: Shungwaya Publishers.

VIAMBATISHO
ORODHA YA VIAMBATISHO

KIAMBATISHO I: MASHAIRI YA KIMAPOKEO

1. MASHAIRI YA ABDILATIF ABDALLA: (*SAUTI YA DHIKI)*
   Mnazi: Vuta N'kuvute ..... Uk. 17-22
   Muwerevu Hajinyowi ..... Uk. 27
   Zindukani ..... Uk. 69-72
   Kutendana ..... Uk. 89-110

2. MASHAIRI YA K. H. A. AKILIMALI SNOW-WHITE:
   (*USANIFU WA USHAIRI)*
   Subira ..... Uk. 6-7
   Alie kwenda kaenda ..... Uk. 11-12
   Mganga Hatajiganga ..... Uk. 53-54
   Umoja ni Ngome Kuu ..... Uk. 111-112

KIAMBATISHO II: MASHAIRI YA KATI

1. MASHAIRI YA ALAMIN MAZRUI: (*CHEMBE CHA MOYO)*
   Usijiangamize ..... Uk. 9
   Hasira Hasara? ..... Uk. 23
   Mgongano ..... Uk. 36
   Kula Njama ..... Uk. 44-47

2. MASHAIRI YA SAID A. MOHAMED: (*JICHO LA NDANI)*
   Mara mia la! ..... Uk. 43
   Jicho Geni ..... Uk. 45
   Kesho ..... Uk. 79
   Nguvu Hazilei ..... Uk. 138

KIAMBITISHO III: MASHAIRI HURU

1. MASHAIRI YA EUPHRASE KEZILAHABI: (*KICHOMI)*
   Mafahali Wapigana ..... Uk. 5
   Nimechoka ..... Uk. 34-35
   Kuchambua Mchele ..... Uk. 63
   Hadithi ya Mzee ..... Uk. 69-72

2. MASHAIRI YA KITHAKA WA MBERIA: (*BARA JINGINE)*
   Hatutaaga Ndoto ..... Uk. 4-5
   Bara Jingine ..... Uk. 10-16
   Mruko wa Nyuki ..... Uk. 20-25
   Nakumbuka Ulivyokuwa ..... Uk. 76-78

KIAMBATISHO IV:

A. HOJAJI KWA WATUNZI WA USHAIRI WA KISWAHILI WANAOZINGATIA ARUDHI ZA KIMAPOKEO

Jibu maswali yote kulingana na maagizo.

Jina: _____ (si lazima)

Jinsia: _____

Umri:

Kati ya (a) 15 – 25 ☐

(b) 26 – 35 ☐

(c) 36 – 45 ☐

(d) 46 na zaidi ☐

Kiwango cha Elimu:

(a) Chini ya darasa la nane ☐

(b) Kati ya kidato cha kwanza hadi cha nne ☐

(c) Zaidi ya kidato cha nne ☐

1. Kwa maoni yako, ni mambo gani ambayo unaweza kupendekeza kuwa ya muhimu katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili kwa upande wa matumizi ya lugha.

   a) Taja mambo hayo.

   _____

   _____

   _____

   _____

   b) Toa maelezo mafupi ya kuunga mkono maoni yako uliyoyataja katika (a).

   _____

   _____

   _____

   _____

2. Baadhi ya watunzi wa mashairi ya Kiswahili hutumia methali.

(a) Methali hizo hutumiwa vipi au kwa namna gani katika mashairi ya Kiswahili?

_____

_____

_____

_____

(b) Matumizi ya methali yana manufaa gani katika utunzi na uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili? Eleza kwa kifupi.

_____

_____

_____

_____

3. Mashairi ya Kiswahili yasiyotumia methali hutumia kauli za aina gani badala yake?

(a) Taja baadhi ya kauli hizo zinazotumiwa katika mashairi ya Kiswahili.

_____

_____

_____

_____

(b) Ni kwa sababu gani mtunzi hutumia aina hizo za kauli ulizotaja katika (a).

_____

_____

_____

_____

4. Ni nini maoni yako kuhusu mashairi ya Kiswahili yanayotumia methali na yale yasiyotumia methali kwa upande wa uwasilishaji wa ujumbe.

_____

_____

_____

_____

5. Kutokana na uzoefu wako wa kutunga mashairi, ni lazima mashairi ya Kiswahili kuweza kutungwa kwa kuzingatia methali?

a) Ndio ☐

b) La ☐

Iwapo jibu lako ni (a) au (b), eleza kwa kifupi maoni yako.

_____

_____

_____

_____

6. Kwa wakati huu wa sasa, mabadiliko mbalimbali yameweza kutokea katika maisha ya jamii hapa Afrika Mashariki.

(a) Kwa maoni yako, eleza kwa kifupi namna mabadiliko hayo ya kijamii yanavyoweza kuathiri matumizi ya methali katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili.

_____

_____

_____

_____

(b) Eleza kwa kifupi matumizi yoyote matatu ya misemo ambayo ilikuwa ikitumiwa katika mawasiliano ya kijamii lakini wakati huu wa sasa hayatumiwi katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili.

_____

_____

_____

_____

7. Mashairi ambayo hutumia methali na yale yasiyotumia methali huweza kutumiwa vipi kuueleza au kuuwasilisha ujumbe wa mtunzi? Eleza kwa kifupi.

_____

_____

_____

8. Kwa ujumla mtunzi wa mashairi ya Kiswahili hupaswa kuwa na ujuzi gani wa lugha? Eleza kwa kifupi.

_____

_____

_____

_____

B. HOJAJI KWA WATUNZI WA USHAIRI WA KISWAHILI WASIOZINGATIA ARUDHI ZA KIMAPOKEO

Jibu maswali yote kulingana na maagizo

Jina: _____ (si lazima)

Jinsia: _____

Umri:

Kati ya (a) 15 – 25 ☐

(b) 26 – 35 ☐

(c) 36 – 45 ☐

(d) 46 na zaidi ☐

Kiwango cha Elimu:

(a) Chini ya darasa la nane ☐

(b) Kati ya kidato cha kwanza hadi cha nne ☐

(c) Zaidi ya kidato cha nne ☐

1. Kwa maoni yako, ni mambo gani unayoweza kupendekeza kuwa ya msingi katika utunzi wa ushairi wa Kiswahili kwa upande wa matumizi ya lugha.

(a) Taja mambo hayo muhimu.

_____

_____

_____

(b) Toa maelezo mafupi ya kuunga mkono maoni ambayo uliyatoa katika (a).

_____

_____

_____

_____

2. Baadhi ya tungo za mashairi huru hazina matumizi ya methali.

(a) Ni kwa sababu gani mashairi hayo hayakutumia methali? Eleza kwa kifupi.

_____

_____

_____

(b) Kama mashairi hayo hayakutumia methali, hutumia aina gani za lugha? Eleza kwa kifupi.

_____

_____

_____

_____

(c) Matumizi hayo ya lugha uliyotaja katika (b) yana manufaa gani katika utunzi na uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili.

_____

_____

_____

_____

3. Kutumia au kutotumia methali katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili kunaweza kupunguza uzuri au ubora katika uwasilishaji wake? Eleza kwa kifupi.

_____

_____

_____

_____

4. Kwa wakati huu wa sasa, mabadiliko mbalimbali yameweza kutokea katika maisha ya jamii hapa Afrika Mashariki.

(a) Kwa maoni yako, eleza kwa kifupi namna mabadiliko hayo yanavyomwathiri mtunzi wa mashairi ya Kiswahili katika uteuzi wa lugha inayotumiwa kwenye utunzi.

_____

_____

_____

(b) Ni vipengele vipi vya lugha ambavyo havitumiwi kwa sasa kutokana na mabadiliko ya maisha yanayotokea katika jamii.

_____

_____

C. HOJAJI KWA WAHAKIKI WA USHAIRI NA FASIHI KWA UJUMLA

Jibu maswali yote kulingana na maagizo.

Jina: _____ (si lazima)

Kiwango cha Elimu: _____

1. Kwa maoni yako, ni mambo gani ambayo unaweza kupendekeza kuwa ya msingi katika

utunzi wa mashairi ya Kiswahili?

(a) Ama (i) Ushairi yanayozingatia arudhi za kimapokeo.

_____

_____

_____

_____

Au (ii) Mashairi yasiyozingatia arudhi za kimapokeo.

_____

_____

_____

_____

(b) Toa maelezo mafupi kuunga mkono maoni yako.

_____

_____

_____

_____

2. Baadhi ya tungo za mashairi ya Kiswahili yanayozingatia arudhi za kimapokeo yana matumizi mengi ya methali katika utunzi na uwasilishaji wake

(a) Eleza kwa ufupi sababu zinazosababisha mashairi ya Kiswahili kutumia methali katika uwasilishaji wake.

_____

_____

_____

_____

(b) Methali hizo hutumiwa kwa namna gani katika muktadha wa utunzi na uwasilishaji wa mashairi ya Kiswahili?

_____

_____

_____

_____

3. Baadhi ya mashairi ya Kiswahili yasiyozingatia arudhi za kimapokeo hayatumii methali. Ni kwa sababu gani? Eleza kwa kifupi.

_____

_____

_____

_____

4. (a) Mashairi ya Kiswahili yasiyotumia methali katika utunzi, hutumia vipengele gani vya lugha badala yake? Eleza kwa kifupi.

_____

_____

_____

_____

(b) Vipengele hivyo ulivyovitaja katika (a) vina nafasi gani katika usawiri na uwasilishaji wa ujumbe kwenye utunzi wa ushairi wa Kiswahili?

_____

_____

_____

_____

5. Ni lazima mashairi ya Kiswahili yatungwe kwa kushirikisha kipengele cha methali? Eleza kwa ufupi.

_____

_____

_____

_____

6. Ni kwa namna gani mabadiliko ya kitamaduni katika jamii huweza kuathiri matumizi ya lugha kama vile methali kwenye utunzi wa ushairi wa Kiswahili?

_____

_____

_____

_____

7. Ukilinganisha mashairi ya Kiswahili yanayozingatia methali na yale yasiyozingatia Methali, ni yapi yaliyo bora kwa upande wa ujumi na uwasilishaji wa maudhui? Eleza kwa ufupi.

_____

_____

_____

_____

8. Mtunzi wa mashairi ya Kiswahili anapaswa kuwa na tajiriba gani ili aweze kutunga na kuuwasilisha ujumbe katika utungo wake? Eleza kwa ufupi.

_____

_____

_____

_____

9. Mashairi ya Kiswahili yanaweza kuainishwa kwa kuzingatia matumizi ya methali Katika uwasilishaji wake? Eleza kwa kifupi.

_____

_____

_____

KIAMBATISHO V: ORODHA YA WAHOJIWA

Kitula King'ei

Ni mtaalamu wa lugha na mhakiki wa fasihi. Amekuwa akitunga mashairi ya Kiswahili na kuyawasilisha kimaandishi. Ni Profesa katika Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Catherine M. Ndungo

Ni mtaalamu wa lugha na mhakiki wa fasihi. Ni Profesa katika Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Edwin W. Masinde

Ni mtaalamu wa lugha na mhakiki wa fasihi. Ni mhadhiri katika Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kimani Njogu

Mtaalamu wa lugha na mhakiki wa fasihi. Ni Profesa na mshirikishi katika Shirika la Twaweza Communication, Nairobi.

Rocha Chimerah

Mtaalamu wa lugha na mhakiki wa fasihi. Ni Profesa katika Idara ya Lugha na Isimu, Chuo Kikuu cha Pwani.

Chacha Nyaigotti – Chacha

Mtaalamu wa lugha na mhakiki wa fasihi. Ni Profesa katika Idara ya Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu cha Egerton.

Ezekiel Alembi

Mtaalamu wa fasihi na mhadhiri katika Idara ya Fasihi, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Marehemu).

Kisa Amateshe

Mtaalamu wa fasihi na mhadhiri mkuu katika Idara ya Fasihi, Chuo Kikuu cha Kenyatta. Amekuwa akitunga mashairi na kuyawasilisha kimasimulizi na kimaandishi kwa lugha ya Kiingereza.

Hamisi O. Babusa

Mtaalamu wa lugha na fasihi. Hutunga mashairi ya Kiswahili na kuyawasilisha kimasimulizi na kimaandishi. Ni mhadhiri katika Idara ya Teknolojia ya Elimu na Mawasiliano, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

James O. Ogolla

Mtaalamu wa lugha na isimu. Ni mhadhiri mkuu katika Idara ya Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu cha Egerton.

Mikhail Gromov

Mtaalamu wa lugha na fasihi. Ni Profesa katika Idara ya Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu cha USIU, Nairobi.

F.E.M.K. Senkoro

Mtaalamu wa lugha na mhakiki wa fasihi. Ni Profesa katika TATAKI, Kitengo cha Fasihi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Said A. M. Khamis

Mtaalamu wa lugha na isimu. Ni Profesa katika TATAKI, Kitengo cha Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Y. M. Kihore

Mtaalamu wa lugha na isimu. Ni Profesa katika TATAKI, Kitengo cha Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Y. I. Rubanza

Mtaalamu wa lugha na isimu. Ni Profesa katika TATAKI, Kitengo cha Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sheikh A. Nabhany

Mkaazi wa Mombasa Kisiwani. Ni mshauri wa masuala ya lugha ya Kiswahili na fasihi katika jamii ya Waswahili. Hutunga mashairi na kuyawasilisha kimasimulizi na kimaandishi.

Amira M. Saidi

Ni mama wa makamo. Anajua kusoma na kuandika. Hutunga mashairi ya Kiswahili na kuyawasilisha kimasimulizi katika sherehe mbalimbali za jamii ya Waswahili.

Zainabu N. Ali

Mwenyeji wa Mombasa Kisiwani. Hutunga mashairi ya Kiswahili na kayawasilisha kimasimulizi. Hivi sasa anasomea shahada ya B.Ed., Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Amina Vuzo

Mtaalamu wa lugha na fasihi ya Kiswahili. Ni mwalimu wa miaka mingi katika shule mashuhuri za upili na vyuo vya walimu nchini Kenya.

Milkah Riga

Mtunzi wa mashairi ya Kiswahili. Amekuwa akiwasilisha tunzo zake kimasimulizi katika sherehe mbalimbali za Chuo Kikuu cha Kenyatta. Ana shahada ya B.Ed.

Mwalimu Majeki

Mkaazi wa Siu huko Vanga. Hana kazi maalumu, na hutunga mashairi ya Kiswahili na kuyawasilisha kimasimulizi na kimaandishi. Mara kwa mara hualikwa katika sherehe mbalimbali ili kutumbuiza.

Hussein Said

Mkaazi wa Lamu Kisiwani. Hutunga mashairi ya Kiswahili na kuyawasilisha kimasimulizi na kimaandishi.

Mohamed Shaban Ali

Ni mkaazi wa Kongowea, Mombasa. Anajulikana pia kwa jina la 'Mpembuzi Mchanga'. Amekuwa akitunga mashairi na kuyachapisha katika gazeti la Taifa Jumapili.

Ismail M. Bakari

Ni mkaazi wa Mombasa Kisiwani. Anajilikana pia kwa lakabu ya 'Swila Mchiriza Sumu'. Amekuwa akitunga na kuyachapisha mashairi yake ya Kiswahili katika gazeti la Taifa Leo.

Ludovick Mbogholi

Mkaazi wa Kitale. Anajulikana pia kwa lakabu ya 'Al-Ustadh Luqman' na 'Ngariba Mtumbi'. Amekuwa akitunga na kuyachapisha mashairi yake ya Kiswahili katika gazeti la Taifa Leo.

Juma Namtola

Mkaazi wa Mombasa. Mtunzi wa mashairi ya Kiswahili na amekuwa akichapisha tungo zake katika gazeti la Taifa Leo.

Irungu Mwangi

Mkaazi wa Thika. Mashairi yake yanatokea mara kwa mara katika gazeti la Taifa Leo. Anajulikana pia kwa lakabu ya 'Fimbo ya Mnyonge". Hutunga mashairi na kuyawasilisha kimaandishi.

Zahran Rashid

Mkaazi wa Kibokoni, Mombasa. Amejifunze kutunga mashairi kutoka kwa wavyele wake. Hajui kusoma, lakini hutunga na kuyawasilisha mashairi kimasimulizi.

Jabali Yusuf Yaa

Mkaazi wa Kinondoni, Dar es Salaam. Anajua kusoma na kuandika. Hutunga mashairi ya Kiswahili na kuyawasilisha kimasimulizi.

Sara M. Mchozi

Mkaazi wa kijiji cha Mabibo, Dar es Salaam. Ameolewa na mama wa makamo. Hutunga mashairi ya Kiswahili na kuyawasilisha kimasimulizi wakati anapoalikwa katika shereh za kijamii.

Boom Dhou Zur

Mkaazi wa Sheikh Lango, Dar es Salaam. Ni mchuuzi wa vipodozi katika Kituo Kiku cha Mabasi, Ubungo. Hutunga na huwasilisha mashairi ya Kiswahili yanapohitajika a katika sherehe za kijamii.

Rajab Kirobo

Mkaazi wa Bagamoyo. Anajulikana pia kwa lakabu ya 'Mzee wa Shamba' na amekuw akiyachapisha katika gazeti la Uhuru.

Mzee Kikowapi

Mkaazi wa Manzese, Dar es Salaam. Mtunzi wa mashairi ya Kiswahili na tungo zak zimekuwa zikitokea mno katika gazeti la Kasheshe.

Tabu M. Mtembanda

Mkaazi wa Magu, Mwanza. Mtunzi wa mashairi ya Kiswahili na tungo zake zimekuw zikichapishwa katika gazeti la Mzalendo.

Mamboshelala Kalima

Mkaazi wa Kigoma. Mtunzi wa mashairi ya Kiswahili na tungo zake zimekuw zikichapishwa katika magazeti ya Uhuru na Mzalendo.

KENYA[illegible]VERSITY LIBRARY